# A Concise English-Swahili DICTIONARY

Kamusi Ya
Kiingereza - Kiswahili

REVISED EDITION

R. A. Snoxall
H. B. Mshindo

OXFORD

Digitized by the Internet Archive
in 2023 with funding from
Kahle/Austin Foundation

https://archive.org/details/conciseenglishsw0000snox_u5u1

11,000/-

# A CONCISE ENGLISH - SWAHILI DICTIONARY

UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

**MINISTRY OF EDUCATION AND CULTURE**

## Certificate of Approval

NO. 348

Title of Publication: A Concise English–Kiswahili Dictionary

Author: R.A. Snoxall & H.B. Mshindo

Publisher: Oxford University Press

ISBN: 9976 4 0016 0

*This book was approved by EMAC on* 6 *(date)* 10 *(month)* 2004 *(year) to be a* Reference *for* Primary and Secondary **Schools** *in Tanzania.*

R. A. Mpama.
*CHAIRPERSON*
***EMAC***

H. A. Lihawa.
*REGISTRAR*
***EMAC***

OXFORD
UNIVERSITY PRESS

Great Clarendon Street, Oxford OX2 6DP

Oxford University Press is a department of the University of Oxford.
It furthers the University's objective of excellence in research,
scholarship, and education by publishing worldwide in

Oxford New York
Auckland Bangkok Buenos Aires Cape Town Chennai
Dar es Salaam Delhi Hong Kong Istanbul Karachi Kolkata
Kuala Lumpur Madrid Melbourne Mexico City Mumbai Nairobi
Sao Paulo Shanghai Singapore Taipei Tokyo Toronto

and an associated company in Berlin

Oxford is a registered trade mark of Oxford University Press
in the UK and in certain other countries.

Published in Tanzania
by Oxford University Press (T) Ltd

© Author 2002

Illustrations by Walter Lema.

The moral rights of the author have been asserted

Database right Oxford University Press (maker)

All rights reserved. No part of this publication may be reproduced,
stored in a retrieval system, or transmitted, in any form or by any means,
without the prior permission in writing of Oxford University Press,
or as expressly permitted by law, or under terms agreed with the appropriate
reprographics rights organization. Enquiries concerning reproduction
outside the scope of the above should be sent to the Rights Department,
Oxford University Press, East Africa Ltd, at the address below.

You must not circulate this book in any other binding or cover
and you must impose this same condition on any acquirer

ISBN

First published 1958
Reprinted (revised) 1961, 1968, 1969, 1970, 1971, 1972, 1973, 1974, 1975, 1976 (Twice),
1978, 1979, 1984, 1985, 1987, 1988, 1989, 1991, 1993, 1994, 1995, 1996, 1997, 1998, 1999, 2000,
2001, 2002 (revised), 2003 (Twice), 2004 (Thrice), 2005,2006

Published by Oxford University Press (T) Ltd,
Mikocheni 'B', Plot No.149,
P. O. Box 5299,
Dar es Salaam, Tanzania.

Design & Typesetting
Bookprint Creative Services LTD.
Nairobi, Kenya.

# PREFACE | DIBAJI

Kutunga kamusi ni kazi kubwa. Ni kazi ya kuendelea, kwani lugha ni chombo hai. Kila baada ya muda kamusi huhitaji kupitiwa na kuandikwa upya kwa kuondoa na kuingiza dhana na tafsiri kongwe na mpya. Ukubwa wa kazi ya kupitia kamusi unatokana na ukweli kwamba mpitiaji hulazimika kutoa uamuzi kuhusu mawazo ya wenzake waliomtangulia katika kuifanyia kazi kamusi husika. Mpitiaji humbidi aamue ni maneno yapi atapaswa kuyaingiza kwenye toleo la kamusi la sasa na yapi atalazimika kuyaacha. Kazi hii si nyepesi, kwani mpitiaji hulazimika kupima hisia za watunzi wenzake kwa upande mmoja na zile za watumiaji kwa upande wa pili. Zaidi ya kazi hiyo, mpitiaji huwa na wajibu wa kuhakiki fasili zote za maneno yaliyomo katika kamusi anayoipitia, ili kuona iwapo fasili hizo, kama zilivyo, bado zinakidhi mawasiliano ya wakati uliopo au zinahitaji kubadilishwa.

Hiyo ndiyo kazi iliyonikabili wakati nilipofikiria kulipitia toleo la mwaka 1988 la kamusi ya *A concise English-Swahili Dictionary* ambayo ni matokeo ya upitiaji uliofanywa na chapisho la awali la kamusi hiyo uliofanywa mwaka 1961.

Msukumo wa kuipitia tena kamusi aliyoiandika Snoxall mwaka 1988 ulitokana na sababu kuu tatu. Kwanza, kamusi kimsingi ni kitabu cha rejea ambacho daima kinatarajiwa kukidhi haja ya wanaokitumia. Kwa vile lugha ni kiumbile kinachobadilika daima, kamusi inapaswa kwenda sambamba na mabadiliko hayo. Vinginevyo itapitwa na wakati na watumiaji wake wataiona haina msaada kwao. Ilivyokuwa haiyumkiniki kuipitia kamusi kila asubuhi na jioni, jambo la busara ni kuipitia kila baada ya muda, alimradi hisia za watumiaji zikijitokeza kuwa kuna haja ya kufanya hivyo. Pili, ni kwamba kasi ya mabadiliko ya lugha ya Kiswahili katika nusu ya pili ya karne ya ishirini imekuwa kubwa sana. Hali hiyo imetokana na mabadiliko makubwa na ya haraka katika nyanja mbalimbali za sayansi na teknolojia. Tatu, na ambayo ndiyo sababu kubwa kuliko hizo mbili za awali, ni mabadiliko ya mwelekeo wa matumizi ya kamusi hii.

Kamusi zilizotangulia chapisho hili zilidhamiria kuwasaidia zaidi wasemaji wa Kiswahili waliopenda kujifunza Kiingereza na wasemaji wa Kiingereza waliopenda kujifunza Kiswahili. Kutimiza lengo hilo, maneno mengi yalichaguliwa kutoka kwenye makala ya vitabu na magazeti. Kwa vile lengo la kamusi hii ni kuwasaidia zaidi watu wanaotaka kukitumia Kiswahili katika mawasiliano yao ya kila siku kwenye nyanja mbalimbali za shughuli zao, jitihada imefanywa kuyaingiza maneno mengi ya Kiingereza ya kawaida na ya kitaaluma ambayo mpitiaji anahisi yatahitajiwa mara kwa mara na watumiaji wa nyanja husika. Msingi wa uteuzi wa maneno haukuwa juu ya lugha ya Kiingereza, bali umeegemezwa kwenye dhana za Kiswahili ambazo mtumiaji wa Kiswahili angependa kuzielewa ili aweze kuwasiliana kwa lugha hiyo na wenzake, bali ambazo kwa sasa zimo katika lugha ya Kiingereza. Ni kwa sababu hiyo basi itabainika kwamba kamusi hii ina maneno yanayohusu utamaduni, uchumi, siasa, sayansi, falsafa na istilahi mbalimbali zinazotumiwa na wanafunzi na walimu wao kwenye masomo mbalimbali.

Bila shaka, katika kupitia kamusi hii kazi yangu haikuwa ngumu sana kama ya watangulizi wangu. Nyenzo zilizokuwa mbele yangu katika kufanya kazi hii zilikuwa bora kuliko za wale wenzangu waliofanya kazi hii katika miaka ya 60 na 70. Hivyo, nitakuwa mwizi wa fadhila nikiacha kuwashukuru wale wote walioandika makamusi ya Kiswahili/Kiswahili, Kiingereza/Kiingereza, na Kiingereza/Kiswahili ambazo zimekuwa msaada mkubwa kwangu wakati wote nilipofanya kazi ya kupitia kamusi hii. Pia sitawasahau wale wote waliofanya kazi ya kuhariri, kusanifu na kuchapisha kamusi hii mpaka ikafika hatua ya kuweza kutumika.

**H. B. Mshindo**
2003

# ORTHOGRAPHY

The present standardized Swahili orthography, as used in this book, employs the following symbols:

1. **Vowels:** *i, e, a, o, u*

They are pronounced as follows:

(a) **i** as in English *'see'*
(b) **e** as in English *'bed'*
(c) **a** There is perhaps no equivalent in English: the sound of falling between the a of cat and that of *father*. The Italian a of *capella* is comparable.
(d) **o** Again there is no equivalent in English. The English o of go is a diphthong *o-u*, of which the first part is perhaps nearest to the Swahili sound. (Scottish, French, or Italian o is also similar to the Swahili sound, though pronounced more tensely).
(e) *u* as in the English *'boot'*.

Vowel length is not significant, as in some of the Bantu languages, and is not marked. In Swahili is linked with *stress*, which occurs on the penultimate syllable, e.g.
*pita! mwezi, mchawi, kidogo, mvuvi.*

Double vowels, do, however, occur, especially:

(a) In loan words where either a 'glottal stop' or an 'ain' would intervene in the original Arabic, e.g. *baada, -laani,* &c.; while the first of these examples is pronounced with an extra long vowel, the majority of such words are pronounced as a disyllable.
(b) Where the noun stem has a vowel initial (e.g. *waana, waalimu, muunda, maandiko*); with the exception of the first two, these also tend to be pronounced as disyllable.
(c) In stressed final position in certain words (e.g. *buu, -kuu, choo, mguu, -komaa, paa*). The historical justification for this need not here be considered.

2. **Consonants**

The following occur:
*b, ch, d, f, g, h, j, k, l, m, n, ng', ny, p, r, s, sh, t, v, w, y, z.*

And the following nasal compounds:
*mb, nch, nd, ng, nj, nk, mp, ns, nsh, ni, mv, mw, nz.*

Three Arabic sounds have also been incorporated into the orthography: *th, dh, gh.*
No other Arabic sounds are represented , though they occur widely on the coast and in Zanzibar. Reference to them may be found in the following works:
'Swahili Phonetics'. A.N. Tucker and E.O.Ashton. **African Studies**. Vol. 1, 2/3, 1942.
'Foreign Sounds in Swahili'. A. N. Tucker, **Bulletin S.O.A.S** vols. xi/4 and xii/1, 1946/7.
'Kimvita' (as inquiry into dialect status and characteristics). W.H. Whitley, **Journal E.A.S.C.**, No. 25 1955.
Further there is no representative of aspiration which is significant on the coast, e.g. *tembo*[1] (elephant) with aspirated t as opposed to *tembo* (palm wine) with unaspirated t.

**Note on the sounds:**
They are pronounced as in English except where otherwise stated:

a. **b, d, g, j** Pronounced implosively on the coast but often as in English elsewhere. Nasal compounds of these sounds are pronounced explosively as in English.
b. **j** A palatal sound. Not as in the English *jam*, but rather like a dy sound, though this is only approximate.
c. **m, n** Both of these may be syllabic, especially where occurring as a prefix, e.g. *mtu, nchi, nge.*
d. **ng'** Pronounced as the ng in singing, e.g. ngoa.
e. **th** As in the English *thin.*
f. **dh** As in English *this.*
g. **gh** Pronunciation varies widely according to the degree of 'Arabicization'. At one extreme it sounds like a *'scrapy' g*, and at the other like a voiced form of the *ch* in Scottish loch.

[1]Written *t'embo* by Taylor and Burt

# Aa

**a** ni neno lisilofasirika kwa Kiswahili isipokuwa pengine maana yake ni -moja, -o -ote, mojawapo. Kwa Kiingereza huitwa *'the indefinite article'*. *e.g. tell a man to go*, mwambie mtu mmoja (yeyote, mmojawapo) aende. Kwa kawaida hutangulia kila nomino ya umoja au ya jumla isipokuwa ni mojawapo maalumu. *e.g. a man*, mtu (mmoja, yeyote, mmojawapo): *a score*, korija (moja, yoyote, mojawapo), lakini mtu yule, *the (that) man;* korija ile, *the (that) score;* yaani *the* huitwa *'the definite article'* kwa Kiingereza. Pengine *an* hutumika badala ya *a*, kutangulia vokali zote isipokuwa *eu* na matamko mengine ya *u*, na kutangulia *h* isiyotamkwa, e.g. *an hour, an egg, an idiot, an orange, an ulcer*, lakini, *a horse, a eulogy, a unit. a* hutumika kutangulia *one*, e.g. *a one thing I don't like.*

**abandon** /ə'bændən/ *v.t.* **1.** acha; tupa; telekeza ~ *hope*, kata tamaa. ~ *one self to*, jitia kabisa katika huzuni, furaha, dhambi etc. **~ed** *adj.* -liyeachwa; -liyetupwa; -liyetelekezwa.

**abbreviate** /ə'bri:vɪeɪt/ *v.t.* fupisha (hadithi au neno), e.g. *Mon.* kwa *Monday; Mr.* kwa *Mister.*

**abdomen** /'abdəmən/ *n.* tumbo. **abdominal** *adj.* -a tumbo: *abdominal pains*, maumivu ya tumbo, fumbatio.

**abduct** /æb'dʌkt/ *v.t.* chukua, iba kwa hila au kwa nguvu; teka nyara. **~ion** *n.* kuchukua kwa hila au nguvu.

**Abelian** *adj.* -enye kuhusiana na mtaalamu wa hisabati wa Norway, Niels H. Abel (1802-1829). *Abelian group (maths.)* kundi la nambari lenye kufuata kanuni ya nadharia ya Abel e.g. 2x3 = 3x2.

**ability** /ə'bɪləti/ *n.* **1.** uwezo; utendaji jambo vyema. a man of great ~, mtu mwenye uwezo mwingi. **2.** *(pl.)* ustadi.

**abiotic** /ˌeɪbʌɪ'ɒtɪk/ *adj.* kisichokuwa hai; -enye kuhusiana na vitu visivyokuwa hai.

**able** /'əɪbl/ *adj.* **1.** -enye uwezo; hodari. **2.** -enye akili nyingi; stadi. **ably** *adv.* kwa ustadi.

**abnormal** /æb'nɔ:ml/ *adj.* -sio ya kawaida au desturi; -siyo tazamiwa; mlemavu. **~ity** *n.* ulemavu.

**abolish** /ə'bɒlɪʃ/ *v.t.* ondoa kabisa. **abolition** *n.* utiaji tamati wa jambo, mfumo au muundo fulani.

**abominable** /ə'bɒmɪnəbl/ *adj.* -a kuchukiza mno. **abominate** *v.t.* chukiza mno; kirihi.

**aborigine** /abə'rɪdʒɪni:/ *n.* wazawa asilia; watu wa asili wa nchi, mfano wa watu wa Australia kabla ya majilio ya wakoloni wa Kiingereza.

**abort** /ə'bɔ:t/ *v.t.* haribu mimba. **abortion** *n.* mimba iliyoharibika; kuharibu mimba kabla wakati wa kuzaa haujafika. **abortive** *adj.* -liyotokea kabla ya wakati ufaao; -liyoharibika.

**abound** /ə'baʊnd/ *v.i.* **1.** -wa -ingi. **2.** jaa tele.

**about** /ə'baʊt/ *adv.* karibu. ~ *twenty people*, karibu watu ishirini. *~12 o'clock*, karibu saa sita; ~ *prep.* **1.** kuhusu. *Tell me ~ him*, niambie kuhusu yeye. *a story ~ a lion*, hadithi kuhusu simba. **2.** katika; kuzunguka. *He fastened a rope ~ his waist*, alijizungushia kamba kiunoni.

**above** /ə'bʌv/ *adv./prep.* **1.** juu; juu (ya); kwa juu. **2.** zaidi (ya). ~ *twenty*, zaidi ya ishirini. **3.** bila. *He is ~ suspicion*, ni mtu ambaye hapaswi kutiliwa mashaka hata kidogo. **~board**, wazi; dhahiri. **abrasive** *n.* msasa.

**abreast** /ə'brest/ *adv.* (kwa watu, mashua, magari, etc.) sambamba; bila ya kutangulia wala kuwa nyuma kuelekea upande mmoja. *keep ~ of the times*, -enda na wakati.

**abridge** /ə'bridʒ/ *v.t.* fupisha; fanya muhtasari wa maneno, hotuba au maandishi.
**abroad** /ə'brɔ:d/ *adv.* **1.** nchi za nje; nga'mbo; ughaibuni. **2.** kwa kuenea kila mahali.
**abrupt** /ə'brʌpt/ *adj.* **1.** -a ghafla; -siyotazamiwa. **2.** (kwa kusema, kwa kuandikia, kwa tabia) -a haraka; pasipo adabu. **~ly** *adv.* ghafla.
**abscess** /'æbses/ *n.* jipu; uvimbe.
**absent** /'æbsənt/ *adj.* *(be)* kutokuwepo; adimika. *He is ~*, hayupo. *v.t. absent oneself from* kutokuja au kutohudhuria kwa makusudi. **~-minded** *adj.* -sahaulifu. **~ee** *n.* mtu asiyekuwepo. **absence** *n.* kutokuwepo. **absenteeism** *n.* tabia ya kuchelewa kazini au shuleni bila ya sababu maalumu.
**absolute** /'absəlu:t/ *adj.* **1.** kamili; halisi. **2.** -tupu, pasina kiasi wala mipaka. *~ zero*, sifuri halisi: halijoto ya chini ambapo hali ya mata ni bwete kabisa.
**absorb** /əb'zɔ:b, -'sɔ:b/ *v.t.* **1.** -la; meza. **2.** shughulisha sana; vuta macho, akili, au mawazo: *~ed in a book*, zama sana katika kusoma kitabu hata kutofikiria mambo mengine. **~ing** *adj.* -a kuvuta nadhari sana. **absorption** *n.* ufyonzaji: unyonyaji au upokeaji ndani kwa kutumia amali ya kemikali au molekuli.
**abstain** /əb'steɪn/ *v.i.* *(from)* jinyima; epukana na. *~ from food*, funga. **~er** *n. total ~*, aliyeacha ulevi.
**abstinence** /'abstɪnens/ *n.* hali ya kujizuia kufanya jambo, e.g. kula, kunywa, etc.; hali ya kufunga. *total abstinence*, kuacha kabisa ulevi.
**abstract** /'abstrækt/ *adj.* -a kuwazika tu; dhahania; jambo la kuwazika tu; lisilowezwa kushikika; etc. *n.* muhtasari. *v.t.* toa katika; tenga. **~ed** *adj.* si -angalifu; si -sikizi. **~ion** *n.* usahaulifu; hali ya kuwaza mengine; hali ya kushughulika na jambo fulani hata kutokumbuka mengine.
**absurd** /əb'sɜ:d/ *adj.* -a upuuzi; -a kuchekesha; -a dhahiri kuwa si kweli wala kuelekea kuwa kweli.
**abundance** /ə'bʌndəns/ *n.* wingi; tele; maridhawa. **abundant** *adj.* tele.
**abuse** /ə'bju:z/ *n.* **1.** matumizi mabaya; kutendea vibaya. **2.** matusi; desturi mbaya isiyokuwa ya haki. *v.t* tumia vibaya; tendea vibaya; tukana; shutumu. **abusive** *adj.* -a kutukana
**abyss** /ə'bɪs/ *n.* shimo kubwa la kwenda chini sana; shimo la maangamizi.
**a. c.** *n.* ufupisho wa *alternating current*: mkondo geu wa umeme.
**acacia** /ə'keɪʃə, -sɪə/ *n.* mti ambao utomvu wake ni buhuri iitwayo ubani.
**academy** /ə'kædəmi/ *n.* chuo; taasisi.
**accede** /ək'si:d/ *v.i.* **1.** *(to)* kubali; ridhia. **2.** fikia mahali; rithi cheo. *When did he ~ to the throne?* alirithi lini ufalme?
**accelerate** /ək'sɛləreɪt/ *v.t./i.* zidisha mbio au mwendo; himiza; zidi mwendo.
**acceleration** /ək,selə'reɪʃn/ *n.* mchapuko: kima cha badiliko la kasi mwelekeo kwa muda maalumu. **accelerator** *n.* chombo cha mashine kinachozidisha mwendo.
**accent** /'aks(ə)nt, -sɛnt/ *n.* **1.** (katika kusema) mkazo wa sauti. **2.** alama ya mkazo; shadda. **3.** lafudhi ya kawaida ya jamii ya watu. *v.t* kaza; tia alama ya mkazo. **~uate** *v.t.* kaza. **~uation** *n.* mkazo; shadda.
**accept** /ək'sept/ *v.t.* kubali; pokea. **~able** *adj.* -a kukubalika. **~ance** *n.* kukubali; kibali.
**access** /'ækses/ *n.* njia ya kuingilia; mlango; ongezeko; ziada. *easy of ~*, rahisi sana kufikika. **~ible** *adj.* -a kuweza kufikiwa. **accessary** *n.* mshiriki katika tendo ovu. **accession** *n.* **1.** kutawazwa katika cheo. **2.** ongezeko.
**accessory** *n.* ongezeko lenye kufaa lakini si la asili. *accessories of a bicycle* (e.g. taa, bomba, etc.).

**accident** /'æksɪdənt/ *n.* tukio; bahati; jambo la hatari; ajali. **~al** *adj.* -a bahati; -a ajali.

**acclaim** /ə'kleɪm/ *v.t.* pokea kwa shangwe na vifijo, shangilia. **acclamation** *n.* vifijo; vigelegele.

**acclimatize** /ə'klaɪmətaɪz/ *v.t.* zoeza tabia na hali ya hewa ya ugenini.

**accommodate** /ə'kɒmədert/ *v.t.* **1.** weka; pangisha chumba au vyumba. **2.** tengeneza; rekebisha. **accomodating** *adj.* -enye hisani; karimu; -pole. **accomodation** *n.* makazi.

**accompany** /ə'kʌmpəni/ *v.t.* fuatana na; sindikiza.

**accomplice** /ə'kʌmplɪs, ə'kɒm-/ *n.* msaidizi au rafiki katika tendo baya.

**accomplish** /ə'kʌmplɪʃ/ *v.t.* timiza; fanya; maliza; tekeleza; faulu; weza. **~ed** *adj.* timilifu; kamili.

**accord** /ə'kɔ:d,/ *n.* mapatano (e.g. baina ya nchi mbili). *of one's own ~*, kwa hiyari yake. *v.t./i.* toa; -pa. *~ a hearty welcome (to)*, karibisha vizuri; patana na; lingana na.

**account** /ə'kaʊnt/ *v.i./t.* **1.** *~ for*, toa hesabu ya; eleza hesabu ya; hesabu; kadiri (fedha au mali). **2.** dhani. *n* **1.** hesabu; idadi. *on ~*, kulipa sehemu tu ya bei. **2.** hadithi au maelezo. **3.** ajili; sababu. *on no (not on any) ~*. sivyo; hapana kabisa; hasha. *on this ~*, kwa sababu hii. **4.** thamani; faida; makuu. *of no ~*, -siofaa hata kidogo. *take into ~*, dhani. *take no ~ of*, toangalia; *on one's own ~*, kujisaidia -enyewe. **~able** *adj. be ~*, wajibika; pasiwa. **~ancy** *n.* kazi ya uhasibu. **~ant** *n.* mhasibu. **~-book** *n.* daftari la hesabu.

**accumulate** /ə'kju:mjʊleɪt/ *v.t./i.* kusanya; limbika; lundika; dunduliza. **accumulation** *n.* mkusanyiko; mlundikano; akiba; wingi.

**accumulator** *gn.* betri ya chaji.

**accurate** /'akjʊrət/ *adj.* sahihi; barabara.

**accuracy** /'ækjərət/ *n.* usahihi.

**accuse** /ə'kju:z/ *v.t.* shtaki; laumu; shutumu; suta. *the ~ d*, mshtakiwa. **accusation** *n.* lawama; usutaji; mashtaka; shutuma. **~r** *n.* mshtaki.

**accustom** /ə'kʌstəm/ *v.t.* zoeza: *~ onesself*, jizoeza.

**ace** /eɪs/ *n.* ree, yaani karata ya kucheza yenye ng'anda moja. *within an ~ off*, karibu sana.

**acetate** /'asɪteɪt/ *n.* asiteti; chumvi ya asidi aseti. **acetic** *adj.* -enye kuhusiana na asidi aseti. **acetic acid**, asidi asetiki.

**acetone** /'asɪtəʊn/ *n.* asetoni: kioevu kisichokuwa na rangi chenye kuwaka kwa urahisi kinachotumiwa kama kimumunyishaji kwa ajili ya rangi na vanishi.

**acetylene** /ə'sɛtɪli:n/ *n.* asetilini: gesi isiyokuwa na rangi inayotumiwa kukatia metali.

**ache** /eɪk/ *n.* maumivu yanayoendelea. *v.i.*uma kwa maumivu yanayoendelea.

**achieve** /ə'tʃi:v/ *v.t.* maliza; faulu; isha; pata. **~ment** *n.* upataji; kufaulu; mafanikio.

**acid** /'æsɪd/ *n.* asidi; tindikali. **~ rain**, asidi zifanyikazo kwa mmumunyiko wa oksidi asidi kwenye mvuke uliomo katika angahewa. *~ reactions*, utendanaji wa asidi na metali au besi. **~ic** *adj.* -enye kuhusiana na asidi. **~ test**, jaribio la kuhakikisha kabisa.

**acknowledge** /ək'nɒlɪdʒ/ *v.t.* **1.** kubali; kiri; ungama. **2.** julisha habari ya kuwa kitu kimewasili. *He is ~d to be an expert on this subject*, amekubaliwa kuwa ni stadi katika somo hili. **~ment** *n.* stakabadhi; risiti; kukubali; kukiri.

**acoustic** /ə'ku:stɪk/ *adj.* -a kuhusu uwezo wa kusikia. **~s** *n.* elimu ihusuyo usikizi wa sauti; elimusauti *The ~ of this room are good*, katika chumba hiki sauti husikika vizuri.

**acquaint** /ə'kweɪnt/ *v.t.* julisha; fahamiana na; pasha habari. *be ~ ed with someone*, juana na mtu fulani.

**acquire** /ə'kwaɪə(r)/ *v.t.* pata; jipatia kwa akili au kwa jitihada.

**~d immunity**, kinga ya kujipatia: aina ya kinga ipatikanayo mwilini baada ya mtu kuugua na kupona. **~ment** *n.* upataji; akili au elimu iliyopatikana kwa kujifunza au kwa kujitahidi.

**acquisition** /ˌakwɪ'zɪʃ(e)n/ *n.* **1.** kupata **2.** pato; yaliyopatikana kwa bidii au kwa bei kubwa; tunu. **acquisitive** *adj.* -enye nia ya kupata.

**acquit** /ə'kwɪt/ *v.t.* **(-tt-)** **1.** hukumu kuwa mtu hana hatia katika jambo aliloshitakiwa; acha huru. **2.** ~ *oneself well,* tenda kwa uhodari; fanya kazi vizuri, etc. **~tal** *n.* toa hatiani kisheria.

**acrobat** /'ækrəbæt/ *n.* mwana-sarakasi anayetumia viungo vya mwili kama vile kutataga kamba iliyonyooshwa kwenye nguzo mbili etc. **~ics** *n.* sarakasi; michezo ya ustadi.

**across** /ə'krɒs/ *adv./prep.* toka upande huu mpaka upande wa pili (wa); ng'ambo (ya).

**act** /ækt/ *v.t./ i.* tenda; fanya; cheza; jifanya; igiza.~ *as,* wakilisha; kaimu. ~ *upon,* fuata. ~ *(up)on,* vuta; geuza; endesha. -*n.* **1.** tendo. *in the ~ of stealing,* katika tendo la wizi. **2.** sheria. **~ing** *adj.* kaimu. *the ~ manager.* **~or** *n.* mwigizaji. **~tress** *n.* mwigizaji wa kike. **~ion** *n.* **1.** kitendo; kufanya; *a time for ~,* wakati wa kutenda; *a man of ~,* mtendaji. *out of ~,* mbovu. **2.** matokeo. *the ~ of the medicine,* matokeo ya kutumia dawa. **3.** tendo. **4.** mapigano; vita. *break off an ~*, acha kupigana. **5.** *(law)* daawa, madai. *bring an ~ (against),* dai. **~ive** *adj.* **1.** -enye juhudi; kakamavu. **~ immunity**, kinga amilifu: kinga ipatikanayo kwa chanjo. **~ transport**, mwendo wa dutu iliyoyeyuka katika seli, kutoka kwenye mmumunyo zimulifu kuelekea kwenye mmumunyo kolezi. **2.** -a kufaa; -a kutumika. *on ~ service* (kwa askari) aliyekwenda kupigana vita. **3.** ~ *voice, (grammar)* kauli ya kutenda. **~ivity** *n.* ukakamavu; bidii; juhudi; shughuli; utendaji; harakati. *outdoor activities,* shughuli za nje.

**actual** /'æktʃuəl, -tʃʊəl/ *adj.* hasa; kweli; -liopo; halisi; hakika. **~ly** *adv.* hasa; kwa kweli.

**acute** /ə'kju:t/ *adj.* **1.** (kwa maumivu, etc.) -kali. **2.** -a akili. *an ~ brain,* akili kali. *an ~ observer,* mwenye macho makali (yasiyopitwa na kitu). **3.** (kwa ugonjwa) -kali. **4. ~ angle**, pembe-kali: yaani pungufu ya pembemraba.

**adapt** /ə'dæpt/ *v.t.* tengeneza; badili; rekebisha; geuza ili kufaa kusudi fulani. **~able** *adj.* rahisi kubadilika. **~ation** *n.* kubadilisha ili kufaa kusudi fulani.

**add** /æd/ *v.t./i.* jumlisha; ongeza; ongezeka. **~ition** *n.* kujumlisha; ongezeko. *in ~ (to),* zaidi; tena. **~ polymerisation**, upolimishaji jumuifu: utendanaji wa kikemikali ambapo molekuli za aina moja huungana kufanya aina mpya za molekuli ndefu. **~itional** *adj.* -a ziada. **~itive** *adj.* -enye kuhusu kujumlisha. *n.* kitu kilichoongezwa kwa kiasi kidogo katika kitu kwa madhumuni maalumu; e.g. rangi au kiungo katika chakula.

**adder** /'ædə(r)/ *n.* namna ya nyoka mdogo mwenye sumu. *puff-~ n.* swila; kifutu.

**addict** /'ædɪkt/ *v.t.* *~ed to* (kwa watu) -enye kushiriki, zoea, pendelea (hasa ubaya, e.g. madawa ya kulevya). *n.* mtu mzoefu (hasa kwa ulevi, desturi mbaya).

**address** /ə'dres/ *v.t.* **1.** andikia; tia anwani. **2.** hutubia. ~ *oneself to a piece of work,* jizatiti kufanya kazi. *n.* **1.** anwani. **2.** hotuba. *a man of pleasing ~,* msemaji mzuri. *pay one's ~es to,* jipendekeza kwa.

**adequate** /'ædɪkwət/ *adj.* -a kutosha; sawa; -a kukifu.

**adequacy** /'ædɪkwəsi/ *n.* hali ya kutosha au kufaa; kifu; utoshelevu.

**adhere** /əd'hɪə/ *v.t.* **1.** ambata; nata; kuganda. **2.** fuata; shika madhehebu. **~nce** *n.* ufuasi; ukereketwa. **~nt** *n.* mfuasi.

**adhesion** /əd'hi:ʒ(ə)n/ *n.* kunata; ufuasi. **adhesive** *adj.* -a kunata; -a kuganda.
**adjacent** /ə'dʒeɪs(ə)nt/ *adj.* -a karibu; -a jirani; -a kupakana.
**adjective** /'ædʒɪktɪv/ *n.* kivumishi: neno liongezalo maana ya jina; sifa.
**adjoin** /ə'dʒɔɪn/ *v.i.* pakana na; tangamana na; ungana na.
**adjourn** /ə'dʒə:n/ *v.t./i.* weka; ahirisha; chelewesha mpaka siku nyingine. **~ment** *n.* uahirisho.
**adjudicate** /ə'dʒu:dɪkeɪt/ *v.t./i.* amua; toa hukumu kama hakimu.
**adjudication** /əˌdʒu:dɪ'keɪʃn/ *n.* hukumu.
**adjust** /ə'dʒʌst/ *v.t.* panga; tengeneza; rekebisha. **~ment** *n.* rekebisho; upatanisho.
**administer** /əd'mɪnɪstə(r) *v.t.* **1.** tawala; simamia; amirisha shamba. **2.** amuru. **3.** -pa; toa. ~ *an oath to sb.*, apisha mtu. ~ *medicine*, -pa dawa.
**administration** /ədˌmɪnɪ'streɪʃn/ *n.* **1.** utawala; uongozi; usimamizi. **2.** serikali ya nchi. **administrative** *adj.* -enye kuhusu utawala. **administrator** *n.* mtu anayesimamia au kuangalia kazi; mtawala; kiongozi.
**admirable** /'ædmərəbl/ *adj.* -zuri; bora; -a kupendeza.
**admirably** /'ædmərəbli/ *adv.* vizuri; barabara.
**admiral** /'ædmərəl/ *n.* jemedari; mkuu wa mabaharia wa manowari.
**admire** /əd'maɪə(r)/ *v.t.* husudu,; penda; sifu. **admiration** /ˌæmə'reɪʃn/ *n.* kuhusudu kwema; sifa.
**admit** /əd'mɪt/ *v.t./i.* **(-tt-)** **1.** ruhusu kuingia; ingiza. ~ *sb. into a house*, ruhusu mtu kuingia nyumbani; pitisha. *windows to ~ light and air*, madirisha ya kupitisha mwanga na hewa. **2.** kiri; ungama; kubali. ~ *of*, acha nafasi kwa. *It ~s of no doubt*, hakuna shaka hata kidogo. **admissible** *adj.* -a kukubali; -a kufaa; - a halali. **admission** *n.* **1.** ruhusa ya kuingia. *admission free*, kiingilio bure. **2.** neno lililokiriwa (kuungamwa, kukubaliwa). **~tance** *n.* ruhusa ya kuingia. *No ~ except on business*, hapana kuingia bila shughuli.
**admonish** /əd'mɒnɪʃ/ *v.t.* onya; gombeza; rudi; karipia; kemea. **admonition** *n.* onyo la upole.
**adolescent** /ˌædə'lesnt/ *n./adj.* kijana mvulana au msichana.
**adolescence** /ˌædə'lesns/ *n.* ujana.
**adopt** /ə'dɒpt/ *v.t.* **1.** kumlea mtoto kwa kumfanya kama uliyemzaa; fanya mtoto wa kupanga. **2.** fuata au kutumia desturi, fikira, itikadi za mtu mwingine. **adoption** *n.* uleaji mtoto.
**adore** /ə'dɔ:(r)/ *v.t.* penda mno; husudu; abudia. **adorable** *adj.* -enye kustahiki kupendwa mno au kuabudiwa. **adoration** *n.* kupenda mno; uabudiaji.
**adorn** /ə'dɔ:n/ *v.t.* pamba; remba. **~ment** *n.* urembo; pambo.
**adrenal** /ə'dri:n(ə)l/ *n.* adrenali.
**adrenalin** /ə'drɛn(ə)lɪn/ *n.* adrenalini: homoni itokanayo na tenzi adrenali yenye kazi ya kurekebisha kiasi cha sukari na chumvi katika damu, pia husisimua mwili.
**adult** /'adʌlt, ə'dʌlt/ *n./adj.* mtu mzima (kwa umri); -pevu.
**adultery** /ə'dʌltəri/ *n.* uzinzi; zinaa.
**adulterate** /ə'dʌltəreɪt/ *v.t.* ghushi; haribu. **adulteration** *n.* ughushi; kughushi; kuharibu.
**advance** /əd'vɑ:ns/ *v.i./t.* **1.** endelea mbele; sogea; leta; endesha mbele. *Let me ~ my opinions*, wacha nitoe mawazo yangu. **2.** karidhi; •lipa kabla/tanguliza malipo; kopesha. *n.* maendeleo. *in ~ (of)*, mbele (ya). **3.** karadha, yaani mkopo usio na riba. **~d** *adj.* -enye maendeleo. **~ment** *n.* maendeleo.
**advantage** /əd'vɑ:ntɪdʒ/ *n.* heri; faida; nafuu. *take ~ of*, tumia (vizuri au vibaya), punja, ghilibu, laghai. *turn to ~*, tumia ili kujipatia faida. *seen to ~*, onekana vizuri. *to the ~ of*, ili kuleta faida. **~ous** *adj.* -a kufaa; -a kuleta faida.

**advent** /'adv(ə)nt, -vɛnt/ *n.* majilio; ujio: muda wa wiki nne kabla ya sikukuu ya krismasi.
**adventure** /əd'ventʃə(r)/ *n.* safari au jambo la kushangaza au la hatari; vituko; visa. **~r** *n.* mjasiri; mtu aliye tayari kufanya mambo ya hatari ili apate sifa au faida. **adventurous** *adj.* -a ujasiri; -enye hatari.
**adverb** /'ædvɜ:b/ *n.* kielezi: neno linaloongeza maana ya kitenzi, kivumishi, au kielezi.
**adversary** /'ædvəsəri/ *n.* adui; hasimu; mtesi; mshindani; mpinzani. **adverse** *adj.* -a uadui; -a hasama; -a utesi; -a ushindani; -a upinzani.
**adversity** /əd'vɜ:səti/ *n.* shari; msiba; jambo baya; taabu; mateso, shida; hasara; dhiki; maafa; masahibu.
**advertise** /'ædvətaɪz/ *v.t./i.* tangaza; vumisha habari za; tembeza; eneza sifa za. **~r** *n.* mtangazaji biashara fulani; mvumisha habari. **~ment** *n.* tangazo.
**advice** /əd'vaɪs/ *n.* ushauri; nasaha.
**advise** /əd'vaɪz/ *v.t.* onya; shauri; shawishi; asa; nasihi; arifu; julisha. *ill- ~d,* si -a akili. *well--d,* -a busara. **advisable** *adj.* -a busara; afadhali; heri; vyema; bora.
**advocate** /'advəkət/ *n.* mwombeaji; mteteaji; wakili. *v.t.* tetea; ombea.
**adze** /adz/ *n.* tezo; chetezo.
**aerate** /'ɛ:reɪt/ *v.t.* tia gesi ya asidi kabonia au nyingine.
**aerial** /ɛ:rɪəl/ *n.* eria; erio: kifaa cha kupokelea mawasiliano ya redio au televisheni. *adj.* -a angani.
**aero** /'ɛ:rəʊ/ *prefix* ya hewa. **~drome** *n.* kiwanja cha ndege. **~plane** *n.* ndege. **~nautical** *adj.* -a kuhusu ndege na uongozaji wake.
**aerobic** /ɛ:'rəʊbɪk/ *adj.* erobia: -enye kuhitaji oksijini ili kuishi. *~ respiration,* uvutaji pumzi unaotokea ndani ya seli na kutoa nishati kwa kutumia oksijeni; mazoezi ya viungo.
**aerodynamics** /ˌeərəʊdaɪ'næmɪks/ *n.* elimu mwendo anga; misogeo anga: sayansi ya hewa na jinsi inavyoathiri mwendo wa vyombo vinavyoruka angani.
**affable** /'æfəbl/ *adj.* -pole; -kunjufu; -enye utu mwema. **affability** /ˌæfə'bɪləti/ *n.* upole; ukunjufu; jamala.
**affair** /ə'feə(r)/ *n.* **1.** jambo; shughuli; kazi; kadhia. *It is not your ~,* hayakuhusu. **2.** **~s** *(pl.)* mambo; kazi; shughuli.
**affect**[1] /ə'fɛkt/ *v.t.* **1.** geuza; badili; athiri. *Our position will not be ~ ed by these events,* msimamo wetu hautaathirika kwa matukio haya. **2.** vutia. **~ing** *adj.* -a kuvutia sana. *~ing scenes,* matukio ya kusisimua sana.
**affect**[2] /ə'fɛkt/ *v.t.* jifanya; jisingizia; jidai. *~ ignorance,* jisingizia ujinga. **~ed.** /ə'fektɪd/ *adj.* -a kujisingizia; -a ugomvi. **~ation** *n.* tabia ya kujisingizia.
**affection** /ə'fekʃn/ *n.* **1.** upendo; mapenzi; huba; shauku. **2.** ugonjwa; uele; maradhi. **~ate** *adj.* -enye moyo wa kupenda.
**affiliate** /ə'fɪlieɪt/ *v.t./i.* shirikisha; pokea kuwa mshirika au mwana katika jamuia; shirikiana na. **affiliation** *n.* ushirikishaji mtu katika familia, chama au ushirika.
**affinity** /ə'fɪnəti/ *n.* ukaribu; ujamaa; udugu; ukoo; ufananaji; mvuto.
**affirm** /ə'fɜ:m/ *v.t.* thibitisha; yakinisha. **~ation** *n.* uthibitisho.
**afflict** /ə'flɪkt/ *v.t.* umiza; tesa; huzunisha; dhuru; onea; dhulumu; sumbua; udhi; adhibu.
**affluent** /'æfluənt/ *adj.* tajiri.
**affluence** /'æfluəns/ *n.* utajiri.
**afford** /əfɔ:d/ *v.t.* **1.** weza. **2.** -pa; toa.
**afoot** /ə'fʊt/ *adv./adj.* kwa miguu; kuwa inaendelea. *There's mischief ~,* kuna mambo mabaya yanaendelea.
**afraid** /ə'freɪd/ *adj. (be)* ogopa; hofu; tishika.
**afresh** /ə'freʃ/ *adv.* tena; upya.
**aft** /ɑ:ft/ *adv.* -a nyuma; karibu sana au kuiendea tezi ya chombo.
**after** /'ɑ:ftə(r)/ *adv.* baadaye; halafu;

nyuma ya. -*conj.* tena; kisha. **~birth** *n.* kondo; kuu: ogani ya mamalia inayounganisha mfumo wa lishe wa mama na ule wa mtoto wakati wa mimba, hivyo kumwezesha kula na kuchuja takataka.

**afternoon** /ˌɑ:ftə'nu:n/ *n.* alasiri.

**afterwards** /'ftəwədz/ *adv.* baadaye; hatimaye; mwishowe; halafu.

**again** /ə'gɛn, ə'geɪn/ *adv.* tena; mara ya pili.

**against** /ə'gɛnst, ə'geɪnst/ *prep.* dhidi ya; juu ya; kushindana na; kukabili; karibu na. *provide ~ hunger,* weka akiba dhidi ya njaa.

**agar** /'eɪga:/ *n.* agaa: dutu inayofanana na jelatini ipatikanayo kwenye mwani mwekundu inayohusiana kikemikali na kabohidreti.

**age** /eɪdʒ/ *n.* umri; zama; enzi. *come (be) of ~,* kua, baleghe. *the stone age,* enzi ya zana za mawe. **1.** *(colloq.)* muda mrefu. *We've been waiting for ~s,* tumengoja mno. **~d** *adj.* - enye umri wa. *a boy ~ five,* mtoto wa umri wa miaka **2.** *an ~ man,* mzee. **~less** *adj.* -a milele; -a dahari.

**agency** /eɪdʒənsi/ *n.* kazi au ofisi ya wakala; uwakala.

**agenda** /ə'dʒɛndə/ *n.* ajenda: orodha ya mambo yaliyokusudiwa kujadiliwa katika mkutano.

**agent** /'eɪdʒənt/ *n.* wakala wa mtu au shirika. *house~,* wakala wa nyumba. *shipping or forwarding ~,* wakala wa meli au wa kusafirisha bidhaa.

**aggravate** /'ægrəveɪt/ *v.t.* kuza; athiri zaidi.

**aggregate** /'agrɪgət/ *n./adj.* jumla -ote. *in the ~,* -ote pamoja; kwa jumla.

**aggression** /ə'greʃn/ *n.* shambulio; chokochoko; uchokozi unaoweza kusababisha vita.

**aggressive** /ə'gresɪv/ *adj.* -gomvi, -shari, enye kutaka maendeleo ya haraka. **aggressor** /*n.* mgomvi; mshari; mchokozi.

**aggrieve** /ə'gri:v/ *adj.* dhuru; athiri; udhi; tia uchungu; sikitisha. *feel ~d,* hisi kuwa umetendewa vibaya.

**agile** /'ædʒaɪl/ *adj.* -epesi wa mwendo. **agility** *n.* wepesi wa mwendo.

**agitate** /'ædʒɪteɪt/ *v.t./i.* tikisatikisa; koroga; harakisha; *~ for,* chochea.

**ago** /ə'gəʊ/ *adv.* zamani. *a little while ~,* punde hivi; *ten days ~,* siku kumi zilizopita.

**agony** /'ægəni/ *n.* uchungu; maumivu makali. **agonizing** *adj.* -a kuumiza sana.

**agree** /ə'gri:/ *v.t.* patana; kubaliana; ridhiana; afikiana. **~able** *adj.* -a kupendeza; -zuri; -tamu; -a kukubalika, -a kuridhisha. **~ment** *n.* mapatano; mkataba; maafikiano; ulinganifu; itifaki; makubaliano.

**agriculture** /'ægrɪkʌltʃə(r)/ *n.* kilimo; ukulima; elimu ya kilimo.

**agrochemical** *n.* kemikali inayotumika katika shughuli za kilimo.

**ahead** /ə'hed/ *adv./adj.* mbele (ya). *(colloq.) go ~,* songa mbele.

**aid** /eɪd/ *v.t./n.* saidia ; auni; msaada.

**AIDS** /eɪdz/ *n.* (ufupisho wa *Acquired Immune Deficiency Syndrome)* maradhi ya ukosefu wa kinga mwilini (UKIMWI) yanayosababishwa na virusi vinavyoambukizwa hususan kwa njia ya kujamiiana.

**ail** /eɪl/ *v.t./i.* ugua; umwa; gonjwa; taabika; sumbuliwa. *What ~s him?* anaumwa na nini? **~ment** *n.* ugonjwa.

**aim** /eɪm/ *v.t/i.* **1.** tunga shabaha; lenga. **2.** kusudia; taka; tamani; azimu. *n.* shabaha; kusudi; nia; azma. **~less** *adj.* bila lengo.

**air**[1] /eə(r)/ n. **1.** hewa; anga; upepo. **2.** *by ~,* kwa ndege. *~ force,* jeshi la anga. *on the ~,* kwa simu ya upepo. *~ what's on the ~ this evening?* kuna habari gani hewani jioni hii? **3.** haiba; wasifu; sura. *He has the ~ of being deaf,* ana sura ya uziwi. *put on ~s,* takabari; -wa na madaha; -enye kiburi; jifaharisha. *v.t.* **1.** anika. **2.** acha hewa kuingia. **3.** eleza wazo kwa watu wengine.

**air**[2] /eə(r)/-*prefix*. **~borne** /'eəbɔ:n/ *adj*. (kwa ndege) -lioanza kuruka hewani; (kwa watu, askari etc.) -liosafirishwa kwa ndege. **~-conditioned** *adj*. (kwa vyumba au magari) sehemu iliyotengenezwa kuwa na hewa baridi. **~craft** *n*. ndege. **~line** *n*. shirika la ndege. **~liner** *n*. ndege kubwa ya kuchukulia abiria. **~man** *n*. rubani wa ndege. **~ pollution**, uchafuzi wa hewa: uingizaji wa vitu vyenye madhara katika angahewa. **~port** *n*. uwanja wa ndege. **~ pressure**, kanieneo ya hewa: kani inayotolewa na chembe za hewa kwenye kizio kimoja cha eneo. **~ resistance**, ukinzani hewa: ukinzani unaosababishwa na kani ya hewa kwenye vitu vinavyotembea katika hewa. **~screw** *n*. rafardha ya ndege. **~ship**, purutangi: puto kubwa lenye injini kwa ajili ya kubebea watu au mizigo.


**aircraft**

**aisle** /aɪl/ *n*. ujia baina ya safu za viti, hasa kanisani kwa marefu.

**alarm** /ə'lɑ:m/ *n*. **1.** kamsa; indhari; tahadhari: sauti au dalili ya kuashiria kuwepo kwa hatari karibu; king'ora cha kuonyea watu. ~ *clock*, saa yenye kengele. **2.** hofu; wasiwasi; mshtuko. *v.t.* piga king'ora; toa indhari; hadharisha.

**alas** /ə'læs/ *int*. ole!

**albino** /al'bi:nəʊ/ *n*. zeruzeru.

**album** /'ælbəm/ *n*. albamu: kitabu cha kuhifadhia picha, etc.

**alchemist** /'alkɪmɪst/ *n*. mkemia aliyeishi mnamo karne ya 12 na 17 aliyejaribu kugeuza metali za msingi kuwa dhahabu au dawa ya uhai wa milele.

**alcohol** /'ælkəhɒl/ *n*. **1.** alkoholi; pombe. **2.** *(chem.)* jamii ya vitu vyenye alkoholi. **~ fermentation**, uvundikaji alkoholi: uwezo wa baadhi ya bakteria au hamira wa kuvunjavunja wanga au sukari na kuwa na nguvu ya kileo. **~ic** *adj*. -a vileo.

**ale** /eɪl/ *n*. aina ya pombe nyepesi.

**alert** /ə'lɜ:t/ *adj*. -epesi; -a tayari; -a macho; makini.

**alga** /'alg:ə/ *n*. mwani.

**algae** /'ældʒi:; 'ælgi:/ *n*. mwani: aina ya mimea inayoishi majini yenye kemikali ya klorofili ambayo haina mfumo changamano wa uzazi pia hufanya usanisinuru.

**algebra** /'aldʒɪbrə/ *n*. aljebra: hesabu zinazotumia herufi na alama nyingine badala ya tarakimu.

**algorithm** /'ælgərɪðəm/ kawaida au utaratibu wa mfumo wa kanuni zinazotumika kupatia ufumbuzi jibu, hasa kwa kompyuta.

**alibi** /'alɪbʌɪ/ *n*. kisingizio cha kudai kuwa mtu anayeshtakiwa kwa kosa fulani hakuwepo wakati kosa lilipotendeka.

**alien** /'eɪliən/ *adj*. **1.** -geni. **2.** ~ *to*, -enye tabia zisizokuwa sawa na. *n*. mgeni.

**alight**[1] /ə'laɪt/ *adj*. **1.** *(be)* waka; ng'aa meta; meremeta. *(fig.) face(s) ~ with happiness*, -enye uso uonyeshao furaha.

**alight**[2] /ə'laɪt/ *v.i.* shuka; teremka; tua. *The bird ~ed on a branch*, ndege alitua juu ya tawi.

**align** /ə'laɪn/ *v.t.* weka au panga katika mstari ulio sawa.

**alike** /ə'laɪk/ *adj*. sawasawa; -enye kufanana.

**aliment** /'alɪm(ə)nt/ *n*. chakula. **~ary** *adj*. -enye kuhusiana na chakula. **~ canal** *n*. njia ya chakula.

**alive** /ə'laɪv/ *adj*. **1.** -zima; hai. **2.** *be ~ to*, tambua; ona; angalia; jua.

**alkali** /'alkəlʌɪ/ *n*. alkali: kemikali inayoyeyuka kwenye maji na kuteza nguvu ya asidi na hivyo kutengeneza chumvi. **~ metals**, metali za alkali: jamii ya metali zenye valensi moja ambazo ni liti, natiri, kali, rubidi, na sizi. **~ne** *adj*. -a alkali: -enye tabia za alkali, yaani kinyume cha asidi. **~ earth metals**, metali ardhi za alkali: jamii ya metali zenye valensi mbili




ambazo ni berili, magnesi, kalisi, stronti, bari, na radi.

**alkaloid** /'alkəlɔɪd/ *n.* alkaloidi: namna ya kemikali kali yenye asili ya kemikali za miti kama vile muarobaini.

**alkane** /'alkɪn/ *n.* alkani: jina la misombo yenye muungo maradufu au zaidi. kama mitheni, itheni na propeni.

**alkene** /'alki:n/ *n.* alkeni· jina la misombo yenye muungo maradufu au zaidi. e.g. ethilini na propini.

**alkyd** /'alkɪd/ *n.* aina ya rezini sanisia zinazotengenezwa kwa asidi na alkoholi.

**alkyl** /'alkʌɪl, -kɪl/ *adj.* -enye kutokana na alkani.

**alkyne** /'alkʌɪn/ *n.* aina ya hidrokaboni ya fungu la asetilini.

**all** /ɔ:l/ *adj.* -ote. *adv.* pia; kabisa. *at ~,* hata kidogo. *(colloq.) He is ~ there,* yu macho; tayari. *pron.* -ote.

**allege** /ə'lɛdʒ/ *v.t.* toa hoja; toa shutuma; dai kuwa jambo ni kweli; *~ that sb. is a thief,* dai kuwa fulani ni mwizi.

**allegation** /ælə'geɪʃn/ *n.* madai; ushahidi; hoja.

**allegiance** /ə'li:dʒəns/ *n.* utii umpasao raia kwa mtawala wa nchi.

**allele** /'ali:l/ *n.* alele: mojawapo ya jeni yenye muundo mbadala baada ya kubadilika kimaumbile, huwepo katika sehemu moja mahsusi katika chembeuzi na hivyo kuathiri urithishaji.

**allergy** /'alədʒi/ *n.* mzio: hali ya kudhuriwa na kitu kwa kukila, kukigusa au kukinusa.

**alleviate** /ə'li:vɪeɪt/ *v.t.* ondoa; tuliza; punguza; nyamazisha ukali wa maumivu.

**alley** /'æli/ *n.* njia ndogo katika mji; kichochoro.

**alliance** /ə'laɪəns/ *n.* ushirikiano; muungano.

**alligator** /'æl'ge'tə(r)/ *n.* namna ya mamba ambao hupatikana sana Marekani.

**alliteration** /əˌlɪtə'reɪʃn/ *n.* utokeaji wa sauti au herufi zifananazo mwanzoni mwa maneno mengi e.g. *ki*tu *ki*kubwa *ki*lichoanguka *ki*likatika.

**allocate** /'æləkeɪt/ *v.t.* gawanya.
**allocation** *n.* mgao.

**allot** /ə'lɒt/ *v.t.* *(-tt-)* gawanya.
**~ment** *n.* mgao hasa wa kipande cha shamba au kikataa.

**allotrope** /'alətrəʊp/ *n.* umbo mojawapo miongoni mwa maumbo mengi ya elementi moja.
**allotropy** *n.* kuwepo kwa maumbo zaidi ya moja ya elementi ya kemikali katika hali moja, hasa gesi.

**allow** /ə'laʊ/ *v.t./i.* **1.** ruhusu. *Smoking is not ~ed,* hairuhusiwi kuvuta sigara. **2.** kubali kutoa (fedha, nafasi). *~ a child thousand shillings a week,* kumpa mtoto shilingi elfu kwa wiki. **3.** *~ for,* kumbuka na kuweka tayari; acha nafasi ya kutosha. **~ance** *n.* posho. *make ~ for,* chukulia. *We must make ~ for this youth,* inatupasa tumchukulie kwa vile ni kijana.

**alloy** /'alɔɪ/ *n.* mchanganyiko wa

metali mbili au zaidi. *v.t.* changanya madini.

**alluvial** /ə'lu:viəl/ *adj.* -a matope ya mito. **~ soil**, udongo tope: udongo uliosombwa na maji na kutuamishwa kwenye bonde.

**alluvium** /ə'l(j)u:vɪəm/ *n.* matope yaliyosombwa na kuachwa na maji ya mto.

**ally** /'alʌɪ/ *v.t.* **1.** ungana; shirikiana. *countries which were allied*, nchi zilizokuwa zimeshirikiana. **2.** wiana; lingana; fanana. *n.* rafiki; mtani. **allied** *adj.* -liounganishwa kwa mapatano; mtani.

**almighty** /ɔ:l'maɪti/ *adj.* -enye nguvu zote. *The ~, God.*, Mwenyezi Mungu.

**almost** /'ɔ:lməʊst/ *adv.* karibu sana; nusura; takriban.

**alone** /ə'ləʊn/ *adv./adj.* pekee; pweke.

**along** /ə'lɒŋ/ *prep./adv.* **1.** kwa mbele; katika. **2.** *~ with*, pamoja na. *adv. come ~*, haya njoo! *all ~*, wakati wote. *~side /adv./prep.* mbavuni; kando (ya), karibu (ya). *go alongside (of ship, jetty*, etc.), karibia; ambaa.

**aloud** /ə'laʊd/ *adv.* kwa sauti kubwa; kwa makelele.

**alpha** /'alfə/ *n.* herufi ya kwanza ya alfabeti ya Kiyunani. **~ particle**, chembe alfa: atomu ya heliumu iliyopoteza elektroni mbili. **~ radiation**, mkondo wa mnururisho wa chembe alfa unaokwenda kwa kasi ya ya mwangaza.

**alphabet** /'ælfəbet/ *n.* alfabeti; abjadi: herufi za lugha zilizopangwa katika utaratibu wa kawaida, yaani *a, b, ch, d*, etc. **~ic(al)** *adj. in ~ order*, kwa mpangilio wa alfabeti.

**alpine** /'ælpaɪn/ *adj.* -a kuhusu milima ya *Alps* au milima mirefu.

**already** /ɔ:l'redi/ *adv.* tayari. *It is done ~*, tayari imekwishafanyika.

**also** /'ɔ:lsəʊ/ *adv.* na; tena; vilevile; pia; aidha.

**altar** /'ɔ:ltə, 'ɒl-/ *n.* **1.** madhabahu; altari. *lead a woman to the ~*, kuoa. **2.** (katika kanisa la kikristo) meza panapotolewa ushirika mtakatifu.

**alter** /'ɔ:ltə, 'ɒl-/ *v.t./i.* badili; geuza; badilika; geuka.

**altercation** /ˌɔ:ltə'keɪʃn/ *n.* ugomvi; ubishani wa maneno makali; mzozo.

**alternate** /'ɔ:ltəneɪt/ *adj.* -a zamu kwa zamu; -a moja baada ya nyingine. *They met on ~ days*, walikutana kila baada ya siku moja. *v.t./i.* **1.** (kwa vitu vya namna mbili) kuja, fanya, tia, panga kwa zamu; badili (kitu kimoja) kwa kingine. *Wet days ~d with sunny days*, siku za mvua zilipishana na siku za jua. *~ kindness with severity*, fuatisha upole kwa ukali. **2.** (kwa vitu viwili) fuatana. *alternating current*, mkondo geu: mkondo wa umeme unaobadilika kwa zamu, huenda na kurudi katika mbembeo mmoja.

**alternative** /ɔ:l'tɜ:nətɪv/ *adj.* -a kuchagua baina ya vitu viwili. *n.* hiari ya mambo mawili; uwezekano mwingine. *I had to go; there was no alternative*, ilinilazimu kwenda kwani sikuwa na njia nyingine.

**alternator** /ɔ:ltəneɪtə(r)/ *n.* kigeuzio: chombo kinachogeuza umeme kutoka mkondo mmoja kwenda mkondo mwingine.

**although** /ɔ:l'ðəʊ/ *conj.* ijapokuwa; ingawa; juu ya hayo.

**altitude** /'æltɪtju:d/ *n.* urefu wa kwenda juu; kimo.

**altogether** /ˌɔ:ltə'geðə(r)/ *adv.* **1.** pamoja; kwa jumla. *I will take them ~*, nitavichukua kwa pamoja. **2.** hasa; kabisa. *It's ~ untrue*, ni uongo kabisa.

**aluminium** /al(j)ʊ'mɪnɪəm/ *n.* alumini: metali nyepesi kama fedha inayotumiwa kusafirishia umeme kwenye njia kuu; metali itengenezewayo vyombo kama masufuria.

**alveolus** /al'vɪələs, ˌalvɪ'əʊləs/ *n.* kijiribahewa: kifuko kidogo cha hewa.

**amalgamate** /ə'malgəmeɪt/ *v.t./i.* unganisha; changanya madini au

vitu; ungana.
**amass** /ə'mæs/ *v.t.* hodhi; limbikiza (hasa mali).
**amateur** /'amətə,-tʃə,-tjʊə, ˌamə'tə:/ *n.* ridhaa; mtu atendaye kazi ya ufundi au sanaa kwa mapenzi, si kwa nia ya pato au mshahara; mwanamichezo asiyetarajia malipo. **~ish** *adj.* si stadi sana.
**amaze** /ə'meɪz/ *v.t.* staajabisha; shangaza; fadhaisha; shtusha.
**ambassador** /æm'bæsədə(r)/ *n.* mjumbe; balozi anayeiwakilisha nchi yake katika mataifa ya nje.
**amber** /'æmbə(r)/ *n.* kaharabu; namna ya gundi iliyogeuka kama jiwe yenye rangi ya manjano.
**ambiguity** /ambɪ'gju:ɪti/ *n.* utata; utatanishi; maana isiyo dhahiri au inayofahamika kwa namna tofauti.
**ambiguous** /am'bɪgjʊəs/ *adj.* -enye utatanishi.
**ambition** /æm'bɪʃn/ *n.* juhudi au tamaa ya umaarufu, utajiri, cheo au heshima.
**ambulance** /'æmbjələns/ *n.* ambulensi: gari ya kuchukulia wagonjwa.
**ambush** /'æmbʊʃ/ *n.* uoteaji; uviziaji. *v.t./i.* otea njiani; vizia kwa siri; shambulia ghafla kutoka mafichoni.
**ameliorate** /ə'mi:lɪəreɪt/ *v.t./i.* tengeneza au fanya bora zaidi; -wa bora; tengeneza; boresha.
**amen** /a:'mɛn,eɪ-/ *n./int.* amin; iwe kama ilivyoombwa.
**amenable** /ə'minəb(ə)l/ *adj.* (kwa watu) -sikivu; -epesi kuongozwa au kushawishiwa.
**amend** /ə'mend/ *v.t./i.* **1.** sahihisha; fanya bora zaidi; tengeneza. *You must ~ your ways,* lazima urekebishe mwenendo wako. **2.** badilisha sheria, kanuni, etc. **~ment** *n.* rekebisho la sheria, kanuni, marekebisho. etc. **~s** *n.* *make ~,* ridhisha; lipa; fidia.
**amenity** /ə'mi:nɪti,-'mɛn-/ *n.* **1.** uzuri. **2.** kitu kinachosaidia kuleta uzuri au furaha.
**amiable** /'eɪmiəbl/ *adj.* -a kupendeka; -pole; -ema.
**amiability** /eɪmiə'bɪl:ti/ *n.* ukunjufu; upole; tabia nzuri.
**amicable** /'amɪkəb(ə)l/ *adj.* -a urafiki; -a amani; -a upole.
**amino acids** /əˌmi:nəʊ 'æsɪd/ *n.* asidi amino: kampaundi ziundazo protini au asidi.
**ammeter** /'amɪtə/ *n.* amita; ameta: chombo cha kupimia ukali wa mkondo umeme katika ampea.
**ammonia** /ə'məʊnɪə/ *n.* amonia: aina ya gesi yenye harufu kali sana inayoyeyuka kwenye maji, hutumika kwa kusafishia.
**ammonite** /'amənʌɪt/ *n.* amoniti: aina ya fili, yaani mabaki ya viumbehai vilivyozikika ardhini miaka mingi iliyopita.
**ammonium** /ə'məʊnɪəm/ *adj.* -a amonia.
**ammunition** /ˌæmju'nɪʃn/ *n.* silaha, hasa risasi na baruti.
**amnesty** /'æmnəsti/ *n.* msamaha kwa watu walioikosea serikali.
**amnion** /'amnɪen/ *n.* utando unaozunguka kiinitete cha reptilia, ndege au mamalia ili kukihifadhi kɔabla ya kuzaliwa.
**amoeba** /ə'mi:bə/ *n.* amiba: aina ya protozoa ambaye huonekana kwa hadubini tu na mwenye uwezo wa kujibadilishabadilisha. **amoebic dysentry**, maradhi ya kuhara damu yanayosababishwa na aina fulani ya amiba.


amoeba (amiba)

**among(st)** /ə'mʌŋst/ *prep.* miongoni mwa; katikati ya; baina ya.
**amorphous** /ə'mɔ:fəs/ *n.* -siyokuwa na umbo wala sura maalumu.
**amount** /ə'maʊnt/ *v.i.* pata kiasi cha au kadiri ya. *n.* -ote pamoja; jumla; kiasi; kadiri; kima.
**amp** /æmp/ *n.* ampea: kizio cha kupimia mkondo wa umeme.
**ampere** /'ampɛ:/ *n.* ampea: kipimo cha nguvu ya umeme.
**amphibian** /æməfɪbiən/ *n.*


frog (chura) tortoise (kobe)
**amphibians**

**(amphibia)** **1.** mnyama awezaye kuishi nchi kavu na majini, kama chura na kobe. **amphibious** *adj.* -enye kuweza kuishi nchi kavu na majini pia. **2.**chombo kama nyambizi chenye sifa na uwezo wa kutembea baharini na nchi kavu.
**amphitheatre** /'æmfɪθɪətə(r)/ *n.* uwanda wa duara wenye viti vingi kuuzunguka wakaapo watu kutazama sanaa za maigizo.
**ample** /'æmpl/ *adj.* -kubwa; -enye nafasi kubwa; -a kutosha; -ingi; tele; maridhawa. *Thousand shillings will be ~ for my needs,* shilingi elfu zitanitosha kabisa kwa haja zangu.
**amplifier** /'æmplɪfaɪə(r)/ *n.* amplifaya: chombo kinachokuza au kinachozidisha, hasa sauti. **amplify** *v.t.* zidisha; kuza; ongeza.
**amplitude** /'æmplɪtju:d/ *n.* tambo: upeo wa bembeo.
**amputate** /'ampjʊteɪt/ *v.t.* kata kiungo cha mwili kwa sababu ya maradhi. **amputation** *n.* ukataji wa mguu au mkono, etc.
**amulet** /'amjʊlɪt/ *n.* talasimu; hirizi; kago; kinga.
**amuse** /ə'mju:z/ *v.t.* pendeza; chekesha; furahisha. **~ment** *n.* mazungumzo; maongezi; mchezo; tafrija; furaha; starehe; burudani.
**amylase** /'amɪleɪz/ *n.* kimeng'enyawanga: kimeng'enya kiwezacho kuvunjavunja wanga na kutengeneza sukari.
**anabolic** /ə'nabəlɪk/ *adj* -a uanaboli. **anabolism** *n.* uanaboli: hali ya jumla ya ujenzi wa kemikali mwilini.
**anaemia** /ə'ni:mɪə/ *n.* upungufu wa damu; kuwa na damu dhaifu; safura.
**anaerobic** /ˌæneə'rəʊbɪk/ *n.* -a anerobi: -enye kuhusu viumbe vyenye kuishi bila ya kutumia oksijeni. **~ bacteria** bakteria anayeweza kuishi bila ya kuwepo kwa oksijeni katika mazingira yake. **~ respiration** upumuaji usiohitaji oksijeni.
**anaesthesia** /ˌanɪs'θi:zɪə/ *n.* hali ya kutosikia maumivu; hali ya kutokuwa na hisia. **anaesthetic** *n.* -a ganzi, -a nusukaputi: -enye sifa ya kuondoa hisia.
**anagram** /'anəgram/ *n.* neno au sentensi iliyotungwa kwa kubadili taratibu za herufi za neno lingine e.g. *nina* na *nani.*
**analogy** /ə'nalədʒi/ *n.* **1.** ulinganifu; mfano; mithali. *The ~ between the heart and a pump,* mithali baina ya moyo na pampu. **analogous** *adj.* -a kulinganishika; -a mfano, -a kufanana.
**analyse** /'ænəlaɪz/ *v.t.* changanua; chambua; pambanua hoja mbalimbali katika mada fulani. **analysis** *n.* mchanganuo; uchambuzi.
**analyst** /'ænəlɪst/ *n.* mchambuzi, mchanganuzi.
**anarchy** /'ænəki/ *n.* ukosekano wa serikali katika nchi; machafuko katika shughuli za utawala. **anarchism** *n.* fikra ya kifalsafa ya kisiasa ya kuwa hakuna haja ya kuwepo serikali wala utawala. **anarchist** *n.* mtu afikiriye hivyo.
**anatomy** /ə'nætəmi/ *n.* elimu ya mwili na viungo vyake jinsi vilivyo kwa binadamu, wanyama na miti.
**ancestor** /'ænsestə(r)/ *n.* mzazi; babu; mtu wa kale. **ancestral** *adj.* -a wazazi, -a babu, ya nasaba. **ancestry** *n.* wazazi; ukoo; nasaba; jadi.
**anchor** /'æŋkə(r)/ *n.* nanga. *way ~,* ng'oa nanga. *lie (be, ride) at ~,* meli kukaa nangani. *v.t. /i.* tia nanga. **~age** *n.* mahali panapokaa meli; gatini.
**ancient** /'eɪnʃənt/ *adj.* **1.** -a kale; si -a siku hizi. *the ~ Greeks,* Wayunani wa kale. **2.** -zee sana.
**anecdote** /'anɪkdeʊt/ *n.* hadithi fupi; kisa; hekaya; ngano; kisa cha kuchekesha.
**anemone** /ə'nɛməni/ *n.* aina ya mti wenye maua ya rangi zing'arazo

na wenye majani yaliyoachana.
**aneroid barometer** /'anərɔɪd/ *n.* barometa aneroidi: ala ya kupimia kani eneo ya angahewa isiyotumia kioevu.
**angel** /'eɪndʒl/ *n.* malaika. **~ic** *adj.* ema tena -takatifu na - zuri.
**anger** /'æŋgə(r)/ *n.* hasira; ghadhabu; chuki; uchungu; ukali.
**angiosperm** *n.* anjispamu: jina la pamoja la miti inayotoa maua yenye mbegu.
**angle** /'æŋgl/ *n.* pembe. **~ of incidence**, pembe mtuo: pembe kati ya mwalimtuo na kisulubi kwenye nukta mtuo ya uso unaoakisi. **~ of reflection**, pembe mrudisho: pembe kati ya mwalimrudisho na kisulubi katika nukta panapotokea urudishaji. **~ of refraction**, pembe mchepuko: pembe kati ya mwalimchepuko na kisulubi katika nukta ya mwalimtuo kwenye mpaka wa midia.
**angry** /'æŋgri/ *adj.* -enye hasira. *be ~*, kasirika; ghadhibika; udhika; hamaki.
**angle**[1] /'æŋgl/ *n.* pembe; nukta inapokutana mistari miwili.



**angle | pembe**

**angle**[2] /'æŋgl/ *v.i.* vua samaki kwa ndoana na chambo. ~ *for, (fig.)* jaribu kupata kitu kwa hila au werevu.
**anglican** /'æŋglɪkən/ n./adj. -a kanisa la Kiingereza.
**anglicize** /'æŋglɪsaɪz/ *v.t.* fanya kitu kiwe cha Kiingereza.
**anglo** /'æŋgləʊ/ *-prefix* -a Kiingeza.
**anguish** /'æŋgwɪʃ/ *n.* uchungu; maumivu makubwa.
**anhydrous** *n.* kampaundi ya kemikali ambayo imepoteza maji, mfano wa mrututu uliochomwa au asidi.
**animal** /'ænɪml/ *n.* mnyama; hayawani; -a mwili si -a moyo wa mtu. ~ *needs*, mahitaji ya kimwili; ~ *spirits*, wingi wa afya nzuri; moyo wa kuchangamka na furaha.
**animate** /'anɪmeɪt/ *v.t.* changamsha; huisha; tia moyo. *A smile ~d her face*, uso wake ulijaa furaha. *The discussion was ~d*, majadiliano yalichangamka. **animation** *n.* wepesi; bidii; uchangamfu.
**animosity** /ˌanɪ'mɒsɪti/ *n.* chuki; uadui; uhasama.
**anion** /'anʌɪən/ *n.* **1.** anioni: atomi au molekuli iliyojiongezea elektroni na hivyo kubakia na chaji hasi. **2.** ioni yenye chaji hasi inayovutwa kwenye elektrodi yenye chaji chanya iitwayo enodi wakati wa elektrolisisi.
**ankle** /'æŋkl/ *n.* kifundo cha mguu.
**annelid** /'an(ə)lɪd/ *n.* anelida: moja ya faila ya minyoo wenye miili yenye tindi au iliyogawanyika kama nyungunyungu au mwata.
**annex** /ə'nɛks/ *v.t.* unganisha; nyang'anya na kuingiza kwenye milki (nchi au shamba). *n.* jengo dogo lililounganishwa na jengo kubwa; kipenu. **~ation** *n.* uchukuzi; unyanganyi.
**annihilate** /ə'nʌɪɪleɪt/ *v.t.* haribu kabisa; angamiza. **annihilation** *n.* maangamizi; uteketezaji; uharibifu mkubwa.
**anniversary** /ˌænɪ'vɜːsəri/ *n.* sikukuu ya ukumbusho wa jambo kila mwaka; maadhimisho.
**announce** /ə'naʊns/ *v.t.* tangaza; piga mbiu; onyesha; -wa dalili ya. **~r** *n.* mtangazaji. **~ment** *n.* tangazo.
**annoy** /ə'nɔɪ/ *v.t.* sumbua; udhi; kera; chokoza.
**annual** /'ænjuəl/ *adj.* **1.** -a kila mwaka. **2.** -a mwaka mmoja tu. -*n.* **1.** mmea unaoishi kwa mwaka mmoja kisha ukafa. **2.** jarida litokalo mara moja kila mwaka. **~ly** *adv.* kila mwaka.
**anode** /'anəʊd/ *n.* anodi: ncha chanya ambapo mkondo umeme huingilia kichanganuzi umeme.
**anoint** /ə'nɔɪnt/ *v.t.* paka mafuta au dawa ya mafuta, hasa kwenye matendo ya ibada ya kikristo kama

ubatizo au kutawazwa kwa mfalme.

**anonymous** /ə'nɒnɪməs/ *adj.* bila jina; -enye jina lisilojulikana na watu. ~ *gift*, zawadi iliyotolewa na mtu ambaye jina lake halijulikani; ~ *letter*, barua isiyotiwa jina.

**anopheles** /ə'nɒfɪli:z/ *n.* anofelesi: mbu wa jenera ya anofelesi ambaye anaweza kubeba viini visababishavyo malaria kwa mtu.

**answer** /'ɑ:nsə(r)/ *n./v.i.* jawabu; jibu; itika. ~ *back*, jibu kwa ujuba. ~ *a purpose*, tosha au faa. ~ *for*, pasiwa; stahili; ridhisha, lipia. ~ *to*, wa sawa na. ~ *to a description*, -wa sawa na sifa iliyotolewa. **~able** *adj.* -enye kuweza kujibiwa; -enye dhamana.

**ant** /ænt/ *n.* mdudu, mchwa: mdudu aishiye katika makundi/makoloni ya kijamaa, hana mabawa isipokuwa kipindi cha kuzaliana. Hujulikana kwa bidii yao ya kazi. *soldier* ~, chungu; *white* ~, mchwa; *brown* ~, siafu; **red ~**, maji moto; *small black* ~, sisimizi. **~-hill** *n.* kichuguu.

**antagonize** /æn'tægə'naɪz/ *v.t.* pinga; fanya mtu adui au hasimu yako.

**antagonist** /ænt'ægənɪst/ *n.* adui; mshindani, hasimu, mpinzani. **~ic** *adj.* -a uadui; -a upinzani; -a ushindani. **~ic muscle pair**, jozi ya misuli yenye mjongeo unaoelekea pande mbili tofauti kiasi kwamba unyweaji wa mmoja hutanua mwingine. **antagonism** *n.* chuki; uadui; upinzani; uhasama; ushindani.

**antarctic** /æn'tɑ:ktɪk/ *adj.* -a ncha ya kusini ya dunia.

**ante** /'anti/ *-prefix* mbele ya. **~date** *v.t.* **1.** tia tarehe katika barua au cheki kabla ya tarehe yake kufika. **2.** tangulia kwa wakati. **~natal** *adj.* -a kabla ya kuzaliwa. **~room** *n.* chumba kidogo kilicho na mwingilio wa kingine kikubwa.

**antecedent** /ˌantɪ'si:d(ə)nt/ *n.* **1.** *(grammar)* kisabiki: neno au fungu la maneno linalotangulia na kurejewa na kiwakilishi, kielezi au kirai fulani. **2.** *(pl.)* matendo, tabia, desturi na habari zilizokwisha pita za mtu au za watu.

**antelope** /'æntɪləʊp/ *n.* mnyama yeyote wa jamii ya paa, pofu, kulungu na palahala.

**antenna** /æn'tenə/ *n.* **1.** antena, erio: chombo kinachorusha au kupokea mawimbi ya redio au televisheni kutoka angani. **2.** papasi jozi za wadudu katika jamii ya anthropodi.

**anthem** /'ænθəm/ *n.* wimbo wa dini. *national* ~, wimbo wa taifa.

**anther** /'ænθə(r)/ *n.* chavulio: sehemu ya stameni ya ua yenye chavuo.

**anthology** /æn'θɑɒlədʒi/ *n.* diwani: mkusanyiko wa mashairi, kazi za fasihi na sanaa za maigizo.

**anthropology** /ˌanθrə'pɒlədʒi/ *n.* anthropolojia: elimu ya binadamu kuhusu historia ya asili, jamii na tamaduni zake.

**anti** /'ænti/ *-prefix* kinyume cha; kushindana na; kutopatana na. e.g. **~aircraft guns**, mizinga ya kupigia eropleni za kivita.

**antibiotic** /ˌæntibaɪ'ɒtɪk/ *n.* kiuavija, kiuavijasumu: kemikali inayoundwa na viumbe kama kuvu ambayo huweza kuangamiza bakteria au virusi au kuzuia ukuaji wake. **~ resistance**, tabia ya bakteria kutouliwa na dawa fulani kutokana na matumizi ya muda mrefu ya dawa hiyo.

**antibody** /'æntibɒdi/ *n.* zindiko; kinga; fingo: aina ya protini inayotengenezwa na mwili ili kujikinga. **~ positive**, hali ya kuwapo zindiko maalumu katika damu.

**anticipate** /æn'tsɪpeɪt/ *v.t.* **1.** fanya kabla ya wakati utazamiwao. **2.** fanya tendo kumtangulia mtu mwingine. **3.** tazamia mbele; tumaini; dhani.

**anticlockwise** /ˌænti'klɒkwaɪz/ *adj.* kinyumesaa: mwendo wa mzunguko kinyume cha mwendo wa saa.

**antics** /'æntɪks/ *n.* matendo ambayo mara nyingi hukusudiwa kuchekesha lakini yanaweza kuudhi pia; matendo ya furaha.

**antidote** /'æntidəʊt/ *n.* dawa

inayozuia dhara ya sumu. e.g. sumu ya chakula au nyoka.
**antigen** /'æntɪdʒən/ *n.* antijeni: protini ngeni ambayo husisimua utengenezaji wa fingo.
**antique** /æn'ti:k/ *adj.* -a kale. **antiquity** *n.* zama za kale.
**antiseptic** /ˌænti'septɪk/ *n./adj.* **1.** antiseptiki: aina ya kemikali inayozuia bakteria kuzaliana kwenye jeraha, ngozi, etc. **2.** -enye salama ya maambukizi.
**antithesis** /an'tɪθəsɪs/ *n.* kinyume; upinzani wa kifikra kwa hoja tofauti.
**antonym** /'antənɪm/ *n.* neno lililo na maana kinyume na lingine.
**anus** /'eɪnəs/ *n.* tundu ya kutolea kinyesi kwa binadamu au mnyama.
**anxiety** /æŋ'zaɪəti/ *n.* mashaka; wasiwasi; fadhaa; shauku. **anxious** *adj.* -enye mashaka; -enye shauku ya kufanya jambo au kupata kitu.
**any** /'eni/ *pron./adj.* *There is not ~,* hapana hata kidogo; sifuri; -ote; *~one, ~body,* yeyote.
**aorta** /eɪ'ɔ:tə/ *n.* mkole: ateri kuu ya damu safi inayoanzia upande wa kushoto wa moyo kwenda mwilini.
**apart** /ə'pɑ:t/ *adv.* mbali; mbalimbali; *~ from,* isipokuwa kwa; mbali ya.
**apartment** /ə'pɑ:tmənt/ *n.* nyumba iliyojengwa kwa kusudi la kupangishwa; chumba cha kupangisha.
**ape** /eɪp/ *n.* nyani. *v.t.* iga mambo na vitendo.
**aperture** /'apətʃə,-tj(ʊ)ə/ *n.* tundu; kidirisha; kipenyo.
**apex** /'eɪpeks/ *n.* kilele; ncha.
**aphid** /'eɪfɪd/ *n.* afidi: mdudu anayefyonza juisi kwenye mimea na ambaye anaweza kusambaza maradhi.
**aphorism** /'afərɪz(ə)m/ *n.* msemo mfupi wenye maana ya hekima na mazingatio; methali.
**apology** /ə'pɒlədʒi/ *n.* **1.** maneno ya kujitetea, ya kuomba radhi au msamaha. **2.** udhuru.
**apologize** /ə'pɒlədʒaɪʒ/ *v.i.* omba radhi; toa udhuru; kiri kosa; jitetea. **apologetic** *adj.* -a kujitetea; -a kuomba radhi.
**apostle** /ə'pɒsl/ *n.* mtume. **apostolic** *adj.* -a utume.
**apostrophe** /ə'pɒstrəfi/ *n.* alama hii (') katika maandishi.
**appal** /ə'pɔ:l/ *v.t.* tisha; fadhaisha; ogofya; shangaza.
**apparatus** /ˌapə'reɪtəs/ *n.* kifaa: chombo au jumla ya vyombo vitumikavyo katika jaribio la kisayansi au la kiufundi.
**apparent** /ə'pærənt/ *adj.* **1.** dhahiri; wazi. **2.** -a kuonekana. *The ~ cause but not the real one, was...,* sababu iliyoonekana lakini si sababu ya kweli, ilikuwa...
**apparition** /ˌæpə'rɪʃn/ *n.* mzuka; kivuli; njozi za majinamizi.
**appeal** /ə'pi:l/ *v.i.* **1.** omba; ita; sihi; lalama. **2.** kata rufaa. **3.** *~ to,* vuta macho; tia tamaa; tamanisha. *n.* **1.** tendo la kuomba. *an ~ for mercy,* omba kuonewa huruma. *~ to high court,* peleka kesi mahakama ya rufaa. **2.** mvuto; kutamanisha.
**appear** /ə'pɪə(r)/ *v.i.* **1.** onekana; fika; tokea; zuka. **2.** elekea kuwa. **~ance** *n.* tendo la kuonekana, la kuhudhuria; sura; wajihi; umbo; kivuli; mzuka.
**appease** /ə'pi:z/ *v.t.* tuliza; ridhisha; nyamazisha; suluhisha. **~ment** *n.* kitulizo, suluhu; mwafaka.
**append** /ə'pend/ *v.t.* tia au ongeza mwishoni. **~age** /ə'pendɪdʒ/ *n.* kilichotiwa mwishoni. **~ix** *n.* **1.** (-ices) kiambatisho, hasa mwisho wa kitabu. **2.** **(-ixes)** apendiksi: kibole kidogo kinachotokeza katika uchango wa tumbo.
**appendicitis** /ə'pendə'saɪtɪs/ *n.* ugonjwa wa apendiksi.
**appertain** /ˌapə'teɪn/ *v.i.* *~ to,* pasa; husu; fungamana.
**appetite** /'æpɪtaɪt/ *n.* uchu, hamu, hasa ya chakula. **appetizing** *adj.* -a kutamanisha; *(of food)* -a kuchapukia.
**applaud** /ə'plɔ:d/ *v.t./i.* shangilia kwa kupiga makofi, vifijo, hoihoi na vigelegele. **applause** *n.* vifijo; makofi; vifijo; vigelegele.
**apple** /'æpl/ *n.* tufaha.
**appliance** /ə'plaɪəns/ *n.*


apple

chombo; samani; ala; zana.
**applicant** /'æplɪkənt/ *n.* mdai; mwombaji.
**application** /ˌæplɪ'kəɪʃn/ *n.* ombi; ardhilhali; matumizi.
**apply** /ə'plaɪ/ *v.t./i.* omba; tumia; paka; husu. ~ *the break,* funga breki. ~ *a bandage,* funga bendeji. ~ *oneself to,* shiriki. **applied** *adj.* liotumiwa.
**appoint** /ə'pɔɪnt/ *v.t.* **1.** weka; amuru; chagua; agiza; teua. ~ *a secretary,* teua katibu. **~ment** *n.* uteuzi; wadhifa; cheo; madaraka; miadi.
**appreciable** /ə'pri:ʃəbl/ *adj.* -a kiasi cha kuonekana.
**appreciate** /ə'pri:ʃieɪt,-sɪ-/ *v.t./i.* husudu; thamini; tathmini; ongezeka au zidi thamani; shukuru. *He ~d his help,* alimthamini msaada wake. *This land has ~d greatly since 1940,* thamani ya shamba hili imezidi sana tangu mwaka wa 1940. **appreciation** *n.* shukrani; kuthamini; tathmini. **appreciative** *adj.* -enye shukrani.
**apprehend** /ˌæpri'hend/ *v.t.* **1.** fahamu; tambua. **2.** ogopa; hofu. **3.** kamata. **apprehension** *n.* kukamatwa. **apprehensive** *adj.* -enye hofu; -enye woga.
**apprentice** /ə'prentɪs/ *n.* mwanafunzi wa kazi *v.t.* fundisha. *bind as an ~,* chukua kama mwanafunzi. *I ~d him into a shoemaker,* nilimfundisha akawa mshona viatu.
**approach** /ə'prəʊtʃ/ *v.t./i.* **1.** karibia; sogelea; tongoza; kabili. **2.** endea kwa kuomba msaada. ~ *one's employer for higher pay,* kumkabili mwajiri kuomba uongezwe mshahara . *n.* kukaribia; njia; mbinu; mkabala.
**approbation** /ˌæprə'beɪʃn/ *n.* kibali; idhini; sifa nzuri.
**appropriate** /ə'prəʊpriət/ *adj.* -a kufaa. *v.t.* jichukulia, iba; nyang'anya; hodhi. **appropriation** *n.* kuchukua; kuiba; kunyang'anya; kuhodhi.
**approval** /ə'pru:vl/ *n.* kibali; idhini.
**approve** *v.t./i.* sifu; pendezwa na; kubali; idhinisha.
**approximate** /ə'prɒksɪmət/ *adj.* -a karibu sawa. *v.t./i.* karibia; kuwa karibu sawasawa; kisia. **approximation** *n.* ukisiaji.
**April** /'eɪprəl/ *n.* Aprili, mwezi wa nne wa mwaka wa kizungu.
**apron** /'eɪprən/ *n.* aproni: vazi maalumu la kuvalia mbele ili kufunika mavazi ya ndani yasichafuke wakati wa kufanya kazi, hasa wakati wa mapishi.
**aptitude** /'æptɪtju:d/ *n.* wepesi; welekevu; ustadi.
**aquarium** /ə'kweəriəm/ *n.* akwaria: tangi au hodhi la maji la kuwekea samaki wa kufuga au mimea.
**aqueduct** /'akwɪdʌkt/ *n.* akwidati; mferejidaraja; mfereji wa maji.
**aqueous** /'eɪkwɪəs/ *adj.* -a majimaji: -enye kuwa na maji kama kimumunyishaji. **~ humour,** ute maji: ute mwepesi wa jicho uliopo baina ya lensi na konea. **~ solution,** mmumunyo unaopatikana kwa kuyeyusha kitu katika maji.
**aquifer** /'akwɪfə/ *n.* akife: tabaka ya mwamba chini ya ardhi ambayo huhifadhi na kutoa maji.
**arable** /'ærəbl/ *adj.* -a kulimika kwa ardhi.
**arachnid** /ə'raknɪd/ *n.* araknida: jamii ya anthropoda inayojumuisha nge, buibui, chawa, kupe, kaa wakubwa, etc.
**arbitrary** /'a:bɪt(rə)ri/ *adj.* -siyofuata sheria wala kanuni au taratibu zinazokubalika. e.g. *an ~ decision,* hukumu iliyokatwa bila ya sababu nzuri. **~ units,** vizio hobela: vizio vya upimaji ambavyo havimo katika matumizi ya jumla nchini.
**arbitrate** /'ɑ:bɪtreɪt/ *v.t./i.* hukumu; amua; patanisha; suluhisha.
**arc** /a:k/ *n.* aki; tao: mkato au sehemu ya kizingo cha duara. **~-light** *n.* taa kubwa ya umeme ing'aayo sana.
**arch** /ɑ:tʃ/ *n.* tao. *a bridge with three ~es,* daraja lenye matao

matatu. *v.t./i.* jenga tao, -a kama tao. *The cat ~ed its back when it saw the dog,* paka alipinda mgongo wake kama tao alipomwona mbwa. **~way** *n.* tao. *adj.* -erevu, -enye hila, - janja.



arch

**arch** /ɑ:tʃ/ *prefix* -kuu. **~bishop** *n.* askofu mkuu. **~deacon** *n.* kasisi mkuu.

**archaeology** *n.* akiolojia: sayansi ya mambo ya kale ya mwanadamu itokanayo na utafiti wa mabaki ya kihistoria.

**archipelago** /ˌɑ:kɪ'peləgəʊ/ *n.* bahari yenye visiwa vidogo vingi.

**architect** /'ɑ:kɪtekt/ *n.* msanifu ujenzi: mhandisi achoraye ramani na kusimamia ujenzi. **~ure** *n.* usanifu ujenzi, ujenzi. **~ural** *adj.* -a ujenzi.

**archives** *n.* nyaraka: mahali pawekwapo kumbukumbu za maandishi.

**arctic** /'ɑ:ktɪk/ *adj.* -a ncha ya kaskazini ya dunia; *(colloq.)* baridi sana.

**ardent** /'a:d(e)nt/ *adj.* -enye bidii; juhudi; hamu.

**ardour** /'a:də/ *n.* shauku; bidii; juhudi.

**arduous** /'a:djʊəs/ *adj.* -gumu; -a kuchosha; -a taabu.

**area** /'eəriə/ *n.* eneo; uwanja.

**arena** /'ri:nə/ *n.* uwanja wa kuchezea ulio katikati ya amfithieta. *(fig.)* mahali pa kushindania.

**argon** /'ɑ:gɒn/ *n.* argoni: aina ya gesi inayotumiwa kwenye taa za umeme.

**argue** /'ɑ:gjiu:/ *v.i./t.* hoji. ~ *sb. into (out of) sth.,* kumshawishi mtu afanye (asifanye) kitu; shindana kwa maneno; jibishana.

**arid** /'arɪd/ *adj.* -kavu sana; -kame; kame; yabisi.

**arise** /ə'raɪz/ *v.i.* **(arose, arisen)** **1.** tokea. *A new difficulty has arisen,* tatizo jipya limetokea. **2.** toka; inuka; panda.

**aristocracy** /ˌærɪ'stɒkrəsi/ *n.* **1.** utawala wa makabaila. **2.** makabaila; ukabaila; umwinyi. **3.** waungwana kwa nasaba.

**arithmetic** /ə'rɪθmətɪk/ *n.* arithmetiki; hesabu; taaluma ya namba.

**ark** /ɑ:k/ *n.* safina kubwa iliyoundwa na mtume Nuhu wakati wa gharika kuu ili kujiokoa pamoja na jozi za wanyama wake; sanduku kubwa.

**arm** /ɑ:m/ *n.* **1.** mkono. **2.** *(pl.)* silaha. *in ~s,* -enye silaha. **3.** jeshi la askari wa nchi. *the air ~,* jeshi la anga. *the infantry ~,* jeshi la ardhini. **4.** *(pl.)* nembo itumikayo kuwa alama ya jamii, ukoo ulio bora au mji. *coat of ~s,* ngao ya taifa. *v.t./i.* **1.** -pa silaha; kaa tayari kwa vita. **2.** -pa kitu cha kulinda au cha kufaa. ~ *sb. with answers to likely questions,* kumpa mtu majibu ya maswali yanayoelekea kuulizwa. **~ament** *n.* **1.** kujitayarisha kivita au kijeshi; jeshi. **2.** zana za vita.

**armature** /'a:mətʃə, -tj(ʊ)ə/ *n.* amecha: misuko ya nyaya katika jenereta au mota ya umeme ambayo huzunguka katika uga wa sumaku.

**armistice** /'a:mɪstɪs/ *n.* mapatano ya kusimamisha vita kwa muda; amani.

**armour** /'ɑ:mərə(r)/ *n.* **1.** vazi la chuma la kivita ili kujikinga; silaha. **2.** kifaru.

**army** /'ɑ:mi/ *n.* **1.** jeshi; kundi kubwa. **2.** umati wa watu. *the salvation ~,* jeshi la wokovu.

**around** /ə'raʊnd/ *adv./prep.* pande zote (za); kandokando ya; kuzunguka karibu ya.

**arouse** /ə'raʊz/ *v.t.* chochea; ibua hisia; chapua.

**arrange** /ə'reɪndʒ/ *v.t.* **1.** tengeneza; ratibu. **2.** panga shughuli ya. ~ *a date for a meeting,* panga tarehe ya mkutano. **3.** patanisha; tuliza; suluhisha; amua.

**arrears** /ə'rəɪz/ *n.* kisicholipwa; deni; bakaa; kiporo. **2.** bakaa ya kazi au barua zinazohitaji kushughulikiwa.

**arrest** /ə'rest/ *v.t.* **1.** simamisha; zuia; kamata; dhibiti. **2.** vutia macho. *n.* kukamata. *make an ~*, kamata. **~ing** *adj.* -a kuvutia.
**arrive** /ə'raɪv/ *v.i.* **1.** fika; wasili. **2.** *~at*, patana; kubaliana; afikiana; fikia. **arrival** *n.* kufika; ufikaji; majilio.
**arrogant** /'ærəgənt/ *adj.* -enye kiburi; -enye majivuno; -enye maringo; -enye kunata; fedhuli; safihi.
**arrow** /'ærəʊ/ *n.* **1.** mshale. **2.** alama kama mshale. **arrowroot** *n.* uwanga.
**arsenal** /'ɑ:sənl/ *n.* ghala kubwa ya kutengenezea na kuhifadhia silaha na zana za kivita.
**arsenic** /'a:s(ə)nɪk/ *n.* asenia: aina ya kemikali nyeupe ya sumu inayotumika katika dawa nyingine kuulia panya etc.
**arson** /'ɑ:sn/ *n.* kuteketeza kwa moto nyumba au shamba za watu kwa kusudi la kuleta uharibifu.
**art** /ɑ:t/ *n.* sanaa; ustadi; ufundi; sanifu; werevu; ujanja. **~ful** *adj.* -erevu; stadi; -janja; -a kisanifu



artery

**artery** /'ɑ:təri/ *n.* ateri: mshipa wowote upokeao damu safi kutoka moyoni na ku-ipeleka kwenye tishu.
**artesian water** /a:'ti:zɪən,-z(ə)n/ *n.* maji yaliyohifadhiwa baina ya tabaka za mwamba chini ya ardhi.
**arthropods** /ˌa:θrə'pəʊds/ *n.* mnyama wa jamii ya wadudu, buibui, krustasia ambaye mwili wake una vipingili na viunzi vyao viko nje ya nyama.


arthropod

**article** /'ɑtɪkl/ *n.* **1.** kitu. **2.** makala. **3.** ibara; kifungu cha sheria au mkataba. **4.** *(grammar)* **a, n,** au **the.**
**articulate** *adj.* **1.** -enye kutamkwa vizuri; fasaha; dhahiri. **2.** -enye kudhihirisha fikira na maono kwa usemi dhahiri, bayana. *v.t./i.* sema; tamka; kwa dhahiri; fasaha, tena vizuri.
**articulation** /ɑ:tɪkjuleɪtɪʃn/ *n.* **1.** uungaji wa mifupa miwili katika kiungo. **2.** tendo la kusema; kutamka .
**artificial** /ˌɑtɪfɪʃl/ *adj.* si -a asili; si halisi; -a kubuni; -a uongo; -a bandia; -a kuigiza. **~ preservative**, kemikali inayozuia kuzaana wadudu waozeshao, na hivyo kutu-miwa kuzuia vyakula visioze. **~ satellite**, chombo chochote kilichoundwa kuzunguka sayari au nyota. **~ selection**, uzalishaji viumbehai kwa kuwakutanisha watu wenye sifa maalumu za kijeni.
**artillery** /a:'tɪləri/ *n.* mizinga; jeshi la mizinga.
**artisan** /'ɑ:tə'zæn, 'a:tɪzan/ *n.* fundi wa kazi za ujuzi wa mikono.
**artist** /'ɑ:tɪst/ *n.* fundi; msanii; stadi; mchoraji. **~ic** *adj.* -a sanaa; -a ufundi.
**as** /az, əz/ *adv.* **1.** kama. *as hard as iron*, -gumu kama chuma. *~ (like) me*, kama mimi. *~ you like*, kama upendavyo. *a thing such ~ a book*, kitu kama kitabu.
**asbestos** /ˌazbɛstɒs, as-, -təs/ *n.* asbestosi: kitu kama jiwe la nyuzinyuzi (kimefanana sana na pamba au katani iliyogandamizwa pamoja) kizuiacho moto na joto lisipenye, wala hakiunguwi.
**ascend** /ə'send/ *v.t./i.* paa; kwea; panda. **~ancy** *n.* nguvu au uwezo mwingi wa kushinda. *gain an ~ over one's enemies*, pata uwezo wa kuwashinda maadui. **~ant** *n.* -enye kushinda, bora. *in the ~*, -enye kuzidi kupata heshima na uwezo. **ascension** *n. the ascension*, kupaa mbinguni kwa Yesu Kristo. **ascent** *n.* upandaji; kilima; mwinuko. *the ascent of a mountain*, mwinuko wa mlima.
**ascertain** /ˌasə'təɪn/ *v.t.* hakikisha; yakinisha.
**ascorbic acid** /ə'skɔ:bɪk/ *n.* asidi

askobiki: vitamini C vipatikanavyo toka kwenye matunda, hukinga na pia hutibu hijabu.
**asexual** /ˌeɪ'sekʃuəl/ *adj.* siyohusiana na uke wala uume; **~reproduction** *n.* uzaliano nafsia: uzazi usiokuwa na muungano wa gameti za kike na za kiume, mfano hamira, nyuki na bakteria huzaliana namna hii.
**ash** /æʃ/ *n.* **1.** jivu; majivu.
**ashamed** /ə'ʃeɪmd/ *adj. (be)* ~, ona haya; aibika; tahayari; fedheheka; fadhaika.
**aside** /ə'saɪd/ *adv.* upande; kando; pembeni.
**ask** /ɑ:sk/ *v.t./i.* **1.** taka; omba; sihi; alika; karibisha. **2.** ~ *a question,* uliza; hoji.
**asleep** /ə'sli:p/ *adv./adj.* **1.** *(be)* ~, lala. **2.** (kwa viungo vya mwili) -fa ganzi.
**aspect** /'æspekt/ *n.* sura; umbo; wajihi; tabia; uso. *a house with a southern ~,* nyumba inayoelekea kusini.
**asphalt** /'asfalt, -əlt/ *n.* aina ya lami ngumu nyeusi itumiwayo kwa kutandazwa juu ya barabara.
**aspire** /ə'spaɪə(r)/ *v.i. (to)* taka sana; tamani.
**aspirin** /'æsprɪn; 'æspərɪn/ *n.* aspirini: dawa ya vidonge ya kutuliza maumivu na kuteremsha kiwango cha joto (homa) mwilini.
**ass** /as/ *n.* punda; mjinga; mpumbavu; juha. *Don't make such an ~ of yourself,* usijipumbaze.
**assassinate** /ə'sæsɪneɪt/ *v.t.* kuua kwa siri au kwa ghafula, kwa sababu za kisiasa au kidini.
**assault** /ə'sɔ:lt/ *v.t.* rukia; shambulia. -*n.* shambulio la ghafla.
**assemble** /ə'sembl/ *v.t./i.* kusanya; kusanyika; kutana; unganisha. **assembly** *n.* mkusanyiko; mkutano.
**assent** /ə'sɛnt/ *v.i./n. (to)* kubali; kiri; idhinisha; idhini; kibali.
**assert** /ə'sɜ:t/ *v.t.* tetea; shadidia; dai. *~ oneself,* jitokeza; jidai. **~ive** *adj.* -enye kushadidia; -nye kushikilia; -enye kudai.
**assess** /ə'ses/ *v.t.* kisia; kadiria; tathmini. **~ment** *n.* makisio; makadirio. **~or** *n.* mkadiriaji; mkisiaji.
**asset** /'æset/ *n.* mali ya mtu au kampuni yenye thamani maalumu.
**assiduous** /ə'sɪdjʊəs/ *adj.* -enye bidii nyingi ya kazi; -tendaji. **assiduity** *n.* bidii; juhudi.
**assign** /ə'ssɪn/ *v.t.* gawanyia; pangia. **~ment** *n.* kazi; jukumu linalopaswa kutimizwa kikamilifu.
**assimilate** /ə'sɪməleɪt/ *v.t./i.* fananisha; linganisha; ingiza katika utamaduni au dini mpya; (kwa mwili) tumia vizuri chakula. *His body cannot ~ potatoes,* viazi vinamdhuru. *food that ~s easily,* chakula kinachosagika upesi tena vizuri tumboni. **assimilation** *n.* mlishizo: shughuli zote za ubadilishaji chakula mwilini.
**assist** /ə'sɪst/ *v.t./i.* saidia; auni. **~ance** *n.* msaada; muawana. **~ant** *n.* msaidizi.
**associate** /ə'seəʊʃieɪt/ *v.t./i.* **1.** unganisha; shirikisha; husisha. *~ Egypt with the River Nile,* husisha Misri na Mto wa Nili. **2.** shirikiana na; ungana na. *n.* mtu anayeshirikiana na wenziwe katika kazi au shughuli; mshirika; mwenza; mbia. **association** *n.* muungano; jumuia; ubia.
**assorted** /ə'sɔ:tɪd/ *adj.* -a aina mbalimbali; -liochanganyika. **assortment** *n.* mkusanyiko wa vitu vya aina nyingi.
**assume** /ə'sju:m/ *v.t.* **1.** sadiki; pokea; chukulia kuwa kama ni kweli. **2.** shika; pata; twaa. **assuming** *adj.* - enye kiburi; -enye majivuno -enye kimbelembele. **assumption** *n.* dhana; tuhuma tu.
**assure** /ə'ʃʊe(r); *v.t.* hakikisha; thibitisha; yakinisha; toa hofu; ahidi. **~dly** *adv.* bila shaka. **assurance** *n.* matumaini; dhamana; bima.
**asterisk** /'æstərɪsk/ *n.* alama hii (*).
**astern** /ə'stɜ:n/ *adv.* shetrini; kwa nyuma; tezini.
**asteroid** /'astərɔɪd/ *n.* asteroidi: mojawapo ya sayari ndogondogo

zinazozunguka jua kwenye obiti za Mirihi na Sumbula.

**asthma** /'asmə/ *n.* ugonjwa wa pumu. **~tic** *adj.* -a pumu.

**astigmatism** /ə'stɪgmətɪz(ə)m/ *n.* uastigmati: kasoro ya macho inayofanya macho yote mawili yaone kitu kimoja kama viwili katika bapa tofauti.

**astonish** /ə'stɒnɪʃ/ *v.t.* ajabisha; shangaza; bumbuwaza; staajabisha. **~ment** *n.* ajabu; mshangao; mastaajabu; bumbuazi; butwaa.

**astray** /ə'streɪ/ *adv./adj. go ~*, potea; kosa; potoka.

**astride** /ə'straɪd/ *adv./adj.* kwa kutagaa mguu mmoja upande huu na mmoja upande huu.

**astrology** /ə'strɒlədʒɪ/ *n.* unajimu: sayansi ya mwendo wa sayari na nyota juu ya mahusiano yake na maisha watu.

**astronaut** /'æstrənɔ:t/ *n.* mwanaanga; astronoti: mtu aliyefundishwa kuendesha vyombo vya anga za juu kama roketi na setilaiti.

**astronomy** /ə'strɒnəmi/ *n.* astronomia: sayansi ya nyota na sayari. **astronomer** *n.* mtalaamu wa astronomia.

**asylum** /ə'saɪləm/ *n.* hifadhi; kimbilio; nyumba ambayo walemavu na maskini hutunzwa. *political ~*, hifadhi ya kisiasa.

**at** /ət/ *prep.* kwa; katika; kwenye; penye; -ni. **~ once**, mara moja; sasa hivi; halan. **~ all**, hata kidogo. *not ~ all*, sivyo kabisa; hasha! *~ length*, hatimaye; baadaye; mwisho; kwa ukamilifu.

**atheism** /'eɪθɪɪz(ə)m/ *n.* itikadi na imani kuwa hakuna Mungu muumba. **atheist** *n.* asiyesadiki kuwa Mungu yuko.

**athletic** /æθ'letɪks/ *adj.* **1.** -a michezo. **2.** -enye kupenda michezo. **~s** *n.* michezo. **athlete** *n.* mwanamichezo.

**atlas** /'ætləs/ *n.* atlasi: kitabu cha ramani.

**atmosphere** /'ætməsfɪə(r)/ *n.* **1.** angahewa; hewa; anga iliyoizunguka dunia. **2.** hali (njema, mbaya,) ambayo hutokea mahali. *an ~ of peace and calm*, hali ya amani na utulivu. **atmospheric** *adj.* -a hewa. **~ conditions**, hali ya hewa. **~ corrosion**, mbabuo angahewa: utendanaji wa metali, oksijeni na maji katika hewa, mfano chuma kuingia kutu. **~ pressure**, kanieneo angahewa: kanieneo inayotokana na gesi ya angahewa. **atmospherics** *n.* hali mbaya ya kama vile radi hewa inayoathiri mawasiliano na vyombo vya anga.

**atom** /'ætəm/ *n.* **1.** atomu; atomi: sehemu ndogo kabisa ya elementi ambayo bado inaonyesha tabia za kikemikali za elementi hiyo. **2.** chembe. *He hasn't an ~ of sense*, hana akili hata chembe. **~ic** *adj.* -a atomu, -a kuhusiana na atomu. **~bomb** *n.* bomu la atomiki. **~ energy**, nishati atomu: nishati iachwayo huru wakati wa utendanaji wa kiatomu ikiwa ni matokeo ya ugeuzaji wa masi kuwa nishati. **~ mass**, masi atomu: jumla ya masi ya protoni, nyutroni na elektroni. **~ mass unit** (amu), kizio cha masi atomu: kizio ambacho hutumika kuainisha uzani wa atomu na molekuli ambao ni sawa na moja ya thenashara ya masi ya kaboni -12. **~ number**, namba ya atomu: idadi ya protoni katika kiini cha atomu.

**atrium** /'eɪtrɪəm/ *n.* atiria: moja ya chemba mbili za juu ya moyo ipokeayo damu kutoka mishipani.

**attach** /ə'tætʃ/ *v.t.* **1.** fungasha; ambatisha;. **2.** kupa: *I ~ much importance to this*, nalipa umuhimu mkubwa jambo hili. **3.** fuatana na; ambatana na. *the advantages ~ing to the position of president*, faida ziambatanazo na cheo cha urais. *be ~ed to*, penda sana. **~ment** *n.* tanji: filisi mali ya mtu kufidia deni; pendo; huba; shauku; ashiki. **~é** *n.* msaidizi wa balozi.

**attack** /ə'tæk/ *v.t./i.* shambulia;

hujumu; shutumu; rukia. -n. shambulio; hujuma; shutuma. *He had a sharp ~ of fever,* alipigwa na homa kali.

**attain** *v.t./i.* fikia; pata. **~able** *adj.* -enye kufikika; -enye kupatikana. **~ment** *n.* upataji; pato.

**attempt** /ə'tempt/ *n./v.t.* jaribio; jaribu; jitahidi; bidii; juhudi.

**attend** /ə'tend/ *v.i./t.* **1.** angalia; sikiliza; hudumia; tumikia; hudhuria. **2.** *(as doctor, nurse)* uguza. **3.** fuatana na. *a method ~ed by great difficulties,* njia yenye mashaka makubwa. **~ance** *n.* mahudhurio; huduma. **~ant** *n.* mhudumu; mlinzi; mtumishi. *adj.* -a kufuatana na. *old age and its ~ evils,* uzee na udhaifu wake. **attention** *n.* uhudumu; utumishi; bidii; uangalifu; usikivu: *stand at ~,* simama wima kwa nidhamu. **attentive** *adj.* -angalifu; -sikivu.

**attitude** /'ætɪtju:d/ *n.* **1.** namna ya kusimama au kukaa; hali. **2.** namna ya kuona mambo, kufikiri au kufanya.

**attract** *v.t.* vutia; karibisha; tamanisha; pendeza; shawishi. *A magnet ~s iron,* sumaku huvuta chuma. **~ion** *n.* mvuto; mvutano; kivutio; kipendezacho. **~ive** *adj.* -a kupendeza, -a kuvutia, -a kutamanisha, -zuri.

**attribute** /ə'trɪbju:t/ *n.* **1.** sifa, dalili, au alama iliyo kiini cha tabia ya mtu au kitu. *Mercy is an ~ of God,* huruma ni sifa ya Mungu. **2.** *(grammar)* kiangama: kivumishi kinachoelezea zaidi nomino katika kundi nomino. *v.t.* sifia; wekea. **attributive** *adj.* *(grammar)* kivumishi kiangama: neno lililomo katika kikundi nomino lenye uamilifu wa kuvumisha. e.g. *'the old man', old* ni kivumishi kiangama.

**auction** /'ɔ:kʃn/ *n.* mnada.

**audible** /*adj.* -a kusikika. **audience** *n.* wasikilizaji; hadhira; baraza. **audio** *n.* sauti iliyorekodiwa kwenye kinasa-sauti.

**audit** /'ɔ:dɪt/ *v.t.* kagua hesabu. *n.* ukaguzi wa hesabu. **~or** *n.* mkaguzi wa hesabu.

**augment** /ɔ:g'mɛnt/ *v.t./i.* ongeza; ongezeka; zidisha; pandisha; kuza.

**August** *n.* Agosti: mwezi wa nane wa mwaka wa kizungu.

**aunt** /ɑ:nt/ *n.* shangazi; ndugu wa kike wa baba au mama.

**aural** /'ɔ:r(ə)l/ *adj.* - a sikio au usikizi.

**auspices** /'ɔ:spɪsɪz/ *n. pl.* msaada; fadhila; himaya. *under the ~ of,* kwa msaada wa. **auspicious** *adj.* heri, -a bahati.

**austere** /ɒ'stɪə, ɔ:-/ *adj.* -enye tabia ya kutopenda maisha ya raha au anasa. **austerity** *n.* ubahili; ugumu.

**authentic** /ɔ:'θentɪk/ *adj.* thabiti; halisi; -liojulikana kuwa kweli. **~ate** *v.t.* thibitisha kuwa ni kweli.

**author** /'ɔ:θə(r)/ *n.* **1.** mtunzi wa vitabu vya mashairi, michezo etc. **2.** Muumba.

**authority** /:θɑrəti/ *n.* **1.** amri; uwezo; amri; mamlaka. **2.** mtu mwenye maarifa yawezayo kusadikiwa juu ya jambo fulani. *He is an ~ in old coins,* ni mtu mwenye maarifa mengi juu ya sarafu za kizamani. **authoritative** *adj.* -enye amri au maarifa mengi. **authorize** *v.t.* ruhusu; idhinisha, amuru; halalisha. **authorization** *n.* ruhusa; amri; idhini; kibali; leseni.

**autobiography** /,ɔ:təbaɪ'ɒgrəfi/ *n.* habari za maisha ya mtu zilizoandikwa na yeye mwenyewe.

**automate** /'ɔ:ttəmeɪt/ *v.t.* dhibiti au ongoza kwa mitambo ya otomatiki inayojiendesha yenyewe.

**automatic** /,ɔ:tə'mætɪk/ *adj.* **1.** (kwa mashine) -a kujiendesha yenyewe. **2.** (kwa matendo) -liofanywa bila kufikiri. *Breathing is ~,* kuvuta pumzi hufanywa bila kufikiri.

**automobile** /'ɔ:təməbi:l/ *n.* gari; motakaa. **automotive** *adj.* -a kuhusu vipando vya moto.

**autonomous** /ɔ:'tɒnəməs/ *adj.* -enye uhuru wa kujitawala enyewe.

**auxiliary** /ɔ:g'zɪlɪəri,ɒg-/ *adj.* -a kuongeza nguvu; -a kusaidia. *n.* kisaidizi; msaidizi.

**avail** /ə'veɪl/ *v.t./i.* faa; weza. *~ oneself of,* tumia. *n.* faida, manufaa. **~able** *adj.* -a kutumika; -a kupatikana. **~ability** *n.* upatikanaji.

**avenge** /ə'vəndʒ/ *v.t.* lipiza kisasi.

**avenue** /'ævənju:/ *n.* **1.** njia yenye safu mbili za miti pembezoni mwake. **2.** *(fig.)* njia ya kufikia au kupatia jambo.

**average** /'ævərɪdʒ/ *n.* wastani. *adj.* **1.** -a wastani. **2.** -a kawaida. *~ speed,* kasi, mwendo wastani: kima cha wastani cha mabadiliko ya umbali na muda.

**averse** /ə'vɜ:s/ *adj.* *(to) be ~ to,* chukia; kutopenda. **aversion** *n.* uchukivu; kitu kisichopendwa; mtu achukiwaye sana.

**avert** /ə'vɜ:t/ *v.t.* kinga; epa; zuia; ambaza; pisha. *~ eyes, gaze,* etc. epa kutazama.

**Aves** /'eɪvi:z, 'a:veɪz/ *n.* nyuni: ngeli ya vetebrata pamoja na ndege ambao hutofautiana na wanyama wingine kutokana na manyoya yao na jamii ya karibu nao ya reptilia kwa kuwa na damu moto, mayai yenye magamba na wajihi mahususi kimofolojia.

**aviation** /ˌeɪvi'eɪʃn/ *n.* taaluma na ufundi wa kuongoza eropleni. **aviator** *n.* rubani wa ndege.

**Avogadro's law** *n.* kanuni isemayo kuwa mijazo ya gesi ikiwa katika halijoto na shinikizo sawa huwa pia na idadi sawa ya molekuli.

**avoid** /ə'vɔɪd/ *v.t.* epuka; ambaa; epa; bari.

**await** /ə'weɪt/ *v.t.* ngojea.

**awake** /ə'weɪk/ *adj./v.i./t.* *(awoke).* amka; amsha; zinduka. *He is ~,* yu macho.

**award** /ə'wɔ:d/ *n.* tunza; zawadi; *n.* *v.t.* toa zawadi; tunuku; tunza; hidaya.

**aware** /ə'weə(r)/ *adj.* *(be)* jua; fahamu; tambua; tanabahi.

**away** /ə'weɪ/ *adv.* mbali. *He has gone ~,* amekwenda zake. *He is ~,* hayupo. *He lives some distance ~ from here,* anakaa mbali kidogo kutoka hapa.

**awe** /ɔ:/ *n.* hofu itokanayo na kitisho au heshima kuu. *v.t.* tisha, ogofya. **~some** *adj.* -a kutisha; -a kustaajabisha. **awful** *adj.* **1.** -a kutisha. **2.** *(colloq.)* -baya sana.

**awhile** /ə'waɪl/ *adv.* kwa muda kidogo; kitambo.

**awkward** /'ɔ:kwəd/ *adj.* **1.** si -a kawaida; si -epesi kutumika; -a kuleta shida au hatari. *an ~ corner,* kona mbaya iwezayo kusababisha ajali. **2.** (kwa mtu au mnyama) -jinga; si stadi. **3.** -a kuleta au -enye matata.

**awl** /ɔ:l/ *n.* msharasi: chombo cha kutobolea vitundu vidogo hususan juu ya vitu vya ngozi.

**awning** /'ɔ:nɪŋ/ *n.* pazia; chandarua.

**axe** /æks/ *n.* shoka. v.t. punguza kazini kwa sababu ya ukosefu wa kazi au wingi wa wafanyakazi. **axillary bud** /ak'sɪlərɪ/ *n.* tumba kwapa: chipuko iliyoko kwenye kwapa ya jani.

**axis** /'aksɪs/ *n.* (axes) **1.** mhimili mkuu wa mzunguko, mstari unaounganisha kitovu cha lenzi na kitovu cha kivimbe cha lenzi. **2.** mstari unaopitia kwenye nukta kati ya kitu kinachozunguka. *The world revolves on its ~ once in twenty four hours,* dunia huzunguka katika mhimili wake mara moja kila saa ishirini na nne. **3.** jira: mstari wa wima au wa mlalo unaotumika katika grafu.

**axle** /'aks(ə)l/ *n.* ekseli: mti au chuma cha katikati ya gurudumu au magurudumu mawili ambapo gurudumu (au magurudumu) huzunguka.

# Bb

**babe** /beɪb/ *n.* **1.** mtoto mchanga. **2.** mtu asiye na hatia/asiyejiweza 3. mwanamke kijana.
**baboon** /bəˈbuːn/ *n.* nyani mkubwa.
**baby** /ˈbeɪbi/ *n.* mtoto mchanga.
**bachelor** /ˈbætʃələ(r)/ *n.* **1.** kapera. **2.** mtu aliyehitimu katika chuo kikuu na kutunukiwa shahada ya kwanza.
**bacillus** /bəˈsɪləs/ *n.* basila: bakteria wenye umbo la pau wanaofanya vibofu katika oksijeni huria.


**bacillus | basila**

**back** /bæk/ *n.* mgongo; sehemu iliyo nyuma. **~bone** *n.* uti wa mgongo: tindi za mifupa zilizoungana kutoka kisogoni mpaka kwenye nyonga. *adv.* nyuma; kinyume. *v.i./t.* **1.** enda au rudisha nyuma. *~ a car into a garage.* **2.** saidia. **~down**, acha kudai au kuomba; shindwa. **~out** *of (a promise or undertaking)*, vunja ahadi au jitoa katika jambo. *~ a horse*, shabikia au unga mkono ya kuwa farasi atashinda wingine. **~er** *n.* msaidizi; mshabikiaji. **~fire** *n.* kishindo kiletwacho na gesi iliyowaka vibaya katika mashine kama motakaa. **~ground** *n.* **1.** mahali pa nyuma; mahali pa kufichia. *keep(stay) in the ~ground*, kaa nyuma ili usionekane. **2.** mambo ya maisha yaliyo-kwishapita. **~ing** *n.* msaada; tegemeo; wasaidizi. **~slide** *v.i.* (kwa mtu) kengeuka; ritadi; rudia mwenendo mbaya. **~ward** *adj.* -sioendelea vizuri; -a nyuma. *a ~ward child*, mtoto aliye mzito wa kuelewa. **~wards** *adv.* nyuma; kinyume. **~water** *n.* sehemu ya mto ambayo mkondo wa maji unarudi nyuma. **~woods** *n.* mwitu.
**bacon** /ˈbeɪkən/ *n.* nyama ya nguruwe iliyotiwa chumvi na kutengenezwa ili isioze.
**bacterium** /bækˈtɪəriəm/ *n.* *(bacteria)* kiumbehai kisicho-onekana kwa macho ila kwa hadubini, baadhi husababisha maradhi na baadhi yao hurutubisha ardhi.



**bacterium | bakteria**

**bad** /bæd/ *adj.* -baya; -ovu. *go to the ~*, potelea mbali; potea; potoa; angamia. *go ~*, oza; vunda.
**badge** /bædʒ/ *n.* beji; alama ya kutambulisha mtu au kitu.
**bag** /bæg/ *n.* mfuko; mkoba; gunia. *v.i.* benuka katika makunjo. *v.t.* chukua.
**baggage** /ˈbægɪdʒ/ *n.* vyombo; mizigo; vikorokoro.
**bail**[1] /beɪl/ *v.t.* dhamini. *~ (sb.) out*, dhamini mtu ili aachwe huru katika kipindi cha kesi. *n.* dhamana; mdhamini.
**bail**[2] /beɪl/ *n.* kijiti kimojawapo cha viwili kinachowekwa juu ya kigingi katika mchezo wa kriketi.
**bail**[3] /beɪl/ *v.t./i.* kumba; futa; tega; teka maji katika chombo.
**bait** /beɪt/ *n.* chambo. *v.t.* tia chambo katika ndoana; ambika; chokoza; sumbua.
**bake** /beɪk/ *v.t./i.* oka; kausha. **~r** *n.* mwokaji mikate. **~ry** *n.* bekari; mahali panapofanywa mikate.
**balance** /ˈbæləns/ *n.* **1.** mizani; kapani. *in the ~*, matokeo hayajajulikana bado. **2.** lingana. **3.** urari; bakaa. **~ sheet** *n.* hati ya kuonyesha mapato na matumizi. *v.t./i.* -wa sawasawa; pima katika mizani; fikiri; sawazisha; linganisha. *~ (oneself) on one foot*, simamia mguu mmoja.


**balance**

**balcony** /'bælkəni/ *n.* roshani.


**balcony**

**bald** /bɔ:ld/ *adj.* **1.** -enye upara; bila nywele, manyoya au majani. **2.** *(fig.)* tupu; -siyopa-mbwa.

**bale** /beɪl/ *n.* robota; mtumba; mzigo; furushi; bunda. *v.i.* **1.** funga katika mitumba. **2.** kumba; teka; futa maji kutoka chomboni. ~ *out,* ruka kutoka kwenye eropleni kwa msaada wa parashuti.

**ball** /bɔ:l/ *n.* **1.** tufe; mpira. **2.** dansi ya watu wengi. **~ and socket joint** kiungo rungu na kikombe: kiungo ambamo mviringo wa mfupa mmoja (rungu) husaki ndani ya nafasi (kikombe) ya mfupa mwingine na kuruhusu mzunguko kwa urahisi.

**balloon** /bə'lu:n/ *n.* baluni: mfuko mkubwa uliojaa namna ya hewa kama gesi wa kurukia angani na huwa na mkoba wa kubebea watu; bofu.

**ballot** /'bælət/ *n.* karatasi ya kura. *v.i.* chagua kwa karatasi ya kura; piga kura.

**bamboo** /ˌbæm'bu:/ *n.* mwanzi.

**ban** /bæn/ *v.t.* *(-nn-)* kataza; piga marufuku; zuia. *n.* tangazo la kupiga marufuku.

**banana** /bə'nɑ:nə/ *n.* ndizi. ~ *plant,* mgomba. *bunch of ~s,* chana la ndizi. *fruit stalk of ~s,* mkungu wa ndizi.

**band** /bænd/ *n.* **1.** kitu chembamba cha kufungia au cha kuungia. **2.** utepe; ukanda. **3.** jamii; kundi; kikosi. ~ *of musicians,* kikosi cha wanamuziki. **~age** *n./v.t.* bendeji; funga bendeji.

**bandit** /'bændɪt/ *n.* mnyang'anyaji; haramia; jambazi.

**bang** /bæŋ/ *n.* mshindo. *v. t.* gonga kwa nguvu.

**bangle** /'bæŋgl/ *n.* bangili; kikuku.

**banish** /'bænɪʃ/ *v.t.* hamishia mbali; fukuza. *(fig.)* sahau shughuli zote. **~ment** *n.* uhamisho; ufukuzaji.

**banisters** /'banɪstəs/ *n.* safu ya viguzo vyenye ubao juu vijengwavyo kwenye ngazi za nyumba ya ghorofa kama mhimili.

**banjo** /'bændʒəʊ/ *n.* zeze la kizungu; gambusi.


**banjo**

**bank**[1] /bæŋk/ *n.* **1.** fungu jembamba la mchanga, udongo, etc. *low ~s of earth between rice - fields,* mafungu membamba ya udongo katikati ya mashamba ya mpunga. **2.** (kwa mto) ukingo; kando; ng'ambo; etc. *v.t./i.* **1.** fanya; funga. ~ *up a fire,* funika kwa makaa ili moto uwake polepole kwa muda mrefu. **2.** (kwa eropleni) wa na bawa moja juu ya bawa la pili wakati wa kugeuka.

**bank**[2] /bæŋk/ *n.* benki. **~-clerk** *n.* karani wa benki. **~er** *n.* mtunzaji; mbadilishaji; mvunjaji fedha benki. **bankrupt** *n.* mtu aliyefilisika. *adj.* -a kufilisika. ~ *of ideas,* -siye na mawazo; maoni kabisa; muflisi. **~cy** *n.* kufilisika.

**banner** /'bænə(r)/ *n.* bendera; bango; beramu.

**banquet** /'baŋkwɪt/ *n.* karamu; dhifa; sherehe.

**baptism** /'bæptɪzəm/ *n.* ubatizo. **~al** *adj.* -a ubatizo.

**baptize** /bæp'taɪz/ *v.t.* batiza; ingiza rasmi katika dini ya kikristo.

**bar** /bɑ:(r)/ *n.* **1.** upau; ufito wa chuma; ubao; sabuni. **2.** kipingwa; komeo. **3.** baraza ya hukumu. *the ~,* jopo la wanasheria. **4.** kilabu ya pombe. *v.t.* *(-rr-)* **1.** kinga; zuia; kataza; zingia; komea. *prep.* (*also ~ring* ) isipokuwa; ila.

**barb** /bɑ:b/ *n.* mwiba kama ule wa chembe cha mshale au ndoana. **~ed** *adj.* enye miba hiyo. *~wire,* waya wenye miba; seng'enge.

**barbarian** /bɑ:'beəriən/ *n./adj.* mshenzi; -shenzi. **barbaric** *adj.* -a kishenzi; katili. **barbarism** *n.* ushenzi. **barbarity** *n.* ukatili; ushenzi; ukorofi; ukali. **barbarous** adj. -a kishenzi; katili; -kali; -korofi; -siostaarabika.

**barchan** /'bɑ:k(ə)n/ *n.* barkani: tuta

la mhanga lenye umbo kama mwezi mchanga katika jangwa.

**barium** /'bɛ:rɪəm/ *n.* bariamu: elementi ya madini yenye rangi nyeupe kama fedha.

**barber** /'bɑ:eə(r)/ *n.* kinyozi.

**bare** /beə(r)/ *adj.* **1.** wazi; -tupu; bila ya mavazi au mapambo. **~headed** bila ya viatu, kofia au mtandio kichwani. *v.t.* acha wazi; funua; vua; weka uchi. **~ly** *adv.* kwa shida.

**bargain** /'bɑ:gən/ *n.* **1.** maafikiano; mapatano; makubaliano. **2.** kitu kilichonunuliwa rahisi kuliko bei yake ya asili. *into the ~,* zaidi; juu; nafuu; faida kama nyongeza. *v.i.* patana kuhusu bei.

**barge** /bɑ:dʒ/ *n.* tishri; tishali; mashua kubwa. *~ into,* pambana na; ingia kwa nguvu.

**bark**[1] /bɑ:k/ n. gome; ganda.

**bark**[2] /bɑ:k/ *n./v.i.* lia kama mbwa au mbweha; bweka.

**bark**[3], **barque** /bɑ:k/ *n.* chombo kama jahazi chenye milingoti mitatu au minne.

**barley** /'bɑ:li/ *n.* shayiri.

**barn** /bɑ:n/ *n.* ghala ya nafaka.

**barometer** /bə'rɒmɪtə(r)/ *n.* barometa: chombo cha kupimia kanieneo ya angahewa.

**barracks** /'bærəks/ *n.* kambi kubwa kikaapo kikosi cha askari; kambi ya jeshi.

**barrage** /'bæra:ʒ/ *n.* **1.** boma la kuzuia maji mtoni. **2.** kupiga mizinga mingi pamoja kwa muda bila ya kusita.

**barrel** /'bærəl/ *n.* **1.** pipa; kasiki. **2.** mtutu; kasiba; mwanzi; mdomo wa bunduki.



barrel

**barren** /'bærən/ *adj.* **1.** *(of land)* kame; jangwa; yabisi. **2.** *(of females)* tasa. *(of animals, plants, trees )* -siozaa. **3.** *(fig.)* -a bure; bila faida.

**barricade** /ˌbarɪ'kəɪd/ *v.t./n.* zuia; linda; zunguka kwa boma; funga eneo; boma.

**barrier** /'bæriə(r)/ *n.* kizuizi; kizingiti; kinga; boma.

**barrow** /'bærəʊ/ *n.* bero: gari dogo lenye gurudumu moja au mawili; mkokoteni; rikwama.

**barter** /'bɒ:tə(r)/ *v.t./n.* badilishana mali, bidhaa etc. *n.* ubadilishanaji mali au bidhaa.

**basalt** /'basɔ:lt, -(ə)lt/ *n.* basati: namna ya majabali meusi magumu sana yatokanayo na volkano.

**base**[1] /beɪs/ *n.* **1.** upande au sehemu ya chini ya kitu; msingi; tako; kikalio. **2.** mahali pa kuwekea zana za kivita; etc. **3.** chanzo; chimbuko; asili. **~less** *adj.* bila sababu au msingi. **~ment** *n.* ghorofa ya chini ya ardhi ya nyumba.

**base**[2] /beɪs/ *adj.* **1.** (kwa watu - tabia, fikira zao, etc.) - ovu. **2.** (kwa madini) -a thamani ndogo.

**baseball** /'beɪsbɔ:l/ *n.* mchezo wa mpira hasa Marekani, ambao hutupwa na kupigwa kwa beti na huwa na wachezaji tisa kila upande kwa mizunguko minne.

**bashful** /'bæʃfl/ *adj.* -enye haya; soni.

**basic** /'beɪsɪk/ *adj.* -a msingi. **~ colours**, rangi msingi: rangi saba za upindemvua, yaani nyekundu, machungwa, manjano, kijani, buluu, nili na urujuani.

**basin** /'be:sn/ *n.* **1.** bakuli; kibia; beseni; bonde.



basketball

**bask** /bɑ:sk/ *v.i.* ota jua; jinyosha; jifurahisha; ona sifa.

**basket** /'bɑ:skɪt/ *n.* kikapu; kapu; pakacha; mkoba. **~ball** *n.* mpira wa kikapu.

**bastard** /'bɑ:stəd, 'bast-/ *n.* mwana wa haramu; mtoto wa nje ya ndoa.

**bat** /bæt/ *n.* **1.** beti: ubao kama kafi wa kuchezea mipira. **2.** popo.

**batch** /bætʃ/ *n.* fungu; jamii; kundi.



bat

**bath** /bɑ:θ/ *n.* bafu; birika;

josho; hamamu; maliwatoni. *v.t./i.* osha; oga.
**bathe** /beɪð/ *v.t./i* **1.** ogesha; oga; osha. *n.* kuoga; kuogelea.
**battalion** /bə'talɪən/ *n.* jeshi la askari lenye vikosi vingi walio tayari kwa vita.
**batter** /'bætə(r)/ *n.* **1.**ponda; sukuma (unga); pigilia. **2.** unga uliopondwa kwa maji.
**battery** /'bætri; -təri/ *n.* **1.** upigaji mizinga mingi pamoja. **2.** betri.
**battle** /'bætl/ *n.* vita; mapigano. *v.i.* pigana; shindana.
**bauxite** /bɔ:ksʌɪt/ *n.* boksiti: aina ya udongo ambao ndani yake hupatikana madini ya alumini.
**bay** /beɪ/ *n.* ghuba. *v.i.* bweka.
**bayonet** *n.* singe; beneti; upanga wa bunduki.
**bazaar** /bə'zɑ:/ *n.* duka; bazari: mtaa au sehemu yenye maduka mengi makubwa kwa madogo yanayouza bidhaa anuwai.
**BCG vaccination** *n.* chanjo iitwayo Bacillus Calmette-Guerin kwa watoto inayokinga kifua kikuu.
**be** /bi; bi:/ *v.i.* -wa.
**beach** /bi:tʃ/ *n.* pwani; ufukwe. *v.t.* pweleza.
**beacon** /'bi:kən/ *n.* bekoni; mnara wa ishara fulani.
**bead** /bi:d/ *n.* shanga; tasbihi; tone; rozari.
**beak** /bi:k/ *n.* mdomo wa ndege; omo la jahazi.
**beam** /bi:m/ *n.* bimu; mhimili; boriti ya mti au chuma; mwonzi mwali wa mwangaza. **~ balance**, mizani mdara: mizani ifanyayo kazi kwa kutumia kanuni ya usawa kati ya momenti kisaa na momenti kinyumesaa. *v.i.* angaza; -wa na uso wa furaha.
**bean** /bi:n/ *n.* mbegu za jamii ya kunde: choroko, kunde, fiwi, mbaazi, haragwe etc.
**bear**[1] /beə(r)/ *v.t./i.* *(bore, borne).* chukua; himili; zaa; *zingatia.* ~ *signs of,* onyesha dalili za. ~ *sb. out,* kubali kuwa fulani asemalo ni kweli. *She can't ~ cats,* hawezi kuwavumilia paka. ~ *to the right,* geuka (ongoza) upande wa kulia. *bring one's energies to ~ on the task,* himiza kazi. ~ *up,* stahamili; vumilia. ~ *on sb.,* shawishi; husiana na. ~ *in mind,* kumbuka. ~ *oneself (well, etc.),* tenda (vizuri, *etc.).* ~ *arms,* chukua, tumia, shika silaha. ~ *a hand,* saidia; auni. **~able** *adj.* -a kustahamilika; -a kuvumilika.


**bear**

**bear**[2] /beə(r)/ *n.* dubu.
**beard** /bɪəd/ *n.* ndevu; sharafa. **~ed** *adj.* -enye ndevu.


**beard**

**bearing** /'beərɪŋ/ *n.* beringi: gololi ambazo huwekwa baina ya sehemu za mashine zinazogusana ili kupunguza ukinzani wakati zinapozunguka.
**beast** /bi:st/ *n.* **1.** mnyama; hayawani. **2.** mtu mwenye desturi za kinyama; mpujufu. **~ly** *adj.* -a kuchukiza; -siopendeza.
**beat** /bi:t/ *v.t./i.* *(beat, beaten)* **1.** piga; chapa; kong'ota; **2.** shinda; pita; tia fora. *n.* pigo; zamu; mdundo.
**beauty** /'bju:ti/ *n.* uzuri; urembo; haiba. **beautiful** *adj.* -zuri; -a haiba; -a kupendeza.
**because** /bɪ'kɒz; -'kəz/ *conj.* kwa sababu; kwa ajili; minajili; kwa kuwa; maadam; madhali.
**beckon** /'bekən/ *v.t./i.* ashiria; pungia mkono; konyeza.
**beck** /bek/ *n.* *be at sb.'s beck and call,* -wa chini ya amri ya mtu fulani wakati wote.
**become** /bɪ'kʌm/ *v.i./t.* (**became** /bɪ'keɪm/) -wa. ~ *of,* kuwa. *What has ~ of him?* amekuwaje? *That hat ~s you,* kofia ile inakupendeza sana.
**becquerel** /'bɛkərɛl/ *n.* kipimo cha unururifu harakatiredio.
**bed** /bed/ *n.* **1.** kitanda. **2.** msingi. **3.** udongo ulio chini ya bahari, mto au ziwa. **4.** tuta.
**bee** /bi:/ *n.* nyuki. *make a ~ line for,* -enda kwa njia ya mkato. **~hive** *n.* mzinga wa nyuki. **~s-wax** *n.* nta.
**beech** /bi:tʃ/ *n.* namna ya mti kama

mfune huko Ulaya.

**beef** /bi:f/ *n.* nyama ya ng'ombe. **~-tea** n. mchuzi wa nyama ya ng'ombe. **~wood** n. mvinje.

**beer** /bɪə(r)/ *n.* bia; pombe; ulevi.

**beet** /bi:t/ *n.* kiazi sukari. *red ~,* figili ipikwayo na kuliwa kama mboga. *white ~,* kiazi cheupe kitengenezewacho sukari.

**beetle** /bi:tl/ *n.* kombamwiko: mdudu wa jamii ya mende mwenye mabawa atambaaye.



beetle

**before** /bɪ'fɔ:(r)/ *prep./conj.* kabla (ya); mbele (ya). **beforehand** *adv.* mbele; kwanza; kabla.

**beg** /beg/ *v.t./i.* **(-gg-)** omba; taka; ng'an-g'ania. *food which is going ~ging,* chakula kisichotakiwa. *I ~ to differ,* sikubali. *I ~ your pardon,* niwie radhi; kunradhi. **~gar** *n.* mwombaji; maskini; fukara; mkata; omba-omba; mlalahoi.

**begin** /bɪ'gɪn/ *v.t./i.* (**began begun** anza; ingia.

**behalf** /bɪ'hɑ:f/ *n.* niaba; *on (in ) ~ of,* kwa niaba ya; -a kuwakilisha.

**behave** /bɪ'heɪv/ *v.i.* tenda; enda; jiweka. **behaviour** *n.* mwenendo; tabia; mazoea; silka; desturi; adabu.

**behind** /bɪ'haɪnd/ *prep./adv.* nyuma (ya); baada (ya). *remain ~,* baki nyuma; salia. *be ~,* chelewa; kawia; ahirika; shindwa; pitwa.

**being** /'bi:ɪŋ/ *n.* **1.** kuwa. **2.** kiumbe. **3.** *The Supreme ~,* Mwenyezi Mungu. *human ~,* mtu; binadamu; mja.

**belief** /bɪ'li:f/ *n.* **1.** imani; shahada; itikadi. **2.** dhana; wazo.

**believe** /bɪ'li:v/ *v.t./i.* amini; sadiki; dhani; tumaini. *~ in,* aminia. **believer** *n.* muumini; mfuasi.

**bell** /bel/ *n.* kengele.

**belligerent** /bə'lɪdʒərənt/ *n.* mfanya vita; enye kupenda vita. *adj.* ushari.

**bellow** /'beləʊ/ *v.i./n.* uga; lia kama ng'ombe; piga kelele kwa hasira; vuma; nguruma; mlio wa ng'ombe; ngurumo; mvumo.

**bellows** /'beləʊz/ *n.* mivuo; mivukuto; viriba.

**belly** /'beli/ *n.* tumbo. *v.i. ~ out,* hutumika kwa matanga yanapovimba kwa upepo; fura; tuna.

**belong** /bɪ'lɒŋ/ *v.i. ~ to,* -wa mali ya; -wa mwanachama; -wa kitu cha; -wa mtu wa; -wa sehemu ya; husu. *Does the dog ~ here?* mbwa huyu ni wa hapa? **~ings** *n.* mali; vikorokoro; mambo.

**beloved** /bɪ'lʌvd/ *adj.* -pendwa; -penzi. *n.* -penzi; mpenzi.

**below** /bɪ'ləʊ/ *adv./prep.* chini (ya).

**belt** /belt/ *n.* **1.** mshipi; ukanda; mkanda. **2.** ukanda mrefu wa ngozi wa kuunganisha magurudumu na kuendesha mashine.

**bench** /bentʃ/ *n.* **1.** ubao wa kukalia; benchi; dawati. **2.** meza ya kazi. **3.** kiti cha hakimu; kadhi; kundi la mahakimu (majaji; makadhi) katika baraza la mahakama.

**bend** /bend/ *v.t./i.* (**bent**) **1.** pinda; kunja. **2.** pindika; geuka; nesa; nepa; kunjika; elekeza (akili, macho, etc.). *~ one's mind to one's work,* elekeza nadhari zote kazini, yaani fanya kazi kwa bidii. *bent on,* -enye nia; -enye bidii. *n.* mpindo; kona; mshazari.

**beneath** /bɪ'ni:θ/ adv./prep. chini (ya).

**benediction** /benɪ'dɪkʃn/ *n.* baraka; dua ya kutakia heri.

**benefaction** /ˌbɛnɪ'fakʃ(ə)n/ *n.* fadhila; jamala; sadaka; tendo la wema; hisani. **benefactor** n. mfadhili; mtenda mema; mhisani.

**benefit** /benɪfɪt/ *n.* faida; fadhila; maendeleo; manufaa; chumo. *v.t./i.* falia; faa; nufaisha; nufaika; faidika.

**benevolent** /bə'nevələnt/ *adj.* -paji; karimu; -ema.

**bent** /bent/ *n.* tabia; mwelekeo wa mtu. *She has a ~ for sewing,* ni hodari sana wa kushona.

**benzene** /'bɛnzi:n/ *n.* benzeni: aina ya mafuta yasiyokuwa na rangi yapatikanayo kwenye lami ya mkaa wa mawe na petroli, hutumika katika utengenezaji wa

plastiki.
**benzine** /'bɛnzi:n/ *n.* benzini: aina ya mafuta yasiyokuwa na rangi yapatikanayo kwenye petroli iliyokuwa haijasafishwa, hutumika kusafishia nguo.
**beryllium** /bə'rɪlɪəm/ *n.* aina ya elementi ya madini ya kijivu na ni nyepesi, hutumika sana katika aloi za shaba.
**berth** /bɜ:θ/ *n.* **1.** kijumba cha melini au garini. **2.** mahali pa meli kutia nanga. *give a wide ~ to,* epa; ambaa; toa nafasi.
**beside** /bɪ'saɪd/ *prep.* kando ya; mbavuni mwa. *He is ~ himself with anger,* amerukwa na akili kwa hasira. *That is ~ the question,* hilo halihusiani na hili. **~s** *prep./adv.* zaidi (ya); juu (ya); tena.
**besiege** /bɪ'si:dʒ/ *v.t.* zingia; zunguka; shambulia pande zote. *~ sb., with requests,* omba sana kwa nguvu bila ya kuachia.
**best** /best/ *adj./adv.* bora; -zuri kuliko -ote; aali. *~ man,* rafiki amsaidiaye bwana arusi siku ya harusi.
**bestial** /'bɛstɪəl/ *adj.* -a hayawani; -a kuchukiza; kama hayawani .
**bestir** /bɪ'stɜ:(r)/ *v.t.* **(-rr-)** *~ oneself,* jiamsha; jishughulisha; amsha; shtua; jihimiza.
**bet** /bet/ *v.t./i.* **(-tt-)** pinga; weka sharti; pakiliana. *n.* sharti ya bahatisho; dau; cheza kamari.
**beta particle** *n.* chembe beta: elektroni inayotokana na mbunguo wa nyutroni fulani.
**beta radiation** *n.* mnururisho beta: miali inayotokana na madini, kama vile urani au plutoni ambayo ina chaji hasi.
**betray** /bɪ'treɪ/ *v.t.* **1.** haini; danganya; saliti. **2.** toa siri (ama kwa bahati mbaya ama kwa kusudi). **3.** bainisha; onyesha wazi.
**better** /'betə(r)/ *adj./adv.* bora; -a kufaa zaidi; -zuri zaidi.
**between** /bɪ'twi:n/ *prep./adv.* katikati (ya); baina (ya); kati (ya). *~ whiles,* pengine (wakati si mahali). *~ ourselves,* kati yetu sisi tu.
**beware** /bɪ'weə(r)/ *v.t./i.* angalia; tahadhari; jihadhari!
**beyond** /bɪ'jɒnd/ *adv./prep.* ng'ambo ya pili (ya); upande wa pili (wa); kupita. *~ measure,* kupita kiasi.
**bi-** /bʌɪ/ *prefix* mara mbili; -a mbili; kila mara ya pili; -enye kuhusisha pande mbili.
**bible** /baɪbl/ *n.* biblia. **biblical** *adj.* -a biblia.
**biceps** /'bʌɪsɛps/ *n.* misuli ya mkono iliyo kati ya kiko na bega.
**bicycle** /'baɪsɪkl/ *n./v.i.* baiskeli; panda baiskeli.


bicycle

**bid** /bɪd/ *v.t./i.* *(-dd-)* **1.** *(bid, bade, bidden)* zabuni; pandisha bei. **2.** amuru; agiza; ambia; aga. **bidder** *n.* mzabuni. *first bid,* rasimu. *final bid,* shtiri. **~ding** *n. do sb's ~ding,* mtii fulani.
**big** /bɪg/ adj. -kubwa; -kuu; -nene. **~bang** *n.* nadharia mgongano: nadharia kwamba vitu vyote ulimwenguni viliumbwa kutokana na mgongano mkubwa.
**bile** /baɪl/ *n.* nyongo; *(fig.)* uchungu; chuki. **bilious** *adj.* -enye ugonjwa uletwao na nyongo wa kushinikiza kutapika.
**bilingual** /'baɪ'lɪŋgwəl/ *adj.* -enye kuzungumza au kuhusu lugha mbili.
**bill**[1] /bɪl/ *n.* mdomo wa ndege.
**bill**[2] /bɪl/ *n.* **1.** bili; hesabu; gharama. **2.** tangazo lililopigwa chapa. **3.** mswada wa sheria. **4.** (katika biashara) **~ of exchange**. hawala; hundi; cheki. **~-poster, ~-sticker** *n.* mwenye kubandika matangazo kutani.
**billiards** /'bɪliədz/ *n.* biliadi: mchezo wa kugonganisha tufe tatu juu ya meza ya kitambaa maalumu kwa kuzigonga nyingine ili kuziingiza ndani ya mifuko ya meza hiyo.
**billion** /'bɪljən/ *n.* milioni milioni, (katika nchi za Amerika na Ufaransa ni milioni elfu).
**bimetallic strip** *n.* pau metalimbili: ufito wenye metali mbili tofauti zilizogandamizwa pamoja.

**bin** /bɪn/ *n.* pipa la kuwekea nafaka; takataka etc.

**binary** /'bʌɪnəri/ *n.* jozi; -enye sehemu au vizio viwili. ~ *code*, mfumo jozi: mfumo wa kuhesabu kwa kutumia tarakimu mbili tu, 0 na **1.** ~ **fission**, mwatuko: **1.** utendanaji wa kinyuklia unaosababisha kiini kizito cha atomu kumegeka katika sehemu mbili na papo hapo zikatoka nyutroni na kutoa kiasi kikubwa sana cha nishati ya kinyuklia. **2.** uzalianaji wa viumbehai ambapo kiumbe wa seli moja hugawika sehemu mbili kupata viumbe viwili hai vikiwa sawa. ~ **system** mfumo jozi: mfumo wa kuhesabu unaotumia tarakimu mbili tu ambazo ni **0** na **1.**

**bind** /baɪnd/ *v.t./i.* *(bound, bound)* **1.** funga; kaza. **2.** jalidi. **3.** gandisha; ambatisha. **4.** funga kwa ahadi; shuruti; ahidi.

**binoculars** /bɪ'nɒkjʊləz/ *n.* darubini ya macho mawili. **binocular vision** uono darubini: uwezo hasa wa wanyama kutumia macho yao kuona vitu kama vilivyo na kuweza kupima masafa.



binoculars

**binomial** /bʌɪ'nəʊmɪəl/ *n.* mtajo-vipeo; mtajozi: mtajo ambao ni jumla au ni tofauti ya mitajo miwili tu katika aljebra, aidha kwa kujumlisha au kutoa.

**biochemistry** /ˌbaɪəʊ'kemɪstri/ *n.* biokemia: sayansi ya kemia ya viumbehai.

**biodegradable** /ˌbaɪəʊdɪ'greɪdəbl/ *adj.* -enye kuweza kuvunjwa-vunjwa na bakteria au viumbehai kwa njia za kibiolojia.

**biogas** *n.* biogesi: gesi inayo-patikana kwa mchanganuo wa mata mahuluku, hasa toka kwenye samadi ya wanyama kama ng'ombe.

**biography** /baɪ'ɒgrəfi/ *n.* maandishi ya habari za maisha ya mtu.

**biology** /baɪ'ɒlədʒi/ *n.* biolojia: elimu ya asili na maumbo ya viumbe vyote hai, yaani binadamu, wanyama na mimea.

**biological control** *n.* udhibiti biolojia: udhibiti wa viumbe waharibifu kwa kutumia njia za kibiolojia, kama kutumia wanyama wingine kuwala wale waharibifu, pasipo kutumia kemikali.

**biomass** /'baɪəʊmæs/ *n.* jumla ya viumbe vyote hai viishivyo katika eneo fulani.

**bionic** /baɪ'ɒnɪk/ *adj.* -a bionia; (kwa mtu) ambaye viungo au nadhari zake zinaongozwa na mitambo ya elektroniki badala ya kuongozwa na akili. **~s** *n.* bioniki: taaluma ihusuyo mashine zinazotumiwa kufanya kazi badala ya viungo au nadhari ya viumbehai.




biosphere (biosfia penye maisha)

**biosphere** | **biosfia**

**biosphere** /'baɪəʊsfɪə(r)/ *n.* biosfia; tabakahai: eneo lote la uso wa dunia ambamo viumbe hai hupatikana.

**biotechnology** /ˌbaɪəʊtek'nɒlədʒi/ *n.* bioteknolojia: matumizi ya viumbehai kibiolojia viwandani kwa manufaa fulani, hususan matumizi ya uhandisi jeni katika utengenezaji wa dawa za kiuavijasumu na homoni.

**biotic** *adj.* /bʌɪ'ɒtɪk/ -nye kuhusiana na viumbehai kibiolojia. ~ **environment** mazingira hai; mazingira yatokanayo na harakati za viumbehai. ~ **factor** kiumbe chochote katika mazingira

kinachoathiri kingine.



bird

**bird** /bɜ:d/ *n.* ndege.

**birth** /bɜ:θ/ *n.* uzazi; uzawa; uzao; nasaba; ukoo. ~ **control**, udhibiti uzazi: mpango wa kuratibu mfumo wa kuongezeka binadamu kwa kiwango maalumu. ~ **rate**, kasi ya uongezekaji watu katika jamii kwa muda maalumu. **birthday** *n.* sherehe ya siku ya kuzaliwa ya kila mwaka.

**biscuit** /'bɪskɪt/ *n.* biskuti.

**bisect** /baɪ'sekt/ *v.t.* kata sehemu mbili zilizo sawa kabisa.

**bishop** /'bɪʃəp/ *n.* askofu. **~bird** *n.* kweche; chekechea. **~ric** *n.* uaskofu; jimbo la askofu; dayosisi.

**bismuth** /'bɪzməθ/ *n.* bisimathi: elementi ya kemikali yenye rangi ya kijivu cheupe ambayo hutumika katika aloi na pia huchanganywa na vitu vingine katika dawa.

**bit**[1] /bɪt/ *n.* kipande; sehemu; chembe. ~ *by* ~, haba na haba; kidogo kidogo. *a* ~, kidogo. *wait a* ~, ngoja kidogo.

**bit**[2] /bɪt/ *n.* **1.** lijamu. **2.** *a brace and* ~, msumari wa kekee.

**bitch** /bɪtʃ/ *n.* jike la mbwa au la mnyama yoyote wa jamii ya mbwa.

**bite** /baɪt/ *v.t./i.* (bit, bitten) uma; tafuna; guguna; donoa; washa; choma.

**bitter** /'bɪtə(r)/ *adj.* **1.** -chungu; -kali; -enye kakasi. **2.** -a kutia huzuni; -ngumu kuvumiliwa; -enye hasira.

**bitumen** /'bɪtjʊmən/ *n.* bitumeni: aina ya lami itokanayo na petroli.

**black** /blæk/ *adj.* **1.** -eusi; -a giza. **2.** (fig.) - baya; -a kisirani; -a nuhusi; -a mkosi. *be in sb.'s ~ book(s)*, kutopendwa na fulani; -wa -mechukiza kwa mtu. **~sheep** *n.* mtu mbaya. ~ **market**, soko la magendo. *n.* weusi; mweusi. **~en** *v.t./i.* fanya -eusi; -wa -eusi. *(fig.) ~ a man's character*, vunja heshima ya mtu; singizia; aibisha. **~guard** *n.* mwovu; ayari; mkorofi. ~ **hole** *n.* ombwe jeusi: uwazi mweusi unaopatikana wakati nyota kubwa inapovunjikavunjika. **~leg** *n.* mtu akubaliye kufanya kazi ingawa wenzake wamegoma wakati wa madai ya nyongeza ya mshahara. **~list** *n.* orodha ya watu, vitu, kazi, etc. walio au vilivyopigwa marufuku. *v.t.* ingiza katika orodha wa walio au vilivyopigwa marufuku. **~mail** *v.t.* tisha mtu ili atoe hongo, mrungura, rushwa, etc. ili ufiche siri yake ya kosa fulani. **~smith** *n.* mhunzi.

**bladder** /'blædə(r)/ *n.* **1.** kibofu. **2.** mpira laini wa ndani ya mpira wa miguu; plada.

**blade** /bleɪd/ *n.* **1.** bapa. **2.** jani. **3.** bapa la kasia au kafi; wembe.

**blame** /bleɪm/ *v.t.* karipia; kemea; laumu; shutumu. *n.* shutuma; lawama. **~less** *adj.* -sio kosa.

**blank** /blæŋk/ *adj.* **1.** -tupu; -eupe. **2.** (kwa uso au macho ya mtu) -a kipumbavu; -liyofadhaika; -liyoduwaa. **3.** ~ *space*, nafasi tupu. ~ *wall*, ukuta usio na milango wala madirisha. ~ *cartridge*, kijaluba kisicho na risasi bali chenye baruti tu. *n.* mahali wazi; uwazi; nafasi wazi.

**blast** /blɑ:st/ *n.* **1.** upepo wa ghafla; dhoruba ya upepo, mfyuko. *a ~ of hot air from a furnace*, upepo wa ghafla wa moto uliotoka kwenye tanuri. *windows broken by ~*, madirisha yaliyovunjika kwa mripuko (wa baruti, kombora, etc.). **2.** mlipuko (wa bomu, etc.) *v.t.* **1.** pasua kwa baruti. **2.** haribu; angamiza. **~-furnace** *n.* kalibu; tanuri; jokomfyuko: joko litumialo mkondo wa hewa moto kuyeyushia madini.

**blaze** /bleɪz/ *n.* moto unaong'aa sana; ndimi za moto. *v.i./t.* waka; ng'aa; mweka; mwesa. ~ *away*, piga mizinga, bunduki, upesi sana bila ya kusita.

**blaze** /bleɪz/ *v.t.* **1.** bandua kipande cha gome mtini kama alama ya kuonyesha njia au mpaka. **2.** tia alama juu ya paji la mnyama.

**bleach** /bli:tʃ/ *v.t./i.* fanya, -wa -eupe

(kwa nguvu za dawa au za jua); chakaa; kwabuka; chabuka; chubua.

**bleak** /bli:k/ *adj* (kwa tabia ya nchi) baridi; -a ukiwa; (kwa mahali) eupe, -a kuvumiwa na upepo mwingi; tazamia mambo ya mbele bila matumaini.

**bleat** /bli:t/ *v.i.* lia kama kondoo; lia kijinga. *n.* mlio kama wa kondoo, mbuzi au ndama.

**bleed** /bli:d/ *v.i./t.* toka damu; toa damu; umika; piga chuku.

**blemish** /'blemɪʃ/ *n.* ila; upungufu; athari; dosari; nakisi; hitilafu; mapungufu ya kiroho au kimwili.

**blend** /blend/ *v.t./i.* changanya; patana. *n.* mchanganyiko.

**bless** /bles/ *v.t.* **(blessed, blest)** **1.** bariki; neemesha; sitawisha; sifu. *God ~ you!* Mungu akubariki. **2.** **(colloq.)** *Bless my soul! well I'm blest!* lahaula! **~ed** *adj.* -takatifu; -enye heri. **~ing** *n.* baraka.

**blight** /blaɪt/ *n.* **1.** maradhi ya mimea. **2.** chochote kiharibucho au kuangamiza. *a ~ upon my hopes,* mkosi katika matumaini yangu. *v.t.* haribu; umbua; fisha; pozesha.

**blind**[1] /blaɪnd/ *adj.* **1.** -pofu; *(fig.)* -jinga. **2.** -siyefikiri. *in ~ haste,* kwa haraka bila ya kufikiri; a pupa. **3.** *a ~ corner,* kona ambayo dereva wa gari haoni mbele. **4.** *~ alley,* uchochoro uliozibwa upande mmoja. *(fig.) ~ alley occupation,* shughuli au kazi isiyo na faida mwishoni. **~ly** *adv.* kijinga; kwa pupa. **~ness** *n.* upofu; chongo. **~fold** *v.t.* fungia kitambaa machoni. *(fig.)* zuga; hadaa; laghai. **~ spot** *n.* doto pofu: kituo katika retina ambapo mishipa yote ya damu na mishipa ya neva huingia katika neva optiki.

**blind**[2] /blaɪnd/ *n.* pazia; hila; uongo; mtego; ghilba.

**blink** /blɪŋk/ *v.t./i.* pepesa; pwesa; metameta. *(fig.) ~ facts,* kukataa kukabili hali halisi ya mambo.

**bliss** /blɪs/ *n.* furaha kubwa; jaha. **~ful** /blɪsfl/ *adj.* -a furaha nyingi; -a raha.

**blister** /blɪstə(r)/ *n.* lengelenge; tumbuja.

**bloated** /'bləʊtɪd/ *adj.* *(be)* **1.** liyevimba kwa maradhi **2.** liyovimba; kubwa kuliko kiasi.

**block** /blɒk/ *n.* **1.** gogo la mti au jiwe. *a chip of(f) the old ~,* mtu afananaye sana na baba yake kwa umbo au kwa tabia. **2.** bloki; nyumba nyingi za fleti pamoja. **3.** kipande cha mti au chuma cha kupigia chapa chenye herufi au picha zilizochorwa juu yake. **4.** uzio; kizuizi; kikwazo. *traffic ~,* msongamano wa vipando barabarani. **5.** *~ letters,* herufi kubwa. *v.t.* **1.** funga njia; zuia. **2.** *~ in,* chora umbo, picha au ramani.

**blockade** /blɒkeɪd/ *n.* uzingiaji; kizuizi; vikwazo. *v.t.* zunguka kwa vita; husuru; zingia. *economic ~,* vikwazo vya uchumi.

**blond(e)** /blɒnd/ *n./adj.* mtu mweupe mwenye nywele za singa za rangi ya shaba au ya dhahabu.

**blood** /blʌd/ *n.* damu. *in cold ~,* bila hasira. *make bad ~ between,* gombanisha. *one's own flesh and ~,* ndugu. *His ~ was up,* alikuwa amekasirika. **~cell** *n.* seli damu: seli yoyote iliyomo katika damu. **~clotting** *n.* kuganda kwa damu. **~hound** *n.* aina ya mbwa mwenye uwezo mkubwa wa kunusa harufu, hutumiwa sana kusakia wahalifu. **~plasma** *n.* plasima ya damu: giligili manjano isaliayo baada ya kuondoshwa viini vya damu katika damu. **~platelets** *n.* chembechembe ndogo katika damu ambazo ni muhimu kuifanya igande. **~poisoning** *n.* hali ambayo damu huwa na sumu, kama vile baada ya kuambukizwa maradhi. **~shed** *n.* mauaji; umwagaji damu. **~shot** *(adj.)* -enye macho mekundu. **~thirsty** *adj.* katili; -enye hamu ya




**red blood cell**

kumwaga damu. **~vessel** *n.* mshipa wa damu ambamo damu hupita inapozunguka katika kiwiliwili.

**bloom** /blu:m/ *n.* ua. *(fig.)* kipindi cha kukamilika. *v.i.* toa maua; chanua; sitawi.

**blossom** /'blɒsəm/ *n.* ua; maua mengi. *v.i.* toa maua; chanua; stawi.

**blouse** /blaʊz/ *n.* blauzi; vazi la kike.

**blow**[1] /bləʊ/ *v.i./t.* **1.** (kwa hewa) vuma. *It was ~ing hard,* upepo ulikuwa unavuma sana. *~ over,* pita. *(fig.)* sahauliwa. **2.** *~ away, ~ about,* (kwa vitu) kusombwa na upepo; peperuka. **3.** (up) tia pumzi. e.g. kwenye mpira. **4.** *~ one's nose,* penga, futa, toa, makamasi. *v.i./t.* **1.** pasuka; pasua; ripua. *The barrel of gunpowder blew up,* pipa la baruti liliripuka. *~ out,* **1.** zima kwa kupuliza; zima kwa maji. **2.** (kwa nyaya za umeme) yeyuka kutokana na umeme mkubwa. **2.** piga; lia. *The trumpet blew,* tarumbeta lililia. *He blew the whistle,* alipiga filimbi. **3.** toa pumzi; puzia. *n.* punga upepo.

**blow**[2] /bləʊ/ *n.* pigo; msiba; maafa; masaibu.

**blue** /blu:/ *n./adj.* rangi ya samawati; buluu. *~ ribon,* alama ya heshima kubwa; cheo kilicho bora. *a bolt from the ~,* tukio la ghafla lisilotarajiwa.

**bluff**[1] /blʌf/ *v.t./i.* danganya; ghilibu; laghai. *n.* udanganyifu; ulaghai; ghiliba.

**bluff**[2] /blʌf/ *n.* jabali kubwa; joma; genge; lililo karibu na bahari au mto.

**bluff**[3] /blʌf/ *adj.* -nyofu; dhalili.

**blunder** /blʌndə(r)/ *n.* kosa; koseo; kashfa. *v.i.* fuja; sitasita; koroga; chafua; kosea; boronga.

**blunt** /blʌnt/ *adj.* **1.** -butu. **2.** (kwa maneno ) -a wazi; -a kweli.

**blur** /blɜ:(r)/ *v.t./i.* **(-rr-)** fanya isiwe dhahiri; fifia, -siofahamika. *n.* waa; doa.

**blurt** /blɜ:t/ *v.t.* *(out)* sema ghafla; payuka.

**boa** /'bəʊə/ *n.* aina ya chatu wa Amerika.

**boar** /bɔ:(r)/ *n.* nguruwe dume mwitu.

**board** /bɔ:d/ *n.* **1.** ubao. **2.** baraza; bodi; halmashauri. **3.** meza. *above ~,* wazi; dhahiri. *sweep the ~,* shinda zawadi nyingi katika mashindano. **4.** chakula kinachotolewa katika vyumba vya kupanga na mabwenini. **5.** jalada. *v.t./i.* **1.** *~ up,* au *~ in,* funga kwa mbao; funika kwa mbao. **2.** pata au -toa chakula katika nyumba ya kupanga. **3.** panda meli, gari au ndege. **~er** *n.* mtu apataye chakula katika nyumba ya kupanga; mwanafunzi alalae na kulishwa bwenini.

**boast** /bəʊst/ *n.* majisifu; majivuno. *v.i./t.* **1.** jiona; jigamba; jiboda. *Our school ~ s a good swimming pool,* shule yetu inajivunia bwawa zuri la kuogelea. **~ful** *adj.* -enye kujisifu; -enye kujiona; -enye kujivuna; -enye makeke na nyodo.

**boat** /bəʊt/ *n.* **1.** mashua; boti; meli. *(fig.) be (all) in the same ~,* -wa wote katika hali moja. *burn one's ~s,* kukata shauri bila kujipa nafasi ya kughairi. **~swain** *n.* serahangi.

**bob**[1] /bɒb/ *v.i./t.n.* **(-bb-)** **1.** rukaruka; tikisika. **2.** *~ up,* zuka; ibuka. **3.** kata; fupisha; fanya butu.

**bob**[2] /bɒb/ *n. (slang)* shilingi.

**body** /'bɒdi/ *n.* **1.** mwili. **2.** kiwiliwili. **3.** maiti; mzoga. **4.** kikosi; jeshi; kundi. **5.** mtu. *any ~,* mtu yeyote. *some ~,* mtu fulani. *every ~,* kila mtu; watu wote. **~-guard** *n.* bodigadi; mlinzi wa mtu au wa kiongozi.

**bog** /bɒg/ *n.* ziwa la matope. **~gy** *adj.* -enye matope; - enye porojo. **~ged** *adj. be (get) ~ down,* lemewa; kwama; kutoweza kuendelea.

**boil**[1] /bɔɪl/ *v.i./t.* **1.** chemka; chemsha; tokosa; pika. **2.** kasirika; hamaki; ghadhibika. **~er** *n.* chombo cha kuchemshia maji au nguo. **~ing** *n.* mchemko: mvukizo wa haraka ambao hutikisa kioevu, nao hutokea wakati kanieneo mvuke inapolingana na ile ya uso wa kioevu. **~point** *n.* kiwango

mchemko: hali joto ya kioevu wakati wa kuchemka.
**boil**² /bɔɪl/ *n.* jipu.
**boistreous** /'bɔɪstərəs/ *adj.* **1.** -enye kupenda kelele; -enye tadi; inda; -enye fujo; enye jeuri. **2.** hali mbaya ya bahari au hewa.
**bold** /bəʊld/ *adj.* shujaa; jasiri; thabiti; -shupavu; -jeuri. **~ness** *n.* **1.** ushujaa; ujasiri; ushupavu; uhodari. **2.** ujuvi; ufedhuli.
**bolster** /'bəʊlstə(r)/ *n.* mto mrefu na mnene wa kulazia kichwa. *v.t.* ~ *(up),* saidia mtu atakae sana msaada lakini pengine asiyestahili kusaidiwa; tegemeza; imarisha.
**bolt**¹ /bəʊlt/ *n.* **1.** komeo. **2.** skurubu, parafujo. **3.** (la kizamani ) mshale, risasi. *v.t.* komea; kaza; funga.


**bolt and nut**

**bolt**² /bəʊlt/ *v.i./t.* **1.** toroka kwa ghafula. **2.** meza kwa pupa. *n.* *make a ~ for it,* kimbia, toroka.
**bomb** /bɒm/ *n.* kombora; bomu; mzinga. **~ard** *v.t.* piga mizinga; tupia makombora. *(fig.)* hoji sana. **~ardment** *n.* shambulio la mizinga, mabomu.
**bond** /bɒnd/ *n.* **1.** sharti; dhamana; bondi; mkataba. *His word is as good as his ~,* neno lake ni sawa na mkataba, yaani havunji ahadi yake. **2.** kiungo. **~ energy**, nishati muungo: nishati iliyomo katika muungo wa kikemikali baina ya atomu mbili. **3.** (kwa biashara) *goods in ~,* bidhaa zilizo forodhani ambazo hazijalipiwa ushuru. **4.** *in ~s,* -liofungwa; -liokatika hali ya utumwa. *burst one's ~s,* -wa huru. **-age** *n.* utumwa; kifungoni.
**bone** /bəʊn/ *n.* **1.**mfupa; mwiba wa samaki. **2.** *(fig.) to the ~,* ndani kabisa. *be dranched to the ~,* roa chapachapa. *have a ~ to pick with sb.,* taka kumshtaki fulani.


**bone joint**

**bonfire** /'bɒnfaɪə(r)/ *n.* moto mkubwa uwashwao kwa sherehe ya jambo fulani.
**bonus** /'bəʊnəs/ *n.* bahashishi; zawadi; malipo ya ziada baada ya kazi, kwa kawaida hutolewa kwa msimu.
**book** /bʊk/ *n.* **1.** kitabu; msahafu; biblia; daftari; sura. **3.** *bring sb. to ~,* shtaki; taka sababu ya kosa; ita ili kutoa maelezo. *be in sb.'s good (black, bad) ~s,* kupendeza (kutopendeza) kwa mtu fulani. *v.t.* **1.** andika katika daftari. **2.** wekeza, oda tiketi ya safari. **~-case** *n.* kabati la vitabu. **~ing-clerk** *n.* karani auzaye tikiti. **~ing-office** *n.* ofisi inayouza tiketi. **~keeper** *n.* karani ambaye kazi yake ni kuandika mahesabu. **~-keeping** *n.* kazi ya kutunza mahesabu ya mapato na matumizi.
**boom**¹ /bu:m/ *n.* **1.** foromali ndogo (ya marikebu). **2.** boriti iliyofungiwa mlingoti kwa kutweka au kutoa shehena melini. **3.** kizuizi kama magogo` kilicho wekwa mtoni au bandarini kuzuia vyombo kuingia.
**boom**² /bu:m/ *v.i./t./n.* (kwa mizinga, ngurumo, etc.) nguruma; mngurumo.
**boom**³ /bu:m/ *n.* ustawi au nafuu ya ghafla kwa bidhaa.
**boomerang** /'bu:məræŋ/ *n.* **1.** gongo bapa mpindiko ambalo likirushwa humrudia mrushaji. **2.** jambo baya linalomrudia mtu mwenyewe aliyekusudia kufanya ubaya.
**boot** /bu:t/ *n.* kiatu cha kutumbukiza mguuni; buti. *have one's heart in one's boots,* ogopa mno.


**boot**

**border** /'bɔ:də(r)/ *n.* **1.** ukingo; pindo; taraza. **2.** mpaka. *v.t.* pakana na; karibia; tarizi; pinda.
**bore**¹ /bɔ:(r)/ *v.t.* toboa; pekecha. *n.* **1.** kitobo. **2.** kipimo cha duara ya tundu ya mtutu wa bunduki, mzinga, etc.
**bore**² /bɔ:(r)/ *v.t.* chosha; chokoza; udhi; sumbua; kera. *n.* mchokozi; muudhi; msumbufu.
**boron** /'bɔ:rɒn/ *n.* elementi ya

kemikali ambayo huvumilia sana joto la kiwango kikubwa, hutumiwa sana katika shughuli za kukazanisha metali na katika vinu vya nyuklia

**borrow** /'bɒrəʊ/ *v.t./i.* azima; kopa; iga; fuatisha.

**bosom** /'bʊzəm/ *n.* kifua; moyo. *a ~ friend,* msiri.

**boss** /bɒs/ *n.* (colloq.) bwana; msimamizi; bosi; mkuu; meneja.

**botany** /'bɒt(ə)ni/ *n.* taaluma ya maumbile, hali, jeni, na aina za jamii ya miti na manufaa yao. **botanist** *n.* mtaalamu wa mimea. **botanical** *adj.* -a mimea.

**both** /bəʊθ/ *adj./n./pron.* -ote -wili (mbili). *conj.* na. *~ this and that,* hiki na kile.

**bother** /'bɒðə(r)/ v.i./t. **1.** sumbua; hangaika; hangaisha; kera; udhi; chokoza. *Don't ~,* haidhuru. *Its no ~,* si kazi kubwa; si kitu. **2.** jikalifu. *n.* udhia; taabu; kisirani; matata; kero.

**bottle** /'bɒtl/ *n./v.t.* chupa; tia katika chupa; ficha hisia.

**bottom** /'bɒtəm/ *n.* chini; tako. *~ upwards,* kifudifudi. *at ~,* hasa, kwa kweli. **~less** *adj.* -a kina kirefu mno. *the ~less pit,* shimo la maangamizi; motoni.

**bough** /baʊ/ *n.* tawi kubwa la mti; utanzu.

**boulder** /'bəʊldə(r)/ *n.* jabali lililolainishwa kutokana na kuroweshwa sana na maji.

**bounce** /baʊns/ *v.i./t.* **1.** ruka kama mpira; dunda. **2.** tupa; tupwa kwa nguvu; ingia kwa ghafla. *~ into a room,* ingia chumbani ghafla.

**bound**[1] /baʊnd/ *n.* mpaka; mipaka; upeo; kikomo; mwisho. *v.t.* weka mipaka ya. **~ary** *n.* mpaka.

**bound**[2] /baʊnd/ *v.i.* ruka. *by leaps and ~s,* upesi, haraka sana. *n.* mruko.

**bound**[3] /baʊnd/ *adj. (for)* wa tayari kwenda. *The ship is ~ for Bombay,* meli inakwenda Bombay.

**bound**[4] /baʊnd/ *p.p.* ya **bind** (kwa matumizi maalumu kama) *The book is well ~,* kitabu kimetiwa jalada vizuri. *I am ~ to go,* lazima niende. *~ up in (be),* shughulika sana (na).

**bounty** /'baʊnti/ *n.* ukarimu; bahashishi; baraka; zawadi. **bounteous, bountiful** *adj.* -paji; karimu; -ingi.

**bout** /baʊt/ *n.* zamu; kipindi; jaribio; shindano.

**bow**[1] /bəʊ/ *n.* **1.** upinde, uta. *draw the long ~,* piga chuku. **2.** fundo.

**bow**[2] /baʊ/ *v.t./i.* inama; salimu; pinda; inamisha. *(fig.) ~ to,* kubali; tii; sujudia.

**bow**[3] /baʊ/ *n.* gubeti; omo.

**bowels** /'baʊəlz/ *n.* matumbo.

**bowl**[1] /bəʊl/ *n.* bakuli.

**bowl**[2] /bəʊl/ *v.i./t.* **1.** tupa mpira katika mchezo wa kriketi. *~ along,* enda upesi. **~er** *n.* **1.** mtupaji mpira katika mchezo wa kriketi. **2.** aina ya kofia.

**box**[1] /bɒks/ *n.* sanduku; bweta; kasha; kijaluba. *Christmas ~,* zawadi ya krismasi.

**box**[2] /bɒks/ *n./v.t./i.* **1.** pigo. **2.** *~ the ears,* piga makofi. **3.** pigana ngumi.

**boy** /bɔɪ/ *n.* **1.** mtoto mdogo wa kiume; mvulana. **2.** boi; mtumishi mwanamme. **~hood** *n.* ujana; utoto. **~ish** *adj.* -a mtoto mwanamme.

**boycott** /'bɔɪkɒt/ *v.t./n.* gomea; piga pande.

**brace**[1] /breɪs/ *n.* kitu cha kufungia au kukazia; ukanda. *~ and brit,* kekee. *v.t.* tia nguvu; burudisha; kaza. *a bracing climate,* hali ya hewa ya kuburudisha.

**brace**[2] /breɪs/ *n.* jozi.

**bracelet** /breɪslət/ *n.* kikuku; bangili; pingu; kingaja; kilinzi.

**braces** *n.* kanda za kushikilia suruali.

**bracket** /'brækɪt/ *n.* **1.** kitegemeo cha mti au cha chuma. **2.**alama za mabano ( ), [ ], { } zitumiwazo katika maandishi.

**brain** /breɪn/ *n.* ubongo, akili. *have a good ~,* -wa na akili nyingi.

**brake** /breɪk/ *n.* kizuio; breki.

**bran** /bræn/ *n.* makapi ya nafaka; kumvi; pumba.

**branch** /brɑ:ntʃ/ *n.* **1.** tawi, sehemu




**brain | ubongo**

ya kitu inayofanana na tawi. ~ *office*, ofisi tanzu ya ofisi kuu. *v.i.* gawika; fanya panda.

**brand** /brænd/ *n.* **1.** kinga; alama; chapa; stempu; muhuri. **2.** alama ichapwayo kwa chuma cha moto; nembo ya biashara. *the best ~s of coffee*, aina bora za kahawa. *v.t.* tia alama ya chuma. *(fig.)* tia alama ya kudumu juu ya. *be ~ed as a coward*, julikana kuwa ni mwoga. **~new** *adj.* -pya kabisa.

**brandy** 'brændi/ *n.* brandi: aina ya mvinyo mkali utengenezwao kwa zabibu.

**brass** /brɑ:s/ *n.* **1.** shaba nyeupe. **2.** *(colloq.)* ufedhuli; usafihi; ujuvi; ushupavu. **~ band** *n.* kundi la wapiga matarumbeta.

**brave** /breɪv/ adj. -shujaa; hodari; shupavu; jasiri; thabiti. **~ly** *adv.* kishujaa; kishupavu; kijasiri; **~ry** *n.* ushujaa; ujasiri; ushupavu.

**brawl** /brɔ:l/ *n./v.i.* ugomvi; gombana kwa kelele.

**brawn** /brɔ:n/ *n.* nguvu ya mwili; gimba; unene. **~y** *adj.* -enye nguvu nyingi.

**bray** /breɪ/ *v.i./n.* lia kama punda; mlio (kama wa punda).

**breach** /bri:tʃ/ *n.* **1.** uvunjaji (sheria, ahadi. etc.). ~ *of the peace*, kuvunja amani kwa kupigana upya. **2.** tundu; ufa (kama katika ukuta au boma lilipobomoka.)

**bread** /bred/ *n.* mkate. **~fruit**, mfenesi wa kizungu; mshelisheli.

**breadth** /bredθ/ *n.* upana; mapana. ~ *of mind*, hali ya kuzingatia fikira za watu wote. *to have ~ of vision*, kupima na kuzingatia mambo.

**break** /breɪk/ *v.t./i.* **(broke, broken)** **1.** vunja; pasua; banja; haribu. **2.** ~ *away*, **1.** tenga. **2.** (kwa mtu) toroka; kimbia. ~ *down*, **1.** (kwa mashine, mashauri) haribika; vunjika. **2.** (kwa afya) legea; dhoofika. **3.** vunjika moyo; bubujika machozi. ~ *sth. down*, bomoa. ~ *in (to)*, ingia kwa nguvu. ~ *in on*, dakiza; ingia kwa ghafla. ~ *sth. off*, **1.** kata; vunja. **2.** komesha. ~ *out*, **1.** (moto,vita, ugonjwa) tokea; onekana; ripuka. **2.** (wafungwa) toroka. ~ *up*, **1.** vunjika; vunja. **2.** poteza nguvu au afya. ~ *a record*, vunja rekodi. ~ *back of*, maliza sehemu ya kazi ngumu. ~ *the ice*, *(fig.)* anza kuzungumza juu ya jambo kubwa. **3.** vunja sheria; halifu; asi. **4.** acha; simama; simamisha kwa muda. **5.** punguza ukali wa. *n.* **1.** mvunjiko; mpasuko. *the ~ of day, day ~*, mapambazuko. **2.** nafasi; mapumziko. *without a ~*, bila kupumzika, mfululizo.

**breakfast** /'brekfəst/ *n.* chakula cha asubuhi; kifungua kinywa; kisabeho.

**breast** /brest/ *n.* **1.** maziwa; machuchu. **2.** kifua; kidari. **3.** moyo. *a troubled ~*, moyo wenye hangaiko. *make a clean ~ of*, kiri; ungama yote.

**breath** /breθ/ *n.* pumzi; roho. **~less** **1.** -a kutwetatweta. **2.** -a kukata pumzi. **3.** -a kupuma. *take away the ~*, shtusha; shangaza. *under the breath*, kwa kunong'ona; kwa hofu; polepole.

**breathe** /bri:ð/ *v.i./t.* **1.** vuta pumzi; pumua; pumzika; tanafasi; ishi. **2.** nong'ona. *Don't ~ a word*, usinong'one kitu. *~e one's last*, kata roho.

**breed** /bri:d/ *v.t./i.* **(bred)**. **1.** zaa; zalisha. **2.** fuga. **3.** lea. **4.** leta; sababisha. *Wars ~ poverty*, vita huleta ufukara. *n.* jamii ya wanyama wa aina moja. **~er** *n.* mfugaji anayezalisha wanyama bora na wenye afya. **~ing** *n.* (hasa)

uzazi; malezi; ufugaji.
**breeze** /bri:z/ *n.* upepo. **breezy** *adj.* -a upepo. *(fig.)* -a furaha; -changamfu.
**brew** /bru:/ *v.t./i.* pika; sindika pombe. **2.** *(fig.)* waza; fikiri; tunga; buni uovu. **~er** *n.* mpika pombe. **~ery** *n.* kiwanda cha kutengeņezea na kusindikia pombe.
**bribe** /braɪb/ *v.t./n.* lisha rushwa; mrungura; hongo. **~ry** *n.* rushwa; hongo; mrungura; ulaji; ulishaji hongo; rushwa.
**brick** /brɪk/ *n./v.t./adj.* tofali; ziba kwa matofali; -a matofali. **~-bat** *n.* kipande cha tofali. **brick-kiln** *n.* tanuri; tanu ya kuchomea matofali. **~layer** *n.* mwashi ajengaye kwa matofali.
**bridal** /'braɪdl/ *adj.* -a bibi arusi; -a arusi.
**bride** /brɪd/ *n.* bibi arusi. **~groom** n. bwana arusi.
**bridge** /brɪdʒ/ *n.* **1.** daraja; kantara. **2.** jukwaa juu ya sitaha ya meli ambapo maafisa hutoa amri zao. **3.** mtatago.



**bridge**

**bridge** /brɪdʒ/ *n.* mchezo wa karata wa watu wanne.
**brief** /bri:f/ *adj.* fupi; -liodumu kwa muda mfupi. *in ~,* kwa ufupi. *hold a ~ for,* tetea; daia. **~ly** *adv.* kwa ufupi; kwa muhtasari. **~ness** *n.* ufupi.
**bright** /braɪt/ *adj.* **1.** -enye kung'aa; -eupe; safi; -angavu; -a furaha; -changamfu; -kunjufu; -cheshi. **2.** *(fig.)* enye akili.
**brilliant** /'brɪliənt/ *adj.* -a kung'aa; -a kumetameta; enye akili; -zuri. **brilliance** *n.* mng'ao; umahiri; uhodari mkubwa.
**bring** /brɪŋ/ *v.t.* *(brought)* leta. *to ~ him to agree,* kumkubalisha. *to ~ to my (his, our, etc.) notice,* kunifahamisha (kumfahamisha, kutufahamisha, etc.). *~ up,* lea; tapika; simamisha. *bring an action against,* shtaki; dai. *bring home,* dhihirisha; thibitisha; eleza bayana.
**brisk** /brɪsk/ *adj.* -a mwendo wa haraka mwepesi. **~ness** *n.* wepesi.
**brittle** /'brɪtl/ *adj.* -epesi kuvunjika japo ngumu; dhaifu.
**broad** /brɔ:d/ *adj.* -pana. *(fig.)* **~-minded** *adj.* mtu mwenye maarifa mapana na huru. *~ daylight,* mchana. *a ~ hint,* dokezo dhahiri. **~en** *v.t./i.* panua; panuka.
**broadcast** /'brɔ:dkɑ:st/ *v.t.* tangaza. *n.* matangazo ya redio au televisheni.
**broker** /'brəʊkə(r)/ *n.* wakala; dalali.
**bromine** /'brəʊmi:n/ *n.* kampaundi ya elementi ya kemikali majimaji ya rangi nyekundu iliyokoza, hutumika katika madawa na fotografia.
**bronchitis** /brɒŋ'kaɪtɪs/ *n.* ugonjwa wa kifua.
**bronze** /brɒnz/ *n.* shaba nyeusi.
**brooch** /brəʊtʃ/ *n.* kifungo cha kujipambia; bizimu.
**brood** /bru:d/ *n.* makinda yaliyo-anguliwa pamoja. *v.i.* atamia. *(fig.)* fikiri; tafakari; shika tama.
**brook** /brʊk/ *n.* **1.** kijito mdogo. **2.** vumilia, hasa upinzani.
**broom** /bru:m/ *n.* ufagio; fagio; mfagio.
**broth** /brɒθ/ *n.* mchuzi wa nyama au samaki.
**brother** /'brʌðə(r)/ *n.* ndugu wa kiume. **~-in-law** *n.* shemeji. **~hood** *n.* udugu; umoja wa watu. (**half-** ~ *n.* ndugu wa baba au mama mmoja tu).
**brow** /braʊ/ *n.* **1.** paji la uso; kipaji; kikomo cha uso. **2.** ukingo wa kilima. **~beat** *v.t.* onea; dhulumu; ogofya; tolea maneno au kazia macho.
**brown** /braʊn/ *adj./n.* rangi kama ya majani makavu; hudhurungi; kahawia; rangi ya udongo.
**browse** /braʊz/ *v.i.* **1.** tafuna majani kama wafanyavyo ng'ombe. **2.** *(fig.)* soma maandishi juujuu bila ya makini makubwa.
**bruise** /bru:z/ *v.t.* chubua; babua; gunyua, chuna. *n.* mchubuko; ubabukaji.

**brute** /bru:t/ *n.* **1.** mnyama; hayawani **2.** mtu mbaya; katili. **brutish** *adv.* -a kinyama; -a kikatili; -enye nguvu bila akili. **brutal** *adj.* katili; -kali; -korofi.

**brutality** /-təli/ *n.* ukatili; ukali; ukorofi.

**bubble** /'bʌbl/ *n./v.i.* povu; toa povu; umuka; chemka. ~ *over,* fufurika.

**buck** /bʌk/ *n.* dume wa jamii ya paa, mbuzi, sungura, etc.

**bucket** /'bʌkɪt/ *n.* ndoo.

**buckle** /'bʌkl/ *n.* kifungo; bizimu. *v.t./ i.* **1.** funga kwa bizimu. **2.** pinda au pindika kwa moto; bonyea.


**buckle**

**bud** /bʌd/ *n.* jicho la ua; tumba; chipukizi. *v.i.* (**-dd-**) chipua; chanua; mea; kua.

**budget** /'bʌdʒɪt/ *n.* **1.** bajeti; makisio. **2.** habari; taarifa.

**buffalo** /'bʌfələʊ/ *n.* (**-oes**) nyati; mbogo.

**bug** /bʌg/ *n.* jamii ya wadudu kama kunguni; kosa au kirusi katika kompyuta.

**build** /bɪld/ *v.t./i* (**built**) **1.** jenga; unda. **2.** ~ *up,* ongeza nguvu; kuza; ziba. ~ *upon,* tumainia; tegemea. *n.* umbo. *a man of powerful ~,* mtu mwenye umbo la nguvu.

**bulb** /bʌlb/ *n.* **1.** umbo la kitunguu. **2.** balbu; tungi (hasa la taa ya umeme). **~ous** *adj.* -a mviringo.

**bulge** /bʌldʒ/ *v.i /t.* vimba; tokeza; betuka. *n.* uvimbe; mbetuko; mtoki.


**bulb**

**bulk** /bʌlk/ *n.* **1.** wingi; ukubwa. **2.** sehemu iliyo kubwa (ya ). *sell by ~,* uza kwa jumla. **~y** *adj.* -kubwa tena -zito. **~head** *n.* kiambaza msaada.

**bull** /bʊl/ *n.* **1.** fahali . **2.** dume la tembo, nyangumi, nyati au wanyama wengine wakubwa. *take the ~by the horns,* jusurisha; kabiliana na jambo kwa ujasiri. **~'s-eye** *n.* katikati kabisa ya shabaha.

**bulldozer** /'bʊldəʊzə(r)/ *n.* buldoza; tingatinga.

**bullet** /'bʊlɪt/ *n.* risasi ya bunduki. **~-proof** *adj.* isiyopenya risasi.

**bulletin** /'bʊlətɪn/ *n.* taarifa rasmi; kijarida cha habari za taasisi fulani kitolewacho mara kwa mara.

**bullock** /'bʊlək/ *n.* ng'ombe maksai.

**bully** /'bʊli/ *n.* mchokozi; mtesi; mshari; jeuri. *v.t.* chokoza; onea; dhulumu.

**bulwark** /'bʊlwək/ *n.* **1.** boma; kinga. **2.** ukuta mdogo uliozunguka sitaha ya merikebu. **3.** nguzo; kakara.

**bump** /bʌmp/ *n.* uvimbe; mtoki; mgongano. *v.t./ i.* gonga; gongana; dunda.

**bumper** /'bʌmpə(r)/ *n.* **1.** kikombe; bilauri; gilasi. ~ *harvest,* mavuno makubwa mno. **2.** bamba linalosaidia gari isiumie wakati inapogonga kitu.

**bun** /bʌn/ *n.* mkate mdogo tena mtamu; andazi; hamuri.

**bunch** /bʌntʃ/ *n.* kicha; chana; fungu; tita; shada la maua. *v.t./i.* kusanya; kusanyika; funga pamoja; songana.

**bundle** /'bʌndl/ *n.* furushi; robota; bunda. *v.t./i.* funga pamoja; tutika; fungasha.

**bungalow** /'bʌŋgələʊ/ *n.* nyumba ndogo; bangaloo.


**buoy**

**bunk** /bʌŋk/ *n.* kitanda maalumu kama sanduku refu melini au kwenye garimoshi.

**buoy** /bɔɪ/ *v.t./n.* weka boya; weka chelezo, boya; chelezo; mlezi. ~ *up,* eleza mtu au kitu majini kisizame; tia moyo. **~ant** *adj.* -a kuelea; -epesi; -tumainifu; changa-mfu; -a furaha. **~ancy** *n.* wepesi; uchanga-mfu.

**burden** /'bɜ:dn/ *n.* mzigo; shehena; udhia; taabu. *beast of ~,* mnyama wa kubebea mizigo.

**bureau** /'bjʊərəʊ/ *n.* **1.** ofisi; dawati; meza yenye vitoto. ~ *de change,*kituo cha kubadilishia fedha.

**burglar** /'bɜ:glə(r)/ *n.* mwizi aingiaye ndani ya jengo kwa kusudi la kuiba, kudhuru au kuharibu mali. **~y** *n.* wizi wa kuingia ndani ya jengo.

**burn** /bɜ:n/ *v.t./i.* (**burnt, burned**) choma; chomeka; unguza; teketea; ungua; teketeza. *n.* kuchomwa; kuungua. ~ *one's fingers*, teseka kwa kuingia katika jambo lisilokuhusu.

**burrow** /ˈbʌrəʊ/ *v.t./i.* **1.** fukua; ingia shimoni. *n.* kishimo cha mnyama; kipango. **2.** *v.t.* chunguza; peleleza; tafuta.

**bursar** /ˈbɜ:sə(r)/ *n.* mtunza fedha. **~y** *n.* fedha za shule au chuo zilipwazo kama ufadhili wa ada ya masomo kwa mwanafunzi.

**burst** /bɜ:st/ *v.t./i.* **1.** pasua; pasuka. **2.** toka, penya, ingia kwa ghafla. *n.* jambo la ghafla kama kupasuka, kucheka, kulia. ~ *into tears*, angua kilio.

**bury** /ˈberi/ *v.t.* **1.** zika; ficha; fukia; sitiri; sahau. *buried in thoughts*, zama katika mawazo, fikira. **burial** *n.* kuzika; mazishi; maziko. *burial-ground*, mava; makaburini.

**bus** /bʌs/ *n.* gari kubwa ya abiria; basi.

**busbar** /ˈbʌsbɑ:/ *n.* kipitishi chenye kuweka na kugawanya umeme. **bush** /bʊʃ/ *n.* pori; kichaka; gugu; msitu. *beat about the* ~, sema kwa mzunguko.

**business** /ˈbɪznəs/ *n.* **1.** shughuli; kazi. **2.** biashara; uchumi. **3.** jambo. *mind your own* ~, hayakuhusu.

**bust** /bʌst/ *n.* kifua cha mtu; sanamu iliyochongwa ya sehemu ya kifua, hasa cha mwanamke.

**bustle** /ˈbʌsl/ *v.t./i.* jishughulisha kwa ghasia; harakisha; pirikisha. *n.* haraka; shughuli nyingi; cha kukingama cha ndani ya meli au ndege.

**busy** /ˈbɪzi/ *adj.* -enye kazi au shughuli nyingi. *v.t.* ~ *oneself*, jishughulisha. **~body** *n.* mpekuzi; mbeya.

**but** /bət/ *conj.* lakini; ila; isipokuwa; tu. *He all* ~ *fell*, nusura aanguke.

**butcher** /ˈbʊtʃə(r)/ *n.* mchinja nyama; muuaji; katili.

**butter** /ˈbʌtə(r)/ *n.* siagi; samli. **~milk** *n.* mtindi wa maziwa. **~fly** *n.* kipepeo.


**butterfly**

**buttock** /ˈbʌtək/ *n.* tako; kitako.

**button** /ˈbʌtn/ *n.* kifungo; kibonye; swichi ya kuwashia umeme.

**buttress** /ˈbʌtrɪs/ *v.t.* kuegemeza. *n.* nguzo ya kuegemeza ukuta wa nje.

**buy** /baɪ/ *v.t.* nunua. ~ *off*, zuia au honga kwa kulipa fedha.

**buzz** /bʌz/ *n.* mvumo kama wa nyuki. *v.i.* vuma kama nyuki; ng'ong'a.

**by** /baɪ/ *prep.* katika; kando ya; karibu na; na; kwa. *He was killed* ~ *a soldier*, aliuliwa na askari. *day* ~ *day*, kila siku ipitayo. ~ *night*, usiku. ~ *noon*, adhuhuri. ~ *themselves*, peke yao.

## Cc

**cab** /kæb/ *n.* **1.** gari ndogo ya abiria. *a taxi~*, gari ya teksi. **2.** chumba cha mwendeshaji katika garimoshi.

**cabbage** /ˈkæbəɪdʒ/ *n.* kabichi; mboga majani yenye umbo kama tufe.


**cabbage**

**cabin** /ˈkæbɪn/ *n.* **1.** nyumba ndogo kama kibanda; **2.** kijumba, hasa cha melini; shetri.

**cabinet** /ˈkæbɪnət/ *n.* **1.** kabati la kutunzia vitu au kuonyeshea biashara. **2.** baraza la mawaziri. **~maker** *n.* seremala atengenezaye samani. **~minister** *n.* waziri.

**cable** /ˈkeɪbl/ *n.* **1.** amari; kamba nene ya katani au ya usumba. **2.** waya wa simu uliotandikwa chini ya ardhi au baharini; simu. *v.t.* piga simu.

**cacao** /kəˈkɒ:əʊ, -ˈkəɪəʊ/ *n.* mkakao; aina ya mti; mbegu zake hutumika kutengeneza kokoa.

**cache** /kaʃ/ *n.* ficho la fedha, vyakula au zana za kivita.
**cackle** /'kækl/ *v.i./n.* tetea; semasema bila ya mpangilio; cheka kwa sauti ya kipumbavu; uteteaji wa kuku.
**cactus** /'kæktəs/ *n.* jamii ya mimea kama mpungate.
**cadet** /kə'dət/ *n.* mwanafunzi, hasa wa ngazi ya afisa katika jeshi.
**cadmium** /'kadmɪəm/ *n.* kadimiamu: elementi ya kemikali ya namba 48, yenye rangi ya fedha na nyeupe inayofanana na bati.
**caecum** /'si:kəm/ *n.* sikamu; chekumu: tawi butu la utumbo baina ya utumbo mpana na utumbo mwembamba.
**caesium** /'si:zɪəm/ *n.* siziamu: elementi ya metali yenye rangi ya fedha.
**caesura** /sɪ'zjʊərə/ *n.* kisito; kituo kidogo katika mstari wa ubeti wa shairi.
**cafe** /'kæfeɪ/ *n.* mkahawa.
**caffeine** /'kæfɪ:n/ *n.* kafeni: aina ya dawa inayopatikana katika buni isisimuayo mwili.
**cage** /keɪdʒ/ *n.* kizimba; tundu. *v.t.* fungia tunduni.
**cake** /keɪk/ *n.* keki; mkate mtamu; donge; kipande. *a ~ of soap*, kipande cha sabuni.
**calabash** /'kaləbaʃ/ *n.* *~ tree*, mbuyu. *~ fruit*, buyu; tungu, tunguri; kibuyu.
**calamity** /ˌkə'læməti/ *n.* janga; msiba mkubwa; hasara; maafa; baa; balaa.
**calcium** /'kælsiəm/ *n.* kalisi; kalisiamu: elementi ya kemikali ya namba atomia 20, ni metali yenye rangi ya kijivu kama fedha na hupatikana kwenye chokaa, jasi au gange. **~ carbonate**, kabonati ya kalisiamu: kampaundi nyeupe isiyomumunyuka inayotokea kimaumbile katika chokaa, jasi au gange. **~ hydroxide**, hidroksidi ya kalisiamu: kampaundi inayo-mumunyuka iliyo kwenye chumvi wakati alkalini inapoongezwa maji. **~ oxide**, oksidi ya kalisiamu: alkalini mango nyeupe inayopatikana kwa kuchomwa kwa gange.
**calculate** /'kælkjuleɪt/ *v.t./i.* hesabu; fikiri; jishauri. *~ upon*, tumainia; tegemea; amini. **calculator** *n.* ala ya elektroniki itumiwayo kufanyia hesabu.
**calculus** /'kalkjʊles/ *n.* kalkulasi: tawi la hisabati linalohusu viwango vya ubadilikaji.
**caldera** /kɒl'dɛ:rə/,-'dɪərə/ *n.* lusoko: bonde lenye umbo la bakuli linalofanyika wakati volkano inapobomoza kileleni mwa mlima.
**calendar** /'kalɪndə/ *n.* kalenda.
**calf**[1] /kɑ:f/ *n.* (**calves**) ndama.
**calf**[2] /kɑ:f/ *n.* (**calves**) misuli ya mguu.
**calibrate** /'kalɪbreɪt/ *v.t.* sawazisha; geza; rekebisha chombo cha kupimia ili kionyeshe data halisi.
**calibration** /ˌkælɪ'breɪʃn/ *n.* ugezaji; kigezotundu; usawazishaji.
**calibre** /'kalɪbə/ *n.* **1.** kipimo cha duara cha tundu ya mwanzi wa bunduki au mzinga. **2.** kima cha akili au uwezo wa mtu.
**call** /kɔ:l/ *v.t./i.* **1.** taja; ita; piga simu; alika, adhini. *Go and ~ him*, nenda ukamwite. **2.** dhani. *I ~ that a mistake*, nadhani hilo ni kosa. *~ out*, lia; guta; piga kelele. **3.** zuru; enda kumjuilia au kumtembelea mtu. *~ for*, taka; hitaji. *Your plan will ~ for a lot of money*, mpango wako utahitaji fedha nyingi. *~ up*, kumbuka. *~ to account*, shtaki; hukumu. *~ together*, kusanya. *n.* kilio; ukelele; ukemi; ziara; haja; ombi; simu; wito.
**callous** /'kæləs/ *adj.* **1.** -gumu; -enye ganzi. **2.** shupavu; katili; -sugu.
**calm** /kɑ:m/ *adj.* shwari; -tulivu; pole; makini. *n.* shwari; utulivu; amani; raha. *v.t./i.* tuliza; tulia; fariji; nyamazisha; tulia; nyamaza.
**calorie** /kæləri/ *n.* kalori: kiasi cha joto kinachohitajika kupandisha kima cha gramu moja ya maji kwa digirii moja ya sentigredi; kizio cha joto sawa na juli 4.18. **calorific value** *n.* thamani ya kalori; idadi

ya kalori zinazotolewa na kitu kinapoungua. **calorimeter** *n.* kalorimita: kifaa cha kupimia kiasi cha joto. **calorimetry** *n.* upimaji joto: sayansi inayohusika na upimaji joto.

**calyx** /'kalɪks, 'keɪ-/ *n.* kaliksi: sehemu yote ya ua inayokingwa na sepali kwa nje.

**cam** /kæm/ *n.* kemu: kipande kitokezacho katika gurudumu la mashine cha kubadili mwendo usiwe wa kuzunguka ila uwe wa kupanda na kushuka.

**cambium** /'kambɪəm/ *n.* kambiamu: seli maalumu hai za mti zinazohusika na ukuaji wa kigogo na mizizi, hutokana na kugawanyika kwa seli hizo.


camel

**camel** /'kæml/ *n.* ngamia.


camera

**camera** /kæmərə/ *n.* kamera: chombo cha kupigia picha kwa kutumia mwanga. *in ~,* faragha; si hadharani.

**camouflage** /'kæməflɑ:ʒ/ *v.t./n.* kudanganya macho; ficha; kidanganya macho; majificho.

**camp** /kæmp/ *n.* kambi; kituo.*v.i.* tua safarini; piga kambi.

**campaign** /kæm'peɪn/ *n.* **1.** muda vita vinapoendelea. **2.** shughuli yenye kusudi maalumu, e.g. -a kushinda maradhi fulani, kampeni etc.

**can**[1] /kən; kæn/ *v.i* (**could**) weza. *It ~ be got;* inaweza kupatikana. *It ~ be heard,* inaweza kusikika.

**can**[2] /kæn/ *n.* kopo la bati; mkebe. *v.t.* (**-nn-**) tia koponi; tia katika mkebe.

**canal** /kə'næl/ *n.* njia ya maji iliyofanywa na watu; mfereji.

**canary** /kə'neəri/ *n.* kirumbizi.

**cancel** /'kænsl/ *v.t.*(**-ll-**) **1.** futa. **2.** tangua; tengua.

**cancer** /'kænsə(r)/ *n.* kansa, saratani: aina ya maradhi yanayosababishwa na kasoro ya ugawanyikaji wa seli mwilini kama vile uvimbe au vidonda.

**candid** /'kændid/ *adj.* -nyofu; -adilifu; -a kusema bila upendeleo; -a kusema bila ya kuficha.

**candour** /'kændə(r)/ *n.* unyofu; uadilifu; maadili; tabia ya kusema bila upendeleo au kuficha.

**candidate** /'kandɪdeɪt/, -dət/ *n.* mtakaji; mtahiniwa. mgombea; mwombaji; ajaribuye kupata cheo, kazi, etc. *The ~ was elected,* mwombaji alichaguliwa.

**candle** /'kændl/ *n.* mshumaa. *The game is not worth the ~,* ni duni kiasi cha kutostahili kushughulikiwa. *burn the ~ at both ends,* poteza kote kuwili.

**cane** /keɪn/ *n.* henzerani; mwanzi mwembamba. *v.t.* piga kwa henzerani. *adj.* -a henzerani. *sugar-~,* muwa. *~ sugar,* sukari ya muwa.

**canine** /'keɪnʌɪn/ *adj.* -a mbwa. *~ teeth,* meno chonge.

**cannibal** /'kænɪbl/ *n.* mtu mla watu. **~ism** *n.* ulaji nyama ya binadamu.

**cannon** /'kænən/ *n.* mzinga. **~ade** *n.* upigaji mizinga. **~-ball** *n.* risasi ya mviringo ya mzinga.

**canoe** /kə'nu:/ *n.* mtumbwi; ngalawa; dau.

**canon** /'kænən/ *n.* **1.** kanuni; sheria. **2.** kasisi mwenyekiti katika halmashauri ya kanisa kuu la jimbo la askofu. **~ical** *adj.* -a kufuata sheria.

**canteen** /kæn'ti:n/ *n.* **1.** mkahawa (hasa katika vyuo, kambi za askari, maofisi). 2 duka la bidhaa za vyakula. **3.** kisanduku cha vyombo vya kupikia na kulia.

**cantilever** /'kantɪli:və/ *n.* wenzo fungwa: mhimili unaozuia roshani.

**canvas** /'kænvəs/ *n.* turubali. *under ~,* kambini; hemani.

**cap** /kæp/ *n.* kofia; kifuniko. *v.t.* vika kofia; funika. *~ block,* faruma.

**capable** /'keɪpəbl/ *adj.* -enye uwezo; stadi; hodari; -enye akili. *a situation ~ of improvement,* hali inayoweza kustawi zaidi. **capability** *n.* uwezo; akili; nguvu.

**capacitor** /kə'pasɪtə/ *n.* kapasita:

chombo cha umeme chenye vipitishi viwili vilivyokaribiana na vilivyotengwa na kihami ili kuhifadhi chaji.




**capacitor | kapasita**

**capacity** /kəˈpæsəti/ *n.* ujazifu: uwezo wa kuweka vitu, wa kufahamu. **capacious** *adj.* -enye nafasi au uwezo mwingi.
**cape**[1] /keɪp/ *n.* vazi lisilo mikono la kuvaa mabegani.
**cape**[2] /keɪp/ *n.* rasi.
**caper** /ˈkeɪp(r)/ *v.i.* rukaruka; randa; chawachawa; chezacheza. *n. cut ~s,* rukaruka.
**capillary** /kəˈpɪləri/ *n.* kapilari: uso wa kioevu unaopanda na kushuka katika neli nyembamba. **~ action**, upandaji na ushukaji wa kioevu katika neli nyembamba.
**capital** /ˈkæpɪtl/ *n./adj.* **1.** mji mkuu wa nchi. **2.** herufi kubwa. **3.** rasilimali; mtaji. **4.** *~ punishment,* adhabu ya kifo. **5.** *(colloq.)* bora. **~ist** *n.* bepari; tajiri. **~ism** *n.* ubepari; mfumo wa uchumi wa kibepari.
**capsize** /kæpˈsaɪz/ *v.t./i.* pindua; pinduka.
**capsule** /ˈkapsjuːl, -sjʊl/ *n.* **1.** kidonge cha dawa kilichovikwa gamba la jelatini. **2.** fumbuza: tunda kavu ambalo hupasuka na kutoa mbegu.
**captain** /ˈkæptɪn/ *n.* **1.** kapteni; nahodha; kiranja. **2.** ofisa mwenye cheo cha kapteni.
**caption** /ˈkæpʃn/ *n.* maelezo mafupi ya habari fulani katika kitabu, gazeti, au chini ya picha.
**captive** /ˈkæptɪv/ *n.* mateka; mfungwa. **captivity** *n.* utumwa; kifungo. **capture** *v.t.* kamata; nyang'anya. *n.* kutia mbaroni; kuteka nyara.
**car** /kɑː(r)/ *n.* gari; motakaa.
**caravan** /ˈkærəvæn/ *n.* **1.** msafara. **2.** nyumba maalumu kwa ajili ya kuishi au kupumzikia, huvutwa na gari ndogo.
**carbohydrate** /ˌkɑbəʊˈhaɪdreɪt/ *n.* kabohaidreti: aina ya chakula cha wanga chenye sukari.
**carbon** /ˈkɑːbən/ *n.* kaboni: elementi yenye namba atomia 6, mkaa (grafiti) ikiwa hali mahuluti na almasi katika hali menyu, pia huwemo katika kampaundi zote mahuluku. **~ cycle**, duru ya kaboni: mzunguko wa kaboni iliyomo katika kaboni dioksidi ya angahewa, viumbehai na mafuta ya nishati. **~ dating**, utaratibu wa kupima ukongwe wa mabaki ya viumbehai kwa kutumia isotopu ya kaboni -14. **~ dioxide**, kaboni dioksidi: aina ya gesi isiyo na rangi wala harufu inayoyeyuka katika maji. **~ monoxide**, kaboni monoksidi: aina ya gesi isiyo rangi wala harufu ambayo ni sumu. **~ paper**, karatasi nyembamba iliyotiwa rangi na kuwekwa katikati ya karatasi nyingine ili kutoa nakala. **~ate** *n.* kaboneti: chumvi ya asidi kaboni. **~iferous** *adj.* -enye kutoa makaa ya mawe.
**carburettor** /ˌkɑːbjʊˈrɛtə/ *n.* kabureta: chombo chenye kuchanganya mvuke wa petroli pamoja na hewa katika mashine, hasa gari.
**carcass, carcase** /ˈkɑːkəs/ *n.* mzoga.
**carcinogen** /kɑːˈsɪnədʒ(ə)n/ *n.* kasinojeni: kitu chochote kinachoweza kusababisha kansa.
**card** /kɑːd/ *n.* karata; kadi. *post ~s,* postikadi: kadi zenye picha na maandishi. *christmas ~s,* kadi za krismasi. *playing ~s,* jozi ya karata. *put one's ~s on the table,* toa mawazo yako yote kuhusu jambo. *playing one's ~s well,* -wa na akili katika kufanya jambo. *be on the ~s,*




**card**

wezekana; elekea kuwa. **~board** *n.* ubao kama karatasi lakini mwembamba.

**cardinal** /'kɑ:dɪnl/ *adj.* -kuu; -a maana. ~ *numbers,* moja, mbili, tatu, etc. ~ *points,* kaskazi, kusi, mashariki, magharibi. *n.* kadinali: mmojawapo wa wakuu wa baraza ya Papa.

**care** /keə(r)/ *n.* **1.** tahadhari; hadhari; uangalifu; utunzaji; usimamizi; himaya. *take ~,* angalia. **2.** taabu; mashaka. *v.i.* shughulika; jali. ~ *for,* penda; tunza; hurumia. **~ful** *adj.* -angalifu. **~less** adj. -zembe. **~taker** *n.* mtunzaji; mwangalizi.

**careen** /kə'rɪə(r)/ *n.* **1.** kazi; ajira. **2.** namna ya maisha; mwenendo; mwendo. *v.i.* enda mbio. ~ *along,* ~ *through (over) a place,* pita upesi bila ya kuangalia.

**caress** /kə'res/ *v.i.* bembeleza; busu; kumbatia; papasa; tomasa.

**cargo** /'kɑ:geʊ/ *n.* (**-oes**) shehena; mizigo.

**carnal** /'kɑ:n(ə)l/ *adj.* -a kuhusu mwili; -a tamaa za kimwili.

**carnival** /'kɑ:nɪvl/ *n.* sikukuu au sherehe ya watu waliovaa mavazi ya mapambo iliyoambatana na ngoma na cherekochereko.

**carnivorous** /kɑ:'nɪv(ə)res/ *adj.* enye kula nyama.

**carol** /'kærəl/ *n.* wimbo wa furaha au kusifu, hasa wa sikukuu ya kuzaliwa kwa Kristo.

**carotid** /kə'rɒtɪd/ *n./adj.* karotidi: mmojawapo wa mishipa ya damu mikuu upelekao damu kwenye kichwa. **~ artery** *n.* ateri ya kichwa: ateri inayotoka kwenye ateri kuu na kupeleka damu kichwani.

**carpal** /'kɑ:p(ə)l/ *adj./n.* -a kilimbilimbi; mmojawapo wa mifupa ya kilimbilimbi.

**carpel** /'kɑ:p(ə)l/ *n.* kapeli: sehemu ya ua ambayo ndani yake mbegu hufanyika.

**carpenter** /'kɑ:pəntə(r)/ *n.* seremala. **carpentry** *n.* useremala.

**carpet** /'kɑ:pɪt/ *n.* zulia. *v.t.* tandaza zulia.

**carry** /'kæri/ *v.t./i.* **1.** chukua. **2.** -wa na. **3.** jitembeza. **4.** shinda; shawishi. ~ *one's point,* shawishi watu wakubali shauri lako. **5.** peleka: *The pipes ~ water to the town,* mabomba hupeleka maji mjini. **6.** endeleza. ~ *all before one,* shinda pingamizi zote. ~ *away,* chukua kupeleka mahali pengine; *(fig.)* vuta nadhari. ~ *forward,* hamishia juu ya ukurasa mwingine. ~ *off,* chukua kwa nguvu. ~ *on,* endeleza; simamia. *carry on!* endelea! ~ *on business,* jishughulisha katika kazi. ~ *on a conversation with someone,* zungumza na fulani. ~ *(sth) through,* timiza; tekeleza; maliza. **carrier** *n.* **1.** mchukuzi; mpagazi; hamali. **2.** kichukuzi: mwambukizaji, aenezaye ugonjwa.

**cart** /kɑ:t/ *n.* gari linalovutwa na mnyama la kuchukua mizigo; mkokoteni. *put the ~ before the horse,* tibua mambo.

**cartilage** /'kɑ:t(ɪ)lɪdʒ/ *n.* ngegedu: aina ya tishu nyororo nyeupe iliyoambatana na ncha za mfupa.

**cartography** /kɑ:'tɒgrəfi/ *n.* uchoraji ramani. **cartographer** *n.* mchoraji ramani.

**cartoon** /kɑ:'tu:n/ *n.* katuni: picha au taswira ya kuchora ya kuchekesha. **~ist** *n.* mchora vikatuni.

**cartridge** /'kɑ:trɪdʒ/ *n.* ala ya risasi ya bunduki. **~ belt** *n.* ukanda wa risasi. **~ paper** *n.* aina ya karatasi nzito, hutumika sana kuchorea picha.

**carve** /kɑ:v/ *v.t./i.* **1.** chora, tia au chonga nakshi. **2.** kata nyama. **carver** *n.* stadi wa kutia nakshi; kisu cha kukatia nyama. **carving** *n.* nakshi.

**case**[1] /keɪs/ *n.* **1.** jambo; kadhia; hali. **2.** mgonjwa. *five ~s of malaria fever,* wagonjwa watano wa malaria. **3.** *(law)* kesi; daawa.

**case**[2] /keɪs/ *n.* kasha; sanduku; bweta; ala.

**cash** /kæʃ/ *n.* fedha; pesa za kutumia; sarafu. *hard ~, spot ~,* fedha taslimu. *v.t.* badili noti; hundi; hawala ya fedha kwa fedha taslimu. **~ier** *n.* mshikafedha. **~book** *n.* daftari la matumizi ya fedha.

**cask** /kɑ:sk/ *n.* pipa; kasiki.

**cassava** /kə'sɑ:və/ *n.* muhogo. *~ leaves,* kisamvu.

**cassock** /'kæsək/ *n.* vazi lililofanana na kanzu, huvaliwa na makasisi, wahudumu na waimbaji wa kanisani.

**cast** /kɑ:st/ *v.t./i.* (**cast**) **1.** tupa; rusha; vurumisha. *~ a vote,* tia voti, piga kura. *~ off clothes,* tupa mavazi makuukuu. *~ anchor,* tia nanga. *~ lots,* piga kura. **2.** mimina, subu katika kalibu. *n.* utupaji; urushaji.

**caste** /kɑ:st/ *n.* jamii ya watu hasa Barahindi wa tabaka lenye hadhi au madhehebu mamoja **2.** kazi, ajira, desturi ya kugawanya watu namna hiyo.


castle

**castle** /'kɑ:sl/ *n.* kasri; ngome; gereza; nyumba yenye boma; husuni. *~s in the air,* mawazo ya kutamani mambo makuu usiyoweza kuyapata.

**castor oil** *n.* mafuta ya mbarika, ya mbono.

**castrate** /kæ'streɪt/ *v.t.* hasi. **~d** *adj.* maksai.

**casual** /'kaʒjʊəl, -zj-/ *adj* . **1.** -a bahati; -a nasibu; -a ajali. **2.** -a zembe. **3.** -a kutokea mara kwa mara. *~ labourer,* kibarua. **~ty** *n.* majeruhi; aliyeuawa; aliyepotea; aliyetoroka vitani; tukio baya; msiba.

**cat** /kæt/ *n.* **1.** paka. *(fig.) Let the ~ out of the bag,* toa nje siri. *Wait for the ~ to jump,* ngojea fikira za watu wengine kabla ya kutoa zako. **2.** mnyama yoyote wa jamii ya paka.

**catalogue** /kætəlɒg/ *n./v.t.* katalogi: orodha ya majina ya vitabu, bidhaa, etc.; orodhesha majina ya vitu kama hivyo.

**catalyst** /'kætəlɪst/ *n.* kichochezi: kitu, kemikali inayobadilisha kasi ya utendanaji.

**catapult** /'kætəpʌlt/ *n.* manati; teo.

**cataract** /'katərakt/ *n.* **1.** maporomoko ya maji. **2.** mtoto wa macho.

**catastrophe** /kə'tastrəfi/ *n.* msiba mkuu; janga.

**catastrophic** /ˌkə'tæstrəfik/ *adj.* -a msiba; -a maangamizi.

**catch** /kætʃ/ *v.t./i.* (**caught**) /kɔ:t/ **1.** kamata; shika; daka; nasa; gwia. **2.** pata; wahi; kuta. *I caught him as he was leaving the house,* nilimkamata alipokuwa akitoka nyumbani. *~ sb. up, ~ up with sb.* au *sth.,* patia; katiza, dakiza maneno. **3.** kutangulia. **4.** patwa, shikwa na ugonjwa. *~ fire,* waka; ungua; ripuka. *~ sb.'s words,* elewa maneno ya fulani. *~ sight of,* ona kwa kitambo kidogo. *~ sb.'s eye,* vuta nadhari ya fulani. *The nail caught her dress,* nguo yake ilinasa msumari. *~ one's breath,* vuta pumzi ghafula kwa sababu ya kushituka. *n.* **1.** udakaji. **2.** hila; mtego. **~ing** *adj.* -a kuambukiza.

**catechism** /'katɪkɪz(ə)m/ *n.* utaratibu wa kimuhtasari wa mafundisho katika mfumo wa maswali na majibu. **catechise** *v.t.* fundisha kwa njia ya kuhoji.

**category** /'kætəgəri/ *n.* aina; namna; jinsi; jamii. **categorical** *adj.* dhahiri; halisi; -a hakika. **categorically** *adv.* kabisa; hasa; bila tofauti.


caterpillar

**cater** /'keɪtə(r)/ *v.i. ~ for,* patia chakula, burudani, etc.

**caterpillar** /'kætəpɪlə(r)/ *n.* **1.** kiwavi; chamvi. **2.** tingatinga; katapila. **3.** ukanda unaounganisha pamoja magurudumu ya mashine; gato.

**cathedral** /kəθi:drəl/ *n.* kanisa kuu katika jimbo la askofu.

**cathode** /'kaθəʊd/ *n.* kathodi:

**1.** elektrodi yenye chaji hasi katika elektrolisisi na kwenye vali themioni. **2.** elektrodi hasi ambapo mkondo umeme unatokea kwenye kuchanganua umeme.

**catholic** /'kæθlɪk/ *adj.* **1.** -a kufaa watu wote popote. **2.** -a kuhusu Wakristo wote. *n.* mfuasi wa kanisa la Roma.

**cation** /'katʌɪən/ *n.* kesheni: molikuli au atomu ambayo ina elektroni chache kuliko protoni na hivyo ioni kubaki na chaji chanya.

**cattle** /'kætl/ *n.* mifugo, yaani ng'ombe, mbuzi, kondoo, etc.

**cauliflower** /'kɑliflaʊə(r)/ *n.* aina ya mboga kama kabechi.



cauliflower

**cause** /kɔ:z/ *n.* **1.** sababu; asili; kusudi. **2.** daawa; kesi; madai. *v.t.* lazimisha; shurutisha; sababisha; amuru. *final ~*, lengo. *ultimate ~*, chanzo; asili. *proximate ~*, sababu.

**causeway** /'kɔ:zweɪ/ *n.* njia ya mawe iliyoinuka juu ya bonde.

**caustic** /'kɔ:stɪk, 'kɒst-/ *adj.* **1.** -a kubabua; -enye uwezo wa kuunguza. **2.** -kali; -chungu. *n.* magadi; chokaa. **~ soda** *n.* soda; magadi.

**cauterize** /'kɔ:tərʌɪz/ *v.t.* choma kwa chuma cha moto au soda ili kuondoa sumu.

**caution** /'kɔ:ʃn/ *n.* uangalifu; hadhari; onyo; indhari. *v.t.* onya; tahadharisha. **cautious** *adj.* angalifu; -enye hadhari.

**cavalier** /ˌkævə'lɪə(r)/ *n.* mpanda farasi.

**cavalry** /'kævlrɪ/ *n.* askari wapanda farasi.

**cave** /kəɪv/ *n.* pango. *to ~ in*, poromoka; bomoka.

**cavity** /'kævəti/ *n.* tundu; shimo; mvungu; ghoba.

**cease** /si:s/ *v.i./t.* koma; tulia; isha; sita.

**cedar** /'si:də(r) *n.* mwerezi; msandali; mkangazi.

**ceiling** /'siɪlɪŋ/ *n.* upande wa chini ya dari.

**celebrate** /'selɪbrəɪt/ *v.t.* **1.** tukuza; sifu; adhimisha; sherehekea. **~d** *adj.* -enye sifa; adhimu; mashuhuri. **celebration** *n.* adhimisho; sherehe; sikukuu. **celebrity** *n.* umaarufu; utukufu; mtu maarufu; mtu mashuhuri.

**celestial** /sə'lestiəl/ *adj.* -a mbinguni.

**celibacy** /'selɪbəsi/ *n.* ujane; useja; ukapera.

**cell** /sel/ *n.* **1.** chumba kidogo; kitundu; seli; mahabusu. **2.** seli: kiini cha asili ya kitu chenye uhai. *All animals and plants are made up of ~s*, wanyama na mimea vyote vimejengwa na seli. **~ body**, sehemu ya nyuroni yenye kiiniseli. **~ division**, mgawanyiko wa seli. **~ membrane**, kiwamboseli: utando wa nje wa seli unaoidhibiti seli pamoja. **~ wall**, ukutaseli: kiambaza cha seli kilichoko nje ya utandoseli kwenye seli za mimea. **dry-cell** *n.* betri.

**cellar** /'selə(r)/ *n.* ghala iliyo chini ya ardhi katika nyumba.

**cellulose** /'sɛljʊləʊz,-s/ *n./adj.* kitu kilicho asili ya nyuzinyuzi ya mimea inayoundwa na kabohidreti kama pamba, katani, etc.; -a seli.

**Celsius** /'sɛlsɪəs/ *adj.* selsiasi; -a sentigredi: kizio cha joto kilichopewa jina la mtaalamu wa Kiswidi, A. Celsius (1701-1744). *~ scale*, kipimo cha Selsiasi: kipimo cha kipimajoto kilichogawanywa katika nyuzi 100.

**cement** /sɪ'ment/ *n.* **1.** saruji; simenti. *v.t.* tia saruji; unga kwa simenti; *(fig.)* imarisha; unganisha.

**cemetery** /'semətri/ *n.* makaburini; mava; maziara.

**censure** /'sɛnʃə/ *v. t./n.* laumu; suta; karipia; fungia; kataza.

**census** /'sensəs/ *n.* sensa; hesabu ya idadi ya watu katika nchi.

**cent** /sent/ *n.* senti: sarafu ya sehemu ya mia kwa moja ya shilingi. *five per ~*, asilimia tano.

**centenary** /sɛn'ti:nəri, -'tɛn-/ *adj./n.* -a baada ya miaka mia; maadhimisho ya kila miaka mia moja kutimia; karne.

**centigrade** /'sentɪgreɪd/ *adj.* -enye digrii 100; e.g. kipimo cha joto kiitwacho ~ *thermometer*, kilichogawanywa sehemu 100. ~ *scale*, kipimo cha sentigradi: kipimajoto kilichogawanywa katika nyuzi 100.
**centimetre** /'sentɪmi:tə(r)/ *n.* kipimo cha sehemu mia kwa moja ya mita, yaani 0.3937 ya inchi.
**centipede** /'sɛntɪpi:d/ *n.* jongoo.
**centre** /'sentə(r)/ *n.* **1.** katikati. **2.** kituo: mahali wanapokutana watu wengi kwa shughuli zao tofauti. *The shopping ~ of a town*, soko la mji. *cultural ~*, kituo cha utamaduni. *information ~*, kituo cha habari. **3.** mtu au kitu kinachovutia. *v.t./i.* weka katikati; -wa katikati. ~ *one's hopes on sth.*, tumainia kitu. **central** *adj.* -a katikati; kuu kabisa. central nervous system, mfumoneva mkuu: mfumo wa ubongo na neva kwenye uti wa mgongo. **central processing unit**, kitengo kikuu cha uchakataji: sehemu ya kompyuta inayofanyayo mikokotoo, kusoma, kufasiri, kuchakata maelezo, kusimamia matumizi ya kumbukumbu na matokeo ya mfumo huo. **centralize** *v.t./i.* weka katikati; -wa katikati.


centipede

**centripetal** /,sɛntrɪ'pi:t(ə)l/ *adj.* tovu: -enye kuelekea katikati. ~ *force*, kani tovu.
**century** /'sentʃəri/ *n.* **1.** muda wa miaka mia. **2.** karne. **3.** mizunguko 100 katika mchezo wa kriketi.
**Cephalopoda** /,sɛfələ'pəʊdə, ,kɛ-/ *n.* sefalopodi: moluska wa jamii ya pweza, ngisi etc.
**cereal** /'sɪəriəl/ *adj./n.* -a nafaka; nafaka.
**cerebrum** /'sɛrɪbrəm/ *n.* ubongo-mbele: sehemu ya mbele ya ubongo wa mnyama.
**ceremony** /'serəməni/ *n.* sherehe. *stand upon ~*, timiza taratibu za jambo kwa ukamilifu. **ceremonial** *adj.* enye kufuata kawaida au taratibu maalumu. **ceremonious** *adj.* - enye sherehe; -enye heshima.
**certain** /'sə:t(ə)n, -tɪn/ *adj.* **1.** yakini; halisi; thabiti; hakika; maalumu; makhsusi. *for ~*, bila shaka. *make ~*, hakikisha. **2.** -moja; fulani. **3.** kidogo; baadhi. *There was a ~ doubt about his health*, kulikuwa na shaka fulani kuhusu afya yake. **~ly** *adv.* bila shaka. **~ty** *n.* yakini; hakika; kweli.
**certificate** /sə'tɪfɪkət/ *n.* hati ya uthibitisho; cheti.
**certify** /'sɜ:tɪfaɪ/ *v.t.* thibitisha; hakikisha. *certified insane*, imethibitishwa na daktari kuwa ni kichaa.
**cervix** /'sə:vɪks/ *n.* mlango wa uzazi: mlango mwembamba wa uterasi unaoungana na uke.
**cessation** /sɛ'seɪʃ(ə)n/ n. kikomo; ukomo; mwisho.
**cesspool** /'sespu:l/ *n.* shimo la kumwagia maji machafu; karo. ~ *of iniquity*, mahali palipojaa maovu.
**CFC** /,si: ef 'i:/ n. ufupisho wa *chlorofluorocarbon*: aina ya kemikali itumikayo katika majokofu na vipozeshaji anuwai inayosadikiwa kuharibu tabaka ya ozoni katika angahewa.
**chafe** /tʃeɪf/ *v.t./i.* **1.** sugua; kanda; chua. **2.** kwaruza; chubua. **3.** udhika; udhi; sumbua. ~ *under insults*, udhika kwa sababu ya matusi.
**chaff** /tʃɑ:f, tʃaf/ *n.* **1.** makapi; kumvi; pumba. **2.** ubishi; mzaha; upuuzi. *v.t.* bishana kwa ucheshi; taniana; fanyiana mzaha.
**chain** /tʃeɪn/ *n.* mnyororo; mkufu; mfuatano; mfululizo. ~ *of mountains*, mfululizo wa milima. ~ *of events*, mfululizo wa mambo. **~ reaction**, utendanaji mfuatano: mfululizo wa mabadiliko ya kikemikali unaotokea kwa kutokea badiliko moja baada ya jingine. *v.t.* funga; fungia mnyororo; zuia.
**chair** /tʃeə(r)/ *n.* kiti. **~man** *n.* mwenyekiti. **~person** *n.* mwenyekiti. *v.t.* ongoza jimbo.

**chalk** /tʃɔ:k/ *n.* chokaa kabla haijachomwa moto; chaki.

**challenge** /'tʃælɪndʒ/ *n.* mwito wa kuja kushindana; changa moto. *v.t.* ita ili kuja kushindana; bishia.

**chamber** /'tʃeɪnbə(r)/ *n.* **1.** (la zamani) chumba; shimo; mvungu. **2.** baraza; mkutano. *~ of commerce,* baraza la wafanya biashara. **3.** ofisi ya mwanasheria. **4.** nafasi katika mzinga au bunduki ambamo hutiwa risasi. **~maid** *n.* mtumishi wa kike anayesafisha vyumba hotelini.

**chameleon** /kə'mi:lɪən/ *n.* kinyonga.

**champagne** /ʃam'peɪn/ *n.* aina ya divai ya kifaransa; shampeni.

**champion** /'tʃæmpiən/ *n.* shujaa; mshindi; bingwa. *v.t.* shindania; pigania; saidia.

**chance** /tʃɑ:ns/ *n.* tukio; bahati; suudi; nafasi; fursa; mwelekeo. *Let ~ decide,* iachie bahati yako ikuamulie. *go on the ~ that sb. will be there,* enda kwa kuwa labda fulani atakuwapo. *take the ~ of a lifetime,* tumia bahati udhaniayo kuwa haitatokea tena maishani. *v.t./i.* tokea kwa bahati. *~ upon,* kuta. *take a ~,* bahatisha.

**chancel** /'tʃɑ:ns(ə)l/ *n.* upande wa kanisa palipo madhabahu.

**chancellor** /'ʃɑ:nsələ(r)/ *n.* (katika nchi nyingine) mkuu wa serikali; mkuu wa chuo kikuu; mkuu wa hazina.

**change** /tʃeɪndʒ/ *v.t./i.* badili; geuza; badilisha; vunja; ghairi; badilika; geuka. *~ one's mind,* ghairi. *The property ~d hands,* mali ilichukuliwa na mtu mwingine. *~ a 1000 shillings note,* vunja noti ya shilingi elfu. *n.* mageuzi; mabadiliko; chenji. *Take a ~ of clothes with you,* chukua nguo za kubadilisha. *~ of state,* badiliko la hali: hali inayotokea wakati dutu fulani inapogeuka kuwa katika hali nyingine, kwa mfano barafu ambayo ni mango kuwa kioevu.

**channel** /'tʃænl/ *n.* **1.** mlangobahari; ufumbi; mfereji; mto. *The ~ is marked by buoys,* mto umewekwa alama kwa maboya. **2.** njia ambayo mawimbi ya sauti hurushwa angani ili yasikike katika redio, televisheni au simu.

**chant** /tʃɑ:nt/ *n.* wimbo. *v.t./t.* imba.

**chaos** /'keɪɒs/ *n.* machafuko; fujo; mparaganyiko; ghasia; mchafukoge. **chaotic** *adj.* -liochafuka.

**chap**[1] /tʃæp/ *v.t./i.* **(-pp-)** (kwa ngozi) pasua; pasuka. *The skin of my hands is ~ped,* ngozi ya mikono yangu imepasuka. *n.* kea; buba.

**chap**[2] /tʃæp/ *n.* *(colloq.)* mwanamme.

**chapel** /'tʃæpl/ *n.* kanisa dogo. **chaplain** *n.* kasisi wa kanisa dogo.

**chapter** /'tʃæptə(r)/ *n.* **1.** sura; mlango. **2.** mfululizo; mlolongo. *a ~ of accidents,* mfululizo wa ajali. *to the end of the ~,* mpaka tamati, mwisho.

**character** /'kærəktə(r)/ *n.* **1.** sifa; wasifu; tabia; hulka; silka; herufi; tarakimu; mwandiko; chapa; mwenendo. *a public ~,* mtu maarufu. *quite a ~,* mtu wa desturi za pekee. **2.** muhusika. **~istic** *adj.* -a peke yake; makhsusi; maalumu. *with his ~ bravery,* kwa ushujaa kama ilivyo desturi yake. **~ize** *v.t.* pambanua; ainisha; fafanua.

**charcoal** /'tʃɑ:kəʊl/ *n.* mkaa; sehemu ya kaboni inayobakia baada ya kitu kuungua.

**charge** /tʃɑ:dʒ/ *n.* **1.** mashtaka. *bring a ~ of murder against sb,* shtaki fulani kwa mauaji. **2.** shambulio. **3.** bei; thamani; gharama; kima; kiasi; malipo. **4.** kiasi cha elektrisiti kilichotiwa katika betri. **5.** utunzaji; ulinzi; dhamana. *be in ~ of,* kuwa dhamana wa. **6.** uagizaji; amri; wasia. *v.t./i.* **1.** shtaki. **2.** shambulia; rukia. **3.** toza; lipisha. *They ~d me 1000 shillings for this shirt,* walinitoza shilingi 1000 kwa shati hii. *How much do you ~ to make a pair of shoes?* utanitoza kiasi gani kushona jozi ya viatu? **4.** tia chaji. *His motor car battery is not ~ d,* betri ya gari yake haina chaji.

5. agiza; amuru. **~r** *n.* **1.** farasi wa vita. **2.** kombe; upatu.
**charity** /'tʃærəti/ *n.* **1.** hisani; huruma; sadaka. **2.** chama cha watu wasaidiao maskini.
**charitable** /'tʃærətəbl/ *adj.* -paji; -enye huruma; -enye hisani.
**charm** /'tʃɑ:m/ *n.* **1.** uzuri; haiba; madaha; upendezaji. **2.** talasimu; hirizi; kago; zinguo; fungo. *v.t. /i.* **1.** vutia; pendeza; liwaza. **2.** roga; zuga. **~ing** *adj.* -enye bashasha; -changamfu; -a kupendeza mno.
**chart** /tʃɑ:t/ *n.* **1.** chati; ramani ya bahari na pwani. **2.** jedwali yenye taarifa za aina yoyote. *v.t.* tengeneza chati.
**charter** /'tʃɑ:tə(r)/ *n.* hati; mkataba. *v.t.* kodi meli au ndege.
**chase** /'tʃeɪs/ *v.t.* winda; saka; fukuza; inga. *n.* uwindaji; usakaji; ufukuzaji.
**chassis** /'ʃasi, -i:/ *n.* chesisi; sehemu ya gari ukiondosha bodi.
**chaste** /tʃeɪst/ *adj.* safi; -takatifu; -zuri; -nyofu. **~n** *v.t.* rudi; ongoza. **chastity** *n.* utakatifu; usafi; ubikira.
**chat** /tʃæt/ *v.i./n.* (**-tt-**) ongea; zungumza; piga soga; piga gumzo. *n.* maongezi; mazungumzo; soga; porojo.
**chatter** /'tʃætə(r)/ *v.i.* **1.** sema upesiupesi. **2.** payuka; poroja.
**cheap** /tʃi:p/ *adj.* rahisi; nafuu; hafifu; duni. **~ly** *adv.* kirahisi. **~en** *v.i.* pungua bei; shuka thamani. **~ness** *n.* urahisi; unafuu.
**cheat** /tʃi:t/ *v.t./i.* danganya; punja; hadaa; laghai; tapeli. *n.* mdanganyifu; mjanja; ayari; laghai; tapeli.
**check** /tʃek/ *v.t.* **1.** pitia kusudi kusahihisha. **2.** zuia; simamisha; pinga; rudi; kemea; karipia. *n.* **1.** masahihisho; ukaguzi. **2.** cheki; hundi; hawala. **3.** kizuizi; uzuiaji. **~mate** *v.t./n.* shinda kabisa au funga bao; mwisho; kipigo cha mwisho.
**cheek** /tʃi:k/ *n.* shavu. **2.** ufedhuli; usafihi; ujuba . *v.t.* sema kwa ujuba.
**cheer** /tʃɪə(r)/ *v.t./i.* furahisha; fariji; changamsha; anisi; -pa moyo; changamka; shangilia; furahia; sifu; tia moyo. ~ *up,* furahi. ~ *sb. up,* furahisha mtu. *n.* furaha; uchangamfu; vifijo. **~ful** *adj.* -a furaha; -changamfu; -kunjufu. **~less** *adj.* bila furaha au faraja; -enye huzuni; -enye kujinamia.
**cheese** /tʃi:z/ *n.* jibini, chizi: aina ya chakula kitengenezwacho kwa maziwa yaliyogandishwa. **~-paring** *n.* bahili.
**chemistry** /'kemɪstri/ *n.* kemia: sayansi ihusuyo uchunguzi wa muundo wa dutu na jinsi dutu hizo na elementi zake vinavyohusiana. **chemical** *adj.* -liotengenezwa kwa au ihusianayo na kemikali. ~ **bond**, muungo wa kikemikali: kani inayoshikamanisha atomu kwenye molekuli. ~ **change**, badiliko kikemikali: badiliko ambalo linahusisha aina na muundo mpya wa atomu au molekuli za dutu. ~ **energy**, nishati kikemikali: nishati iliyo-hifadhiwa ndani ya atomu au molekuli. ~ **equation**, mlinganyo wa kemikali: muhtasari wa fomula na namba ya atomu au molekuli za kemikali zinazotendana na zinazotokana na utendanaji huo. ~ **formula**, alama inayoonyesha idadi na aina ya atomu zinazo-jenga msombo. ~ **reaction**, utendanaji kikemikali: mabadiliko kikemikali yanayotokea wakati vitendanaji vinapoathiriana kuje-nga aina nyingine ya dutu. ~ **symbol**, alama kemikali: herufi ziwakilishazo jina la elementi. **chemical** *n.* kemikali: kitu kinachopatikana katika kemia au kinachotengenezwa kwa njia ya kemia. **chemist** *n.* mtaalamu wa kemia; mtu atengenezaye au auzaye zana za kemia, kemikali, au madawa.
**cheque** /tʃek/ *n.* hawala; cheki; hati ya fedha; hundi.
**cherish** /'tʃerɪʃ/ *v.t.* tunza; linda; tendea wema; chunga; lea.
**chess** /'tʃes/ *n.* mchezo wa chesi.

**chest** /ˈtʃest/ *n.* **1.** kasha; sanduku. *a ~ of drawers*, almari. **2.** kifua; kidari.



chess

**chick** /ʃi:k/ *n.* kifaranga cha kuku au kinda la ndege. **~en** *n.* kifaranga hasa cha kuku; nyama ya kuku. **~pox** *n.* tetekuwanga.

**chief** /tʃi:f/ *n.* mkuu; jumbe; chifu. *adj.* -kuu; -kubwa; bora; -a kwanza. **~ly** *adv.* kwanza; zidi; hasa; aghlabu. **~minister** *n.* waziri kiongozi.

**child** /tʃaɪld/ *n.* (**children** ) mtoto; mwana; kijana. *be with ~,* chukua mimba; -wa mja mzito. **~birth** *n.* uzazi. **~hood** *n.* utoto. *second* **~hood,** ukongwe; uzee. **~ish** *adj.* -a kitoto; -a kipuuzi; -a kijinga. **~like** *adj.* -a kama mtoto; bila hatia wala kosa.

**chill** /tʃɪl/ *n.* **1.** baridi. **2.** homa ya baridi. *v.t.* tia baridi; gandisha kwa barafu. **~y** *adj.* -a baridi. *a ~ breeze,* upepo wa baridi; *(fig.)* bila furaha.

**chime** /tʃaɪm/ *n.* sauti za kengele zikigongwa taratibu; ulinganifu wa sauti. *v.t./i.* gonga kengele taratibu; lingana; patana. *~ in with,* patana; lingana na.

**chimney** /tʃɪmni/ *n.* **1.** dohani; bomba la kutokea moshi **2.** tungi la taa ya kandili au karabai; chemni.

**chimpanzee** /ˌʃɪmpæn'zi:/ *n.* sokwe, aina ya nyani mkubwa.

**chin** /tʃɪn/ *n.* kidevu.

**China** /ˈtʃaɪnə/ *n.* **1.** Uchina. **china** *n.* vyombo vya kaure.

**chip** /ˈtʃɪp/ *n.* kipande kidogo sana; chembe; chenga. *v.t./i.* kata, vunja katika vipande vidogo; katika, vunjika vipande vidogo. *things which ~ easily,* vitu vivunjikavyo kirahisi.

**chisel** /ˈtʃɪz(ə)l/ *n./v.t.* (**-ll-**) patasi; kata kwa patasi. *(fig.)* laghai; ghilibu.

**chlorine** /ˈklɔ:ri:n/ *n.* klorini: aina ya gesi ya kijani kibichi yenye harufu kali sana, hutumika kuulia bakteria na kwa matumizi mengine ya kikemia.

**chlorofluorocarbon** *(cfc)* *n.* gesi yoyote iliyo kampaundi ya kaboni, hidrojeni, klorini, na florini, hutumika katika mafriji na inaaminika kuwa huathiri tabaka ya ozoni katika angahewa.

**chloroform** /ˈklɒrəfɔ:m/ *n.* klorofomu; nusukaputi; aina ya gesi itumikayo kutia usingizi au ganzi.

**chlorophyll** /ˈklɔ:rəfɪl, ˈklɒ-/ *n.* klorofili: kemikali ya rangi ya kijani katika mimea.

**chloroplast** /klɔ:rə(ʊ)plast/ *n.* kloroplasti, kiwiti: kiriba ndani ya seli ya mmea chenye klorofili wakati usanisinuru unapotokea.

**chock** /tʃɒk/ *n.* kipande au kabari la kukazia. *v.t.* kaza kwa kabari. *~-full adj.* -liojaa kabisa; pomoni.

**chocolate** /ˈtʃɒklət/ *n.* chokoleti; chakula kitengenezwacho kwa unga wa kakao. *adj.* chakleti; hudhurungi.

**choice** /tʃɔɪs/ *n.* chaguo; hiari; haki. *A large ~ of books was shown,* vitabu vya aina nyingi vilio-nyeshwa. *adj.* -lioteuliwa; bora; -teule.

**choir** /ˈkwaɪə(r)/ *n.* kwaya; kundi la waimbaji. **chorister** *n.* mwimbaji wa kwaya. **chorus** *n.* waitikiaji.

**choke** /tʃəʊk/ *v.i./t.* kaba; songa roho; zuia pumzi; kabwa; paliwa. *The pipe is ~d up with rubbish,* bomba limezibwa na takataka.

**choose** /tʃu:z/ *v.t./i* (**chose, chosen**) **1.** chagua; teua; pambanua; taka; hiari; kusudia. *Do whatever you ~,* fanya upendavyo. *pick and ~,* chagua kwa uangalifu.

**chop** /tʃɒp/ *v.t./i.* (**-pp-**) kata; chanja; changa; tema; geukageuka. *~ wood; ~ a tree down,* kata mti. *chop and change,* geukageuka; ghairi. *n.* mfupa wa mbavu wenye kipande cha chama. **~per** *n.* shoka. **~py** *adj.* -enye mawimbi.

**chord** /kɔ:d/ *n.* **1.** mtambuko: mstari mnyoofu utokao kwenye nukta moja hadi nukta nyingine, nao huwa ni mfupi kuliko kipenyo cha duara. **2.** sambo: noti kadhaa

za sauti zinazokwenda pamoja. **3.** uzi wa kinanda; utari; uzi.

**christian** /'krɪstɪən, -tʃ(ə)n/ *n. adj.* -a kikristo, -a Kristo; mkristo; mmasihi; mnasara. **~ity** *n.* dini ya Kristo.

**Christmas** /'krɪsməs/ *n.* sikukuu ya kumbukumbu ya kuzaliwa Kristo, tarehe 25 Disemba.

**chromatography** /ˌkrəʊmə'tɒgrəfi/ *n.* kromatografia: utenganishaji wa sehemu za mchanganyiko wa kemikali kwa kupitisha kimumunyishaji kwenye mchanganyiko huo.

**chromium** /'krəʊmiəm/ *n.* kromiamu: elementi nyeupe ya kemikali ngumu, hutumika katika chuma cha pua na hupakazwa kwenye metali nyingine.

**chromosome** /'krəʊməsəʊm/ *n.* kromosomu: nyuzi katika kiini cha seli zenye jeni zinazohusika na urithi wa tabia na maumbile kutoka kwa wazazi.




**chromosome | kromosomu**

**chromosphere** *n.* kromosfia: tabaka la angahewa la jua linalozunguka fotosfia, huweza kuonekana pale jua linapopatwa lote.

**chrysalis** /'krɪs(ə)lɪs/ *n.* buu: gamba linalomfunika funza kabla ya kutoka kwake.

**chuck** /tʃʌk/ *v.t. (colloq.)* tupa. ~ *away rubbish,* tupa taka. ~ *sth. up,* acha. ~ *up one's job,* acha kazi.

**chuckle** /tʃʌkl/ *v.i./n.* jichekea; chekelea; kicheko; mlio wa kuku.

**chunk** /tʃʌŋk/ *n.* kipande kinene cha kitu chochote, e.g. cha mkate au nyuma.

**church** /tʃɜ:tʃ/ *n.* kanisa.

**churn** /tʃɜ:n/ *n.* chombo cha kusukia maziwa; tungu. *v.t./i* suka maziwa ili kupata mtindi na siagi; yagandisha yawe samli.

**chutney** /'tʃʌtni/ *n.* chatne: achari ya embe, pilipili, siki, etc.

**cigar** /sɪ'gɑ:(r)/ *n.* sigara. **~ette** *n.* sigareti; sigara.

**cilium** /'sɪlɪəm/ *n.* (**cilia**) siliamu: uzi kama unywele uotao kwenye baadhi ya seli kwa kazi maalumu.

**cinder** /'sɪndə(r)/ *n.* kaa lenye moto ndani kwa ndani.

**circle** /'sɜ:kl/ *n.* **1.** duara. **2.** jamii ya watu wenye shughuli za aina moja; duru. *v.t./i* zungusha; zunguka.

**circuit** /'sɜ:kɪt/ *n.* **1.** mzunguko. **2.** saketi: muunganisho wowote wa vijenzi mbalimbali vya kupitishia umeme. **~ breaker**, kikata saketi: kifaa ambacho hukata umeme unapozidi kiwango kinachotakiwa. **parallel ~**, saketi sambamba. **series ~**, saketi mfulizo.

**circular** /'sɜ:kjələ(r)/ *adj.* -a duara. *n.* toleo: tangazo, barua, etc. iliyopelekewa watu wengi.

**circulate** /'sɜ:kjəleɪt/ *v.i/t.* zunguka; enea; zungusha; eneza; tangaza; vumisha; sambaa. **circulatory system**, mfumo wa mzunguko wa damu.

**circumcise** /'sə:kəmsʌɪz/ *v.t.* tahiri. **circumcision** *n.* tohara; tia jandoni.

**circumference** /sə'kʌmf(ə)r(ə)ns/ *n.* mzingo; mstari wa kuzunguka umbo la duara.

**circumspect** /'sɜ:kəmspekt/ *adj.* -angalifu; -enye hadhari; -enye busara.

**circumstance** /'sɜ:kəmstəns; -stɑ:ns; -stæns/ *n.* jambo; neno; kadhia; tukio; hali ya mambo. *in/under the ~s,* kwa hali mambo ilivyo. *under no ~s,* haiwezekani kabisa.

**circus** /'sɜ:kəs/ *n.* **1.** kiwanja cha kuchezea sarakasi. **2.** mchezo wa sarakasi.

**cistern** /'sɪstən/ *n.* tangi; hodhi.

**citadel** /'sɪtəd(ə)l, -dɛl/ *n.* ngome (ndani ya mji).

**cite** /sʌɪt/ *v.t.* nena; taja; nukuu; ita mahakamani.
**citation** /sʌɪ'teɪʃ(ə)n/ *n.* notisi; dondoo.
**citizen** /'sɪtɪzn/ *n.* raia; mwananchi. **~ship** *n.* uraia.
**citric acid** /ˌsɪtrɪk 'æsɪd/ *n.* asidi sitriki: asidi itokanayo na matunda ya jamii ya machungwa.
**citron** /'sɪtr(ə)n/ *n.* mbalungi; balungi. **citrus** *adj.* -a mti wa jamii ya miti ya michungwa.
**city** /'sɪti/ *n.* mji mkubwa; jiji.
**civet** /'sɪvɪt/ *n.* ngawa; ~ *cat*, fungo.
**civic** /'sɪvɪk/ *adj.* -a kuhusu nchi na watu wake. **~s** *n.* elimu ya uraia: haki na wajibu wa raia wa nchi.
**civil** /'sɪvl/ *adj.* **1.** -a jamii. ~ *law*, sheria za nchi. ~ *war*, vita vya wenyewe kwa wenyewe. **2.** -a serikali. ~ *servant*, mtumishi wa serikali. **3.** -enye adabu; - enye heshima; -a kiungwana. **~ity** *n.* uungwana; adabu; heshima. **~ly** *adv.* kwa adabu; kwa hesima. **~ian** *n.* raia; mwananchi. **civilize** *v.t.* staarabisha.
**civilization** /ˌsɪvəlaɪ'zeɪʃn/ *n.* ustaarabu.
**claim** /kleɪm/ *v.t.* dai; jidai. *n.* haki; haja; madai; daawa. **~ant** *n.* mdai.
**clamber** /'klæmbə(r)/ *v.i.* panda kwa shida; paramia. e.g. ~ *over a wall.*
**clamour** /'klæmə(r)/ *n.* makelele; ghasia; hoihoi; vifijo. *v.t.* piga makelele.
**clan** /klæn/ *n.* kabila; ukoo. **~ship** *n.* udugu; ukoo. **~sman** *n.* ndugu wa kiume katika kabila.
**clap** /klæp/ *v.t./i.* (**-pp-**) piga makofi; shangilia. ~ *sb. in prison*, tupa mtu gerezani ghafla. **~-trap** *n.* maneno matupu; domo kaya.
**clarify** /'klarɪfʌɪ/ *v.t./i.* dhihirisha; safisha; dhihirika; bainisha; fafanua; hakikisha. **clarification** *n.* ufafanuzi.
**clarity** /'klærəti/ *n.* udhahiri; uwazi.
**clash** /klæʃ/ *v.i./t./n.* gongana; pambana; kinzana; kaidiana; tofautiana. *n.* mshindo mkubwa; mabishano.
**clasp** /klɑ:sp/ *n.* kifungo; bizimu; ufumbataji; ukumbatiaji. *v.t./i.* funga; kumbatia; kamata; fumbata. **~ knife** *n.* kisu cha kukunja.
**class** /klɑ:s/ *n.* aina; darasa; cheo; daraja; jinsi. *v.t.* ainisha; weka katika makundi. **~ic** adj. bora; -zuri. *n.* mwandishi, mchora picha, kitabu, kazi ya sanaa, etc. bora kabisa hasa -a zamani. **~ical** *adj.* bora na -a zamani. **~ify** *v.t.* ainisha.
**clause** /klɔ:z/ *n.* **1.** kishazi: tungo ndogo yenye uoanifu ndani yake iwezayo kusimama peke yake au kuwa sehemu ya sentensi. **2.** kifungu, aya, ibara, katika sheria.
**claw** /klɔ:/ *n.* ukucha; gando. *v.t.* piga makucha; papura.
**clay** /kleɪ/ *n.* udongo; tope. ~*cold*, baridi sana.
**clean** /kli:n/ *adj.* safi; -eupe; bila hatia; tohara. *show a ~ pair of heels*, toroka; kimbia. *v.t./i.* safisha; wa safi; toharisha; takasa. *adv.* kabisa; pia. *We ~ forgot you were coming*, tulisahau kabisa kuwa utakuja. **~liness** *n.* usafi; unadhifu. **~se** *v.t.* safisha sana.
**clear** /klɪə(r)/ *adj.* -eupe; dhahiri; bayana; wazi; safi. ~ *gain*, faida safi. ~ *head*, akili timamu. *v.t./i.* safisha; takasa; fyeka; takata. *The sky is ~ing*, mawingu yanatakata. ~ *up*, panga vitu vizuri. ~ *out*, toka; kimbia. **~ance** *n.* ruhusa; usafishaji; nafasi baina ya vitu viwili. **~ing** *n.* mahali peupe, palipofyekwa.
**cleave** /kli:v/ *v.t./i.* (**cleft**, **clove**, **cloven**) katika; pasuka; pasua; choma. *cloven hoof*, kwato ya ng'ombe, ya shetani. **cleavage** *n.* mpasuko.
**clench** /klentʃ/ *v.t./i.* kaza sana meno, vidole au ngumi.
**clergy** /'klə:dʒi/ *n.* kiongozi katika kanisa la kikristo. **~man** *n.* mmoja wa viongozi wa chini ya cheo cha askofu.
**clerk** /klɑ:k/ *n.* karani. **clerical** *adj.* -a karani; -a kuhusu dini.
**clever** /'klevə(r)/ *adj.* -enye akili;

hodari; -juzi; stadi; bingwa; mahiri. **~ness** *n.* ujuzi; ustadi.
**click** /klɪk/ *v.i./n.* mwaliko; sauti ya kualika kama vile kidoko, mtambo wa bunduki, etc.; alika; piga kidoko.
**client** /'klaɪənt/ *n.* mteja. **~ele** *n.* wanunuzi; wateja.
**cliff** /klɪf/ *n.* jabali; genge.
**climate** /'klaɪmət/ *n.* hali ya hewa ya sehemu.
**climax** /'klaɪmət/ *n.* mwisho; kikomo; kipeo. **~ community**, jamii upeo: jamii ya mimea iliyotengemaa katika mazingira fulani na kuendelea kuishi bila ya mabadiliko yoyote ya kimsingi.
**climb** /klaɪm/ *v.t./i.* panda; kwea. *~ing plant*, mmelea; kirukia.
**clinch** /klɪntʃ/ *v.t./i* kaza sana meno, vidole au ngumi; kwaana. *~ an argument*, toa ithibati ya maneno.
**cling** /klɪŋ/ *v.i.* (**clung**) shika; nata; ambatana; shikamana.
**clinic** /'klɪnɪk/ *n.* hospitali; zahanati; kituo cha afya. **~al** *adj.* -a hospitali. **~ thermometer**, kipimajoto: kifaa kituwamicho na daktari kupimia halijoto ya mtu.
**clip**[1] /klɪp/ *n.* klipu; kibanio; kishikizo. *v.t.* (**-pp-**) shikiza; bana kwa klipu.




**clinic thermometer | kipimajoto**

**clip**[2] /klɪp/ *v.t.* (**-pp-**) kata kwa mkasi; fupisha; punguza.
**clitoris** /'klɪt(ə)rɪs/ *n.* kisimi; kinembe.
**cloak** /kləʊk/ *n.* vazi kama joho; **(fig.)** chochote kifichacho au kufunika. *v.t.* **(fig).** ficha; sitiri.
**clock** /klɒk/ *n.* saa. *go like ~work*, endelea vyema.
**clog**[1] /klɒg/ *n.* kiatu cha mti; matarawanda.
**clog**[2] /klɒg/ *v.t./i.* (**-gg-**) ganda; zuia; zibika; zuilika.
**clone** /kləʊn/ *v.t.* *n* **1.** toa kopi iliyofanana. *n.* mnyama au mmea ambao kijenetiki hufanana na mzazi wake kwa hali zote. **2.** Kiumbe kilichozalishwa kutoka kwa mzazi mmoja katika maabara bila tendo la kujamiiana.
**close** /kləʊz/ *v.t./i.* funga; ziba; fungika; fumbika. *~ up*, sogea; sogeza. *~ in (upon)*, zunguka; zingia. *~ with an offer*, patana. *n.* kikomo; mwisho; uwanja. *adj.* -finyu; -liyofungwa; -embamba; bahili; karibu; -a siri. *a ~ friend*, msiri; rafiki wa ndani.
**clot** /klɒt/ *n.* kidonge. *The blood is ~ted*, damu imeganda.
**cloth** /klɒθ/ *n.* kitambaa.
**clothe** /kləʊð/ *v.t.* (**clothed**) vika; visha. **~s** *n.* nguo.
**clothing** /'kləʊðɪŋ/ *n.* nguo.
**cloud** /klaʊd/ *n.* **1.** wingu; ghubari. **2.** kundi kubwa. **3. (fig.)** hali ya taabu, hofu au huzuni. *be under a ~ of suspicion*, -wa umeshukiwa, au umetuhumiwa.
**clove** /kləʊv/ *n.* karafuu. *~ tree*, mkarafuu.
**cloze test** *n.* utaratibu wa makusudi wa kuacha maneno katika makala kwa ajili ya zoezi la ufahamu.
**club** /klʌb/ *n.* **1.** chama; klabu. **2.** rungu; gongo. *v.t.* piga kwa rungu.
**cluck** /klʌk/. *v.i./n.* lia kama kuku anayewaita vifaranga vyake; mlio kama wa kuku anayewaita vifaranga.
**clue** /klu:/ *n.* alama; dalili; kidokezo.
**clump** /klʌmp/ *n.* **1.** kichaka. **2.** bonge. **3.** fungu.
**clumsy** /'klʌmzi/ *adj.* -zito; zembe; -enye umbo si zuri.
**cluster** /'klʌstə(r)/ *n.* tawi; shada; kundi; chana. *v.i.* kusanyika; jumuika.
**clutch**[1] /klʌtʃ/ *v.t./i.* shikilia; fumbata; shikilia au kamata imara. *in the ~ es of*, chini ya amri kali ya. *n.* mtambo (wa motakaa au mashine) uunganishao na kutenga mashine na mtambo uzungushao magurudumu.
**clutch**[2] /klʌtʃ/ *n.* jumla ya mayai

yaliyoatamiwa na kuku katika fuko moja; vifaranga vilivyo-anguliwa katika fuko moja.

**clutter** /'klʌtə(r)/ *v.t.* chafua; fuja; paraganya. *n.* machafuko; fujo.

**co-** /kəʊ/ *prefix* kiambishi awali kifahamishacho ushiriki. *co-author*, mwandishi mwenza. *co-education*, elimu ya wanaume na wanawake pamoja.

**coach** /kəʊtʃ/ *n.* **1.** gari; behewa. **2.** kocha. **3.** mwalimu. *v.t./i.* fundisha; elekeza; safiri katika gari. **~man** *n.* mwendeshaji wa gari.

**coal** /kəʊl/ *n.* makaa ya mawe. **~-gas** *n.* gesi ya makaa, hutumika kama nishati. **~mine** *n.* mgodi wa makaa ya mawe; machimbo ya makaa. **~-tar** *n.* lami ya makaa ya mawe.

**coalesce** /ˌkəʊə'lɛs/ *v.i.* ungana; fungamana; shirikiana. **~nce** *n.* muungano.

**coalition** /ˌkəʊə'lɪʃn/ *n.* muungano; shirikisho, mapatano.

**coarse** /kɔ:s/ *adj.* -a kukwaruza; siyo laini; duni; hafifu. ~ *language*, maneno yasiyo heshima; matusi.

**coast** /kəʊst/ *n.* pwani; mwambao; ufukwe; ufuko. *v.i./t.* **1.** pita, ambaa pwani kwa pwani. **2.** teremka mlima kama kwa baiskeli bila ya kutumia nguvu.

**coat** /kəʊt/ *n.* **1.** koti; ngozi ya mnyama au manyoya. **2.** mpako wa rangi. *v.t.* paka.

**coax** /kəʊks/ *v.t./i.* bembeleza; rairai; shawishi; rubuni. **~ing** *n.* ushawishi.

**cobalt** /'kəʊbɔ:lt, -ɒlt/ *n.* metali ngumu ing'aayo kama fedha, hutumika katika aloi mbalimbali.

**cobra** /'kəʊbrə, 'kɒbrə/ *n.* kobra: aina ya nyoka.

**cobweb** /'kɒbweb/ *n.* utando wa buibui.

**coccyx** /'kɒksɪks/ *n.* kifandugu; kinyunguu: mfupa wa tindi ya mwisho ya uti wa mgongo.

**cochlea** /'kɒklɪə/ *n.* komboli; koa: muundo mzongomano ndani ya sikio ambao umeungana na neva sikizi.

**cock**[1] /kɒk/ *n* jogoo; ndege dume. **~ade** *n.* kishada cha kofia. **~-crow** *n.* alfajiri; jogoo la kwanza. **~- sure** *adj.* hakika kabisa.

**cock**[2] /kɒk/ *n.* **1.** koki; bilula; bulula. **2.** mtambo wa bunduki. *v.t.* jaza mtambo wa bunduki.

**cockroach** /'kɒkrəʊtʃ/ *n.* mende.

**cocoa** /'kəʊkəʊ/ *n.* unga wa kakao; kinywaji kitengenezwacho kwa unga huo.

**coconut** /'kəʊkənʌt/ *n.* nazi. ~ *tree*, mnazi. *green* ~, dafu.

**cocoon** /ke'ku:n/ *n.* kokuni: nyumba ya mdudu ambayo huitengeneza kwa kujiunganishia nyuzinyuzi.

**code** /kəʊd/ *n.* kanuni; sheria; taratibu; kawaida.

**coefficient** /ˌkəʊɪ'fɪʃ(ə)nt/ *n.* kizigeu: uwiano kati ya vipimo viwili hasa katika aljebra.

**coelenterate** /si:'lɛnt(ə)rət, -reɪt/ *n.* kolentrate: jamii ya wanyama wa baharini wasio na uti wa mgongo kama jeli yavuyavu etc.

**coerce** /kəʊ'ɜ:s/ *v.t.* shurutisha; lazimisha; zuia; teza nguvu. **coercion** *n.* lazima; nguvu; utezaji nguvu. **coercive** *adj.* -enye nguvu.

**coffee** /'kɒfi/ *n.* buni; kahawa. ~ *plant*, mbuni.

**coffin** /'kɒfɪn/ *n.* jeneza.

**cog** /kɒg/ *n.* jino la gurudumu. **~-wheel** *n.* gurudumu lenye meno.

**cogent** /'kəʊdʒ(ə)nt/ *adj.* -a nguvu; -a maana; -a lazima kwa hoja.

**cogitate** /'kɒdʒɪteɪt/ *v.i./t.* waza; fikiri sana; kumbuka.

**cohere** /kə(ʊ)'hɪə/ *v.i.* ambatana; shikamana; fungamana. **~nce**, **~ncy** *n.* mshikamano; fungamano; mwambatano. **~nt** *adj.* (hasa kwa usemi, fikira, mawazo) dhahiri; -epesi kufahamika. **cohesion** *n.* uambatanaji; mshikamano. **cohesive** *adj.* -a kushikamana.

**coil** /kɔɪl/ *v.t./i.* kunja; zunguka; zonga; zungusha; zongomana. *n.* pindi; koili: sukepindi la nyaya.

**coin** /kɔɪn/ *n.* sarafu; fedha; pesa. *v.t.* buni; tunga; zua. *to pay a man in his own ~s*, lipizia mtu kama

alivyokutendea.

**coincide** /ˌkəʊɪn'saɪd/ *v.i.* lingana; patana; -wa sawa; tokea wakati mmoja. **~nce** *n.* ulinganifu; utokeaji wa mambo sawia na kwa bahati tu.


coils

**coke** /kəʊk/ *n.* makaazimwe: aina ya kaboni inayofanywa kutokana na makaa ya mawe yasiyo na gesi.

**cold** /kəʊld/ *adj.* -baridi. *in ~ blood,* bila huruma. *throw ~ water on,* vunja moyo. *give the ~ shoulder to,* -pa kisogo; puuza. *n.* baridi; makamasi; mafua. **~-blooded** *adj.* -enye damu baridi; katili. **~ chisel** *n.* tindo. **~-hearted** *adj.* bila huruma.

**collaborate** /kə'labəreɪt/ *v.i.* shiriki katika kazi; saidia. **collaborator** *n.* mshiriki; msaidizi.

**collapse** /kə'læps/ *v.i.* anguka; vunjika; zimia; zirai; poromoka; kata tamaa; vunjika moyo. *n.* uangukaji; uporomokaji; hali ya kuzimia au ya kukata tamaa.

**collapsible**, /kə'læpsəbl/ *adj.* -a kuweza kukunjwa.

**collar** /'kɒlə(r)/ *n.* ukosi; ukanda uzungukao shingo ya mnyama. *v.t.* kamata kwa ukosi. **~-bone** *n.* mtulinga.

**colleague** /'kɒli:g/ *n.* mwenza; mshiriki; rafiki.

**collect** /kə'lɛkt/ *v.t./i.* kusanya; kusanyika; changa; kutanika. **~ed** *adj.* -tulivu; liokusanyika au -liokusanywa. **~ion** *n.* ukusanyaji; mchango; sadaka. **~ive** *adj.* -a jumla; -a pamoja.

**college** /'kɒlɪdʒ/ *n.* chuo cha elimu ya juu; jamii ya walimu na wanafunzi wa chuo; taasisi; jumuia ya wataalamu. *the ~ of surgeons,* jumuia ya waganga wapasuaji.

**collegiate** /kə'li:dʒiət/ *adj.* -a kuhusu chuo.

**collide** /kə'laɪd/ *v.i.* gongana. **collision** *n.* mgongano.

**colloid** /'kɒlɔɪd/ *n.* vunju; koloidi: chembe za kemikali za aina moja ambazo zimesambaa katika dutu kemikali nyingine kwa njia ya hewa au uoevu.

**colloquial** /kə'ləʊkwɪəl/ *adj.* -a usemi tu; simo.

**collusion** /kə'lu:ʒn/ *n.* mapatano ya hila; udanganyifu; hila.

**colon**[1] /'kəʊlən/ *n.* alama hii ( : ).

**colon**[2] /'kəʊlən, -lɒn/ *n.* utumbo mpana: sehemu ya chini ya utumbo mkubwa.

**colonel** /kə:n(ə)l/ *n.* kanali: mkubwa wa rejimenti ya askari.

**colony** /'kɒləni/ *n.* koloni: nchi iliyotawaliwa na wageni; kundi; jumuia. *The African ~ in Paris,* jumuia ya Waafrika waishio mji wa Paris. *a ~ of artists,* kundi la wasanii.

**colonial** /kə'ləʊniəl/ *adj.* -a wakoloni; a ukoloni; -a koloni.

**colonialism** /kə'ləʊniəlɪzəm/ *n.* ukoloni. **neo-colonialism** *n.* ukoloni mamboleo. **colonize** *v.t.* tawala nchi si yako. **colonization** *n.* kutawala nchi nyingine.

**colossal** /kə'lɒsl/ *adj.* -kubwa mno; zidi ukubwa.

**colour** /'kʌlə(r)/ *n* rangi. *give (lend) ~ to,* fanya jambo kama litakiwavyo. **(fig.)** *He is off ~,* anaumwa. *stick one's ~,* kataa kabisa kuacha imani yako. *come off with flying ~s,* fanikiwa vizuri sana. **~-blind** *n.* upofu wa kupambanua rangi. **~less** *adj.* -sio na rangi. **(fig.)** *a ~ person,* mtu dufu.

**colt** /kəʊlt/ *n.* farasi, aghlabu chini ya miaka minne asiyehasiwa; kijana mdogo asiye na uzoefu.

**column** /'kɒləm/ *n.* nguzo; mhimili; mnara; safu.

**coma** /'kəʊmə/ *n.* usingizi mzito sana; kuzirai. **~tose** *adj.* - enye kuzimia; -enye kusinziasinzia kwa kutumia dawa.

**combat** /'kɒmbæt/ *n./v.t./i.* vita; pambano; shindano; shindana; pambana. **~ant** *adj. /n.* mpiganaji; mshindani.

**combine** /kəm'bʌɪn/ *v.t./i.* unganisha; unga; ungana; changanya; shirikiana. *n.* shirika la

wafanya biashara. **combination** *n.* uunganishaji; muungano; mchanganyiko; uchanganyaji; watu wanaoshirikiana katika shughuli moja.

**combustible** /kəm'bʌstəbl/ *adj.* -a kuweza kuwaka upesi.

**combustion** /kəm'bʌstʃən/ *n.* mwako; hali ya kuwaka.

**come** /kʌm/ *v.i.* (**came** /keɪm/ **come**) -ja; wasili; fika. ~ *by (sth.),* pata kitu kwa bahati. ~ *to,* ~ *round one's senses,* pata fahamu baada ya kuzimia. ~ *into (a fortune),* rithi mali nyingi. ~ *out,* chapishwa; julikana. *His book has ~ out,* kitabu chake kimechapishwa. *The hole affair has ~ out,* kadhia yote imejulikana. ~ *off,* tokea kama ulivyotarajia. ~ *of age,* baleghe. ~ *to blows,* anza kupigana. ~ *about,* tokea. ~ *across,* ~ *upon,* kuta, ona kwa bahati. ~ *true,* -wa kweli. ~ *of,* tokea. *What came of the conversation?* mazungumzo yalikwendaje? ~ *to,* kuweza. *How did you ~ to hear of this affair?* uliijuaje habari ya jambo hili? *in years to ~,* katika miaka ijayo. *a coming man,* mtu afikiriwaye kuwa maarufu baadaye. **~back** *n.* kupata tena hali ya zamani. **~down** *n.* kutofaulu katika mambo; kuanguka.

**comedy** /'kɒmədi/ *n.* kichekesho: mchezo wa kuigiza wa kuchekesha. **comedian** *n.* mtu aigizaye vichekesho.

**comet** /'kɒmɪt/ *n.* nyotamkia; kimondo.

**comfort** /'kʌmfət/ *n.* faraja; kitulizo; liwazo; raha; starehe; fanaka. *v.t.* fariji; tuliza; liwaza; burudisha. **~able** *adj.* -a kufariji; -enye raha; -enye faraja; -a kuburudisha; -a kupendeza; -a kuliwaza. **~less** *adj.*-a bila raha; -a bila faraja; -a bila starehe.

**comic** /'kɒmɪk/ *adj* -a mzaha; cheshi; -chekeshaji.

**comma** /'kɒmə/ *n.* koma: alama hii ( , ).

**command** /kə'mɑ:nd/ *v.t./i.* amrisha; tawala: ~ *respect and sympathy,* stahili heshima na huruma. *The fort on the hill ~s the plain,* ngome iliyo kilimani inaangalia kwenye bonde. *n.* amri; uwezo; utawala; sehemu ya jeshi iliyo chini ya amri ya fulani. **~ant** *n.* kamanda. **~eer** *v.t.* twaa kwa matumizi ya vita au ya majeshi ya askari. **~er** *n.* kamanda wa askari au wa manowari. **~ment** *n.* amri; sheria; agizo. **~o** *n.* komando: askari stadi wa kikosi maalumu katika mapambano.

**commemorate** /kə'meməreɪt/ *v.t.* adhimisha kumbukumbu ya tukio fulani kwa hotuba au maandishi.

**commence** /kə'mens/ *v.t./i.* anzisha; anza. **~ment** *n.* mwanzo; chanzo; chimbuko.

**commend** /kə'mend/ *v.t.* sifu; tukuza; pongeza. **~able** *adj.* -a kustahili sifa, pongezi, tunzo. **~ation** *n.* sifa.

**commensurate** /kə'mɛnʃ(ə)rət, sjə-/ *adj.* -a kipimo au kadiri iliyo sawa na; -a kulingana na; -a kufaa.

**comment** /'kɒment/ *n.* ufafanuzi; tamko. *v.t.* eleza; fafanua; toa maoni. **~ary** *n.* ufafanuzi; maelezo. *broadcast ~ on a football match,* tangaza mpira wa miguu redioni. **~ator** *n.* mtangazaji wa matukio hai katika redio au televisheni.

**commerce** /'kɒmɜ:s/ *n.* biashara; uchumi. **commercial** *adj.* -a kuhusu biashara. **commiserate** *v.t./i.* sikitikia; hurumia; hani; -pa mtu pole.

**commissar** /ˌkɒmɪ'sɑ:/ *n.* kamisaa; mwanasiasa katika taasisi ya kazi.

**commissariat** /ˌkɒmɪ'sɛ:rɪət/ *n.* kitengo kitoacho chakula na zana za kivita jeshini.

**commission** /kə'mɪʃn/ *n.* **1.** agizo; amri; cheo cha afisa. **2.** utendaji. **3.** faida; ushuru; malipo. **4.** hati au cheti cha kumpa mtu nguvu, cheo au amri fulani. **5.** tume. *be in ~,* (kwa meli) tayari kusafiri baharini. **~er** *n.* kamishna; wakili; mjumbe; mwagizaji. *district ~,* mkuu wa wilaya. *regional ~,* mkuu wa mkoa.

~ *of police*, kamishna wa polisi.

**commit** /kə'mɪt/ *v.t.* (**-tt-**) **1.** tenda; fanya. **2.** aminisha; ahidi; funga; ingiza. **~ment** *n.* sharti; ahadi. ~ *to memory*, hifadhi akilini. ~ *suicide*, jiua. ~ *murder*, ua mtu.

**committee** /kə'mɪti/ *n.* kamati; halmashauri.

**commodity** /kə'mɒdɪti/ *n.* kifaa; bidhaa; mali; kitu.

**common** /'kɒmən/ *adj.* -a siku zote; -a kawaida; -a watu wote. *a ~ language*, lugha ya pamoja. *~ knowledge*, ifahamikayo na wengi. *House of Commons*, Halmashauri ya Bunge la Uingereza. *in ~*, -a watu wote. *out of the ~*, -si -a kawaida. **~ly** *adv.* kwa kawaida; kwa desturi; aghlabu; mara nyingi. **~er** *n.* mtu wa kawaida. **~place** *n./adj.* -a kawaida. **~wealth** *n.* milki au utawala wa pamoja.

**Commonwealth** /'kɒmənwelθ/ *n.* Jumuia ya Madola.

**commotion** /kə'məʊʃn/ *n.* udhia; kishindo; ghasia; fitina; makelele; rabsha.

**communal** /'kɒmjʊn(ə)l, kə'mju:-/ *adj.* -a watu wa mtaa au mji mmoja.

**commune** /'kɒmju:n/ *v.i.* ongea; zungumza; shauriana.

**communicate** /kə'mju:nɪkeɪt/ *v.i./t.* wasiliana; pasha; toa; arifu; eleza; julisha; pokea ushirika mtakatifu. **communicable** *adj.* -a kuweza kuwasilishwa. **communication** *n.* mawasiliano. *communication satellite*, setilaiti ya mawasiliano. **communicative** *adj.* -enye tabia ya kuzungumza.

**communion** /kə'mju:niən/ *n.* ushirika; mazungumzo; maongezi; urafiki.

**communique** /kə'mju:nɪkeɪ/ *n.* habari au tangazo lililotolewa na taasisi fulani; ripoti; tamko.

**communism** /'kɒmjunɪzəm/ *n.* mfumo wa jamii uliobuniwa na Marx uliokusudia kupiga vita matabaka na uliotaka rasilimali ya taifa umilikiwe na wananchi wote, pia mtu hulipwa na kuchangia kulingana na uwezo wake katika jamii. **communist** *n.* mkomunisti: muumini wa mfumo huo wa jamii.

**community** /kə'mju:nəti/ *n.* jamii; watu waishio mahali pamoja.

**commutative** /kə'mju:tətɪv, 'kɒmjʊ, tətɪv/ *adj.* (katika hesabu) -enye kutoa jawabu lilelile japo mpangilio wa tarakimu ni tofauti. e.g. 7x5 5x7

**commutator** /'kɒmjʊˌtəɪtə/ *n.* kibadilishi; komuteta: chombo kinachotumiwa kubadili umeme.

**commute** /kə'mju:t/ *v.t.* **1.** badilisha; punguza adhabu. **2.** enda na kurudi kazini kila siku kwa usafiri fulani.

**compact** /kəm'pækt/ *n./adj./v.t.* imara; thabiti; -a karibukaribu; gandamiza; maafikiano; mapatano. **~ disc**, diski songani: diski ambayo taarifa dijitali huhifadhiwa kwenye tabaka ya mtali nururishi.

**companion** /kəm'pæniən/ *n.* mwenza; rafiki; mwandani.

**company** /'kʌmpəni/ *n.* **1.** rafiki; mwenza; wageni waalikwa; watu waliopo. **2.** shirika; kampuni. **3.** jumla ya watu wafanyao kazi pamoja. **4.** sehemu ya jeshi.

**comparable** /'kɒmp(ə)rəb(ə)l/ *adj.* -a kuweza kulinganishwa na.

**comparative** /kəm'parətɪv/ *adj.* **1.** linganifu. **2.** -sio sawasawa kabisa ila ni karibu sawasawa. **3.** -a kupimika kwa kulinganisha na kingine.

**compare** /kəm'peə(r)/ *v.t.* linganisha; fananisha; mithilisha. *Yours is not to be ~d to mine*, yako hailingani na yangu.

**comparison** /kəm'pærisn/ *n.* ulinganifu; ulinganishaji.

**compartment** /kəm'pa:tmənt/ *n.* chumba; behewa.

**compass** /'kʌmpəs/ *n.* dira; eneo; duara; upeo; kikomo; mpaka; mzingo.



compass

**compassion** /kəm'pæʃn/ *n.* huruma. **~ate** *adj.* -enye huruma; -pole.

**compatible** /kəm'pætəbl/ *adj.* -a kupatana; -a kuelekeana; -a kutangamana; -a kuchukuana. **compatibility** *n.* upatanifu; ulinganifu; uchukuanaji.

**compatriot** /kəm'patrɪət, -'peɪt-/ *n.* mtu wa nchi moja na mwingine.

**compel** /kəm'pel/ *v.t.* (**-ll-**) shurutisha; lazimisha; teza nguvu.

**compensate** /'kɒmpenseɪt/ *v.t./i.* lipa; fidia. **compensation** *n.* ridhaa; fidia; malipo.

**compete** /kəm'pi:t/ *v.i.* shindana. **competition** *n.* ushindani; shindano; mashindano.

**competent** /'kɒmpɪtənt/ *adj.* -enye nguvu, akili, uwezo etc. wa kutenda jambo. **competence** *n.* uwezo; nguvu; ustadi; akili. **competitive** *adj* -a kushindaniwa; a ushindani; -a shindano.

**competitor** /kəm'petɪtə(r)/ *n.* mshindani.

**compile** /kəm'paɪl/ *v.t.* kusanya. **compilation** *n.* ukusanyaji .

**complacent** /kəm'pleɪs(ə)nt/ *adj.* -kinaifu; -a kuridhika; -a kutoshelezeka. **complacency** *n.* utulivu; kinaya.

**complain** /kəm'pleɪn/ *v.i.* nung'gunika; lalamika; shtaki. **~ant** *n.* mshitaki; mlalamikaji. **~t** *n.* lalamiko; nung'uniko; shtaka.

**complaisant** /kəm'pleɪz(ə)nt/ *adj.* -enye kutaka kupendeza wengine; -pole. **complaisance** *n.* ridhaa; adabu; upole.

**complement** /'kɒmplɪm(ə)nt/ *n.* kitimizo; kijalizo; bakaa. *v.t.* kamilisha; jaliza; timiza. **~ary** adj. timizaji; kamilishaji: **~ angles**, pembe kamilishi. **~ colours**, rangi kamilishi: rangi mbili ambazo zikichanganywa hutoa rangi mng'aro nyeupe, mfano buluu na manjano.

**complete** /kəm'pli:t/ *adj.* kamili; -zima; timilifu; kabisa. *a ~ stranger*, mgeni kabisa. *v.t.* timiza; kamilisha; maliza; hitimisha. **~ly** *adv.* kabisa; halisi. **completion** *n.* umalizaji; mwisho; tamati.

**complex** /'kɒmpleks/ *adj.* -gumu kufahamika; changamano; -a fumbo; -enye kinyongo. *n.* kinyongo. **~ity** *n.* uchangamano; matatizo; kinyongo.

**compliance** /kəm'plʌɪəns/ *n.* kibali; ridhaa. *in ~ with*, kulingana na. **compliant** *adj.* -tii; -sikivu; -pole; maridhia.

**complicate** /'kɒmplɪkeɪt/ *v.t.* tatiza; tatanisha; zonga. **~d** *adj.*-enye mazonge; -enye kutatiza. **complication** *n.* mafumbo; ugumu; matata.

**compliment** /'kɒmplɪm(ə)nt/ *n.* sifa; salamu; shukrani. *v.t.* salimu; sifu; shukuru. **~ary** *adj.* -a kusifu; -a kusalimu; -a kuheshimu. *~ ticket*, tiketi iliyotolewa bure.

**comply** /kəm'plʌɪ/ *v.i.* kubali; tii; fanya; timiza; fuata.

**component** /kəm'pəʊnənt/ *adj.* liyomo; -liyo sehemu ya. *n.* kitu kilichomo; sehemu.

**compose** /kəm'pəʊz/ *v.t./i.* tunga; buni; andika; tuliza; panga herufi za chapa. *~ oneself*, jituliza. **~d** *adj.* tulivu; makini; -taratibu. **~r** *n.* mtungaji wa muziki.

**compositor** /kəm'pɒzɪtə/ *n.* mpangaji herufi za chapa.

**composite** /'kɒmpəzɪt/ *adj.* liofanywa na sehemu nyingine au na vitu mbalimbali.

**composition** /ˌkɒmpə'zɪʃn/ *n.* insha; utungaji; utunzi; mpango; mchanganyiko.

**compost** /'kɒmpɒst/ *n.* mbolea; mboleavunde; mboji.

**composure** /kəm'pəʊʒə(r)/ *n.* utulivu; makini.

**compound** /'kɒmpaʊnd/ *n./adj.* **1.** msombo: kitu kilichoundwa kwa elementi zaidi ya moja; **2.** uwa.**3.** kiwanja cha nyumba; kambi ya wafanyakazi; enye sehemu zaidi ya moja. **~ bar**, pau metalimbili: ufito wenye metali mbili zilizogandamizwa pamoja. **~ eye**, jichomzolenzi: jicho lenye lenzi zaidi ya moja hasa katika wadudu na kurustasia.

**comprehend** /ˌkɒmprɪ'hɛnd/ *v.t.* fahamu; tambua; elewa; -wa na;

weka. **comprehensible** *adj.* -a kufahamika; -a kueleweka. **comprehension** *n.* ufahamu; ujuzi. **comprehensive** *adj.* enye uwezo wa kufahamu mengi; enye vitu vingi.

**compress** /kəm'prɛs/ *v.t.* bana; shindilia; gandamiza; sindika; kaza; kamua; fupisha. **~or** *n.* kishindilio; kompresa: mtambo unaobana gesi au hewa.

**comprise** /kəm'praɪz/ *v.t.* -wa na. e.g. *The book ~s all sorts of knowledge,* kitabu kina maarifa ya namna nyingi. **comprising** *adj.* -enye.

**compromise** /'kɒmprəmaɪz/ *n.* mapatano; maridhiano; maafikiano; makubaliano. *v.t./i.* patana; ridhiana; kubaliana; afikiana; sikilizana; hatarisha.

**compulsion** /kəm'pʌlʃn/ *n.* shurutisho; nguvu; lazima. **compulsory** *adj.* -a lazima.

**compunction** /kəm'pʌlsəri/ *n.* majuto; toba; masikitiko; uchungu.

**compute** /kəm'pju:t/ *v.t.* kokotoa; hesabu; kadiria. **computation** *n.* hesabu; ukadiriaji. **~er** *n.* tarakilishi; kompyuta: mashine ya elektroniki yenye uwezo wa kupokea, kuhifadhi na kuchambua data zilizoingizwa kwa programu maalumu au kuongoza mitambo kiutomatiki.




computer (kompyuta)

**computerize** /kəm'pju:təraɪz/ *v.t.* hifadhi au chambua data za kompyuta; fanya mitambo iongozwe kwa kompyuta.

**comrade** /'kɒmreɪd/ *n* rafiki mwenza.

**concave** /'kɒnkeɪv/ *adj.* -a mvungu, enye shimo, -a kubonyea **~ lens** lenzi mbonyeo: lenzi ambayo upande mmoja au pande zote mbili zimebonyea. **~ mirror**, kioo mbonyeo: kioo ambacho uso unaoakisi nuru umebonyea.



concave

**conceal** /kən'si:l/ *v.t.* ficha; sitiri. **~ment** *n.* maficho; sitara; ufichaji.

**concede** /kən'si:d/ *v.t.* kubali; kiri; acha; achilia; toa ruhusa. **concession** *n.* kukubali; ruhusa; ridhaa; fadhila; mkataba.

**conceit** /kən'si:t/ *n.* majivuno; kiburi. **~ed** *adj.* -enye kiburi; -enye majivuno; -enye kudeka.

**conceive** /kən'si:v/ *v.t./i.* chukua mimba; waza; dhani; ona; fahamu. **conceivable** *adj* -a kuwazika; -a kuonekana; -a kufahamika.

**concentrate** /'kɒnsntreɪt/ *v.t./i.* kusanya; kusanyika; ongeza nguvu. *~ on,* fikiri sana juu ya. **~d** *adj.* kolevu; -enye nguvu nyingi. **concentrated solution**, mmumunyo kolevu. **concentration** *n.* ukolezi: kiasi cha masi ya dutu katika mchanganyiko kwa kila kizio kimoja.

**concept** /'kənsept/ *n.* wazo; dhana. **~ion** *n.* wazo; dhana; uchukuaji mimba.

**concern** /kən'sɜ:n/ *v.t.* pasa; husu; juzu; sumbua; udhi; hangaisha; shughulisha. *~ oneself with,* jishughulisha na jambo. *be ~ed about the future,* hangaikia mambo ya maisha ya baadaye. *n.* **1.** shirika; kampuni. **2.** shaka; hangaiko. **~ing** *prep.* kuhusu.

**concert** /'kɒnsət/ *n.* tafrija ya pamoja; umoja wa shauri. *in ~ with,* kwa mashauriano na; kwa mapatano na. **~ed** *adj.* -a pamoja. *~ action,* tendo la pamoja.

**conciliate** /kən'sɪlɪeɪt/ *v.t.* patanisha; suluhisha; tuliza.

**conciliation** /kən,sɪli'eɪʃn/ *n.* upatanishi; usuluhishi.

**conciliatory** /kən'sɪɪliətəri/ *adj.* -

upatanishi; -suluhifu.
**concise** /kən'saɪs/ *adj.* -fupi; -enye habari nyingi katika maneno machache; -dogo.
**conclave** /'kɒŋkleɪv/ *n.* baraza ya siri; njama; mzengwe.
**conclude** /kən'klu:d/ *v.t./i.* koma; isha; komesha; hitimisha; dhani; maliza. **conclusion** *n.* mwisho; hitimisho; hukumu. **conclusive** *adj.* - enye nguvu; -a kuthibitisha; -a mwisho.
**concord** /'kɒŋkɔ:d/ *n.* mapatano; umoja; itifaki; mkataba; urafiki. **~ance** *n.* upatanifu.
**concourse** /'kɒŋkrɪ:t/ *n.* mkutano; kundi; umati.
**concrete** /'kɒŋkri:t/ *adj.* -a kushikika; -a kuonekana. e.g. *a ~ example,* mfano halisi. *n.* kangiriti; zege.
**concur** /kən'kɜ:(r)/ *v.i.* **(-rr-)** patana; kubali; ridhika; tokea chanjari. **~rence** *n.* mapatano; makubaliano. **~rent** *adj.* -a wakati mmoja; chanjari. **~rently** *adv.* chanjari; sawia; sambamba.
**concussion** /kən'kʌʃn/ *n.* mtikisiko; mgongano; kuzirai kwa sababu ya kipigo cha kichwa.
**condemn** /kən'dem/ *v.t.* laumu; patiliza; hukumu; batilisha. **~ation** *n.* lawama; laana; hukumu; upatilizaji.
**condense** /kən'dens/ *v.t./i.* fanya -zito; punguza; fanya muhtasari wa; punguka na kuwa -zito zaidi; owevya; tonesha. *a ~d account of an event,* maelezo ya tukio kwa muhtasari. **~r** *n.* . kondensa; kitoneshi; kiowevya. **conde-nsation** *n.* uoevukaji; utoneshaji, mtonesho: hali ya kubadilika mvuke kuwa matone; mbadiliko wa kikemia wa molekuli mbili na kutengeneza nyingine kubwa. **condensation poly-merization**, upolima mtonesho: utendanaji wa kikemikali ambao molekuli ndogo huungana kuunda na molekuli kubwa.
**condescend** /ˌkɒndɪ'send/ *v.i.* **1.** tendea hisani kwa lengo la kujionyesha. **2.** fanya au kubali kitu kilicho chini ya hadhi yako.
**condescension** /ˌkɒndɪ'senʃn/ *n.* wema wenye lengo la kujionyesha.
**condition** /kən'dɪʃn/ *n.* tabia; hali; hulka; cheo; kanuni; sharti; mapatano; siha; afya. **~al** *adj.* shurutia; -a muda tu; -enye masharti. **~ed** *adj.* -enye hali fulani.
**condole** /kən'dəʊl/ *v.i.* hurumia; sikitikia; hani; -pa pole; peleka rambirambi. **~nce** *n.* rambirambi.
**condom** /'kɒndɒm/ *n.* kondomu.
**condone** /kən'dəʊn/ *v.t.* achilia; samehe.
**conduce** *v.i.* faa; saidia; elekea kuleta. **conducive** *adj.* -a kufaa kwa; -a kuelekea kuleta.
**conduct** /'kɒndʌkt/ *n.* mwenendo; matengenezo; usimamizi; uongozi; tabia. v.t./i. ongoza; peleka; tengeneza; endesha. **~ivity** *n.* upitifu: kima cha upitishaji katika midia. **~or** *n.* **1.** mwongozaji; kiongozi. **2.** kipitishi: midia yoyote inayoweza kupitisha umeme au joto.
**conduit** /'kɒndɪt/, -jʊɪt/ *n.* mfereji; neli; bomba; konjuti: paipu inayohifadhi nyaya za umeme.
**cone** /kəʊn/ *n.* koni: kitu cha mviringo chini kilichochongoka juu; pia. **~ cell**, seli koni: moja ya seli katika retina zinazofasiri mwanga wa rangi kuwa seli za fahamu. **conic, conical** *adj.* - enye umbo la koni.


cones

**confection** /kən'fekʃn/ *n.* chakula chenye utamu kama sukari. **confectionery** *n.* aina ya vyakula vitamu kama halua, kashata, maandazi, peremende, etc. **confectioner** *n.* muuzaji vitu vitamu hasa vya sukari.
**confederate** /kən'fɛd(ə)rət/ *adj.* -a shirikisho. *n.* rafiki; mwenza; mshirika; msaidizi. **confe-deration** *n.* shirikisho; urafiki.
**confer** /kən'fə:/ *v.t./i.* **(-rr-)** **1.** toa; -pa;

jalia; tunza; tunukia shahada, cheti. **2.** shauriana; ongea; barizi. **~ence** *n.* mkutano; mazungumzo; baraza.
**confess** /kən'fes/ *v.t./i.* kiri; kubali; ungama; ungamisha. **~ion** *n.* uungamaji; kukiri. **~ional** *n.* kizimba cha siri kanisani ambapo kasisi huungamisha wakosaji. **~or** *n.* muungamishi.
**confide** /kən'fʌid/ *v.t./i.* ambia kwa siri; aminisha. *~ in,* tumainia; amini; tegemea.
**confidant** /'kɒnfɪdant, ˌkɒnfɪ'dant, -dɑ:nt/ *n.* msiri. **~nce** *n.* siri; ushupavu; matumaini; imani; ujasiri. **~nt** *adj.* -tumainifu; -shupavu; jasiri; -enye hakika. **~ntial** *adj.* -a siri. *~ secretary,* mwandishi wa siri.
**configuration** /kənˌfɪgə'reɪʃ(ə)n, -gjʊ-/ *n.* umbo; wasifu; hali; tabia; sura.
**confine** *v.t.* wekea mpaka; funga; zuia; husika na. **~s** *n.* mipaka; ukingo. **~d** *adj.* -enye kujifungua; -enye kuzaa; -embamba; enye mipaka. **~ment** *n.* kifungo; uzazi; kizuizi.
**confirm** /kən'fɜ:m/ *v.t.* thibitisha; imarisha; idhinisha; -pa kipa imara. **~ation** *n.* uthibitisho.
**confiscate** /'kɒnfɪskeɪt/ *v.t.* filisi; nyang'anya; twaa mali ya mtu mwingine kwa nguvu ya serikali; adhibu mtu kwa kutwaa mali zake.
**conflagration** /ˌkɒnflə'greɪʃ(ə)n/ *n.* moto mkubwa.
**conflict** /'kɒflɪkt/ *n.* mapigano; vita; ugomvi; mzozo; mapambano; suitafahamu. *v.i.* pambana; hitilafiana; pingana; zozana; tofautiana.
**confluence** /'kɒnflʊəns/ *n.* mahali inapokutana mito miwili; makutano.
**conform** /kən'fɔ:m/ *v.i./t.* fanana; fuata; sawazisha; patana; tii; kubali. **~ation** *n.* umbo; tabia; hali; sura. **~ity** *n.* usawa; upatanaji; ulinganifu; taa.
**confront** /kən'frʌnt/ *v.t.* kabili; pinga; pambanisha; piganisha. **~ation** *n.* mapambano; mgongano.
**confuse** /kən'fju:z/ *v.t.* changanyisha; chafua; changanya; fadhaisha; paraganya. **~ed** *adj.* -a wasiw a s i ; - liochanganyika; liyechanganyikiwa. **confusion** *n.* ghasia; machafuko; fujo; rabsha; wasiwasi; fadhaa.
**congeal** /kən'dʒi:l/ *v.t./i.* gandisha; ganda.
**congenial** /kən'dʒi:nɪəl/ *adj.* -a kupatana; -a kupendeza kitabia.
**congenital** /kən'dʒɛnɪt(ə)l/ *adj.* -a kuzaliwa na. *a ~ sickness,* ugonjwa wa kurithi.
**congested** /kən'dʒestɪd/ *adj.* -enye kusongana mno; -enye kujaa sana. *The streets were ~ with people,* njia zilijaa watu wengi; -enye damu nyingi kuliko kiasi. *His lungs were ~,* mapafu yake yalikuwa na damu nyingi. **congestion** *n.* msongamano.
**conglomerate** /kən'glɒm(ə)rət/ *n.* jabali lililofanyika kwa sedimenti ya kokoto au changarawe.
**congratulate** /kən'grætʃuleɪt/ *v.t.* shangilia; pongeza. **congratulation** *n.* pongezi; hongera.
**congregate** /'kɒŋgrɪgeɪt/ *v.t./i.* kusanya; kusanyika; kutanika.
**congregation** /'kɒŋgrɪ'geɪʃn/ *n.* mkusanyiko; kundi; jumla ya watu waabuduo.
**congress** /'kɒngres/ *n.* **1.** mkutano. **2.** baraza kuu katika bunge, hasa la Marekani.
**conifer** /'kɒnɪfə/ *n.* mti wa jamii ya msonobari.
**conjecture** /kən'dʒɛktʃə/ *v.i./t.* bahatisha; kisia; dhani. *n.* dhana; maoni.
**conjugate** /'kɒndʒʊgeɪt/ *v.t./i.* ainisha; pambanua; nyambua; ungana. **conjugation** *n.* uainishaji; unyambuaji; mnyambuliko.
**conjuction** /kən'dʒʌŋkʃn/ *n.* kiunganishi; muungano. *in ~ with,* pamoja na. **conjuctive** *adj.* -a kuunganisha.
**conjure** /'kʌndʒə/ *v.t./i.* fanya kiini macho; fanya mizungu; fanya mazingaombwe; omba kwa bidii; sihi. *~ up,* tunga; buni; fifiliza. **conjuror (conjurer)** *n.* mfanya

kiini macho, mizungu, mazinga ombwe.
**connect** /kə'nekt/ *v.t./i.* unganisha; unganika; shikamana; husu . **~ion**, **connexion** *n.* **1.** uunganishaji; kiungo. *bicycle pump ~*, kiungo cha pomu ya baiskeli. **2.** uwiano; uhusiano. *These affairs have no ~ with each other*, mambo haya hayahusiani. *in this ~*, kuhusiana na hili; **3.** ndugu; jamaa.
**conquer** /'kɒŋkə(r)/ *v.t.* shinda; teka; tiisha. **conquest** *n.* ushindi; mateka; ngawira.
**conscience** /'kɒnʃəns/ *n.* nadhari; moyo. *Have a clear (guilty) ~*, -wa na moyo mtulivu (wenye wasiwasi). *~ money*, fedha ilipwayo kama fidia kwa mtu aliyetendewa dhara fulani.
**conscientious** /ˌkkɒnʃi'enʃəs/ *adj.* enye bidii kufanya mema yote yapasayo; -aminifu.
**conscious** /'kɒnʃes/ *adj.* razini; -enye fahamu. *be ~ of*, fahamu; ona; sikia; jua. -enye haya; -enye soni. **~ness** *n.* fahamu; urazini.
**conscript** /kən'skrɪpt/ *v.t.* andikisha (askari) kwa lazima. *n.* askari au baharia aliyeandikishwa kwa amri ya serikali. **~ion** *n.* uandikishaji wa lazima.
**consecrate** /'kɒnsɪkreɪt/ *v.t.* weka wakfu; tabaruku; toa kwa ajili ya dini. **consecration** *n.* uwekaji wakfu.
**consecutive** /kən'sɛkjʊtɪv/ *adj.* -a kufuatana mfulizo. **~ly** *adv.* mfululizo; mtawalia; moja kwa moja.
**consensus** /kən'sɛnsəs/ *n.* mapatano; makubaliano; mwafaka.
**consent** *v.i./n.* kubali; ridhia; ruhusu; idhinisha; kibali; idhini; ruhusa; ridhaa; radhi.
**consequence** /'kɒnsɪkwəns/ *n.* **1.** matokeo. **2.** ukubwa; cheo; heshima; umaarufu. *It's of no ~*, haina maana; si kitu; basi; haidhuru. *a person of ~*, mtu mwenye cheo kikubwa. **consequent** *adj.* -a baadaye. **consequential** *adj.* -a kufuatana; -enye majivuno; -a fahari. **consequently** *adv.* hatimaye; baadaye.
**conserve** /kən'sə:v/ *v.t.* hifadhi; tunza; linda. **conservation** *n.* utunzaji; hifadhi; ulinzi. **conservation of energy**, hifadhi ya nishati: matumizi bora ya mafuta au nishati ili kupunguza upoteaji wake. **conservation of mass**, hifadhi ya masi: kanuni ambayo wakati wa utendenaji wa kemikali atomi hujipanga upya bila ya kuundika tena au kuharibika. **conservation of momentum**, hifadhi ya momenta: kulingana kwa momenta kabla na baada ya tukio.
**conservative** /kən'sɜ:vətɪv/ *n./adj.* muhafidhina; asiyependa kubadili mambo; *(colloq.)* -enye hadhari; -a kiasi.
**consider** /kən'sɪdə(r)/ *v.t./i.* fikiri; kumbuka; pima; dhani; angalia; dhania. **~able** adj. -a kustahili kufikiriwa; -kubwa kidogo; -a kiasi. **~ate** *adj.* -enye huruma; -pole; angalifu; -enye busara. **~ation** *n.* fikira; uangalifu; huruma; wema. *take into ~*, angalia; zingatia; kumbuka. **~ing** *prep.* kwa kuwa; kwa sababu; kwa kuzingatia.
**consign** /kən'sʌɪn/ *v.t.* peleka; wekea; weka; pelekea. **~ee** *n.* mpelekewaji. **~ment** *n.* upelekaji; bidhaa, mzigo, vitu, shehena, ipelekwayo.
**consist** /kən'sɪst/ *v.i.* -wa. *~ of*, -wa na. *~ in*, -wa na asili ya. **~ence**, **~ency** *n.* uthabiti; usawa; kutobadilika. *mix flour and milk to the right ~*, changanya unga na maziwa yawe na uzito ufaao. **~ent** *adj.* thabiti; -aminifu; -a kulingana sawa; -a kupatana na.
**console** /kən'səʊl/ *v.t.* fariji; tuliza; liwaza. **consolation** *n.*faraja; kitulizo; maliwazo.
**consolidate** /kən'sɒlɪdent/ *v.t./i.* imarisha; unganisha; ungana; imarika. **~ed** *adj.* imara; thabiti; -ngumu; -enye umoja.
**consonant** /'kɒns(ə)nənt/ *n.*

konsonanti: herufi isiyokuwa vokali kama b, c, d. *adj.* -sawa; -a kufanana; -a kulingana; - a kupatana. **consonance, consonancy** *n.* upatano; ulinganifu.

**conspicuous** /kən'spɪkjʊəs/ *adj.* -enye kuonekana; wazi; bayana; bora; mashuhuri.

**conspire** /kən'spaɪə(r)/ *v.i.* shauriana; ungana (hasa kwa ubaya); panga njama. *Events ~d to bring about his failure,* mambo yaliyopangwa kumuangusha. **conspirator** *n.* mshiriki katika uovu. **conspiracy** *n.* njama.

**constable** /'kʌnstəb(ə)l, 'kɒn-/ *n.* polisi . **constabulary** *n.* ofisa wa polisi wa cheo cha chini kabisa.

**constancy** /'kɒnstənsi/ *n.* uthabiti; uaminifu.

**constant** /'kɒnstənt/ *adj.* -a siku zote; -a daima; thabiti; -siyobadilika; -aminifu. **~ly** *adv.* mara nyingi; daima; mara kwa mara.

**constellation** /ˌkɒnstə'leɪʃn/ *n.* kundinyota: kundi la nyota.

**consternation** /ˌkɒnstə'neɪʃn/ *n.* hofu kuu; mshangao; fadhaa.

**constipate** /'kɒnstɪpeɪt/ *v.t.* zuia choo. **constipation** *n.* hali ya kuzuia choo; uyabisi wa tumbo.

**constituent** /kən'stɪtjuənt/ *adj.* **1.** enye haki ya kutunga au kubadilisha katiba, kupiga kura. **2.** -a sehemu ya kitu kizima. *n.* mpiga kura.

**constitute** /'kɒnstɪtju:t/ *v.t.* weka; simamisha; anzisha; fanya; -wa.

**constitution** /ˌkɒnstɪ'tju:ʃn/ *n.* **1.** sheria; kanuni; katiba. **2.** tabia; asili; umbo; afya. **~al** *adj.* -a sheria; halali; -a katiba; -a asili; -a afya. *a ~ ruler,* mtawala wa kisheria.

**constrain** /kən'streɪn/ *v.t.* lazimisha; shurutisha; zuia. **~ed** *adj.* -a sharti; -a lazima; -enye kuzuiwa. **~t** *n.* nguvu; sharti; kikwazo; kizuizi.

**constrict** /kən'strɪkt/ *v.t.* bana; songa; minya; nyonga. **~ed** *adj.* -embamba; -finyu. **~ion** *n.* ufinyu; ubanaji.

**construct** /kən'strʌkt/ *v.t.* jenga; unga; fanya; unda; tunga. **~tion** *n.* jengo; ujenzi; muundo; tafsiri; maana. **~ive** *adj.* -a kujenga; -a kusaidia.

**consul** /'kɒns(ə)l/ *n.* balozi. **~ar** *adj.* -a kibalozi. **~ate** *n.* ubalozi.

**consult** /kən'sʌlt/ *v.t.* shauriana; tafuta habari katika maandishi. **~ant** *n.* stadi; mtaalamu; bingwa. **~ation** *n.* mashauriano; mkutano wa kushauriana.

**consume** /kən'sju:m/ *v.t./i.* -la; nywa; tumia; maliza; teketeza; haribu; lika; dhofu; haribika. **~r** *n.* mlaji; mtumiaji; mnunuzi. **consumption** *n.* ulaji; utumiaji.

**consumptive** /kənsʌmptɪv/ *adj.* -enye kuugua kifua kikuu au ukimwi.

**contact** /'kɒntakt/ *n.* mgusano; mkutano; mawasiliano. *be in ~ with sb.,* kutana, onana, wasiliana na mtu. **~ metamorphism,** badiliko mgusano: ubadilikaji wa majabali unaotokana na kugusana na magima moto.

**contain** /kən'teɪn/ *v.t.* **1.** -wa ndani; weka ndani; chukua ndani. **2.** zuia.

**content** /'kɒntent/ *n.* maudhui; kilichomo ndani. *table of contents,* yaliyomo; fahirisi; faharasa.

**contaminate** /kən'tæmɪneɪt/ *v.t.* tia uchafu, najisi; haribu; ambukiza.

**contamination** /kənˌtæmɪneɪʃn/ *n.* uchafu; ambukizo; najisi.

**contemplate** /'kɒntɛmpləɪt/ *v.t.* tazama sana; fikiri sana; zingatia kwa makini; tafakari.

**contemplation** /ˌkɒntəm'pleɪʃn/ *n.* fikira; mawazo; hali ya kushika tama.

**contemporary** /kən'tɛmp(ə)r(ər)i/ *adj.* -a rika moja; -a wakati ule ule. *a ~ record of events,* kumbukumbu za nyakati moja. *n.* mtu wa hirimu moja. *We were contemporaries at school,* tulisoma shule wakati mmoja. **contemporaneous** *adj.* -a wakati uleule.

**contempt** /kən'tempt/ *n.* dharau; utwezaji; bezo; aibu; unyonge;

udhalilishaji. *treat with ~,* dharau; beua; beza; tweza; hizi; dhalilisha. *~ of court,* vunja amri ya mahakama. **~ible** *adj.* -a kudharauliwa; duni. **~uous** *adj.* -a kudharau.

**contend** /kən'tend/ *v.i.* jitahidi; shindana; pigana; pingana; kaidi; bishana; jadili; hoji. **contention** *n.* hoja; ushindani; ukinzani; kauli. *the bone of contention,* kisa cha ugomvi au ushindani.

**contentious** /kən'tenʃəs/ *adj.* gomvi; -bishi; -shindani; - kaidi.

**content** /kən'tɛnt/ *adj.* ridhisha. *be ~,* ridhi, ridhika; ridhia; -wa radhi. *be self ~ed,* kinai. *n.* radhi; ridhaa; kinaya. **~ed** *adj.* *be ~,* ridhika. **~ment** *n.* uradhi; radhi; ridhaa; kinaya.

**contest** /'kɒntɛst/ *v.t./i.* shindana; kana; bisha; kaidi. *n.* ugomvi; utesi; mabishano; shindano. **~ant** *n.* mshindani.

**context** /'kɒntɛkst/ *n.* muktadha; mazingira ambamo jambo hutokea; maneno yanayotangulia na kufuata maneno mengine ambayo hudhihirisha maana yake.

**contiguity** /ˌkɒntɪ'gju:ɪti/ *n.* utanga-mano; ujirani; ukaribiano.

**contiguous** /kən'tɪgjʊəs/ *adj.* -a kukaribiana; -a kugusana; -a jirani; a kupakana; -a kutangamana.

**continent** /'kɒntɪnənt/ *adj.* **1.** zuilifu wa tamaa, hasa ya kike na kiume. **2.** *n.* kontinenti;. bara. *~al drift,* msogeomrama wa bara: msogeomrama wa taratibu wa tabaka za dunia unaosababisha mabara kutengana.

**contingent** /kən'tɪndʒ(ə)nt/ *adj.* -sio hakika; -a bahati; -a kutegemea jambo jengine. *n.* sehemu ya kundi la askari. **contingency** *n.* jambo la nasibu; bahati. *In such a ~, we cannot agree,* mambo yakitokea hivi hatuwezi kukubali.

**continue** /kən'tɪnju:/ *v.i./t.* endelea; dumu; endesha; fululiza; zidi. **continual** *adj.* -a daima; -a kuendelea; -a moja kwa moja. **continuance** *n.* maisha; uende-levu. **continuation** *n.* mfuatano; mfululizo.

**continuity** /ˌkɒntɪ'nju:ɪti/ *n.* mfulizo; uendelevu. **continuous** *adj.* -enye kuendelea; -enye kufululiza.

**contour** /'kɒntʊə(r)/ *n.* kontua; umbo; sura; namna. *~line,* mstari uliochorwa katika ramani kuonyesha miinuko sawa ya nchi.

**contra** /'kɒntrə/ *prefix* kinyume cha; dhidi ya.

**contraceptive** /ˌkɒntrə'septɪv/ *n.* kinzamimba: kitu au dawa ambayo huzuia mwanamke asitunge mimba.

**contract** /'kɒntrækt/ *n.* mapatano; maafikiano; makubaliano; ahadi; kandarasi. *v.t./i.* patana; pata; patwa na; punguza; punguka; fupika; sinyaa; katibiana; afikiana; kubaliana: *~ debts,* daiwa. *~ a disease,* patwa na ugonjwa. *Iron ~s when it becomes cool,* chuma hupunguka kikipoa. **~ion** *n.* upunguaji; ufupisho; usinyaaji; unyweaji. **~or** *n.* kontrakta; mkandarasi; mzabuni.

**contradict** /ˌkɒntrə'dɪkt/ *v.t.* kana; kanusha; kinza; pinga; bisha; kaidi; hitilafiana; -wa kinyume cha. **~ion** *n.* mabishano; ukinzani; hitilafu; tofauti; kinyume.

**contrary** /'kɒntrəri/ *adj.* **1.** -a mbalimbali; -a kinyume; -a namna nyingine kabisa. **2.** -kaidi; -bishi; -tundu. *n.* kinyume. *on the ~,* bali; kinyume chake. *Have you finished?' 'On the ~ I have just started'.* 'umemaliza?' 'kinyume chake, ndio kwanza nimeanza'. **contrariness** *n.* ukaidi; ubishi.

**contrast** /'kɒntrɒ:st/ *v.t./i.* **1.** pambanisha; linganisha. **2.** -wa namna nyingine kabisa; -wa kinyume cha; -wa mbalimbali na. *n.* tofauti; hitilafu; kinyume; kitu kilicho tofauti kabisa.

**contravene** /ˌkɒntrə'vi:n/ *v.t.* shindana na; vunja (sheria, desturi, etc.) halifu; asi. **contravention** *n.* uhalifu; uasi; ukinzani; ushindani.

**contribute** /kən'trɪbju:t/ *v.t./i.* saidia; toa; shiriki; -wamo; changa; peleka habari kuchapishwa katika

jarida. **contribution** *n.* mchango; msaada; sadaka; sehemu. **contributor** *n.* mchangaji.

**contrive** /kən'trʌɪv/ *v.t./i.* tengeneza; buni; fanya; tunga. **contrivance** *n.* kitu kilichobuniwa; hila; mbinu.

**control** /kən'trəʊl/ *n.* amri; utawala; usimamizi; udhibiti; uongozaji. v.t. (**-ll-**) weza; zuia; dhibiti; simamia; ongoza; tawala. **~ler** *n.* mdhibiti; mwongozaji; msimamizi; mtawala.

**controversy**/'kɒntrəvə:si,/ *n.* ugomvi; ushindani wa maneno; ubishani; majadiliano yenye utata.

**convalescent** /ˌkɒnvə'lesnt/ *n./adj.* -a katika hali ya kupona; mtu anayepata ahueni.

**convection** /kən'vekʃn/ *n.* myuko: namna mvuke, joto n.k. vinavyosafirishwa katika kimiminiko kwa njia ya msogeo. ~ *current*, mkondo myuko: mkondo wa mtiririko unaosababishwa kwa njia ya myuko.

**convene** /kən'vi:n/ *v.t./i.* kusanya; ita kwenye mkutano; kutanisha; kusanyika; kutana; kutanika.

**convenient** /kən'vi:niənt/ *adj.* -a kufaa; rahisi kufikika; -a kuwepo tayari kutumika. **convenience** *n.* kifaacho; nafasi; nafuu; raha; wasaa; manufaa. *make a convenience of sb*, tumilia bila huruma mtu aliye tayari kusaidia. *at your convenience*, kwa wakati wako wa wasaa.

**convent** /'kɒnvənt/ *n.* jamii au nyumba ya watawa.

**convention** *n.* mkutano; mapatano; makubaliano; maagano; jambo la desturi. **~al** *adj.* -a desturi.

**converge** /kən'və:dʒ/ *v.i./t.* endea mahali pamoja; karibiana; sogeleana; kutana; kutanisha katika nukta moja.

**conversant** /kən'vɜ:snt/ *adj.* -zoefu; -enye kujua sana habari za mambo, watu.

**conversation** /ˌkɒnvə'seɪʃn/ *n.* mazungumzo; maongezi. **~al** *adj.* mzungumzaji; -a mazungumzo.

**converse** /kən'vɜ:s/ *n.* mazungumzo; maongezi. *v.i.* zungumza; ongea; sema.

**converse** /kən'və:s/ *n./adj.* kitu kilicho kinyume cha kingine; -a kinyume; -a upande wa pili. **~ly** *adv.* kwa upande wapili.

**conversion** /kən'vɜ:ʃn/ *n.* ubadilikaji; ugeukaji; kuritadi; usilimishaji.

**convert** /kən'vɜ:t/ *v.t.* geuza; badili; ritadi; badilisha dini ya mtu; silimu. *n.* muritadi: aliyerudia dini yake ya zamani.

**converter** /kən'vɜ:tə(r)/ *n.* kigeuzi: tanuri ya kutengenezea chuma; chombo cha kubadilisha mwelekeo wa umeme; chombo cha kubadilisha masafa.

**convex** /'kɒnvɛks/ *adj.* -a mbinuko: -enye umbo la kivimbe. ~ **lens**, lenzi mbinuko ambayo upande mmoja au zote mbili zimebinuka.


convex

**convey** /kən'veɪ/ *v.t.* **1.** chukua; peleka. **2.** julisha; arifu; ambia. **3.** (kwa wanasheria) wahilisha; sihia; kabidhi; salimisha; toa; fikisha; wasilisha. **~ance** *n.* **1.** uchukuzi; gari. **2.** hati ya kubadilisha au kuwahilisha mali.

**convict** /kən'vɪkt/ *v.t.* tia hatiani; thibitisha hatia ya kosa. *n.* mfungwa. **~ion** *n.* **1.** uthibitisho wa hatia ya kosa. **2.** usadikishaji; uthibitishaji; hakika. **3.** nia; dhana.

**convince** /kən'vɪns/ *v.t.* sadikisha; julisha; aminisha; shawishi; ridhisha.

**convoy** /'kɒnvɔɪ/ *v.t.* fuatana au sindikiza kwa ajili ya kulinda; linda njiani. *n.* ulinzi; walinzi wa msafara; msafara wenye walinzi.

**convulse** /kən'vʌls/ *v.t* sukasuka; tikisa; tetemesha. **convulsion** *n.* **1.** kifafa; (kwa watoto) degedege; kukutika. **2.** msukosuko; machafuko.

**cook** /kʊk/ *v.i./i./n.* pika; mpishi; iva; pikika. **~er** *n.* kuka; jiko; seredani. **~ery** *n.* upishi.

**cool** /kʊ:l/ *adj.* **1.** -a baridi kidogo. **2.** -tulivu. **3.** legevu; -tepetevu; -vivu; -

zembe; -enye macho makavu. **4.** -shupavu; fedhuli; -safihi; -juvi. *v.t./i.* poza; tulia; tuliza; zimua; poa; burudika; baridika; zizima. **~ant** *n.* kipozeshi; kipozi; kimiminiko kitumiwacho kushusha joto. **~ing** *n.* upozaji; uteremshaji wa kiwango cha hali joto kwa kitu.

**coolie** /'ku:li/ *n.* kuli; mchukuzi; hamali.

**coop** /ku:p/ *n.* kitundu; kizimba (cha kuku, etc.). *v.t.* funga, zuia zizini au kizimbani. **~er** *n.* mtengeneza mapipa.

**co-operate** /kəʊ'ɒpəreɪt/ *v.i.* fanya kazi pamoja; shirikiana; fanya ubia; saidia; saidiana. **co-operation** *n.* ushirikiano; ushirika; shirika. **co-operative** *adj.* -a kushirikiana; -a kusaidiana. *co-operative shop,* duka la ushirika. *co-operative society,* chama cha ushirika.

**co-opt** *v.t.* fanywa mwanakamati au pewa cheo chengine mkutanoni kutokana na uamuzi wa wana-chama.

**co-ordinate** /kəʊ'ɔ:dɪneɪt/ *adj.* a hadhi ileile; -a kulingana sawa. *v.t.* linganisha; patanisha; sawazisha; ratibu sehemu zinazohusika ili ziweze kufanya kazi pamoja kwa ufanisi.

**cope**[1] /kəʊp/ *n.* vazi la sherehe la kasisi.

**cope**[2] /kəʊp/ *v.i.* ~ *with,* weza; faulu; shindana na.

**copper** /'kɒpə(r)/ *n.* shaba nyekundu. **~ sulphate** *n.* mrututu.

**copra** /'kɒprə/ *n.* mbata; nazi kavu.

**copy** /'kɒpi/ *n.* kopi; nakala; mwigo. *v.t./i.* kopia; nakili; fuatisha; iga; igiza. **~right** *n.* hakimiliki: haki ya msanii ya kuzuia wingine wasiigize au kunakili kazi yake ya sanaa bila ya ruhusa yake.

**coral** /'kɒrəl/ *n. red* ~, marijani. **white~**, matumbawe. **~line** *adj.* a matumbawe; -a marijani.

**cord** /kɔ:d/ *n.* kamba nyembamba; ugwe. *spinal* ~, uti wa mgongo. *umbilical* ~, utovuti; kiungamwana. **~ite** *n.* utambi; aina ya baruti yenye umbo la ugwe.

**cordial** /'kɔ:diəl/ *adj.* -kunjufu; changamfu. *a ~ welcome,* mapokezi ya furaha. *n.* jambo linalofurahisha moyo; kiburudisho.

**corduroy** /'kɔ:dərɔɪ, -djʊ-/ *n.* kodurai; kodrai: aina ya nguo nzito tena ngumu.

**core** /kɔ:(r)/ *n.* moyo; kiini; sehemu ya katikati; maana halisi. **~r** *n.* kisu cha kutolea kokwa.

**cork** /kɔ:k/ *n.* gome la muoki; kizibo; koki. *v.t.* ziba. **~-screw** *n.* kizibuo.

**corn**[1] /kɔ:n/ *n.* nafaka; *maize* ~, mahindi. *wheat* ~, ngano. *grain of* ~, punje. **~-cob** *n.* gunzi; bunzi; gurunzi. *~-flour,* unga wa mahindi.

**corn**[2] /kɔ:n/ *n.* (kwa mguu) suguru; (kwa paji la uso) sijida.

**cornea** /'kɔ:nɪə/ *n.* konea: sehemu nyeupe ya jicho inayowezesha mionzi ya mwanga kupenya.

**corner** /'kɔ:nə(r)/ *n.* **1.** kona; pembe; nukta ambapo mistari miwili hukutana; ncha. *turn the* ~, (**fig.**) okoka hatarini. *a tight* ~, hatari kubwa. **2.** (kwa biashara) *make a ~ in wheat, etc.,* nunua ngano yote ili kupandisha bei. *v.t.* tia hatarini; weka pembeni; nunua bidhaa yote ili kupandisha bei; dhiisha. **~-stone** *n.* (**fig.**) msingi.

**corolla** /kə'rɒlə/ *n.* korola: jumla ya petali katika ua.

**coronation** /ˌkɒrə'neɪʃn/ *n.* kutawaza; kutawazwa kwa mfalme au malkia.

**coroner** /'kɒr(ə)nə/ *n.* afisa mchunguzi wa vifo vya ghafla vihusishwavyo na mauaji au ajali.

**corporal**[1] /'kɔ:pərəl/ *n.* koplo; cheo cha askari chini ya sajenti.

**corporal**[2] /'kɔ:pərəl/ *adj.* -a mwili. *~ punishment,* adhabu ya viboko.

**corporation** /ˌkɔ:pə'reɪʃn/ *n.* **1.** shirika; ushirika. **2.** madiwani wa manispaa. *the mayor and ~,* meya na madiwani wake. *public ~,* shirika la umma.

**corporate** /'kɔ:pərət/ *adj.* -a jamii; -a shirika.

**corps** /kɔ:/ *n.* kundi la askari. *carrier ~,* kikosi cha wachukuzi.

*diplomatic ~,* jamii ya mabalozi.
**corpse** /kɔ:pəs/ *n.* maiti; mzoga.
**corpuscle** /'kɔ:pʌs(ə)l/ *n.* seli au viini vyekundu au vyeupe vya damu.
**correct** /kə'rekt/ *adj.* sahihi; bila kosa; barabara. *v.t.* sahihisha; tia adabu; rudi; ongoa; rekebisha. **~ion** *n.* masahihisho; rekebisho; adhabu. **~ly** *adv.* barabara; sawasawa; kwa usahihi; vizuri. **~ness** *n.* usahihi.
**correspond** /ˌkɒrə'spɒ:nd/ *v.i.* **1.** lingana; fanana; afikiana; elekeana; shabihiana. **2.** wasiliana kimaandishi. **~ence** *n.* **1.** usawa; ulinganifu; mshabaha. **2.** mawasiliano ya maandishi; masjala. *~ clerk,* karani masjala. **~ent** *n.* **1.** mwenza. **2.** mwandishi wa habari maalumu au toka nje ya nchi.
**corridor** /'kɒrɪdɔ:(r)/ *n.* mlia; ujia mwembamba nyumbani uunga nishao vyumba; ukumbi.
**corrode** /kə'rəʊd/ *v.t./i.* -la; haribu; lika; haribika; babua kwa kemikali.
**corrosion** /kə'rəʊʒn/ *n.* uharibifu wa kuliwa na kutu au tindikali. **corrosive** *n./adj.* -enye uwezo wa kubabua kama kutu au asidi.
**corrugated** /'kɒrəgeɪtɪd/ *adj.* -enye mikunjo au migongomigongo midogo. *~iron sheets,* mabati ya kuezekea. **corrugation** *n.* migongomigongo; mikunjokunjo; makunyazi.


**corrugated iron sheets**

**corrupt** /kə'rʌpt/ *adj.* -ovu; -bovu; -potofu; -chafu; fisadi; fasiki; habithi; -baya. **~air,** hewa chafu.*v.t./i.* chafua; ozesha; haribu; fisidi; badili; geuza; lisha rushwa; honga; haribika. **~ible** *adj.* -enye kula rushwa. **~ion** *n.* rushwa; uozo.
**cortex** /'kɔ:tɛks/ *n.* **1.** koteksi: tabaka ya nje ya ubongo; figo. **2.** ganda; gamba; gome.
**cosmopolitan** /ˌkɒzmə'pɒlɪt(ə)n/ *adj.* a kuhusu sehemu zote za ulimwengu.
**cost** /kɒst/ *v.i./t.* gharimu; uzwa kwa bei fulani. *What does it ~?* kiasi gani? *n.* **1.** bei; kima; thamani; gharama. **2.** gharama ya kuendesha kesi kortini. *at all ~s,* kwa vyovyote. **~ly** *adj.* a thamani kubwa; ghali; -a tunu.
**costume** /'kɒstju:m/ *n.* mavazi ya kawaida. **2.** koti fupi na sketi ya kike. **costumier** *n.* mtengenezaji, muuzaji, muazimaji nguo za sherehe.
**cosy** /'kəʊzi/ *adj.* -a raha nyingi; -a anasa.
**cot** /kɒt/ *n.* kitanda cha mtoto mdogo; nyumba ndogo.
**cotangent** /kəʊ'tandʒ(ə)nt/ *n.* kotanjiti: tanjiti kamilishi ya pembe.
**cottage** /'kɒtɪdʒ/ *n.* nyumba ndogo. **~er** *n.* mkulima; kibarua anayeishi ndani ya nyumba ya shamba.
**cotton** /'kɒtn/ *n.* pamba. *~ wool,* pamba. *~ cake,* mashudu ya pamba.
**cotyledon** /ˌkɒtɪ'li:d(ə)n/ *n.* kotiledoni; jani la kwanza linalochipua kwenye mbegu.
**couch** /kaʊtʃ/ *n.* sofa; kochi; kitanda. *v.t./i.* **1.** eleza kwa maneno. **2.** jikunyata; jificha; jilaza.
**cough** /kɒf/ *v.i.* kohoa. *n.* kikohozi.
**council** /'kaʊnsl/ *n.* baraza; diwani; halmashauri; mkutano. **city ~,** halmashauri ya jiji. **revolutionary ~** baraza la mapinduzi. **legislative ~,** baraza la kutunga sheria. **~lor** *n.* mshauri; mjumbe wa baraza; diwani; mshauri; msiri.
**counsel** /'kaʊnsl/ *n.* shauri; fikira; maoni; nasaha; mawaidha; waadhi; wasia; wakili; mwanasheria. *keep one's own ~,* ficha nia. *hold ~ with (sb.), take ~ together,* shauriana. *v.t.* **(-ll-)** shauri; onya; nasihi. **~lor** *n.* mshauri; msiri.
**count**[1] /kaʊnt/ *v.t./i.* **1.** hesabu; adidi. **2.** tegemea; tumainia. *He does not ~,* hana maana. **3.** dhania; ona. *n.* **1.** hesabu; kuhesabu; idadi. *take the ~ (boxing),* hesabiwa kuwa umeshindwa katika ndondi. **2.** shtaka; mashtaka. **~er** *n.* kaunta: sehemu ya kupokelea fedha au kuwekea vitu vya kuuza. **~less** *adj.* siohesabika; -ingi mno.
**count**[2] /kaʊnt/ *n.*cheo cha heshima

katika baadhi ya nchi. **~ess** *n.* mke wa mtu mwenye cheo hicho.

**counter**[1] /'kaʊntə(r)/ *n.* sarafu bandia zitumikazo katika michezo tu.

**counter**[2] /'kaʊntə(r)/ *adv.* kwa mkabala wa kupinga.

**counter**[3] /'kaʊntə(r)/ *-prefix* **1.** -a kinyume au ya kupinga. **2.** -a kujibu; -a kulipiza; dhidi ya.

**counteract** /'kaʊntər'ækt/ *v.t.* kinza; zuia; shinda.

**counterbalance** /'kaʊntə, bal(ə)ns/ *n.* uzito ulio sawa na uzito mwingine katika mizani. *v.t.* sawazisha kwa kuongeza uzito, nguvu, upande ulio mwepesi.

**counterfoil** /'kaʊntəfɔɪl/ *n.* nakala; kopi ya stakabadhi.

**counterpart** /'kaʊntəpɑ:t/ *n.* mwenza; kifanani; nakala.

**countersign** /'kaʊntəsaɪn/ *n.* ishara au neno la siri, alama watumiao askari katika zamu. *v.t.* tia saini mara ya pili; thibitisha kwa kutia saini.

**country** /'kʌntrɪ/ *n.* nchi; bara; shamba. **~man** *n.* mkulima; mtu wa nchi moja; ndugu wa kabila moja.

**county** /'kaʊnti/ *n.* mkoa, jimbo au wilaya.

**coup** /ku:/ *n.* kipigo; dhoruba; mapinduzi. *~ d'etat,* mapinduzi ya kijeshi. *~ de grace,* pigo la kifo.

**couple** /'kʌpl/ *n.* **1.** kiungo; jozi; watu (au vitu) wawili wa namna moja au pamoja; wachumba; maharusi. **2.** mume na mke. *v.t.* **1.** unga au weka vitu pamoja. **2.** ungana; unganika.

**coupon** /'ku:pɒn/ *n.* kuponi; cheti.

**courage** /'kʌrɪdʒ/ *n.* ushujaa; uhodari; uthabiti; ushupavu; ujasiri. *take ~,* jipa moyo; kaza moyo; piga moyo konde. **~ous** *adj.* shujaa; hodari; jasiri; thabiti.

**course**[1] /kɔ:s/ *n.* **1.** mwendo; njia; maendeleo; majira. *the ~ of events,* jinsi mambo yaendavyo. *A railway was in ~ of construction,* reli ilikuwa inajengwa. *In the ~ of his childhood he often went hunting,* wakati wa utoto wake aghlabu alikuwa akiwinda. *in ~ of time,* halafu; baadaye. *in ~ of conversation,* katika kuongea. *in due ~,* kwa wakati wake. *of ~,* ndiyo; naam; bila shaka. **2.** mwenendo; maisha. **3.** uwanja wa mashindano. **4.** mfululizo; safu; mstari. **5.** sehemu au aina moja ya chakula, katika wakaa.

**course**[2] /kɔ:s/ *v.t./i.* **1.** winda kwa mbwa. **2.** tiririka; enda kasi; piga mbio.

**court** /kɔ:t/ *n.* **1.** korti; mahakama; mahakimu; majaji. **2.** ikulu; kasri; wafuasi wa kiongozi wa nchi. **3.** uwanja; kitalu; uwa. **4.** heshima. *v.t.* chumbia; jipendekeza kwa; bembeleza; posa; heshimu. **~ious** *adj. n.* -a adabu; -a heshima; -a staha. **~ier** *n.* mfuasi wa kiongozi wa nchi. **~martial** *n.* baraza ya hukumu ya majeshi. **~ship** *n.* posa; ubembelezi; uchumba.

**cousin** /'kʌzn/ *n.* mtoto wa ndugu wa baba au mama; binamu.

**covalent bond** *n.* muungo kikovalenti: muungo wa atomu mbili katika molekuli ambapo kila atomu inachangia elektroni moja.

**covalent compound** *n.* msombo uliojengwa kwa muungo kikovalenti.

**cover** /'kʌvə(r)/ *v.t.* **1.** funika; tanda; gubika; enea. *The water ~s the whole plain,* maji yameenea uwanda mzima. **2.** enda; safiri. *~ ten miles in an hour,* enda maili kumi kwa saa. **3.** lenga (kwa bunduki au bastola ). **4.** linda; hifadhi; katia bima. **5.** tosheleza. *n.* kifuniko; jalada; gamba; ala; kificho.

**cow**[1] /kaʊ/ *n.* ng'ombe; jike la mnyama mkubwa. **~herd** *n.* mchunga ng'ombe. **~-hide** *n.* ngozi ya ng'ombe.

**cow**[2] /kaʊ/ *v.t.* ogofya; tisha; vunja moyo. **~ed** *adj.* -oga; -enye hofu; -nyonge.

**coward** /'kaʊəd/ *n.* mwoga. **~ly** *adj.* -oga. **~ice** *n.* woga; hofu.

**cowrie** /'kaʊ(ə)ri/ *n.* kauri; kaure.

**crab** /kræb/ *n.* kaa wa pwani;

chanje.


crab

**crack** /kræk/ *n.* **1.** ufa; mwatuko. **2.** mwaliko; kishindo; mtataliko; radi. **3.** pigo la ghafla. *v.t./i.* fanya ufa; tia ufa; vunja; pasua; vunjika; pasuka; alika; alisha. **4. (colloq.)** ~ *up,* haribika ghafla; ~ *sb. or sth. up,* vumisha; sifu mno. ~ *a joke,* fanya mzaha. **~er** *n.* **1.** namna ya mkate mwembamba tena mgumu. **2.** fataki ya kuchezea. **~le** *v. i./n.* data; tatalika; alika.

**cradle** /'kreɪdl/ *n.* kitanda kidogo cha mtoto; susu.

**craft** /krɑ:ft/ *n.* **1.** ufundi; ustadi; amali; ubingwa; umahiri. **2.** hila; werevu; ujanja; udanganyifu. **3.** vyombo vya baharini. **~sman** *n.* fundistadi. **~y** *adj.* -a hila; -erevu. **~ily** *adj.* kiujanja; kifundi; kihila. **~iness** *n.* werevu; hila; ujanja; udanganyifu.

**cramp** /kræmp/ *n.* kiharusi; jiriwa. *v.t.* bana kwa jiriwa; pata kiharusi. **~ed** *adj.* -embamba; siyotosha; finyu; enye herufi ndogo zilizosongana na ngumu kusomeka.


crane

**crane** /kreɪn/ *n.* **1.** *(bird)* korongo. **2.** slingi; winchi. *v.t. /i.* nyoosha shingo; jinyoosha.

**crank** /kræŋk/ *n.* kombo; hendeli. **~ shaft** *n.* mtaimbo kombo. *v.t.* piga hendeli.

**crash** /kræʃ/ *v.t./i.* **1.** enda au anguka kwa kishindo; vunjika kwa kishindo. ~ *into,* dunda, gonga kwa nguvu. **2.** (kwa kampuni ya biashara au kwa serikali) filisika. *n.* **1.** kishindo cha kuanguka. **2.** kufilisika.

**crate** /kreɪt/ *n.* sanduku; kreti; tenga.

**crater** /'kreɪtə(r)/ *n.* kreta; kasoko: shimo la katikati la mlima lililosababishwa na volkano.

**crawl** /krɔ:l/ *n./v.i.* tambaa; jikokota; enda polepole.

**crayon** /'kreɪən/ *n.* krayoni; chaki au penseli ya rangi.

**crazy** /'kreɪzi/ *adj.* -enye wazimu; kichaa. **craze** *n.* **1.** wazimu; kichaa. *v.t.* tia kichaa; tia wazimu; rusha akili; tia wasiwasi; tia wahka.

**creak** /kri:k/ *v.i/n.* lia kwa sauti ya mkwaruzo.

**cream** /kri:m/ *n.* **1.** maziwa ya mtindi; malai; krimu. **2.** sehemu iliyo bora. **3.** rangi ya krimu; rangi ya samli. *v.t./i.* fanya mtindi; engua mtindi. **~ery** *n.* pauzwapo au patengenezwapo siagi, maziwa, jibini, na mtindi.

**crease** /kri:s/ *n.* **1.** mkunjo. **2.** mstari uliochorwa juu ya ardhi kwa chokaa katika mchezo wa kriketi. *v.t./i.* kunja; kunjana.

**create** /kri'eɪt/ *v.t.* umba; vumbua; fanya; buni; tunga; zua. **creation** *n.* uumbaji; ulimwengu; viumbe vyote. **creator** *n.* muumba; mfanyaji; *The Creator,* Mwenyezi Mungu. **creature** *n.* kiumbe.

**credible** /'kredəbl/ *adj.* -a kustahili kusadikika; -a kusadikika; -a kuaminika.

**credit** /'kredɪt/ *n.* **1.** imani; itibari; mkopo; muamana; uaminifu. **2.** sifa njema. **3.** heshima. **4.** muda wa kulipa deni. **5.** fedha alizo nazo mtu katika benki. *v.t.* amini; kopesha; karidhi. **~able** *adj.* -enye kuleta heshima. **~or** *n.* mdai.

**credulous** /'krɛdjʊləs/ *adj.* -epesi kuamini au kusadiki bila ushahidi.

**creed** /kri:d/ *n.* imani; nguzo ya dini.

**creek** /kri:k/ *n.* hori; ghuba ndogo; kijito. *be up the ~,* wa mashakani.

**creep** /kri:p/ *v.i.* (**crept**) /krept/ ambaa; enda polepole; jikokota *the* **~s,** hali ya damu kusisimka; msisimko. *creep up to,* nyatia; nyemelea. **~er** *n.* mnyama au mti wenye kutambaa. **~y** *adj.* a kuleta msisimko.

**cremate** /krə'meɪt/ *v.t.* unguza; choma maiti badala ya kuzika. **cremation** *n.* uchomaji maiti.

**crescent** /'krɛz(ə)nt,-s / *n.* mwezi mwandamo; mwezi koongo; mwezi mchanga; kitu chenye umbo koongo.

**crest** /krest/ *n.* **1.** shungi; unyunju

wa jogoo; upanga wa jogoo; kishada. **2.** alama ya kuonyesha nasaba ya ukoo, kama chapa ya nishani. **3.** kilele; ncha ya juu. **~fallen** *adj.* -a majonzi; -a kukata tamaa.

**cretaceous** /krɪ'teɪʃəs/ *adj.* -a chaki; ~ *age*, zama za kijiolojia ambapo miamba ya chaki iliumbika.

**crew** /kru:/ *n.* jumla ya wafanyakazi wa melini, ndegeni au relini.

**cricket**[1] /'krɪkɪt/ *n.* nyenje; panzi; senene.

**cricket**[2] /'krɪkɪt/ *n.* mchezo wa kriketi. *Not ~, (colloq.)* si desturi; si haki.



**cricket**

**crime** /kraɪm/ *n.* uhalifu; kosa; dhambi; uvunjaji sheria. **criminal** *adj.* -a kuvunja sheria; -ovu. *n.* mhalifu; mvunja sheria. **criminology** *n.* taaluma ya kisayansi ya makosa ya jinai.

**crimson** /'krɪmz(ə)n/ *adj./n.* -a rangi nyekundu; wekundu uliokoza karibu na uzambarau.

**cripple** /'kripl/ *n.* kiwete; kilema; mlemavu. v.t. fanya mtu kiwete; haribu; punguza sana nguvu; lemaza.

**crisis** /'kraɪsɪs/ *n.* (**crises**) / si:s/ **1.** kipeo; upeo wa mgogoro; hatari; ugonjwa etc. **2.** hali ya hatari; hali ya wasiwasi mkubwa.

**crisp** /krɪsp/ *adj.* **1.** -kavu hata kuweza kufikichika. **2.** (kwa hewa) -a kuburudisha; -a baridi. **3.** (kwa nywele) -a kipilipili. **4.** (kwa tabia) -epesi; thabiti; bila shaka.

**criterion** /krʌɪ'tɪərɪən/*n.* (**criteria**) kigezo; ruwaza.

**critic** /'krɪtɪk/ *n.* mhakiki; mkosoaji. **~ism** n. uhakiki; lawama. **~ize** *v.t./i.* hakiki; laumu; kosoa; toa maoni.

**critical** /'krɪtɪkl/ *adj.* **1.** muhimu kabisa. **2.** -a uhakiki. **3.** - a lawama. **~ angle**, pembe pambanuzi. **~ mass**, masi pambanuzi. **~ point**, nukta, kiwango pambanuzi. **~ speed**, kasi pambanuzi. **~ temperature**, halijoto pambanuzi.

**croak** /krəʊk/ *n.* mlio kama wa chura au kunguru. *v.t./i.* **1.** lia kama chura au kunguru. **2.** bashiri mambo mabaya.

**crock**[1] /krɒk/ *n.* chombo cha udongo, kaure au kigae. **~ery** *n.* vyombo vya udongo, kaure au kigae.

**crock**[2] /krɒk/ *n. (colloq.)* mnyama mzee tena dhaifu (hasa farasi ); mtu asiyeweza kufanya kazi vizuri kwa sababu ya ugonjwa.

**crocodile** /'krɒkədaɪl/ *n.* mamba.

**crook** /krʊk/ *n.* **1.** fimbo ndefu iliyopindika mwishoni. **2.** kingoe; kingosho; matege. **3.** mjanja; -enye hila; tapeli; jagari. **~ed**. *adj.* si sawasawa; -danganyifu; -enye matege.

**crop**[1] /krɒp/ *n.* mavuno; mazao; matunda.

**crop**[2] /krɒp/ *n.* **1.** umio; kibofu cha kooni; gole la ndege. **2.** mchapo; mjeledi. **3.** mkato wa nywele kuwa fupi sana.

**crop**[3] /krɒp/ *v.t./i.* (**-pp-**) **1.** -la machipukizi au vilele vya mimea. **2.** kata; nyoa kuwa fupi. ~ *up*, onekana; zuka; tokea ghafla.

**cross** /krɒs/ *n.* **1.** msalaba. **2.** chotara wa wanyama au mimea. *adj.* **1.** -a hasira; -kali; -a chuki. **2.** -a kupinga njia. *be at ~ purposes*, kabiliwa na mambo mawili yasiyowiana. *v.t.i.* **1.** pita; vuka. *~ a cheque*, saini cheki kwa namna ambayo haivunjiki ila kwa idhini ya benki tu. **2.** changanya mbegu. **3.** zuia; pinga. *~ one's mind*, kumbuka. **~-examine** *v.t.* hoji; saili. **~-eyed** *adj.* -enye makengeza. **~roads** *n.* njia panda. **~word** (**puzzle**) *n.* chemsha bongo ya maneno yaliyopangwa kwenye mraba. **~section** *n.* eneomkato sulubi: eneo la kitu kilichokatwa kuonyesha sehemu za ndani.



**crossword**

**crouch** /kraʊtʃ/ *v.i.* jikunyata;

jikunja; inama; chutama; fuama.
**crow**[1] /krəʊ/ *n.* kunguru. *as the ~ flies,* kwa mwendo wa njia ya mkato moja kwa moja.
**crow**[2] /krəʊ/ *v.i.* (**crowed** au **crew**, **crowed**) **1.** (kwa jogoo) wika. **2.** (kwa watoto wachanga) cheka. *~ over,* jivunia; cheka; simanga; shangilia.
**crowbar** /ˈkrəʊbɑː(r)/ *n.* mtaimbo.
**crowd** /kraʊd/ *n.* kundi; umati; msongamano; halaiki. *v.i.* songana; kusanyika; -ja kwa wingi; jaa. *v.t.* songa; jaza sana. *~ round,* zongea.
**crown** /kraʊn/ *n.* **1.** taji. **2.** serikali. **3.** utosi. **4.** sehemu ya juu; kilele. **5.** uzuri; ubora; ukamilifu; utimilifu. *v.t.* **1.** visha taji; tawaza. **2.** wa juu ya. *a hill ~ed with trees,* kilima kilichofunikwa na miti. **3.** -wa matokeo ya. *Success will ~ his effforts,* matokeo ya jitihada yake ni kufuzu. *~ prosecutor,* wakili au mwendesha mashtaka wa serikali.
**crucial** /ˈkruːʃ(ə)l/ *adj.* -a maana; -a umuhimu mkubwa.
**crucible** /ˈkruːsɪb(ə)l/ *n.* chombo kitumiwacho kuyeyushia metali ndani yake.
**crucifix** /ˈkruːsɪfɪks/ *n.* sanamu au taswira ya Yesu Kristo akiwa amesulubiwa msalabani. **cruciform** *adj.* nye sura ya msalaba.
**crucify** /ˈkruːsɪfʌɪ/ *v.t* sulubisha; sulubu. **~ion** *n.* kusulibiwa.
**crude** /kruːd/ *adj.* **1.** bichi; -sio safika; changa; isiyotengenezwa; si a adabu; -jinga; isiyofanywa vizuri.
**cruel** /kruːdəti/ *adj.* -katili; -kali; bila huruma; jahili; -baya; dhalimu; -korofi; habithi. **~ty** *n.* ukatili; ukorofi; udhalimu.
**cruise** /kruːz/ *v.i.* zunguka; tembea kwenye chombo kwa kujistarehesha. *n.* matembezi. **~r** *n.* **1.** manowari ya vita iendayo kasi. **2.** chombo cha baharini cha kutembelea kianasa.
**crumb** /krʌm/ *n.* chembe; chenga. **~s** makombo.
**crumble** /ˈkrʌmbl/ *v.t./i.* fikicha; finya; vurugika; geuka mavumbi; mung'unyuka; meng'enya.
**crumbly** /ˈkrʌmbli/ *adj.* tifutifu; -a kuweza kufikichika.
**crumple** /ˈkrʌmpl/ *v.t./i.* kunjakunja; kunjamana; poromoka.
**crunch** /krʌntʃ/ *v.t./i.* saga kwa meno; kutafuna kwa kelele.
**crush** /krʌʃ/ *v.t./i.* ponda; fyata; fyanda; vunja nguvu ya; angamiza; sagika; pondeka. *n.* msongano wa watu.
**crust** /krʌst/ *n.* ganda (la mkate, etc.); ukoko; koya; gaga; ukungu; utando. **earth ~**, uso wa dunia; ardhi. **~acean** *n.* kurustasia: anthropodi wa majini wenye gimba lililofunikwa kwa gamba kama vile kaa, kamba na duvi. **~y** *adj.* **1.** -enye ganda gumu. **2.** -kali; -enye ghadhabu; -enye hasira.
**crutch** *n.* mkongojo.
**cry** /kraɪ/ *v.i./t.* (**cried**) lia; tangaza; guta; lalama; omboleza; piga mayowe; toka machozi. *~ out at,* pigia kelele. *~ against,* tetea; bisha. *~ for the moon,* omba muujiza. *n.* mlio; ukelele; ukemi; ukwenzi; yowe; kigelegele; hoihoi. *in full ~,* (kwa mbwa) bweka wote pamoja katika kuwinda. *a far ~,* mbali sana; masafa marefu. *within ~ of,* karibu sana; masafa mafupi. **~ing** *adj.* -kubwa sana: *a ~ need,* haja kubwa sana.
**cryogenics** /ˌkrʌɪə(ʊ)ˈdʒɛnɪks/ *n.* tawi la sayansi ya fizikia kuhusu viwango vya chini sana vya halijoto na athari zake.
**crystal** /ˈkrɪstl/ *n.* jiwe kama kioo; fuwele. **2.** *(science)* chembe yenye mpangilio maalumu wa atomu zilizopangika katika umbo la kijometria. **~line** *adj.* -a fuwele; -enye tabia au umbo la fuwele. **~lize** *v.t./i.* fuwesha; gandisha; ganda; *(fig.)* (kwa mawazo, mashauri, etc.) dhihirisha; dhihirika. **~lization** *n.* ufuwelishaji: uundaji polepole wa fuwele kutoka kwenye miyeyuko au mimu-munyo.
**cub** /kʌb/ *n* mtoto wa mnyama wa mwitu au mbwa.
**cube** /kjuːb/ *n.* mchemraba: umbo la miraba sita iliyo sawasawa. *~ root,*

kipeuo cha tatu. **cubic** *adj.* -a mchemraba. **~unit**, kizio cha mjao. **cubism**, mtindo wa uchoraji hasa wa kutumia maumbo ya kijometria.

**cubicle** /kju:bɪkl/ *n.* kichumba kidogo.

**cucumber** /'kju:kʌmbə(r)/ *n.* tango; tangopepeta. ~ *tree,* mbirimbi.

**cuddle** /'kʌdl/ *v.t.* sogeza kifuani; kumbatia; bembeleza; beba; pakata. *v.i* kumbatiana; jikunyata; jikunja.

**cue**[1] /kju:/ *n.* ishara; kidokezi; dokezo.

**cue**[2] /kju:/ *n.* fimbo ndefu ya kuchezea biliadi.

**cuff** /kʌf/ *n. (of a coa t, etc.)* sijafu. *off the* ~, papo hapo; bila maandalizi.

**culminate** /'kʌlmɪneɪt/ *v.i.* fika upeo; kamilika; fika kikomo; isha; timia. **culmination** *n.* utimilifu; mwisho; upeo.

**culpable** /'kʌlpəbl/ *adj.* -enye hatia; mkosa; -a kupasa kuhukumiwa; -a kupasa kulaumiwa.

**culprit** /'kʌlprɪt/ *n.* mkosaji; mwenye hatia; mhalifu.

**cult** /kʌlt/ *n.* imani ya dini ya kuabudia kitu au uungu fulani, imani ambayo huleta taathira za kimawazo kwa waumini kutokana shinikizo lake; kupenda kitu sana hadi kufikia kuwa kama dini.

**cultivate** /'kʌltɪveɪt/ *v.t.* **1.** lima; panda mbegu; otesha. **2.** fanya juhudi na uangalifu mwingi katika kufanya jambo. **3.** endeleza; kuza; idilisha. ~ *a person,* jaribu kujenga urafiki na mtu. **~d** *adj.* enye malezi mema; -staarabu; -liolimwa; -enye kuelimika.

**culture** /'kʌltʃə(r)/ *n.* **1.** malezi; elimu. **2.** adabu; ustaarabu; utamaduni; uungwana. **3.** kilimo; ukulima. **~d** *adj.* -enye kuelimika; -staarabu; -a adabu; -enye malezi mazuri.

**culvert** /'kʌlvət/ *n.* kalvati; mtaro; bomba ya kupitishia maji au nyaya za umeme.

**cumulative** /'kju:mjələtɪv/ *adj.* -a kulimbikiza; -a kukusanyika kidogo kidogo.

**cunning** /'kʌnɪŋ/ *adj.* **1.** -erevu; -janja; -stadi; mahiri; hodari. *n.* werevu; ujanja; hila; ustadi.

**cup** /kʌp/ *n.* kikombe; kopo; kombe (la michezo) *v.t.* umika; piga chuku.

**cupboard** /'kʌpbəd/ *n.* kabati. ~ *love,* mapenzi njaa; mapenzi tumbo.

**cupidity** /kju:'pɪdɪti/ *n.* tamaa; uchu; uroho; ulafi; shauku (hasa ya mali).

**curd** /kɜ:d/ *n.* maziwa yaliyoganda; maziwa mabivu. **~le** *v.t./i.* gandisha; ganda; iva (maziwa).

**cure** /kjʊe(r)/ *v.t.* **1.** ponya; ponyesha: ~ *poverty,* ondelea mbali ufukara. **2.** (ng'onda) tia chumvi au dawa isioze. *n.* dawa; kuponya au kutibu.

**curable** /'kjuərəbl/ *adj.* -a kuponyeka; -a kutibika. **curative** *adj.* -a kuponya; -a dawa.

**curfew** /'kə:fju:/ *n.* kafyu; amri ya kutotembea wakati fulani; ishara ya kuzuia watu kutembea; kipindi cha kutotembea.

**curious** /'kjʊəriəs/ *adj.* **1.** -chunguzi; dadisi. **2.** -a tunu; -geni; -a ajabu. **curiosity** n. **1.** upekuzi; udadisi; upekepeke; uchunguzi. **2.** tunu; kitu kigeni; ajabu. **~ly** -*adv.* kiajabu; kwa mshangao; kiuchunguzi.

**curl** /kɜ:l/*n.* msongo wa nywele; msokoto; singa. *v.t.* sokota; pinda; kunja; suka; jinyonganyonga. *v.i.* pindana; zongomana. **~y** *adj.* -a singa. ~ *headed,* -enye nywele za kipilipili.

**currant** /'kʌrənt/ *n.* zabibu kavu ndogo zisizo na mbegu.

**currency** /'kʌrənsi/ *n.* **1.** desturi; matumizi. **2.** sarafu; fedha.

**current**[1] /'kʌrənt/ *adj.* **1.** -a desturi. **2.** -a kutumika au kutendeka sasa au siku hizi. **3.** -a kukubaliwa na wengi.

**current**[2] /'kʌrənt/ *n.* **1.** mkondo. **2.** mkondo wa nguvu za umeme. **alternating ~**, mkondogeu: mkondo wa umeme ubadilishao mwelekeo. **direct ~**, mkondo fulizo: mkondo usiobadilishabadilisha mwelekeo. **3.** mfululizo wa

mambo.

**curriculum** /kʌ'rɪkjʊləm/ *n.* mtalaa; mtaala. ~ *developer*, mkuza mitalaa. **~ vitae**, maelezo binafsi ya mtu kuhusu elimu na uzoefu katika kazi, etc.

**curry** /'kʌri/ *n.* mchuzi. ~ *powder*, bizari.

**curse** /kɜ:s/ *n.* laana; matusi; maapizo; ukuba; mateso: *Gambling is often a ~*, kamari ni chanzo cha laana. *v. t./i.* laani; tukana; apiza; tesa; jiapiza: *be ~d with continual ill health*, patwa na ugonjwa wa daima. *be ~d with idle children*, teswa na watoto wavivu. **~d** *adj.* -a kuchukiwa; -a kuchukiza; laanifu; -liolaaniwa.

**curtail** /kə:'teɪl/ *v.t.* fupisha; punguza; kata; katisha; katiza ziara au matembezi.

**curtain** /'kɜ:tn/ *n.* pazia. *draw a ~ over sth.*, acha kabisa kuzungumzia jambo fulani. *It will be ~s for you*, itakuwa mwisho wako.

**curvature** /'ke:vətʃə/ *n.* **1.** mpindo; kigosho; mpindiko. **2.** kivimbe. *radius ~*, kivimbe nusukipenyo: urefu kutoka nukta kwenye tao hadi kwenye kitovu cha mpindo.

**curve** /kɜ:v/ *n.* kizingo; tao; pindi; kigosho; ukombo. *v.i.* kunja; bina; pinda; pindika.

**cushion** /'kʊʃn/ *n.* mto; takia.

**custody** /'kʌstədi/ *n.* ulinzi; utunzaji; usimamizi; uangalizi; kifungo. *have in safe ~*, tunza vyema. **custodian** *n.* mlinzi; mtunzaji; msimamizi.

**custom** /'kʌstəm/ *n.* **1.** desturi; kawaida; mazoea; ada; mila. **2.** biashara ya kawaida. **~s** *n.* ~ *duties*, ushuru wa forodha. **~ary** *adj.* -a desturi; -a kawaida; -a mazoea. **~er** **1.** mnunuzi; mteja; mshitiri. **2.** *(colloq.)* mtu wa kuleta matata au mashaka. **~(s) house** *n.* forodha.

**cut** /kʌt/ *v.t./i.* (**cut**) **1.** kata; pasua; chonga; chenga; tema; changa; chanja; chonga nakshi. ~ *down*, punguza. ~ *off*, simamisha; zuia; katiza. ~ *out*, ondoa. *be ~ out for*, faa kwa. *He's not ~ out for that sort of work*, hafai kwa kazi ya namna ile. ~ *up*, kata vipandevipande. *be ~ up by sth.*, huzunishwa sana na jambo. ~ *dead*, -pa kisogo. ~ *a tooth*, ota jino. ~ *both ways*, (kwa maneno) faa na kutofaa wakati mmoja. ~ *a loss*, tupilia mbali biashara ya hasara kwa ya faida. ~ *and dried*, tayari yote tangu hapo. *n.* **1.** mkato. **2.** mtindo. **3.** pigo katika mchezo wa kriketi **4.** jeraha. **~ter** *n.* **1.** mkataji. **2.** chombo chembamba chenye mlingoti mmoja; dau; mashua. **~-throat** *n.* muuaji; katili. **~ting** *n.* **1.** mkato; nakshi; kitawi kipandikizi. **2.** maneno yaliyokatwa kutoka gazetini. *adj.* -kali; -a kuchukiza.

**cute** /kju:t/ *adj.* -erevu; -enye hila; -enye akili; -enye kupendeza.

**cycle** /'saɪkl/ *n.* **1.** mbembeo: mfululizo wa matukio yanayojirudiarudia ambayo mwisho wake ni sawa na mwanzo wake. **2.** duru; saiko; mzunguko; muhula mzima; mfuatano. *the ~ of the seasons of the year*, mfuatano wa miongo ya mwaka. **3.** baiskeli. *v.i.* panda baiskeli. **cyclist** *n.* mpanda baiskeli. **cyclic** *adj.* **1.** dawari; saikilia; -enye kutokeza kwa mfuatano au mzunguko. **2.** -a mzunguko.

**cyclone** /'sʌɪkləʊn/ *n.* tufani; dhoruba; kimbunga.

**cylinder** /'sɪlɪndə/ *n.* **1.** mcheduara; silinda: chombo mcheduara katika injini ambamo kanieneo ya gesi au kioevu husogeza pistoni. **2.** kitu chochote kirefu cha mviringo kama bomba.

**cytoplasm** /'sʌɪtə(ʊ)plaz(ə)m/ *n.* sitoplazimu: sehemu inayozingira kiini cha seli na kuzingirwa na kiambaza seli au kiwambaseli.

# Dd

**dad** (**dy**) /'dædi/ *n.* baba (usemi wa kitoto).
**daily** /'deɪli/ *eadj./adv.* -a kila siku; siku zote. *n.* gazeti la kila siku.
**dairy** /'deəri/ *n.* **1.** mahali patengenezwapo maziwa na bidhaa zake. **2.** duka linalouza vitu vya maziwa. **3.** kiwanda cha kusindika maziwa. ~ *farm*, shamba la ng'ombe wa maziwa.
**daisy** /'deɪzi/ *n.* aina ya ua.
**dam** /dæm/ *n.* lambo; bwawa; kuko.
**damage** /'dæmɪdʒ/*n.* **1.** hasara; uharibifu; madhara; maafa. **2.** *(law)* faini; fidia. *v.t.* haribu; vunja. *be ~d*, haribika; vunjika.
**damn** /dæm/ *v.t.* tia adhabu ya milele; laani; apiza; tukana. *a book ~ed by the critics*, kitabu kilichodharauliwa mno na wahakiki asilani. ~ *you I won't do it*, naapa sifanyi. **~able** *adj.* -a kustahili laana; -a kuchukiza mno. **~ation** *n.* laana; apizo; maapizo.
**damp** /dæmp/ *adj.* -nyevu, -a majimaji; mbichi; liyo chapachapa. *wipe a window with a ~ cloth*, pangusa dirisha kwa kitambaa kinyevu. *n.* unyevu; umajimaji. *v.t.* rowesha kidogo; fanya chapachapa; punguza furaha; punguza matumaini. ~ *down a fire*, punguza mwako wa moto. **~er** *n.* vali ya kudhibiti uingiaji wa hewa katika jiko au tanuri.
**dance** /dɑ:ns/ *v.i.* cheza ngoma. *v.t.* chezesha ngoma; muziki. *n.* ngoma; dansi.
**danger** /'deɪndʒə(r)/ *n.* hatari; janga; baa. **~ous** *adj.* -a hatari. **~ly** *adv.* kihatari.
**dare** /deə(r)/ *v.t.* thubutu; jusurisha; jaribu; -pa changamoto. *I ~ you to strike me*, huthubutu kunipiga. **~-devil** *adj./n.* jasiri mno. **daring** *n./adj.* ujasiri; jasiri.
**dark** /dɑ::k/ *n./adj.* giza; utusitusi; -eusi; -a giza. *keep sth. ~*, tunza siri. *look on the ~ side of things*, waza mambo yasiyo na furaha. *be in the ~ about sth.*, -tojua chochote juu ya mambo fulani. **~en** *v.t./i.* tia giza; kozesha; ondoa mwangaza; huzunisha. **~ness** *n.* giza.
**darling** /'dɑ:lɪŋ/ *n./adj.* mpenzi; kipenzi; muhibu; mahabubu; penzi; mwandani.
**darn** /dɑ:n/ *v.t./i.* tililia; shona. *n.* mshono wa kutililia; kiraka.
**dart** /dɑ:t/ *v.t./i.* ruka; toka, enda upesi au kwa ghafla; tokeza kwa ghafla; tupa; toa ghafla. *n.* **1.** kishale kitumiwacho kucheza dati. **2.** mruko wa ghafla.



dart

**Darwinism** *n.* nadharia ya mabadiliko ya viumbe hai kutokana na uteuzi asilia ya mwanahistoria wa maumbile Charles Darwin ya mwaka 1859.
**dash** /dæʃ/ *v.t./i.* **1.** tupa kwa nguvu; enda mbio; ruka; kurupuka. **2.** vunja; haribu. ~ *a person's hopes*, vunja matumaini ya mtu. **3.** (kwa mawimbi, etc.) pigapiga. **4.** tia kwa haraka; fanya kwa haraka. *n.* **1.** mwendo wa mbio. *make a ~ for shelter*, kimbilia pa kujificha. **2.** kishindo cha mawimbi yakipiga-piga. **3.** kidogo. *a ~ of pepper in the food*, pilipili kidogo katika chakula. **4.**. alama hii ( - ) katika maandishi. **5.** bidii; ujasiri. *cut a ~*, ponda mali.
**data** /'deɪtə/ *n.* data: taarifa au takwimu inayotumiwa katika kuamua, kufanya jambo au kuchambuliwa na kompyuta. **~ capture**, uwekaji taarifa katika hali iwezayo kuchambuliwa na kompyuta. **~ logging**, kuingiza na kurekodi data kiotomatiki kwa kompyuta. **~ processing**, ucha-mbuzi wa data kwa kompyuta ili kupata au kuratibu habari iliyokusudiwa. **~ protection**, udhibiti wa data katika kompyuta ili kuepusha matumizi haramu. **~bank** *n.* hifadhi kubwa ya data za

kompyuta. **~base** *n.* hifadhi na mpangilio wa taarifa za kompyuta zinazohusu jambo maalumu.

**date**[1] /deɪt/ *n.* **1.** tarehe. *out of ~,* -a zamani; -a kale; -enye kupitwa na wakati. *up to ~,* -a siku hizi; -a sasa; -pya; -enye kwenda na wakati. **2.** *(colloq.)* miadi; kiaga. *v.t./i.* tia tarehe.

**date**[2] /deɪt/ *n. ~ tree,* mtende; *~ fruit,* tende.

**daughter** /'dɔ:tə(r)/ *n.* binti; mtoto wa kike. *~-in-law,* mkwe (mke wa mwana).

**dawn** /dɔ:n/ *n.* **1.** mapambazuko; alfajiri. **2.** mwanzo; asili; chimbuko. *v.i.* pambazuka; -cha. *It ~ed upon me,* imeanza kunifahamikia.

**day** /deɪ/ *n.* **1.** siku; mchana; kutwa. *have one's ~,* fanikiwa kwa kipindi. **2.** wakati; muda; maisha; aushi. *all ~,* mchana kutwa. *~ by ~,* kila siku. *~ after day,* siku kwa siku. *~ after tomorrow,* keshokutwa. *~break,* mapambazuko. **~dream** *v.i. /n.* ndoto za mchana; ndoto za alinacha.

**dazzle** /dæzl/ *v.t.* fanya kiwi; shangaza; staajabisha. *- n.* kiwi; mng'ao.

**d. c.** /di: 'si:/ *n.* ufupisho wa *direct current:* mkondo fulizo: mkondo usiobadilisha mwelekeo.

**deacon** /'di:k(ə)n/ *n.* shemasi.

**dead** /ded/ *adj.* **1.** -fu; -liokufa; -kavu; dhaifu; pooza. **2.** (*be*) fariki; -fa. *the ~ hours of the night,* usiku wa manane. *come to a ~ stop,* simama kabisa. *The telephone is ~,* simu haifanyi kazi. *~ letter,* sheria, amri isiyo na nguvu; barua isiyojulikana mwenyewe. *~ heat,* sare (suluhu) katika shindano. *~ shot,* shabaha barabara. *in the ~ centre,* katikati kabisa. **~lock** *n.* hali ya kutatiza kiasi cha jambo kutoendelea. **~ly** *adj.* -a kufisha; -a mauti; -enye sumu iuayo.

**death** /deθ/ *n.* mauti; kifo; ajali; faradhi. *be at death's door,* chungulia kaburi; kuwa katika hali ya kukata roho. *~ rate,* kiwango cha watu wanaokufa mahali katika kila mia kwa muda wa mwaka mmoja.

**deaf** /def/ *adj.* ziwi; *(fig.)* -siotaka kusikiliza. *a ~ mute,* mtu aliye kiziwi na bubu pia. **~en** *v.t.* tia uziwi.

**deal**[1] /di:l/ *n.* msonobari. *~ furniture,* samani ya msonobari.

**deal**[2] /di:l/ *v.t./i.* (**dealt**) **1.** gawa; gawanya. *~ out money,* gawa pesa. *~ a blow,* piga; jaribu kupiga. **2.** fanya biashara. **3.** shughulika na. *The writer ~s with Africa,* mwandishi anayeandika habari za Afrika. **4.** tendea. *~ fairly with one's neighbours,* tendea wema majirani zako. **5.** simamia; tengeneza. *a difficult problem to ~with,* tatizo gumu kulitatua. *n.* mgao; mapatano. *a new ~,* mapatano mapya. *a square ~,* mgao wa haki. *It's a ~,* ni makubaliano. **~er** *n.* **1.** mfanyabiashara; mgawa karata. **~ings** *n.* mambo; matendo; biashara; mwenendo.

**dean** /di:n/ *n.* **1.** paroko; mkuu wa makasisi wa parokia. **2.** mkuu wa kitivo. **~ery** *n.* ofisi au nyumba ya paroko au mkuu wa kitivo.

**dear** /dɪə(r)/ *adj.* ghali; -a thamani kubwa; -penzi. *n.* mpenzi. *oh dear!, dear me!,* Mungu wangu! lahaula!

**debate** /dɪ'beɪt/ *n.* mjadala; majadiliano; mabishano; hoja; mdahalo. *v.t./i.* bishana; jadiliana; fanya mdahalo; hojiana. **debatable** *adj.* -enye kustahiki kujadiliwa.

**debit** /'debɪt/ *n.* mtoe; hesabu ya upande wa madeni wa daftari. *v.t.* andika, rajisi madeni.

**debris** /'dɛbri:, 'deɪbri/ *n.* takataka; kifusi.

**debt** *n.* deni. *be in ~,* wiwa; daiwa. *have in one's debts;* wia; dai. **~or** *n.* mdeni.

**decade** /'dɛkeɪd, dɪ'keɪd/ *n.* mwongo; kipindi cha miaka kumi.

**decadent** /'dekədənt/ *adj.* -a kupungua; kupooza; kuharibika; kuchakaa. **decadence** *n.* upungufu; uchakavu; uharibifu; upoozaji.

**decapitate** /dɪ'kapɪteɪt/ *v.t.* kata kichwa au sehemu ya juu.

**decay** /dɪ'keɪ/ *v.i.* oza; haribika; chakaa. *n.* uozaji; uharibifu; uchakavu.~ **organism**, mbunguaji: mnyama au mmea wenye uwezo wa kuvunjavunja viumbe vifu kuwa dutu sahili.
**deceive** /dɪ'sɪ:v/ *v.t.* danganya; punja; hadaa; ghilibu; rubuni; laghai. **deceit** *n.* hila; udanganyifu; uwongo; ulaghai; hadaa; ujanja; ghilba. **deceitful** *adj.* -danganyifu; mwongo; -janja. **deception** *n.* udanganyifu; hila; ghilba. **deceptive** *adj.* -danganyifu; -a hadaa.
**December** /dɪ'sembe(r)/ *n.* Disemba; mwezi wa kumi na mbili wa mwaka wa kizungu.
**decent** /'di:snt/ *adj.* -a adabu; -a heshima; -enye haya; -enye adabu; -a kufaa; -enye staha; -zuri; -a kupendeza. **decency** *n.* adabu; heshima; staha.
**decentralize** /ˌdi:'sentrəlaɪz/ *v.t.* ondoa madaraka kutoka ngazi ya juu kupeleka ngazi ya chini.
**deci-** /'desɪ-/ *prefix* sehemu ya kumi.
**decibel** /'dɛsɪbɛl/ *n.* desibeli: kizio kinachotumiwa kupimia kiwango cha sauti na elektrisiti katika mawasiliano.
**decide** /dɪsaɪd/ *v.t./i.* kata shauri; amua; azimia; kusudia. **~d** *adj.* -enye nia; thabiti; imara; -enye kudhamiria. **decision** *n.* hukumu; uamuzi; uthabiti. **decisive** *adj.* mkataa; -a kuamua.
**deciduous** /dɪ'sɪdjʊəs/ *adj.* -enye kupukutika majani au mbawa kwa majira maalumu.
**decimal** /'desɪml/ *adj.* -a kumi; -a sehemu za kumi. ~ *system*, mfumo wa kuhesabu kwa makumi.
**decipher** /dɪ'sʌɪfə/ *v.t.* fumbua maandiko ya siri au ya fumbo.
**deck** /dek/ *n.* deki; sitaha. *clear the ~s,* kaa tayari kwa vita; *(fig.)* kaa tayari kwa lolote.
**declare** /dɪ'kkleə(r)/ *v.t./i.* tangaza; arifu; julisha. **declaration** *n.* tangazo; taarifa; ilani; tamko; azimio.
**decline** /dɪ'klaɪn/ *v.t./i.* kataa; shuka; pungua; inama. *a declining birth-rate,* upungufu wa kiwango cha uzazi. *prices beginning to ~,* bei zianzazo kushuka. *an empire that has ~d,* dola iliyodhoofika. *a man's declining years,* miaka ya makamo na uzeeni mwa mtu. *n.* upungufu; uharibifu; uchakavu; mteremko; mwinamo. *fall into a ~,* pungua nguvu; ugua kifua kikuu.
**decode** /ˌdɪ:'kəʊd/ *v.t.* fasiri maandiko ya siri.
**decompose** /ˌdi:kəm'pəʊz/ *v.i.* **1.** oza; haribika. **2.** changanua; geuza. **3.** vunja; vunjika: geuza misombo kemikali kuwa katika vijenzi vyake. **decomposition** *n.* **1.** uozaji; mchanganuo. **2.** uvunjikaji: uvunjikaji wa molekuli kuwa sehemu ndogondogo.
**decorate** /'dekəreɪt/ *v.t.* pamba; remba; visha nishani; tia nakshi. **decoration** *n.* mapambo; nishani; upambaji; urembo. **decorative** *adj.* -a kupamba; -a urembo. **decorator** *n.* mpambaji.
**decrease** /dɪ'krɪ:s/ *v.i./t.* pungua; punguza; tulia; tuliza; fifia; nyamaa. *n.* upungufu; nakisi. *Crime is on the ~,* uhalifu unapungua.
**decree** /dɪ'kri/ *n.* amri; hukumu; sheria; agizo. *v.t./i.* amuru; hukumu.
**dedicate** /ˌdedɪkeit/ *v.t.* weka wakfu; andikia ukumbusho; tabaruku. **dedication** *n.* kutabaruku; uwekaji wakfu.
**deduce** /dɪ'djus:/ *v.t.* dhihirisha; hitimisha kimantiki kwa kutumia taarifa uliyopewa. **deduct** *v.t.* toa; chukua; punguza; kata; ondosha; kusuru. **deduction** *n.* **1.** upunguzaji; upungufu. **2.** dhihirisho; udhihirishaji.
**deed** /di:d/ *n.* tendo; kitendo; mkataba. *be rewarded for one's good ~s,* tunzwa kwa matendo mema. *title ~,* hatimiliki; waraka.
**deep** /di'p/ *adj.* **1.** -a kwenda chini; -enye kina kirefu au kilindi. **2.** -enye kukoza. ~ *red,* -ekundu ya kukoza. **3.** (kwa sauti) -zito; -a chini. ~ *respect,* heshima kubwa. ~ *silence,* kimya

kingi. ~ *darkness*, giza nene. ~ *thought*, fikira nyingi.~ *secret*, siri kubwa. *soldiers six* ~, askari safu sita. **~en** *v.t./i.* ongeza kina; ongezeka. **depth** *n.* kina.

**deer** /dɪə(r)/ *n.* paa; kulungu; mbawala.

**defecation** *n.* kunya: utoaji wa kinyesi.

**default** /dɪ'fɔ:lt/ *v.i.* shindwa kutekeleza jambo ulilotakiwa kufanya. *n.* ushindwaji kutekeleza jambo. *win a case by* ~, shinda kesi kwa kuwa mdai hakuhudhuria. ~ *of*, ikiwa hapana; bila. **~er** *n.* mkosaji.

**defeat** /dɪ'fi:t/ *v.t.* shinda; vunja; angamiza. *n.* ushinde; ushindwaji; upotezaji. **~ism** *n.* imani rahisi ya kushindwa tu. **~ist** *n.* mtu anayeamini kwamba atashindwa tu.

**defect** /'di:fɛkt, dɪ'fɛkt/ *n.* ila; kombo; upungufu; waa; dosari; kasoro; walakini. *~s in a system of education*, kasoro katika mfumo wa elimu. **~ion** *n.* uhalifu; kosa; uasi. **~ive** *adj.* -enye kasoro.

**defence** /dɪ'fens/ *v.t.* ulinzi; himaya; utetezi; kinga. **~less** *adj.* -dhaifu; bila ulinzi au kinga.

**defend** /dɪ'fend/ *v.t.* linda; hami; kinga; tetea. **~ant** *n.* mshtakiwa; mdaiwa. **defensible** *adj.* -a kulindwa, -a kulindika. **defensive** *adj.* -a kujilinda; -a kujitetea; -a kujihami. *be on the defensive*, jiweka tayari kwa kujilinda au kujitetea.

**defer**[1] /dɪ'fə:/ *v.t.* (**-rr-**) ahirisha; kawilisha. **~ment** *n.* uahirisho.

**defer**[2] /dɪ'fə:/ *v.i.* (**-rr-**) ridhi kwa kustahi; stahi. **~ence** *n.* kukubali; ridhaa; staha; heshima. **~ential** *adj.* -nyenyekevu; -a heshima; stahifu.

**deficient** /dɪ'fɪʃ(ə)nt/ *adj.* -pungufu; -kosefu; haba; -dogo. *He is ~ in sense*, hana akili timamu. **deficit** *n.* hasara; upungufu; nakisi, hasa ya fedha au mali.

**define** /dɪ'faɪn/ *v.t.* **1.** ainisha; fasili; fafanua. **2.** weka mpaka. ~ *a country's boundaries*, weka mipaka ya nchi. **definite** *adj.* halisi; dhahiri; wazi; bayana; **definition** *n.* **1.** maelezo; fasili; tafsiri; ufafanuzi. **2.** udhahiri wa umbo au taswira. **definitive** *adj.* -a mkataa; -a hakika; tama.

**deflate** /dɪ'fleɪt/ *v.i.* **1.** punguza upepo; punguza pumzi. **2.** punguza jumla ya fedha itumiwayo katika nchi kudhibiti mfumuko wa bei ili kupandisha thamani yake.

**deflect** /dɪ'flekt/ *v.t./i.* ~ *from*, vuta upande; potosha; geuza uwelekeo; kengeusha; enda upande; potoka; geuka; kengeuka. **~ion** *n.* mkengeuko; mkengeuo; mgeuko.

**deforest** /dɪ:'fɒrɪst/ *v.t.* fyeka; tema; haribu misitu. **~ation** *n.* uharibifu, ufyekaji misitu.

**deform** /dɪ'fɔ:m/ *v.t.* umbua; lemaza; haribu; kashifu. **~ation** *n.* uumbuaji; kashfa; ulemavu. **~ed** *adj.* -lemavu; -enye kuumbuka; kombo. **~ity** *n.* kilema; kombo.

**defraud** /dɪ'frɔ:d/ *v.t.* danganya; punja; nyang'anya; ghilibu kiuhalifu.

**defy** /dɪ'faɪ/ *v.t.* **1.** taka shari; taka vita. **2.** kataa katakata. **3.** dharau; asi. **4.** chokoza; tolea ujuvi. *I ~ you to prove I have cheated*, natoa changamoto mthibitishe kama nimedanganya. **defiance** *n.* ukaidi; changamoto; wito wa shari au vita. *in defiance of orders*, bila kujali amri. **defiant** *adj.* -a kutaka vita au shari; -dharaulifu.

**degenerate** /dɪˌdʒenəreɪt/ *v.i.* haribika tabia; pungua; dhoofika. *adj.* -liyoharibika; -liyodhoofika; -liyopunguka. **degeneration** *n.* uharibifu wa tabia; udhaifu; upungufu; upotovu.

**degradable** /dɪ'greɪdəbl/ *adj.* -enye kuweza kuvunjwavunjwa kwa njia za kikemikali au kibiolojia.

**degree** /dɪ'gri/ *n.* **1.** kipeo; uzi; digirii. **2.** cheo; daraja; kiwango. **3.** shahada. **4.** kadiri; kiasi. *by degrees*, kidogo kidogo.

**dehydrate** /di:'hʌɪdreɪt/ *v.t.* nyevua; kutoa maji; kupoteza maji kutoka mwilini. **dehydration** *n.* mpweo:

upotevu wa maji mwilini.

**deify** /ˈdeɪɪfʌɪ, ˈdi:ɪ-/ *v.t.* fanya Mungu; abudia au heshimu kama Mungu.

**dejected** /dɪˈdʒektɪd/ *adj.* -enye huzuni; -enye kuvunjika moyo; -enye majonzi. **dejection** *n.* huzuni; masikitiko; majonzi.

**delay** /dɪˈleɪ/ *v.t./i.* kawilisha; kawia; chelewesha; chelewa; ahirisha; ahirika; taahari. *n.* ukawiaji; taahira.

**delegate** /ˈdelɪgət/ *v.t.* wakilisha; tuma; agiza. *n.* wakili; mjumbe; kaimu; makamu; wakala. **delegation** *n.* uwakilishi; wakala; mjumbe; ujumbe.

**delete** /dɪˈli:t/ *v.t.* futa; ondoa; dondosha. **deletion** *n.* kufuta; udondoshaji: utoaji wa kipashio kutoka mfumo maalumu wa lugha. **deletion transformation**, ugeuza-maumbo dondoshi.

**deliberate** /dɪˈlɪbərət/ *v.t./i.* fikiri; pima; waza; shauriana. *adj.* **1.** -a kusudi. **2.** -a hadhari; bila haraka. **~ly** *adv.* kwa uangalifu; makusudi; taratibu.

**deliberation** /dɪˌlɪbəɪreɪʃn/ *n.* fikira; uamuzi; azimio; shauri.

**delicate** /ˈdelɪkət/ *adj.* **1.** ororo. *as ~ as silk*, -ororo kama hariri. **2.** -epesi kuvunjika, kuugua; dhaifu. *~ cups*, vikombe vyepesi kuvunjika. *a ~ looking child*, mtoto dhaifu. *a ~ matter*, jambo gumu kuamua. **3.** -enye adabu. **4.** (kwa chakula) -tamu. **delicacy** *n.* chakula kitamu; uangalifu; malezi mema. **delicious** *adj.* -a kupendeza sana; -a kufurahisha sana; tamu; -zuri.

**delight** /dɪˈlaɪt/ *v.t./i.* pendeza sana; penda sana; furahi; penda. *n.* furaha; anasa. **~ed** *adj.* -enye furaha. **~ful** *adj.* -a kufurahisha sana; zuri sana.

**delinquent** /dɪˈlɪŋkw(ə)nt/ *n./adj.* -kosaji; mtundu; nunda; mwenye hatia. **delinquency** *n.* kosa; hatia; utundu; utukutu.

**delirium** /dɪˈlɪrɪəm/ *n.* upayukaji; wazimu; uwewesekaji; upagawaji; uchagawaji. **delirious** *adj.* -enye kupayukapayuka; kuweweseka; kupagawa au kuchagawa.

**deliver** /dɪˈlɪvə(r)/ *v.t.* peleka; okoa; fanya huru; toa. *~ a speech*, toa hotuba. *be ~ed of a child*, jifungua; zaa. **~ance** *n.* wokovu; uhuru; ukombozi; uzazi. **~y** *n.* upelekaji; uhutubiaji; uzaaji.

**delta** /ˈdeltə/ *n.* mahali mto unapojigawa sehemu mbili au zaidi kabla ya kuingia baharini au ziwani. **arcuate ~**, deltao: delta yenye umbo la nusu au robo duara. **digitate ~**, delta ambayo mto hufanya matawi kabla ya kuingia baharini au ziwani.

**deluge** /ˈdɛlju:dʒ/ *n.* gharika; mafuriko ya maji; mvua kubwa sana. *v.t.* gharikisha.

**demagnetize** *v.t.* sumakua: haribu sumaku katika gimba.

**demand** /dɪˈmɑ:nd/ *v.t.* taka; omba; hitaji; uliza. *n.* haja; matakwa; swali. *on ~*, itakapohitajika. *a great ~ for good clerks*, kuna mahitaji makubwa ya makarani hodari.

**democracy** /dɪˈmɒkrəsi/ *n.* **1.** demokrasia: mfumo wa uongozi unaowashirikisha wananchi wote katika maamuzi ya utawala kwa kupitia wawakilishi wao. **2.** wananchi waimarishao mfumo wa demokrasia. **democrat** *n.* mfuasi wa demokrasia. **democratic** *adj.* -a demokrasia; -enye kuunga mkono demokrasia; -a kidemokrasia.

**demolish** /dɪˈmɒlɪʃ/ *v.t.* bomoa; vunja; haribu. **demolition** *n.* ubomoaji; uharibifu; uvunjaji.

**demon** /ˈdɪ:mən/ *n.* pepo; shetani; jini; mtu katili.

**demonstrate** /ˈdemənstreit/ *v.t./i.* **1.** fafanua; dhihirisha; thibitisha; onyesha. **2.** andamana. **demonstration** *n.* uthibitisho; ufafanuzi; onesho; maandamano; ushahidi. **demonstrative** *adj.* -a kuonyesha; -a kuthibitisha. **demonstrator** *n.* mtu afundishaye kwa vielelezo; mwandamanaji.

**demoralize** /dɪˈmɒrəlaɪz/ *v.t.* potosha; potoa; vunja moyo.

**demoralization** /dɪˌmɒrəlaɪ'zeɪʃn/ *n.* upotofu; uvunjikaji moyo.

**den** /den/ *n.* **1.** shimo la mnyama wa mwitu; pango. **2.** pakutanapo waovu. **3.** *(colloq.)* chumba cha faragha cha kazi au starehe.

**denitrifying bacteria** *n.* mnai trishuaji: bakteria mwenye uwezo wa kugeuza chumvi za naitreti na amonia kuwa gesi ya nitrojeni.

**denomination** /dɪˌnɒmɪ'neiʃn/ *n.* aina; namna; jinsi; jina; madhehebu.

**denominator** /dɪ'nɒmɪneɪtə(r)/ *n.* kigawanyo; asili.

**denote** /dɪ'nəʊt/ *v.t.* maanisha; onyesha; wa ishara ya; -wa jina la; -wa dalili ya. **denotation** *n.* jina; alama; maana.

**denounce** /dɪ'naʊns/ *v.t.* shtaki; suta; shutumu; laumu; tangaza kusudio la kuvunja mkataba au mapatano. **denunciation** *n.* shutuma; lawama; mashtaka; usutaji.

**dense** /dens/ *adj.* -nene; -zito; -liosongamana; -ingi. **density** *n.* densiti; uzito; msongamano: **1.** kiasi cha masi katika kizio kimoja cha ujazo wa dutu. **relative ~**, uzito husaniafu: uwiano kati ya masi ya mata katika ujazo fulani na masi ya maji yenye ujazo sawa. **2.** kiasi cha tabiaumbile katika kizio kimoja cha urefu, eneo, au ujazo.

**dent** /dent/ *n.* kishimo; kibonyeo. *v.t./i.* bonyeza; bonyea.

**dental** /'dentl/ *adj.* -a meno. **dentifrice** *n.* dawa ya kusugulia meno. **dentist** *n.* daktari wa meno.

**dentition** /dɛn'tɪʃ(ə)n/ *n.* mpango wa meno; mkato wa meno. **denture** *n.* meno bandia.

**deny** /dɪ'nʌɪ/ *v.t.* kana; kanisha; kataa; kataza; kaidi; nyima; hini. **denial** *n.* ukanaji; unyimaji; katazo.

**deoxygenated blood** *n.* damu isiyo na oksijeni ambayo rangi yake ni nyekundu isiyokoza.

**depart** /dɪ'pɑ:t/ *v.i. (from)* ondoka; toka; enda; safiri; fariki; kengeuka; acha. *~ from old customs,* acha mila za zamani. **~ure** *n.* kuondoka; kuacha; safari. *a new ~,* mwelekeo; mtazamo mpya.

**department** /dɪ'pɑ:tmənt/ *n.* idara; sehemu.

**depend** /dɪ'pend/ *v.i.* tegemea. *The old man still ~s on his own earnings,* mzee bado anategemea mapato yake mwenyewe. *Good health ~s on balanced diet,* afya njema hutegemea lishe bora. **2.** amini. *You can always ~ on him,* waweza kumtegemea siku zote. **~able** *adj.* -a kutumainika; tumainifu. **~ant** *n.* anayetegemea mwingine. **~ance** *n.* utegemezi. **~ency** *n.* koloni. **~ent** *adj.* -a kufuatana na; -a kutegemea; -a kutumaini.

**deplete** *v.t* punguza idadi; tumia na kumaliza; fanya -tupu.

**deplore** /dɪ'plɔ:/ *v.t.* sikitikia; jutia; lilia. **deplorable** *adj.* -a kusikitisha; -a kuhuzunisha; -baya.

**depopulate** /ˌdi:pɒpjuleɪt/ *v.t.* punguza idadi ya watu. *AIDS ~s the world,* ukimwi unapunguza idadi ya watu ulimwenguni. **depopulation** *n.* upungufu wa watu.

**deport** /dɪ'pɔ:t/ *v.t.* hamisha; fukuza; ondoa katika nchi. **~ation** *n.* kufukuza au kufukuzwa nchini. *oneself,* jiweka. *~ oneself with dignity,* jiweka kwa heshima. **~ment** *n.* mwenendo, tabia; kikao.

**deposit** /dɪ'pɒzit/ *v.t.* weka; toa; salimisha; acha mashapo au tope. *The river ~s mud on the fields in the rainy season,* mto huacha matope katika mashamba siku za mvua. *n.* amana; rubuni; akiba; rehani; mashapo. **~or** *n.* mwekaji akiba benki. **~ory** *n.* ghala; bohari.

**depot** /'dɛpəʊ/ *n.* ghala; depo; bohari.

**depreciate** /dɪ'pri:ʃɪeɪt/ *v.t./i.* punguza, punguka, thamani; rahisisha.

**depreciation** /dɪˌpri:ʃi'eiʃn/ *n.* upungufu wa thamani ya kitu.

**depress** /dɪ'pres/ *v.t.* inamisha; shusha; huzunisha; punguza nguvu; dhoofisha; sikitisha. **~ing** *adj.* a kuhuzunisha. **~ion** *n.* huzuni; unyovu; bonde; shimo; mwinamo.

**deprive** /dɪ'prʊɪv/ *v.t.* nyima. **deprivation** *n.* unyimaji.
**depute** /dɪ'pju:t/ *v.t.* tuma; wakilisha; agiza; weka naibu; weka makamu. **deputy** *n.* wakala; naibu; kaimu; makamu. **deputation** *n.* ujumbe. **deputize** *v.i.* fanya kwa niaba; kaimu.
**derelict** /'derəlɪkt/ *adj.* -lioachwa; -liotupwa; pangupakavu.
**derive** /dɪ'rʌɪv/ *v.t./i.* pata kutokana na; tokana na; chimbuka; nyambua; nyambulisha. **derivation** *n.* asili; mwanzo; chimbuko;unyambulishaji; unyambuaji. **derivative** *adj./n.* zalika; kinyambuo; mnyambuo; kitu au neno lililotoka katika lingine; kitokanacho na.
**dermis** /'də:mɪs/ *n.* tabakandani: tabaka ya ndani ya ngozi.
**derogatory** /dɪ'rɒgət(ə)ri/ *adj.* a kuvunja heshima; -a kuaibisha; -a dharau.
**desalination** /ˌdɪ:sælɪ'neiʃn/ *n.* utochumvishi: utoaji chumvi katika maji bahari ili yaweze kutumika kama ya kawaida.
**descend** /dɪ'send/ *v.i./t.* shuka; teremka; inama; zaliwa. *be ~ ed from,* tokana na ukoo fulani. *His bravery ~s from his father,* ushujaa wake ameurithi kwa baba yake. *~ upon,* angukia; shambulia; vamia. **~ant** *n.* mtoto; uzao; dhuria. **descent** *n.* **1.** mshuko; mteremko; mwinamo; nasaba; ukoo; uzao; jadi. **2.** uvamizi; shambulio la ghafula.
**describe** /dɪ'skraɪb/ *v.t.* eleza; eleza wasifu; fafanua; hadithia. **description** *n.* maelezo; wasifu; habari. *(colloq.)* namna. *of any description,* -a namna yoyote. **descriptive** *adj.* -a kueleza; -a kuainisha.
**desert**[1] /dɪ'zə:t/ *v.t./i.* acha; toroka; kimbia; tupa; hama; telekeza. *a ~ed person,* mkiwa. *a ~ed village,* mahame.
**desert**[2] /'dɛzət/ *n.* jangwa.
**desert**[3] /dɪ'zə:t/ *n.* haki; stahili; rada. *get one's ~s,* pata stahili yake.
**deserve** /dɪ'zɜ:v/ *v.t.* stahili. **deserving** *adj.* -a kustahili. **~dly** *adv.* kwa haki; kama ilivyostahili.
**design** /dɪ'zain/ *n.* dizaini; kielelezo; picha; mpango; kusudi; mradi; nia; hila; mtego. *have ~s on,* -wa na kusudio baya juu ya. *v.t./i.* buni; vumbua; tunga; sanii; kusudia. **~edly** *adv.* makusudi. **~er** *n.* mtungaji; -enye kubuni. **~ing** *adj.* -erevu; - janja; -a hila.
**designate** /'dɛzɪgneɪt/ *v.t.* onyesha; taja; agiza; chagua; teua; -wa na maana fulani; -wa dalili ya. *~ boundaries,* onyesha mipaka. *He ~d me as his successor,* aliniteua niwe mrithi wake.
**designation** /ˌdezɪg'neiʃn/ *n.* maana; jina; maelezo; uteuzi; cheo.
**desire** /dɪ'zaɪə(r)/ *n.* tamaa; shauku; haja; uchu; hamu; matakwa; utashi; mapenzi; matilaba; ashiki. *v.t.* taka; tamani; ashiki; omba. *I ~d him to sit down,* nilimuomba aketi. **desirable** *adj.* -a kupendeza; -a kutamanika. **desirous** *adj* -enye kutaka; -enye kutamani.
**desk** /desk/ *n.* meza ya kuandikia; dawati; deski.
**desolate** /'dɛs(ə)lət/ *adj.* -liyoachwa; -a jangwa; -liyoachwa; -siyostahili kukalika; -a ukiwa; -a huzuni; -a upweke. *v.t.* huzunisha; tia majonzi. **desolation** *n.* ukiwa; majonzi; huzuni.
**despair** /dɪ'speə(r)/ *v.i./n.* kata tamaa; -fa moyo; vunjika moyo; tokwa na matumaini; kukata tamaa; kufa moyo. **desperate** *adj.* -enye kukata tamaa; bila tumaini; tayari kufanya lolote; -sioponyeka; -baya mno. **desperation** *n.* hali ya kukata tamaa.
**desperado** /ˌdɛspə'ra:dəʊ/ *n.* katili; tayari kufanya lolote; jasiri.
**despise** /dɪ'spʌɪz/ *v.t.* tweza; dharau. **despicable** *n.* -a kustahili kudharauliwa; nyonge; dhaifu.
**despite** /dɪ'spʌɪt/ *prep.* ijapokuwa. *in ~ of his wishes,* ijapokuwa hataki.
**despond** /dɪ'spɒnd/ *v.i.* kata tamaa; -fa moyo. **~ency** *n.* hali ya kukata

tamaa; kufa moyo majonzi. **~ent** *adj.* -a kukata tamaa; bila tumaini.

**despot** /ˈdɛspɒt/ *n.* dikteta; dhalimu; mtawala mwenye madaraka yote peke yake. **~ic** *adj.* -enye madaraka peke yake. **~ism** *n.* udikteta; udhalimu.

**destination** /ˌdestɪˈneiʃn/ *n.* mahali mtu (au kitu) anapopelekwa, au akusudiapo kufika.

**destined** /ˌdestɪnd/ *v.t.* -liokusudiwa kuwa; jaalia. *He is ~ for the army,* anakusudiwa kuwa askari. **destiny** *n.* majaaliwa; jaala; bahati.

**destitute** /ˈdɛstɪtju:t/ *adj.* fukara; maskini; mkata. *~ of,* bila ya. **destitution** *n.* ufakiri; ufukara; umaskini; uhitaji; ukiwa.

**destroy** /dɪˈstrɔɪ/ *v.t.* haribu; vunja; angamiza. **~er** *n.* mharibifu; mwangamizaji; manowari yenye mizinga. **destruction** *n.* uharibifu; maangamizi; mauaji. **destructive** *adj.* -enye kuharibu; -haribifu.

**detach** /dɪtætʃ/ *v.i.* tenga; bandua; peleka kikosi cha askari kutoka jeshi kubwa. **~ed** *adj.* -adilifu; -siopendelea. **~able** *adj.* -adilifu; -siopendelea. **~ment** *n.* utengaji; mbanduko;. uadilifu; kikosi maalumu; upweke.

**detail** /ˌdɪteɪl/ *n.* kila kitu; habari zote. *v.t.* eleza kinaganaga; tuma kufanya kazi maalumu.

**detain** /dɪˈteɪn/ *v.t.* kawilisha; zuia; tia ndani; weka kizuizini; funga. **detention** *n.* kifungo; mahabusu; uzuwiaji.

**detect** /dɪˈtekt/ *v.t.* gundua; ona; peleleza. **~ion** *n.* ugunduzi; upelelezi. **~ive** *n.* mpelelezi; askari kanzu; jasusi; kachero.

**deter** /dɪˈtɜ:/ *v.t.* (**-rr-**) kataza; zuia; viza. **~rent** *n./ adj.* kizuizi; -a kuzuia; -enye kuviza.

**detergent** /dɪˈtɜ:dʒənt/ *n.* ditajenti; sabuni ya unga; dawa ya maji ya kusafishia.

**deteriorate** /dɪˈtɪərɪəreɪt/ *v.t./i.* punguza thamani; pungua thamani; haribika; chakaa; fifia. **deterioration** *n.* uchakavu; uharibikaji.

**determine** /dɪˈtɜ:mɪn/ *v.t./i.* **1.** weka mpaka. *The supply of food ~s the size of the army,* ugavi wa chakula hubainisha ukubwa wa jeshi. **2.** weka; kusudia; amua; kata maneno; maliza. **3.** yakinisha. *~ the meaning of a word,* ainisha maana ya neno. **~d** *adj.* imara; thabiti. **determination** *n.* kusudi; nia; bidii; shauri; uthabiti; ushupavu.

**detest** /dɪˈtest/ *v.t.* chukia sana; kirihi. **~able** *adj.* -a kuchukiza; makuruhi. **detestation** *n.* karaha.

**detonate** /ˈdɛtəneɪt/ *v.t./i.* ripua; ripuka. **detonation** /ˌdetəˈneɪʃn/ *n.* mripuko; uripukaji; uripuaji.

**detour** /ˈdɪ:tʊə(r)/ *n.* njia ya kuzunguka; mzunguko. *make a ~,* zunguka.

**detract** /dɪˈtrækt/ *v.i.* punguza sifa au thamani ya; toa; dunisha; umbua. **~ion** *n.* udunishaji; usingiziaji.

**detriment** /ˈdɛtrɪm(ə)nt/ *n.* hasara; dhara. **~al** *adj.* enye kutia hasara; -enye kudhuru.

**deuterium** /dju:ˈtɪərɪəm/ *n.* duteri: isotopu ya hidrojeni yenye namba ya masi mara mbili zaidi.

**devastate** /ˈdɛvəsteɪt/ *v.t.* haribu; teketeza.

**devastation** /ˌdevəˈsteɪʃn/ *n.* uharibifu; uteketeaji.

**develop** /dɪˈveləp/ *v.t./i.* kuza; endeleza; sitawisha; kua; fafanua; eleza. *~ a film,* safisha picha. **~ment** *n.* ukuzaji; ukuaji; maendeleo; usitawi. *community development,* usitawi wa jamii. *development studies,* taaluma ya maendeleo.

**deviate** /ˈdi:vɪeɪt/ *v.i.* enda upande; potoka; kengeuka; chepuka; hitilafiana. **deviation** *n.* mwachano; mkengeuko; upotovu.

**device** /dɪˈvaɪs/ *n.* **1.** hila; mbinu; mpango. *leave sb. to his own ~s,* mwache afanye apendavyo. **2.** chombo; ala; zana; kitu; nyenzo. **3.** chapa; alama; picha.

**devil** /ˈdevl/ *n.* shetani; bilisi. *a poor ~,* maskini; fukara. **~ish** *adj.* kama shetani; -baya mno; -katili; -ovu sana.

**devious** /ˈdi:vɪəs/ *adj.* -enye kuzunguka;

-a chinichini; - janja.

**devise** /dɪ'vʌɪz/ *v.t.* fanya; vumbua; tunga; buni; zaa, waza shauri au hila. ~ *to,* rithisha; usia.

**devoid** /dɪ'vɔɪd/ *adj.* bila; pasipo. *He is ~ of sense,* hana akili.

**devolve** /dɪ'vɒlv/ *v.t./i.* kabidhi; hamishia; wakilisha. *When the boss is ill, work ~s upon me,* bosi akiumwa, kazi huwa juu yangu.

**devote** /dɪ'vəʊt/ *v.t.* tenga. ~ *oneself,* jibidiisha. **~d** *adj.* -a kupenda sana; -enye bidii; -aminifu. *be devoted to,* jibidiisha. **~e** *n.* mshabiki; walii; sufii; mtawa. **devout** *adj.* -enye kumcha Mungu.

**dew** /dju:/ *n.* umande: unyevu unaotokea juu ya majani au vitu vyengine kutokana na hali joto kushuka sana. ~ *point,* kiwango umande: kiwango cha halijoto ambapo mvuke wa maji hewani hugeuka kuwa matone.


dhow

**dhow** *n.* jahazi.

**diabetes** /ˌdʌɪə'bi:ti:z/ *n.* kisukari: ugonjwa unaosababishwa na upungufu wa homoni ya insulini ambayo hurekebisha sukari itumiwe kupata nishati mwilini.

**diagnose** /'dʌɪəgnəʊz/ *v.t.* baini, tambua ugonjwa kwa dalili zilizopo. **diagnosis** *n.* uchunguzi yakinifu wa jambo.

**diagonal** /dʌɪ'ag(ə)n(ə)l/ *adj.* ulalo; -a kutoka pembe mpaka pembe mkabala; -a mshazari. *n.* mstari wa kukata mraba pembe kwa pembe; mshazari; hanamu.


diagonal

**diagram** /'dʌɪəgram/ *n.* picha inayoonyesha kiolwa kilivyo; mfano; kielelezo; kiolezo.

**dial** /'daɪəl/ *n.* uso wa saa; chombo cha simu chenye nambari juu yake. *v.t./i.* piga simu.

**dialect** /'dʌɪəlɛkt/ *n.* lahaja. *the ~ of Zanzibar,* Kiunguja. *the ~ of Mombasa,* Kimvita.

**dialogue** /'daɪəlɒg/ *n.* mazungumzo; mashauriano.

**diameter** /dʌɪ'amɪtə/ *n.* kipenyo; mstari ulionyooka upitao katikati ya duara. **diametrically** *adv.* kabisa; halisi. *be ~ opposed,* kabiliana kabisa; -wa kinyume kabisa.


diamond

**diamond** /'daɪəmənd/ *n.* almasi. ~ *wedding,* ndoa iliyodumu kwa miaka sitini au sabini na tano.

**diaphragm** /'dʌɪəfram/ *n.* kiwambotao: utando unaogawa kifua na fumbatio; kiwambo.

**diarrhoea** /ˌdʌɪə'rɪə/ *n.* tumbo la kuendesha, la kuhara.

**diary** /'daɪəri/ *n.* shajara; kitabu cha kumbukumbu za kila siku.

**diatom** /'dʌɪətəm/ *n.* diatomu: mwani wa selimoja anayeonekana kwa hadubini na huwa na kuta seli za silika. **~ic gas**, gesi yenye atomu mbili kwenye molekuli moja, kama gesi ya hidrojeni.

**dictate** /dɪk'teɪt/ *v.t.* toa imla; amuru; agiza.

**dictation** /dɪk'teiʃn/ *n.* imla; agizo; amri. **dictator** *n.* dikteta; mtawala wa mabavu, wa kiimla.

**diction** /'dɪkʃn/ *n.* ufasaha: uteuzi na matumizi sahihi ya maneno katika mawasiliano.

**dictionary** /'dɪkʃənri/ *n.* kamusi: kitabu cha orodha ya maneno yaliyopangwa na maana zake.


dice

**die**[1] /'daɪ/ *v.i.* fa; fariki; kata roho.

**die**[2] /'daɪ/ *n.* (**dice**) dadu.

**die**[3] /'daɪ/ *n.* (**dies**) zana za kuchorea na kupigia chapa sarafu.

**diet** /'daɪət/ *n.* chakula; ulaji; maakuli; lishe kamili.

**differ** /'dɪfə(r)/ *v.i.* hitilafiana; tofautiana; achana. **~ence** *n.* hitilafu; tofauti. ~ *of opinion,* tofauti ya maoni. **~ent** *adj.* mbalimbali; -ingine; tofauti. **~entiate** *v.t./i.* pambanua; ainisha; hitilafiana; tofautisha; achana; tengua.

**differential** /ˌdɪfə'rɛnʃ(ə)l/ *n.* difu;

difrensha; tenguo. ~ *cage*, wigo difu. ~ *coefficient*, kizigeu tenguo. ~ *equation*, mlinganyo tenguo. ~ *gear*, gia difu.

**difficult** /'dɪfikəlt/ *adj.* -gumu; -zito; -a shida. *n.* shida. **~y** *n.* shida; matatizo; dhiki; ugumu. *difficulty index*, faharasa ngumu.

**diffidence** /'dɪfidəns/ *n.* haya; woga; wasiwasi.

**diffident** /'dɪfidənt/ *adj.* -oga; -enye haya; -siojiamini.

**diffuse** /dɪ'fju:z/ *v.t./i.* eneza; tawanya; enea; tawanyika; toa; zagaa; sambaa. *adj.* -a maneno mengi; enye kuzagaa. **diffusion** *n.* mweneo. *diffusion coefficient*, kizigeu cha mweneo. *diffusion equation*, mlinganyo wa mweneo.

**dig** /'dɪg/ *v.t./i.* (**dug**) lima; chimbua; chimba; fukua. **~ging** *n.* ulimaji; uchimbaji.

**digest** /dʌɪ'dʒɛst, dɪ-/ *v.t./i.* saga chakula kwa kutumia kimeng'enya maalumu ndani ya tumbo; yeyuka. **~ion** *n.* mmeng'enyo; umeng'enyaji.

**digital** /'dɪdʒtl/ *n.* dijitali: taarifa iliyohifadhiwa kwa mfululizo wa tarakimu.

**dignify** /'dɪgnɪfaɪ/ *v.t.* tukuza; heshimu; adhimisha.

**dignified** /'dɪgnɪfaɪd/ *adj.* -a heshima; adhimu.

**dignitary** /'dɪgnɪt(ə)ri/ *n.* mheshimiwa; mwadhamu.

**dignity** /'dɪgnəti/ *n.* heshima; adhama; daraja; cheo.

**digress** /dʌɪ'grɛs/ *v.i.* toka nje ya mada. **~ion** *n.* mzunguko; uachaji; utokaji nje ya mada.

**dilapidated** /dɪlæpɪdeɪtɪd/ *adj.* -bovu; gofu.

**dilate** /dʌɪ'leɪt/ *v.t./i.* tanua; panua; vimbisha; tanuka; panuka; vimba. ~ *upon a subject*, sema maneno mengi juu ya jambo. **dilation** *n.* mpanuko; mtanuo; mpanuo; mtanuko.

**dilatory** /'dɪlət(ə)ri/ *adj.* -vivu; zembe; -enye kuchelewesha.

**dilemma** /dɪ'lɛmə, dʌɪ/ *n.* hali ambayo inabidi kutoa uamuzi mmoja kutoka kwenye fursa ya kuchagua kati ya mambo kadhaa; tatizo; hali ngumu. *You are on the horns of a ~*, uko katika hali ngumu sana.

**diligent** /'dɪlɪdʒənt/ *adj.* -enye bidii; -tendaji; -angalifu; -enye juhudi. **~ly** *adv.* kwa juhudi; kwa uangalifu; kwa bidii. **diligence** *n.* bidii; juhudi; uangalifu; jitihada.

**dilute** /dʌɪ'l(j)u:t, dɪ-/ *v.t.* zimua: punguza ukolevu; ghushi; punguza nguvu. *adj.* zimulifu: -enye kufanya hafifu kutokana na kuongezwa dutu chapwa. **dilution** *n.* uzimuaji.

**dim** /'dɪm/ *v.t./i.* tia giza; ingia giza; fifia. *adj.* -a giza kidogo; siyoonekana vizuri; -siyosikilikana vizuri; -siyofahamika vizuri akilini; si dhahiri; -liyofifia. *His eyes are ~*, macho yake yana giza. **~ness** *n.* giza; utusitusi.

**dimension** /dɪ'mɛnʃ(ə)n, dʌɪ-/ *n.* kipimo: kiasi cha urefu, upana, au kina.

**diminish** /dɪ'mɪnɪʃ/ *v.t./i.* punguza; pungua; punguka.

**dimunition** /ˌdɪmɪ'nju:ʃ(ə)n/ *n.* upungufu; upunguzaji.

**din** /dɪn/ *n.* mshindo; kelele; ghasia. *v.t./i.* fanya kelele au ghasia mfululizo.


dinosaur

**dinosaur** *n.* mnyama aliyeishi miaka milioni nyingi zilizopita.

**dine** /daɪn/ *v.t./i.* -la chamchana au chajio; karibisha kwenye chakula cha mchana. *dining-room*, chumba cha kulia. **dinner** *n.* chamchana au chajio.

**ding-dong** /'dɪŋ dɒŋ/ *n.*mlio wa kengele au uliofanana nao; mpumbavu.

**dinghy** /'dɪŋgɪ, 'dɪŋi/ *n.* mashua ndogo; kihori.

**dingy** /'dɪn(d)ʒi/ *adj.* -chafu; liyofifia; -eusi; -enye gizagiza.

**diocese** /'dʌɪəsɪs/ *n.* dayosisi; jimbo la askofu. **diocesan** *adj./n.* -a jimbo la askofu; askofu.

**diode** /'dʌɪəʊd/ *n.* diodi: kifaa cha elektroniki kinachopitisha umeme

kwa urahisi aghlabu kuelekea upande mmoja tu.

**dioxide** /dʌɪ'ɒksʌɪd/ *n.* dioksidi: oksidi yenye atomu mbili za oksijeni kwa kila molekuli, zote mbili zikiwa zimebabadika kwenye atomi ya elementi nyingine.

**dip** /dɪp/ *v.t./i.* chovya; zamisha; ogesha; inama; *n.* uchovyaji; uzamaji; josho; mwinamo.

**diphtheria** /dɪp'θɪərɪə, dɪf-/ *n.* dondakoo: ugonjwa wa koo wa kuambukiza unaosababishwa na bakteria na pia huleta homa na shida ya kupumua.

**diphthong** /'dɪfθɒŋ/ *n.* irabuunganifu: irabu, vokali mbili zinazotamkwa kama kwamba ni moja tu.

**diploma** /dɪ'pləʊmə/ *n.* diploma; stashahada.

**diplomacy** /dɪ'pləʊməsi/ *n.* diplomasia; upatanishi; usuluhishi; busara; hekima. **diplomat** *n.* mwanadiplomasia; balozi; mtaalamu wa mambo ya uhusiano.

**diplomatic** /ˌdɪplə'mætɪk/ *adj.* -a kidiplomasia. ~ *corps,* maofisa wa ubalozi katika nchi. ~ *immunity,* kinga ya kidiplomasia. ~ *relations,* uhusiano wa kibalozi.

**direct** /dɪ'rɛkt, dʌɪ-/ *v.t.* ongoza; elekeza; simamia; amuru; agiza. ~ *attention to,* angalia; tazama; onyesha. *adj.* -nyofu; sawasawa; halisi. **~ current**, mkondo fulizo: mtiririko mfululizo wa elektroni kwenye kipitishio wenye uwelekeo wa upande mmoja. **~ion** *n.* majira; upande; welekeo; agizo; amri; elekezo; uongozi; usimamizi; maelezo. **~ly** *adv.* moja kwa moja; waziwazi; mara moja; sasa hivi. **~or** *n.* mkurugenzi; mwongozaji; msimamizi; mkuu. *board of directors,* bodi ya wakurugenzi. **~ory** *n.* kitabu chenye orodha na taarifa za watu au taasisi fulani. *telephone directory,* kitabu cha orodha ya simu.

**dirt** /dɜ:t/ *n.* uchafu; taka. *cheap as ~,* rahisi mno. **~y** *adj.* -chafu.

**dis-** /dɪs/ *prefix* kiambishi awali chenye maana ya 'si' au chenye kuligeuza neno kuwa kinyume chake.

**disable** /dɪs'eɪbl/ *v.t.* lemaza; ondolea nguvu; dhoofisha; vunja. **~d** *adj.* -lemavu. **disability** *n.* udhaifu; ulemavu; kilema.

**disaffected** /dɪse'fektid/ *adj.* -enye chuki; -a kutaka maasi; - enye uadui. **disaffection** *n.* chuki; uchungu.

**disagree** /dɪsə'gri:/ *v.i.* gombana; tetana; bishana; -topatana. *This food ~s with me,* chakula hiki kinanidhuru. **~able** *adj.* -chungu; -gumu; -enye chuki; -sumbufu. **~ment** *n.* ugomvi; kutokubaliana.

**disallow** /ˌdɪsə'laʊ/ *v.t.* kataza; kanusha.

**disappear** /ˌdɪsə'pɪə(r)/ *v.i.* toweka; didimia; tokomea; potea. **~ance** *n.* kutoweka; upotevu.

**disappoint** /ˌdɪsə'pɔɪnt/ *v.t.* vunja moyo; sikitisha; vunja matarajio. **~ed** *adj.* -enye kuvunjika moyo; -enye kupoteza matumaini. **~ment** *n.* masikitiko; hali ya kuvunjika moyo; mtu avunjaye moyo.

**disapprove** /ˌdɪsə'pru:v/ *v.i.* kataa; toridhia.

**disarm** /dɪs'ɑ:m/ *v.t./i.* **1.** nyang'anya silaha. **2.** punguza silaha; punguza majeshi. **3.** tuliza; zima; punguza nguvu. **~ament** *n.* upunguzaji silaha za kivita.

**disaster** /dɪ'zɑ:ste(r)/ *n.* msiba; baa; hasara; janga; masaibu; maafa. **disastrous** *adj.* -a msiba; -a maafa.

**disc, disk** /dɪsk/ *n.* sahani; kisahani; diski.

**discard** /dɪ'skɒ:d/ *v.t.* tupa; ondosha; kataa; acha; beza.

**discern** /dɪ'sə:n/ *v.t./i.* ona; fahamu; tambua; pambanua; hisi; nabihika; maizi. **~ing** *adj.* -a akili; -juzi. **~ment** *n.* busara; akili; utambuzi; ufahamu.

**discharge** /dɪs'tʃɑ:dʒ/ *v.t.* **1.** shusha; teremsha (shehena kutoka melini). **2.** piga; fyatua (bunduki etc.); tupa (mshale etc.). **3.** toa (maji, mvuke, nguvu za umeme etc.). **4.** ondosha; toa katika kazi. **5.** lipa

deni. *n.* mripuko; usaha; ruhusa ; kufukuzwa au kufukuza kazini; utokaji.

**disciple** /dɪ'sʌɪp(ə)l/ *n.* mwanafunzi; mfuasi; sahaba.

**discipline** /'dɪsɪplɪn/ *n.* **1.** malezi; maongozi. **2.** taratibu; nidhamu; utii; usikivu. **3.** maadili. *v.t.* adilisha; rudi; ongoza. **disciplinarian** *n.* -enye kushadidia nidhamu na taratibu. **disciplinary** *adj.* -a kurudi; -a kuadilisha; -a kuongoza.

**disclaim** /dɪs'kleɪm/ *v.t.* kana; kataa; kanusha.

**disconcert** /ˌdɪskən'sɜ:t/ *v.t.* sumbua; tia wasiwasi; babaisha; kanganya; vuruga akili.

**disconnect** /ˌdɪskə'nekt/ *v.i.* tenga; fungua; tungua; kata; ungua. **~ed** *adj.* (kwa maneno au fikira) siyofungamana vizuri; -siyofuata barabara; -liyokatwa.

**discontent** /ˌdɪskən'tent/ *n.* uchungu; ukosefu wa ridhaa; chuki; manung'uniko. **~ed** *adj.* -a kutoridhika.

**discontinue** /ˌdɪskən'tinju/ *v. t./i.* komesha; koma; acha; kataza; isha; hulu.

**discount** /'dɪskaʊnt/ *n.* turuhani; punguzo la bei. *be at a ~,* kwa bei nafuu. *v.t.* kata faida; punguza bei; sadiki nusu tu ya habari.

**discourage** /dɪs'kʌrɪdʒ/ *v.t.* vunja moyo; katisha tamaa; pinga. **~ment** *n.* jambo au hali ya kukatisha tamaa.

**discourteous** /dɪs'kɜ:tiəs/ *adj.* -sio na heshima au adabu.

**discover** /dɪ'skʌvə(r)/ *v.t.* vumbua; gundua; kuta; fumania; onyesha; funua. **~er** *n.* mvumbuzi; mgunduzi. **~y** *n.* uvumbuzi; ugunduzi; jambo jipya.

**discredit** /dɪs'kredɪt/ *v.t.* tosadiki; aibisha; tahayarisha; fedhehesha. *n.* aibu; fedheha. **~able** *adj.* a aibu; -a kutiliwa wasiwasi.

**discreet** /dɪ'skri:t/ *adj.* a busara; -angalifu; -enye tahadhari; makini katika mazungumzo au matendo. **discretion** *n.* busara; nadhari; makini; akili; uchunguzi; uteuzi. *surrender at discretion,* jisalimisha bila masharti. *at your discretion,* kwa hiari yako.

**discrepancy** /dɪs'krɛp(ə)nsi/ *n.* tofauti; kutopatikana; hitilafu.

**dicriminate** /dɪ'skrɪmɪneɪt/ *v.t./i.* pambanua; chagua; ainisha; tofautisha; pendelea; onea; bagua. **discriminating**. *adj.* -enye uwezo wa kupambanua; -onevu; -baguzi. **discrimination** *n.* ubaguzi; upambanuzi.

**discuss** /dɪ'skʌs/ *v.t.* zungumza juu ya; hoji; jadili. **~ion** *n.* mazungumzo; mjadala; masha-uriano.

**disease** /dɪ'zɪ:z/ *n.* ugonjwa; maradhi. **~d** *adj.* -gonjwa.

**disgorge** /dɪs'gɔ:dʒ/ *v.t.* tapika; kokomoka; hozomoka. *(fig.)* rudisha kwa nguvu (vitu vilivyo -nyang'anywa).

**disgrace** /dɪs'greɪs/ *n.* aibu; ila; fedheha; soni; izara; muadhara; kitu au mtu aletae aibu. *v.t.* aibisha; fedhehi; adhiri. **~ful** *adj.* -a aibu.

**disgruntled** /dɪs'grʌntld/ *adj.* sioridhika; -siopendezwa; - enye kuudhika.

**disguise** /dɪs'gaɪz/ *v.t.* geuza; ficha. *n.* mavazi ya kujigeuza; ulaghai; hila.

**disgust** /dɪs'gʌst/ *n.* chuki; karaha; maudhi. *v.t.* chukiza; kirihi. **~ing** *adj.* -a kuchukiza.

**dish** /dɪʃ/ *n.* dishi; sufuria; chakula. *v.t.* pakua; andalia chakula.

**dishearten** /dɪs'hɑ:tn/ *v.t.* vunja moyo; ogofya.

**dishonour** /dɪs'ɒnɪst/ *n.* aibu; fedheha; dharau; kitu au mtu aletae fedheha. *v.t.* aibisha; fedhehesha; hizi; tahayarisha. *~ a cheque,* -tokubali cheki. **~able** *adj.* -a aibu; si -aminifu.

**disillusion** /ˌdɪsɪ'l(j)u:ʒ(ə)n/ *v.t.* ondosha dhana; onyesha ukweli. **~ment** *n.* uono wa ukweli.

**disinfect** /dɪsɪn'fekt/ *v.t.* ua viini vya maradhi kwa kufukiza au kusafisha kwa dawa za kemikali. **~ant** *n.* dawa ya kuua viini vya maradhi. *adj.* -a dawa hiyo.

**disintegrate** /dɪs'ɪntɪgreɪt/ *v.t./i.*

vunja; tenga sehemu mbali mbali; vunjika; tengeka sehemu mbalimbali.

**disinterested** /dɪs'intrəstɪd/ *adj.* si -enye kupendelea; si -enye kutaka faida. *a ~ person,* mtu mwadilifu.

**disjointed** /dɪs'dʒɔɪntɪd/ *adj.* -siyofungamana; -siyofuatana moja kwa moja; -liyokatikakatika.

**dislocate** /'dɪsləkeɪt/ *v.t.* tegua; vuruga; chafua; fuja.

**dislodge** /dɪs'lɒdʒ/ *v.t.* ondoa; ondosha; hamisha; fukuza; ng'oa.

**dismal** /'dɪzm(ə)l/ *adj.* -a kufisha moyo; -a kuhuzunisha; -a kuchukiza; -a kuondoa furaha; -enye huzuni.

**dismantle** /dɪs'mæntl/ *v.t.* pambua; kongoa; vunja; bomoa. *~ a machine,* kongoa mashine.

**dismay** /dɪs'meɪ/ *n.* hofu; fadhaa. *v.t.* ogofya; fadhaisha.

**dismiss** /dɪs'mɪs/ *v.t.* ondosha; uzulu; fukuza; achia mbali; ruhusu. *~ thoughts of revenge,* ondoa mawazo ya kisasi. **~al** *n.* ruhusa; kufukuzwa; kutolewa; kuondoshwa.

**disorder** /dɪs'ɔ:də(r)/ *n.* fujo; machafuko; ghasia; fujo; maradhi; rabsha; zahama. *v.t.* chafua; fuja. **~ly** *adj.* shaghalabaghala; bila mpango; -asi. *a ~ house,* nyumba chafu; danguro.

**disorganize** *v.t.* chafua; haribu; fuja; pangua.

**disown** /dɪs'əʊn/ *v.t.* kana; kataa; kanusha.

**disparity** /dɪ'spærəti/ *n.* hitilafu; tofauti.

**dispassionate** /dɪs'pæʃənet/ *adj.* -siopendelea; -a haki; -siohemkwa; -siotawaliwa na jazba.

**dispatch**, **despatch** /dɪ'spætʃ/ *v.t.* tuma; peleka; fanya upesi; maliza; ua; nyonga. *n.* utumaji; upelekaji; barua; waraka; wepesi; haraka. *act with ~,* fanya upesi.

**dispense** /dɪ'spens/ *v.t./i.* gawanya; toa; changanya na kutoa dawa. *~ with,* acha kutumia; achana na; fanya bila ya. **~r** *n.* mchanganyaji na mgawaji dawa.

**dispensary** /dɪ'spɛns(ə)ri/ *n.* zahanati; chumba cha kutolea dawa.

**dispensation** *n.* ruhusa; fatwa; ruhusa maalumu itolewayo katika mfumo wa kidini au kisiasa unaoendelea; majaliwa ya Mungu.

**disperse** /dɪ'spə:s/ *v.t./i.* tawanya; tawanyika; eneza; enea; ondoa; ondoka; sambaza; sambaa. **dispersal** *n.* mtawanyiko; msambao; uenezi. **dispersion** *n.* **1.** mtawanyiko: kutandawaa kwa mnururisho wa sumakuumeme kwenye midia. **2.** msambao wa data.

**displace** /dɪs'pleis/ *v.t.* hamisha; toa mahali pake. **~ment** *n.* **1.** uhamisho. **2.** kima cha maji kilichohamishwa na kitu kinachoelea juu yake. **3.** umbali mwelekeo: umbali wa kunyooka kuelekea upande fulani. *~ reaction,* mmenyuko msogezo: utendanaji ambapo metali yenye nguvu huchukua nafasi ya metali dhaifu katika mchanganyiko wa kampaundi.

**display** /dɪ'spleɪ/ *v.t.* onyesha; angaza; tembeza. *n.* onyesho; tamasha. *make a ~,* jifaharisha.

**dispose** /dɪ'spəʊz/ *v.i./t.* panga; tengeneza; ongoza; amuru; kata shauri. *~ of,* komesha; acha; toa; katia hukumu. *be ~d to,* taka; penda; elekea. **disposal** *n.* matumizi; uuzaji; matengenezo; madaraka; hukumu. *at your ~,* kwa matumizi yako. **disposition** *n.* madaraka; mpango; taratibu; tabia; silka; moyo; nia.

**dispossess** /ˌdɪspə'zes/ *v.t.* nyang'anya; pokonya; pora; toa; punga shetani. **~ion** *n.*unyang'anyi; uporaji; upokonyaji.

**dispute** /dɪ'spju:t/ *v.t./i.* shindana; bishana; kaidi; kana; gombana; pinga; jadiliana. *n.* shindano; mabishano; ugomvi; manza. *beyond ~,* bila shaka yoyote.

**disregard** /ˌdɪsrɪ'gɑ:d/ *v.t.* tojali; toangalia; tofikiri; dharau; puuza; acha. *n.* kutoangalia; dharau; upuuzaji.

**disrepute** /ˌdɪsrɪ'pju:t/ *n.* tabia mbaya; utovu wa heshima. *fall into*

~, poteza sifa njema. *bring into ~*, adhiri; aziri tia aibuni.

**disrupt** /dɪs'rʌpt/ *v.t.* chafua; vunja; vuruga; katiza; ingilia kati; dakiza; tenganisha. **~ion** *n.* mpasuko; mvunjiko; uchafuzi. **~ive** *adj.* -a kuchafua.

**dissect** /dʌɪ'sɛkt, dɪ-/ *v.t.* changua; kata vipande vipande kwa ustadi. tawanya; sambaza.

**dissent** /dɪ'sɛnt/ *v.i.* tokubali; kaidi, kataa. *n.* mfarakano **dissension** *n* ukaidi; kutopatana; mfarakano; ugomvi. **~er** *n.* asiyekubali mafundisho ya madhehebu fulani ya dini.

**dissertation** /ˌdɪsə'teɪʃ(ə)n/ *n.* tasnifu: insha au hotuba ndefu juu ya mada fulani chuoni.

**dissipate** /'dɪsɪpeɪt/ *v.t./i.* fukuza; tawanya; tawanyika; tapanya; fuja; badhiri; fanya ufasiki. **~d** *adj.* a uasherati; -badhirifu. **dissipation** *n.* ubadhirifu; utapanyaji.

**dissolve** /dɪ'zɒlv/ *v.t.* yeyusha; mumunyisha; yeyuka; vunja, vunjika; toweka polepole; fifia komesha.

**dissuade** /dɪ'sweɪd/ *v.t.* shawishi vingine; jaribu kuzuia kwa shauri au kwa maneno. **dissuasion** *n.* ushawishi.

**distance** /dɪstəns/ *n.* masafa, umbali; mwendo; muda. **distant** /dɪstənt/ *adj.* -a mbali. *a ~ relative*, jamaa wa mbali.

**distaste** /dɪs'teɪst/ *n.* chuki, maudhi. **~ful** *adj.* -siopendeza; -a kuchukiza.

**distend** /dɪ'stend/ *v.t./i.* vimbisha; tanua; vimba; tanuka; futuka kutokana na kanieneo toka ndani.

**distil** /dɪ'stɪl/ *v.t./i.* evusha; keneka: fanya kioevu kuwa mvuke na kukigeuza kuwa kioevu tena. **~lation** *n.*mwevusho, mkeneko ugeuzaji kioevu kuwa mvuke kisha kikageuzwa kuwa kioevu tena. **~led water** *n.* maji mkeneko: maji yaliyokenekwa au yaliyopatikana kwa kutonesha mvuke maji. **~lery** *n.* kiwanda cha kuevushia.

**distinct** /dɪ'stɪŋkt/ *adj.* epesi kusikika; *epesi* kuonekana, dhahiri bayana; ingine; -a mbalimbali **~ly** *adv.* kwa uwazi. **~ive** *adj.* a kupambanua; -a kuonyesha; a mtindo; a peke yake. **~ features** sifa bainifu: katika nadharia ya Chomsky na Halle huwa ni sifa zinazopambanua vipashio vya kifonolojia.

**distinction** /dɪ'stɪŋkʃn/ *n.* tofauti heshima; sifa

**distinguish** /dɪ'stɪŋgwɪʃ/ *v.t.* pambanua; bainisha; ainisha, chagua; weka mbali; tukuza; jipatia sifa. **~ed** *adj.* tukufu; mashuhuri, teule; bora.

**distort** /dɪ'stɔ:t/ *v.t.* geuza vibaya, potoa; potosha; umbua; haribu maana ya. *a face ~ed by pain*, uso uliogeuka kwa maumivu. **~ion** *n* kilema; uumbukaji; uharibifu, upotovu

**distract** /dɪ'strakt/ *v.t.* elekeza mawazo pengine; elekeza nadhari kwenye shughuli nyingine fadhaisha. **~ed** *adj.* -enye wasi wasi; -enye mawazo yaliyo elekea pengine. **~ion** *n.* fadhaa; wasiwasi burudani

**distress** /dɪ'stres/ *v.t.* sumbua; udhi dhiisha; lemea; taabisha. *n.* huzuni, fadhaa; shida; dhiki; udhia, msiba mashaka; kibuhuti, wasiwasi, hangaiko.

**distribute** /dɪ'strɪbju:t, 'dɪstrɪbju:t/ *v.t.* toa; eneza; tanda; gawanya, ainisha; panga. **distribution** *n* mgao; mgawanyo; ugawaji; usambazaji. **distributor** *n.* mgawaji; kigavi distribyuta.

**district** /dɪstrɪkt/ *n.* jimbo; wilaya mtaa.

**distrust** /dɪs'trʌst/ *v.t.* shuku totumaini; tuhumu; dhania. *n* tuhuma; shaka.

**disturb** /dɪ'stɜ:b/ *v.t.* chafua; vuruga, sumbua; udhi. **~ance** *n.* machafuko; ghasia; zahama; fujo.

**ditch** /dɪtʃ/ *n.* handaki; shimo mtaro; mfereji; ufumbi. *die in the last ~*, linda mpaka mwisho.

**dive** /daɪv/ *v.i.* zamia majini; piga mbizi; shuka upesi; tia mkono

(majini, chomboni, mfukoni, etc.) *n.* uzamaji; uzamiaji. **~r** *n.* mzamiaji; mpiga mbizi.

**diverge** /dʌɪ'vəːdʒ, dɪ-/ *v.i.* achana; fuata njia mbalimbali; chepuka; tawanyika. **~nce** *n.* mwachano; tofauti. **~ncy** *n.* uachanaji. **~nt** *ad.* -enye kuachana; -enye mwelekeo mbalimbali. **diverging lens**, lenzi tawanyishi: lenzi inayotawanya miali. **diverging mirror**, kioo tawanyishi: kioo kinachotawanya miali kiliyoiakisi.

**diverse** /dʌɪ'vəːs, 'dʌɪvəːs/ *adj.* -a namna mbalimbali; anuai.

**diversity** /dʌɪ'vəːsɪfʌɪ, dɪ-/ *n.* hali ya kuwa anuwai.

**divert** /dʌɪ'vəːt, dɪ-/ *v.t.* geuza upande; elekeza kwingine; kengeusha; furahisha. **~ing** *adj.* -a kufurahisha; -enye kuelekeza kwengine. **diversion** *n.* mkengeuko; mwelekeo mwingine; mchezo; tafrija.

**divest** /dʌɪ'vɛst, dɪ-/ *v.t.* vua; nyang'anya; uzulu; vua madaraka. ~ *a man of his rank and honours,* vua mtu madaraka yake yote. **~iture** *n.* tendo la uuzaji wa sehemu ya hisa za biashara na vitega uchumi.

**divide** /dɪ'vaid/ *v.t/i.* gawanya; gawa; kasimu; tenga; kata; fitini; farikisha; tengana; gawanyika; farikiana. **~er** *n.* kigavi. **~nd** *n.* gawio; kigawanyo; sehemu ya faida. **divisible** *adj.* -a kugawanyika.

**division**. /dɪ'vɪʒn/ *n.* ugawanyaji; kugawanyika; mstari ugawao katika sehemu; fungu; divisheni. **divisor** *n.* kigawanyo.

**divine** /dɪ'vaɪn/ *adj.* -a Mungu; -takatifu. *v.t.* agua; bashiri; bahatisha; kisia. **divination** *n.* uaguzi; ramli; falaki; bishara.

**divorce** /dɪ'vɔːs/ *n.* talaka; utengano. *v.t.* taliki; acha; tangua ndoa. **~e** *n.* mjane mwanamke.

**divulge** /dʌɪ'vʌldʒ, dɪ-/ *v.t.* toa siri; weka wazi; tangaza.

**dizzy** /'dɪzi/ *adj.* -enye kizunguzungu; - enye kutia kizunguzungu. **dizziness** *n.* kizunguzungu.

**DNA** /ˌdɪː en 'eɪ/ *n.* deoksiriboasidi nyuklia: chembechembe zinazohifadhi taarifa za urithi wa viumbe hai, zimo katika kromosomu.

**do** /də; du/ *v.t./i.* (**did**, **done**) **1.** fanya; tenda. **2.** faa. **3.** pika. *The meat isn't done yet,* nyama haijaiva bado. **4.** *(colloq.)* danganya; punja; laghai; rubuni; ghilibu. **5.** *(colloq.)* haribu. ~ *for sb.,* ua au dhuru mtu. *be done for,* haribika. *be done up,* choka sana. ~ *sth. up,* safisha; fanya kama -pya tena; funga kifurushi au bumba; funga vifungo. ~ *with,* tumia; ridhika na. *I could ~ with a drink,* kinywaji kitanifaa. *He could ~ with a new hat,* anahitaji kofia mpya. ~ *without,* totumia; tohitaji; totaka. ~ *away with,* ondoa kabisa. *have to ~ with;* husu; husiana na. *have done with,* achana na. ~ *come,* tafadhali njoo.

**docile** /'dəʊsʌɪl/ *adj.* -tii; -sikivu; -tiifu; -sikizi; -elekevu; makini. **docility** *n.* welekevu.

**dock**[1] /dɒk/ *n.* gudi; majahaba; gati. **dockyard** *n.* gatini. *v.t./i.* funga gati; ingia gatini. **~er** *n.* mpagazi; hamali; kuli.

**dock**[2] /dɒk/ *n.* kizimba akaapo mshtakiwa kortini.

**dock**[3] /dɒk/ *v.t.* kata; katisha; fupisha; punguza.

**doctor** /dɒkte(r)/ *n.* daktari; mganga; tabibu; daktari wa falsafa; mtu aliye na shahada ya falsafa ya taaluma fulani. *v.t.* *(colloq.)* tibu; ganga; ghushi: ~ *accounts* (evidence), geuza hesabu (ushahidi).

**document** /'dɒkjʊm(ə)nt/ *n.* hati; waraka; cheti; mkataba.

**dodge** /dɒdʒ/ *v.t./i.* epa; epuka; piga chenga; kwepa. *n.* hila; mtego; werevu; mbinu.

**doe** /dəʊ/ *n.* jike la kulungu au wa jamii hiyo.

**dog** /dɒg/ *n.*mbwa. *go to the ~s,* haribika; potoka. *lead a ~'s life,* ishi maisha ya kuhangaika na yasiyo

na furaha. *v.t.* (**-gg-**) fuata karibu sana. **~-tired** *adj.* -liochoka kabisa .
**dogma** /dɒgmə/ *n.* imani; itikadi. **~tic** *adj.* -a kufuatwa bila hoja. **~tize** *v.t.* weka kanuni; shikilia kauli binafsi.
**doldrums** /dɒldrəmz/ *n.* huzuni; masikitiko; ukanda wa bahari ulio shwari.
**dole** /dəʊl/ *v.t.* (**out**) gawia kidogo. *n.* sadaka; posho kwa wasio na kazi.
**doleful** /'dəʊlfl/ *adj.* -a huzuni; zito.
**doll** /dɒl/ *n.* mtoto wa bandia; mwanasesere.
**dollar** /'dɒlə(r)/ *n.* dola, aina ya sarafu.
**dolomite** /'dɒləmʌɪt/ *n.* aina ya madini yenye rangi nyeupe au wardi yenye kalisi na maginesi kabonati katika umbo la fuwele pembesita.


dolphin

**dolphin** /'dɒlfin/ *n.* mnyama wa baharini aitwaye pomboo.
**dome** /dəʊm/ *n.* kuba.


dome

**domestic** /də'mestɪk/ *adj.* **1.** -a nyumbani. **2.** si -geni; -zalia; - a nchi yenyewe. *~ news,* habari za ndani ya nchi. **3.** (kwa wanyama) -liofugwa. **~ate** *v.t.* fundisha; fuga; lea; idilisha. **~ity** *n.* maisha ya nyumbani.
**dominate** /'dɒmɪneɪt/ *v.t./i.* tawala; amuru; -wa juu ya.
**dominant** /'dɒmɪnənt/ *adj.* -kuu; -enye nguvu; -enye amri; - enye kutawala. *dominant gene,* jenitawala: moja ya jeni mbili za alele ambayo tabia yake ndiyo inayorithiwa. **domination** *n.* utawala; nguvu.
**domineer** /ˌdɒmɪ'nɪe/ *v.i.* fanya jeuri; kandamiza; onea.
**dominion** /də'mɪniən/ *n.* utawala; amri; mamlaka; nchi.
**dominoes** *n.* mchezo wa dhumna wenye seti 28 na alama kuanzia 0 hadi 6.


dominoes

**donate** /dəʊ'neɪt/ *v.t.* -pa, toa msaada; changa.
**donation** /dəʊ'neɪʃn/ *n.* mchango; sadaka; msaada.
**donkey** /'dɒŋki/ *n.* punda; mpumbavu; mkaidi.
**donor** /'dəʊnə, -nɔ:/ *n.* mhisani; mfadhili; mtoaji sadaka.
**doom** /du:m/ *n.* maangamizi; kifo; ajali; mauti. **~s day** *n.* siku ya kiama. **~ed** *adj.* -lioandikiwa; liojaaliwa.
**door** /dɔ:(r)/ *n.* mlango. *next ~,* jirani; karibu. *out of ~s,* nje. *to lay at his ~,* kumshitaki. **~keeper** *n.* bawabu. *~chain,* tumbuu. **~post** *n.* mwimo. **~step** *n.* kizingiti.
**dormant** /'dɒ:mənt/ *adj.* -a kulala; -siotumika; -a kupumzika. **dormancy** *n.* ubwete: hali ambapo kiumbe, hasa mimea na mbegu, inakuwa katika metaboli shikizo na huwa ukuaji umesita hasa wakati wa majira ya baridi.
**dormitory** /'dɔ:mɪt(ə)ri/ *n.* bweni; dakhalia.
**dose** /dəʊs/ *n.* kipimo cha dawa. *v.t.* nywesha dawa.
**dosimeter** /dɪʊ'sɪmɪtə/ *n.* dosimita: chombo cha kupimia kima cha mnururisho uliofyonzwa.
**dot** /dɒt/ *n.* nukta. *v.t.* (**-tt-**) tia nukta. *be ~ted about,* tapakaa. *on the ~,* juu ya alama.
**double** /dʌbl/ *adj.* **1.** maradufu; mara mbili. **2.** -enye sehemu mbili. *a ~ barrelled gun,* bunduki yenye mitutu miwili. *a ~ bed,* kitanda cha watu wawili. *adv.* **1.** mara mbili. *cost ~,* -wa na bei mara mbili zaidi. **2.** kwa jozi. *n.* kiasi cha mara mbili. *at the ~,* mbio. *v.t./i.* zidisha au ongeza mara mbili; kunja sehemu mbili. *~ back,* rudi mbio. *~ up,* pinda; kunja; pindika; kunjika; jikunja kwa maumivu. **~-dealer** *n.* mjanja.
**doubt** /daʊt/ *n.* shaka; wasiwasi; tuhuma. *without a ~,* bila shaka. *no ~,* pasina shaka. *v.t./i.* shuku; tuhumu. **~ful** *adj.* -enye wasiwasi; si hakika. **~less** *adv.* bila shaka; hakika; yakini.
**dough** /dəʊ/ *n.* unga uliotiwa maji na hamira halafu ukakandwa na

tayari kuokwa.

**dove** /dʌv/ *n.* hua; njiwa; tetere; pugi. **~-coloured** *adj.* -a rangi ya njiwa. **~tail** *v.t./i.* umanisha kwa ndimi; funga kwa urahisi.

**down**[1] /dɒʊn/ *adv.* chini. *prep.* chini ya. *v.t. put ~ tools,* goma kufanya kazi. *~ an enemy,* shinda adui. **~cast** *adj.* -enye huzuni; -zito. **~fall** *n.* maanguko; maporomoko. *(fig.)* maangamizi. **~-hearted** *adj.* - enye huzuni. **~pour** *n.* mvua nyingi. **~right** *adj.* -nyofu; wazi; halisi. *adv.* kabisa; sana. **~trodden** *adj.* a kudhulumiwa; -a kuonewa. **~ward** *adj.* -a kwenda au kuelekea chini. **~wards** *adv.* chini.

**down**[2] /dɒʊn/ *n.* nchi ya vilima vilima vyenye majani.

**down**[3] /dɒʊn/ *n.* laika, malaika.

**dowry** /'daʊ(ə)ri/ *n.* mahari.

**draft** /dra:ft/ *n.* **1.** rasimu; kiolezo; kielelezo. **2.** hundi; hawala; cheki. **3.** kundi la askari lililopangiwa kazi maalumu. **4.** mchezo wa dama. *v.t.* andika rasimu; chagua watu kwa kazi maalumu. **~sman** *n.* mchora ramani; mwandishi wa rasimu.

**drag** /dræg/ *v.t./i.* (**-gg-**) kokota; burura; kokoteza; vuta; buruta; enda kwa shida; chelewa; kawia. *n.* wavu; kizuizi.

**dragon** /drægən/ *n.* dragoni: joka (la hadithini) lenye mabawa, magamba, miguu yenye makucha, litoalo moto kinywani. **~-fly** *n.* kereng'ende; kurumbiza.

**drain** /drein/ *n.* **1.** mfereji; ufumbi; bomba; mtaro; funda la maji. **2.**gharama kubwa; *v.t./i.* ondoa maji kwa mtaro; tiririka na kukauka; tumia kidogo kidogo; -nywa yote. **~age** *n.* kuondoa maji; kukauka; bomba la maji machafu.

**drama** /dra:mə/ *n.* drama; tamthilia; mchezo wa kuigiza; mfululizo wa matukio ya kuvutia. **~tics** *n.* taaluma ya kuigiza au kuongoza michezo ya kuigiza. **~tist** *n.* mwandishi wa tamthilia. **~tize** *v.t.* igiza tamthilia; tia chumvi; geuza.

**draught** /drɒ:ft/ *n.* **1.** upepo. **2.** uvuaji samaki kwa wavu. **3.** kina cha maji kinachohitajika ili meli ielee. **4.** funda. *take large ~s,* piga mafunda. **5.** -a kutumiwa kwa kazi ya kukokotwa. *a ~horse,* farasi akokotaye gari. *~oxen,* ng'ombe wa gari. **6.** mchezo wa dama. **~y** *adj.* -a upepo mwingi. **~sman** *n.* mchora ramani za kiufundi.

**draw** /drɔ:/ *v.t./i.* (**drew, drawn**) **1.** vuta; kokota; burura; buruta. *~ a cork,* vuta kizibo. *~ a tooth,* ng'oa jino. **2.** pokea; gawiwa. *~ rations,* pokea posho ya kila siku. *~ money from a bank,* chukua fedha kutoka benki. *~ out,* ongeza urefu kwa kuvuta; nyuua. **3.** vutia; pendeza. **4.** hitaji kina cha maji ili kuelea. *The ship ~s six feet of water,* meli inahitaji maji ya kina cha futi sita. **5.** shawishi mtu kusema yote ajuayo. *~ towards, away from, level with, to an end,* etc. -ja (enda) karibu, kutoka, sawa, mwishoni, etc. *~ a game, competition,* etc., toka sare. **6.** piga mstari; chora ramani, picha, etc. *~ the line at,* kataa kuendelea; weka mpaka. *~ a cheque,* andika hundi. *~ up (out) agreement, etc.,* andika mkataba, mapatano, etc. *~ in,* punguka. *~ out,* ongezeka. *~oneself up,* jinyosha. *~ up,* jiweka tayari. *n.* uvutaji; mvuto; upigaji kura; sare. **~n** *adj.* -liochoka. **~back** *n.* kizuizi; kikwazo. **~-bridge** *n.* daraja liwezalo kuinuliwa au kuvutwa. **~er** *n.* mtoto wa meza. **~ers** *n.* suruali . **~ing** *n.* upigaji mstari; picha ya kuchora. **~ing room** *n.* sebule.

**dread** /dred/ *n.* woga; hofu. *v.t./i.* ogopa; hofu.

**dream** /dri:m/ *n.* ndoto; njozi; ruya. *v.t./i.* ( **dreamed dreamt**) ota ndoto; waza. **~y** *adj.* -enye kusinzia. *~y eyes,* macho ya usingizi; si hadhiri; si dhahiri; -sio ya kweli. **.~ily** *adv.* kindoto; kinjozi.

**dress** /dres/ *n.* nguo; nguo. *v.t./i.* vaa; valia; panga; chana; funga dawa; vika; pamba. *be ~ ed in,* vika. **~er** *n.* msaidizi wa dakitari; meza au kabati la jikoni. **~ing** *n.* dawa ya kubandika; mchuzi; kitoweo.

**drift** /drɪft/ *v. i./t.* chukuliwa na mkondo wa maji au hewa; peperushwa. *(fig.)* ishi kiholela. *n.* mkondo wa maji au upepo; *(fig.)* maana; mwelekeo wa mambo.

**drill**[1] /drɪl/ *n.* kekee. *v.t./i.* toboa; pekecha.

**drill**[2] /drɪl/ *n.* gwaride; mazoezi.

**drill**[3] /drɪl/ *n.* mfuo wa kupandia mbegu; mashine ya kupandia mbegu; safu ya mbegu zilizo pandwa.

**drill**[4] /drɪl/ *n.* dreli: aina ya kitambaa kizito.

**drink** /drɪŋk/ *v.t./i.* (**drank**, **drunk**). -nywa; lewa. *~sth. in,* pokea, sikia, ona, kwa furaha. **~able** *adj.* -a kunyweka. *be drunk,* lewa. **drunkard** *n.* mlevi. **drunkness** *n.* ulevi.

**drip** /drɪp/ *v.t./i.* tiririsha; churu-risha; toja; tiririka; chururika; tona. *n.* mtiririko; tone; tojo; sauti ya maji kutoja. **dripping** *n.* uto wa nyama; manyonyoto; manyunyu; matojo.

**drive** /draɪv/ *v.t./i.* (**drove**, **driven**). **1.** endesha; **2.** chunga wanyama. *~n by steam,* -enye kuendeshwa kwa mvuke. **3.** chukua kwa gari. *~ a friend to the town,* kumchukua rafiki mjini kwa gari. **4.** lazimisha. *~n to steal through hunger,* liolazimishwa na njaa kuiba. *~ at,* taka. *What's he driving at?* anakusudia nini? *~ a bargain,* patana. **5.** pigilia; gongomea; piga mpira katika mchezo kama wa golfu. *let ~,* piga. *n.* njia ya gari; barabara. **6.** mpigo wa mpira; mrusho. *(fig.)* nguvu. **~r** *n.* dereva.

**drone** /drəʊn/ *n.* nyuki dume; mvivu; goigoi; uvumi; mvumo. *v.i./t.* vuma kama nyuki; sema au imba kivivu kusiko na msisimko wowote.

**droop** /dru:p/ *v.i./t.* shuka; inama; fifia; dhoofika; shusha; inamisha.

**drop** /drɒp/ *n.* tone; tojo; upungufu; mwanguko. *a ~ in price,* upungufu wa bei. *v.i./t.* (**-pp-**) **1.** angusha. **2.** punguza; pungua; legea. *The wind ~ped suddenly,* upepo ulilegea ghafula. **3.** acha. *~ a bad habit,* acha desturi mbaya. *~ behind,* chelewa. *~ in (on sb.),* zuru. *~ off,* pungua; sinzia. *~ (sb.) at,* teremsha. *Please ~ me at the post office,* tafadhali niteremshe posta. *~sb. a hint,* onya mtu; dokeza.

**drought** /draʊt/ *n.* ukame; ukavu; kiu.

**drown** /draʊn/ *v.t./i.* zama; zamisha; fa maji; tumbukia; tumbukiza; hanikiza.

**drug** /drʌg/ *n.* dawa; dawa ya kulevya. **~gist** *n.* muuza dawa.

**drum** /drʌm/ *n.* ngoma. ear kiwambo cha sikio. *v.t./i.* (**-mm-**) piga ngoma. *~ something into sb.'s head,* sisitiza ili asisahau. **~mer** *n.* mpiga ngoma.

**dry** /draɪ/ *adj.* -kavu; yabisi; kame; si -a kupendeza; -kali; -chungu; -enye kiu. *~ cell,* seli kavu (betri): seli msingi ambamo elektroliti imefyonzwa kwenye mango na kutengenezwa lahamu. *v.t./i.* kausha; kauka; anika; nyauka.
**drily** *adv.* waziwazi. **~ness** *n.* ukavu; ukame; uyabisi. **~er** *n.* mashine ya kukaushia.

**dual** /'dju:əl/ *adj.* -a watu wawili; -a vitu viwili.

**dubious** /'dju:bɪəs/ *adj.* -enye mashaka; si hakika; -a wasiwasi; -enye kutia wasiwasi.

**duck**[1] /dʌk/ *n.* bata; kootwe; salile; mpenzi; muhibu. *make ~s and drakes of,* tapanya; fuja; tupa -tojali.

**duck**[2] /dʌk/ *v.t./i.* inama; jikunja; zama ghafula; chovya majini. *n.* kuinama ghafula. **~ling** *n.* bata mchanga.

**duct** /dʌkt/ *n.* **1.** mchirizi; kifereji; nyweleo. **2.** neli au tyubu ya kupitishia kioevu, gesi, hewa, waya, etc. **3.** tyubu ipitishayo vioevu mwilini.

**due** /dju:/ *adj.* -a haki; -a halali. *When is the ship ~?* meli yatazamiwa lini? *~ to,* kwa sababu ya. *adv.* barabara; sawasawa. *~ north,* kaskazini barabara. *n.* haki; ushuru; kodi; ada.

**duet** /dju'et/ *n.* wimbo wa watu wawili.

**dull** /dʌl/ *adj.* -siong'aa; -sio kali; -zito; pumbavu; pocho; goigoi; butu.

*Trade is ~,* biashara si nzuri. **~ness** *n.* weusi; giza; upocho; upumbavu.
**dumb** /dʌm/ *adj.* bubu. *~show,* igizo la vitendo bila ya maneno. **~found** *v. t.* duwaza; shangaza; fadhaisha; pigwa na bumbuwazi.
**dummy** /dʌmi/ *n.* mfano; mwigo; sanamu. *adj.* -a uwongo; -a kuigiza; -a bandia.
**dump** /dʌmp/ *n.* jaa la taka; dampo; jalala; ghala la zana za vita. *v.t.* tupa takataka; anguka ghafula; uza kwa ya kutupa.
**dung** /dʌŋ/ *n.* mavi; kinyesi; samadi.
**duodenum** /ˌdju:ə'di:nəm/ *n.* duodeni: sehemu ya kwanza ya utumbo mdogo mwembamba kutokea kwenye tumbo.
**duplicate** /'dju:plɪkət/ *v.t./n.* nakili; rudufu; zidisha kuwa mbili; nakala; kopi. *-adj.* sawa na ya kwanza.
**durable** /'djʊərəbl/ *adj.* -a kudumu sana; -a aushi; -sioharibika upesi. **duration** *n.* maisha; muda; wakati; kipindi.
**during** /'djʊərɪŋ/ *prep.* wakati wa.
**dusk** /dʌsk/ *n.* giza la jioni; magharibi; utusitusi.
**dust** /dʌst/ *n.* vumbi; tifutifu; unga. *throw ~ in sb.'s eyes,* danganya; kosesha; laghai. *shake the ~ off one's feet,* ondoka kwa hasira. *v.t./i.* pangusa; nyunyiza; kung'uta. **~bin** *n.* chombo cha kutia taka. **~man** *n.* mzoa taka; mchukuaji taka. **~er** *n.* kitambaa cha kufutia vumbi; dasta; kifutio.



dustbin

**duty** /dju:ti/ *n.* wajibu; kazi; haki; ushuru; kodi. *it is my ~,* ni wajibu wangu. *~ bids me,* inanibidi. **dutiful** *adj.* -tii; -tiifu , -sikivu; -sikizi.
**dwarf** /dwɔ:f/ *n.* mbilikimo. *adj.* -dogo kuliko kawaida. *v.t.* dumaza; viza.
**dwindle** /'dwɪndl/ *v.i.* pungua; dhoofika; punguka; sinyaa; fifia.
**dye** /daɪ/ *v.t./i.* tia rangi; tilika rangi. *n.* dutu sanisia au asilia inayotumika kutia rangi; rangi. *fast ~,* rangi isiyochujuka.
**dynamic** /dʌɪ'namik/ *adj.* -enye nguvu; -enye bidii; mkakamavu. **~s** *n.* tawi la taaluma ya umakanika kuhusu mwendo wa mitambo unaosababishwa na mwendo wa kani.
**dynamite** /'daɪnəmait/ *n.* aina ya baruti yenye nguvu nyingi.
**dynamo** /'dainəməʊ/ *n.* dainamo: chombo cha kuzalishia umeme.

## Ee

**each** /i:tʃ/ *adj./pron.* kila -moja; -moja.
**eager** /i:gə(r)/ *adj.* -enye bidii; -enye shauku. **~ness** *n.* shauku; bidii; juhudi.
**eagle** /i:gl/ *n.* tai; koho; furukombe. **~-eyed** *adj.* -enye macho makali. **~t** *n.* tai mdogo.



eagle

**ear** /ɪə(r)/ *n.* sikio; shuke la nafaka. *give ~,* tega sikio. *bring about ~s,* letea matatizo. **~drum** *n.* kiwambo cha sikio. **~mark** *v.t.* tenga kwa kusudi fulani. **~shot** *n.* masafa ya kuweza kusikia.
**early** /'ɜ:li/ *adj.* -a kale; -a zamani. *adv.* mapema; mwanzo; mwanzoni.
**earn** /ɜ:n/ *v.t.* pata ujira au tijara. **~ings** *n.* ujira; mshahara; chumo; mapato.
**earnest** /'ə:nɪst/ *adj.* -enye juhudi; -a -enye bidii; -a -enye ari; -enye ukweli. *in ~,* kwa moyo mmoja. **~ly** *adv.* kwa bidii.
**earth** /ɜ:θ/ *n.* **1.** dunia; ulimwengu. **2.** nchi; bara; nchi kavu. **3.** ardhi; udongo. **4.** pango la mnyama wa mwitu. *v.t.* fukia. **~en** *adj.* -a udongo. **~enware** *n.* vyombo vya udongo. **~ing** *n.* uunganishaji kifaa cha umeme na



earth

ardhi kwa kutumia kipitishi. **~ly** *adj.* -a dunia hii. **~ closet** *n.* choo cha lindi. **~quake** *n.* tetemeko la ardhi. *~'s atmosphere,* angahewa dunia: gesi inayoizunguka dunia. **~work** *n.* boma la udongo.

**ease** /i:z/ *n.* raha; utulivu; amani; faraja nafuu; ahueni. *be at ~,* starehe; poa; burudika. *be ill at ~,* fadhaika; ona wasiwasi. *with ~,* bila shida; kirahisi. *v.t./i.* tuliza; fariji; pumzisha; legeza; punguza; legea; pungua; pumzika.

**easel** /'i:z(ə)l/ *n.* kiegemeo cha picha au ubao wa kuandikia.

**east** /i:st/ *n./adj./adv.* Mashariki; -a Mashariki. **~wind** *n.* matlai. *far ~,* Mashariki ya Mbali. *middle east,* Mashariki ya Kati.

**Easter** /i:ste(r)/ *n.* Pasaka: sikukuu ya kufufuka kwa Yesu Kristo.

**eat** /ɛt/ *v.t./i.* (**ate**, **eaten**) -la; tafuna; haribu. *~ one's words,* rudisha kauli. **~ery** *n.* mkahawa; hoteli.

**ebb** /eb/ *v.i.* -pwa; rudi; dhoofika; pungua; punguka; fifia. **~-tide** *n.* maji kupwa; maji mafu.

**ebony** /'ɛb(ə)ni/ *n.* mpingo; enye rangi nyeusi tititi.

**eccentric** /ɪk'sɛntrɪk, ɛk-/ *adj.* si -a kawaida; -geni. **~ity** *n.* ajabu; ugeni; upekee wa tabia.

**ecclesiastic** /ɪ,kli:ziæstik/ *n.* kasisi; padri.

**echo** /'ekəʊ/ *n.* mwangwi; mfano; itiko. *v.i./t.* toa mwangwi; fuatisha maneno; kariri. **~ sounder** *n.* kipima kina: kifaa kitumiacho mwangwi kupima kina cha bahari.

**eclipse** /ɪ'klɪps/ *n.* kupatwa mwezi au jua; *(fig.)* onekana kupunguka akili, nguvu, sifa njema. *v.t.* pinga; shinda; pita; acha nyuma. *be ~d,* patwa; liwa; shindwa.

**ecology** /ɪ'kɒlədʒi, ɛ-/ *n.* ikolojia: sayansi ya mahusiano ya viumbe na mazingira yao. **ecosystem** *n.* mfumo ikolojia.

**economy** /ɪ'kɒnəmi/ *n.* uchumi. **economic** *adj.* -a kiuchumi. **economics** /,ɪ:kə'nɒmiks/ *n.* uchumi: sayansi ya uzalishaji, usambazaji, utumiaji bidhaa na fedha. **economical** *adj.* rahisi; -a gharama ndogo. **economize** *v.t./i.* punguza gharama; bana matumizi.

**ecosystem** /'ikəʊsɪstəm/ *n.* mfumikolojia: mfumo unaohusisha mitagusano kati ya jumuia na mazingira yake ikiwemo vitu visivyokuwa hai.

**ecstacy** /'ɛkstəsi/ *n.* **1.** upeo wa furaha; hali ya kurukwa na akili. **2.** aina ya dawa ya kulevya sanisia ya kupumbaza hisia na akili.

**ectopic** /ɛk'tɒpɪk/ *adj.* -a mahali si pa kawaida.

**ectoplasm** /'ɛktə(ʊ)plaz(ə)m/ *n.* uteselinje: sehemu ya nje ya uteseli inayopakana na kiwamboseli.

**eczema** /'ɛksɪmə, 'ɛkzɪmə/ *n.* ukurutu.

**edge** *n.* **1.** makali. *His nerves were on ~,* alikuwa amefaidhaika sana. **2.** ukingo; upindo; mpaka. *give an ~ to,* noa. **~ways**, **~wise** *adv.* kwa upande, ubavuni. *I could not get a word in ~ways,* sikuweza kusema hata neno moja kwani alikuwa akinidakuliza kila niliposema.

**edible** /'ɛdɪb(ə)l/ *adj.* -a kulika na wanadamu.

**edify** /'ɛdɪfʌɪ/ *v.t.* fundisha mema; adilisha; ongoza vizuri kiakili.

**edification** /,edɪfɪ'keɪʃn/ *n.* wema; maadili.

**edit** /'edɪt/ *v.t.* hariri; panga data ili iingizwe kwenye kompyuta. **~ion** *n.* toleo. **~or** *n.* mhariri. **~orial** *adj.* -a mhariri. *n.* tahariri.

**educate** /'ɛdjʊkeɪt/ *v.t.* funza; elimisha; fundisha; somesha. **education** *n.* elimu; mafundisho; malezi. **educationist** *n.* mtaalamu wa elimu.

**educator** /'edʒukeɪte(r)/ *n.* mwalimu.

**eel** /i:l/ *n.* mkunga; nyoka maji.



eel

**efface** /ɪ'feis/ *v.t.* futa; ondoa; haribu kabisa. *~ oneself,* jinyweza.

**effect** /ɪ'fekt/ *n.* athari; matokeo. *of no ~,* bure; -siofaa. *in ~,* kwa kweli. *take ~,* anza kufanya kazi. *talk for ~,*

sema ili kushawishi. *v.t.* fanya; tekeleza. **~ive** *adj.* -a kufaa; -a kuleta lililotarajiwa; tayari kwa kupigana. **~ual** *adj.* -a kuleta lililotakiwa.

**effervesce** *v.i.* chemka; fanya povu; umuka; fofomoka. **~nce** *n.* mchemko; mcheu; povu; **~ent** *adj.* -enye kuchemka.

**efficient** /ɪ'fɪʃnt/ *adj.* -a kufaa; stadi; madhubuti; fanisi. **efficiency** *n.* ufanisi: uwiano wa ufanisi juu ya zao la kazi na kazi iliyoingizwa kwenye mashine.

**effort** /'efət/ *n.* bidii; nguvu; jitihada; juhudi; idili.

**effusion** /ɪ'fju:ʒn/ *n.* utokaji; umwagaji; umwagikaji.

**effusive** /ɪ'fju:sɪv/ *adj.* -kunjufu; -changamfu.

**egestion** *n.* ijesheni: utoaji wa vitu visivyotumika au takataka kutoka mwilini.

**egg**[1] /eg/ *n.* yai. *white of an ~,* ute mweupe wa yai. *~ yolk,* kiini. *~ shell,* ganda. **eggplant** *n.* mbilingani.

**egg**[2] /eg/ *v.t.* *~sb. on,* sukuma; sukumiza; chocha; himiza; harakisha.

**eight** /eɪt/ *n./adj.* -nane. **~een** *n./adj.* kumi na nane. **~y** *n./adj.* themanini.

**either** /'ʌɪðə, 'i:-/ *adj./pron.* -moja -o -ote; -mojawapo. *conj./adv.* ama au; wala. *Nor did I do that ~,* wala hilo sikulifanya.

**ejaculation** /iˌdʒækju'leɪʃn/ *n.* utoaji manii wakati wa kujamiiana.

**eject** /i'dʒekt/ *v.t.* fukuza; toa; tapika; fuka; ondosha.

**elaborate** /ɪ'læbəret/ *adj.* -liochanganuliwa; -liofafanuliwa; -lionakishiwa. *v.t.* tia madoido; fafanua; eleza kinaganaga.

**elapse** /ɪ'læps/ *v.i.* pita kwa wakati.

**elastic** /ɪ'lastɪk/ *adj.* nyumbufu; -a kunyumbulika; -a kunepa; -a kunyuuka. *n.* mpira. **~ity** *n.* unyumbufu.

**elbow** /'elbəʊ/ *n.* kisugudi; kiwiko. *out at ~s,* (kwa mavazi) -kuu-kuu. *v.t.* piga kikumbo.

**elder** /'eldə(r)/ *adj.* mzee; -kubwa. *n.* mzee; mwenye umri zaidi ya mwingine. **~ly** *adj.* -zee. **eldest** *adj.* -lio -zee kuliko wengine; kifungua mimba.

**elect** /ɪ'lɛkt/ *v.t.* chagua; *adj.* -teule. *president ~,* rais mteule. **~ion** *n.* uchaguzi. *by* **~ion** *n.* uchaguzi mdogo. **~ioneering** *n.* ufanyaji kampeni. **~or** *n.* mpiga kura. **~orate** *n.* wapiga kura.

**electricity** /ˌɪlɛk'trɪsɪti, ɛl-, ˌi:l-/ *n.* umeme. **electric charge**, chaji umeme: kiasi cha umeme kilichomo katika kitu. **electric current**, mkondo umeme: mtiririko au msongo wa elektroni au chaji umeme katika kipitishi umeme. **electric motor**, mota: mashine inayogeuza nishati umeme kuwa nishati mwendo. **electrical energy**, nishati umeme: nishati inayotokana na nguvu za umeme.

**electrochemical cell** *n.* seli elektrokemikali: seli itengenezayo umeme kwa kutumia utendanaji kikemikali.

**electrocute** /ɪ'lektrəkju:t/ *v. t.* ua kwa umeme.

**electrode** /ɪ'lɛktrəʊd/ *n.* elektrodi: kipitishi ambacho huingiza au kutoa mkondo umeme kwenye elektroliti wakati wa elektrolisisi au kwenye tao umeme au katika neli ombwe.

**electrolysis** /ˌɪlɛk'trɒlɪsɪs, ˌɛl-/ *n.* elektrolisi: uionishaji kikemikali utokanao na kupitishwa kwa umeme kwenye mmumunyo au myeyuko wa dutu.

**electrolyte** /ɪ'lɛktrəlʌɪt/ *n.* elektroliti: msombo mmumunyo au myeyuko ambao hupitisha mkondo wa umeme.

**electromagnetic** /ɪ'lektrəʊmæg'netik/ *adj.* -a sumakuumeme: -enye kuhusisha umeme na usumaku pamoja. **~ energy**, nishati sumaku-umeme: nishati inayotokana na mnururisho sumakuumeme. **~ radiation**, mnururisho sumaku-umeme: mnu-rurisho unaotokana na suma-kuumeme wenye nishati iendayo kwa kasi ya mwangaza. **~ spectrum**, spektra suma-

kuumeme: hududi yote ya mnururisho sumakuumeme iliyopangwa kwa mujibu wa lukoka.

**electromotive force** *n.* kani mwendoumeme: chanzo cha nishati cha kiumeme kinachotakikana kuunda mkondo wa umeme katika mzunguko.

**electron** /ɪ'lɛktrɒn/ *n.* elektroni: **1.** chembe hasi ya kimsingi iliyomo katika kila atomu. **2.** sehemu ya atomu yenye chaji hasi inayozunguka kiini katika mzunguko maalumu. **~ shell** mzingo elektroni: mzunguko wa elektroni zilizopangwa kuzunguka kiini katika mizingo tofauti. **~ics** *n.* elektroniki: sayansi inayohusu tabia na nyendo za elektroni. **electronic world,** ulimwengu pepe.

**electroplating** *n.* mpakazokiumeme: mpakazo wa tabaka ya metali juu ya kitu kwa njia ya elektrolisi.

**elegant** /'elɪgənt/ *adj.* -nzuri; -a madaha; -usanii.

**element** /'elɪmənt/ *n.* **1.** elementi: dutu isiyoweza kugawanywa kikemikali katika dutu nyingine ndogo zaidi. **2.** jambo la asili au msingi. *the ~s of geometry,* misingi ya jiometri. *He is in his ~,* anajihisi kama kwake. **~ary** *adj.* -a asili; -a mwanzo. *~ particles,* chembe msingi: chembe mbalimbali zifanyazo mata yote katika ulimwengu.

**elephant** /'elɪfənt/ *n.* tembo; ndovu.


elephant

**elevate** /'ɛlɪveɪt/ *v.t.* inua; pandisha; kweza.

**elevation** /ˌelɪ'veɪʃn/ *n.* mwinuko; kimo; ramani ya upande mmoja wa jengo.

**elevator** /'elɪveɪtə(r)/ *n.* lifti.

**eleven** /ɪ'levn/ *adj./n.* kumi na -moja. *at the ~th hour,* dakika za mwisho.

**elicit** /ɪ'lɪsɪt/ *v.t.* toza; tokeza; dhihirisha. *~ a reply,* shawishi mtu ajibu.

**eligible** /'ɛlɪdʒɪb(ə)l/ *adj.* -a kufaa; -a kustahiki. **eligibility** *n.* haki; ufaaji.

**eliminate** /ɪ'lɪmɪneɪt/ *v.t.* toa; futa; ondosha; acha. **elimination** *n.* utoaji; ufutaji; uachaji.

**ellipse** /ɪ'lɪps/ *n.* duaradufu; umbo la yai. **ellipsis** *n.* ufutaji maneno katika maandishi au hotuba. **elliptical** *adj.* -enye umbo la yai; -liofuta maneno.


ellipse

**El Nino** /ɛl'ni:njəʊ/ *n.* Elninyo: mfumo wa hali ya hewa katika bahari ya Pasifiki unaoathiri kwa namna tofauti dunia nzima.

**elongate** /'i:lɒŋgeɪt/ *v.t./i.* refusha; refuka; nyosha. *adj.* refu. **elongation** *n.* urefukaji; . urefushaji; nyongeza ya urefu.

**else** /els/ *adv.* tena; zaidi; juu ya hayo; vinginevyo; ama sivyo. **elsewhere** *adv.* pengine; pengi nepo.

**elucidate** /ɪ'l(j)u:sɪdeɪt/ *v.t.* eleza; fafanua.

**elucidation** /i'lu:'sɪdeɪʃn/ *n.* maelezo; ufafanuzi.

**elude** /ɪ'l(j)u:d/ *v.t.* epuka; epa; epusha; okoka kwa mbinu. **elusion** *n.* hila; werevu; mbinu. **elusive** *adj.* -a hila; -danganyifu; -telezi.

**e-mail** /'i:meɪl/ *n.* **(electronic mail)** barua; barua pepe; pepesi.

**emanate** /'ɛməneɪt/ *v.i.* tokea; anzia.

**emancipate** /ɪ'mansɪpeɪt/ *v.t.* komboa; weka huru; toa utumwani.

**embankment** *n.* boma la kuzuia maji; njia ya juu kwa juu; tuta la reli.

**embargo** /ɛm'bɒ:gəʊ, ɪm-/ *n.* (**-oes**) kikwazo; kizuizi. *lay an ~ on,* piga marufuku; zuia; fungia; ekea vikwazo.

**embark** /ɪm'bɑ:k/ *v.i./t.* panda; ingia; pakia; ingiza chomboni. *~ upon, ~ on,* anza; anzisha; ingia. **~ation** *n.* upandaji; upakizi; uingiaji chomboni.

**embarrass** /ɪm'barəs, ɛm-/ *v.t.* fadhaisha; sumbua; tahayarisha; zuia. **~ment** *n.* fadhaa; haya; soni; wasiwasi.

**embassy** /'embəsi/ *n.* ubalozi; ofisi na kazi za balozi; balozi na maofisa wake.

**embellish** /ɪm'belɪʃ/ *v.t.* pamba; remba; tia madoido; tia chumvi. **~ment** *n.* mapambo; madoido; urembo; chuku.
**embitter**/ɪm'bɪtə(r)/ *v.t.* chukiza; tia uchungu; kirihi. **~ment** *n.* chuki; uchungu; karaha.
**emblem** /'ɛmbləm/ *n.* nembo; mfano; alama; ishara.
**embody** /ɪm'bɒdi, ɛm-/ *v.t.* dhihirisha mawazo, maoni; jumuisha; unganisha. **embodiment** *n.* udhahiri.
**embrace** /ɪm'breɪs/ *v.t.* kumbatia; kumbatiana; kubali; jumuisha; ingiza; fahamu; fuata. *n.* kumbatio.
**embroider** /ɪm'brɔɪdə(r)/ *v.i.* tarizi; nakshi; tia chumvi. **~y** *n.* nakshi; taraza; darzi.
**embryo**/'ɛmbrɪəʊ/ *n.* kiinitete; kitu kilicho katika hatua ya mwanzo ya ukuaji. **~nic** *adj.* -a hatua ya awali. **~logy** *n.* embriolojia: sayansi ya biolojia na tiba kuhusu maisha ya kiinitete.
**emend** /ɪmɛnd/ *v.t.* sahihisha; rekebisha. **~ation** *n.* sahihisho; usahihishaji.
**emerald** /'emərəld/ *n.* kito cha zumaridi.
**emerge** /ɪ'mə:dʒ/ *v.i.* zuka; tokea; onekana; dhihirika; ibuka; julikana. **~ncy** *n.* dharura. *state of ~ncy,* hali ya hatari. *~ exit,* mlango wa dharura au wa kuokolea.
**EMF** *n.* ufupisho wa *electromotive force:* kani mwendoumeme.
**emigrate** /'ɛmɪgreɪt/ *v.i.* hama; hajiri; hamia. **emigrant** *n.* mhamiaji. **emigration** *n.* uhamaji; uhamiaji.
**eminent** /'emɪnənt/ *adj.* tukufu; maarufu; adhimu; mashuhuri. **~ly** *adv.* sana; kabisa. **eminence** *n.* mwinuko; utukufu. *His Eminence,* mwadhama; mhashamu.
**emir**/ɛ'mɪə/ *n.* amiri; sheikh; kadhi.
**emit** /i'mit/ *v.t.* toa; tokeza. **emission** *n.* utoaji; utokezaji.
**emotion** /ɪ'məʊʃn/ *n.* hisia; jazba; mshtuko. **~al** *adj.* -enye jazba; -a jazba.
**emperor** /'empərə(r)/ *n.* mfalme. **empress** *n.* mtawala wa kike, yaani mke wa mfalme au mjane wa mfalme.
**emphasis** /'ɛmfəsɪs/ *n.* mkazo; nguvu; msisitizo. **emphasize** *v.t.* sisitiza; tilia mkazo. **emphatic** *adj.* -a nguvu; -a mkazo; -a msisitizo. **emphatically** *adv.* kwa msisitizo; kwa nguvu.
**empire** /'empaɪə(r)/ *n.* milki; ufalme; mamlaka.
**emplacement** /ɪm'pleɪsmənt/ *n.* mahali pa kuweka silaha.
**employ** /ɪm'plɔɪ/ *v.t.* ajiri; tumia; tuma. **~ment** *n.* kazi; uajiri. **~ee** *n.*mwajiriwa; mfanyakazi; kibarua. **~er** *n.* mwajiri.
**empower**/ɪm'paʊe(r)/ *v.t.* wezesha; -pa idhini; -pa mamlaka.
**empty** /'empti/ *adj./v.t./i.* -tupu. *v.t.* mwaga; mimina; toa. *v.i.* mwagika; -wa tupu.
**emulate** /'ɛmjʊleɪt/ *v.t.* iga; igiza; fuatisha; husudu; shindana na.
**enable**/ɪ'neɪbl/ *v.t.* wezesha.
**enact** /ɪ'nækt/ *v.t.* tunga sheria; igiza. **~ment** *n.* amri; sheria iliyopitishwa.
**enamel** /ɪ'næml/ *n.* enameli: sehemu ya nje ya jino iliyo ngumu na nyeupe yenye kung'ara inayotokana na mgandamano maalumu wa kemikali ya kalisi.
**enamoured** /ɪ'næmed/ *adj.* ashiki; tamani; penda; pendezwa na; vutiwa na.
**encampment** /ɪn'kæmpmənt/ *n.* kituo; kambi.
**enchant** /ɪn'tʃa:nt/ *v.t.* pendeza mno; liwaza; roga; zuga. **~er** *n.* mliwazaji; mchawi; mrogaji; mganga. **~ment** *n.* maliwazo; uchawi; uramali.
**encircle** /ɪn'sɜ:kl/ *v.t.* zunguka; zungusha; zingia; zingira.
**enclose** /ɪn'kləʊz/ *v.t.* zunguka kabisa; zungusha kabisa; tia ndani ya; ambatanisha. **enclosure** *n.* kiambatisho; eneo lililozungushiwa ukuta au uwa.
**encore**/'ɒŋkɔ:/ *int.* tena !; rudia!. *v.t.* omba tukio lirudiwe.
**encounter**/ɪn'kaʊntə(r)/ *v.t.* kutana na; pigana na; pambana na; kuta;

pata. *n.* mkutano; pambano; pigano.

**encourage** /ɪn'kʌrɪdʒ/ *v.t.* tia moyo; tia nguvu; saidia; fariji. **~ment** *n.* msaada; faraja.

**encroach** /ɪn'krəʊtʃ/ *v.i.* nyang'anya; iba; jiingiza; jipenyeza. **~ment** *n.* kujiingiza.

**encyclopaedia** /ɛnˌsʌɪklə(ʊ)'piːdɪə, ɪn-/ *n.* ensaiklopidia: kitabu au seti ya vitabu vyenye taarifa kamili za mambo mengi.

**end** /end/ *n.* mwisho; kikomo; mpaka; ncha; kusudi; nia; madhumuni; matakwa; azma; mradi. *for hours on ~,* kwa muda wa saa nyingi bila kusita. *make both ~s meet,* mudu kujikimu. *put an ~ to, make an ~ of,* komesha. *be at a loose ~,* -wa bila kazi. *to gain one's ~,* pata mradi wake. *v.i/t.* isha; koma; komesha; kata; maliza; hitimisha. **~ing** *n.* mwisho; kikomo. **~less** (**ly**) *adj./adv.* -a daima; -a milele; isiyo na mwisho. **~ways** , **~wise** *adj.* kwa ncha; kiwimawima.

**endanger** /ɪn'deɪndʒer/ *v.t.* hatarisha; ponza. *~ered animal,* mnyama adimu: mnyama ambaye idadi yao duniani ni ndogo mno kiasi cha kuhofiwa kutoweka kabisa katika uso wa dunia.

**endear** /ɪn'dɪə, ɛn-/ *v.t.* fanya kupendeza. **~ment** *n.* tamko la upendo; upendezaji.

**endeavour** /ɪn'dɛvə, ɛn-/ *n./v.t.* jaribio; juhudi; jaribu; jitahidi; jitihada; bidii.

**endemic** /ɛn'dɛmɪk/ *n.* ndwele: -enye kuathiri watu au kiambo maalumu, kama vile ugonjwa wa malaria.

**endocrine** /'ɛndə(ʊ)krʌɪn, -krɪn/ *adj.* (kwa tezi) -enye kumwaga homoni moja kwa moja katika mkondo wa damu. **~ gland** *n.* tezi ndani: tezi inayotengeneza homoni na kuzitia moja kwa moja katika mfumo wa damu bila kupita kwenye vichirizi maalumu.

**endorse** /ɪn'dɔːs, ɛn-/ *v.t.* thibitisha; ridhia; kubali; unga mkono; idhinisha. **~ment** *n.* kibali; uthibitisho; ridhaa.

**endothermic reaction** *n.* utendanaji nyonyajoto: utendanaji kemikali mmenyuko unaonyonya joto kutoka nje.

**endow** /ɪn'daʊ, ɛn-/ *v.t.* weka wakfu. *be ~ed with,* jaliwa. **~ment** *n.* wakfu; kipaji; majaliwa.

**endure** /ɪn'djʊə, ɛn-/ *v.t./i.* vumilia; stahamili; dumu; ishi. **endurance** /ɪn'djuərəns/ *n.* uvumilivu; ustahamilivu; jambo la kuvumiliwa.

**enemy** /'enəmi/ *n.* adui; hasimu. **enmity** *n.* uadui; hasama.

**energy** /'enədʒi/ *n.* nguvu; bidii; nishati: uwezo wa kutenda kazi. **atomic ~,** nishati atomu. **chemical ~,** nishati kikemikali. **kinetic ~,** nishati mwendo. **mechanical ~,** nishati mekanika. **nuclear ~,** nishati nyuklia. **potential ~,** nishati tuli. **solar ~,** nishati ya mionzi ya jua. **thermal ~,** nishati joto. **thermonuclear ~,** nishatijoto nyuklia. **energetic** *adj.* -enye nguvu; bidii; juhudi.

**enervate** /'ɛnəveɪt/ *v.t.* dhoofisha; legeza; nyong'onyeza. *adj.* dhaifu; -tepetevu. **enervation** *n.* udhaifu; ulegevu; unyong'onyevu.

**enfeeble** /ɪn'fiːbl/ *v.t.* dhoofisha; legeza; nyong'onyeza.

**enfold** /ɪn'fəʊld, ɛn-/ *v.t.* kumbatia; funga kwa kuzungushia.

**enforce** /ɪn'fɔːs/ *v.t.* shurutisha utiifu; lazimisha; tilia nguvu. **~ment** *n.* nguvu; utumiaji nguvu.

**enfrenchise** /ɪn'fran(t)ʃʌɪz, ɛn-/ *v.t* -pa haki ya kupiga kura; toa katika utumwa. **~ment** *n.* uhuru; uraia.

**engage** /ɪn'geɪdʒ/ *v.t/i.* **1.** tuma; ajiri. **2.** ahidi. *be ~d in,* shughulika na. **3.** pigana; piganisha. **4.** (kwa sehemu za mashine) ingia; shika; ingiza. **~d** *adj.* -liposa; -enye kazi; -liochumbia. **~ment** *n.* ahadi; sharti; mapigano; mapatano; kazi; uchumba. **engaging** *adj.* cheshi; a kuvutia; -changamfu.

**engender** /ɪn'dʒɛndə, ɛn-/ *v.t.* sababisha; zaa; fanya; anzisha; -wa

asili ya; leta.
**engine** /'endʒɪn/ *n.* injini; mashine; chombo; mtambo. **~ driver** *n.* dereva (hasa wa treni). **~er** *n.* mhandisi. *v.t.* buni; tunga; handisi. *(colloq.) ~ scheme,* buni mpango. **~ering** *n.* uhandisi.
**engrave** /ɪn'greɪv/ *v.t.* chora; tia; kata nakshi. **engraving** *n.* sanaa ya uchoraji, ukataji na utiaji nakshi katika vitu anuwai; sanaa iliyonakishiwa.
**engulf** /ɪn'gʌlf/ *v.t.* meza; didimiza; gharikisha.
**enhance** /ɪn'hɑ:ns, -hans, ɛn-/ *v.t* ongeza; kuza; zidisha; endeleza. **~ment** *n.* ziada; mwongezeko; ukuzaji.
**enjoin** /ɪn'dʒɔɪn/ *v.t.* amuru; agiza; lazimisha.
**enjoy** /ɪn'dʒɔɪ/ *v.t.* penda; furahia; faidika na. *~ oneself,* furahi; jistarehesha. **~able** *adj.* -a kufurahisha. **~ment** *n.* furaha; raha; anasa; starehe.
**enlarge** /ɪn'lɑ:dʒ/ *v.t./i* kuza; ongeza; tanua. **~ment** *n.* ukuzaji; uongezaji.
**enlighten** /ɪn'laɪtn/ *v.t* elimisha; taalamisha; ongoa; angaza. **~ment** *n.* hekima; elimu; uongofu; werevu; mwangaza.
**enlist** /ɪn'lɪst/ *v.t./i.* andikisha; jiandikisha; changa. **~ment** *n.* uandikishaji; mchango.
**enormity** /ɪ'nɔ:məti/ *n.* ukubwa. **enormous** *adj.* -kubwa mno; -a kupita kiasi.
**enough** /ɪ'nʌf/ *adj./n./adv.* -a kutosha. *It is ~,* basi; inatosha. *be ~,* tosha; kifu. *have ~,* shiba; kinai.
**enquire**, **inquire** /ɪn'kwaɪə(r)/ *v.i./t.* uliza; hoji; saili; tafiti. **inquiry** *n.* hoja; swali; uchunguzi; baraza la uchunguzi.
**enrage** /ɪn'reɪdʒ/ *v.t.* kasirisha; ghadhibisha.
**enrich** /ɪn'rɪtʃ/ *v.t.* tajirisha; sitawisha. **~ment** *n.* utajiri; utajirisho.
**enrol** /ɪn'rəʊl, ɛn-/ *v.t.* andika; andikisha; orodhesha; changa. **~ment** *n.* uandikishaji; mchango.
**en route** /ɒn 'ru:t/ *adv.* njiani; katika safari.
**enslave** /ɪn'sleɪv/ *v.t.* tia utumwani; tumikisha.
**ensue** /ɪn'sju/ *v.i* fuata; fuatana; tokea.
**ensure** /ɪn'ʃʊə, ɛn-/ *v.t.* hakikisha; salimisha.
**entail** /ɪn'teɪl/ *v.t* lazimisha; hitaji; taka; husisha; weka wakfu.
**entangle** /ɪn'tæŋgl/ *v.t.* tega; tatanisha; tatiza; zongomeza. **~ment** *n.* mtego; tatizo; matatizo.
**enter** /'entə(r)/ *v.t./i.* ingia; shiriki; anza; jiunga; penya. **entrance** *n.* mlango; njia; uingiaji. *entrance fee,* kiingilio. **entry** *n.* mlango; uingiaji; ingizo; kitomeo.
**enterprise** /'entəpraɪz/ *n.* **1.** jambo kubwa; kazi; uhodari; ujasiri. **2.** shirika; kampuni; biashara. **enterprising** *adj.* hodari; jasiri.
**entertain** /ˌentə'teɪn/ *v.t/i.* karibisha; pokea; burudisha; furahisha; kirimu; fikiria; wazia. **~ing** *adj.* -a kupendeza; -a kufurahisha. **~ment** *n.* dhifa; burudani.
**enthral** /ɪn'θrɔ:l, ɛn-/ *v.t* (**-ll-**) vutia sana; furahisha sana; shangaza. **~ment** *n.* mshangao.
**enthrone** /ɪn'θrəʊn/ *v.t.* tawaza mfalme. **~ment** *n.* kutawazwa.
**enthusiasm** /ɪn'θju:ziæzəm/ *n.* shauku; idili. **enthusiast** *n.* mwenye shauku. **enthusiastic** *adj.* -enye shauku; -enye bidii. **enthusiastically** *adv.* kwa shauku.
**entice** /ɪn'tʌɪs, ɛn-/ *v.t* laghai; shawishi; bembeleza; rubuni. **~ment** *n.* ushawishi; chambo.
**entire** /ɪn'tʌɪə, ɛn-/ *adj.* -zima; -ote; kamili. **~ly** *adv.* kabisa. **~ty** *n.* utimilifu; ukamilifu.
**entomology** /ˌɛntə'mɒlədʒi/ *n.* entomolojia: tawi la zuolojia kuhusu taaluma ya wadudu.
**entrance** /ɪn'trɑ:ns, ɛn-/ *v.t.* n. **1.** furahisha; vutia; pendeza; shangaza; pumbaza. **2.** mlango, njia ya kupitia/kuingilia
**entrant** /'entrənt/ *n.* aingiaye; mshindani.

**entrench** /ɪn'trentʃ/ *v.t* zungushia handaki au boma. ~ *oneself*, ingia katika handaki; *(fig.)* jiweka salama mahali. **~ment** *n.* handaki; boma.
**entropy** /'ɛntrəpi/ *n.* entropi: kiasi fulani cha joto kinachowezesha mikokotoo na kueleza vizuri matokeo ya miendojoto.
**entrust** /ɪn'trʌst/ *v.t.* amini; aminisha; kabidhi; wekea amana.
**enumerate** /ɪ'nju:məreɪt/ *v.t.* hesabu; taja kwa mpangilio. **enumaration** *n.* kuhesabu; kutaja moja moja.
**enunciate** /ɪ'nʌnsɪeɪt/ *v.t./i.* nena; tamka; nena wazi na kwa ufasaha; tangaza. **enunciation** *n.* tamko; kunena wazi.
**envelop** /ɪn'vɛləp, ɛn-/ *v.t.* zunguka; zungusha; funga; gubika; funika. *be ~ed in smoke*, zungukwa na moshi.
**envelope** /'ɛnvələʊp, 'ɒn-/ *n.* bahasha.
**environment** /ɪn'vairanmənt/ *n.* mazingira; hali.
**envisage** /ɪn'vɪzɪdʒ, ɛn-/ *v.t.* taamuli; hisi; fikiria; wazia.
**envoy** /'ɛnvɔɪ/ *v.t./n.* mjumbe; balozi.
**envy** /'envɪ/ *v.t./n.* husudi; husudu; husuda; wivu; kijicho. **enviable** *adj.* -a kuhusudiwa; -a kutamaniwa. **envious** *adj.* -enye husuda; -enye kijicho; hasidi.
**epicentre** /'epɪsentə(r)/ *n.* mahali ambapo tetemeko la ardhi hutokeza kwenye uso wa dunia.
**epidemic** /ˌepɪ'demɪk/ *n./adj.* ugonjwa wa mripuko; -a kuambukiza watu wengi pamoja.
**epidermis** /ˌɛpɪ'də:mɪs/ *n.* ngozinje: seli za gamba la nje katika mimea na wanyama.
**epilepsy** /'ɛpɪlɛpsi/ *n.* kifafa. **epileptic** *adj.* -a kifafa. *n.* mgonjwa wa kifafa.
**episode** /'epɪsəʊd/ *n.* kisa; kipindi; tukio katika mfululizo wa matukio.
**epithet** /'ɛpɪθɛt/ *n.* kivumishi; lakabu; kisifa.
**epoch** /'i:pɒk/ *n.* kipindi maalumu chenye matukio muhimu katika historia.
**equable** /'ɛkwəb(ə)l/ *adj.* si -a kubadilika; sawasawa. *an ~ climate*, hali ya hewa isiyobadilika mara kwa mara.
**equal** /'ikwəl/ *adj.* sawa; sawasawa; -a kulingana. *n.* hirimu; rika. *v.t.* (**-ll-**) -wa sawa na; lingana na. **~ly** *adv.* sawasawa. **~ity** *n.* usawa. **~ize** *v.t.* sawazisha; linganisha.
**equanimity** /ˌɛkwə'nɪmɪti, i:-/ *n.* utulivu wa moyo; upole; utaratibu hasa wakati wa matatizo.
**equate** /ɪ'kweɪt/ *v.t.* linganisha na; sawazisha. **equation** *n.* usawazishaji; mlinganyo.
**equator** /ɪ'kweɪtə(r)/ *n.* istiwai; ikweta. **~ial** *adj.* - a ikweta; -a karibu na ikweta.
**equestrian** /ɪ'kwɛstrɪən, ɛ-/ *n./adj.* mpanda farasi; -a kupanda farasi. *an ~ statue*, sanamu ya mpanda farasi. *~ skill*, ustadi wa kupanda farasi.
**equidistant** /ˌi:kwɪ'dɪstənt/ *adj.* -enye umbali sawa.
**equilateral** /ˌi:kwɪ'lat(ə)r(ə)l, ɛkwɪ-/ *adj.* -enye pande zote sawa. *~ triangle*, pande sawa tatu.
**equilibrium** /ˌi:kw'lɪbrɪəm, ˌɛkwɪ-/ *n.* msawazisho; msawazo: hali tuli baina ya kani au athari zinazopingana. **~ constant**, msawazisho kibaki. **neutral ~**, msawazisho suluhu. **stable ~**, msawazisho thabiti. **unstable ~**, msawazisho dhaifu.
**equinox** /'i:kwɪnɒks, ˌɛkwɪ-/ *n.* ikwinoksi, sikusare: siku mlingano ambapo jua huvuka mstari wa ikweta hivyo kuufanya mchana na usiku uwe sawa. **equinoctial** *adj.* -a ikwinoksi.
**equip** /ɪ'kwɪp/ *v.t* (**-pp-**) tayarisha; andaa; zatiti. **~ment** *n.* vifaa; zana; vyombo.
**equivalent** /ɪ'kwɪv(ə)l(ə)nt/ *n./adj.* sawa; badala; linganifu.
**era** /'ərə/ *n.* enzi; zama. *the christian ~*, enzi ya dini au mwaka wa kikristo.
**eradicate** /ɪ'radɪkeɪt/ *v.t.* ng'oa; futa; haribu.
**eradication** /ɪ'rædɪ'keɪʃn/ *n.* uharibifu; ufutaji; ung'oaji.
**erase** /ɪ'reɪz/ *v.t.* futa. **erasable** *adj.*

enye kufutika. **~r** *n.* kifutio.
**erect** /ɪ'rekt/ *adv.* -a wima. *v.t.* simamisha; jenga. **~ion** *n.* usimamishaji; ujenzi.
**erg**[1] /ɜ:g/ *n.* kizio cha kani au kazi.
**erg**[2] /ɜ:g/ *n.* (**~s**, **areg**) eneo kubwa jangwani lenye milima ya mchanga inayohamahama kwa upepo hasa katika jangwa la Sahara.
**erode** /ɪ'rəʊd/ *v.t.* mong'onyoa; momonyoa.
**erosion** /ɪ'rəʊʒn/ *n.* mmong'onyoko; mmomonyoko.
**err** /ɜ:/ *v.i.* kosea; potoka; fanya dhambi. **~atic** *adj.* -potofu; -a kugeukageuka. **~oneous** *adj.* si sahihi; -enye kosa. **~ing** *adj.* -enye hatia; -enye kufanya dhambi. **~or** *n.* kosa.
**errand** /'erənd/ *n.* safari fupi; ujumbe. *He has gone on an ~,* ametumwa. **~-boy** *n.* mtumishi wa nje; tarishi.
**erupt** /ɪ'rʌpt/ *v.i.* foka; bubujika; ripuka; fumuka. **~ion** *n.* kufoka kwa volkano; kuzuka vita; kutokwa na ukurutu.
**erythrocyte** /ɪ'rɪθrə(ʊ)sʌɪt/ *n.* selidamu nyekundu: seli ya damu iliyo na protini yenye rangi nyekundu iitwayo hemoglobini.
**escalator** /'eskaleɪtə(r)/ *n.* eskeleta: ngazi ya umeme.
**escapade** /'ɛskəpeɪd, ˌɛskə'peɪd/ *n.* tendo la ujinga; utundu; ujasiri; upuuzi; utani unaosababisha matatizo; mwishowe.
**escape** /ɪ'skeɪp/ *v.i./i.* okoka; epuka; kimbia; toroka; epa. *n.* wokovu; ukimbiaji; utorokaji. *have a narrow ~,* okoka kwa shida. **~ velocity,** kasimwelekeo nasuzi: kasi-mwelekeo ndogo kabisa ambayo kitu lazima kifikie ili kujinasua na uvutano wa graviti ya ardhi.
**escort** /'ɛskɔ:t/ *n.* mlinzi; mpambe; msindikizaji. *v.t.* sindikiza; linda.
**especial** /ɪ'spɛʃ(ə)l, ɛ-/ *adj.* -a peke yake; bora; mahsusi; maalumu. **~ly** *adv.* zaidi; hasa; hususan.
**essay** /'ɛseɪ/ *n.* **1.** insha. **~ist** *n.* mwandishi wa insha au makala. **2.** bidii; juhudi; jaribio.
**essence** /'esns/ *n.* **1.** asili; nafsi; dhati. **2.** mafuta; uturi; marashi.
**essential** /ɪ'sɛnʃ(ə)l/ *adj.* -a lazima; muhimu; -a msingi. **~ly.** *adv.* kimsingi. **~ element,** elementi lazima: elementi ambayo mnyama lazima aipate katika lishe yake ili aweze kuwa na afya bora.
**establish** /ɪ'stæbliʃ/ *v.t.* amirisha; weka; asisi; anzisha; imarisha; thibitisha. **~ment** *n.* uimarishaji; uasisi; uwekaji; uanzishaji; serikali; shirika; kampuni.
**estate** /ɪ'steɪt/ *n.* shamba; mali; rasilimali. *~ agent,* wakala anaye nunua na kuuza mali.
**esteem** /ɪ'sti:m/ *v.t.* heshimu; stahi; tukuza; enzi; ona; fikiri; dhani; chukulia. *n.* heshima; taadhima; itibari; enzi; staha. **estimable** *adj.* a kuheshimiwa; -a kusifiwa.
**estimate** /'ɛstɪmət/ *v.t.* kadiri; kisia; pima. *n.* kisio; makadirio. **estimation** *n.* heshima; sifa; maoni; mtazamo. *in my ~,* nionavyo mimi. *be held in high ~,* heshimiwa sana.
**estuary** /'ɛstjʊ(ə)ri/ *n.* hori; mlango wa mto.
**et cetera** /ɛt'sɛt(ə)rə, ɪt-/ *n.* (hufupishwa kuwa *etc.*) na kadhalika (n.k.).
**eternal** /ɪ'tə:n(ə)l, i:-/ *adj.* -a milele; -a daima. **eternity** *n.* milele; ahera.
**ethane** /'i:θeɪn, 'ɛθ-/ *n.* etheni, ethani: alkali au hidrokaboni iliyojaa hidrojeni yenye atomu mbili za kaboni.
**ethanol** /'ɛθənɒl/ *n.* etani ambayo atomu moja ya hidrojeni imebadilishana na kikundi kimoja cha hidroksili.
**ether**[1] /'i:θə/ *n.* kioevu kisicho rangi kinachotengenezwa kwa asidi na alkoholi kinachotumika kama nusukaputi na pia kama kimumunyishaji.
**ether**[2] /'i:θə(r)/ *n.* anga ya juu; mbingu. **~eal** *adj.* -a mbinguni; -a peponi.
**ethics** *n.* elimuadili; maadili. **ethical** *adj.* -a maadili.

**ethyl** /'εθʌɪl, θɪl, 'iː-/ *n.* ethili: redikali ya kikaboni itokanayo na etheni.
**etiolate** /'iːtɪəˌleɪt/ *v.t.* fanya mmea upoteze rangi ya kijani kwa kuunyima mwangaza.
**etiquette** /'εtɪkεt, εtɪ'kεt/ *n.* adabu; taratibu za itifaki; miiko.
**etymology** /ˌεtɪ'mɒlədʒi/ *n.* etimolojia: taaluma inayochunguza historia ya maumbo na maana za maneno. **etymological** *adj.* -a etimolojia.
**eucalyptus** /ˌjuːkə'lɪptəs/ *n.* aina ya mti uitwao mkaratusi, huota sana Australia.
**Eucharist** /'juːk(ə)rɪst/ *n.* Ekaristi. *the ~,* ushirika mtakatifu wa kikristo.
**eulogy** /'juːlədʒi/ *n.* maneno ya kusifu kwa maandishi au hotuba. **eulogize** *v.t.* sifu.
**euphemism** /'juːfəmɪz(ə)m/ *n.* tasfida: matumizi ya maneno mbadala ili kukwepa matusi au karaha.
**eureka** /jʊ(ə)'riːkə *n.* mchanganyiko wa shaba na nikeli unaotumiwa kwenye filamenti na nyaya za umeme. **~ can,** keni ya yureka.



**eureka can**

**eutrophication** *n.* utrofikesheni: uchafuzi wa mazingira ya maziwa ambapo mata oganiki iliyooza huifyonza oksijeni yote iliyomo kwenye maji na kuua viumbe hai vilivyomo.
**evacuate** /ɪ'vakjʊeɪt/ *v.t.* ondoka; hama; hamisha; kunya; tapika. **evacuation** *n.* uhamaji; uhamishaji. **evacuee** *n.* mtu aliyehamishwa.
**evade** /ɪ'veɪd/ *v.t.* epa; epuka; piga chenga; kwepa; tegea.
**evasion** /ɪ'veɪʒn/ *n.* ukwepaji; uepukaji; kisingizio; hila.
**evasive** /ɪ'veɪsɪv/ *adj.* -a kukwepakwepa.
**evaluate** /ɪ'væljueɪt/ *v.t.* tathmini; kadiria. **evaluation** *n.* tathmini; ukadiriaji; makadirio. **evaluator** *n.* mkadiriaji.
**evangelical** /ˌiːvæn'dʒelɪkl/ *adj.* -a kiinjili; -a kiprotestanti; -a kilokole. *n.* mlokole. **evangelist** *n.* mmoja wa waandishi wa injili; mwinjilisti.
**evaporate** /ɪ'vapəreɪt/ *v.t./i.* **1.** geuka mvuke; geuza mvuke. **2.** vukiza: geuza kioevu kuwa mvuke bila kufikia kiwango mchemko. **evaporation** *n.* mvukizo; ugeukaji mvuke.
**eve** /iːv/ *n.* mkesha.
**even**[1] /'iːvn/ *n.* (*poet.*) jioni; magharibi.
**even**[2] /'iːvn/ *adj.* sawasawa; laini; linganifu; -enye urari; tulivu; sawa; shufwa. **~ly** *adv.* sawasawa.
**even**[3] /'iːvn/ *adv.* sawasawa. *~ as,*kama -vyo. *~ as expected,* kama ilivyotarajiwa. *~ if,* ijapokuwa; hata. *~ if you die,* hata ukifa.
**evening** /iːvnɪŋ/ *n.* jioni; magharibi. *~ star,* zuhura: (nyota) sayari ya pili katika mfumo wa jua inayoonekana magharibi ya dunia.
**event** /i'vent/ *n.* jambo; tukio; mkasa. **~ful** *adj.* -enye mambo mengi; -a ajabu. **~ual** *adj.* -a mwisho; -a baadaye. **~ually** *adv.* mwishowe; hatimaye. **~uality** *n.* tukio; tokeo; hatima.
**ever** /'evə(r)/ *adv.* siku zote; daima; kila mara; wakati wowote. *whoever,* yeyote. *now and for ~,* maisha na milele. **~green** *n./adv.* -enye majani mabichi mwaka mzima. **~lasting** *adj.* -a milele; -a kudumu. **~more** *adv.* milele.
**every** /'evri/ *adj.* kila; -ote.
**evidence** /'evɪdəns/ *n.* ushahidi. *give ~,* toa ushahidi.
**evident** /'evɪdənt/ *adj.* dhahiri; wazi. **evidently** *adv.* kidhahiri.
**evil** /':vl/ *adj.* -ovu; -baya; fisadi. *n.* uovu; dhambi; ubaya; ufisadi. *adv.* kwa uovu. **~ly** *adv.* kwa uovu.
**evolution** /ˌiːvə'luːʃ(ə)n, 'εv-/ *n.* ukuaji; mabadiliko; mageuko. *theory of ~,* nadharia inayoshikilia kwamba viumbe hai changamano vilitokana na viumbe hai sahili.
**evolve** /i'vɒlv/ *v.t./i.* kua; endelea;

geuka; badilika; toa; tokeza; bainisha.


ewe

**ewe** /'eɪweɪ/ *n.* kondoo jike.

**ex-** /eks/ *prefix.* kiambishi awali chenye maana ya -a zamani'. **~-president**, rais wa zamani.

**exact**[1] /ɪg'zækt/ *adj.* halisi; barabara; hasa; kamili; -enye bidii. **~ly** *adv.* kabisa; kamili. **~ness**, **~itude** *n.* uhalisi; usahihi; uaminifu.

**exact**[2] /ɪg'zækt/ *v.t.* toza; lipisha kwa nguvu; hitaji; taka. **~ing** *adj.* -enye kuhitaji bidii nyingi; -enye kuonea. **~ion** *n.* kutoza kodi isiyokuwa halali au rushwa kwa nguvu.

**exaggerate** /ɪg'zadʒəreɪt, ɛg-/ *v.t./i.* tia chumvi; kuza jambo.

**exaggeration** /ɪg'zædʒə'reɪʃn/ *n.* utiaji wa chumvi jambo; ukuzaji.

**exalt** /ɪg'zɔ:lt, ɛg-/ *v.t.* kuza; sifu sana; tukuza. **~ed** *adj.* -tukufu; adhimu. **~ation** *n.* nderemo; furaha; adhama; utukufu.

**examination** /ɪg'zæmi'neɪʃn/ *n.* mtihani; ukaguzi; uchunguzi.

**examine** /ɪg'zæmin/ *v.t.* kagua; chunguza; tahini.

**example** /ɪg'za:mpl/ *n.* mfano; kielelezo; funzo. *Let this be an ~ to you,* hili liwe fundisho kwako. *I will make an ~ of him,* nitamwadhibu ili liwe funzo kwa wengine.

**exasperate** /ɪg'zasp(ə)reɪt, ɛg-/ *v.t.* kasirisha; udhi; ghadhibisha; kera. **exasperation** *n.* ghadhabu; uchungu; hasira.

**excavate** /'ɛkskəveɪt/ *v.i.* chimba; chimbua; fukua. **excavator** *n.* mchimbaji; chimbulio. **excavation** *n.* uchimbuzi; uchimbaji.

**exceed** /ɪk'si:d/ *v.t.* pita; shinda; ruka mpaka; zidi; -wa zaidi ya. **~ingly** *adv.* zidi sana.

**excel** /ɪk'sɛl, ɛk-/ *v.t./i.* (**-ll-**) pita; -wa bora kuliko; tia fora; zidi. **~lent** *adj.* -ema sana; bora. **~lence** *n.* ubora; uzuri; wema. *Your (His) ~lency n.* mheshimiwa; mtukufu.

**except** /ɪk'sept/ *prep.* ila; isipokuwa. *v.t.* acha; tenga; weka mbali; tohesabu. **~ion** *n.* jambo lisilo la kawaida; mtu asiye wa kawaida; kitu kisicho cha kawaida. *take ~ to,* kataa; kinza; kerwa na. **~ional** *adj.* si -a kawaida; -a pekee; -bora sana. **~ionally** *adv.* kwa kiasi kisicho cha kawaida.

**excerpt** /'ɛksə:pt/ *n.* dondoo.

**excess** /ɪk'sɛs, ɛk-, 'ɛksɛs/ *n.* ziada; tendo lililopindukia mpaka. *in ~ of,* zaidi ya. *~ luggage,* mzigo uliozidi. **~ive** *adv.* mno; zaidi; -a kupita kiasi.

**exchange** /ɪks'ʃndʒ/ *v.t.* badili; badilisha; badilishana. *~ blows,* pigana. *~ words,* zozana. *n.* ubadilishaji; ubadilishanaji; ofisi; soko. **the stock ~**, soko la hisa. *telephone ~,* ofisi ya simu. *labour ~,* ofisi ya kazi. *rate of ~,* kima cha kubadilishana fedha. **foreign ~**, fedha za kigeni. *~ control,* udhibiti wa fedha za kigeni.

**exchequer** /ɪks'tʃɛkə, ɛks-/ *n.* wizara ya fedha; waziri wa fedha; hazina hasa huko Uingereza.

**excise**[1] /'ɛksʌɪz/ *n.* ushuru; kodi ya bidhaa. **excisable** *adj.* -enye kutozeka ushuru. **~man** *n.* mtoza ushuru; ofisa wa forodha.

**excise**[2] /ɪk'sʌɪz, ɛk-/ *v.t.* kata sehemu. **excision** *n.* ukataji sehemu.

**excite** /ɪk'saɪt/ *v.t.* sisimua; chochea. **excitable** *adj.* -epesi -a hisia; -enye kuweza kusisimuliwa. **excitability** *n.* uwezo wa kusisimka. **~ment** *n.* wasiwasi; msisimko; taharuki.

**exclaim** /ɪk'skleɪm/ *v.t./i.* shangaa. **exclamation** *n.* mshangao. *exclamation mark,* alama ya mshangao hii ( ! ).

**exclude** /ɪk'sklu:d/ *v.t.* zuia; tenga; toa. *~ sb. from membership of a club,* zuia mtu uanachama wa klabu. **exclusion** *n.* utoaji; utolewaji; uzuiaji. **exclusive** *adj.* pweke; zuifu; -liojitenga; -a watu maalumu. *exclusive of,* isipokuwa; minghairi; ghairi ya.

**excrement** /'ɛkskrɪm(ə)nt/ *n.* mavi; kinyesi; choo kikubwa; haja kubwa.

**excrete** *v.t.* kunya; toa takamwili; enda haja kubwa. **excretory system**, mfumo takamwili: mfumo wa maungo watumiayo wanyama changamano kutolea taka mwilini.
**excursion** /ɪk'skɜ:ʃn/ *n.* matembezi; safari; pikniki. ~ *ticket*, tiketi ya bei nafuu.
**excuse** /ɪk'skju:z, ɛk-/ *v.t.* samehe; wia radhi; ruhusu. ~ *oneself from a duty*, omba ruhusa ya kutofika kazini. *n.* sababu; udhuru; kisingizio.
**execute** /'ɛsɪkju:t/ *v.t.* **1.** tekeleza; timiza; fanya. **2.** ua; nyonga. **3.** tia saini; **4.** cheza; onyesha jukwaani. **executant** *n.* mtekelezaji jambo. **execution** *n.* utekelezaji; utimizaji; uchezaji; upigaji; uuaji; unyongaji; unyongwaji. **executioner** *n.* mnyongaji; muuaji.
**executive** /ɪg'zɛkjʊtɪv, ɛg-/ *adj.* -a utendaji; -enye amri, madaraka au mamlaka. *the* ~, serikali. ~ *order*, amri ya rais. **executor** *n.* kabidhi wasii; msimamizi wa mirathi. **executrix** *n.* kabidhi wasii mwanamke.
**exemplary** /ɪg'zemplərі/ *adj.* -a kupigiwa mfano; -enye kufaa kufuatwa. **exemplify** *v.t.* onyesha kwa mfano; -wa mfano.
**exempt** /ɪg'zɛm(p)t, ɛg-/ *v.t./adj.* samehe; ruhusu; achilia. **~ion** *n.* msamaha; ruhusa.
**exercise** /'eksəsaɪz/ *n.* matumizi; zoezi; mazoezi; drili. *the of patience*, subira; uvumilivu. ~ *of the body and its limbs*, mazoezi ya mwili na viungo vyake; mamacheza. *v.t./i.* zoeza; jizoeza; tumia, hangaisha; jaribu. ~ *patience*, subiri. *He was ~d about his faults*, alihangaishwa na makosa yake.
**exert** /ɪg'zə:t, ɛg-/ *v.t.* tumia; weka; wekea; gandamiza. ~ *oneself*, fanya juhudi; jitahidi. **~ion** *n.* bidii; juhudi; jitihada; utumiaji; ugandamizaji.
**exhale** /ɪks'heɪl, ɛks-/ *v.t./i.* toa pumzi; toa mvuke (harufu, uvundo); toka (kama mvuke, etc.).
**exhaust** /ɪg'zɔ:st, ɛg-/ *v.t.* maliza kabisa; toa -ote; ondoa -ote; tumia ote; chosha kabisa; chemua. *n.* ekzosi; chemuo. **~ion** *n.* mavune; uchovu; umalizikaji. **~ive** *adj.* kamilifu; timilifu.
**exhibit** /ɪg'zɪbɪt, ɛg-/ *v.t.* onyesha hadharani; tembeza; dhihirisha. *n.* maonyesho; kizibiti; ushahidi. **~ion** *n.* tamasha; maonyesho; uonyeshaji; udhamini apewao mwanafunzi shuleni au chuoni. *make an ~ of oneself*, jiaibisha; fanya vituko hadharani.
**exhilarate** /ɪg'zɪləreɪt, ɛg-/ *v.t.* changamsha; furahisha; tia moyo; sisimua. *exhilarating news*, habari za kusisimua.
**exile** /'eksaɪl/ *v.t.* fukuza; hamisha; kimbia kutoka nchi yake. *n.* ufukuzaji; uhamishaji; ukimbiaji kutoka nchi yake; mkimbizi.
**exist** /ɪg'zɪst/ *v.i.* -wa; ishi; -wako.
**exit** /'eksɪt/ *n.* mlango wa kutokea; utokaji.
**exocrine gland** *n.* tezi kemikali: tezi ambayo hutoa kemikali na kuziingiza katika sehemu maalumu ya kiumbe kupitia kwenye tyubu au uwazi maalumu badala ya mkondo wa damu.
**exonerate** /ɪg'zɒnərəɪt, ɛg-/ *v.t.* toa lawamani au hatiani kwa tamko rasmi ; achilia huru.
**exorbitant** /ɪg'zɔ:bɪt(ə)nt/ *adj.* (kwa bei au haja) -a kupita sana kiasi; kubwa mno.
**exoskeleton** *n.* kiunzinje: gamba au manyoya yanayofunika kiwiliwili cha mnyama. e.g. gamba la kaa.
**exothermic reaction** *n.* utendanaji toajoto: utendanaji unaotoa joto nje.
**expand** /ɪk'spand, ɛk-/ *v.t./i.* panua; eneza; panuka; enea; kuza; kunjua; funua; -wa -kunjufu. **expanse** *n.* eneo pana na wazi. **expansion** *n.* upanuzi; uenezi; mpanuko. **expansive** *adj.* enye kupanua; -enye kupanuka; -enye kuvimba; -pana sana; -kunjufu.
**expatriate** /ɪks'patrɪət/ *n./adj/v.t.* mtaalamu wa kigeni; mtu akaaye nje ya nchi yake; ondoka; kataa

uraia wako; ondosha na fukuza nchini.

**expect** /ɪk'spekt/ *v.t.* tazamia; tarajia. **~ancy** *n.* matarajio; matazamio; matumaini. **~ation** *n.* matazamio; matumaini; matarajio. *~ of life,* miaka mtu atumainiayo kuishi.

**expedient** /ɪk'spi:dɪənt, ɛk-/ *n./adj.* manufaa; faida; -a manufaa; -a kufaa.

**expedite** /'ɛkspɪdʌɪt/ *v.t.* harakisha; himiza.

**expedition** *n.* safari; hima; wepesi; haraka; msafara maalumu.

**expel** /ɪk'spel/ *v.t.* (**-ll-**) fukuza; ondosha; toa. **expulsion** *n.* ufukuzaji; uondoaji; utoaji.

**expend** /ɪk'spend/ *v.t.* tumia. **~iture** *n.* matumizi; gharama.

**expense** /ɪk'spens/ *n.* gharama. **expensive** *adj.* ghali.

**experience** /ɪk'spɪəriəns/ *n.* uzoefu; tajriba; maarifa; ustadi. *v.t.* pata uzoefu katika jambo; pitia. **~d** *n.* -zoefu; stadi.

**experiment** /ɪk'speriment/ *n.* jaribio. *v.i.* jaribu. **~al** *adj.* -a kujaribia; -a majaribio.

**expert** /'ekspɜ:t/ *n.* mzoefu; stadi; bingwa. *adj.* -zoefu; stadi; bingwa; mahiri. **~ise** *n.* ubingwa; ripoti ya tathmini. **~ly** *adv.* kistadi; kiufundi. **~ness** *n.* ustadi; ubingwa; umahiri.

**expire** /ɪk'spʌɪə, ɛk-/ *v.i.* **1.** koma; isha; malizika. **2.** vuta pumzi; pumua; -fa; kata roho. **expiration** *n.* uvutaji pumzi; umalizikaji. **expiry** *n.* kikomo. *expiry date,* tarehe ya mwisho ya matumizi.

**explain** /ɪk'spleɪn/ *v.t./i.* eleza; fasiri; fasili; fafanua. *~ oneself,* jieleza. **explanation** *n.* maelezo; ufafanuzi; tafsiri; fasili. **explanatory** *adj.* -a kueleza; fafanuzi.

**explicit** /ɪk'splɪsɪt, ɛk-/ *adj.* wazi; dhahiri; bayana. **~ly** *adv.* waziwazi; bayana.

**explode** /ɪk'spləʊd/ *v.t./i.* ripua; ripuka; tengua; haribu. *~ with laughter,* angua kicheko. *~ with rage, anger,* pasuka kwa hamaki.

**explosion** *n.* mripuko. **explosive** *n./adj.* -enye kuripuka; baruti.

**exploit**[1] /ɪk'splɔɪt, ɛk-/ *v.t.* tumia; tumilia; nyonya; chimba madini; endeleza nguvu za asili. **~ation** *n.* unyonyaji; utumiaji; uendelezaji; ukandamizaji.

**exploit**[2] /ɪk'splɔɪt, ɛk-/ *n.* tendo la ujasiri.

**explore** /ɪk'splɔ:(r)/ *v.t.* peleleza; vumbua; talii; tafiti; gundua; chunguza. **~r** *n.* mpelelezi; mgunduzi; mchunguzi; mtafiti; mvumbuzi. **exploration** *n.* upelelezi; uvumbuzi; ujasusi; uchunguzi.

**exponential growth** *n.* ongezeko nambakipeo: ongezeko fulani la kasi ambalo hutegemea idadi ya viumbe vilivyopo.

**export** /ɪk'spɔ:t, ɛk-, 'ɛk-/ *v.t.* kuuza au kusafirisha bidhaa nchi nyingine. *n.* bidhaa za nje. **~ation** *n.* usafirishaji bidhaa nje.

**expose** /ɪk'spəʊz/ *v.i.* funua; weka wazi; fichua; ingiza mwanga; hatarisha; chongea; onyesha. **exposure** *n.* uwazi; uingiaji mwangaza; ufunuaji; ufunukaji.

**express** /ɪk'sprɛs, ɛk-/ *v.t.* eleza; onyesha; dhihirisha; simulia; peleka kwa njia ya haraka. *~ one's feelings,* eleza hisia zako. *adj.* halisi; dhahiri; -a haraka; muhimu. *an ~ command,* agizo muhimu. *an ~ train,* treni ya mwendo wa kasi. *adv.* kwa haraka. **~ion** *n.* usemi; neno; sura. **~ive** *adj.* -enye kuonyesha hisia; -a maana; -enye kuelezea.

**exquisite** /'ɛkskwɪzɪt, ɪk'skwɪzɪt, ɛk-/ *adj.* bora sana; -kali sana; tamu sana. *n.* mmaridadi; mlimbwende; mtanashati.

**extant** /ɪk'stant, ɛk-, 'ɛkst(ə)nt/ *adj.* -liopo.

**extend** /ɪk'stend/ *v.t./i.* nyoosha; ongeza; refusha; tandaza; enea; ongeza. **extension** *n.* nyongeza; upanuzi; uenezi. *an ~ to a hotel,* sehemu iliyoongezwa ya hoteli. **extensive** *adj.* -enevu; -kubwa; -pana. **extent** *n.* urefu; eneo; kiasi. *to a certain extent,* kwa

kiasi fulani.

**extenuate** /ɪk'stɛnjʊeɪt, ɛk-/ *v.t.* punguza ukubwa au makali ya kosa. **extenuation** *n.* udhuru wa kupunguza ukubwa wa kosa.

**exterior** /ɪk'stɪəriə(r)/ *adj./n.* -a nje; umbo la nje; sura.**~ angles**, pembe za nje.

**exterminate** /ɪk'stə:mɪneɪt, ɛk / *v.t.* maliza; ua -ote; teketeza; angamiza. **extermination** *n.* maangamizi.

**external** /ɪk'stɜ:nl/ *adj.* -a nje; -lio nje.

**extinct** /ɪk'stɪŋt/ *adj.* -liotoweka; -liozimika; -siyokuwepo tena. **~ion** *n.* kufa; kuzimika; kutoweka; kutokuwepo tena. *~ volcano,* volkano zimwe.

**extinguish** /ɪk'stɪŋgwɪʃ/ *v.t.* zima; komesha; haribu; futa. **~er** *n.* kizimamoto.

**extort** /ɪk'stɔ:t, ɛk / *v.t.* toza au lipisha kwa nguvu; pora; nyang'anya; pokonya. **~ion** *n.* uporaji; unyang'anyi; toza bei kubwa mno.**~ionate** *adj.* -a kutaka -ingi kupita kiasi; ghali mno; poraji; -nyang'anyi.

**extra** /'ekstrə/ *adj.* -a ziada; -a nyongeza. *adv.* zaidi. *~ special,* -zuri zaidi. *n.* ziada; nyongeza.

**extract** /ɪk'strakt, ɛk-/ *v.t.* ng'oa; ondoa; toa; kongoa; chopoa; sindika; dondoa; zidua. *n.* kiziduo; dondoo; sehemu. **~ion** *n.* uziduaji; utoaji; udondoaji; usindikaji; asili. *of African ~ion,* -a asili ya Kiafrika.

**extradite** /'ɛkstrədʌɪt/ *v.t.* rudisha mhalifu katika nchi aliyofanya makosa ili akahukumiwe. **extradition** *n.* urudishaji mhalifu namna hiyo.

**extraordinary** /ɪk'strɔ:d(ə)n(ə)ri, ɛk-, ˌɛkstrə'ɔ:dɪn(ə)ri/ *adj.* -a ajabu; si -a kawaida; -a pekee; -a dharura. *~ beauty,* uzuri wa ajabu; *~ meeting,* mkutano wa dharura.

**extravagant** /ɪk'stravəg(ə)nt, ɛk-/ *adj.* -badhirifu; -a kupita kiasi. **extravagance** *n.* ubadhirifu. **~ly** *adv.* kibadhirifu.

**extreme** /ɪk'stri:m/ *adj.* mno; kabisa; -a kupindukia mpaka. *n.* mwisho; upeo; kipeo; ncha. *the ~ s of heat and cold,* vipeo vya joto na baridi. *go to ~s,* zidi; vuka mpaka. **extremist** *n.* -enye siasa kali. **extremity** *n.* ncha; kikomo; mpaka; upeo; mwisho; *(pl.)* **1.** mikono na miguu. **2.** vitendo vya kikatili; hali ngumu na mashaka.

**extricate** /'ɛkstrɪkeɪt/ *v.t.* toa; okoa; nasua. **extrication** *n.* uokoaji; uokokaji; unasuaji.

**extrude** /ɪk'stru:d, ɛk-/ *v.t.* toa nje; sukumia nje; toka nje; tokeza nje.

**exult** /ɪg'zʌlt/ *v.i.* furahia sana; shangilia sana. **~ant** *adj.* -a furaha nyingi; -a shangwe. **~ation** *n.* furaha kuu; shangwe.




**eyeball | soketi ya jicho**

**eye** /aɪ/ *n.* jicho; tundu ya sindano. *see ~ to ~ (sb.),* patana naye. *have an (a good) ~ for,* elewa; jua sana. *with an ~ to,* -enye kutumaini. *make ~ s at,*jipendekeza kwa; jikomba. **~ball** *n.* soketi ya jicho. *v.t.* tazama. **~sore** *n.* kitu kilicho kisichopendeza machoni. **~witness** *n.* shahidi aliyeshuhudia tukio kwa macho yake.

# Ff

**fable** /ˈfeɪb(ə)l/ *n.* ngano fupi; hekaya za maadili aghlabu wanyama huwa wahusika wakuu; habari za uzushi. e.g. *Aesop's ~s.* **fabulous** *adj.* -a kubuni; -a uzushi; -a uongo.

**fabric** /ˈfæbrɪk/ *n.* kitambaa; kiunzi; mfumo; jengo. **~ate** *v.t.* jenga; zua; buni; tunga; ghushi; tengeneza. **~ation** *n.* uzushi; uwongo; jengo.

**facade** /fəˈsɒ:d/ *n.* upande wa mbele wa nyumba.

**face** /feɪs/ *n.* uso; sura; wajihi; upande wa mbele. *make (pull) a ~ (at),* kunjia uso; geuza uso. *save ones ~,* jiepusha na aibu. *the ~ of a clock,* uso wa saa. *~ value,* thamani iliyoandikwa. *on the ~ of it,* kama inavyoonekana. *v.t./i.* tazama; elekea; kabili; tomea. *~ the music,* kabili hatari. *~ it out,* kabili kishujaa. *a stone wall ~d with cement,* ukuta wa mawe uliotomewa kwa saruji. **facial** *adj.* -a uso.

**facile** /ˈfasʌɪl,-sɪl/ *adj.* -epesi; rahisi; sahili; kufanyika au kupatikana; -a juujuu tu; -pole. **facilitate** *v.t.* rahisisha; saidia; sahilisha. **facility** *n.* urahisi; wepesi; kifaa; nyenzo; welekevu; upole.

**fact** /fækt/ *n.* jambo la hakika; kweli; hakika. *in (point of) ~, as a matter of ~,* kwa kweli. **~ual** *adj.* -enye ukweli.

**faction** /ˈfækʃn/ *n.* kikundi ndani ya kundi kubwa; ugomvi baina ya vikundi vya kundi moja. **factious** *adj.* - a ugomvi wa mgawanyiko.

**factor** /ˈfæktə(r)/ *n.* sababu; kipengele; kigawo; kigawanyo; zao mtiririko; e.g. 2, 3, 4, 6 ni vigawanyo vya 12.

**factory** /ˈfæktri; teri/ *n.* kiwanda; karakana; banda la kazi.

**faculty** /ˈfæklti/ *n.* welekevu (ustadi, uwezo) wa kufanya jambo; nguvu; akili; kitivo cha chuo kikuu.

**fade** /feɪd/ *v.t./i.* fifisha; chujusha; fifia; chujuka; chakaa; pauka; paua; punguza; pungua.

**faeces** /ˈfi:si:z/ *n.* kinyesi: mabaki ya chakula ambacho haki-kumeng'enywa.

**fail** /feɪl/ *v.i.t.* shindwa; feli; felisha; kosekana; haribika; dhoofika; sahau kufanya; filisika. *He ~ed me,* alishindwa kutinimizia ahadi. *Come without ~,* usikose kuja. **~ing** *n.* kasoro; dosari. **~ure** *n.* ushinde; kutofaulu; ukosefu; mkosefu; ufilisikaji.

**faint** /feɪnt/ *adj.* dhaifu; -sioonekana vyema; si dhahiri; -a kuzimia; -nyonge. *v.i.* zimia; zirai; fifia; dhoofu. *n.* uzimiaji; kuzirai. *in a dead ~,* zirai kabisa. **~ly** *adv.* kidogo kidogo. **~-hearted** *adj.* -oga.

**fair**[1] /feə(r)/ *adj.* -a haki; -adilifu; -zuri; -eupe; safi. *a ~ chance,* bahati nzuri. *~ weather,* hali ya hewa nzuri. *the ~ sex,* wanawake. *~ copy,* nakala safi. *~ name,* sifa njema. **~ly** *adv.* kwa haki; kidogo. *speak Kiswahili ~ well,* zungumza Kiswahili vizuri kidogo. **~ness** *n.* haki; usawa.

**fair**[2] /feə(r)/ *n.* soko lifunguliwalo katika vipindi maalumu; tamasha; maonyesho. *a day before the ~,* mapema mno. *~ ground,* uwanja wa maonyesho. *international trade fair,* maonyesho ya biashara ya kimataifa.

**fairy** /ˈfeəri/ *n.* pepo; jini; zimwi; kibwengo. **~ tale** *n.* ngano za mazimwi; ngano.

**faith** /feɪθ/ *n.* imani; itikadi; dini; ahadi; miadi; utiifu; uaminifu. *in good ~,* kwa nia safi; *in bad ~,* kwa nia mbaya. **~ful** *adj.* amini; -aminifu. **~fully** *adv.* kwa uaminifu. **~less** *adj.* -danganyifu; -ongo.

**fake** /feɪk/ *v.t./adj./n.* iga; ghushi; mwigo; -a bandia.

**fall** /fɔ:l/ *v.i.* anguka; poromoka; tekwa; punguka; nyesha; shuka; pukutika. *~ in love (with),* penda. *~ asleep,* sinzia; lala. *~ shot (of),* punguka. *~ back,* enda nyuma; rudi. *~ back on,* rudia kutumia badala ya -ingine -isiyofaa. *~ in,* jipanga. *~ in with,* kubaliana na. *~ off,* punguka. *~ on,* shambulia. *~ out with.*

gombana. *it fell out that,* ilitokea kwamba. ~ *through,* tanguka. ~ *to,* shika jambo. **falling star** *n.* kimondo: gimba la kumetameta kutoka anga za mbali ambalo huweza kuanguka kwenye uso wa dunia. *n.* uangukaji; maporomoko; upungufu; kosa; mteremko.

**fallacy** /'faləsi/ *n.* kosa; uwongo; hoja ya uwongo; dhana yenye kosa. **fallacious** *adj.* -a uwongo; -enye kupotosha; -danganyifu.

**fallible** /'falɪb(ə)l/ *adj.* -a kuweza kukosa; -a kuweza kuwa na kosa.

**fallopian tube** *n.* neli ya falopi: neli inayounganisha ovari na uterasi.

**fallow** /'fæləʊ/ *n./adj.* iliyolimwa na kuachwa bila kupandwa; -a kulimwa na kuachwa bila kupandwa kwa mwaka mzima.

**false** /fɔ:ls/ *adj.* si kweli; -a uwongo; si halisi; -danganyifu; -nafiki; -a bandia. *adv.* kwa udanganyifu. *play sb.* ~, haini; danganya. **~ly** *adv.* kiudanganyifu. **~hood** *n.* uwongo; uzushi.

**falsify** /'fɔ:lsɪfʌɪ/ *v.t.* **1.** danganya; ghushi; potosha.~ *fears,* -wa kinyume cha vile ulivyoogopa. **falsification** *n.* uwongo; udanganyifu.

**falter** /'fɔ:ltə, 'fɒl-/ *v.i.* sita; sema kwa kigugumizi.

**fame** /fem/ *n.* umaarufu; sifa. *house of ill* ~, danguro.

**familiar** /fə'mɪliə(r)/ *adj.* mashuhuri; -zoefu; -a siku zote; -a kawaida. *be* ~ *with,* jua sana. ~ *friend,* msiri; sahibu; rafiki wa ndani. *over* ~, -enye kujipendekeza. **~ity** *n.* mazoea; utani; uzoefu; urafiki. **~ize** *v.t.* zoeza; tangaza; eneza.

**family** /'fæməli/ *n.* familia; jamaa; ahali; aila; ukoo; nasaba. *a person of* ~, mtoto wa watu. *be in the* ~ *way,* -wa mja mzito.

**famine** /'famɪn/ *n.* njaa. **famish** *v.i./t.* ona njaa sana; shindisha na njaa.

**famous** /'feɪməs/ *adj.* maarufu; mashuhuri.

**fan**[1] /fæn/ *n.* feni; upepeo; kipepeo. *v.t./i.* (**-nn-**) pepea; peta; pepeta; punga.



fan

**fan**[2] /fæn/ *n.* *(colloq.)* shabiki. *film ~s,* mashabiki wa sinema.

**fanatic** /fə'natɪk/ *n./adj.* mlokole; mtu ashikiliaye sana jambo, imani au itikadi bila kuhoji undani wake. **~al** *adj.* -a kilokole; -a kukithiri. **~ism** *n.* ulokole.

**fancy** /'fænsi/ *n.* wazo; fikira; ndoto; shauku; dhana. *adj.* -liorembewa; -a kupendeza macho; ghali sana. ~ *dress,* vazi la fahari. *v.t.* waza; dhani; hisi; fikiri; penda. ~ *oneself,* jiona. **fanciful** *adj.* -bunifu; -a umbo la ajabu; -dhanifu; -a njozi. **~-work** *n.* darizi.

**fang** /faŋ/ *n.* chonge; jino refu; jino lenye sumu la nyoka.

**fantastic** /fæn'tæstik/ *adj.* -a ajabu; -a kutisha; -a kuchekesha; -a kuwazika tu. **~ally** *adv.* kiajabu; kimawazo tu.

**far** /fɑ:(r)/ *adv.* **1.** mbali. *in so ~ as, as ~ as,* kwa kadiri. ~ *and away better,* sana. *adj.* -a mbali. *be a ~ cry (from),* -wa mbali sana (kutoka). **~-away** *adj.* -a mbali sana. **~-fetched** *adj.* -sioingia akilini; -sioaminika. **~-off** *adj.* ya mbali sana. **~-reaching** *adj.* -enye athari nyingi. **~-seeing**, **~-sighted** *adj.* *(fig.)* -enye kuona mbali; -enye kuona mbele.

**fare** /feə(r)/ *n.* **1.** nauli; uchukuzi. **2.** mlo. *bill of* ~, orodha ya vyakula. *v.i.* safiri; endelea; enda: *How did you ~?* uliendeleaje? *He ~d well,* alifanikiwa. **~well** *int.* kwaheri. *n.* maagano; buriani. *bid ~well,* agana; peana buriani.

**farm** /fɑ:m/ *n.* shamba; konde. ~ *house,* nyumba ya mkulima shambani. *v.t./i.* lima; fuga. ~ *out,* limisha. **~er** *n.* mkulima; mfugaji. **~ing** *n.* ukulima.

**fascinate** /'fæsɪneɪt/ *v.t.* vutia sana. **fascination** *n.* kivutio; uzuri; mvuto.

**fashion** /'fæʃn/ *n.* mtindo. *the Zanzibar ~s,* mitindo ipendwayo

Zanzibar. *changes of ~*, mabadiliko ya mitindo. *out of ~*, zilipendwa. *in ~*, -a mtindo wa kisasa. *be have in a strange ~*, -wa na tabia ngeni. *after a ~*, kulingana na mtindo. *v.t.* umba; tengeneza; unda. **~able** *adj.* -a mtindo; -a siku hizi. *a ~ hotel*, hoteli ya kisasa. **~ably** *adv.* kimtindo.

**fast**[1] /fɑ:st/ *adj.* **1.** imara; madhubuti. **2.** -aminifu. **3.** -a kudumu. *adv.* imara. *be ~ asleep*, lala foo. *play ~ and loose with*, badilisha msimamo mara kwa mara. *stand ~*, simama imara; kataa kuyumbishwa.

**fast**[2] /fɑ:st/ *adj.* -epesi ; -a haraka; -badhirifu; -a anasa; -enye kukimbia. *adv.* upesi; haraka; hima. *rain ~*, nyesha sana. *live ~*, ishi kianasa.

**fast**[3] /fɑ:st/ *v.i.* funga: (kidini) kujizuia kula na kunywa na mambo mengine yaliyokatzwa wakati wa kufunga. *n.* funga; mfungo; saumu. *break one's ~*, futuru; funguza; fungua saumu.

**fasten** /fɑ:sn/ *v.t./i.* funga; fungika; kaza. *~ upon*, shikilia. **~er** , **~ing** *n.* kifungio; mfungo. *a zip fastner*, zipu.

**fat** /fæt/ *n.*mafuta; shahamu; uto. *live on the ~ of the land*, ishi maisha ya anasa. *adj.* -enye mafuta; - nene; -nono; -liojaa. **~-head** *n.* mpumbavu. **~ten** *v.t. /i.* nonesha; nenepa; nona.

**fatal** /'feɪt(ə)l/ *adj.* -a kuua; -a ajali. **~ly** *adv. ~ wounded*, -liojeruhiwa vibaya mno. **~ism** *n.* kuamini kuwa matukio yote ya maishi ni ya kiajali hivyo binadamu hana nguvu za kuyazuia wala kuyaepuka. **~ist** *n.* mtu anayeamini hivyo. **~istic** *adj.* -a imani hiyo. **~ity** *n.* ajali; mauti.

**fate** /feɪt/ *n.* majaliwa; jaala; amri ya Mungu. mauti; maangamizi. **~d** *adj.* -a ajali; -lioandikwa. **~ful** *adj.* -a jaala; -a majaliwa.

**father** /'fɑ:ðə(r)/ *n.* **1.** baba. *adoptive ~*, baba wa kupanga. *putative ~*, baba wa kudhaniwa. *step ~*, baba wa kambo. **2.** kasisi; padre. **3.** mwanzilishi; kiongozi wa awali. *~ of the nation*, baba wa taifa.*v.t.* asisi. *~ sth. on. sb.*, singizia. **~-in-law** *n.* mkwe mwanamme. **~ly** *adj.* -a baba au -a kama baba.

**fathom** /'fæðəm/ *n.* pima; futi sita; mita **1.8.** *v.t.* pima kina cha; elewa. **~less** *adj.* -siopimika kina; sioleweka.

**fatigue** /fə'ti:g/ *n.* uchovu; mavune; kazi ya sulubu. *v.t.* chosha.

**fault** /fɔ:lt, fɒlt/ *n.* kosa; dosari; hitilafu; ila; kasoro. *find ~ with*, lalamikia. *be at ~*, sitasita. *It's your own ~*, ni kosa lako mwenyewe. **~less** *adj.* bila kosa; kamili. **~y** *adj.* -enye kosa. **~ily** *adv.* kimakosa.

**fauna** /'fɔ:nə/ *n.* fauna: jumla ya wanyama wote katika mazingira fulani.

**favour** /'feɪvə(r)/ *n.* fadhila; hisani; wema; jamala. *in ~ of*, kwa upande wa; kwa faida ya; kwa ajili ya. *do me a ~*, nisaidie. *v.t.* pendelea; unga mkono; fadhili. **~able** *adj.* -enye kufaa; -enye kusaidia. **~ably** *adv.* kwa kufaa; kwa kupendeza. **~ite** *n./adj.* kipenzi; mpenzi. **~itism** *n.* upendeleo.

**fax** /fæks/ *n* . nukushi. *~ machine*, nukunishi.

**fear** /fɪə(r)/ *n.* hofu; woga; uchaji. *the ~ of God*, ucha Mungu. *v.t./i.* ogopa; chelea; hofu; -cha; chelea. **~ful** *adj.* -a kuogofya; -a kutisha; -oga. **~fully** *adj.* kwa woga. **~less** *adj.* jasiri; shupavu; bila woga.

**feasible** /'fi:zɪb(ə)l/ *adj.* -enye kuwezekana; enye kuyumkinika; **feasibility** *n.* uwezekano. *feasibility study*, uchunguzi yakinifu.

**feast** /fi:st/ *n.* sikukuu; karamu; dhifa. *v.t./i.* kirimu; -la karamu. **festival** *n.* sikukuu; sherehe; tamasha.

**feat** /fi:t/ *n.* tendo kubwa la ujasiri lililofanikiwa.

**feather** /'feðə(r)/ *n.* unyoya. *birds of a ~*, watu wa namna moja. *show the white ~*, onyesha hofu. *in high ~*, kwa furaha. *v.t.* tia manyoya. *~ one's nest*, jitajirisha. **~y** *adj.* -enye manyoya; laini; -epesi.

**feature** /'fi:tʃe(r)/ *n.* wasifu; sura; sifa; makala katika gazeti; filamu

ndefu. *v.t.* onyesha.
**February** /'fɛbrʊəri, 'fɛbjʊəri/ *n.* Februari: mwezi wa pili wa mwaka wa kizungu.
**federal** /'fedərəl/ *adj.* -a shirikisho; -a kuhusu serikali ya shirikisho. **~ism** *n.* ushirikishaji. **federate** *v.t./i.* unganisha; ungana kuwa shirikisho. **federation** *n.* shirikisho; uundaji wa shirikisho.
**fee** /fi:/ *n.* ada; karo; kiingilio. *estate in ~ simple,* mali inayorithiwa bila ya masharti yoyote.
**feeble** /'fi:bl/ *adj.* dhaifu; goigoi; hafifu. **feebly** *adv.* kidhaifu.
**feed** /fi:d/ *v.t./i.* (**fed**) lisha; -la; jilisha. *be fed up with,* choshwa na. *~ing bottle,* chupa ya kunyonyeshea. *n.* chakula; malisho.
**feel** /fi:l/ *v.t./i.* (**felt**) papasa; gusa; tomasa; hisi; ona. *~ like doing sth.,* taka kufanya kitu. *~ for,* hurumia. *~ sure,* -wa na hakika. *n.* hisia; msisimko; mguso. **~er** *n.* papasi; jambo. **~ing** *n.* hisia; huruma; chuki. *a ~ of comfort,* hisia ya faraja. *hurt a man's ~s,* udhi mtu. *~ for art, beauty, etc.* penda sana sanaa, uzuri. *adj.* - enye huruma; -ema.
**felicity** /fə'lɪsəti/ *n.* heri; furaha kuu; nyemi; suudi; baraka; ufasaha; maneno fasaha.
**fell** /fel/ *v.t.* angusha; kata mti. *run and ~ a seam in sewing,* piga bandi.
**fellow** /'feləʊ/ *n.* **1.** *(colloq.)* mtu; jamaa. **2.** mwenza; mshiriki. **3.** msomi; mwanazuoni. *adj.* -a namna moja. *~ citizen,* mwananchi mwenzio. *~ passengers,* abiria wenzako. **~-feeling** *n.* huruma. **~ship** *n.* ushirika; urafiki; uanachama; uanazuoni.
**felt** /felt/ *n.* kitambaa cha manyoya ya mnyama yaliyogandamizwa kwenye kitu kingine kwa gundi.
**female** /'fi:meɪl/ *adj.* -ke; -a mwanamke; -a kike. *n.* mke; mwanamke; jike.
**feminine** /'femənɪn/ *adj.* -a kike; -ke. **feminism** *n.* harakati za kuleta haki na usawa wa kijinsia kwa wanawake. **feminist** *n.* mshabiki wa harakati hizo.

**fence**[1] /fens/ *v.t.* zungushia ua, boma au seng'enge. *n.* boma; ua; seng'enge.
**fence**[2] /fens/ *v.i.* **1.** cheza kwa panga au vitara. **2.** *(fig.)* epuka kujibu swali. **fencing** *n.* uwa; vifaa vya kujengea uwa; mchezo wa panga.



**fenches**

**fend** /fend/ *v.t./i.* *~ off,* kinga; linda; jilinda; epusha. **2.** *~ for,* tunza; kimu; ruzuku.
**ferment** /fə'ment/ *v.t./i.* vundika; umua; chachuka; umuka. *n.* uchachu; chachu; hamira. *be in a ~,* *(fig.)* fujika; chafuka; kasirika. **~ation** *n.* uchachukaji; uumukaji; mchachuko.
**fern** /fɜ:n/ *n.* jamii ya mimea: dege la watoto; mkangaga; madole matano.



**fern**

**ferocious** /fə'rəʊʃəs/ *adj.* -a kali; katili. **ferocity** *n.* ukali; ukatili.
**ferret** /'ferɪt/ *n.* mnyama kama cheche au nguchiro. *v.t./i.* winda kwa kutumia mnyama huyo. *~ out sth.,* chunguza; peleleza.
**ferric** /'fɛrɪk/ *n.* feria: ioni ya feri yenye chaji chanya tatu.
**ferrous** /'fɛrəs/ *n.* ferasi: ioni ya feri yenye chaji chanya mbili.
**ferry** /'feri/ *n.* kivuko; feri. *v.t./i.* vusha; vuka; safirisha. **~ boat** *n.* boti ya kuvushia. **~man** *n.* mvushaji. **~ pontoon** *n.* pantoni.
**fertile** /'fə:tʌɪl/ *adj.* -enye rutuba; -zazi; -enye akili za kivumbuzi; -enye kuzaa sana. **fertility** *n.*rutuba; uzaaji. **fertilize** *n.* rutubisha; tungisha mimba.
**fertilization** /ˌfɜ:təlaɪzeɪʃn/ *n.* urutubishaji; utungishaji.
**fertilizer** /'fɜ:təlaɪzə(r)/ *n.* mbolea.
**fervent** /'fə:v(ə)nt/ *adj.* -enye joto; -enye kuwaka; enye ari; -enye hamasa; -enye shauku. **fervency** *n.* juhudi; bidii. **fervid** *adj.* -enye bidii; enye hamasa; -enye ari. **fervour** *n.* bidii; ari; hamasa; moyo wa bidii; nguvu.

**fester** /'festə(r)/ *v. i./t.* **1.** tunga usaha. **2.** kasirisha; kereketa moyoni.
**festive** /'festɪv/ *adj.* -a sikukuu; -a sherehe; -kunjufu; changamfu. **festivity** *n.* shangwe; furaha; shamrashamra. *wedding festivities,* shamrashamra za arusi.
**fetch** /fetʃ/ *v.t./i.* leta; toza; (kwa bidhaa) uzwa kwa; pata.
**fête** /feɪt/ *n.v.t.* fete; sikukuu; tamasha; shangilia; sherehekea.
**fetish**, **fetich** /'fɛtɪʃ/ *n.* miungu ya sanamu; mizimu. **~ism** *n.* imani ya masanamu au mizimu.
**fetter** /'fetə(r)/ *n.* pingu za miguu; kizuizi. *v.t.* tia pingu; zuia. *make a ~ of,* penda mno; husudu.
**fever** /'fi:və(r)/ *n.* homa; wasiwasi. *yellow ~,* homa ya manjano. **~ish** *adj.* -enye homa; -enye wasiwasi.
**few** /fju:/ *adj./n.* -chache; haba. *a ~ of,* baadhi.
**fez** /fɛz/ *n.* tarbushi; tunga.
**fiancé(e)** /fɪɒnseɪ/ *n.* mchumba mwanamme; mchumba mwanamke.
**fibre** /faɪbə(r)/ *n.* uzi. **fibrous** *adj.* -a nyuzinyuzi.
**fiction** /'fɪkʃn/ *n.* hadithi ya kubuni; riwaya; habari ya kubuni. **fictitious** *adj.* -a kubuni; -a uwongo.
**fiddle** /'fɪdl/ *n.* fidla; udi. *be fit as a ~,* -wa mzima sana; *play second ~,* -wa msaidizi. *v.t./i.* piga fidla; piga udi; chezacheza na; chezeachezea. **~sticks** *int.* upuuzi mtupu.
**fidelity** /fɪ'dɛlɪti/ *n.* uaminifu.
**fidget** /'fɪdʒɪt/ *v.t./i.* chezacheza; totulia; sumbua; hangaika.
**field** /fi:ld/ *n.* konde; shamba; uwanja; tawi la taaluma; machimbo; eneo; mbuga ya malisho. *rice ~,* shamba la mpunga. *landing ~,* eneo la kutulia ndege. *~ events,* mashindano ya michezo isipokuwa ya mbio. *v.i./t.* -wa tayari kudaka au kuzuia mpira. **~-glasses** *n.* darubini; bainokula. **~-marshal** *n.* jemadari mkuu; amirijeshi mkuu.
**fierce** /fɪəs/ *adj.* -kali; -a nguvu; katili. **~ly** *adv.* kwa ukali; kwa ukatili. **~ness** *n.* ukatili; ukali; nguvu.
**fiery** /'faɪəri/ *adj.* -a moto; -kali; -a joto; -enye hasira.
**fifteen** /ˌfɪfti:n/ *n./adj.* kumi na -tano. **fifty** *n./adj.* hamsini. *the fifties,* miaka ya 50.
**fig** /fig/ *n. ~ tree,* mtini; *~ fruit,* tini. *don't care a ~,* haidhuru hata kidogo, haina faida yoyote.
**fight** /faɪt/ *v.t./i.* (**fought**) pigana. *~ shy of,* epukana na. *~ it out,* pambana hadi suluhu ipatikane. *n.* vita; mapigano; mapambano. **~er** *n.* ndege ya kivita; mpiganaji; mwanamasumbwi.
**figure** /'fɪgə/ *n.* **1.** tarakimu. **2.** bei. *buy sth. at a low ~,* nunua kitu kwa bei ndogo. **3.** umbo. *have a fine ~,* -wa na umbo zuri. **4.** mtu mashuhuri. *Nyerere is a great ~ of our times,* Nyerere ni mtu mashuhuri wa zama zetu. **5.** sanamu ya kuchonga au ya kuchora. *~ of speech,* tamathali ya usemi. **6.** mchoro; kielelezo; chati; ramani. *v.i./t.* **1.** jitokeza; onekana; onyesha; -wa mashuhuri. **2.** hesabu; fikiria; elewa. **3.** onyesha kwa picha au sanamu. **~head** /'fɪgəhed/ *n.* kiongozi asiye na madaraka ya maamuzi yoyote ya maana; sanamu ya kuchonga ya kichwa na kifua itumikayo kama pambo.
**filament** /'fɪləm(ə)nt/ *n.* filamenti: nyaya nyembamba ndani ya balbu.
**file**[1] /faɪl/ *n.* jalada; faili. *v.t.* hifadhi katika jalada; faili; sajili; andikisha jambo mahakamani.
**file**[2] /faɪl/ *n.* tupa. *v.t.* piga tupa; chonga; kata kwa tupa. **filings** *n.* vumbitupa.
**file**[3] /faɪl/ *n.* safu. *v.i.* fuatana, andamana katika safu. *~ in,* ingia kwa safu. *~ out,* toka kwa safu. *in single ~,* chanjari. *the rank and ~,* askari wasiokuwa maofisa; watu wa kawaida.
**fill** /fɪl/ *v.t./i.* jaza; jaliza; jaa. *~ out,* nenepa; tanuka; vimba. **filling station** *n.* kituo cha petroli. *n.* kijazi; kijazo; shibe; shehena. *eat one's ~,* shiba.

**film** /fɪlm/ *n.* utando; filamu; sinema. *v.t./i.* tanda; piga picha ya sinema; tandaza. **~ star**, mcheza sinema nyota. **~y** /'fɪlmi/ *adj.* -mbamba; -a utando; -epesi.

**filter** /'fɪltə(r)/ *n.* chujio; kichujio; kung'uto. *v.t./i.* chuja; *(fig.)* penya; sambaa; ingia; enea; rishai; vuja. ~ *feeder*, mchujaji: mnyama yoyote ambaye hupata chakula chake kwa kuchuja viumbe wadogowadogo kutoka kwenye maji. **filtration** *n.* uchujaji: mfanyiko wa kutenganisha mango kutoka kwenye kioevu kwa kutumia chujio.

**filth** /fɪlθ/ *n.* uchafu; taka; kinyaa; najisi. **~thy** *adj.* -chafu; najisi. **~ily** *adv.* kichafu.

**fin** /fɪn/ *n.* pezi la samaki. **~ny** *adj.* -enye mapezi. *tail ~*, mkia wa ndege.

**final** /'faɪnl/ *adj.* -a mwisho; a kukata maneno. *n.* mtihani wa mwisho; fainali. **~e** *n.* a mwisho katika mfululizo. **~ly** *adv.* mwishowe; hatimaye.

**finance** /fʌɪ'nans/ *n.* usimamizi wa fedha; fedha za serikali kampuni. **~ company**, kampuni ya kushughulikia gharama za fedha. *v.t.* gharimia. **financial** *adj.* -ya fedha. ~ *year*, mwaka wa fedha. **financier** *n.* mtaalamu wa mambo ya fedha; mgharimiaji; mdhamini.

**find** /faɪnd/ *v.t.* (**found**) **1.** ona; pata; kuta. ~ *one's feet*, (kwa mtoto) anza kutembea; anza kujitegemea katika mambo yako. **2.** tafuta. ~ *a solution to the problem*, tafuta ufumbuzi kwa tatizo. **3.** tafiti; hakikisha; chunguza. **4.** gundua; kuta kwa bahati. *He found a treasure*, aligundua kasiki la mali.~ *favour with*, kubalika. **5.** hukumu; amua. ~ *for*, amua kutoa ushindi kwa. **~ing** *n.* matokeo ya uchunguzi; uamuzi wa mahakama.

**fine** /fʌɪn/ *n.* faini; fidia. *v.t.* toza faini. *adj.* -zuri; -embamba; -kali; laini; -ororo; safi. **~ art(s)**, sanaa za uchoraji. *call sb. by ~ names*, ita mtu kwa kutumia tasfida.

**finger** /'fɪŋgə(r)/ *n.* kidole; chanda. *have a ~ in*, shiriki. *burn one's ~s*, pata matatizo. **~ alphabet**, mfumo wa ishara wa alfabeti kwa vidole wa kuzungumza na viziwi. *v.t.* tia vidole; papasa; tomasa; gusa. **~-print** *n.* alama ya kidole.

**finish** /'fɪnɪʃ/ *v.t./i.* maliza; timiza; hitimisha; kamilisha. *n.* mwisho; ukamilifu.

**finite** /'fʌɪnʌɪt/ *adj.* -enye mpaka au kikomo; -enye kukubaliana kiima, kiidadi na pia kinafsi. ~ *state grammar*, sarufi miundo ukomo. ~ *verb*, kitenzi ukomo.

**fire** /'faɪə(r)/ *n.* **1.** moto. **2.** mlio wa bunduki. **3.** hasira; hasara. *v.t./i.* **1.** washa moto; unguza; choma; teketeza; kaanga; oka katika tanuri. **2.** piga silaha yoyote ya risasi. **3.** *(colloq.)* fukuza (mtumishi). **~ alarm** *n.* king'ora. **~arm** *n.* silaha ya risasi. **~brand** *n.* fitina; mchochezi; kijinga cha moto. **~ brigade** *n.* zimamoto; kikosi cha askari wazima moto. **~damp** *n.* hewa ya mitheni. **~ engine** *n.* mashine ya kuzimia moto. **~ escape** *n.* ngazi ndefu ya kuokolea watu ya wazimamoto; njia ya dharura utokeapo moto katika jengo. **~fly** *n.* kimulimuli; kimetameta; kimetemete. **~man** *n.* askari zimamoto. **~place** *n.* meko; jiko. **~proof** *adj.* -sioshika moto; -sioungua. **~wood** *n.* kuni. **~work** *n.* fataki; fashifashi.


fireplace

**firm**[1] /fɜ:m/ *adj.* **1.** -gumu; thabiti; imara. **2.** shupavu;- sioteteteka; -sioyumba; madhubuti. *adv.* imara; madhubuti. **~ly** imara; madhubuti. **~ness** *n.* uthabiti; uimara.

**firm**[2] /fɜ:m/ *n.* kampuni; shirika; washirika; wabia.

**firmament** /'fə:məm(ə)nt/ *n.* mbingu; anga.

**first** /fɜ:st/ *adj./n/adv.* -a kwanza; kwanza; -a mwanzo; mwanzo. **~ class** *adj.* -a daraja la kwanza; bora. **~-hand** *adj.* -pya kabisa; a

asili. **~-rate** *adj.* bora; -a hali ya juu. **~ly** *adv.* kwanza; awali ya yote.

**fish** /fɪʃ/ *n./ v.i./t.* **1.** samaki. **2.** vua samaki. **3.** vuua; opoa. ~ *for information,* tafuta habari kwa hila. ~ *sth. up (out of),* vuua; opoa. **~erman** *n.* mvuvi. **~monger** *n.* mchuuzi; muuza samaki. **~y** *adv. (colloq.)* -enye vumba; enye shombo; -sioaminika. *a ~ story,* hadithi ya uzushi.

**fission** /'fɪʃ(ə)n/ *n.* uatukaji; mwatuko: ubandukaji; ugawikaji; umegukaji; ugawanyikaji katika sehemu. **nuclear ~**,mwatuko unaokisababisha kiini cha atomu nzito kama ya urani kugawanyika katika sehemu mbili na kutoa nishati ya nyuklia.

**fissure** /'fɪʃə(r)/ *n.* ufa.

**fist** /fɪst/ *n.* ngumi; konde. *put up one's ~,* jitayarisha kupigana.

**fit**[1] /fɪt/ *adj.* **1.** -a kufaa; -enye kustahili. **2.** -a haki : sawasawa. *think ~ to do sth.,* amua ufanye kitu. **3.** -enye afya nzuri. *v.t./i.* (**-tt-**) **1.** faa; kaa. *His clothes ~ him,* nguo zake zimemkaa. **2.** jigeza; jipimisha. **3.** patana na. *n.* kifaacho; matengenezo. **~ter** *n.* mshonaji nguo; fundi muunganishaji sehemu za mashine. **~ting** *adj.* -a kufaa; stahiki; kifaa. *n. electric light ~,* mfumo wa vifaa vya taa za umeme.

**fit**[2] /fɪt/ *n.* ugonjwa wa ghafla wa muda mfupi. *a ~ of coughing,* kipindi cha kukohoa. *epileptic ~,* kifafa. *hysteria ~,* kicheko au kilio cha ghafla. *by ~s and starts,* kwa vipindi vifupivifupi. **~ful** *adj.* -a kugeukageuka; -enye kutokea kwa vipindi vifupi.

**five** /faɪv/ *n./adj.* tano; -tano. **~fold** *adj.* mara tano zaidi.

**fix** /fɪks/ *v.t./i.* kaza; imarisha; amua; tengeneza; vutia; toa picha; honga; lipiza kisasi. ~ *up a friend for the night,* karibisha rafiki kulala nyumbani. ~ *up quarrel,* suluhisha. *n.* mashaka; matatizo. **~ed** *adj.* imara; thabiti. **~edly** *adv. look ~ at,* kazia; kodolea macho. **~ture** *n.* **1.** samani iliyopo mahali pa kudumu. **2.** ratiba ya mashindano.

**fizz** /fɪz/ *v.i./n.* chemka. **~le** *v.i.* chemka. *-le out,* fifia.

**flag** /flæg/ *n/v.t.* bendera; pamba kwa bendera; ashiria kwa bendera. **~ship** *n.* manowari yenye admirali. **~staff** *n.* mlingoti wa bendera. *v.i.* legea; pungua; fifia. *His strength ~s,* nguvu zake zinapungua.

**flagrant** /'fleɪgr(ə)nt/ *adj.* -siyo na haya; dhahiri shahiri.

**flake** /fleɪk/ *n.* chembe; vipande vidogovidogo. *snow ~ s,* chembechembe za theluji.

**flame** /fleɪm/ *n.* mwale; mwako; ulimi, mrija wa moto. *v.i.* waka; ripuka; fanana na miale kwa rangi. *~ tree,* kifabakazi.

**flamingo** /flə'mɪŋgəʊ/ *n.* korongo; flamingo.

**flank** /flæŋk/ *n.* ubavu; upande wa mtu, mnyama au mlima. *a ~ movement,* mwendo wa kupita upande; mzunguko. *v.i./t.* pakana na; -wa kando ya; -wa ubavuni; zunguka au shambulia kwa pembeni.

**flannel** /'flænl/ *n.* kitambaa cha kusafishia; fulana; suruali na fulana ya michezo.

**flap** /flæp/ *v.t./i.* (**-pp-**) (kwa mabawa, matanga, etc.) pigapiga; punga; papatika. *n.* pigo; kipande; upindo. *be in a ~,* hangaika.

**flare** /fleə(r)/ *v.i.* waka; ripuka; tanuka. *~ up,* hamaki; ugomvi wa ghafula. *~ skirt,* sketi pana. *n.* mwako; moto; mripuko.

**flash** /flæʃ/ *n.* mwako; umweso; nuru ya mwanga unamulika ghafla. *in a ~,* kufumba na kufumbua. *~ light,* taa; tochi. *a ~ in the pan,* ulimbukaji. *news ~,* taarifa motomoto. *v.t./i.* mulika; metameta ghafla; mwesa; zagaa upesi. *News -ed across the world,* habari zilizagaa ulimwengu mzima. **~y** *adj.* -a madaha; -shaufu; -a maringo.

**flat** /flæt/ *adj.* **1.** sawa; bapa. *-land,* ardhi tambarare. **2.** -sio tamu; chapwa. **3.** (kwa muziki) -a sauti ya kuteremka. *a ~ denial,* kukana

kabisa. ~ *rate*, bei moja. *n.* **1.** bapa (kwa upanga). **2.** mahali sawa na papana. **3.** (kwa muziki) kiteremsho. **4.** ghorofa ya nyumba. **~ly** *adv.* kabisa. **~ten** *v.t./i.* sawazisha; tandaza.

**flatter** /ˈflætə(r)/ *v.t.* **1.** sifu mno; visha kilemba cha ukoka. **2.** pendeza; furahisha. *be ~ed by an invitation*, pendezwa kwa mwaliko. **3.** (kwa picha) fanya -zuri kuliko -a kweli. ~ *oneself*, jivuna. **~er** *n.* msifuji mno. **~y** *n.* majisifu.

**flavour** /ˈfleɪvə(r)/ *n.* ladha. *v.t.* tia viungo; chapua.

**flaw** /flɔ:/ *n.* kombo; ufa; hitilafu; dosari; ila. **~less** *adj.* kamili; bila kasoro.

**flea** /fli:/ *n.* kiroboto. **~bite** *n.* alama ya kuumwa na kiroboto; jambo dogo sana. **~market** *n.* gulio; bazari.

**flee** /fli:/ *v.i.* (**fled**) kimbia.

**fleet**[1] /fli:t/ *n.* kundi la vyombo vya baharini, nchi kavu au angani chini ya mamlaka moja.

**fleet**[2] /fli:t/ *adj.* -epesi; -enye kasi. **~ing** /ˈfli:tɪŋ/ *adj.* -a kupita; -a muda mfupi tu.

**flesh** /fleʃ/ *n.* **1.** nyama. *one's own ~ and blood*, ndugu wa damu. **2.** mwili; asili. *the sins of the ~*, dhambi za matamanio ya kimwili.

**flex** /fleks/ *n.* waya wa umeme. *v.t./i.* nepa; nyoosha; nyumbua. **~ible** *adj.* -a kuweza kunepa; *(fig.)* -enye kukubali mabadiliko. **~ibility** *n.* ubadilikaji; unepaji.

**flick** /flɪk/ *v.t./n.* piga kidogo; papasa; pigo jepesi; ufyekuzaji.

**flicker** /ˈflɪkə(r)/ *v.i.* **1.** (kwa nuru) sinzia. **2.** yumbayumba; tikisika. *~ing shadows*, vivuli vinavyoyumba.

**flight**[1] /flaɪt/ *n.* **1.** kuruka; masafa ya mruko. **2.** safari ya angani. **3.** kundi la ndege warukao pamoja. *a ~ of pigeons*, kundi la njiwa warukao pamoja. **4.** ngazi. **~y** *adj.* -shaufu; -a kigeugeu.

**flight**[2] /flaɪt/ *n.* ukimbiaji; ukimbizi. *put to ~*, fukuza; kimbiza. *take to ~*, kimbia.

**flimsy** /ˈflɪmzi/ *adj.* (kwa karatasi au kitambaa) -epesi; -embamba; shashi. *a ~ excuse*, udhuru wa kizembe.

**flinch** /flɪn(t)ʃ/ *v.i.* nywea; epa; jikunyata; jikunja.

**fling** /flɪŋ/ *v.t./i.* (**flung**) **1.** vurumisha; vurumiza; ondoka kwa hasira. ~ *caution to the winds*, fanya jambo bila kujali matokeo. *n.* utupaji; upungaji mikono; uvurumishaji. *have a ~ at*, jaribu; bahatisha. *have one's ~*, starehe sana. **2.** jitolea. *~into the job*, jitolea kufanya kazi.

**flint** /flɪnt/ *n.* namna ya jiwe gumu sana.

**flit** /flɪt/ *v.i.* (**-tt-**) rukaruka harakaharaka; hama kimyakimya ili kukimbia wadeni.

**float** /fləʊt/ *v.i./.* **1.** elea; ogelea; eleza. **2.** acha udhibiti wa thamani ya fedha. *n.* chelezo; boya.

**flock** /flɒk/ *n.* kundi; umati; jeshi. *v.i.* kusanyika. ~ *out*, toka kwa makundi. *The people around ~ed to see the accident*, watu waliokuwepo walikusanyika kutazama ajali ile.

**flog** /flɒg/ *v.t.* piga kwa fimbo, kiboko au mjeledi. ~ *a dead horse*, poteza nguvu bure. **~ging** *n.* adhabu ya kuchapwa viboko.

**flood** /flʌd/ *n.* gharika; mafuriko; leleji; wingi; mbubujiko. ~ *of anger*, wingi wa hasira. ~ *tide*, maji kujaa; maji majale; maji makuu. *v.t./i.* **1.** gharikisha; furika; peleka kwa wingi. ~ *a market with fruits*, peleka matunda mengi sokoni. **~light** *n.* taa kubwa yenye mwangaza mkali.

**floor** /flɔ:(r)/ *n.* **1.** sakafu. **2.** ghorofa. **3.** ukumbi wa bunge. *take ~*, pata nafasi ya kuongea katika mjadala. *v.t.* sakafu; shinda; tatiza. ~ *a man in a boxing match*, angusha mtu kwenye ndondi. **~ing** *n.* mbao za sakafu.

**flop** /flɒp/ *v.i.* (**-pp-**) **1.** enda, anguka, ovyo ovyo. **2.** jipweteka; jitupa. *n.* kishindo cha mpweteko. **~py** *adj.* laini sana. ~ *disk*, diski laini ya kompyuta. ~ *house*, hoteli ya hali ya chini kabisa.

**flora** /'flɔ:rə/ *n.* flora: jumla ya mimea katika mazingira fulani. **~l** *adj.* -a maua. **floriculture** *n.* kilimo cha maua. **florist** *n.* muuza maua.

**flour** /'flaʊə(r)/ *n.* unga. **~ mill** mashine ya kusagia nafaka.

**flourish** /'flʌriʃ/ *v.t./i.* **1.** sitawi; shamiri; fanikiwa; tononoka. **2.** punga; tikisa. *n.* upungaji; urembo; usitawi; madoido; chereko.

**flow** /fləʊ/ *v.i.* tiririka; bubujika; (kwa nywele au nguo) ning'inia. *n.* mkondo; mtiririko; mbubujiko. *~ chart,* chati mtiririko.

**flower** /'fləʊə(r)/ *n.* **1.** ua. *in ~,* -enye maua. *~ bed,* kitalu cha maua. **2.** *(fig.)* sehemu bora. *the ~ of the nation's youth,* walio bora miongoni mwa vijana wa taifa. *~s of speech,* semi. *v.i.* toa maua; chanua. *~ing plant,* mti maua: mti wenye kutoa maua. **~y** *adj.* -enye maua mengi.




**flower structure | muundo wa ua**

**flu** /flu:/ *n.* makamasi; mafua; homa ya mafua.

**fluctuate** /'flʌktʃʊeɪt, -tjʊ-/ *v.i.* badilikabadilika; panda na kushuka. **fluctuation** *n.* mabadiliko.

**fluent** /'flu:ənt/ *adj.* -epesi kusema; -semaji; fasaha. **fluency** *n.* ufasaha.

**fluff** /flʌf/ *n.* kibonge cha sufi; manyoya; malaika; pamba. **~y** *adj.* laini.

**fluid** /'flu:ɪd/ *n./adj.* kioevu; maji; hewa; -siokazana.

**fluorescent** /ˌflɔ:'resnt; ˌflʊə'r-/ *adj.* memetevu; mulikaji: enye kutoa nuru ya rangirangi baada ya kupigwa na mnururisho fulani; -enye kuakisi mwanga. *~ light,* taa ya kumetameta. **~ tube,** taa ya mshumaa. **fluorescence** *n.* mmemeto.

**fluorine** /'flʊəri:n, 'flɔ:-/ *n.* florini: elementi ya kikemikali katika hali ya gesi yenye rangi ya manjano kavu nyepesi katika kutendana kuliko zote.

**flush** /flʌʃ/ *v.i./t.* iva uso; vuta maji; piga bomba. *~ed with happines,* iva uso kwa furaha. *n.* wekundu usoni; ufurikaji; ububujikaji; msisimko; ustawi. *adj.* -enye kulingana na; a kujaa pomoni.

**flute** /flu:t/ *n.* filimbi; zumari. **flutist** *n.* mpiga mojawapo ya ala hizo.

**flutter** /'flʌtə(r)/ *v.t./i.* pigapiga mabawa; papatika; pepesuka; hangaika. *n.* upapatikaji; wasiwasi; fadhaa.

**fly**[1] /flaɪ/ *v.t./i.* (**flew flown**) **1.** ruka; chukuliwa na upepo. **2.** (kwa bendera.) pepea hewani; pandisha. **3.** kimbia; pita upesi. *~ to the rescue,* kimbilia uwokovu. *a ~ing visit,* ziara fupi. *~ open,* funguka ghafula. *~ to into pieces,* pasuka vipandepande. *let ~ at, ~ into a rage,* panda hamaki. **4.** endesha ndege; safiri kwa ndege. **flier, flyer** *n.* rubani wa ndege. **~leaf** *n.* ukurasa wa kwanza au wa mwisho wa kitabu usiopigwa chapa. **~wheel** *n.* gurudumu tegemeo.

**fly**[2] /flaɪ/ *n.* inzi. **~blow** *n.* yai la inzi. **~blown** /'flaɪbləʊn/ *adj.* (kwa nyama, mkate, etc.) -lio karibu kuoza kwa kung'ong'wa na inzi. **~catcher** *n.* mtego wa nzi; tiva; shore kishungi. **~-bomb** *n.* bomu la masafa marefu.

**foal** /fəʊl/ *n.* farasi au punda mchanga. *in ~,* (kwa farasi) zaa au wa na mimba pevu.

**foam** /fəʊm/ *n./v.i.* povu; toa povu.

**focus** /'fəʊkəs/ *n.* (**focuses, foci**) **1.** fokasi, kitovu: nukta ya mkutano wa miali baada ya kukengeuka. **2.** mahali kitu kinapoonekana vizuri. **3.** uwekaji kitu mahali kinapo-onekana vizuri. **4.** mahali

penye jambo hasa. *v.t./i.* kutanisha miale mahali pamoja; weka kitu ili kukiona vyema. **focal** *adj.* -a fokasi; -lio kwenye fokasi; -liolenga. *focal length,* umbali wa fokasi: umbali kutoka kitovu cha kioo kivimbe au lenzi hadi fokasi kuu. *focal point,* nukta fokasi: nukta ya mkutano wa miali baada ya kukengeuka.

**fodder** /ˈfɒdə(r)/ *n.* chakula cha mifugo.

**foe** /fəʊ/ *n.* adui; hasimu.

**foetus** /ˈfi:təs/ *n.* kijusi: mtoto wa binadamu katika hatua zake za awali za ukuaji katika tumbo la mama kwenye umri wa takriban wiki nane au zaidi kidogo.




**foetus | kijusi (kichanga)**

**fog** /fɒg/ *n.* ukungu. **~horn** *n.* parapanda inayoashiria hatari ya ukungu, hasa baharini. **~gy** *adj.* -enye ukungu.

**foil** /fɔɪl/ *v.t.* kwamisha; zuia.

**fold** /fəʊld/ *v.t./i.* kunja; kunjana; pindika; pinda. *n.* mkunjo; pindo. **~er** *n.* folda; brosha.

**foliage** /ˈfəʊlɪɪdʒ/ *n.* majani.

**folk** /fəʊk/ *n.* **1.** watu. **2.** *(colloq.)* ndugu au jamaa. **~dance** *n.* ngoma ya asili. **~lore** *n.* mila na desturi za jamii fulani.

**follow** /ˈfɒləʊ/ *v.t./i.* **1.** fuata; andama. **2.** fahamu; elewa. **3.** fanya (kazi). *~ the sea,* fanya kazi ya ubaharia. **4.** iga; fuatisha. **5.** tokana na. *it ~ s from what you say,* kutokana na maelezo yako. *That does not ~ at all,* haiendani kabisa. *~ sth. up,* fuatilia. *as ~s,* kama ifuatavyo. **~er** *n.* mfuasi; msaidizi. **~ing** *adj.* -enye kufuata; -a baadaye.

**folly** /ˈfɒli/ *n.* upuuzi; upumbavu.

**fond** /fɒnd/ *adj.* -enye kupenda. *be very ~ of,* penda sana.

**font** /fɒnt/ *n.* **1.** chombo kitiliwacho maji ya ubatizo. **2.** aina ya herufi za chapa.

**food** /fu:d/ *n.* chakula; maakuli. **~stuffs** *n.* vyakula. *~ for thought,* jambo la kuzingatiwa. *~ chain,* mtungo wa chakula: utaratibu wa ngazi za mahitaji ya chakula katika viumbe hai. **~ poisoning** ugonjwa wa chakula sumu: ugonjwa wowote unaosababishwa na sumu iliyomo katika chakula. **~ preservation** hifadhi ya chakula: kuzuia chakula kisiharibike kwa kutumia kemikali au njia nyingine. **~ web**, wando chakula: utaratibu ambao kiumbe hula kiumbe kingine katika mtungo wa chakula nacho kikaliwa na kingine na kujenga mfumo wa kulana miongoni mwao.

**fool** /fu:l/ *n.* mpumbavu; mjinga. *make a ~ of,* danganya. *make a ~ of oneself,* jipumbaza. *a ~'s errand,* kazi isiyo faida. *~'s paradise,* -wa na furaha ya kipumbavu isiyodumu. *v.i./t.* **1.** jipumbaza; fanya upuuzi. **2.** danganya. *~ away one's time,* poteza wakati. **~ery** *n.* upuuzi. **~-hardy** *adj.* jasiri mno; -enye kujihatarisha bure. **~ish** *adj.* -pumbavu; -jinga; -puuzi. **~ishly** *adv.* kipuuzi; kipumbavu. **~-proof** *adj.* -siyo na hitilafu. **~scap** *n.* karatasi ya inchi 17 kwa inchi 13.

**foot** /fʊt/ *n.* (**feet**). **1.** mguu. *sole of ~,* wayo; unyayo. *cloven ~,* ukwato. *on ~,* kwa miguu. *set sth. on ~,* anzisha jambo. *set (sb.) on his feet,* saidia mtu kujitegemea. *fall on one's feet,* fanikiwa; bahatika. *put one's ~ down,* kataa; pinga; shikilia msimamo. *carry sb. off his feet,* athiri sana mtu. *put one's ~ in it,* kosea. **2.** upande wa chini. *the ~ of*

*a page*, upande wa chini wa ukurasa. **3.** futi. *v.t./i.* fuma mguu wa soksi; enda kwa miguu. ~ *the bill*, lipa gharama. **~ball** *n.* mpira wa miguu; soka; kandanda. **~fall** *n.* kishindo cha hatua. **~hills** *n.* vilima vidogo chini ya mlima mkubwa; safu ya milima. **~hold** *n.* kidato; mahali pa salama. **~ing** *n.* kidato; msingi; cheo. **~man** *n.* mtumishi wa kiume. **~note** *n.* rejeo au tanbihi chini ya ukurasa. **~path** *n.* njia ya miguu. **~print** *n.* wayo; alama ya mguu. **~step** *n.* sauti ya hatua.

**for** /fə(r)/ *conj.* kwa kuwa; kwa maana; maanà. *prep.* kwa; kwa ajili ya; badala ya; muda wa; mwendo wa. *fight* ~, pigania. *~my sake*, kwa ajili yangu. ~ *nothing*, bure.

**forbear** /fɔ:'bɛ:/ *n.* babu; mhenga.

**forbid** /fə'bɪd/ *v.t.* (**forbade forbidden**) gombeza; kataza; kanya; piga marufuku; asa; zuia. **~ding** *adj.* -a kuogofya; -kali; -chungu.

**force** /fɔ:s/ *n.* **1.** nguvu; kani; nguvu. *the ~ of a blow*, nguvu ya pigo. *the ~s of nature*, nguvu za maumbile. **2.** bidii; jitihada; juhudi. **3.** jeshi. *join the ~s*, jiunga na jeshi. **4.** amri; uwezo. *put a law into ~*, fanya sheria itumike. *v.t.* **1.** lazimisha; shurutisha; vunja, pasua kwa nguvu. ~ *a person's hand*, lazimisha mtu kufanya kitu. *~d march*, mwendo wa kijeshi. **2.** otesha; ivisha; pevusha kabla ya wakati. **~ful** *adj.* -enye nguvu; -enye bidii. **forcible** *adj.* -liofanywa kwa nguvu. *forcible entry*, kuingia kwa nguvu. **forcibly** *adv.* kwa nguvu.

**forceps** /'fɔ:sɛps, -sɪps/ *n.* koleo ya kungolea meno.

**ford** /fɔ:d/ *n.* kivuko. *v.t.* vuka kwa miguu.

**fore**[1] /fɔ:(r)/ *n.* mbele; upande wa mbele. *come to the ~*, -wa maarufu. *adj./adv.* -a mbele; -a omo; -a kutangulia; kwa mbele.

**fore**[2] /fɔ:(r)/ *prefix* -a mbele; -a kutangulia; kwa mbele; kabla ya wakati.

**forearm** /'fɔ:rɑ:m/ *n.* kigasha, mkono toka kiko mpaka kitanga.

**forecast** /'fɔ:kɑ:st/ *v.t.* tabiri. *n.* utabiri. *the weather ~*, utabiri wa hali ya hewa.

**forehead** /'fɒrɪd, 'fɔ:hɛd/ *n.* paji la uso; kikomo cha uso.

**foreign** /'fɒrɪn/ *adj.* **1.** -geni, -a nchi za nje; -a kigeni. **2.** -siohusu. **3.** -a nje. *a ~ body in the eye*, kitu cha nje kilichoingia jichoni; dodo; puku-puku. **~er** *n.* mgeni.

**foreman** /'fɔ:mən/ *n.* msimamizi; mnyapara; kiongozi wa baraza la wazee.

**foremost** /'fɔ:məʊst/ *adj./adv.* -a kwanza; -kuu; muhimu.

**forensic medicine** *n.* tiba forensiki: matumizi ya taaluma ya tiba katika kutafuta ushahidi unaoweza kutumika mahakamani unaothibitisha kuwa uhalifu umetendeka.

**foresight** /'fɔ:saɪt/ *n.* uono wa mbele; busara.

**forest** /'fɒrɪst/ *n.* msitu. **~er** *n.* msimamizi wa misitu; bwana misitu. **~ry** *n.* elimu ya upandaji na usimamizi wa misitu.

**forestall** /fɔ:'stɔ:l/ *v.t.* **1.** vuruga mambo kwa kufanya kitu mapema bila kutegemewa. **2.** ficha bidhaa ili kuuza baadaye kwa bei ya juu; langua.

**foretell** /fɔ:'tel/ *v.t.* tabiri; bashiri; agua.

**forethought** /fɔ:θɔ:t/ *n.* busara; uono wa mbele.

**foreword** /'fɔ:wɜ:d/ *n.* dibaji; utangulizi.

**forfeit** /'fɔ:fɪt/ *v.t.* tozwa faini kwa adhabu ya kosa. *n.* faini; fidia. **~ure** *n.* utozwaji kikombozi.

**forge**[1] /fɔ:dʒ/ *v.i* endelea mbele polepole; ongoza.

**forge**[2] /fɔ:dʒ/ *n.* kiwanda cha mhunzi. *v.t.* fua chuma.

**forge**[3] /fɔ:dʒ/ *v.t./i.* ghushi; buni. **~r** *n.* mdanganyifu. **~ry** *n.* uda-nganyifu.

**forget** /fə'get/ *v.t./i.* (**forgot forgotten**) sahau; pitikiwa; ~ *oneself*, jisahau. **~ful** *adj.*

-sahaulifu.

**forgive** /fə'gɪv/ *v.t./i.* (**forgave** **forgiven**) samehe. **~ness** *n.* msamaha; usamehevu. **forgivable** *adj.* -a kusameheka. **forgiving** *adj.* -samehevu; -enye huruma.

**forgo** /fɔ:'gəʊ/ *v.t.* (**forwent** **forgone**) samehe; acha.

**fork** /fɔ:k/ *n.* uma; panda. *v.t./i.* twaa kwa uma; (kwa njia) gawanyika. **~-lift truck** *n.* foko.

**form** /fɔ:m/ *n.* **1.** umbo; sura; jinsi. **2.** taratibu; kawaida; desturi. **3.** muundo; aina. **4.** fomu. *income tax ~,* fomu ya kodi ya mapato. *be in good ~,* -wa katika afya nzuri. *be out of ~,* -wa katika hali ya uchovu. **5.** fomu; benchi. **6.** kidato; darasa. **7.** fani. *v.t./i.* **1.** umba; umbika; unda. **2.** tengeneza; tengenea; tunga. **3.** -wa sehemu ya. **4.** anzisha. **~al** *adj.* rasmi; -a fani; -a umbo la nje. **~ality** *n.* urasimu; kanuni; utaratibu. *legal ~alities,* taratibu za kisheria. **~ation** *n.* uumbaji; utengenezaji; muundo; mpango. **~less** *adj.* bila umbo maalumu. -sio dhahiri.

**former** /'fɔ:mə(r)/ *adj.* -liopita; -a zamani; -liotajwa mwanzo. **~ly** *adv.* kwanza; zamani.

**formidable** /'fɔ:mɪdəb(ə)l, fɔ:'mɪd-/ *adj.* **1.** -a kutisha; -a kuogofya. **2.** -kubwa; -gumu. *~ opposition,* upinzani mkali.

**formula** /'fɔ:mjʊlə/ *n.* **1.** virai vitumikavyo sana kwenye mazungumzo; e.g. *How do you do?* **2.** fomula: kanuni; kawaida; taratibu; maelezo ya kufanya jambo. **~te** *v.t.* changanua kanuni au taratibu za kufanya jambo.

**forsake** /fə'seɪk/ *v.t.* (**forsook** **forsaken**) kataa; acha; tupa; telekeza; toroka. *~ one's family,* telekeza familia.

**fort** /fɔ:t/ *n.* ngome; boma; husuni.

**forth** /fɔ:θ/ *adv.* **1.** nje. **2.** mbele; kwenda mbele. *from this day ~,* kutoka leo na kuendelea. *back and ~,* nyuma na mbele. *and so ~,* na kadhalika. **~coming** *adj.* **1.** -lio karibu kutokea. *be ~coming,* -wa tayari kupatikana. **~right** *adj.* wazi; kweli. **~with** *adv.* sasa hivi; mara moja; bila kukawia.

**fortify** /'fɔ:tɪfʌɪ/ *v.t.* imarisha ongeza nguvu.

**fortification** /ˌfɔ:tɪfɪ'keɪʃn/ *n.* uongezaji nguvu; uimarishaji; ngome; boma.

**fortitude** /'fɔ:tɪtju:d/ *n.* uvumilivu wa maumivu na shida; ushupavu; ustahamilivu.

**fortnight** /'fɔ:tnaɪt/ *n.* wiki mbili; siku kumi na nne. **~ly** *adj./adv.* -a wiki mbili; kila wiki mbili.

**fortress** /'fɔ:trəs/ *n.* mji uliojengwa kama ngome; boma; ngome; husuni.

**fortune** /'fɔ:tʃu:n/ *n.* bahati; mafanikio; neema; baraka; ustawi; utajiri; rasilmali. *have ~ on one's side,* -wa na bahati njema. *tell sb.'s ~,* agua; bashiri; piga ramli. *a ~-teller,* mpiga ramli; mwaguzi.

**fortunate** /'fɔ:tʃənət/ *adj.* -a bahati; -enye bahati.

**forty** /'fɔ:ti/ *n./adj.* arobaini.

**forward** /'fɔ:wəd/ *adj.* -a mbele; -a kutangulia; -a kuendeleza. *n.* fowadi; mchezaji wa mbele. *v.t.* saidia; himiza; endeleza mbele; peleka; safirisha barua. *adv.* mbele. *bring sth. ~,* wasilisha jambo kwa wengine kwa mashauriano. *come ~,* jitolea; jitokeza. *look ~ to,* tazamia; tegemea; tarajia; ngojea.

**fossil** /'fɒs(ə)l, -sɪl/ *n.* kisukuku: mabaki na alama za kale za kiumbe. **~ fuel,** fueli kisukuku: fueli inayofanyika kutokana mabaki ya kaboni ya viumbe hai vilivyoishi kale kama vile gesi na mkaa wa mawe. **~ record,** rekodi kisukuku: ushahidi wote wa hali ya kale utokanao na taarifa zipatikanazo kwa kuchunguza visukuku.

**foster** /'fɒstə(r)/ *v.t.* lea; tunza; kimu. **~-parent** *n.* walezi. **~-mother** *n.* mama mlezi. **~-father** *n.* baba mlezi. **~-brother** (**-sister**) *n.* ndugu wa kulea.

**foul** /faʊl/ *adj.* **1.** -a kuchukiza; -a kunuka; -chafu. **2.** -ovu; -potevu; -a matusi; -a dhoruba. *~ play,* tendo au mchezo uliokiuka sheria. *adv. fall ~ of,* (kwa meli) gongana na; *(fig.)*

gombana na. *v.t./i.* **1.** chafua; chafuka. **2.** (kwa meli) gongana na; (kwa nanga, minyororo, nyavu, etc.) katika; tatana; zongomana. **3.** fanya faulu.

**found** /faʊnd/ *v.t.* weka msingi wa; anzisha. ~ *a new school,* anzisha shule mpya. **~ation** *n.* msingi wa jengo; uanzishaji; mfuko wa kusaidia. ~ *stone,* jiwe la msingi. **~er** *n.* mwanzilishi; mwasisi.

**fountain** /faʊntən/ *n.* chemchemi; bomba la kurusha maji juu kwa nguvu. **~ pen** *n.* kalamu ya wino.

**four** /fɔ:(r)/ *n./adj.* nne; -nne. *on all ~s,* kwa kutambaa. **~score** *adj.* themanini. **~teen** *n./adj.* kumi na nne.

**fovea** /'fəʊvɪə/ *n.* kibonye: kishimo katika mfupa au kiungo kingine katika mwili hasa katika retina ya jicho.

**fowl** /faʊl/ *n.* **1.** (la zamani) ndege yoyote. **2.** kuku. **~er** *n.* mwindaji ndege. **~ing-piece** *n.* bunduki ya kupigia ndege. **~pox** *n.* ndui. **~ typhoid** *n.* kideri. **~pest** *n.* mdondo; kideri.

**fox** /fɒks/ *n.* **1.** mbweha. **2.** mjanja; ayari; laghai. **~y** *adj.* -a kama mbweha; -janja.


fox

**fraction** /'frakʃ(ə)n/ *n.* sehemu; kipande; tarakimu isiyo kamili; e.g. 0.76. **decimal ~**, sehemu desimali. ~ *indices,* vipeo sehemu. **~al** *adj.* -a sehemu. **~ distillation**, mwevusho sehemu: mchakato wa kuevusha kwa ajili ya kubaidisha viowevu vyenye viwango vya kuchemka vinavyokaribiana. **~ating column**, chubu wima inayotumiwa kupokea mivuke mbalimbali na kuwezesha kila aina ya mvuke kuowevishwa katika kiwango chake tofauti .

**fracture** /'fræktʃə(r)/ *n.* mvunjiko; uvunjikaji. *He has a ~ of the leg,* amevunjika mguu. *v.t./i.* vunja; vunjika.

**fragile** /'fradʒʌɪl/ *n.* -a kuvunjika upesi; dhaifu. **fragility** *n.* hali ya kuvunjika upesi.

**fragment** /'frægmənt/ *n.* kipande; sehemu. **~ary** *adj.* -a vipande-pande.

**frail** /freɪl/ *adj.* dhaifu; -enye kuvunjika upesi. **~ity** *n.* udhaifu.

**frame** /freɪm/ *n.* kiunzi; fremu; mwili; umbo; gimba. ~ *of mind,* hali ya akili. *v.t./i.* tunga; buni; tengeneza; tia fremu; singizia. **~work** *n.* mfumo; kiunzi.

**franc** /fraŋk/ *n.* faranga: aina ya pesa.

**franchise** /'fran(t)ʃʌɪz/ *n.* haki apewayo raia na nchi yake.

**frank**[1] /fræŋk/ *adj.* -nyofu; -enye kusema kweli. **~ly** *adv.* kwa kweli.

**frank**[2] /fræŋk/ *v.t.* tia stempu au muhuri kuonyesha kwamba gharama ya usafirishaji imeshalipwa.

**frantic** /'fræntɪk/ *adj.* kama -enye wazimu.

**fraternal** /frə'tə:n(ə)l/ *adj.* -a ndugu; -a kidugu. **fraternity** *n.* **1.** udugu. **2.** chama; shirika; jamii ya watu wenye hali moja. **fraternize** *v.i.* suhubiana na; fanya urafiki.

**fraud** /frɔ:d/ *n.* udanganyifu; hila; ulaghai; mdanganyifu; laghai. **~ulent** *adj.* laghai; -danganyifu.

**freak** /fri:k/ *n.* **1.** kioja; wazo tendo, jambo lisilo la kawaida. **2.** kiumbe kisicho cha kawaida, e.g. kuku mwenye vichwa viwili. **~ish** *adj.* a kioja.

**free** /fri:/ *adj.* huru; -enye hiari; -siozuiwa; huria; bure; wazi. *have a ~ hand,* fanya upendavyo. *the ~ church,* kanisa huria. *a ~ port,* bandari huru. ~ *translation,* tafsiri huria, isiyokuwa ya neno kwa neno. *make ~ with,* tumia bila ruhusa. ~ *fight,* mapigano ambayo yeyote anaweza kuingia. ~ *will,* hiari; utashi. *v.t.* weka huru; okoa; komboa. **~dom** *n.* uhuru. **~hand** *adj.* - liochorwa bila kutumia zana za kupimia. **~ handed** *adj.* -karimu. **~hold** *n.* umilikaji ardhi bila masharti. **~ly** *adv.* bila kizuizi. **~man** *n.* mtu huru. **~thinker** *n.* mtu anayekataa miongozo ya

kidini iliyokubaliwa katika jamii na kufuata misimamo huru.

**freeze** /fri:z/ *v.i./t.* (**froze frozen**) ganda; -wa baridi sana. *frozen roads*, barabara zilizofunikwa na barafu. ~ *the blood*, ogofya. ~ *drying*, ukaushi baridi: namna ya ukaushaji ambapo maji hutolewa katika dutu iliyo katika halijoto ya chini bila ya kubakia. **freezing-point** *n.* kiwango cha kuganda: kiasi cha halijoto wakati dutu inapoanza na kuendelea kuganda na kuwa mango.

**freight** /freɪt/ *n.* gharama za uchukuzi wa mizigo; mizigo; shehena. **~er** *n.* meli au ndege ya mizigo.

**frequent** /'fri:kw(ə)nt/ *adj.* -a mara nyingi; -a kawaida; -a mara kwa mara. *v.t.* enda mahali mara nyingi; zoea kwenda (kukaa, kuzuru) mara kwa mara. **~ly** *adv.* mara kwa mara. **frequency** *n.* **1.** kadiri ya urudiaji; urudiaji. **2.** kasimawimbi: idadi ya mibembeo katika kizio kimoja kwa muda fulani. **resonant ~**, kasimawimbi pata: marudio ya kulingana na marudio asili ya kitu.

**fresh** /freʃ/ *adj.* -bichi; -pya; -ingine; (kwa chakula) -tamu, -siotiwa chumvi; (kwa maji) -siokuwa ya bahari; (kwa sura mtu) safi, -enye afya nzuri; (kwa hali ya hewa) baridi. ~ *air*, hewa safi. **~ly** *adv.* sasa hivi; mapema. **~ness** *n.* upya; ubaridi.

**friction** /'frɪkʃn/ *n.* **1.** usuguanaji wa vitu au mawazo. **2.** msuguano: hali ya kuwepo kani inayozuia msogeo kati ya vitu vinavyogusana. **coefficient of ~**, kizigeu cha msuguano. **fluid ~**, msuguano kimiminiko. **kinetic ~**, msuguano mwendo. **static ~**, msuguano tuli.

**Friday** /'fraɪdeɪ; -di/ *n.* Ijumaa. *Good ~*, Ijumaa Kuu.

**friend** /frend/ *n.* rafiki; sahibu; msaidizi; mhisani. *make ~ s with*, wa marafiki. **~ly** *adj.* -a kirafiki; -ema. **~liness** *n.* urafiki; upole; wema. **~ship** *n.* urafiki; usuhuba.

**frigate** /'frɪgət/ *n.* manowari sindikizaji.

**fright** /fraɪt/ *n.* hofu; woga; mshituko; kichekesho; mzaha. *give sb. a ~*, shtusha. **~en** *v.t.* ogofya; shtusha. **~ful** *adj.* -a kuogofya; -a kuchukiza; -a kutisha. **~fully** *adv.* kwa hofu sana.

**frigid** /'frɪdʒɪd/ *adj.* baridi; si kunjufu; -sio na ashiki. **~ity** *n.* ubaridi; ukosefu wa ashiki.

**frisk** /frɪsk/ *v.t.* **1.** rukaruka; chezacheza; randa. **~y** *adj.* -enye kurukaruka; -enye kuchezacheza. **2.** pekua; tafuta kitu au silaha harakaharaka.

**frivolous** /'frɪvələs/ *adj.* -a kipuuzi; -enye kupenda anasa; puuzi. **frivolity** *n.* upuuzi.


frog

**frog** /frɒg/ *n.* chura. *have a ~ in the throat*, koroma. **~man** *n.* mpiga mbizi; mzamiaji.

**from** /frəm/ *prep.* kwa; katika; toka; kutoka; tangu; kutoka kwa; -tokana na. *He is ~ home*, ametoka. *What is it ~?* sababu yake nini?

**fronds** /frɒnds/ *n.* majani makubwa ya miti ya aina ya mikangaga, minazi etc.

**front** /frʌnt/ *n.* upande wa mbele; mbele; medani; uwanja; barabara ya ufukweni; uso; umoja. *put on a bold ~*, kabili kwa ujasiri. *v.t./i.* kabili; kabiliana na; tazama; elekea; pinga. **~age** *n.* upande wa mbele wa nyumba au shamba. **~al** *adj.* a mbele.

**frontier** /'frʌntɪə, frʌn'tɪə/ *n.* mpaka; kikomo.

**frost** /frɒst/ *n.* **1.** theluji; ukungu. **2.** jambo lisilofanikiwa. **~bite** *n.* ugonjwa wa kuganda tishu kwa baridi kali na huweza kusababisha gangrini.

**froth** /frɒθ/ *n.* povu; upuuzi. *v.i.* toa povu; foka; fofomoka; umuka.

**fruit** /fru:t/ *n.* tunda; faida; mapato; chumo; mafanikio; matokeo. *v.i.* zaa matunda. **~erer** *n.* muuza matunda. **~ful** *adj.* -enye kuzaa matunda; *(fig.)* -a faida; -a kufaa.

**~ion** *n.* kuzaa matunda; kupata mafanikio; kupevuka; kufaulu. **~less** *adj.* -sio matunda; -a bure; -sio manufaa.
**frustrate** /frʌ'streɪt/ *v.t.* zuia; changanya mtu kisaikolojia; vunja moyo; katisha tamaa. **frustration** *n.* kizuizi; uvunjikaji moyo.
**fry** /fraɪ/ *v.t./i.* kaanga; kaangika. *n.* samaki wachanga.
**fuel** /'fju:əl/ *n.* fueli: kitu chochote kitoacho nishati; *(fig.)* kichochezi. *v.t./i.* tia fueli; tia mafuta. *add ~ to the flames,* chochea; palilia.
**fugitive** /'fju:dʒətɪv/ *n./adj.* mtoro; mkimbizi; -toro; -a kupita.
**fulcrum** /'fʊlkrəm, 'fʌl-/ *n.* egemeo: mahali ambapo wenzo huegemea.
**fulfil** /fʊl'fɪl/ *v.t.* (**-ll-**) timiza; tekeleza; kamilisha. **~ment** *n.* ukamilishaji.
**full** /fʊl/ *adj.* -enye kujaa; tele; -zima; -ote; kamili. *~ face,* uso wote. **~ moon** *n.* mwezi mpevu: umbo la mwezi la duara kamili kama linavyoonekana tarehe 14 mwandamo. *in ~,* -ote. *to the ~,* kabisa. *at ~ speed,* kwa kasi sana. *adv.* kamili. **~-grown** -liopevuka. **~-blown** (kwa maua) -liochanua. **~y** *adv.* kikamilifu; kabisa.
**fumble** /'fʌmbl/ *v.t./i.* papasa; shikashika; babaisha; sitasita.
**fume** /fju:m/ *n.* moshi; mvuke; hasira; ghadhabu. *v.i./t.* toa mvuke; fuka; kasirika; foka.
**fumigate** /'fju:mɪgeɪt/ *v.t.* fukiza; tia buhuri. **fumigation** *n.* ufukizaji. **fumigator** *n.* chetezo; mfukizaji.
**fun** /fʌn/ *n.* mchezo; furaha; burudani; raha; mzaha; kichekesho. *make ~ of, poke ~ at,* fanyia mzaha. *~fair,* kiwanja cha michezo.
**function** *n.* kazi; shughuli; tamasha; adhimisho; tafrija. *v.i.* fanya kazi; faa. **~al** *adj.* enye kufaa; -enye kufanya kazi. **~ary** *n.* mtendaji; mfanyakazi.
**fund** /fʌnd/ *n.* akiba; hazina; mfuko. *a ~ of common sense,* akiba ya maarifa. *public ~s,* hazina ya serikali. *social security ~,* mfuko wa hifadhi ya jamii.
**fundamental** /fʌndə'mɛnt(ə)l/ *adj.* -a asili; muhimu; -a msingi. *n.*msingi; kanuni; asili. **~ism** *n.* ulokole. **~ist** *n.* -enye imani kali; mlokole; mujahidina.
**funeral** /'fju:nərəl/ *n.* maziko; mazishi.
**fungus** /'fʌŋəs/ *n.* ukungu; kuvu; uyoga.
**fungicide** /'fʌngɪsaɪd/ *n.* dawa ya kuulia kuvu.
**funk** /fʌŋk/ *n.* hofu kubwa; mwoga. *v.i./t.* ogopa.
**funnel** /'fʌnl/ *n.* faneli; bomba; dohani.
**funny** /'fʌni/ *adj.* -a kuchekesha; -geni; -a ajabu; -gumu kufahamika. **~ born** *n.*mfupa wa kiko cha mkono upitishao neva-ulna.*~ farm,* hospitali ya vichaa.
**fur** /fɜ:(r)/ *n.* manyoya (ya wanyama); ngozi ya mnyama yenye manyoya; koya. **~red** *adj.* -liofunikwa kwa manyoya. **~ry** *adj.* -a manyoya; -enye manyoya.
**furious** /'fjʊəriəs/ *adj.* -a ghadhabu; -kali mno.
**furnace** /'fɜ:nɪs/ *n.* joko; kalibu; tanuu.
**furnish** /'fɜ:nɪʃ/ *v.t.* toa; patia; pamba; -pa. **~ings** *n.* samani.
**furniture** /'fɜ:nɪtʃə(r)/ *n.* samani; fanicha.
**furrow** /'fʌrəʊ/ *n.* mfuo; mfereji; mtaro; kunyanzi. *v.t.* fanya kunyanzi; tengeneza mtaro.
**further** /'fɜ:ðə(r)/ *adv.* mbele zaidi; mbali; zaidi; tena; juu ya hayo; zaidi ya hayo. *adj.* -a zaidi. *v.t.* saidia; endeleza. **furthest** *adj./adv.* mbali kabisa. **~more** *adv.* zaidi; tena; juu ya hayo; zaidi ya hayo. **~most** *adj.* mbali kabisa.
**furtive** /'fə:tɪv/ *adj.* -a siri; -a hila; -a chinichini. *a ~ glance,* kijicho upembe.
**fury** /'fjʊəri/ *n.* ghadhabu kali; mwanamke mkali.
**fuse** /fju:z/ *v.t./i.* yeyungana; yeyusha; yeyuka; ungana; unganika. *n.* fyuzi; utambi.
**fuselage** /'fju:zəlɒʒ, -lɪdʒ/ *n.* kiunzi cha eropleni.

**fusion** /fju:ʒn/ *n.* myeyungano uyeyunganishaji. *the ~ of copper and tin,* uyeyunganishaji wa shaba na bati.
**fuss** /fʌs/ *n.* udhia; wasiwasi; kiherehere. *v.i./t.* shughulika; shughulikia; sumbua; sumbuka; hangaika. **~y** *adj.* -sumbufu; -enye kuhangaika mno.
**futile** /'fju:taɪl/ *adj.* -sioleta manufaa; -sio na maana; siyefanya lolote la maana. **futility** *n.* upuuzi; hali ya kutokuwa na manufaa yoyote.
**future** /'fju:tʃə(r)/ *n./adj.* wakati ujao; -a baadaye. *for the ~,* kwa siku za baadaye.
**futurity** /fju'tjʊərəti/ *n.* wakati ujao; jambo la baadaye.

# Gg

**gabble** /'gæbl/ *v.t./i.* sema upesi bila kutamka vizuri maneno; payuka. *n.* upayukaji; maneno yasiyoeleweka.
**gable** /'geɪbl/ *n.* gebo: ukuta wa pembetatu baina ya mapaa ya nyumba ya mgongo. *a ~ roof,* paa la mgongo.
**gadget** /'gædʒɪt/ *n.* chombo cha kazi; ala; zana.
**gag** /'gæg/ *n.* **1.**namna ya kitambaa kinachofanya kinywa kikae wazi wakati wa matibabu ya meno au upasuaji. **2.** kichekesho katika maigizo.
**gain** /geɪn/ *v.t./i.* pata; chuma; ongeza. *~ one's living,* jipatia riziki. *~ time,* jipatia muda wa ziada; vuta muda. *~ up(on),* shinda; karibiana na; pita. *n.* pato; chumo; faida; ongezeko la mali, uwezo, nguvu. **~ful** *adj.* -a faida; -a manufaa.
**galaxy** /'gæləksi/ *n.* **1.** galeksi: kundi la nyota liundalo mfumo huru katika anga. *the ~,* mfumo huru wa nyota ambamo ndani yake imo ardhi. *the milky way ~,* mfumo wa nyota nyingi ndogo zionekanazo kama wingu mbinguni. **2.** kundi la watu maarufu.
**gale** /geɪl/ *n.* upepo mwingi; dhoruba.
**gall bladder** *n.* kibofunyongo: kifuko kinachohifadhi nyongo karibu na ini la wanyama.
**gallery** /'gæləri/ *n.* **1.** nyumba ya sanaa. **2.** watu wanaokaaa kwenye sehemu rahisi katika thieta. **3.** ghorofa ya juu. **4.** ujia ulioezekwa.
**gallium** /'galɪəm/ *n.* galiamu: elementi laini ya metali ya rangi ya bahari inayotumiwa kutengenezea vipitishi katika transista.
**gallon** /'galən/ *n.* galoni.
**gallop** /'gæləp/ *v.i./t.* enda shoti; chapuka; endesha shoti. *n.* mwendo wa shoti.
**gallows** /'gæləʊz/ *n.* kiunzi cha miti cha kunyongea. **~-bird** *n.* mtu astahiliye kunyongwa. *send sb. to the ~,* hukumu mtu kunyongwa.
**galvanized iron** *n.* chuma galvaniwa: kipande cha bamba la feri lililopakazwa tabaka la zinki ili kuzuia lisilike na kutu.
**galvanometer** /ˌgalvə'nɒmɪtə/ *n.* galavanometa: chombo cha kuonyesha au kupima mikondo midogo dhaifu ya umeme.
**gamble** /'gæmbl/ *v.i./t.* cheza kamari; cheza bahati nasibu. *n.* kubahatisha. **~r** *n.* mcheza kamari. **gambling** *n.* kamari.
**game** /geɪm/ *n.* **1.** mchezo. *play the ~,* fuata kanuni za jambo. **2.** mashindano ya michezo. *the Olympic ~s,* michezo ya Olimpiki. **3.** raundi. *win three ~,* shinda raundi tatu. **4.** hila. *make ~ of,* fanyia mzaha; dhihaki. *The ~ is up,* shauri limeshindikana **5.** wanyama wa kuwinda. **~ reserve** hifadhi ya wanyama. *v.i.*cheza kamari. **~keeper** *n.* mlinzi wa wanyama wa kuwinda. **~licence** *n.* leseni ya kuwinda.
**gamete** /'gami:t/ *n.* gameti: seli

ambazo zikikamilika zina uwezo wa kuungana na kuwa seli moja katika uzaliano kijinsia.




**gamete | gameti**

**gamma radiation** *n.* mnururisho gama: mnururisho unaosababishwa na miali gama.
**gander** /'gandə/ *n.* bata bukini dume.
**gang** /gæŋ/ *n.* kundi la watu wafanyao jambo pamoja; genge; gengi. **~ster** *n.* jambazi. **gangway** *n.* ujia; kidaraja; ubao wa kuingilia au kutoka melini.
**gangrene** /'gaŋgri:n/ *n.* gangrini; kidonda kinachosababishwa na kuoza minofu. **gangrenous** *adj.* -liooza.
**gaol** *n.* gereza; jela. **~-bird** *n.* mfungwa mzoefu. **~er** *n.* askari jela; mlinzi wa gereza. **1.** chumba kirefu chembamba. **2.** njia ndani ya machimbo ya madini. *play to the ~,* jipendekeza kwa umma.
**gap** /gæp/ *n.* ufa; nafasi; hitilafu; uwazi; pengo; mwanya.
**gape** /geɪp/ *v.i.* achama; pasuka; fanya ufa; piga miayo. *n.* miayo.
**garage** /'garɑ:(d)ʒ, -ɪdʒ, gə'rɑ:ʒ/ *n.* gereji.
**garden** /'gɑ:dn/ *n.* bustani ya maua, mboga au matunda. *kitchen ~,* bustani ya mboga. *v.i.* lima bustani. **~er** *n.* mkulima wa bustani. **~ing** *n* kilimo cha bustani.
**garland** /'gɑ:lənd/ *n.* shada la maua; koja; diwani mchanganyiko. *v.t.* visha shada la maua.
**garlic** /'gɑ:lɪk/ *n.* kitunguu saumu. *a clove of ~,* tumba la kitunguu saumu.
**gash** /gæʃ/ *n.* toja; keketa; chanja.
**garment** /'gɑ:mənt/ *n.* vazi; nguo.
**garrison** /'gærɪsn/ *n.* askari walinzi wa mji, ngome, au boma. *v.t.* linda kwa askari hao.
**gas** /gæs/ *n.* gesi: dutu yenye chembechembe zitembeazo huru na ambazo hazigeuki kioevu au maada katika joto la kawaida; petroli; nusu kaputi; soga. *laughing* gesi ya kuchekesha. *v.t.* ua, kufa kwa gesi; bwabwaja. **~bag** *n.* *(colloq.)* mpayukaji; mfuko wa gesi. **~eous** *adj.* -a gesi; kama gesi. **~ exchange**, ubadilishanaji gesi: mpito wa gesi moja kutoka upande mmoja wa kiwambo wakati gesi nyingine inapita toka upande wake mwingine. **~ometer** *n.* chombo cha kuhifadhia na kupimia gesi.
**gash** /gæʃ/ *n.* jeraha kubwa. *v.t.* jeruhi kwa kukata; keketa; chanja.
**gasolene** /'gæsəli:n/ *n.* petroli.
**gasp** /gɑ:sp/ *n.* kutweta; kuhema. *be at one's last ~,* choka kabisa; gharighari ya kufa; sakarati ya mauti. *v.i./t.* tweta; hema; vuta pumzi kwa shida.
**gastric** /'gæstrɪk/ *adj.* -a tumbo. *~ fever,* homa ya tumbo. *~ juice,* majitumbo. *~ ulcer,* kidonda tumbo. *gastritis,* uvimbe-tumbo.
**gastropod** *n.* moluska (mfano konokono) atembeaye kwa tumbo na ana macho na minyiri.
**gate** /geɪt/ *n.* geti; mlango; lango. **~keeper** *n.* bawabu. *between you and me and the ~-post,* siri yetu sisi wawili tu. **~way** *n.* lango.
**gather** /'gæðə(r)/ *v.t./i.* **1.** kusanya; kusanyika. **2.** chuma. **3.** fahamu; elewa. *What did you ~ from his statement?* ulifahamu nini kutokana na maelezo yake? **4.** tunga usaha. **5.** tia marinda. **~ing** *n.* mkutano; mkusanyiko; uchumaji; jipu.
**gaudy** /'gɔ:di/ *adj.* -a urembo mwingi hadi kuchusha.
**gauge** /geɪdʒ/ *n.* geji; kipimo; upana wa pau au baina ya gurudumu za gari la moshi; unene. chombo cha kupimia. *v.t.* pima; kadiria; kisia.
**gaunt** /gɔ:nt/ *adj.* -liokonda sana; -liochukiza sana.
**gauze** /gɔ:z/ *n.* shashi; kitambaa chembamba sana kinachoonyesha; wavu wa nyuzi kama chandarua.
**gay** /geɪ/ *adj.* -a furaha; changamfu;

-a kupendeza; -a bashasha. **gaiety** *n.* furaha; shangwe; bashasha; ukunjufu. **gaily** *adv.* kwa furaha; kwa shangwe; kwa uchangamfu.

**gaze** /geɪz/ *v.i./n.* kazia macho; tazama; angaza; mtazamo.

**gazelle** /gə'zel/ *n.* paa; swala.

**gazette** /gə'zet/ *n.* gazeti la serikali. *v.t.* tangaza katika gazeti. **~er** *n.* faharasa ya majina ya kijiografia.

**gear** /gɪə(r)/ *n.* **1.** zana za kazi maalumu. *hunting ~,* vifaa vya kuwindia. *steering ~,* usukani. *the landing ~ of an aircraft,* miguu ya kutulia ndege. **2.** gia. *be in ~,* -wa katika gia. *be out of ~,* kutokuwemo katika gia. *high ~,* gia ya nguvu. *low ~,* gia ndogo.


**gear wheels**

**Geiger counter** /'gaɪgə kaʊntə(r)/ *n.* kihesabio Geiger: ala ya kupimia harakatiredio na nguvu ya miali ya alfa, beta na gama.

**gem** /dʒem/ *n.* kito; johari; kitu kithaminiwacho sana kwa sababu ya uzuri wake.

**gender** /'dʒendə(r)/ *n.* jinsi; jinsia. *feminine ~,* jinsi ya kike. *masculine ~,* jinsi ya kiume. *neuter ~,* jinsi si ya kike wala ya kiume; huntha.

**gene** /dʒi:n/ *n.* jeni: sehemu ya DNA inayorithisha tabia au umbile fulani.

**general** /'dʒenrəl/ *adj.* **1.** -a jumla; -a juujuu; -kuu; -a -ote; si maalumu. *a matter of ~ interest,* lihusulo watu wote. *~ knowledge,* maarifa. *a ~ practitioner,* daktari anayetibu maradhi yote. *as a ~ rule,* kwa kawaida. *in ~,* kwa kawaida. **inspector ~**. *n.* inspekta mkuu. **~ity** *n.* ujumla; kawaida. **~ize** *v.i./t.* jumuisha; hitimisha; sambaza. **~ization** *n.* **~ly** *adv.* mara nyingi; kwa kawaida.

**generate** /'dʒenəreɪt/ *v.t.* fanyiza; tokeza; leta; zaa; zalisha: *~ heat,* toa joto. *~ bitter feelings,* sababisha uchungu. **generation** *n.* **1.** uzazi. **2.** kizazi. *three ~s,* vizazi vitatu (baba, mwana na mjukuu). **3.** rika. **generator** *n.* jenereta.

**generous** /'dʒenərəs/ *adj.* karimu; -paji; -ema; -zuri; -ingi; enye kutoa nyingi. **generosity** *n.* ukarimu.

**genesis** /'dʒɛnɪsɪs/ *n.* asili; mwanzo; chimbuko.

**genetic** /dʒɪ'nɛtɪk/ *adj.* -a uzazi; -a kizazi. **~s** *n.* jenetikia: taaluma ya urithishano na mwachano wa viumbe hai. **~ engineering**, uhandisi jeni: ubadilishaji jeni za viumbe hai ili kupata vizazi bora zaidi.

**genitive** /'dʒɛnɪtɪv/ *n./adj.* jinsi ya nomino, kiwakilishi, kivumishi, kujijulisha -enyewe.

**genius** /'dʒi:niəs/ *n.* kipaji; mtu mwenye kipaji asilia.

**gentle** /'ʒentl/ *adj.* pole; -tulivu; raufu; latifu; - uungwana. **~folk** *n.* waungwana. **~man** *n.* muungwana mwanamme. **~manly** *adj.* -a adabu; -pole; -a kiungwana. **~woman** *n.* muungwana mwanamke. **gently** *adv.* kwa upole. **gentry** *n.* waungwana.

**genuine** /'dʒenjuɪn/ *adj.* -a kweli; halisi.

**genus** /'dʒi:nəs/ *n.* (**genera**) **1.** jenasi (jenera) : uainishaji wa spishi zenye sifa zinazofanana. *genus homo,* binadamu. **2.** jinsi; namna; aina; jamii.

**geodesy** /dʒɪ'ɒdɪsɪ/ *n.* tawi la hisabati kuhusu umbo, ukubwa na vipimo vya dunia. **geodesic** *adj.* -a umbo au ukubwa wa dunia.

**geography** /dʒi'ɒgrəfi/ *n.* jiografia: sayansi ya habari za maeneo ya uso wa dunia na viumbe vilivyomo. **geographer** *n.* mtaalamu wa jiografia. **geographical** *adj.* -a jiografia.

**geology** /dʒi'ɒlədʒi/ *n.* jiolojia: sayansi inayohusu umbile na historia ya miamba inayounda dunia. **geological** *adj.* -a jiolojia. *geological time scale,* kipima wakati kijiolojia: kipima wakati ambacho kinadhihirisha historia ya dunia kijiolojia. **geologist** *n.* mtaalamu wa jiolojia.

**geomagnetism** *n* usumakuardhi: usumaku unaotokana na ardhi.

**geometry** /ˌdʒɪˈɒmɛtrɪ/ *n.* jiometri: tawi la hisabati linaloshughulika na tabia, uhusiano na upimaji wa nukta, mistari, maumbo na mango. **plane ~**, jiometria bapa. **motion ~**, jiometria jongeo. **geometric (al)** *adj.* -a jiometri. **geometrical isomerism**, uisoma wa kijiometri.

**geomorphology** /ˌdʒi:ə(ʊ)mɔ:ˈfɒlədʒi/ *n.* sayansi ya umbo la uso wa sayari inayojumuisha uhusiano na umbile lake kijiolojia.

**geostationary satellite** *n.* setilaiti: setilaiti inayozunguka dunia mara moja kwa kila saa 24, na iliyo umbali takriban wa kilomita 35,800 kutoka uso wa dunia.

**geosyncline** *n.* bonde kubwa kama beseni lililofanyika kwenye uso wa ardhi kutokana na ushukaji wa tabaka za miamba.

**geothermal energy** *n.* nishatijoto ardhi: nguvu za joto zitokanazo na majabali yaliyoyeyuka chini ya ardhi.

**germ** /ˈdʒɜ:m/ *n.* **1.** kiini; mimba; mbegu; yai; asili; mwanzo. ~ *cell*, selizazi. **2.** kijidudu kinachosababisha ugonjwa. **~icide** *n.* dawa ya kuulia vijidudu vya maradhi. **~inate** *v.t./i.* ota; mea; chipua. **~ination** *n.* umeaji; uotaji; uchipuaji.

**germanium** /dʒə:ˈmeɪnɪəm/ *n.* jemani: elementi metali adimu, aghlabu tetravalensia, yenye rangi kijivu- cheupe.

**gestation** /ˈdʒeˈsteɪʃn/ *n.* ujauzito: kipindi cha kuwa katika fuko la uzazi hadi kuzaliwa kwa kiumbe.

**gesture** /ˈdʒestʃə(r)/ *n.* ishara ya kichwa au mikono. *v.i.* ashiria.

**get** /get/ *v.t./i.* (**got**) **1.** pata; nunua; chuma; leta; pewa; pokea; fahamu; tambua; elewa. **2.** pata kuwa; geuka; fanya; ita; fanyiza. ~ *tired*, choka; ~ *a door open*, sindua (fungua) mlango. ~ *sb. selected*, fanya mtu achaguliwe. **3.** fika; enda; fikisha; peleka. ~ *home*, fika nyumbani. ~ *the children to bed*, laza watoto. **4.** patwa; ugua; sikia; ona. ~ *a shock*, patwa na mshtuko. ~ *one's hair cut*, katwa nywele. **5.** shawishi kuja; alika. ~ *the doctor to come tomorrow*, ita daktari aje kesho. ~ *about*, enea; safiri. ~ *sth. across*, fahamisha; elewesha. ~ *along*, endelea. ~ *on with one's neighbours*, patana na jirani. ~ *at*, fikia; vumbua; *(colloq.)* honga. ~ *away (with)*, okoka; pona. ~ *by heart*, hifadhi kwa moyo. ~ *in*, fika; wasili; chaguliwa. ~ *sth. in*, kusanya; vuna; ~ *off*, anza; pona. ~*on*, endelea; karibia. *The time is ~ting on for four o'clock*, inakaribia saa kumi. ~ *out of*, epukana na; acha desturi. ~ *over*, shinda; mudu; pona; maliza. ~ *round*, epa. ~ *round sb.*, bembeleza. ~ *through*, faulu; maliza kazi; tumia fedha zote. ~ *to*, anza. ~ *to know*, suhubiana na. ~ *up*, simama; amka; (kwa upepo) vuma sana. ~ *up to*, fikia. ~ *up to mischief*, -wa -tundu. ~ *sth. up*, tengeneza. *have got*, paswa. *have not got to*, sipaswi. **~-at-able** *adj.* -a kufikika; -pole; -a kuambilika. **~-up**, mtindo; mavazi. *Asha came in a new ~-up*, Asha alikuja amevaa mavazi mapya.

**geyser** /ˈgi:zə/ *n.* **1.** chemchemi ya maji moto. **2.** chombo cha kupashia maji moto.

**ghost** /gəʊst/ *n.* **1.** mzuka; pepo; zimwi. **2.** (la zamani) roho. *give up the ~*, kata roho. *The Holy ~*,Roho Mtakatifu. *not the ~ of an apportunity*, hakuna fursa hata ndogo. **~ly** *adj.* - a mzuka; -a kama mzuka; -a kiroho.

**giant** /ˈdʒaɪənt/ *n.* jitu; jibaba; mwenye sifa inayopindukia mipaka ya kawaida.

**giddy** /ˈgɪdi/ *n.* kupenda raha; -sio na makini; -sio na msimamo thabiti. **giddiness** *n.* kizunguzungu; kisuunzi.

**gift** /gɪft/ *n.* zawadi; hiba; kipaji; kipawa. *a person with a ~ for foreign languages*, mtu mwenye kipaji cha lugha za kigeni. **~ed** *adj.* -enye kipaji.

**gigantic** /dʒaɪ'gæntɪk/ *adj.* -a kupita kiasi; -kubwa mno; -refu mno.
**giggle** /'gɪgl/ *n./v.i.* kicheko; chekacheka.
**gild** /gɪld/ *n.* mpako wa dhahabu; rangi ya dhahabu. *v.t.* paka dhahabu; chovya katika maji ya dhahabu; pamba; remba. **~ed** *adj.* -nye kupakwa dhahabu. **gilt** *n./adj.* mpako wa dhahabu; -enye kupakwa dhahabu.
**gill**[1] /dʒɪl/ *n.* shavu la samaki.
**gill**[2] /dʒɪl/ *n.* kipimo cha robo painti.
**gimlet** /'gɪmlɪt/ *n.* kekee ndogo. *~ eyes,* macho makali.
**gin**[1] /dʒɪn/ *n.* jini: aina ya pombe kali.
**gin**[2] /dʒɪn/ *n.* **1.** kinu cha kuchambulia pamba. **2.** mtego wa wanyama; fyuka; kidato. *v.t.* (**-nn-**) chambua pamba kwa kinu; tega kwa fyuka.
**ginger** /'dʒɪndʒə(r)/ *n.* tangawizi.
**giraffe** /dʒə'rɑ:f/ *n.* twiga.
**girder** /'gɜ:de(r)/ *n.* boriti; mhimili (wa ubao au chuma).
**girdle** /'gɜ:dl/ *n.* **1.** mshipi; ukanda. **2.** kitu kizungukacho kama ukanda; utunda; ukama; mkaja; mkwiji. *v.t.* zunguka; zingira.
**girl** /gɜ:l/ *n.* msichana. *house ~,* msaidizi wa ndani wa kike. *~ scout,* skauti wa kike.
**give** /gɪv/ *v.t./i.* (**gave**, **given**) toa; pa. *~ sth. away,* toa siri. *~ sb. away,* haini. *~ the bride away,* bibi arusi kwa mumewe. *~ in,* shindwa; acha kujitahidi. *~ out,* malizika; kwisha. *~ (sth.) out,* gawa; peleka. *~ over,* acha. *~ up,* acha; toa kwa mwingine. *~ up your seat to a lady,* pisha mwanamke kwenye kiti chako. *~ a laugh,* cheka. *~ a groan,* piga kite. *~ a push,* sukuma kidogo. *~ a hand,* saidia. *~ evidence of,* jionyesha kuwa na. *~ ground,* rudi nyuma. *~ rise to,* anzisha. *~ way,* pasuka; vujika; katika; shindwa. *~ place to,* fuatana na; ondokea. *~ sb. to understand that,* fahamisha fulani kuwa. *at a ~n time and place,* mahali na wakati maalumu. *~n to,* shikilia.
**gizzard** /'gɪzəd/ *n.* firigisi; finingi.
**glacial** /'gleɪʃ(ə)l, -sɪəl/ *adj.* -a theluji; -a barafu; -a zama za barafu. **glaciated** *adj.* -liofunikwa na mito ya barafu. **glacier** *n.* mto wa barafu uendao polepole.
**glad** /glæd/ *adj.* -enye furaha; kunjufu; -changamfu. **~den** *v.t.* furahisha. **~ly** *adv.* kwa furaha. **~ness** furaha; uchangamfu; bashasha; shangwe; nderemo.
**glamour** /'glæmə(r)/ *n.* haiba; heba; uzuri. **~ous** *adj.* *(colloq.)* (kwa wanawake tu) -zuri sana.
**glance** /glɑ:ns/ *n.* mtazamo; mng'aro. *v.i./t.* **1.** tupia jicho; angalia kidogo. **2.** (kwa vitu vyenye kung'aa ) ng'aa. **3.** (kwa silaha) paruza.


**gland cell** | **seli tezi**

**gland** /glænd/ *n.* tezi: sehemu ya mwili inayochambua vitu vya kutumika au kutolewa mwilini. **~ular** *adj.* -a tezi au kama tezi.
**glare** /gleə(r)/ *n.v./i.* ng'aa; mng'aro; mtazamo wa hasira au ukali; ng'aa. **glaring** *adj.* wazi; dhahiri; bayana; -a kutia kiwi.
**glass** /glɑ:s/ *n.* **1.** kioo. **2.** bilauri; gilasi. **3.** darubini. **4.** baromita. *eye ~es,* miwani. *~ house,* jengo la kioo kwa ajili ya kuoteshea mimea. **~y** *adj.* -a kama kioo; (kwa macho) meupe.
**glaze** /gleɪz/ *n./v.t./i.* mpako wa rangi ya kioo; ung'arishaji; tia kioo; paka rangi ing'aayo (kama sahani na vikombe).
**glee** /gli:/ *n.* furaha; shangwe; kwaya. **~ful** *adj.* -enye furaha. **~fully** *adv.* kwa furaha.
**glib** /glɪb/ *adj.* -epesi wa kusema maneno ya udanganyifu; -enye maneno mengi.
**glide** /glaɪd/ *n.* utelezaji; unyererekaji; mtiririko. *v.i.* teleza; nyerereka; tiririka. **~r** *n.* nyiririko. **gliding** *n.* mchezo wa kunyiririka.
**glimmer** /'glɪme(r)/ *n./v.i.* mwangaza hafifu; mulika kidogo kidogo. *not a ~ of hope,* hakuna matumaini hata kidogo.

**glimpse** /glɪmps/ *n./v.t.* mtazamo wa mara moja; ona kidogo tu.
**glisten** /'glɪsn/ *v.i.* ng'aa; meremeta.
**glitter** /'glɪte(r)/ *n./v.i.* mng'aro; metameta; ng'aa.
**globe** /gləʊb/ *n.* ramani ya tufe; tufe; mviringo. *the* ~,dunia. **~fish** *n.* bunju. **~trotter** *n.* mtembezi sana nchi mbalimbali. **global** /'gləʊb(ə)l/ *adj.* -a ulimwengu mzima; -a jumla. **~ warming**, ongezeko joto la dunia: uongezekaji wa hali joto katika angahewa ya dunia usababishwao na gesi za viwandani. **globular** *adj.* -enye umbo la mviringo. **globule** *n.* tone. **globalization** *n.* utandawazi.
**glomerulus** /glɒ'mɛr(j)ʊles/ *n.* (**glomeruli**) mkusanyiko wa vijishipa vya damu hasa katika figo au mishipa ya fahamu.
**gloom** /glu:m/ *n.* utusitusi; huzuni; majonzi; ghamu. **~y** *adj.* -a huzuni; -a gizagiza.
**glory** /'glɔ:ri/ *n.* sifa kuu; uzuri; fahari; utukufu.. *v.i.* furahia; jivunia. **glorify** *v.t.* tukuza; kuza; adhimisha; faharisha. **glorious** *adj.* adhimu; -a kupendeza; -a kufurahisha.
**gloss** /glɒs/ *n.v.t.* mng'ao; sura danganyifu; ng'arisha. ~ *sth. over*, sitiri; funika. **~y** *adj.* -a kung'aa.
**glove** /glʌv/ *n.* glavu. *be hand in ~with*, -wa chanda na pete.
**glow** /gləʊ/ *n./v.i.* mng'ao; mwanga wa moto; mweka; waka bila kutoa ndimi za moto; ona joto. **~worm** *n.* kimulimuli; kimetameta.
**glucose** /'glu:kəʊs, -z/ *n.* glukosi.
**glue** /glu:/ *n.* gundi. *v.t.* gandisha kwa gundi. **glutinous** *adj.* -a kunata.
**glut** /glʌt/ *n./v.t.* wingi mno; ufurikaji; sheheneza; furisha; jaza sana. ~ *oneself*, -la mno; vimbiwa.
**glycogen** /'glʌɪkədʒ(ə)n/ *n.* glikojeni: **1.** aina ya polisakaridi ambayo hutengenezwa na ini kutokana na kuunganishwa kikemikali kwa sukari ya glukosi iliyomo ndani ya damu. **2.** aina ya wanga unaopatikana kwenye mimea au wanyama.
**gnash** /naʃ/ *v.i./t.* saga meno.
**gnat** /nat/ *n.* aina ya usubi.
**gnaw** /nɔ:/ *v.t./i.* tafuna; guguna; sumbua; udhi.
**GNP** /ˌdʒi: en 'pi:/ *n.* ufupisho wa **gross national product**: jumla ya pato la nchi kutoka ndani na nje.
**gnu** /nu:; nju/ *n.* kongoni.
**go** /gəʊ/ *v.i.* (**went**, **gone**) **1.** enda. **2.** fika. *How far does this road ~?* njia hii inaishia wapi? **3.** pata kuwa. ~ *blind*, pofuka. ~ *bad*, oza. ~ *asleep*, sinzia. **4.** fanya kazi; enda vizuri. *Is your clock ~ing?* saa yako inakwenda? **5.** -wa; ishi. *Always ~ armed*, nenda na silaha daima. ~ *naked*, enda uchi. **6.** weka. *These books always ~ on the top*, vitabu hivi huwekwa juu siku zote. **7.** vunjika. *The mast went in the storm*, mlingoti ulivunjika kwa dhoruba. **8.** (kwa fedha) tumiwa. ~ *about sth.*, anza kufanya. *We're not ~ing about our work properly*, hatuendelei vizuri katika kazi yetu. ~ *ahead*, anza; endelea. ~ *after*, jaribu kupata au kufuata. ~ *back (up)on*, vunja ahadi. ~ *by*, fuata. *a good rule to ~ by*, kawaida nzuri ya kuifuata. ~ *by the name of*, itwa jina. ~ *down*, zama; tulia; pokewa vizuri au kwa furaha. ~ *for*, shambulia. ~ *for a shilling*, uzwa kwa shilingi. ~ *in for*, ingia. ~ *into*, ingia; angalia kwa makini; gawanyika bila kubaki. ~ *off*, ripuka; poteza ladha. ~ *off well*, faulu; fanikiwa. ~ *on*, endelea. *be ~ing on for*, karibia. e.g. *It's ~ing on for twelve o'clock*, inakaribia saa sita. ~ *out*, zima; zimika. ~ *over*, tazama kwa uangalifu. ~ *round*, tosheleza. e.g. *The food will not ~ round*, chakula hakitatosha. ~ *through*, vumilia; pitia. ~ *through with*, timiza. ~ *together*, andamana; fuatana. ~ *with*, (kwa rangi) lingana. ~ *without*, kosa kupata. ~ *to sea*, -wa baharia. ~ *halves*, shiriki. ~ *to law*, enda mahakamani. ~ *to pieces*, haribika; vunjika. ~ *to seed*, dhoofika. *n.* nguvu; bidii. *He's full of*

~, ana bidii nyingi. *have a ~ at sth.*, jaribu. *be on the ~*, -wa -tendaji; *all the ~*, mtindo wa siku hizi. **~-between** *n.* mjumbe; msuluhishi; tarishi; mshenga; kuwadi.

**goal** /gəʊl/ *n.* **1.** goli; bao. **2.** kusudi; nia; lengo; shabaha; mradi. **~keeper** *n.* golikipa; mlinda mlango.

**goat** /gəʊt/ *n.* mbuzi. **~herd** *n.* mchunga mbuzi. **goatee** *n.* ndevu kama za mbuzi.

**God** /gɒd/ *n.* **1.** Mungu. **2.** Mola; (kwa Waislamu) Allah. **~child**, **~daughter**, **~son** *n.* mtoto wa ubatizo. **~dess** *n.* mungu wa kike. **~father**, **~mother**, **~parent** *n.* mzazi wa ubatizo. **~-fearing** *adj.* chaji Mungu. **~-forsaken** *adj.* (kwa mahali) pabaya. **~less** *adj.* ovu; siyeamini Mungu. **~ly** *adj.* -tawa, enye kushika dini; -ema. **~send** *n.* bahati kubwa isiyotazamiwa.

**godown** /'gəʊdaʊn, gəʊ'daʊn/ *n.* ghala; bohari.

**goggle** /'gɒgl/ *n.* miwani ya kuzuilia mavumbi. *v.i.* kodolea macho.

**gold** /gəʊld/ *n.* dhahabu: elementi ya kemikali yenye namba atomia 79 ya rangi ya manjano kavu, hutumika kama mapambo na kama kizio cha thamani ya fedha. **~en** *adj.* -a dhahabu; kama dhahabu; -enye rangi ya dhahabu; -a thamani sana. **~ wedding**, maadhimisho ya miaka 50 ya ndoa. **~field** *n.* machimbo ya dhahabu. **~ leaf** *n.* jalibosi. **~smith** *n.* mfua dhahabu; sonara.

**golf** /gɒlf/ *n.* mchezo wa gofu. **~ course** *n.* uwanja wa gofu. **~er** *n.* mchezaji gofu.

**gong** /gɒŋ/ *n.* upatu; mbiu.

**gonorrhoea** /,gɒnə'rɪə/ *n.* kisonono: ugonjwa wa zinaa wa kuambukiza unaotunga usaha kwenye sehemu za siri.

**good** /gʊd/ *n.* wema; uzuri; heri; faida. **~s** *n.* mali; bidhaa; shehena. *do sb. ~*, faa; nufaisha. *for ~*, kabisa. *adj.* **1.** -ema. *be ~ for*, faa. **2.** -a kweli. **3.** zaidi ya. *He took a ~ half of the loaf*, alitwaa zaidi ya nusu mkate. *It's a ~ five miles*, ni zaidi ya maili tano. **4.** -ingi. *a ~ many*, -ingi. *a ~ few*, -ingi kidogo. *a ~ way*, mbali kidogo. **5.** *as ~ as*, kama; sawa na. **6.** *in ~ time (for)*, mapema. *all in ~ time*, wakati ukiwadia. **7.** -zuri; -siooza. **8.** *be ~ for*, wa na uwezo wa. *be ~ for a ten mile walk*, -wa tayari kutembea maili kumi. *~ for Tshs. 1,000*, -enye kumiliki shilingi elfu moja na zaidi. *make sth. ~*, rudisha; lipa; timiza ahadi; thibitisha. **~-bye** *n.* kwa heri. **~-for-nothing** *adj.* hafifu; ovyo. **~-looking** *adj.* -zuri. **~ly** *adj.* -zuri; -ema. **~-natured** *adj.* -ema; -pole; -kunjufu. **~ness** *n.* wema; uzuri; hisani; nguvu; utamu. **~will** *n.* hisani; huruma; urafiki; ukarimu; mapenzi.

**goose** /gu:s/ *n.* (**geese**) bata bukini; salile; mjinga; baradhuli; mbumbumbu. **~step** *n.* kwenda bila kukunja magoti.

**gorge** /gɔ:dʒ/ *n.* **1.** koo; umio. **2.** korongo; genge. *v.t./i.* vimbisha kwa chakula kingi; -la kwa pupa.

**gorgeous** *adj.* -zuri sana; -enye marembo mengi.

**gorilla** /gə'rɪlə/ *n.* sokwe.

**gospel** /'gɒspl/ *n.* injili. *~ truth*, kweli kabisa.

**gossip** /'gɒsɪp/ *n.* mmbeya; mdaku; umbeya; udaku; soga. *v.i.* ongea; piga domo; sengenya.

**gouge** /gaʊdʒ, gu:dʒ/ *n.* patasi. *v.t.* piga mfuo; toa; ng'oa.

**gourd** /gʊəd, gɔ:d/ *n.* kibuyu; jamii ya mung'unye; tungu.

**govern** /'gʌv(ə)n/ *v.t./i.* tawala; zuia; ongoza. *be ~ed by the opinions of others*, ongozwa na mawazo ya wengine. **~ment** *n.* utawala; serikali; dola. **~or** *n.* gavana; mjumbe wa bodi ya taasisi; kidhibiti mwendo katika mashine.

**gown** /gaʊn/ *n.* gauni; joho.

**grab** /græb/ *n.* unyakuzi. *v.t./i.* (**-bb-**) nyakua; pokonya; nyang'anya.

**grace** /greɪs/ *n.* uzuri; madaha; adili adabu; hisani; mapenzi; rehema; dua; neema. *be in sb.'s good ~s*, tendewa hisani na. *do sth. with a good ~*, fanya jambo kwa moyo safi.

*act of* ~, fadhila; hisani. *His, Her, Your* ~, muhasham; mtukufu. *v.t.* pamba; tunuku. **~ful** *adj.* -zuri, enye madaha. **~fully** *adv.* kwa madaha. **~less** *adj.* -baya; -bovu; bila adabu. **gracious** *adj.* -enye hisani; -enye neema; enye rehema. *good ~!* lahaula! **~ly** *adv.* kwa huruma.

**gradate** *v.i./t.* geuka polepole; panga katika daraja. **gradation** *n.* mgeuko wa polepole; daraja ya maendeleo; apofonia. **grade** *n.* cheo; daraja; hadhi; mteremko; mwinamo. *v.t.* panga katika daraja; sawazisha ardhi. **gradient** *n.* mteremko; mshuko. **gradual** *adj.* kidogo kidogo; -a polepole. **~ly** *adv.* polepole; kwa taratibu.

**graduate** /'gradʒʊət, -djʊət/ *n.* mhitimu. *v.i.* panga kwa daraja; pata shahada; hitimu. **graduation** *n.* mahafali.

**graft**[1] /grɑ:ft/ *n.* **1.** kipandikizi: kitawi cha mti kilichopandikizwa kwenye mti mwingine. **2.** kipande cha ngozi au mfupa, cha mtu au cha mnyama, kilichotiwa mwilini au katika sehemu nyingine ya mwili uleule. *v.t./i.* pandikiza.

**graft**[2] /grɑ:ft/ *n.* rushwa; udanganyifu. *v.i.* -la rushwa; danganya.

**grain** /greɪn/ *n.* punje; chembe; nafaka; kizio kidogo kabisa cha uzito; mpangilio asili wa fumwale katika mbao. *without a ~ of sense,* bila akili hata. *against the ~,* vigumu; haipendezi. *go against the ~,* chukiza; kasirisha.

**grammar** /'græmə(r)/ *n.* sarufi. **grammatical** *adj.* -a sarufi, -enye kufuata kanuni za sarufi.

**gram(me)** /græm/ *n.* gramu: kizio cha uzito katika mfumo wa metriki.

**granary** /'grænəri/ *n.* ghala ya nafaka.

**grand** /grænd/ *adj.* -kubwa; kuu; muhimu; maalumu; kamili; -zima; -tukufu; -a fahari; -a heshima; ashrafu; -zuri sana; -adilifu. *have a ~ time,* furahi sana. **~eur** *n.* fahari; utukufu. **~child,** mjukuu. **~daughter,** mjukuu wa kike. **~son,** mjukuu wa kiume. **~parent,** babu au bibi. **~father,** babu. **~mother,** bibi.

**granite** /'granɪt/ *n.* itale: aina ya mawe magumu ya kijivu yanayotumika sana katika ujenzi.

**grant** /grɑ:nt/ *n.* hiba; ruzuku. *v.t.* ruhusu; idhinisha; ridhia; kubali. *take sth. for ~ed,* chukulia kuwa jambo ni la kweli au litatokea.

**granulocyte** /'granjʊlə(ʊ)sʌɪt/ *n.* selipunje: seli nyeupe ya damu yenye punjepunje katika uteseli.

**grape** /greɪp/ *n.* zabibu. **grapefruit** *n.* balungi. **~vine** *n.* mzabibu.

**graph** /grɒ:f, graf/ *n.* grafu. **~ic** *adj.* -a alama zinazoonekana; bayana; -a dhahiri. **~ically** *adv.* kwa kuandika au kuchora; bayana; waziwazi; dhahiri.

**graphite** /'græfaɪt/ *n.* grafiti: aina ya kaboni laini nyeusi itenge nezewayo penseli.

**grapple** /'græpl/ *v.t./i.* kamatana na; ng'ang'ania; *(fig.)* shughulikia, jitahidi sana kutatua jambo fulani.

**grasp** /grɑ:sp/ *n.* uwezo wa kushika; ufahamu. *v.t./i.* shika; fumbata; fahamu. *~ at,* jaribu kukamata; pokea kwa bidii **~ing** *adj.* -choyo; bahili.

**grass** /grɑ:s/ *n.* majani. **~hopper** *n.* panzi.

**grate**[1] /greɪt/ *v.t./i.* kuna; paruza; kwaruza; lia kwa kuparuza; chukiza. *~ coconut,* kuna nazi. *coconut ~r,* mbuzi.

**grate**[2] /greɪt/ *n.* chanja za chuma kwenye tanuri. **grating** *n.* kiunzi cha nondo kitumikacho kuwa kinga.

**grateful** /'greɪtfl/ *adj.* -enye shukrani; -a kupendeza; - tamu. **gratify** *v.t.* pendeza; furahisha; ridhisha. **gratitude** *n.* shukrani.

**gratis** /'gratɪs, 'grɑ:-, 'greɪ-/ *adv./adj.* bure; bila malipo. **gratuitous** *adj.* bure; bila malipo; bila sababu. *a ~ insult,* tusi la bila sababu. **gratuity** *n.* zawadi; bahashishi; kiinua mgongo.

**grave**[1] /greɪv/ *n.* kaburi; ziara. *have*

*one foot in the ~,* chungulia kaburi. **~-clothes** *n.* sanda. **~-digger** *n.* mchimba kaburi. **~yard** *n.* mava; makaburini.

**grave**[2] /greɪv/ *adj.* -enye kuhitaji makini; -kubwa; -a hatari. *a ~ offence,* kosa kubwa.

**gravity** /'grævəti/ *n.* uzito; utaratibu; ukubwa; mvutano. **specific gravity**, uzito wa kitu kulingana na ule wa maji. **gravitational acceleration**, mchapuo graviti: mchapuko wa gimba linapoanguka kuelekea ardhini. **gravitational collapse**, mporomoko graviti: mporomoko wa nyota kutokana na kani ya mvutano wake yenyewe. **gravitational field**, uga wa uvutano: nafasi inayozunguka gimba kubwa ambamo gimba kubwa lingine hupata kani ya uvutano.

**gravel** /'grævl/ *n.* changarawe; kokoto.

**gravy** /'greɪvi/ *n.* mchuzi; rojo.

**graze**[1] /greɪz/ *v.i./t.* -la majani; lisha; chunga.

**graze**[2] /greɪz/ *n.* mchubuko; mkwaruzo. *v.t.* paruza; chubua kidogo.

**grease** /gri:s/ *n.* shahamu iliyoyeyushwa; grisi. *v.t.* tia mafuta (hasa katika mashine).

**great**[1] /greɪt/ *adj.* -kubwa; -kuu; maarufu; ingi; adhimu; muhimu. **~ness** *n.* ukuu; ukubwa; utukufu; nguvu.

**great**[2] /greɪt/ *pref.* **~-grandfather**, baba mzazi wa babu. **~-grandson**, kitukuu.

**greed** /grɪ:d/ *n.* choyo; ulafi; uroho. **~ily** *adv.* kiroho; kichoyo. **~iness** *n.* choyo; ulafi; uroho. **~y** *adj.* -lafi; -choyo; -roho.

**green** /grɪ:n/ *n.* **1.** rangi ya kijani. **2.** mboga za kijani. **3.** kiwanja cha kuchezea. *adj.* kijani kibichi; chanikwiti; -bichi, (kwa mti) -bichi; -zuzu; -jinga. **~ery** *n.* majani ya kijani. **~grocer** *n.* muuza mboga na matunda. **~horn** *n.* mjinga; zuzu. **~house** *n.* nyumba ya kuoteshea maua na matunda. **~house gas** *n.* gesijoto: gesi yoyote katika hewa inayofyonza nishati joto inayotolewa na ardhi.

**GMT** /ˌdʒi: 'em 'ti/ *n.* ufupisho wa *Greenwich Mean Time:* wakati juu ya mstari wa longitudo upitao Greenwich, hutumiwa kuwa ni msingi wa nyakati za nchi zote duniani.

**greet** /grɪ:t/ *v.t.* salimu; amkia; pokea. **~ing** *n.* salamu; maamkizi; e.g. shikamoo! hujambo!

**gregarious** /grɪ'gɛ:rɪəs/ *adj.* -enye kukaa makundi makundi.

**grenade** /grə'nəɪd/ *n.* kombora.

**grey** /greɪ/ *adj./n.* (**gray**) -a kijivu; rangi ya kijivu. **~hound** *n.* aina ya mbwa wa kuwindia.

**grid** /grɪd/ *n.* **1.** gridi: mfumo wa nyaya zipitishazo umeme **2.** mstariramani: mfumo wa miraba ya mistari katika ramani. **3.** chanja za chuma za kukaangia nyama. **~dle** *n.* kikaango.

**grief** /grɪ:f/ *n.* huzuni; majonzi; kibuhuti; kihoro; kitu kiletacho huzuni. *come to ~,* pata hasara.

**grievance** /'gri:vəns/ *n.* nung'uniko; lalamiko; dai. **grieve** *v.t./i.* sikitisha; huzunisha; sikitika; huzunika.

**grievous** /'gri:vəs/ *adj.* -a kuhuzunisha; -a kusikitisha.

**grim** /grɪm/ *adj.* -kali; -zito; -katili; -a kuogofya. **~ace** *n.* mkunjo wa uso. *v.i.* kunja uso.

**grin** /grɪn/ *n./v.i.* (**-nn-**) tabasamu; kenua; kenya.

**grind** /graɪnd/ *n.* kazi ngumu ya muda mrefu. *v.t./i.* saga; sagika; onea; dhulumu; chua; noa; fanya kazi kwa bidii. **~stone** *n.* kinoo; cherehe. *keep sb.'s nose to the ~-stone,* lazimisha kufanya kazi bila ya kupumzika.

**grip** /grɪp/ *n.* ushikaji; ukamataji; nguvu; uwezo; klachi. *v.t./i.* (**-pp-**) shika, kamata sana; fahamu; shikamana. *have a good ~ of a problem,* fahamu vyema tatizo. *come to ~s with the enemy,* shambulia adui kwa nguvu.

**grit** /grɪt/ *n.* mchanga; changarawe;

ujasiri; uvumilivu.*v.t.* (**-tt-**) ~ *the teeth*, saga meno; jikaza kisabuni. **~ty** *adj.* jasiri; -enye mchanga.
**groan** /grəʊn/ *n.* kite; uuguaji; koroma; gumia; piga kororo. *v.i.* ugua; piga kite.
**grocer** /'grəʊsə(r)/ *n.* muuza vyakula. **~y** *n.* biashara ya kuuza vyakula; bidhaa za vyakula.
**groin** /grɔɪn/ *n.* manena; kinena.
**groove** /gru:v/ *n.* **1.** mfuo. **2.** *(fig.)* desturi; mazoea. *He has got into* ~, afuata mkondo. *v.t.* kata mfuo.


groove

**gross** /grəʊs/ *n.* dazeni kumi na mbili. *adj.* **1.** -sio na adabu. **2.** -baya sana. **3.** -nene; -zito. ~ *eater*, -lafi kamili. **4.** jumla; kamili; yote. ~ *amount*, jumla yote. **~ly** *adv.* sana; mno.
**ground** /graʊnd/ *n.* **1.** nchi; ardhi. *Our plans fell to the* ~, mipango yetu iliharibika. *hold one's* ~, simama imara; shikilia msimamo. *shift one's* ~, ghairi; badili msimamo. *suit sb. down to the* ~, falia sana mtu. *cover* ~, safiri; eleza mambo mengi. **2.** kiwanja. *cricket* ~, kiwanja cha kuchezea kriketi. *fishing* ~*s*, vuo. **3.** eneo; nafasi. **4.** sababu ya kusema, kufanya au kusadiki jambo. *v.t./i.* **1.** pweleza; pwelewa; (kwa mashine) kukaa bila kufanya kazi kwa sababu ya ubovu. **2.** panda mwamba. **3.** zoeza katika jambo. **~ing** *n.* mafundisho ya msingi. **~less** *adj.* bila sababu nzuri. **~(s) man** *n.* mtu atunzaye kiwanja cha kuchezea. **~nut** *n.* njugu mawe. **~ rent** *n.* kodi ya kiwanja. **~swell** *n.* kujengeka kwa maoni fulani katika sehemu kubwa ya jamii; mawimbi. **~work** *n.* msingi; asili; mwanzo.
**group** /gru:p/ *n.* jamii; kundi; kikosi; bendi; kikundi; fungu. *v.t.* panga katika makundi. *v.i.* kusanyika pamoja.
**grove** /grəʊv/ *n.* kichaka.
**grow** /grəʊ/ *v.i./t.* (**grew**, **grown**) **1.** kua; ota; mea. ~ *up*, pevuka. **2.** kuza; otesha. **3.** zidi; ongezeka: ~ *older*, konga; chakaa. ~ *less*, pungua. **4.** ~ *upon*, zidi kupendeza. *This habit* ~*s upon me*, nazidi kufuata tabia hii. *This book* ~*s on me*, nazidi kukipenda kitabu hiki. **~er** *n.* mwoteshaji mimea. *a tomato-*~*er*, mwoteshaji nyanya. **~n- up** *n.* mtu mzima. **~th** *n.* uotaji; ukuaji; uendeleaji.
**growl** /graʊl/ *n.* ngurumo; manung'uniko; mvumo. *v.i.* nguruma; vuma; nung'unika.
**grudge** /grʌdʒ/ *n.* fundo; kinyongo. *v.t.* nyima; husudi. *bear a* ~ *against*, kamia; chukia; -wa na kinyongo kwa; -wa na kisasi kwa. **grudgingly** *adv.* kwa unyimivu; kwa chuki.
**gruff** /grʌf/ *adj.* (kwa mtu) wa tabia mbaya; (kwa sauti) a kukwaruza.
**grumble** /'grʌmbl/ *n.* nung'uniko; lalamiko. *v.i.* nung'unika; lalamika. **~r** *n.* mnung'unikaji.
**grumpy** /'grʌmpi/ *adj.* -enye kisirani; enye hasira.
**grunt** /grʌnt/ *n./v.i./t.* mguno; guna; koroma.
**guano** /'gwa:nəʊ/ *n.* guano; kinyesi cha ndege wa bahari kitumikacho kama mbolea.
**guarantee** /,gærən'ti:/ *n.* **1.** dhamana. **2.** ahadi. **3.** mdhamini. *be* ~ *for your friend's good behaviour*, chukua dhamana kwa mwenendo mzuri wa rafiki yako. **4.** amana; rehani. **5.** *(colloq.)* hakikisho. *v.t.* dhamini; weka rehani; toa hakikisho; ahidi. **guarantor** *n.* mdhamini.
**guard** /ga:d/ *n.* **1.** hadhari; lindo. *be on one's* ~, jihadhari. *keep* ~, linda. **2.** mlinzi. **3.** kinga. e.g. *fire* ~, kinga-moto. *mud* ~, kinga-matope. *v.t./i.* linda; hifadhi. ~ *against*, kinga; epuka kwa hadhari. **~ cell** *n.* seli linzi; mojawapo ya seli mbili ambazo huzingira tundu ya stomata katika mimea. **~ed** *adj.* -a hadhari; -angalifu. **~room** *n.* mahabusu. **guardian** *n.* mlinzi; mlezi. **~ship** *n.* ulinzi; ulezi.

**guerilla** /gəˈrɪlə/ *n.* mpiganaji wa msituni.

**guess** /ges/ *n./v.t./i.* kisio; bahatisho; dhanio; kisia; bahatisha; dhani.

**guest** /gest/ *n.* mgeni. ~ *house*, hoteli; nyumba ya wageni. ~ *of honour*, mgeni wa heshima. ~ *room*, chumba cha wageni.

**guide** /gaɪd/ *n.* kiongozi; kielekezi; kiashirio; kishawishi. *girl* ~, skauti wa kike. *~book*, kitabu cha kuongoza wageni. *~line*, mwongozo; maelekezo. *v.t.* ongoza; elekeza; onyesha njia. **guidance** *n.* mwongozo; elekezo; ushauri.

**guild** /gɪld/ *n.* chama; ushirika; jumuia.

**guilt** /gɪlt/ *n.* kosa; hatia; uovu. **~y** *adj.* -enye kosa. *he is ~y*, ana hatia.

**guinea-pig** *n.* nungubandia.

**guitar** /gɪˈtɑ:(r)/ *n.* gita.

**gulf** /gʌlf/ *n.* hori; ghuba; shimo kubwa; korongo; *(fig.)* tofauti kubwa baina. *Persian* ~, Ghuba ya Uajemi.

**gull** /gʌl/ *n.* shakwe; membe.

**gullet** /ˈgʌlɪt/ *n.* umio; koo; kimio.

**gully** /ˈgʌli/ *n.* mfereji; mfereji wa maji machafu.

**gulp** /gʌlp/ *v.t./i.* meza upesi; gugumiza; bwia.

**gum**[1] /gʌm/ *n.* ufizi; sine.

**gum**[2] /gʌm/ *n.* gundi; urimbo; sandarusi. *chewing* ~, ubani. **~boot** *n.* buti ya mpira.

**gun** /gʌn/ *n.* bunduki. *stick to one's ~s*, shikilia msimamo wako. **~boat** *n.* manowari ndogo inayobeba mizinga. **~cotton** *n.* baruti ya pamba. **~ner** *n.* mpiga mzinga. **~powder** *n.* baruti. **~shot** *n.* mpigo wa bunduki; masafa ya risasi inapofika. **~smith** *n.* mfua bunduki.

**gurgle** /ˈgɜ:gl/ *n.* mbubujiko wa maji. *v.i.* sukutua; gugumia; bubujika.

**gush** /gʌʃ/ *n./v.i.* ububujikaji; ufokaji; bubujika; foka; zungumza kwa shauku.

**gust** /gʌst/ *n.* dharuba; mvua ya ghafla; moto wa ghafla. ~ *of anger*, hasira -a ghafla.

**gusto** /ˈgʌstəʊ/ *n.* furaha; pupa.

**gut** /gʌt/ *n.* **1.** matumbo; utumbo. **2.** *(fig.)* ujasiri. *He has no ~s*, hana ujasiri. **3.** uzi wa utumbo wa mnyama utumikao kwa kutengenezea zeze. *v.t.* (**-tt-**) teketeza. *a house ~ted by fire*, nyumba iliyoteketezwa kwa moto.

**gutter** /ˈgʌtə(r)/ *n.* mchirizi; mfereji; mlizamu. *v.i.* (kwa mshumaa) waka kwa vipindi.

**guttural** /ˈgʌt(ə)r(ə)l/ *adj.* (sauti) -a kooni, (kama sauti ya *gh* katika *ghafla*).

**gymkhana** /dʒɪmˈkɑ:nə/ *n.* tamasha ya michezo; kiwanja cha michezo.

**gymnasium** /dʒɪmˈneɪzɪəm/ *n.* ukumbi wa michezo ya mazoezi ya viungo. **gymnast** *n.* mwanamichezo stadi wa michezo hiyo. **gymnastic** *adj.* -a mazoezi ya viungo. **~s** *n.* mazoezi ya viungo.

# Hh

**Haber process** *n.* mfanyikotendani wa Haber: mfanyikotendani wa kutengeneza amonia kutokana na hidrojeni na nitrojeni kwa uwianisho wa 1:3 ( moja kwa tatu).

**habit** /ˈhæbɪt/ *n.* mazoea; desturi; mwenendo; tabia; hali; vazi; nguo. *riding-~*, mavazi ya kuvaliwa kwa kupanda farasi. **~able** *adj.* -a kukalika. **~at** *n.* makazi; mazingira. **~ation** *n.* ukaazi; kuishi; makazi; nyumba. **~ual** *adj.* -a mazoea; -a kawaida; -a desturi; -zoefu; liokubuhu. **~ually** *adv.* kwa desturi; kwa kawaida. **~uate** *v.t.* zoeza.

**hack**[1] /hæk/ *v.t./i.* **1.** katakata; tema; chonga. *a ~ing cough*, kikohozi kikavu. **~saw** *n.* msumeno wa kukatia chuma. **2.** tumia kompyuta

ili kupata data kwa njia haramu au kuharibu programu kwenye mtandao.

**hack**[2] /hæk/ *n.* farasi wa kukodi; mtu aliyeajiriwa kufanya kazi ngumu isiyopendeza. **~neyed** *adj.* -liotumika sana (hata kuchakaa au kuchosha).

**hacker** /'hækə(r)/ *n.* gwiji wa kompyuta; mwizi wa taarifa na data za kompyuta.

**haemoglobin** /ˌhi:mə'gləʊbɪn/ *n.* hemoglobini: kemikali katika seli nyekundu za damu inayosafirisha oksijeni mwilini.

**haemophilia** /ˌhi:mə'fɪlɪə/ *n.* hemofilia: ugonjwa wa kurithi unaotokana na ukosefu wa kemikali zinazozuia damu kutoka kwa wingi mtu anapojeruhiwa.

**haemorrhage** /'hɛmərɪdʒ/ *n.* utokaji damu.

**haggard** /'hægəd/ *adj.* -liokonda; -liosawijika; -liodhoofika.

**haggle** /'hægl/ *v.i.* patana bei sana.

**hail**[1] /heɪl/ *n.* mvua ya mawe; wingi; mfululizo. *v.i.t.* -nya mvua ya mawe; -ja kwa wingi.

**hail**[2] /heɪl/ *n.* salamu; wito. *v.t./i.* salimu; ita; pigia kelele; pongeza. *~ from,* toka, tokea. *within ~,* -wa karibu hata kuweza kuitwa. *be ~ fellow well met with (sb.),* wa kunjufu mno.

**hair** /heə(r)/ *n.* unywele; nywele; malaika; manyoya; singa. *not turn a ~,* kutoogopa hata kidogo. *make sb.'s ~ stand on end,* tisha sana. **~dresser** *n.* kinyozi. **~ follicle** *n.* shina la nywele: kishimo kama tyubu katika ngozi ya mamalia kwenye mzizi unaosababisha nywele kuota. **~pin** *n.* chupio. **~pin bend** *n.* kona kali. **~-splitting** *adj.* -a kuleta mabishano ya bure. **~y** *adj.* -enye nywele nyingi; -liofunikwa kwa nywele.

**half** /hɑ:f/ *n./adj.* nusu. *go halves with sb. in sth.,* gawana nusu kwa nusu. *do sth. by halves,* fanya jambo ovyoovyo. *too clever by ~,* -sio na akili ya kutosha. *one's better ~, (colloq.)* mke; mume. *not ~!* naam; hasa. **~blood** *n.* ndugu wa kuchangia mzazi mmoja. **~-hearted** *adj.* -zembe, -sio na bidii. **~holiday** *n.* nusu siku. **~-life** *n.* nusumaisha: muda unaotumiwa na nusu atomi na kusababisha mbunguo katika sampuli ya harakatiredio hivyo kuifanya iwe nusu. **~mast** *n.* nusu mlingoti. **~-witted** *adj.* -pungufu wa akili.

**hall** /hɔ:l/ *n.* ukumbi; bwalo; bweni; sebule.

**hallelujah** /ˌhalɪ'lu:jə/ *n./int.* aleluya.

**hallo** *int.* halo: ukelele wa kuita.

**Halley's comet** *n.* nyotamkia ya Halley: nyota mkia inayoonekana katika anga la dunia kila baada ya miaka 76.

**halogen** /'halədʒ(ə)n, 'heɪl-/ *n.* halojeni: elementi simetali yenye nafasi saba za valensi kwenye elektroni juu ya mzingo wake wa nje.

**halt** /hɔ:lt/ *n./v.t./i.* kituo; simamisha; simama. **~ingly** *adv.* kwa kusitasita.

**halter** /'hɔ:ltə(r)/ *n.* hatamu.

**halve** /hɑ:v/ *v.t.* gawa nusu nusu; punguza kwa nusu yake.

**ham** /hæm/ *n.* hemu: paja la nguruwe lililokaushwa; paja la mnyama.

**hammer** /'hæmə(r)/ *n.* nyundo; mnada. *go at sth. ~ and tongs,* fanya kwa bidii nyingi; gombana kwa kelele. *come under the ~,* uzwa mnadani. *v.t./i.* gongomea; piga nyundo; piga mfululizo. *~ out a solution,* fikia suluhisho baada ya mjadala mrefu.



**hammock**

**hammock** /'hæmək/ *n.* kitanda cha bembea.

**hamper** /'hæmpə(r)/ *v.t.* zuia; tatanisha.

**hand** /hænd/ *n.* mkono; uwezo; mamlaka; madaraka; ustadi; mshiriki; mzoefu; akrabu; upande; mwandiko. *at ~,* karibu. *live from ~ to mouth,* ishi maisha ya kijungumeko. *in ~,* tayari; -

naotendeka; -naoendelea. *out of ~,* -sioweza kudhibitiwa. *win ~s down,* shinda kwa urahisi. *keeps one's ~in,* dumisha umahiri. *with a heavy ~,* kwa ukali. *with a high ~,* kwa ukaribu. *The matter is in your ~s,* ni juu yako. *on the right ~,* upande wa kulia. *on all ~s,* pande zote. *~writing,* mwandiko. *v.t.* -pa; pitisha; saidia kwa mkono. **~bag** *n.* mkoba; begi. **~book** *n.* kitabu cha maelekezo; kiongozi. **~cuff** *n.* pingu. **~ful** *n.* konzi; kiasi kidogo; -chache; tukutu, sumbufu.

**handicap** *n.* kikwazo; kilema; upungufu. **~icraft** *n.* sanaa ya ufundi.

**handkerchief** *n.* leso; hanjifu.

**handle** *n.* mpini; mkono; kipete. *v.t.* gusa; shika; simamia; tendea; nunua; uza. **~bar** *n.* usukani.

**handsome** *adj.* -zuri; -kubwa.

**hang** /hæŋ/ *n.* mning'inio; maana. *get the ~ of sth.,* elewa kilichosemwa au kuandikwa; elewa jinsi ya kutumia kitu. *He doesn'nt care a ~,* hajali kabisa. *v.t./i.* (**hung hanged**) tundika; ning'iniza; ning'inia; nyonga. *~ a door,* tia mlango bawaba. *~ the head,* inamisha kichwa kwa aibu. *~ fire,* kawia kufyatuka; endelea polepole. *~ about,* randaranda. *~ back,* sita. *~ on to,* shikilia. *~ together,* saidiana; shirikiana. *be hung up,* kawishwa; cheleweshwa; katishwa tamaa. **~dog** *adj.* -danganyifu tena -a kuona aibu; -a kufedheheka. **~er** *n.* henga. **~-on** *n.* mdoezi. **~ings** *n.* mapazia.

**hangar** /'haŋə/ *n .* banda la ndege.

**haphazard** /hap'hazəd/ *n./adv.* bahati; -a ovyo; ovyoovyo; shaghalabaghala.

**happen** /'hæpən/ *v.i.* tokea; jiri; tendeka. *~on,* kuta; ona; pata kwa bahati. **~ing** *n.* jambo; tukio.

**happy** /'hæpi/ *adj* -a furaha; -a bahati; -lioridhika. **~-go-lucky** *adj.* -enye kubahatisha maisha bila ya juhudi za makusudi.

**harass** /'harəs, hə'ras/ *v.t.* udhi; sumbua; bughudhi; shambulia mara nyingi.

**harbour** /'hɑ:bə(r)/ *n.* bandari; *(fig.)* kimbilio; kituo. *v.t.* linda; ficha; hodhi; tia nanga; hifadhi. *~ a criminal,* hifadhi mhalifu.

**hard** /hɑ:d/ *adj.* -gumu; -isiyokuwa rahisi; -a tabu; -a dhiki; -a shida; -kali; -korofi; -kavu; -kakamavu; -enye juhudi. *~ cash* fedha taslimu. *~ water,* maji magumu. *be ~ of hearing,* tosikia vyema; *~ labour,* kazi ngumu. *~ and fast rules,* kanuni zisizobadilika. *~ luck,* bahati mbaya. *~ times,* siku za dhiki au shida. *adv. be ~up,* zidiwa; -wa bila ya fedha. *be ~ put to it,* -wa katika shida. *~ by,* karibu. *~ upon,* sio nyuma sana. **~en** *v.t./i.* fanya -gumu; -wa gumu. **~-headed** *adj.* -a busara; -a akili barabara. **~-hearted** *adj.* -enye moyo mgumu; katili. **~ihood** *n.* uhodari; uthabiti; ujasiri. **~ly** *adv.* kwa shida; tu. **~ness** *n.* ugumu; uyabisi; ushupavu; ukali. **~ship** *n.* taabu; shida; dhiki. **~ware** *n.* vifaa vya chuma na mabati, ujenzi na kompyuta. **~ water** *n.* maji magumu: maji ambayo hayatoi povu la sabuni kwa urahisi kwa sababu yana chumvi, misombo halisi, magnesi na feri iliyomumunyika kwenye maji hayo. **~y** *adj.* hodari; -jasiri; -stahamilivu.



**hare**

**hare** /heə(r)/ *n.* sungura. **~-brained** *adj.* -pumbavu.

**harem** /'hɑ:ri:m/ *n.* harimu: nyumba ya wake na masuria.

**hark** /hɑ:k/ *v.i.* sikiliza kwa makini.

**harm** /hɑ:m/ *n./v.t.* madhara; dhuru. **~ful** *adj.* -a kudhuru. **~less** *adj.* si -a kudhuru.

**harmonium** /hɑ:'məʊnɪəm/ *n.* kinanda; harmoni.

**harmony** /hɑ:məni/ *n.* upatanifu; amani; ulinganifu; mwafaka. **harmonious** *adj.* -patananifu; linganifu. **harmonize** *v.t./i.* patanisha; linganisha; lingana; patana.

**harpoon** /hɑ:pu:n/ *n.* chusa. *v.t.* vua

kwa chusa; piga chusa.
**harrow** /'hærəʊ/ *n.* haro. *v.t.* lima kwa haro; *(fig.)* huzunisha; udhi.
**harsh** /hɑ:ʃ/ *adj.* -a kuchukiza; -kali; katili.
**harvest** /'hɑ:vɪst/ *n.* mavuno; mazao; matokeo. **~er** *n.* mvunaji; mashine ya kuvunia.
**hasp** /hɑ:sp/ *n.* kipete; pete ya kufungia.
**haste** /heɪst/ *n.* wepesi; haraka; hima. *make ~*, fanya hima. **~n** *v.i./t.* fanya hima; himiza; jihimu; harakisha. **hasty** *adj.* -a haraka; -a ghafla.
**hat** /hæt/ *n.* kofia; chepeu; heti. *talk through one's ~(colloq.)* bwabwaja.
**hatch** /hætʃ/ *v.t./i.* angua; totoa; buni; tunga. *~ a plot*, buni njama. **~ery** *n.* mahali pa kuangulia mayai.
**hatchet** /'hætʃɪt/ *n.* kishoka; shoka. *bury the ~*, acha ugomvi; patana.
**hate** /heɪt/ *n./v.t.* chuki; chukia. **~ful** *adj.* -a kuchukia, -a kuchukiza. **hatred** *n.* chuki.
**haughty** /'hɔ:ti/ *adj.* -enye kiburi; -enye kujivuna; -enye maringo.
**haul** /hɔ:l/ *n.* vuo; pato; gharama ya usafirishaji. *v.t.* kokota, burura; buruta. *~ sb. over the coals*, karipia; kemea.
**haunch** /hɔ:ntʃ/ *n.* paja la mnyama au binadamu.
**haunt** /hɔ:nt/ *n.* maskani; makazi; makao. *v.t.* rudia, tembelea mara kwa mara. *the ~ of criminals*, makao ya wahalifu. **~ed** *adj.* -pa kuzuriwa sana na mashetani.
**have** /həv; əv; hæv/ *v.t.***1.** -wa na. **2.** pata; patia; kubali; chukua. *I won't ~ you saying such things*, sitaki useme mambo kama hayo. **3.** fanyisha. *~ the eggs cooked well*, pikisha vizuri mayai. *~ a leg broken*, vunjwa mguu. *~ one's father die*, fiwa na baba. **4.** lazima; sharti. *I ~ to go*, lazima niende. **5.** *(colloq.)* punja; danganya. *he's been had*, amedanganywa; amepatikana. *~ to do with*, shughulika na; husika na. *~ sth. to do with*, husika na. *~ sth. out of sb.*, fanikiwa kupata jambo kutoka kwa mtu.
**haven** /'heɪvn/ *n.* kimbilio; kituo; mahali pa usalama.
**havoc** /'hævək/ *n.* maangamizi; uharibifu mkubwa; vurumai; nakama.
**hawk** /hɔ:k/ *n.* shakevale; kozi; mwewe.
**hawker** /'hɔ:kə(r)/ *n.* mchuuzi; mmachinga.
**hay** /heɪ/ *n.* nyasi kavu.
**hazard** /'hazəd/ *n.* hatari. *v.t.* hatarisha; bahatisha; jaribu. **~ous** *adj.* -enye hatari.
**haze** /heɪz/ *n.* ukungu; mvuke; umande; utusitusi. **hazy** *adj.* enye ukungu; *(fig.)* si bayana.
**HCF** *n.* ufupisho wa *highest common factor*, kigawanyo kikubwa cha pamoja.
**he** /hi; i:; i/ *pron.* yeye mwanamme.
**head** /hed/ *n.* **1.** kichwa; kitu chenye umbo la kichwa. **2.** akili. *lose one's ~*, changanyikiwa. *off one's ~*, -enye wazimu. *take it into one's ~ that* amini kuwa. *talk above their ~s*, zungumza kwa maneno magumu wasiyoyaelewa. **3.** mtu. *crowned ~s*, wafalme, malkia. **4.** *Fifty ~ of sheep*, kondoo hamsini. **5.** juu. *at the ~ of the list*, juu katika orodha. **6.** mkuu. *the ~ of the school*, mkuu wa shule. **7.** sura. **8.** kipeo; upeo. *v.t./i.* ongoza; -wa juu; -wa mwanzo; piga kichwa; elekea; endea. **~ing** *n.* anwani; dibaji; kichwa cha habari. **~land** *n.* rasi. **~quaters** *n.* makao makuu. **~strong** *adj.* -kaidi, siyesikia shauri la mtu; -shupavu. **~way** *n.* maendeleo. **~y** *adj.* -a kulevya haraka.
**heal** /hi:l/ *v.t./i.* ponya; pona. **health** *n.* uzima; afya; siha.
**heap** /hi:p/ *n.* fungu; chungu; rundo; *(colloq.)* -ingi; tele. *There were ~s of things there*, palikuwa na chungu nzima ya vitu. *v.t.* rundika; limbikiza.
**hear** /hɪə(r)/ *v.t./i.* (**heard**) sikia; sikiliza; kubali. *~ from*, pata habari kutoka. *~ of*, pata habari ya. *hear! hear!* toboa! sema! waambie! **~ing** *n.* usikivu; umbali wa kusikika;

fursa ya kusikilizwa; usikilizaji kesi mahakamani. **~say** *n.* tetesi; uvumi; fununu.

**heart** /hɑ:t/ *n.* moyo; tabia; roho; nia; bidii; huruma; asili; kiini; kipenzi; katikati. *have the ~ to,* thubutu. *lose ~,* kata tamaa. *take ~,* jipa moyo. *take sth. to ~,* athiriwa na jambo. *change of ~,* majuto. *after one's own ~,* a kupendeza hasa. *in the ~ of the forest,* katikati ya mwitu. **~ache** *n.* huzuni kubwa. **~beat** *n.* pigo la moyo. **~-breaking** *adj.* -a kuhuzunisha sana; -a kuvunja moyo. **~broken** *adj.* enye huzuni nyingi. **~burn** *n.* kiungulia. **~burning** *n.* kijicho. **~en** *v.t.* tia moyo; changamsha; fariji. **~felt** *adj.* -a dhati. **~less** *adj.* -sio na huruma; -katili. **~-rending** *adj.* -a kuvunja moyo. **~y** *adj.* -kunjufu; -a kweli; -enye afya njema; enye nguvu. *a ~ meal,* chakula kizuri. **~ily** *adv.* kwa nia njema.

**hearth** /hɑ:θ/ *n.* meko; moto.

**heat** /hi:t/ *n.* moto; joto; hasira; kushurufu; (kwa mashindano) mara; zamu. *v.t./i.* pasha moto; pata joto. **~ radiation**, unururishi joto: unururishi sumakuumeme usio onekana. **~ transfer**, kuhawilisha joto: usafirishaji wa nishati kutoka kwenye gimba au sehemu moja hadi nyingine kama matokeo ya halijoto.

**heave** /hi:v/ *n.* uvurumishaji; unyanyuaji. *-v.t./i.* inua; tupa; vurumisha; puma. *~ anchor,* ng'oa nanga. *~ a sigh,* ugua.

**heaven** /'hevn/ *n.* pepo; mbinguni; anga; mbingu; mahali pa raha zote. *good ~s!* Mungu wangu! **~ly** *adj.* - a mbinguni.

**heavy** /'hevi/ *adj.* -zito; -kubwa; -pumbavu. **heavily** *adv.* *time hanging ~ on his hands,* saa zikipita polepole. **heaviness** *n.* uzito; uzani.

**hectare** /'hɛktɛ:, -ɑ:/ *n.* hekta: kipimo cha eneo sawa na mita za mraba 10,000.

**heckle** /'hekl/ *v.t.* hanikiza; dakizadakiza.

**hedge** *n.* uwa wa miti iliyooteshwa. *v.t./i.* zungushia uwa; jibu kwa hadhari sana. **~hog** *n.* nungu-nungu. **~row** *n.* uwa.



hedge

**heed** /hi:d/ *n./v.t.* usikizi; hadhari; jali; tii. **~ful** *adj.* -angalifu; -sikivu. **~less** *adj.* siokuwa na hadhari.

**heel** /hi:l/ *n.* kisigino. *take to one's ~s,* kimbia. *cool one's ~s,* lazimishwa kungoja. *come to ~,* fuata karibu sana. *(fig.)* tii. *down at ~,* (kwa viatu) vilivyolika visigino.

**heifer** /'hɛfə/ *n.* mtamba wa ng'ombe.

**height** /haɪt/ *n.* kimo; kilele; ukomo; upeo. *the ~ of folly,* upeo wa ujinga. **~en** *v.t./i.* refusha; refuka; zidi; zidisha.

**heir** /ɛ:/ *n.* mrithi. **~ess** *n.* mwanamke mrithi. **~loom** *n.* mali ya urithi irithiwayo toka kizazi hadi kizazi.

**helicopter** /'helɪkɒptə(r)/ *n.* helikopta.

**helium** /'hi:lɪəm/ *n.* heli: gesi bwete nyepesi isiyo na rangi itumiwayo katika vyombo vya anga.

**helix** /'hi:lɪks/ *n.* (**helices**) hesi; msokoto; mzingo ndani ya sikio. **helical** *adj.* -enye hesi; liosokotwa.

**hell** /hel/ el*n.* jahanamu; motoni; mahali pa mateso. *go to ~,* potelea mbali.

**hello** /hə'ləʊ/ *int.* halo.

**helmet** /'helmɪt/ *n.* helmeti: kofia ya chuma au plastiki ngumu.

**help** /help/ *n.* msaada; msaidizi. *v.t./i.* saidia; auni; zuia; jizuia. *I can't ~ doing it,* sina budi kufanya. *It can't be ~ed,* hakizuiliki. *There's no ~ for it,* haiwezekani chochote. *~ yourself,* jisaidie mwenyewe. **~er** *n.* msaidizi. **~ful** *adj.* -enye kusaidia. **~ing** *n.* mpakuo wa mlo. **~less** *adj.* bila msaada; hoi; dhaifu. **~mate** *n.* mwenza hasa mume au mke.

**hem** /hem/ *n.* pindo; upindo. *v.t.* kunga; pinda. *~ in,* zingia.

**hemi** *prefix* nusu. **~sphere** *n.* nusu mviringo; nusu ya dunia.

**hen** /hen/ *n.* kuku; ndege mke.

**~pecked** *adj.* enye kutawaliwa na mkewe.
**henna** /'henə/ *n.* hina; mhina.
**hepatic** /hɪ'patɪk/ *adj.* -a kuhusu ini. **hepatitis** *n.* homa ya manjano.
**heptagon** /'hɛptəg(ə)n/ *n.* umbo bapa lenye pembe saba.
**her** /hə(r); ɜ:(r); ə(r)/ *pron./adj.* yeye mwanamke; -ake mwanamke. **~s** *pron.* -ake mwanamke.
**herb** /hɜ:b/ *n.* mmea; mtishamba. **~alist** *n.* mtaalamu wa madawa ya mitishamba.
**herbivore** /'hə:bɪvɔ:/ *n.* mlamea: mnyama ambaye hula mimea tu.
**herd** /hɜ:d/ *n.* **1.** kundi la wanyama. **2.** makabwela. **~sman** *n.* mchunga; mchungaji.
**here** /hɪə(r)/ *adv.* huku; humu; hapa. *~ and there,* huku na huko. *It's neither ~ nor there,* si hapa wale pale. **~abouts** *adv.* hapahapa. **~after** *adv./n.* baadaye; ahera. **~upon** *adv.* kwa hayo. **~with** *adv.* pamoja na hivi.
**hereditary** /hɪ'rɛdɪt(ə)ri/ -a kurithi. **heredity** *n.* urithi. **heritage** *n.* urithi.
**heresy** /'hɛrɪsi/ *n.* uasi wa kidini. **heretic** *n.* mwasi. **heretical** *adj.* -a uasi wa kidini.
**hermaphrodite** /hə:'mafrədʌɪt/ *n.* huntha: kiumbe chenye mifumo yote ya uzazi wa kike na wa kiume.
**hermetic** /hə:'mɛtɪk/ *adj.* -liozibwa kabisa hata hewa haiwezi kupita.
**hermit** /'hɜ:mɪt/ *n.* mtawa; walii; anayekaa pweke. **~age** *n.* makao ya mtawa au walii wa aina hiyo.
**hero** /'hɪərəʊ/ *n.* shujaa; jasiri. **~ic** *adj.* -a kishujaa, -a kijasiri. **~ine** *n.* shujaa mwanamke. **~ism** *n.* ushujaa.
**heron** /'herən/ *n.* kulastara.
**hertz** /hə:ts/ *n.* hezi: kipimo cha mzunguko mmoja kwa nukta.
**hesitate** /'hezɪteɪt/ *v.i.* sita. **hesitant** *adj.* enye kusita. **hesitation** *n.* kusita; wasiwasi; usitaji.
**hew** /hju:/ *v.t.* tema; kata; chanja.
**hexagon** /'hɛksəg(ə)n/ *n.* umbo lenye pembe sita.
**hibernate** /'haɪbəneɪt/ *v.i.* bumbwaa; kaa bila kazi; (kwa wanyama) kaa bila harakati nyakati za majira ya baridi.
**hiccup**, **hiccough** /'hɪkʌp/ *n./v.i.* kekefu; kwikwi; -wa na kwikwi.
**hide**[1] /haɪd/ *v.t./i.* (**hid**, **hidden**) ficha; jificha. **hiding** *n.* maficho. *go into hiding,* jificha. *be in hiding,* -wa mafichoni. **hideout** *n.* maficho, hasa wa aliyevunja sheria.
**hide**[2] /haɪd/ *n.* ngozi ya mnyama. **~bound** *adj.* -enye mtizamo finyu na kushikilia mambo ya kimila yaliyopitwa na wakati. **hiding** *n.* kipigo. *give someone a good hiding,* piga mtu barabara.
**hideous** /'hɪdiəs/ *adj.* -enye sura mbaya sana; -a kutisha.
**high** /haɪ/ *adj.* **1.** -a juu; -refu (kwa kwenda juu). *~ light,* sehemu ya picha yenye kuakisi mwanga. *~ priest,* kuhani mkuu. *~way,* barabara kuu. *~ school,* sekondari ya juu. *the ~ seas,* bahari kuu. *a ~ sea,* mwiza; bahari ya mawimbi makubwa. *a ~ tea,* mchanganyiko wa chai na chakula cha jioni. **2.** (kwa wakati au majira) -kuu. *~ noon,* mchana mkubwa. *~ summer,* majira ya joto kali. *It's ~ time you started,* wakati wa kuanza umewadia. **3.** (kwa nyama) anza kuoza. *adv. play ~,* cheza na kupinga fedha nyingi. *run ~,* (kwa mawimbi) ruka juu sana. **~-brow** *n./adj.* -enye akili lakini -enye majivuno pia. **~-flown** *adj.* -enye makeke; -enye mbwembwe. **~-handed** *adj.* dhalimu; -onevu. **~lands** *n.* milima. **~lander** *n.* mkaa milimani. **~-minded** *adj.* -enye msimamo; -enye maadili. **~ness** *n.* utukufu; fahari. *His (Her, Your) Highness,* mtukufu; mheshimiwa. **~ly** *adv.* sana; vema. *speak ~ of someone,* sifu sana mtu. *a ~ paid man,* mtu alipwaye mshahara mkubwa. **~ly-strung** *adj.* -epesi wa kuchochewa.
**hill** /hɪl/ *n.* kilima. **~ock** *n.* kichuguu; kiduta. **~y** *adj.* -enye vilima.
**him** /hɪm/ *pron.* yeye mwanamme.

**hind**[1] /haɪnd/ *n.* paa mke.
**hind**[2] /haɪnd/ *adj.* -a nyuma. *the ~ legs,* miguu ya nyuma. **~most** *adj.* -a nyuma kabisa. **~er** *v.t.* zuia; pinga; kawilisha. **hindrance** *n.* kizuizi; kipingamizi; pingamizi.
**hinge** /hɪndʒ/ *n.* pete; bawaba. *v.t./i.* funga kwa pete. *~ on,* tegemea.
**hint** /hɪnt/ *n.* dokezo; ishara. *v.t./i.* dokeza; ashiria.
**hinterland** /'hɪntəland/ *n.* bara.
**hip** /hɪp/ *n.* nyonga.
**hippopotamus** /ˌhɪpə'pɒtəməs/ *n.* kiboko.
**hire** /'haɪə(r)/ *n.* ujira; kodi. *v.t.* kodi; kodisha; panga; pangisha. **~ling** *n.* mamluki; mfanyakazi wa kukodiwa. **~purchase** *n.* mkopo wa kulipa kwa vipingili.
**his** /hɪz/ *pron.* -ake mwanamme.
**hiss** /hɪs/ *n./v.i./t.* mlio wa nyoka; lia kama nyoka.
**histogram** /hɪstəgræm/ *n.* histogramu: chati inayotumiwa katika takwimu kuonyesha thamani ya data kwa kutumia miraba.
**history** /'hɪstri/ *n.* historia. **historian** *n.* mtaalamu wa historia; mwanahistoria. **historic** *adj.* -a historia. **historical** *adj.* -a historia; -a kutegemea matukio ya kweli ya kihistoria.
**hit** /hɪt/ *n.* pigo; ushindi. *v.t./i.* (**-tt-**, **hit**) piga; gonga; pata. *~ it off with sb.,* patana. *be hard ~,* hasirika. *~ on,* pata kwa bahati. *lucky ~,* jambo la bahati. *make a ~,* pendeza sana kwa mtu.
**HIV** /ˌeɪʃ aɪ 'vi:/ *n.* ufupisho wa *human immunodeficiency virus:* kirusi kinachosababisha ukosefu wa kinga mwilini (ukimwi). *~ positive,* mwenye virusi vya ukimwi: hali ya kuwa na virusi vya ukimwi katika damu na hivyo kuwa tayari kuweza kuathirika na ukimwi.


**HIV magnified | kirusi kimekuzwa**

**hitch** /hɪtʃ/ *n.* mvuto; fundo; kikwazo. *v.t./i.* vuta. fungia; funga; nasa. *Everything went off without a ~,* mambo yote yalikwenda sawasawa.
**hive** /haɪv/ *n.* mzinga wa nyuki.
**hoard** /hɔ:d/ *n.* akiba; hazina. *v.i./t.* weka akiba; hodhi.
**hoarse** /hɔ:s/ *adj.* (kwa sauti) -a gonda; -a madende; (kwa mtu) -enye sauti gonda.
**hoax** /həʊks/ *n.* ubishi; mzaha; shere; dhihaka; hila. *v.t.* danganya; dhihaki; cheza shere.
**hobble** /'hɒbl/ *n.* mwendo wa kuchechemea. *v.i./t.* chechemea; tawa mnyama; funga miguu.
**hobby** /'hɒbi/ *n.* jambo afanyalo mtu kuwa ni burudani.
**hock** /hɒk/ *n.* goti la mguu wa nyuma wa mnyama.
**hockey** /'hɒki/ *n.* hoki: mpira wa magongo.
**hoe** /həʊ/ *n.* jembe. *v.t.* lima; palilia.
**hog** /hɒg/ *n.* nguruwe; *(fig.)* mtu mchafu; mlafi; mchoyo. *go the whole ~,* fanya jambo kwa ukamilifu.
**hoist** /hɔɪst/ *v.t.* inua; tweka; pandisha kwa roda.
**hold**[1] /həʊld/ *n.* mshiko; kushika; uwezo wa kushika; amri; madaraka; shikio. *v.t./i.* (**held**) **1.** shika; kamata; nasa. *~ back,* sita. *~ sth. back,* fanya kitu kisite. *~ oneself back,* jizuia. *~ by,* fuata. *~ forth,* jigamba; sema kwa kujikweza; hubiri mno. *~ off,* jitenga; kaa mbali; chelewesha. *~ out,* vumilia; stahimili; endelea kuwepo. *~ out sth.,* toa. *~ sb. or sth. up,* chelewesha; shika; zuia; shikilia kwa nguvu. *~ with,* kubali. **2.** weka; chukua. **3.** dhani; dhania; chukulia. *I ~ the view that a promise is a debt,* nachukulia kuwa ahadi ni deni. **4.** zuia. *~ the breath,* zuia pumzi. *~ one's tongue,* nyamaza. **5.** -wa na; -wa mwenyewe wa. **6.** fanya. *~ a meeting,* fanya mkutano. **7.** dumu. *~ good,* -wa na nguvu; faa. *~ hard! (colloq.)* ngoja kwanza! *~ one's own ground,* simama imara.
**hold**[2] /həʊld/ *n.* ngama (ya meli); tumbo (la meli); falka.
**hole** /həʊl/ *n.* tundu; shimo; pango;

tobo. *pick ~s in*, tafuta kosa. *be in a ~, (colloq.)* wa na mashaka. *~ and corner methods*, uayari; ujanja.
**holiday** /ˈhɒlədeɪ/ *n.* siku ya mapumziko; sikukuu; likizo.
**hollow** /ˈhɒləʊ/ *n.* shimo; mvungu; bonde. *adj.* **1.** wazi ndani; -tupu. **2.** si kweli; si halisi; enye hila. *beat sb.~*, pata ushindi usio na thamani yoyote. *~ware*, kibia; chungu.
**holy** /ˈhəʊli/ *adj.* **1.** -a kuhusiana na Mungu au dini. **2.** -takatifu. **holiness** *n.* utakatifu; usufii; uwalii.
**homage** /ˈhɒmɪdʒ/ *n.* heshima kuu; taa; staha. *pay ~*, toa heshima.
**home** /həʊm/ *n./adv.* makazi; nyumbani; maskani; nyumba ya wazee; familia. *at ~*, nyumbani. *bring sth. ~ to sb.*, elewesha mtu jambo. *feel at ~*, starehe. **~ economics** *n.* sayansi kimu. **~less** *adj.* bila maskani. **~like** *adj.* kama -a nyumbani. **~-made** *adj.* -liotengenezwa nyumbani. **~page** *n.* ukurasa wa mtandao wa mtu, kampuni au jumuia. **~sick** *adj.* enye kukumbuka nyumbani. **~spun** *n./adj.* -liofumwa nyumbani. **~stead** *n.* nyumba ndani ya shamba. **~ward** *adj./adv.* -a kuelekea nyumbani. **~ly** *adj.* -a ka waida; -a kukumbusha nyumbani.
**homicide** /ˈhɒmɪsaɪd/ *n.* kuua mtu; muuaji mtu. **homicidal** *adj.* -a mauaji.
**hominoid** /ˈhɒmɪnɔɪd/ *n.* hominidi: wanyama wa familiasafu ya binadamu na wanaofanana nao (masokwe).
**homoeostasis** *n.* **1.** tabia ya miili ya viumbe hai kusawazisha mahitaji yao yote (joto, mapigo ya moyo, sukari, etc.) katika kiwango kinachohitajika kimaumbile. **2.** tabia ya idadi ya viumbe hai kubakia ileile katika eneo fulani.
**homogeneous** /ˌhɒmə(ʊ)ˈdʒiːnɪəs/ *adj.* -a namna sawa; -a muundo sawa; -liundwa kwa sehemu za namna moja.
**homoiotherm** *n.* mnyama mwenye uwezo wa kusawazisha joto mwilini mwake na kubaki katika kiwango kinachostahili hata kama hali ya mazingira yake imebadilika.
**honest** /ˈɒnɪst/ *adj.* -aminifu; -nyofu; -kweli. **~ly** *adv.* kwa uaminifu. **~y** *n.* uaminifu; ukweli.
**honey** /ˈhʌni/ *n.* asali ya nyuki. **~comb** *n.* sega. *v.t.* toboa tundu. **~moon** *n.* fungate.
**honour** /ˈɒnə(r)/ *n.* **1.** heshima; utukufu. **2.** sifa njema; uaminifu; uadilifu. *on my ~*, naahidi. *debt of ~*, deni ya ahadi, si ya sharti. **3.** mheshimiwa; mtukufu. *Your (His) ~*, mheshimiwa. **4.** mtu (au kitu) aletaye heshima. *an ~ to the school*, fahari ya shule. **5.** nishani; cheo. *the ~s list*, orodha ya vyeo vya heshima vilivyotolewa na mtawala. *an ~s degree*, digirii ya daraja la juu. *v.t.* heshimu; tukuza; adhimisha; pokea na lipa kwa wakati uliopangwa. *~ a promise*, timiza ahadi. **~able** *adj.* a heshima; -tukufu; mheshimiwa.
**hood** /hʊd/ *n.* kifuniko; ukaya; shela; skafu; boneti.
**hoof** /huːf/ *n.* ukwato. *cattle on the ~*, ng'ombe hai.
**hook** /hʊk/ *n.* kingoe; ndoana. *by ~ or by crook*, kwa vyovyote vile. *v.t.* vua; ngoeka. *~ a fish*, vua samaki. **~ed** *adj.* kama ndoana. **~worm** *n.* tegu.
**hoop** /huːp/ *n.* pete kubwa ya mti, chuma au plastiki; gurudumu; duara.
**hoot** /huːt/ *n.* mlio wa bundi; mlio wa honi. *v.t.* zomea; piga honi; lia kama bundi. **~er** *n.* king'ora; honi.
**hop**[1] /hɒp/ *n.* mhopi: mmea mrefu wa kutambaa; maua ya mhopi.
**hop**[2] /hɒp/ *n.* mruko mfupi; mruko wa mguu mmoja; nyunju. *v.i./t.* (**-pp-**) ruka kwa mguu mmoja; chupa; piga nyunju.
**hope** /həʊp/ *n.* tumaini; tarajio; tegemeo. *v.t./i.* tumaini; tarajia; tegemea. **~ful** *adj.* -enye kutumaini; -a kutia matumaini. **~less** *adj.* -a kukata tamaa; -sio na matumaini.
**horde** /hɔːd/ *n.* kundi kubwa.
**horizon** /həˈraɪzn/ *n.* mstari wa upeo wa macho; upeo. **~tal** *adj.* -a kwenda sambamba na upeo wa

macho; -a mlalo.

**hormone** /'hɔːməʊn/ *n.* homoni: kampaundi anuwai za kemikali zinazosafirishwa na tezi ndani na huleta mabadiliko maalumu kwenye kiungo fulani mwilini au kwenye mimea.

**horn** /hɔːn/ *n.* pembe ya mnyama; baragumu; honi. **~bill** *n.* hondohondo; kwembe.

**hornet** /hɔːnɪt/ *n.* nyigu; uvi; zinengo; mburunzi.

**horror** /'hɒrə(r)/ *n.* kitisho; hofu; chukizo. **horrible** *adj.* -a kuogofya; -a kuchukiza. **horrid** *adj.* -a kutisha; -a kuchukiza; -a kuudhi. **horrify** *v.t.* ogofya; shtusha; tisha.

**horse** /hɔːs/ *n.* farasi. **~-play** *n.* mchezo wenye ghasia. **~power** *n.* nguvu-farasi: nguvu sawa na wati 750 kwa sekunde.


horse

**horticulture** /'hɔːtɪ'kʌltʃə/ *n.* kilimo cha bustani.

**hose**[1] /həʊz/ *n.* mpira wa maji. **~pipe** *n.* bomba la mpira. *v.t.* mwagilia maji; safisha kwa kutumia mpira wa maji.


hosepipe

**hose**[2] /həʊz/ *n.* soksi. **hosier** *n.* muuza soksi na nguo za ndani. **hosiery** *n.* bidhaa za muuza nguo za ndani kama chupi na soksi.

**hospitable** /hɒ'spɪtəb(ə)l, 'hɒspɪt-/ *adj.* karimu.

**hospital** /'hɒspɪtl/ *n.* hospitali.

**hospitality** /ˌhɒspɪ'tæləti/ *n.* ukarimu.

**host** /həʊst/ *n.* **1.** mwenyeji; kimelea. **~el** *n.* dakhalia; hosteli; bweni. **~ess** *n.* mwenyeji wa kike. **2.** (la zamani) wingi; jeshi. **3.** hostia: mkate mtakatifu. **~age** *n.* mateka. *give ~s to fortune,* fanya uamuzi wenye madhara baadaye.

**hostile** /'hɒstaɪl/ *adj.* -a adui; -a uhasama. **~ility** *n.* uadui; uhasama; vita.

**hot** /hɒt/ *adj.* -a moto; -enye joto; -kali; -enye hasira; -enye ashiki nyingi. *get into ~ water,* ingia matatani; *~ air,* maneno matupu; ahadi za uwongo. *~ on the trail of sb.,* fuata karibu sana. **~bed** *n.* tuta lenye mbolea au samadi; *(fig.)* mahali penye maovu mengi. **~headed** *adj.* -a harara; -epesi wa hasira. **~house** *n.* kibanda cha kuoteshea maua na matunda.

**hotel** /həʊ'tel/ *n.* hoteli.

**hound** /haʊnd/ *n.* mbwa mkubwa wa kuwindia; mtu mbaya. *v.t.* fukuza; winda kwa mbwa.

**hour** /'aʊə(r)/ *n.* **1.** saa. *at the eleventh ~,* katika dakika za mwisho. *the small ~s,* usiku wa manane. **2.** muda; kipindi; wakati; saa. *what is the ~?* saa ngapi? **3.** vipindi vya kazi. *office ~s,* saa za kazi ofisini. *keep good ~s,* lala mapema. **4.** wakati maalumu. *in the ~ of danger,* wakati wa hatari. *questions of the ~,* mambo ya leo. **~ly** *adj./adv.* -a kila saa; baada ya kila saa.

**house** /haʊs/ *n.* **1.** nyumba; makazi. *keep ~,* kimu familia. **2.** bunge. *~ of parliament,* bunge. *enter the ~,* chaguliwa kuwa mbunge. **3.** hadhira. *a full ~,* ukumbi pomoni. *bring down the ~,* chekesha sana wote waliopo. **4.** ukoo; jamaa; aila. *v.t.* karibisaha; hifadhi; linda. *Where can I ~ my books?* naweza kuweka wapi vitabu vyangu? **~agent** *n.* wakala wa nyumba. **~ breaker** *n.* mwenye kazi ya kubomoa majumba; mwizi wa kuvunja nyumba. **~hold** *n.* kaya; aila. **~holder** *n.* mwenye nyumba. **~keeper** *n.* msimamizi wa nyumba. **~maid** *n.* mtumishi wa kike wa nyumbani. **~wife** *n.* mke.

**hover** /'hɒvə(r)/ *v.i.* (kwa ndege) simama mahali pamoja angani; ngojea; zengea. **~craft** *n.* hovakrafti: chombo kiendacho majini na nchi kavu chenye mashine ya ndege.


hovercraft

**how** /haʊ/ *adv.* jee? jinsi gani? vipi? **~ever** *adv.* kwa hali yoyote. *He will*

*buy it ~ dear it is,* atanunua hata iwe ghali kiasi gani. *conj.* hata hivyo.

**howl** /haʊl/ *n.* mlio; mvumo. *~ of laughter,* kwakwa. *v.i.* lia; bweka. *v.t.* lia kwa kelele; piga kwakwa; vuma; zomea. *~ a speaker down,* zomea msemaji. **~er** *n.* kosa la kijinga; kichekesho.

**hub** /hʌb/ *n.* kitovu cha gurudumu; habu; kituo cha shughuli.

**hug** /hʌg/ *n.* kumbatio. *v.t* (**-gg-**) kumbatia; shikilia; ng'ang'ania; (kwa meli) ambaa pwani.

**huge** /hju:dʒ/ *adj.* -kubwa mno.

**hull** /hʌl/ *n.* **1.** fremu ya merikebu. **2.** ganda; kumvi; kumbi. *v.t.* menya; papatua; koboa.

**hullo** *int.* halo.

**hum** /hʌm/ *n.* mvumo. *v.t./i.* (**-mm-**) vuma kama nyuki; imba hali midomo imefumba.

**human** /'hju:mən/ *adj.* -a binadamu; -a watu; -enye utu. *a ~ being,* mtu. **~ rights**, haki za binadamu. **~e** *adj.* -ema; -enye huruma. **~ism** *n.* elimu ya ubinadamu isiyohusisha uungu. **humanitarian** *adj./n.* -a huruma; -a hisani; mhisani; mfadhili. **~ity** *n.* binadamu; utu; huruma; wema. *the humanities,* sayansi za jamii.

**humble** /'hʌmbl/ *adj.* nyenyekevu; -nyonge; maskini; duni; -siotaka makuu. *v.t.* dunisha; dhalilisha.

**humerus** /'hju:m(ə)rəs/ *n.* humerusi: mfupa mkubwa utokao begani hadi kwenye kiko cha mkono.

**humid** /'hju:mɪd/ *adj.* nyevunyevu. **~ity** *n.* unyevu: kiasi cha mvuke hewani.

**humiliate** /hju:'mɪlieɪt/ *v.t.* fedhehesha; aibisha; dhalilisha; tweza.

**humility** /hju:'mɪləti/ *n.* unyenyekevu; uvumilivu; haya.

**humour** /'hju:mə(r)/ *n.* kichekesho; uchekeshaji; ucheshi; hali ya mtu. *sense of ~,* ucheshi. *He is in a good ~,* yu mchangamfu. *He is not in the ~ for work,* hana hamu ya kufanya kazi. *aqueous ~,* ute maji: ute mwepesi wa jicho unaojaa kati ya konea na ute mzito, ndani yake kuna lenzi na irisi. *vitreous ~,* ute ng'arifu: jeli inayojaza sehemu ya nyuma ya jicho la vetebra. *v.t.* bembeleza; changamsha.

**humorist** *n.* mcheshi; mchekeshaji.

**humorous** /'hju:mərəs/ *adj.* -epesi kuona, kufanya na kufahamu mambo ya mzaha; -a kuchekesha.

**hump** /hʌmp/ *n.* nundu; kigongo; kibyongo. **~back** *n.* -enye kibyongo.

**humus** /'hju:məs/ *n.* mboji: mbolea yenye rangi nyeusi inayotokana na mchanganuo wa mata za mimea au wanyama.

**hunch** /hʌntʃ/ *n.* kigongo; kibyongo; nundu; kipande kinene. *have a ~ that,* hisi kwamba. *v.t.* pinda mgongo. **~back** *n.* kibyongo.

**hundred** /'hʌndrəd/ *n./adj.* mia. **~weight** *n.* ratili mia na kumi na mbili, yaani wastani wa kilo 50.8.

**hunger** /'hʌŋgə(r)/ *n.* njaa; tamaa; hamu; shauku. *go on a ~ strike,* goma kula. *~ march,* maandamano ya wasio na kazi. *v.i.* tamani sana. **hungry** *adj.* -enye njaa. **hungrily** *adv.* kinjaa.

**hunt** /hʌnt/ *n.* msako; uwindaji. *v.t./i* winda; tafuta; saka; fukuza.

**hurdle** /'hɜ:dl/ *n.* kiunzi; kikwazo. *~ race,* mbio za kuruka viunzi.

**hurl** /hɜ:l/ *n.* uvurumishaji. *v.t.* tupa kwa nguvu; vurumisha; vukutiza.

**hurrah**, **hurray** /hə'rɑ/ *int.* hure!

**hurricane** /'hʌrɪk(ə)n, -keɪn/ *n.* tufani; kimbunga. *~ lamp,* kandili.

**hurry** /'hʌri/ *n.* haraka; hima. *v.t./i.* himiza; harakisha; fanya haraka. **hurried** *adj.* -liofanywa kwa haraka; -enye haraka.

**hurt** /hɜ:t/ *n.* maumivu; madhara. *v.t./i.* dhuru; umiza; uma; sononesha.

**husband** /'hʌzbənd/ *n.* mume. *v.t.* tumia kwa uangalifu; hifadhi. **~man** *n.* (la zamani) mkulima. **~ry** *n.* (la zamani) ukulima. *animal ~,* ufugaji.

**hush** /hʌʃ/ *v.t./i.* nyamazisha; nyamaa; nyamaza. *~ sth. up,* sitiri; ficha. **husk** /hʌsk/ *n.* ganda; kapi; kumvi; kumbi. **~y** *adj.* kavu kama kumbi; (kwa sauti) -a gonda. **~ily** *adv.* kwa ukavu.

**hustle** /'hʌsl/ *n.* kikumbo; msukumo. *v.t.* songa; sukuma; sukumiza.
**hut** /hʌt/ *n.* kibanda. **~ment** *n.* ago; dago; kambi ya vibanda.
**hybrid** /'hʌɪbrɪd/ *n./adj.* mahuluti; chotara; mvyauso: kiumbe kinachopatikana kwa muungano wa jeni za jamii mbalimbali.
**hydrate** /'hʌdreɪt/ *n.* hidrati: msombo wenye maji yaliyo-unganika kikemikali na dutu.
**hydraulic** /hʌɪ'drɔ:lik, hʌɪ'drɒlik/ *adj.* hidroliki: -enye kuhusiana na kanieneo katika kimiminiko; -a maji; -enye kuendeshwa kwa maji.
**hydro-** /'haɪdr(əʊ)/ *prefix* haidro: a maji; -enye kuhusiana na maji.
**hydrocarbon** /ˌhaɪdrəˌkabən/ *n.* hidrokaboni: kampaundi mahuluku yenye kaboni na hidrojeni tu.
**hydrochloric acid** *n.* asidi hidrokloriki: mmumunyo wa gesi isiyokuwa na rangi yenye harufu inayounguza.
**hydroelectric** /ˌhaɪdrəʊɪ'lektrɪk/ *adj.* -a umeme wa nguvu za maji.
**hydrogen** /'hʌɪdrədʒ(ə)n/ *n.* hidrojeni: gesi inayowaka isiyo harufu wala rangi, huungana na oksijeni kikemikali kufanya maji. **~ chloride** kloridi hidrojeni: gesi yenye harufu kali inayoyeyuka katika maji kufanya asidi hidrokloriki. **~ sulphide** hidrojeni sulfaidi: gesi isiyo na rangi inukayo kama mayai viza.
**hydrosphere** *n.* hidrosfia: tabaka yote ya maji iliyoko juu ya ardhi pamoja na mvuke ulioko angani.
**hydroxide** *n.* hidroksidi: besi au alkali yenye ioni.
**hyena** /haɪ'i:nə/ *n.* fisi.
**hygiene** /'haɪdʒi:n/ *n.* elimusiha; usafi. **hygienic** *adj.* -a afya; -a kuleta afya.
**hygrometer** /hʌɪ'grɒmɪtə/ *n.* kipima-unyevu: chombo kinachopima unyevu wiani wa angahewa.
**hymn** /hɪm/ *n.* wimbo wa kidini.
**hyper-** /'haɪpə(r)/ *prefix* hipa, -a zaidi; -a kupita kiasi.
**hyperbola** /hʌɪ'pə:bələ/ *n.* hipabola: mchirizo unaofanywa na bapa wakati linapokata uso wa pia.
**hyperbole** /hʌɪ'pə:bəli/ *n.* mubalagha: kutia chumvi sana katika kueleza jambo.
**hyperlink** /'haɪpəlɪŋk/ *n.* kiungo hipa; kiungo.
**hypertext** /'haɪpətekst/ *n.* waraka wenye habari au data unaowakilishwa na kiungo-hipa; kiungwa.
**hypha** /'hʌɪfə/ *n.* kikungunyanzi: mojawapo ya vijiuzi katika mwili wa kuvu vinavyosambaa ndani au juu ya vitu vilivyokufa, ambavyo vinavyofyonza chakula katika vitu vinavyooza.
**hyphen** /'hʌɪf(ə)n/ *n.* alama hii (-) katika maandishi.
**hypnotism** /'hɪpnətizəm/ *n.* uzugaji; ulazaji; upumbazaji.
**hypocrisy** /hɪ'pɒkrəsi/ *n.* unafiki; uzandiki. **hypocrite** *n.* mnafiki; mzandiki.
**hypodermic** /ˌhaɪpə'dɜ:mik/ *adj.* -a chini ya ngozi. **~ syringe** sindano ya kuingiza chini ya ngozi.
**hypotenuse** /hʌɪ'pɒtənju:z, -s/ *n.* kiegama: upande mrefu wa pembetatu.
**hypothermia** /ˌhʌɪpə(ʊ)'θə:mɪə/ *n.* hipothemia: hali ya kuanguka halijoto ya mwili na kuwa chini ya kiwango chake cha kawaida.
**hypothesis** /hʌɪ'pɒθɪsɪs/ *n.* nadharia tete.
**hypothetic(al)** /ˌhʌɪpə'θɛtɪk(ə)l/ *adj.* -a nadharia tete; -a kubuni; -sio na uhakika bado.
**hysteria** /hɪ'stɪəriə/ *n.* hali ya kupagawa. **hysterical** *adj.* -enye kupagawa.

# Ii

**ice** /aɪs/ *n.* barafu. *break the ~,* anza kitu kigumu; vunja ukimya. *v.t.* gandisha kwa baridi; funika kwa barafu; ikiza keki sukari. **~berg** *n.* kisiwa barafu. **~-bound** *adj.* liokingwa na barafu. **~cream** *n.* malai; koni. **~field** *n.* uwanda barafu. **icicle** *n.* mchirizi wa barafu. **icy** *adj.* baridi sana; *(fig.)* si changamfu; -liofunikwa kwa barafu.


iceberg

**idea** /aɪ'dɪə/ *n.* wazo; fikra; shauri; dhana; nia; lengo; mpango; azimio; imani; hisia. **~l** *adj.* **1.** -lio bora; kamilifu; -a njozi. *n.* maadili; wazo bora; wazo kamilifu; mfano bora. **~lism** *n.* kanuni za maisha; ulimbwende; udhanifu. **~list** *n.* mdhanifu. **~lize** *v.t.* fanya kamilifu; dhania kuwa kamilifu. **~ly** *adv.* kikamilifu.

**identical** /aɪ'dentikl/ *adj.* sawa-sawa; pacha; -a kufanana *~ twins,* mapacha. **~ly** *adv.* sawasawa.

**identify** /aɪ'dentɪfaɪ/ *v.t.* tambua; tambulisha; jihusisha; fananisha; shirikisha; funganisha.

**identification** /aɪ'dentɪfikeɪʃn/ *n.* kuthibitisha (kuthibitishwa) nafsi. **identity** *n.* sura; kufanana; kuwa sawa kabisa.

**ideology** *n.* /ˌʌɪdɪ'ɒlədʒi, ɪd- / itikadi. **ideological** *adj.* -a itikadi.

**idiom** /'ɪdiəm/ *n.* lugha; lahaja; nahau; usemi. **~atic** *adj.* -a nahau; -enye nahau.

**idiot** /'ɪdiət/ *n.* mpumbavu; mjinga; zuzu; juha. **idiocy** *n.* upumbavu; uzuzu. **~ic** *adj.* -pumbavu; -a upuuzi. **~ically** *adv.* kipuuzi; kijinga.

**idle** /aɪdl/ *adj.* -siofaa; -a bure; -sio na kazi; -vivu; legevu; -zembe. *v.i./t.* -wa bila kazi; -wa -vivu. **~r** *n.* mvivu. **idly** *adv.* kivivu. **~ness** *n.* uvivu.

**if** /ɪf/ *conj.* kama; ikiwa; iwapo. *even ~,* hata kama. *as ~,* kama kwamba; kama vile. *~ only,* laiti; endapo tu.

**igneous** /'ɪgnɪəs/. -a moto -liofanyika kwa kubaridika mawe ya volkano. *~ rock,* jabali magima: jabali lililofanyika kwa kubaridika magima ya volkano. **ignite** *v.t./i.* washa; waka; tia moto. **ignition** *n.* mwako; uwashaji; uwakaji.

**ignorant** /'ɪgnərənt/ *adj.* -jinga; -kosefu wa maarifa; -siojua. **ignorance** *n.* ujinga. **ignorant** *adj.* -jinga; -siojua; -a kijinga.

**il-** *prefix* kinyume cha; -sio.

**ill** /ɪl/ *n.* **1.** uovu; ubaya; madhara. *do ~,* fanya uovu. **2.** mkosi; kisirani; matatizo; hasara. *adj.* **1.** -gonjwa. *fall ~,* -wa mgonjwa. *be taken ~,* ugua. **2.** -baya; -ovu; -a madhara. *~ health,* afya mbaya. *adv.* vibaya; ovyoovyo; kwa kutoridhisha. *~ at ease,* -jihisi vibaya. *I can ~ afford it,* naweza kulipa kwa shida. **~-bred** *adj.* -sio na adabu; -liolelewa vibaya. **~-fated** *adj.* enye kisirani; -enye mkosi. **~gotten** *adj.* -liopatikana kwa njia mbaya au haramu. **~-natured** *adj.* kali, -korofi; -enye hasira. **~ness** *n.* ugonjwa. **~-treat** *v.t.* tesa; dhulumu. **~-use** *v.t.* tendea mabaya; tumia vibaya.

**illicit** /ɪ'lisit/ *adj.* haramu; marufuku; -liokatazwa.

**illiterate** /ɪ'lɪt(ə)rət/ *n./adj.* mjinga; (mtu) asiyejua kusoma wala kuandika. **illiteracy** *n.* kutojua kusoma wala kuandika.

**illuminate** /ɪ'l(j)uːmɪneɪt/ *v.t.* **1.** tia nuru; angaza; mulika; fafanua. **2.** pamba kwa taa; pamba kwa rangi ya dhahabu. **illumination** *n.* kupamba mji kwa taa; taa za mapambo. **illumine** *v.t.* tia nuru.

**illusion** /ɪ'l(j)uːʒ(ə)n *n.* njozi; uongo; mauzauza; udanganyifu; mazinga-ombwe. **illusive**, **illusory** *adj.* -a njozi; -a uongo.

**illustrate** /'ɪləstrəɪt/ *v.t.* eleza kwa mifano, picha, au vielezo; chora vielezo katika kitabu au jarida. **illustration** *n.* kielezi; kueleza kwa mifano. **illustrator** *n.* mchora picha

za vitabu.

**im-** *prefix* kinyume cha; siyo; hapana; bila.

**image** /ˈɪmɪdʒ/ *n.* sanamu; picha; kifani; mfano; nakala; sura. *be the very ~ of sb.*, fanana kabisa na fulani. **~ry** *n.* sanamu; picha; michoro; matumizi ya tamathali za usemi katika maelezo.

**imagine** /ɪˈmædʒɪn/ *v.t.* waza; dhania; fikiria; dhani; kisia; amini. **imaginable** *adj.* -a kuweza kufikirika; -a kuweza kubunika. **imaginary** *adj.* -a mawazo tu; -a kufikirika; -a kubuni. **imagination** *n.* ubunifu; wazo; fikra; dhana. **imaginative** *adj.* bunifu; -enye mawazo mengi.

**imago** /ɪˈmeɪgəʊ/ *n.* mdudu kamili: hatua ya mwisho ya kukua kwa mdudu na kukamilika, baada ya kupitia hatua zote za ukuaji kuanzia yai.

**imbecile** /ˈɪmbəsiːl/ *n.* punguani; bozi; mzembe; mpumbavu. *adj.* punguani; -pumbavu.

**imbecility** /ˌɪmbəˈsɪləti/ *n.* upunguani; upuuzi.

**imitate** /ˈɪmɪteɪt/ *v.i.* iga; fuatisha; nakili; fanana; wa kama; fananisha na. **imitation** *n.* wigo; mfano; nakala; uigaji; mfano; bandia. *imitation gold*, dhahabu bandia. **imitative** *adj.* -a kuiga; -a kufuatisha.

**immediate** /ɪˈmiːdiət/ *adj.* -a jirani; -a karibu sana; -a mara moja; -a sasa hivi. *my ~ neighbours*, jirani zangu wa karibu. *an ~ answer*, majibu ya mara moja. **~ly** *adv.* sasa hivi; mara moja; papo hapo.

**immense** /ɪˈmens/ *adj.* -kubwa sana. **~ly** *adv.* mno; kwa kiasi kikubwa; sana; hasa; kwa wingi. **immensity** *n.* ukubwa wa kupita kiasi.

**immerse** /ɪˈmɜːs/ *v.t.* chovya; tosa; zamisha; tumbukiza; shughulisha. *be ~d in*, shughulika sana na; -wa katika shida sana ya. **immersion** *n.* mchovyo; mzamo; utumbukiaji; mshughuliko.

**immortal** /ɪˈmɔːtl/ *adj.* -a kuishi milele; -siosahauliwa; -siokufa. *the ~s*, miungu ya Kiyunani na ya Kirumi. **~ity** *n.* maisha ya milele; kutokufa. **~ize** *v.t.* -pa maisha ya milele; -pa sifa ya daima.

**immovable** /ɪˈmuːvəbl/ *adj.* siohamishika; imara; thabiti; madhubuti. **~ property**, mali isiyohamishika (nyumba na shamba).

**immune** /ɪˈmjuːn/ *adj.* huru; -sioweza kupatwa na ugonjwa. **~ response**, kinga: uwezo wa kiumbe hai wa kutoa zindiko mwilini mwake. **immunity** *n.* kinga. **diplomatic immunity**, kinga ya kidiplomasia. **immunize** *v.t.* -pa kinga maradhi; chanja. **immunization** *n.* mchanjo.

**impact** /ˈɪmpækt/ *n.* mgongano; athari; matokeo; nguvu zipatikanazo wakati vitu viwili vigonganapo; nguvu zipatikanazo kutokana na athari ya mawazo fulani.

**impair** /ɪmˈpeə(r)/ *v.t.* haribu; dhoofisha.

**impartial** /ɪmˈpɑːʃl/ *adj.* -adilifu; -siopendelea; -enye haki. **~ity** *n.* uadilifu. **~ly** *adv.* kwa uadilifu.

**impassable** /ɪmˈpɑːsəbl/ *adj.* siopitika.

**impassioned** /ɪmˈpæʃnd/ *adj.* -enye hamaki; -enye hamasa.

**impassive** /ɪmˈpæsɪv/ *adj.* baridi; -tulivu; -sioonyesha hisia.

**impeccable** /ɪmˈpekəbl/ *adj.* maasumu; -siokosea; bila kosa.

**impedance** /ɪmˈpiːdns/ *n.* ukinzanijumla: jumla ya ukinzani katika saketi ya umeme unaopinga mwendo wa umeme.

**impede** /ɪmˈpiːd/ *v.t.* zuia; pinga; kwamisha. **impediment** *n.* kizuizi; kikwazo; kigugumizi.

**impending** /ɪmˈpendɪŋ/ *adj.* -a karibu sana; -a kuelekea kutokea upesi. *the ~ storm*, dhoruba ya karibu sana.

**imperative** /ɪmˈperətɪv/ *adj.* -a lazima; -a kuangaliwa mara moja; -a kusikiwa; a kutiiwa; muhimu; -a kuamuru; a sharti; -liotolewa kwa uthabiti; (sarufi) -a amri.

**imperial** /ɪmˈpɪəriəl/ *adj.* -a kifalme;

-a kibeberu; bora; -kubwa. **~ism** *n.* ubeberu: utawala wa mabavu wa makusudi au wa hadaa wa nchi moja kwa nyingine kwa kutumia biashara au diplomasia.

**imperil** /ɪm'perəl/ *v.t.* (**-ll-**) hatarisha; ponza.

**impermeable** /ɪm'pə:mɪəb(ə)l/ *adj.* -siopenywa na maji.

**impersonal** /ɪm'pɜ:sənl/ *adj.* -sioathiriwa na hisia; vitenzi visivyohusishwa na vitu hai; -siohusishwa na mtu maalumu. **impersonate** *v.t.* iga; geuka; jifanya; jisingizia.

**imperturbable** /ˌɪmpə'tə:bəb(ə)l/ *adj.* -siosisimka; -siohangaika; -tulivu.

**impervious** /ɪm'pə:vɪəs/ *adj* -siopenyeka; -siosikia; -siokubali ushauri.

**impetus** /'ɪmpɪtəs/ *n.* nguvu; kichocheo; msukumo.

**implant** /ɪm'pla:nt/ *v.t.* tia fikra moyoni; kaza ndani imara; pandikiza.

**implement** /'ɪmplɪm(ə)nt/ *n.* kifaa; chombo cha kazi. *v.t.* tekeleza. **~ation** *n.* utekelezaji.

**implicate** /'ɪmplɪkeɪt/ *v.t.* tia hatiani; ingiza lawamani; ingiza hatarini. **implication** *n.* kutia hatiani; maana; kidokezi.

**imply** /ɪm'plaɪ/ *v.t.* dokeza; husika na; wa na maana; onyesha bila kutaja. *Silence implies consent,* kunyamaza ni sawa na kukubali.

**import** /ɪm'pɔ:t/ *n.* maduhuli: bidhaa ziingizwazo nchini; maana; uingizaji. *v.t.* leta bidhaa nchini kutoka nchi nyingine; maanisha; onyesha. **~er** *n.* mletaji bidhaa nchini.

**important** /ɪm'pɔ:tnt/ *adj.* -a maana; muhimu; -kuu; -enye amri. **~ly** *adv.* **importance** *n.* umuhimu; ukuu.

**importunity** *n.* usumbufu wa kuombaomba.

**impose** /ɪm'pəʊz/ *v.t./i.* **1.** toza; amuru; lazimisha; lipisha. **2.** ~ *upon,* tumilia. **imposing** *adj.* -a kuvutia; -a fahari. **imposition** *n.* utozaji; ulipishaji; amri; utumiliaji.

**impostor** *n.* ayari; mpunjaji; laghai; jambazi. **imposture** *n.* ulaghai; utapeli.

**impossible** /ɪm'pɒsəbl/ *adj.* -siowezekana; -siofanyika.

**impotent** /'ɪmpət(ə)nt/ *adj.* bila nguvu; -siofaa neno; dhaifu. **impotence** *n.* udhaifu wa nguvu za kiume.

**impound** /ɪm'paʊnd/ *v.t.* piga mali tanji; zuia katika kituo cha polisi.

**impoverish** /ɪm'pɒvərɪʃ/ *v.t.* fanya kuwa maskini; fukarisha; punguza nguvu; dhoofisha; chakaza.

**impracticable** /ɪm'præktikəbl/ *adj.* -siotekelezeka; siopitika; muhali.

**impregnable** /ɪm'pregnəbl/ *adj.* -sioshindika; -sioingilika; -a kuweza kustahamili mashambulio yote.

**impregnate** /'ɪmprɛgneɪt/ *v.t.* tia mimba; jaza; kifu.

**impress** /ɪm'pres/ *v.t.* **1.** gandmiza; piga chapa; piga muhuri. **2.** shawishi; vutia; athiri. *I was not much ~ed,* sikuvutiwa sana. **~ion** *n.* **1.** alama; chapa. **2.** fikra; dhana; uono; picha. **~ionable** *adj.* -epesi kuathiriwa; -epesi kushawishika. **~ive** *adj.* -enye kuvutia; -enye kuathiri; enye kuchochea hisia.

**imprint** /ɪm'prɪnt/ *n.* alama; wazo moyoni. *v.t.* chapa; piga muhuri; tia moyoni. *ideas ~ed on the mind,* fikra zilizotiwa moyoni.

**imprison** /ɪm'prɪzn/ *v.t.* funga; tia jela. **~ment** *n.* kifungo.

**improve** /ɪm'pru:v/ *v.t./i.* endeleza; -wa zuri zaidi; sitawisha; tengeneza vizuri zaidi. **~ment** *n.* maendeleo; ukuaji.

**improvise** *v.t./i.* buni; tunga papo hapo.

**impudent** /'ɪmpjʊd(ə)nt/ *adj.* fedhuli; -juvi; safihi. **impudence** *n.* ufedhuli; ujeuri; usafihi.

**impugn** /ɪm'pju:n/ *v.t.* bisha; kana; tilia mashaka.

**impulse** /'ɪmpʌls/ *n.* msukumo; raghaba; hamu; mhemko wa ghafla. **impulsive** *adj.* -a msukumo; -a kuamua ghafla.

**impurity** /ɪm'pjuərəti/ *n.* uchafu; takataka; najisi.

**in-** /ɪn/ *prefix* si; pasipo; bila.
**inadvertent** *adj.* si -angalifu; -a kughafilika. **~ly** *adv.* si -a makusudi. **inadvertence** *n.* kupitikiwa.
**inane** /ɪ'neɪn/ *adj.* -sio na maana, -puuzi; pumbavu. **~ly** *adv.* kipuuzi. **inanity** *n.* upuuzi.
**inanimate** /ɪn'ænɪmət/ *adj.* -fu; si -enye uhai; -liopooza; chapwa. *~ conversation,* mazungumzo chapwa.
**inapt** *adj.* si stadi; -siohusiana na jambo linalozungumzwa.
**inaugurate** /ɪ'nɔ:gjəreɪt/ *v.t.* fungua; zindua; ingia rasmi; anzisha; simika; tawaza; tambu lisha rasmi. **inaugural** *adj.* -a kuzindua; -a kuanzisha; -a kufu-ngua. **inauguration** *n.* ufunguzi; uzinduzi.
**inborn** /ɪn'bɔ:n/ *adj.* -a asili; -a kuzaliwa nao; -a silika; -a maumbile.
**inbred** /'ɪn'bred/ *adj.* -a asili; -a kuzaliwa nao; -liozaliwa na wazazi wa nasaba moja. **inbreeding** *n.* uzao baina ya wazazi wa nasaba moja.
**incandescent** /ɪnkæn'desnt/ *adj.* -enye kung'aa kwa joto jingi.
**incapacity** /ˌɪnkə'pæsɪteɪt/ *n.* kutoweza; ukosefu wa uwezo.
**incendiary** /ɪn'sendiəri/ *n./adj.* uchomaji mali kwa makusudi; mchochezi; -a kuteketeza; cho chezi.
**incense**[1] /'ɪnsens/ *v.t.* kasirisha; ghadhibisha.
**incense**[2] /'ɪnsens/ *n.* ubani; uvumba; udi; buhuri.
**incentive** /ɪn'sentɪv/ *n.* kichocheo; kishawishi; motisha; kifuta jasho; marupurupu.
**incessant** /ɪn'sesnt/ *adj.* bila kukoma; -a kufululiza; -a daima.
**incest** /'ɪnsest/ *n.* zinaa baina ya maharimu wasioruhusiwa kuoana kwa mujibu wa dini au utamaduni wao. **~uous** *adj.* -a uzinzi wa maharimu.
**inch** /ɪntʃ/ *n.* inchi; kiasi kidogo; chembe. *by ~es,* kidogo kidogo. *every ~ a soldier,* askari mzuri kabisa.
**incidence** /'ɪnsɪdəns/ *n.* jinsi jambo linavyoathiri mambo; tukio. *the ~ of a disease,* jinsi ugonjwa unavyoathiri watu. *the ~ of a tax,* jinsi kodi inavyoathiri walipaji. **incident** *n.* jambo; neno; tukio; kadhia. **incidental** *adj.* -dogo-dogo; -a dharura; -a ziada; -inayoweza kutokea; inayoambatana na.
**incinerate** /ɪn'sɪnəreɪt/ *v.t.* choma; teketeza. **incinerator** *n.* tanuri la kuchomea taka.
**incision** /ɪn'sɪʒn/ *n.* mkato; chanjo; mtai; chale. **incisive** *adj.* -kali; -enye kukata; -erevu. **incisor** *n.* jino la mbele; chonge.
**incite** /ɪn'saɪt/ *v.t.* chochea; shawishi; vuta. **~ment** *n.* kichocheo; kishawishi.
**inclination** /ˌɪnklɪ'neɪʃn/ *n.* mwelekeo; mapenzi; tamaa; matakwa; mbetuko; mwinamo. **incline** *v.i./t.* elekea; elekeza; inamisha; inika; betuka. *n.* mteremko; mwinamo.
**include** /ɪn'klu:d/ *v.t.* tia, weka ndani; -wa pamoja na. *price is 2,000/-, postage ~d,* bei ni elfu mbili pamoja na gharama ya posta. **inclusion** *n.* uwekaji ndani. **inclusive** *adj.* -ote pamoja; pamoja na.
**income** /'ɪnkʌm/ *n.* mapato; chumo; pato; kipato. *national ~,* pato la taifa. *~ tax,* kodi ya mapato.
**incongruity** /ˌɪnkɒn'gru:əti/ *n.* hitilafu; tofauti. **incongruous** *adj.* -siopatana; -siofaa mahali.
**inconvenient** /ˌɪnkən'vi:əniənt/ *adj.* -sumbufu; -siofaa; -sio na raha.
**incorporate** /ɪn'kɔ:pəreɪt/ *v.t.* unga; unganisha; shirikisha; ungana na; -wa shirika. *adj.* -liounganishwa; -lioshirikishwa. **incorporation** *n.* ushirikiano.
**increase** /ɪn'kri:s/ *n.* nyongeza; ziada; ongezeko. *v.t./i.* ongeza; zidisha; kithiri.
**increment** /'ɪŋkrəmənt/ *n.* nyo-ngeza; ongezeko.
**incriminate** /ɪn'krɪmɪneɪt/ *v.t* ponza; tia hatiani; chongea.
**incubate** /'ɪŋkjubeɪt/ *v.t.* atamiza

mayai kwa kutumia mashine; atamia mayai. **incubator** *n.* kiatamizi; kiangulio; kitotozi.

**inculcate** /ˈɪnkʌlkeɪt/ *v.t.* fundisha kwa marudio, hasa juu ya maadili ya jamii.

**incumbent** /ɪnˈkʌmbənt/ *n.* padri wa mji; kasisi; mtu ashikiliaye cheo. *adj.* -a kubidi. *It is ~ upon me,* inanipasa; inanibidi.

**incur** /ɪnˈkɜ:(r)/ *v.t.* (**-rr-**) pata; patwa na.

**indebted** /ɪnˈdetɪd/ *adj.* -enye kuwiwa; -enye deni; -a kupaswa kushukuru.

**indeed** /ɪnˈdi:d/ *adv.* kweli; hasa; ndio; naam.

**indefatigable** /ˌɪndɪˈfatɪgəb(ə)l/ *adj.* -siochoka; -siochoshwa.

**indefinite** /ɪnˈdefɪnət/ *adj.* -sio dhahiri; -sio na mwisho; sio mipaka. **~ article**, *(grammar)* neno **a** au **an**.

**indelible** /ɪnˈdɛlɪb(ə)l/ *adj.* -siofutika; siosahaulika.

**indemnify** /ɪnˈdɛmnifʌɪ/ *v.t.* lipa fidia; linda; kinga. **indemnity** *n.* fidia; bima.

**indent** /ɪnˈdɛnt/ *n.* hati ya kuagiza bidhaa. *v.t.* tia pengo; bonyeza; jongeza mstari ndani; agiza bidhaa kwa agizo maalumu.

**independent** /ˌɪndɪˈpendənt/ *adj.* -enye kujitawala; huru; enye kujitegemea. **independence** *n.* uhuru; upekee; kujitegemea.

**index** /ˈɪndɛks/ *n.* (**~es**, **indices**) kielezo; alama; ishara; faharasa; nambapeo. *v.t.* orodhesha; fahirisisha. **~ fossil**, kisukuku gezaji; kisukuku cha mnyama aliyeishi katika kipindi maalumu cha kijiolojia na hivyo kinaweza kutumiwa kupimia umri wa miamba kilimo.

**indicate** /ˈɪndɪkeɪt/ *v.t.* elekeza; onyesha; dokeza; ashiria.

**indication** /ˌɪndɪˈkeɪʃn/ *n.* alama; dalili; ishara. **indicative** *adj.* -a kuarifu; -wa alama ya. **indicator** *n.* alama; indiketa; ishara; dalili.

**indifferent** /ɪnˈdɪfrəns/ *adj* siojali; -a kawaida. **indifference** *n.* kutojali; kutojihusisha; kutojiingiza. *It's a matter of complete ~ to me,* ni mamoja kwangu kwani hayanihusu.

**indigenous** /ɪnˈdɪdʒənəs/ *adj.* -zalia, -a asili; enyeji.

**indigestion** /ˌɪndɪˈdʒestʃən/ *n.* vimbizi; kuvimbiwa.

**indignant** /ɪnˈdɪgnənt/ *adj.* -enye uchungu; -a kuudhika. **~ly** *adv.* kwa uchungu. **indignation** *n.* uchungu; hasira. **indignity** *n.* ufedhuli.

**indigo** /ˈɪndɪgəʊ/ *n.* nili.

**indispensable** /ˌɪndɪˈspensəbl/ *adj.* -a lazima.

**indisposed** /ˌɪndɪˈspəʊzd/ *adj.* gonjwa; -a kutopenda; a kutotaka. **indisposition** *n.* ugonjwa mdogo.

**individual** /ˌɪndɪˈvɪdʒuəl/ *n.* mtu binafsi; mtu; binadamu. *adj.* -a mmoja mmoja, -a kitu kimoja. **~ly** *adv.* kila -moja peke yake; -moja -moja. **~ity** *n.* nafsi; dhati.

**indoctrinate** /ɪnˈdɒktrɪneɪt/ *v.t.* funza; fundisha; tia kasumba.

**indoor** /ˈɪndɔ:(r)/ *adj.* -a ndani ya nyumba; -a kufanya ndani ya nyumba. **~s** *adv.* ndani ya nyumba.

**induce** /ɪnˈdju:s/ *v.t.* **1.** vuta; shawishi. **2.** anzisha; sababisha; dukiza; toa umeme. **~ment** *n.* mvuto; kishawishi; kivutio; motisha.

**induction** /ɪnˈdʌkʃn/ *n.* udukizaji: tendo la kitu kupatwa na tabia ya kitu kingine kilichopo karibu yake bila ya kugusana. **electric ~**, udukizaji umeme. **electrostatic ~**, udukizaji umemetuamo. **electromagnetic ~**, udukizaji sumakuumeme. **magnetic ~**, udukizaji sumaku. **mutual ~**, udukizanaji. **self ~**, kujidukiza.

**indulge** /ɪnˈdʌldʒ/ *v.t.* pendelea; endekeza; deka; jiingiza. **~nce** *n.* starehe; kujiachia; kudekeza; kuendekeza; kujiingiza; kipendacho moyo. **~nt** *adj.* -pole; -ema mno; -taratibu.

**industry** /ˈɪndəstri/ *n.* utendaji; bidii; uchapaji kazi; kiwanda; tasnia. **industrial** *adj.* -a kiwanda.

**industrial revolution**, mapinduzi ya viwanda. **industrious** *adj.* -enye bidii ya kazi; -chapakazi.

**inert** /ɪ'nɜ:t/ *adj.* -fu; kama kifu; kama kufa; -tepetevu. **~ gas**, gesi ajizi: kundi la elementi sita za heli, neoni, agoni, kriptoni, zenoni, na radoni zilizomo kwenye kundi sifuri la jedwali mrudio. **~ia** *n.* inesha: tabia ya gimba kutokubadilika mwendo kwa shinikizo la kani.

**inevitable** /ɪn'evɪtəbl/ *adj.* -sioepukika; -siozuilika.

**inexperience** /,ɪnɪk'spɪəriəns/ *n.* ukosefu wa uzoefu; ukosefu wa ujuzi.

**inexpressible** /,ɪnɪk'spresəbl/ *adj.* -sioelezeka.

**infallible** /ɪn'fæləbl/ *adj.* -sioweza kukosa; -nye hakika; - siokosea; -a uhakika.

**infant** /'ɪnfənt/ *n.* mtoto mchanga; mtoto; -changa; -a kitoto. **infancy** *n.* utoto; uchanga; ukembe; mwanzo. *Aviation is no longer in its infancy,* urukaji hewani umepevuka. **~icide** *n.* uuaji mtoto mchanga mara tu anapozaliwa. **~ile** *adj.* -a kitoto; -a mwanzoni.

**infantry** /'ɪnfəntri/ *n.* askari wa miguu.

**infect** /ɪn'fekt/ *v.t.* ambukiza; eneza; chafua. **~ion** *n.* uambukizaji; ugonjwa wa kuambukiza. **~ious** *adj.* -a kuambukiza; -a kuenea; enye kushawishi.

**inferior** /ɪn'fɪəriə(r)/ *n.* mtu duni. *adj.* -a chini; duni; dhalili. **~ity** /ɪn,fɪəri'ɒrəti/ *n.* udhalili.

**infernal** /ɪn'fɜ:nl/ *adj.* -a jehanamu; -a shetani; -baya sana; -liolaaniwa. **inferno** *n.* jahanamu; motoni; tukio la kutisha.

**infest** /ɪn'fest/ *v.t.* tapakaa; zagaa; jaa tele. *warehouses ~d with rats,* ghala zilizojaa panya.

**infidel** /'ɪnfɪdəl/ *n.* kafiri. **~ity** *n.* ukafiri; uzinzi.

**infiltrate** /'ɪnfɪltreɪt/ *v.i* penyeza; penya.

**infiltration** /,ɪnfɪl'treɪʃn/ *n.* upenyaji.

**infinite** /'ɪnfɪnət/ *adj.* -siyokoma; -sio na kikomo; -sio na mwisho; -siopimika; -kubwa sana; -ingi sana. *the ~,* Mungu. **~ly** *adv.* mno. **~simal** *adj.* -dogo mno; -siopimika. **infinitive** *adj./n.* kitenzijina; -a kitenzijina. **infinity** *n.* pasipo mwisho au kikomo; *(maths.)* namba isiyo na kikomo.

**infirm** /ɪn'fɜ:m/ *adj.* dhaifu; -lemavu; -gonjwa. **~ary** *n.* (la zamani) hospitali. **~ity** *n.* udhaifu; ugonjwa; ulemavu.

**inflame** /ɪn'fleɪm/ *v.t./i.* hamasisha; hamakisha; chochea; kasirisha; washa; waka; choma; vimba; vimbisha. **inflammable** *adj.* -a kuwaka; -a kuwashika; -a kushika moto; -a kukasirika; -a kuchomeka. **inflammation** *n.* mwako; moto; uvimbeuchungu. **inflammatory** *adj.* -a kuwasha; -a kuchochea; -a kuhamakisha; -enye uvimbe.

**inflate** /ɪn'fleɪt/ *v.t./i.* jaza upepo; tia pumzi; vimbisha; panua; ongeza; kuza. *~d with pride,* liovimba kwa kiburi. **inflation** *n.* kuvimba; kupanda gharama za maisha; mfumuko wa bei.

**inflect** /ɪn'flekt/ *v.t.* badili; geuza; *(grammar)* ambisha. **~ion, inflexion** *n.* uambishaji.

**inflict** /ɪn'flɪkt/ *v.t.* piga; umiza; tesa; lazimisha; shurutisha. *~ oneself on sb.,* fuatana na mtu bila hiari yake. **~ion** *n.* adhabu; mateso.

**influence** /'ɪnfluəns/ *n.* mvuto; ushawishi; athari; uwezo wa kuathiri. **influential** *adj.* -enye uwezo; -enye kuvutia; -enye kushawishi.

**influenza** /,ɪnflu'enza/ *n.* homa ya mafua; makamasi; mafua.

**influx** /'ɪnflʌks/ *n.* uingiaji kwa wingi.

**inform** /ɪn'fɔ:m/ *v.t./i* arifu; juvya; julisha; pasha habari. *~ against sb.,* shtaki; semea; toa habari juu ya; ripoti. **~ant** *n.* mtoa habari; mjumbe. **~ation** *n.* habari; taarifa. *information bureau,* ofisi ya habari; maelezo. **~er** *n.* infoma; mtoa habari.

**informal** /ɪn'fɔ:ml/ *adj.* si rasmi; si -

a taratibu; -a kienyeji. **~ly** *adv.* kienyeji. **~ity** *n.* hali ya kutokuwa rasmi.

**infrared** /ˌɪnfrəˈred/ *adj.* infraredi: aina ya miali ya rangi nyekundu ya nuru ya lukoka ndefu ambayo haiwezi kuonekana lakini hutoa joto. **~ rays**, miali ya infraredi.

**infringe** /ɪnˈfrɪndʒ/ *v.t./i.* vunja; asi; halifu. **~ment** *n.* uasi; uvunjaji; uhalifu.

**infuriate** /ɪnˈfjʊərieɪt/ *v.t.* ghadhibisha; kasirisha.

**infuse** /ɪnˈfju:z/ *v.t./i.* tilia moyoni; rowesha; rowana; nywesha. **infusion** *n.* kumwagia maji; unyweshaji.

**ingenious**[1] /ɪnˈdʒi:niəs/ *adj.* -erevu; -vumbuzi; stadi; -bunifu; -liofanywa kwa ustadi. **ingenuity** *n.* ustadi; ubingwa; umahiri.

**ingenuous**[2] /ɪnˈdʒi:niəs/ *adj.* -sio na hila; adilifu; kweli.

**ingestion** *n.* kula: uingizaji chakula katika kiwiliwili.




**ingestion | umezaji**

**ingot** /ɪŋgət/ *n.* kinoo; kipande; kidonge; kibongemetali.

**ingrained** /ɪnˈgreɪnd/ *adj.* -liotopea; liokolea sana; -ingi; -liojazana; lioshika.

**ingredient** /ɪnˈgri:diənt/ *n.* kiambato; sehemu; kichanganyiko.

**inhabit** /ɪnˈhæbɪt/ *v.t.* kaa katika; kalia; ishi. **~able** *adj.* -a kukalika. **~ant** *n.* mkazi.

**inhale** /ɪnˈheɪl/ *v.t./i.* vuta pumzi; vuta hewa.

**inherent** /ɪnˈhɪər(ə)nt, -ˈhɛr(ə)nt/ *adj.* -a ndani; -a asili.

**inherit** /ɪnˈherɪt/ *v.t.* rithi. **~ance** *n.* kurithi; urithi; mirathi.

**inhuman** /ɪnˈhju:mən/ *adj.* -katili; -a kinyama. **~ity** *n.* ukatili; unyama.

**inimitable** /ɪˈnɪmɪtəb(ə)l/ *adj.* -sio na kifani; -sioigika.

**iniquitous** /ɪˈnɪkwɪtəs/ *adj.* -ovu sana; dhalimu. **iniquity** *n.* uovu; udhalimu.

**initial** /ɪˈnɪʃl/ *n.* herufi ya kwanza ya jina la mtu. *adj.* -a mwanzo; -a kwanza; -a awali. *v.t.* tia saini kwa kutumia herufi za kwanza za majina. **initiate** *n.* mwari; mtu aliyeingizwa katika kundi au chama. *v.t.* anza; anzisha; ingiza; fundisha; tia jandoni; kumbini au unyagoni. **initiation** *n.* mwanzo; ufunzwaji; uingizwaji; jando; unyago. **initiative** *n.* ari; uwezo wa kuanzisha jambo; moyo wa kujituma; haki ya raia kutunga sheria zao nje ya bunge.

**inject** /ɪnˈdʒekt/ *v.t.* ingiza kwa nguvu; piga sindano. **~ion** *n.* kuingiza; dawa ya sindano.

**injure** /ˈɪndʒə(r)/ *v.t.* dhuru; umiza; jeruhi. **injurious** *adj.* -a kudhuru; -a kutia hasara; -a kuumiza. **injury** *n.* madhara; hasara; maumivu; jeraha.

**injustice** /ɪnˈdʒʌstɪs/ *n.* udhalimu; tendo lisilo la haki; uonevu. *do sb. an ~*, -tomtendea haki.

**ink** /ɪŋk/ *n.* wino. *v.t.* paka , tia wino. *~ well*, kidawa. *~ pad*, kikausho.

**inland** /ˌɪnˈlænd/ *adj.* -a bara; -a ndani ya nchi. *adv.* kuelekea bara.

**inlet** /ˈɪnlet/ *n.* hori; ghuba ndogo; njia; mlango.

**inmate** /ˈɪnmeɪt/ *n.* mkazi mwenza.

**inmost** /ˈɪnməʊst/ *adj.* -a ndani kabisa.

**inn** /ɪn/ *n.* hoteli; mkahawa.

**inner** /ˈɪnə(r)/ *adj.* -a ndani; -a ndani zaidi. **~most** *adj.* -a ndani kabisa.

**innocent** /ˈɪnəsnt/ *adj.* maasumu; -sio na kosa; -siodhuru; -siojua uovu; -jinga. **innocence** *n.* ujinga; hali ya kutokuwa na hatia.

**innocuous** /ɪˈnɒkjʊəs/ *adj.* -siodhuru; -sioumiza; -sio na madhara.

**innovation** /ˌɪnəˈveɪʃn/ *n.* uzushi; bidaa; uvumbuzi.

**innumerable** /ɪˈnju:mərəbl/ *adj.* -siohesabika; -ingi mno.

**inoculate** /ɪˈnɒkjʊleɪt/ *v.t.* chanja;

tia kasumba. **inoculation** *n.* chanjo; uchanjaji.

**inorganic** /ˌɪnɔ:'gænɪk/ *adj.* si -a kikaboni; -sio na uhai; -sioelezeka kietimolojia. **~ compound**, kampaundi simahuluku: kampaundi yoyote isiyokuwa na atomu za kaboni.

**inquest** /'ɪŋkwest/ *n.* uchunguzi rasmi wa kisheria.

**inquire** *v.t.* uliza; taftishi; tafiti. *~ into,* chunguza; peleleza; dadisi. *~ after,* ulizia hali. *~ for,* taka; omba. **~r** *n.* mdadisi. **inquiry** *n.* uchunguzi; kuuliza; maulizo. **inquisition** *n.* uchunguzi rasmi. **inquisitive** *adj.* -pekuzi; -enye udaku; -dadisi.

**insatiable** /ɪn'seɪʃəb(ə)l/ *adj.* -siotosheka; sioridhika; -sioshiba.

**inscribe** /ɪn'skraɪb/ *v.t.* andika; chora. **inscription** *n.* mwandiko; maandiko.

**inscrutable** /ɪn'skru:təbl/ *adj.* siofahamika; -a fumbo; -a siri.

**insect** /'ɪnsekt/ *n.* mdudu. **~icide** *n.*dawa ya kuua wadudu.

**inselberg** /'ɪns(ə)lb:g, -z-/ *n.* mlima uliojitenga ulio wima na wenye kilele cha duara.

**insensible** /ɪn'sensəbl/ *adj.* -siohisi; -liozirai; -siofahamu; -siojali; -liokufa ganzi; -dogo sana. **insensibility** *n.* kutoona; kutotambua; kutohisi.

**insert** /ɪn'sɜ:t/ *n.* kitu kilicho-ingizwa. *v.t.* tia; penyeza; ingiza; weka.

**inside** /ˌɪn'saɪd/ *n./adj./adv./prep.* ndani; -a ndani; ndani ya; upande wa ndani.

**insidious** /ɪn'sɪdiəs/ *adj.* -enye kudhuru kwa siri.

**insight** /'ɪnsaɪt/ *n.* busara; umaizi; utambuzi.

**insinuate** /ɪn'sɪnjueɪt/ *v.t.* penyeza kidogo kidogo kijanja; dokeza; singizia.

**insipid** /ɪn'sɪpɪd/ *adj.* chapwa; -sio na ladha.

**insist** /ɪn'sɪst/ *v.t./i.* shikilia; sisitiza. **~ence** *n.* msisitizo. **~ent** *adj.* -enye kushikilia; -a kusisitiza.

**insolent** /'ɪnsələnt/ *adj.* -fedhuli; -enye jeuri; enye dharau. -enye kutakabari. **insolence** *n.* ujeuri; takaburi

**insoluble** /ɪn'sɒljəbl/ *n.* isomu-munyika: isiyoweza kuunda mmumunyo katika maji au kimumunyishaji kingine makh-susi.

**insomnia** /ɪn'sɒmniə/ *n.* ukosefu wa usingizi; kurukwa na usingizi.

**inspect** /ɪn'spekt/ *v.t.* kagua; angalia. **~ion** *n.* ukaguzi. **~or** *n.* mkaguzi; mrakibu.

**inspire** /ɪn'spaɪə(r)/ *v.t.* shajiisha; ongoza; tia moyo. **inspiration** *n.* ilhamu; maongozi; mtu aongozaye.

**install** /ɪn'stɔ:l/ *v.t.* funga chombo sehemu. **~ation** *n.* uwekaji; chombo kilichowekwa.

**instalment** /ɪn'stɔ:lmənt/ *n.* sehemu; fungu; kipingili.

**instance** /'ɪnstəns/ *n.* mfano; namna. *for ~,* kwa mfano. *at the ~ of,* kwa ombi la fulani. *v.t.* toa kama mfano; taja.

**instant** /'ɪnstənt/ *adj.* -a mara moja; -a mwezi huu; -a haraka; -a papo hapo. *this ~,* sasa hivi. *the ~ that,* mara. **~ly** *adv.* mara moja. **~aneous** *adj.* -a mara moja; -a papo hapo.

**instead** /ɪn'sted/ *adv.* mahali pa; badala ya.

**instep** /'ɪnstep/ *n.* kiganja cha mguu (juu ya unyayo).

**instigate** /'ɪnstɪgeɪt/ *v.t.* chochea. **instigation** *n.* uchochezi. **instigator** *n.* mchochezi.

**instinct** /'ɪnstɪŋkt/ *n.* silka. **~ive** *adj.* -a silka; bila kufikiri.

**institute** /'ɪnstɪtju:t/ *n.* taasisi; chuo. *~ of Kiswahili and Foreign Languages,* Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni. *v.t.* anzisha; weka; asisi. **institution** *n.* desturi; chama; shirika; asasi; sheria.

**instruct** /ɪn'strʌkt/ *v.t.* fundisha; funza; amuru; agiza; arifu. **~ion** *n.* mafunzo. **~ive** *adj.* -a kufundisha; -a kuelimisha. **~or** *n.* mwalimu.

**instrument** /'ɪnstrəmənt/ *n.* chombo; ala; zana; kifaa; hati rasmi; mtumishi. **~al** *adj.* -a ala; -a

kusaidia; a kutumika; -a kuhusika.
**insubordinate** /ˌɪnsəˈbɔːdɪnət/ *adj.* -asi; -kaidi. **insubordination** *n.* uasi; kuasi; uhalifu; ukaidi.
**insufferable** /ɪnˈsʌfrəbl/ *adj.* enye kujiona sana; enye majivuno sana; -siovumilika; -siostahamilika.
**insular** /ˈɪnsjələ(r)/ *adj.* -a kisiwa; -enye maarifa finyu; -enye tabia za watu wa visiwa kwa kuwa mbali na wenzao. **~ity** *n.* ufinyu wa mawazo; ukinaifu; kuwa kama kisiwa.
**insulate** /ˈɪnsjuleɪt/ *v.t.* funika kwa mpira; tenga; hami; kinga. **insulation** *n.* kutengwa; kukingwa. **insulator** *n.* kihami: mata au dutu inayozuia umeme au sauti kupita.
**insulin** /ˈɪnsjelɪn/ *n.* insulini: homoni inayorekebisha kiwango cha sukari katika damu, hutengenezwa katika tezi zinazoitwa vijisiwa vya *Langerhans* vilivyopo katika kongosho ya wanyama wenye uti wa mgongo.
**insult** /ɪnˈsʌlt/ *n.* tusi. *v.t.* tukana.
**insuperable** /ɪnˈsuːpərəbl/ *adj.* sioshindika; -sioondoleka.
**insurance** /ɪnˈʃʊərəns/ *n.* bima; malipo ya bima; kinga. **~ policy** *n.* hati ya bima. **insure** *v.t.* kata bima.
**insurrection** /ˌɪnsəˈrekʃn/ *n.* uasi; upinzani dhidi ya serikali.
**intact** /ɪnˈtækt/ *adj.* -zima; kamili; sioharibiwa.
**intake** /ˈɪnteɪk/ *n.* mlango; kipenyo; kiingizio; idadi iingiayo mahali kwa muda fulani.
**intangible** /ɪnˈtændʒəbl/ *adj.* sioshikika; -sioeleweka kirahisi; tatanishi.
**integer** /ˈɪntɪdʒə/ *n.* kitu kizima; namba kamili. **integral** *adj.* -a lazima; muhimu; kamilifu; zima; -enye namba kamili; -rejeo.
**integrate** /ˈɪntɪgreɪt/ *v.t.* kamilisha; unganisha; changanya.
**integrity** /ɪnˈtegrəti/ *n.* uadilifu; uaminifu; ukamilifu.
**intellect** /ˈɪntəlekt/ *n.* akili. **~ual** *adj.* -a akili; -somi. -enye akili nyingi. *n.* msomi.
**intelligence** /ɪnˈtelɪdʒəns/ *n.* akili; ufahamu; ujuzi. **intelligent** *adj.* -enye akili. **intelligentsia** *n.* tabaka la wasomi. **intelligible** *adj.* dhahiri; -a kufahamika. **intelligibility** *n.* udhahiri; ufahamikaji.
**intend** /ɪnˈtend/ *v.t.* kusudia; nuia; dhamiria; azimu.
**intense** /ɪnˈtens/ *adj.* -a nguvu; kali sana. **intensify** *v.t./i.* ongeza; zidisha; zidi; ongezeka. **intensity** *n.* nguvu; mkazo; ukali.
**intent** /ɪnˈtent/ *n.* nia; azimio; dhamira; kusudi. *adj.* -enye bidii; -enye dhamira. **intention** *n.* nia; kusudi; dhamira. **~al** *adj.* -a makusudi. **~ally** *adv.* kwa kudhamiria hasa.
**inter** /ɪnˈtɜː(r)/ *v.t.* (**-rr-**) zika. **~ment** *n.* mazishi; kuzika.
**inter-** /ˈɪntə(r)/ *prefix* kati ya; miongoni mwa; baina.
**intercede** /ˌɪntəˈsiːd/ *v.i.* ombea; tetea. **intercession** *n.* maombezi; utetezi.
**intercept** /ˌɪntəˈsɛpt/ v.t. kamata; zuia njiani; ingilia kati.
**interchange** /ɪntəˈtʃeɪn(d)ʒ/ *n.* badiliko; ubadilishaji; *v.t.* badilishana; badili.
**intercourse** /ˈɪntəkɔːs/ *n.* ushiri kiano; maingiliano; biashara; kubadilishana vitu; kujamiiana.
**interest** /ˈɪntrəst; -trest/ *n.* **1.** moyo wa kutaka kujua; **2.** udadisi; mvuto; raghaba. **3.** upendeleo. *His chief ~s are business and football.* anapenda sana biashara na kandanda. **4.** faida; riba; hisa. *He charges 5 per cent. ~,* anatoza asilimia tano. **~ing** *adj.* -a kuvutia; -a kupendelea.
**interfere** /ˌɪntəˈfɪə(r)/ *v.i.* jiingiza; jitia kati; jidukiza; ingilia; zuia. **~nce** *n.* uingiliaji; kuzuia; kizuizi.
**interim** /ˈɪnt(ə)rɪm/ *n.* muda; wakaa. *in the ~,* kwa wakati huu.
**interior** /ɪnˈtɪəriə(r)/ *n.* ndani; upande wa ndani; bara. *adj.* -a ndani; -a bara; si -a pwani; -a nchini; si -a kigeni.
**interlock** /ˌɪntəˈlɒk/ *v.t./i.* unga nisha; ungamana; ungana.

**interlude** /'ɪntəlu:d/ *n.* mapumziko; nafasi kati ya matukio mawili.
**intermediate** /ˌɪntə'mi:dɪət/ *adj.* -a kati; a baina ya.
**interminable** /ɪn'tɜ:mɪnəbl/ *adj.* -sio mwisho; -a kuchosha; -a kuchusha.
**intermittent** /ˌɪntə'mɪtənt/ *adj.* -a vipindi.
**intern** /'ɪntə:n/ *v.t.* funga; zuia. **~ee** *n.* mfungwa. **~ment** *n.* kifungo. **~al** *adj.* -a ndani; -a nchi; -a asili; -a moyoni. **~ combustion engine**, injini mwako ndani: injini ambayo mchanganyiko wa petroli na hewa huingia kwenye silinda ya injini na kuripuliwa na cheche.
**international** /ˌɪntə'næʃnəl/ *adj.* -a kati ya mataifa; -a mataifa; -a kimataifa.
**internet** /ˌɪntənet/ *n.* mdahalishi (mtandao): mtandao wa kimataifa wa mawasiliano ya habari na data unaounganisha kompyuta duniani kwa kutumia modemu na setilaiti. **~ cafe** *n.* kituo cha huduma za mdahalishi (mtandao).
**interplanetary space** *n.* masafa baina ya jua na sayari nyingine katika mfumo wa jua.
**interpret** /ɪn'tɜ:prɪt/ *v.t./i.* fasiri; agua; eleza; fafanua. **~er** *n.* mkalimani; mwaguzi. **~ation** *n.* tafsiri; maelezo; ufafanuzi; uaguzi.
**interrogate** /ɪn'terəgeɪt/ *v.t.* hoji; saili; dodosa.
**interrogation** /ɪnˌterə'geɪʃn/ *n.* kuhoji; usaili. **interrogative** *adj.* a kuuliza.
**interrupt** /ˌɪntə'rʌpt/ *v.t./i.* dakiza; katiza; dakuliza; ingilia kati; pinga. **~ion** *n.* kudakiza; pingamizi.
**intersect** /ˌɪntə'sekt/ *v.t./i.* gawa kwa kukata; katana. **~ion** *n.* ukatanaji; mkingamano; ungano; nukta mistari inapokingamana.
**interval** /'ɪntəvl/ *n.* wakati baina ya matukio mawili; nafasi baina ya vitu au vituo viwili; tofauti ya sauti baina ya noti mbili. *at ~s,* kwa vipindi.
**intervene** /ˌɪntə'vi:n/ *v.i.* ingilia kati; jitia kati; -wa kati ya. **intervention** *n.* uingiliaji kati.
**interview** /'ɪntəvju:/ *n.* mahojiano; usaili. *v.t.* hoji; saili. **~ee** *n.* msailiwa; mhojiwa. **~er** *n.* mhojaji; msaili.
**intestine** /ɪn'təstɪn/ *n.* matumbo. **small ~**, utumbo mwembamba. **large ~**, utumbo mpana.
**intimate** /'ɪntɪmət/ *adj.* a moyoni; -a ndani; -a siri; -a moyo *an ~ friend,* msiri; mwandani. *v.t.* arifu; eleza; onyesha bayana. **intimacy** *n.* urafiki wa ndani; ngono; kuja-miiana; mwandani.
**intimidate** /ɪn'tɪmɪdeɪt/ *v.t.* tisha; ogofya. **intimidation** *n.* kitisho.
**intoxicate** *v.t.* levya; lewesha; rusha akili; tia jazba.
**intricate** /'ɪntrɪkət/ *adj.* tatanishi; -enye matatizo. **intricacy** *n.* matatizo; utatanishi.
**intrigue** /ɪn'tri:g/ *n.* hila; werevu; njama. *v.i.* -la njama; vutia sana.
**introduce** /ˌɪntrə'dju:s/ *v.t.* leta; anza; julisha; anzisha; ingiza; penyeza. **introduction** *n.* uingizaji; utangulizi; dibaji; utambulisho; ufahamisho. **introductory** *adj.* a mwanzo; -a kuanzisha; -a utambulisho.
**introspection** /ˌɪntrə'spekʃn/ *n.* kujiangalia nafsi.
**intrude** /ɪn'tru:d/ *v.t./i.* dukiza; ingia bila kukaribishwa. **~r** *n.* mdukizi. **intrusion** /ɪn'tru:ʒn/ *n.* kujidukiza; kuingilia.
**intuition** /ˌɪntju'ɪʃn/ *n.* uwezo wa kuelewa haraka; welewa bila ya kufikiri.
**inundate** /'ɪnʌndeɪt/ *v.t.* gharikisha. **inundation** *n.* gharika; mafuriko.
**invade** /ɪn'veɪd/ *v.t.* shambulia; vamia; ingilia; hujumu; ingilia haki ya mtu. **~r** *n.* mvamizi. **invasion** *n.* uvamizi; shambulio.
**invalid**[1] /ɪn'vælɪd/ *n./adj.* mgonjwa; gonjwa; siojiweza; -a kufalia wagonjwa *an ~ chair,* kiti cha kiwete. *v.t./i.* toa (tolewa) kazini kwa ugonjwa.
**invalid**[2] /ɪn'vælɪd/ *adj. (leg.)* batili; -liotanguka; -a bure. **~ate** *v.t.* batilisha; tangua.
**invaluable** /ɪn'væljuəbl/ *adj.* -a thamani

sana; -siopimika kwa kuwa na thamani sana; -a tunu.

**invent** /ɪn'vent/ *v.t.* vumbua; buni; tunga; unda. **~ion** *n.* uvumbuzi; ubunifu; bidaa; uwongo; hila; werevu. **~ive** *adj.* -vumbuzi; -zushi; -bunifu. **~or** *n.* mzushi; mvumbuzi.

**inventory** *n.* orodha; hesabu.

**inversion** /ɪn'vɜ:ʃn/ *n.* upinduzi; ugeuzi; mpinduo: matokeo ya kubadili utaratibu wa kawaida wa mpangilio wa maneno katika sentensi. **invert** *v.t.* pindua; weka kinyume; geuza.

**invertebrate** /ɪn'vɜ:tɪbrət/ *n.* mnyama asiye na uti wa mgongo. *adj.* -sio na uti wa mgongo;

**invest** /ɪn'vest/ *v.t./i.* tega uchumi; wekeza; nunua; -pa; vika; pamba; zingira; fanya mazingara. **~ment** *n.* kitega uchumi. **~or** *n.* mwekezaji.

**investigate** /ɪn'vestɪgeɪt/ *v.t.* chunguza; peleleza. **investigation** *n.* upelelezi; uchunguzi. **~or** *n.* mpelelezi; mchunguzi.

**invincible** /ɪn'vɪnsəbl/ *adj.* -sioshindika.

**invite** /ɪn'vaɪt/ *v.t.* alika; omba; taka; vuta; shawishi; karibisha. **invitation** *n.* mwaliko. **inviting** *adj.* - a kuvutia.

**in vitro** /ɪn 'vɪ:trəʊ/ *adj.* -a halighushi: -a mchakato wa kibiolojia unaotokea nje ya kiumbe hai kama kwenye tesitubu au kiolezo.

**in vivo** /ɪn 'vɪ:vəʊ/ *adj.* -a kiasili: -a mchakato unaotokea ndani ya kiumbe hai.

**invoice** /'ɪnvɔɪs/ *n./v.t.* ankara; bili; tengeneza ankara au bili.

**invoke** /ɪn'vəʊk/ *v.t.* omba kwa Mungu, mizimu etc.; omba; sihi; ita mashetani. **invocation** *n.* maombi; dua; utambikaji.

**involuntary** /ɪn'vɒləntri/ *adj.* -siokusudiwa; bila kujua; bila hiari.

**involve** /ɪn'vɒlv/ *v.t.* husisha; ingiza matatani; sababisha; -wa sababu ya; maanisha **~d** *adj.* husika kwenye jambo au na mtu. *I'm not ~ in this matter,* sihusiki na jambo hili.

**inward** /'ɪnwəd/ *adj.* -a ndani; -a rohoni. **~ly** *adv.* moyoni; rohoni.

**iodine** /'ʌɪədi:n, -ʌɪn, -ɪn/ *n.* aidini; madini ya joto.

**ion** /'aɪən/ *n.* ioni: molekuli au atomu iliyo na chaji kutokana na kupokea au kutoa elektroni. **~ic bond** muungo kiioni: muungo kikemikali ulioundwa kwa njia ya kiume metuamo wa ioni. **~ic compound** kampaundi ionia: kampaundi iliyoundwa na ioni zenye chaji chanya na zenye chaji hasi. **~izing radiation** mnururisho ioni: mnururisho unaobadilisha kampaundi kemikali kuwa ioni.

**ionosphere** /ʌɪ'ɒnəsfɪə/ *n.* tabaka ya tatu toka angahewa ya dunia baada ya tabakastrato, hutumika sana kwa mawasiliano ya redio.

**ir** - *prefix* si.

**irate** /ʌɪ'reɪt/ *adj.* a hasira.

**ire** /'aɪə(r)/ *n.* (*liter.*) hasira.

**iris** /'aɪrɪs/ *n.* duara ya rangi izungukayo mboni ya jicho.

**iron** /'aɪən/ *n.* chuma; pasi. *Strike while the ~ is hot,* udongo upate ungali maji (rekebisha kasoro katika hatua za awali). *a man of ~,* katili. *have too many ~s in the fire,* shughulikia mambo mengi kwa wakati mmoja. *~s,* pingu; minyororo. *put a man in ~s,* funga minyororo. *v.t.* piga pasi. **~monger** *n.* muuza bidhaa za chuma. **~mongery** *n.* biashara ya bidhaa za chuma. **~-mould** *n.* doa la kutu au wino.

**irony** /'ʌɪrəni/ *n.* kejeli; kinaya; jambo la kinyume. *the ~ of fate,* dhihaka ya majaliwa. **ironic(al)** *adj.* -a kejeli; -a kinaya.

**irradiation** /ɪˌreɪdi'eɪʃn/ *n.* unururikaji: unang'anikaji kutokana na miali ya nuru inayopiga uso wa gimba.

**irresistible** /ˌɪrɪ'zɪstəbl/ *adj.* -siokatalika; -sozuilika; -siovumilika.

**irrespective** /ɪrɪ'spektɪv/ *adj.* bila kujali; bila kuzingatia; bila kuangalia.

**irresponsible** /ˌɪrɪ'spɒnsəbl/ *adj.* -siopaswa; -siowajibika; -sioaminika;

-siotumainiwa.
**irrigate** /'ɪrɪgeɪt/ *v.t.* mwagilia; jenga mfumo wa umwagiliaji maji. **irrigation** *n.* umwagiliaji.
**irritate** /'ɪrɪteɪt/ *v.t.* washa; kasirisha; choma; udhi; kera; sumbua. **irritable** *adj.* -epesi wa hasira. **irritant** *n./adj.* kitu kinachowasha; -enye kuwasha; -enye kukera. **irritation** *n.* mwasho; kichomi; uchungu.
**island** /'aɪlənd/ *n.* kisiwa. **~er** *n.* mzaliwa au mkazi wa kisiwani. **isle** *n.* kisiwa. **islet** *n.* kisiwa kidogo.
**isobar** /'ʌɪsə(ʊ)ba:/ *n.* isobaa; msawakani: mstari unaounganisha sehemu zenye kanieneo ya angahewa inayolingana; mstarikani.
**isohyte** *n.* isohiti: mstari unao unganisha sehemu zote zenye kiwango sawa cha mvua kwa kipindi fulani.
**isolate** /'aɪsəleɪt/ *v.t.* tenga. **isolation** *n.* utengaji; upweke; upekee.
**isomer** /'ʌɪsəmə/ *n.* isoma: mojawapo ya misombo yenye mtungo na uzito wa molekuli sawa lakini hutofautiana katika muundo.
**isosceles** /ʌɪ'sɒsɪli:z/ *adj.* enye pande mbili sawa. ~ *triangle,* pembetatu yenye pande mbili sawa. safari; njia ya safari.
**isotherm** /'ʌɪsə(ʊ)θə:m/ *n.* msawajoto: mstari unaounganisha sehemu zenye halijoto inayolingana.
**isotope** /'ʌɪsətəʊp/ *n.* isotopu: atomi yenye uzito tofauti na atomu nyingine.
**issue** /'ɪʃ(j)u:, 'ɪsju:/ *n.* kutoka; kitokeacho; utoaji; toleo; suala; hoja; matokeo. *v.i./t.* toka; -ja; tokea; toa; chapisha; gawanya. *die without ~,* kufa bila ya mtoto.
**ismuths** /'ɪsθməs, 'ɪstməs, 'ɪsməs/ *n.* shingo ya nchi iliyounganisha mabara mawili.
**it** /ɪt/ *pron.* hii; hiki; hicho; huyu; huyo; huu; kile; ile; ule; etc.
**italic** /ɪ'talɪk/ *adj.* -a italiki; -a mlazo; -a herufi *hizi.*
**itch** /ɪtʃ/ *n.* mwasho; shauku. *v.i.* chochota; washa; -wa na shauku.
**item** /'aɪtəm/ *n.* kitu kimoja; aya; kipengele; maelezo.
**itenerant** /ɪ'tɪn(ə)r(ə)nt, ʌɪ-/ *adj.* -a kutembeatembea; -a kuzunguka zunguka.
**itenerary** /ʌɪ'tɪn(ə)(rə)ri, ɪ-/ *n.* mpango wa safari; njia ya safari;.
**ivory** /'aɪvəri/ *n.* pembe ya ndovu.

# Jj

**jab** /dʒæb/ *n.* kipigo cha nguvu; dhoruba. *v.t.* (**-bb-**) piga kwa nguvu.
**jack** /dʒæk/ *n.* jeki; bendera ya meli; kikombe cha ngozi; baharia. ~ *up,* inua kwa jeki. **~ass** *n.* punda dume; mpumbavu. **~-of-all-trades** *n.* mtu ajuaye kila kazi japo si kwa ustadi.




**jackal** /'dʒakəl, -kɔ:l/ *n.* mbweha.
**jacket** /'dʒækɪt/ *n.* jaketi; kifuniko; kidhibiti joto; maganda ya viazi; gamba.
**jaded** /'dʒeɪdɪd/ *adj.* hoi.
**jag** *n.* chonge; ncha; jino la msumeno. **~ged** *adj.* -enye vichonge. ~ *rocks,* majabali yenye ncha.
**jaguar** /'dʒagjʊə/ *n.* aina ya chui wa Amerika.
**jail** /dʒeɪl/ *n.* jela; gereza.
**jam**[1] /dʒæm/ *n.* msongano; ukwamaji; hali ngumu. *v.t./i.* (**-mm-**) bana; kwamisha; kwama; shindilia; funga kwa nguvu; songamana; rundika; ingilia mawimbi ya sauti. *He ~med on the brakes,* alifunga breki ghafla.
**jam**[2] /dʒæm/ *n.* mraba; jamu; jemu.

**January** 'dʒænjuəri *n.* Januari: mwezi wa kwanza wa mwaka wa kizungu.

**jar** 'dʒa:(r) *n.* mkwaruzo: mtete meko: mshtuko: mtungi: gudulia: kasiki: chupa. *v.i. t.* **(-rr-)** gonga na kutoa sauti ya kukera: shtua: shtuka.

**jargon** 'dʒa:g(ə)n *n.* istilahi: lugha ya kitaalamu: lugha ya mtaani.

**jaundice** 'dʒɔ:ndɪs *n.* homa ya manjano: wivu: husuda. **~d** *adj.* enye wivu: enye husuda.

**javelin** 'dʒæv(ə)lɪn *n.* javelini: mkuki.

**jaw** 'dʒɔ: *n.* taya: utaya: kinywa: *(fig.)* mwingilio wa bonde: pango hasa wa mahali pa hatari: jirawa. *(colloq.)* hotuba ndefu ya kuchosha. *v.t. i. (colloq.)* piga domo: karipia.

**jazz** dʒæz *n.* jazi.

**jealous** 'dʒeləs *adj.* enye wivu: enye husuda: ona gele. *be ~* ona wivu. *be ~ of sb else's success* ona kijicho dhidi ya mafanikio ya mwenzio. *be ~ of reputation* wa mwangalifu wa heshima. **~y** *n.* wivu: husuda **~ly** *adv.* kiwivu: kihusuda.

**jeer** 'dʒɪə(r) *n.* dhihaka: mzaha: cheko. *v.i.* dhihaki: cheka: zomea.

**jelly** 'dʒeli *n.* ute: jeli. **~fish** *n.* konyeza: kiwavi bahari.


jelly fish

**jeopardy** 'dʒepədi *n.* hatari: mashaka. *put in ~* tia hatarini.

**jeopardize** 'dʒepədaɪz *v.t* hatarisha.

**jerk** 'dʒ3:k *n. v.t. i.* mshtuo: mshtuko: mazoezi ya viungo: shtua: shtuka: shtusha. *The train stopped with a ~* gari la moshi lilisimama ghafla. **~y** *adj.* enye kushtukashtuka. **~ily** *adv.* kwa mshtuko.

**jersey** 'dʒ3:zi *n.* fulana nzito: jezi: sweta.

**jet** 'dʒet *n.* mchirizi wa ghafla wa maji etc: utokao kwenye kipenyo: upenyo wa kutokea maji etc. **~aircraft** *n.* jeti. **~ propulsion** usukumaji wa jeti: mbinu ya kuleta kani ya usukumaji kwenye chombo cha hewani au majini kwa kutumia mjibutiko wa jeti ya velositi ya juu.

**jewel** 'dʒu:əl *n.* kito: johari: almasi: jiwe la thamani: kitu (au mtu) cha thamani. **~ler** *n.* muuza vito. **~lery ~ry** *n.* mapambo ya vito.

**jig** dʒɪg *n.* dansi ya mtindo wa yosayosa. *v.i. t.* **(-gg-)** cheza yosayosa: rukaruka: rusharusha. **~-saw puzzle** *n* chemshabongo.

**jigger** *n.* chepu: funza.

**job** 'dʒɒb *n.* kazi: ajira: wadhifa. *That's a good ~* ni kazi nzuri *v.t. i.* **(-bb-)** fanya kazi ndogondogo za namna nyingi. *a ~bing gardener* mlimaji bustani.

**jockey** 'dʒɒki *n.* mpanda farasi katika mashindano. *v.t.* hadaa: ghilibu: danganya: laghai.

**jog** dʒɒg *n. v.t. i.* **(-gg-)** kujogi: mbio za polepole: mkutuo: kikumbo: jogi: kutua: piga kikumbo. *(fig.) ~ sb's memory* kumbusha. *~ along (fig.)* jikongoja. **~trot** *n.* mwendo wa polepole.

**join** dʒɔɪn *n.* kiungo: fundo. *v.t. i.* unga: ingia: ungana na: fuatana na: changanyika na. **~er** *n.* seremala. **~ery** *n.* useremala. **~t** *n. adj.* kiungo: fundo: -a pamoja. *~ stock* mali ya pamoja.

**joke** dʒəʊk *n.* mzaha: masihara: kichekesho: dhihaka. *It's no ~* si mchezo: si utani. **~r** *n.* chale: mcheshi.

**jokingly** d'ʒəʊkɪŋli *adv.* kimzaha: kimasihara.

**jolly** 'dʒɒli *adj.* -a furaha: changamfu: -a kupendeza: zuri. *adv.* sana. **jollification** *n* shamrashamra.

**jollity** 'dʒɒləti *n.* furaha.

**jolt** dʒəʊlt dʒɒlt *n. v.t. i.* mshtuko: mshtuo: mtikisiko: shtusha: shtuka: rusharusha.

**jot** 'dʒɒt *n.* kipande: kidogo: nukta. *He hasn't a ~ of honesty* hana hata chembe ya uaminifu. *v.t* **(-tt-)** *~ (sth.) down* andika upesiupesi. **~ter** *n.* kidaftari. **~tings** *n.* kumbukumbu.

**joule** dʒu:l *n.* juli: kizio cha kazi

(nishati au joto): ni kazi iliyofanywa wakati nukta ya matumizi ya kani ya nyutoni moja inaposogezwa mita moja kuelekea upande wa kani.

**journal** /ˈdʒɜ:n(ə)l/ *n.* gazeti; jarida; kitabu cha mambo ya kila siku. **~ese** *n.* lugha chapwa ya kigazeti. **~ism** *n.* uandishi wa habari. **~ist** *n.* mwandishi wa habari.

**journey** /ˈdʒɜ:ni/ *n.* safari; mwendo. *v.i.* safiri.

**jovial** /ˈdʒəʊvɪəl, vj(ə)l/ *adj.* kunjufu; changamfu; -a furaha; -a bashasha. **~ity** *n.* ukunjufu; bashasha; furaha.

**joy** /dʒɔɪ/ *n.* furaha; shangwe; nderemo. **~ful** *adj.* -a furaha; -a kufurahisha. **~fully** *adv.* kwa furaha. **~less** *adj.* -a huzuni. **~lessly** *adv.* bila furaha. **~ous** *adj.* -a furaha.

**jubilant** /ˈdʒu:bɪlənt/ *adj.* -a shangwe. **jubilation** *n.* shangwe; furaha. **jubilee** *n.* jubilii; sikukuu ya ukumbusho. *silver jubilee*, jubilii ya mwaka wa 25. *golden ~*, jubilii ya mwaka wa 50. *diamond ~*, jubilii ya mwaka wa 60 au wa 75.

**judge** /dʒʌdʒ/ *n.* jaji; hakimu; mwamuzi. *v.t./i.* hukumu; toa hukumu; amua; dhani; ona. *I ~ it better to postpone a meeting*, nadhani afadhali kuahirisha mkutano. *~ a man by his actions*, pima mtu kwa vitendo vyake. **~ment** *n.* hukumu; maamuzi; akili; busara; ujuzi; maoni.

**judicial** /dʒuˈdɪʃl/ *adj.* -a jaji; -a haki; -a kimahakama. **judicious** *adj.* [illegible] **judiciously** [illegible] **judiciousness** [illegible]

**jug** [illegible]


jug

**juggle** [illegible]

[illegible]

enye maji mengi.

**July** /dʒuˈlaɪ/ *n.* Julai; mwezi wa saba wa mwaka wa kizungu.

**jumble** /ˈdʒʌmbl/ *n.* fujo; mchanganyiko; vurugu. *v.t./i.* changanya; chafua; chafuka; fuja; vuruga; parganya. *~ sale*, seli ya vitu vikuukuu.

**jump** /dʒʌmp/ *n.* mruko; mchupo; mshtuo; upandaji wa ghafla; nyunju. *v.i./t.* ruka; chupa; shtuka; panda ghafla. *~ at*, pokea kwa furaha. *~ up at sb.*, karipia. *There was a ~ in the price of rice*, bei ya mchele ilipanda ghafla. **~er** *n.* mrukaji; sweta; aproni. **~y** *adj.* epesi kushtuka.

**junction** /ˈdʒʌŋkʃn/ *n.* njia panda; kiungo. **juncture** *n.* muungano; hali ya jambo. *at this ~*, hapa sasa katika hali hii.

**June** /dʒu:n/ *n.* Juni; mwezi wa sita wa mwaka wa kizungu.

**jungle** /ˈdʒʌŋgl/ *n.* kichaka; msitu. *law of the ~*, sheria ya mabavu.

**junior** /ˈdʒu:nɪə(r)/ *n./adj.* mdogo (kwa umri, kwa cheo); -dogo; -a chini.

**junk**[1] /dʒʌŋk/ *n.* takataka; vikorokoro.

**junk**[2] /dʒʌŋk/ *n.* jahazi la kichina.

**Jupiter** /ˈdʒu:pɪtə(r)/ *n.* sumbula; sayari ya tano kutoka kwenye jua iliyo kubwa kupita zote.

**jurassic** /dʒʊˈræsɪk/ *adj.* -a kijura; -a zama za kijiolojia ilipoanza miamba ya chokaa, mijusi mikubwa na ndege. *~* **period** kipindi cha kijura; kipindi cha kijiolojia katika historia ya miaka 140 hadi 190 milioni iliyopita.

**jurisdiction** [illegible] *n.* hukumu; amri; mamlaka; mamlaka ya kisheria. **jurisprudence** *n.* maarifa ya sheria; sayansi na falsafa ya sheria ya binadamu.

**jurist** /ˈdʒʊərɪst/ *n.* mwanasheria. **juror** *n.* mzee wa baraza. **jury** *n.* baraza la wazee wa mahakama; waamuzi; mtu anayeapishwa. **juryman** *n.* mzee wa baraza. **jury-mast** *n.* mlingoti wa muda.

**just**[1] /dʒʌst/ *adv.* barabara

sawasawa; tu. ~ *now*, sasa hivi. *He has ~ come*, ndio kwanza kafika. *He ~ succeeded*, amefaulu punde hivi. *That is ~ right*, ndivyo hasa. ~ *what I said*, ndivyo hasa nilivyosema.

**just**[2] /dʒʌst/ *adj.*-a haki; -liostahili; -adilifu. **~ice** *n.* haki; uadilifu; jaji. *Treat all man with ~*, tendea haki watu wote. *do ~ to*, tenda haki. *bring a man to ~*, leta mtu mbele ya sheria. *justice of the peace*, hakimu. **justifiable** *adj.* -a kuthibitishika kuwa -a haki. **justification** *n.* haki; uhalali; ithibati. **justify** *v.t.* thibitisha uhalali wa jambo; halalisha; -wa sababu ya kufanya jambo.

**jut** /dʒʌt/ *n.* utokezaji. *v.i.* **(-tt-)** ~ *out*, tokeza; chomoza.

**juvenile** /ˌdʒuːvənʌɪl/ *n.* kijana; mtoto. *adj.* -a kitoto; -a kijana.

**juxtapose** /ˌdʒʌkstə'pə'pəʊz/ *v.t.* weka sambamba. **juxtaposition** *n.* hali ya kuwa sambamba.

# Kk

**kangaroo** /ˌkæŋgə'ruː/ *n.* kangaruu. ~ *court*, mahakama isiyo halali.


kangaroo

**karst** /kaːst/ *n.* eneo lenye miamba ya chokaa yenye mivungu mingi chini yake ipitayo michirizi ya maji.

**keel** /kiːl/ *n.* mkuku. *be on an even ~*, *(fig.)* tulia.

**keen** /kiːn/ *adj.* -kali; -enye bidii; hodari; -enye kupenda sana. *(fig.) a ~ wind*, upepo mkali. **~ly** *adv.* kwa bidii. **~ness** *n.* bidii; juhudi.

**keep** /kiːp/ *v.t./i.* (**kept** /kept/)
**1.** tunza; weka; shika. **2.** fuata.
**3.** ruzuku; kimu; fuga; tunza; simamia. **4.** zuia; tuliza; kinga; nyamazisha. **5.** fululiza; dumu.
**6.** -wa na; miliki. **7.** linda; hifadhi. ~ *goats*, fuga mbuzi. ~ *a ledger*, tunza leja. ~ *your own consel*, ficha maoni yako. ~ *quiet*, nyamaza. ~ *the children quiet*, bembeleza watoto. *Traffic in Zanzibar ~s to the left*, Zanzibar gari hupita kushoto. ~ *straight on*, nenda moja kwa moja. *They were all kept indoors by the rain*, wote walibakia ndani kwa sababu ya mvua. *Meat does not ~ in a hot country*, nyama huoza upesi katika nchi ya joto. *(fig.) That news will ~*, hakuna haraka kutoa habari hizo. *Why does he ~ laughing?* kwa nini aendelea kucheka? *What kept you from meeting me?* jambo gani lilikuzuia kuonana nami? ~ *at*, shikilia. ~ *away*, epuka; epusha. ~ *down*, zuia; tuliza; punguza. ~ *from*, epukana na; epusha. ~ *in*, zuia kama adhabu. ~ *in with sb.*, patana na.

**kelvin** /'kelvɪn/ *n.* kelvini: kizio cha SI cha halijoto halisi.

**kennel** /'kenl/ *n.* tundu la mbwa; kibanda cha mbwa.

**kernel** /'kəːn(ə)l/ *n.* kiini.

**kerosene** /'kɛrəsiːn/ *n.* kerosini; mafuta ya taa.

**kettle** /'ketl/ *n.* birika; buli. *This is a pretty ~ of fish*, mambo yameparaganyika. *~drum n.* ngoma ndogo ya shaba nyeupe.

**key** /kiː/ *n.* **1.** ufunguo. **2.** *(fig.)* ufumbuzi; tafsiri; majawabu. ~ *industries*, viwanda muhimu.
**3.** kibonyezo cha kinanda, tapureta; kompyuta; piano etc. cha kupigwa kwa vidole. **~board** safu ya vibonyezo hivyo. **4.** mfululizo wa noti au sauti za muziki. **~ note** *(fig.)* wazo la msingi; noti ya muziki ya msingi. *all in the same ~*, -a namna moja; -a sauti moja. *v.t.* linganisha sauti. ~ *up*, *(fig.)* chochea. *~stone n.* jiwe la katikati ya tao.


keyboard

**khaki** /'kaːki/ *n./adj.* kitambaa cha kaki; -enye rangi ya kaki.

**kHz** *n.* ufupisho wa *kilohertz*: hezi 1000.

**kick** /kik/ *n.* teke; kiki; msisimko; mshtuko. *v.t./i.* piga teke. ~ *one's*

*heels*, kaa bure. ~ *off*, anzisha. ~ *up a row*, *(colloq.)* sababisha fujo. *get a ~ out of sth.*, ona furaha kwa kufanya jambo. *(fig.) He has no ~ left in him*, hana nguvu tena hata chembe.

**kid** /kɪd/ *n.* **1.** mwana mbuzi. **2.** ngozi ya mwana mbuzi. **3.** *(colloq.)* mtoto. **~dy** *n.* mtoto.

**kidnap** /'kɪdnæp/ *v.t.* (**-pp-**) iba mtoto; teka nyara. **~per** *n.* mtekaji nyara; mwizi wa mtoto.

**kidney** /'kɪdni/ *n.* figo.

**kill** /kɪl/ *n.* kuua; windo. *v.t.* **1.** ua; fisha. **2.** poteza; haribu. ~ *time*, poteza wakati.

**kiln** /kɪln/ *n.* tanuri; joko.

**kilo-** /'kɪləʊ/ *prefix* 1000. **kilogram** /'kɪləgræm/ *n.* gramu 1000.

**kilohertz** /'kɪləhɜ:ts/ *n.* hezi 1000. **kilometre** /'kɪləmi:tə(r)/ *n.* mita 1000.

**kilowatt** /'kɪləwɒt/ *n.* wati 1000. **~ hour**, kilowati: kizio cha kibiashara kitumikacho kupimia nguvu za umeme zinazotumika.

**kin** /kɪn/ *n.* ukoo; jamaa; ndugu. *next of ~*, ndugu wa karibu zaidi. **~dred** *n./adj.* udugu; ukoo; ufungu; -a namna moja. *claim ~ with sb.*, panga usuli na mtu.

**kind**[1] /kaɪnd/ *n.* namna; aina; kabila; ngeli; asili; tabia. *in kind*, kwa vitu. *pay in ~*, lipa kwa vitu. *repay sb. in ~*, tendea jinsi alivyokutendea.

**kind**[2] /kaɪnd/ *adj.* -ema; -pole; -enye huruma; -karimu. **~ly** *adv.* kwa huruma; kwa ukarimu. ~ *tell me*, tafadhali niambie. **~ness** *n.* wema; upole; huruma; ukarimu.

**kindergarten** /'kɪndəˌgɑ:t(ə)n/ *n.* skuli ya watoto wadogo.

**kindle** /'kɪnd(ə)l/ *v.t./i.* **1.** washa; waka. **2.** *(fig.)* raghibisha; chochea.

**kinetic** /kɪ'nɛt:ɪk, kʌɪ-/ *adj.* -a mwendo; -a kuhusiana na mwendo. **~s** *n.* mihanjo: sayansi ya uhusiano kati ya mwendo wa vitu na kani zinazohusika. **~ energy**, nishati mwendo: nishati inayotokana na mwendo wa kiolwa au gimba. **~ theory of matter**, nadharia hanji ya mata. **~ theory of gases**, nadharia hanji ya gesi.

**king** /kɪŋ/ *n.* mfalme; mtu mashuhuri; kete kuu. **~dom** *n.* ufalme; himaya; eneo; sehemu; mgao mkubwa wa viumbe ulimwenguni. **the animal ~**, jamii ya wanyama na binadamu. **vegetable ~**, jamii ya mimea. **mineral ~**, jamii ya madini. **~fisher** *n.* mdiria; chepea. **~ly** *adj.* a fahari; -a kifalme.

**kiosk** /'ki:ɒsk/ *n.* kioski; kibanda cha kuuzia bidhaa; kibanda cha simu.

**kiss** /kɪs/ *n.* busu. *v.t./i.* busu.

**kit** /kɪt/ *n.* vyombo; vifaa; zana za askari, baharia, msafiri au fundi; vifaa vya mchezo. **~bag** *n.* shanta; koba.

**kitchen** /'kɪtʃɪn/ *n.* jiko. **~garden** *n.* bustani ya mboga.

**kite** /kaɪt/ *n.* mwewe; kozi; kipanga; tiara; kishada.

**kitten** /'kɪtn/ *n* mtoto wa paka. *have ~s*, -wa na wahaka.

**knack** /næk/ *n.* ubingwa; wepesi; weledi; welekevu; ustadi.

**knead** /ni:d/ *v.t.* kanda; ponda; sukuma, hasa unga wakati wa kutengeneza mkate, chapati, maandazi.

**knee** /ni:/ *n.* goti. **~cap** *n.* pia ya goti. **~-deep** *adv./adj.* -nayofikia magotini. **~-high** *adj./adv.* - a magotini. **~l** *v.i.* (**knelt**) piga magoti.

**knife** /naɪf/ *n.* (**knives**) kisu.

**knit** /nɪt/ *v.t./i.* (**-tt-**) suka; sokota; fuma; unganisha; unga. ~ *the brows*, kunja uso. **~ting** *n.* msokoto; ufumaji; nyuzi za kufumia.

**knob** /nɒb/ *n.* kirungu; kinundu; kifundo. **~bly** *adj.* -enye vifundo. **~by** *adj.* -a vifundo. **~kerrie** *n.* rungu.

**knock** /nɒk/ *n.* pigo; kipigo; hodi. *v.t./i.* gonga; gota; bisha; piga. ~ *down*, angusha kwa kupiga. ~ *about the world*, safiri sana. ~ *sb. out*, shinda katika ndondi; *(fig.)* shangaza kabisa. ~ *off work*, acha kazi. ~ *a shilling off a bill*, toa; punguza bei. ~ *sb. up*, amsha kutoka usingizi; ~ *sth. up*, kamilisha haraka.

**knot** /nɒt/ *n.* fundo; kifundo; tindi; shida; tabu; kikundi; noti. *tie oneself up into ~s,* -wa katika matata. *a ship of 16 ~s,* meli iendayo noti 16 kwa saa. *v.t.* funga fundo; piga fundo. **~ty** *adj.* -a matata, -gumu kufahamu; -enye vifundo.

**know** /nəʊ/ *v.t./i.* (**knew known**) jua; fahamu; tambua. *You ought to ~ better than to do that,* unastahili kujua kuwa ni vibaya kufanya hivyo. *~ one's own mind,* jifahamu. *He ~s what's what,* hadanganyiki. *~ one's own business,* -wa na akili. *in the ~,* -enye habari. **~ing** *adj.* -juzi; stadi; -erevu. **~ingly** *adv.* makusudi; kwa ujuzi. **~ledge** maarifa; elimu. *to the best of my ~,* kwa kadiri nijuavyo.

**knuckle** /'nʌkl/ *n.* konde; konzi. *v.i. ~ under,* salimu amri.

**kowtow** /kaʊ'taʊ/ *v.i.* nyenyekea; sujudia kwa ishara ya heshima, tabia hii hufuatwa na Wachina.

**kraal** /krɑ:l/ *n.* (katika nchi ya Afrika ya Kusini) kitongoji; zizi.

**krypton** /'krɪptɒn/ *n.* kriptoni: aina ya gesi isiyo na rangi wala harufu inayotumiwa katika taa za mishumaa na glopu .

**kudu** /'ku:du:, 'kʊdʊ/ *n.* tandala.

# Ll

**label** /'leɪbl/ *n./v.t.* lebo; kitambulisho chenye anwani; tia lebo; weka kitambulisho.

**laboratory** /lə'bɒrəˌt(ə)ri,/ *n.* lebo; maabara.

**labour** /'leɪbə(r)/ *n.* kazi; wafanya-kazi; nguvukazi; uchungu wa uzazi. *a ~ of love,* kazi ya mkwe, yaani kazi isiyo na ujira.

**lac**[1] *n.* aina ya utomvu mwekundu wa miti utumiwao kutengenezea rangi.

**lac**[2] *n.* laki; 100, 000.

**lace** /leɪs/ *n.* lasi; uzi; kimia. *v.i./t.* funga viatu kwa nyuzi; pamba nguo kwa lasi. Kitambaa chenye urembo kinachoungwa kwenye kitambaa/nguo ili kuongeza mapambo


lace

**lack** /læk/ *n.* uhitaji; upungufu; ukosefu. *no ~ of,* tele. *for ~ of,* kwa ukosefu wa. *v.t.* hitaji; pungukiwa na; kosa. *be ~ing,* kosekana.

**ladder** /'lædə(r)/ *n.* ngazi; ufumukaji wa soksi. *v.i.* (kwa soksi) fumuka.

**laden** /'leɪdn/ *adj.* -enye mizigo; -enye shehena; tele; -liojaa. **lading** *n.* mizigo; shehena. *bill of lading,* orodha ya mizigo; idhini ya kutoa mizigo.

**ladle** /'leɪdl/ *n.* upawa. *v.t. ~ (out)* teka kwa upawa.


ladle

**lady** /'leɪdi/ *n.* bibi; bibiye; mke. **~like** *adj.* -a adabu; -a heshima. *Your, Her, ~ship,* mheshimiwa, mtukufu (mwanamke).

**lag** /læg/ *v.i* (**-gg-**) chelewa; kawia; enda polepole. *~ behind,* bakia nyuma. **~gard** *n.* mvivu.

**lager** /'lɑ:gə(r)/ *n.* bia isiyokuwa kali sana.

**lagoon** /lə'gu:n/ *n.* wangwa.

**lair** /leə(r)/ *n.* liya; malalo ya mnyama wa mwitu.

**lake** /leɪk/ *n.* ziwa.

**lamb** /læm/ *n.* mwana kondoo; nyama ya kondoo.


lamb

**lame** /leɪm/ *adj.* -lemavu; kiwete; kiguru; -siofaa, si -zuri. **~ly** *adv.* kilemavu. **~ness** *n.* ulemavu.

**lament** /lə'ment/ *n.* masikitiko; maombolezo; kilio. *v.t./i.* lilia; lia; omboleza; sikitika. **~able** *adj.* -a kusikitisha. **~ation** *n.* maombolezo; kilio.

**lamp** /læmp/ *n.* taa. **~-post** *n.* nguzo ya taa.

**lance** /lɑ:ns/ *n.* mkuki; fumo. *v.t.* tumbua; pasua (jipu, etc.). **~t** *n.* kisu kidogo cha kupasulia.

**land** /lænd/ *n.* nchi; ardhi; shamba;

konde; bara. *v.t./i.* shusha; teremsha. **2.** fikisha; leta; fika. **~ed** *adj.* -enye shamba. **~ing** *n.* kituo; gati; mahali pa kuteremkia; ushukaji; uteremkaji. **~lady** *n.* mwanamke mwenye nyumba ya kupangisha. **~lord** *n.* kabaila; mwenye kupangisha shamba au nyumba. **~mark** *n.* alama ya mpaka; alama (mlima, mnara, etc.) ya kuongoza njia; jambo kubwa. **~scape** *n.* mandhari; picha ya mandhari. **~slide** *n.* mporomoko wa ardhi.

**language** /'læŋgwɪdʒ/ *n.* lugha. *~ laboratory,* maabara ya lugha. *bad, strong ~,* matusi; lugha chafu. *technical ~,* lugha ya kitaalamu.

**languid** /'læŋgwɪd/ *adj.* chovu; tepetevu; -nyong'onyevu; -legevu.

**lantern** /'læntən/ *n.* kandili; fanusi. *~ jawed,* -enye taya ndefu nyembamba.

**lap**[1] /'læp/ *n.* paja; pajani. *live in the ~ of luxury,* ishi maisha ya anasa.

**lap**[2] /'læp/ *n.* mzunguko. *v.t.* zungusha; funga; kunja; pita; pitana; -nywa kwa ulimi kama paka. **~el** *n.* mkunjo wa koti kifuani.

**lapse** /læps/ *n.* **1.** kuteleza kwa ulimi; kosa dogo. *a ~ of memory,* kupitiwa. **2.** (kwa wakati) kupita. **3.** *(law)* kuisha (kwa sababu ya kutotumiwa). *v.i.* potoka; shuka hadhi; rudia dhambi; poteza haki kwa kutoidai.

**lard** /lɑ:d/ *n.* mafuta ya nguruwe. **larder** *n.* chumba au kabati la kuhifadhia chakula na nyama.

**large** /lɑ:dʒ/ *adj.* -kubwa; kuu; -ingi; -karimu; -ema. *at ~,* huru. *people at ~,* watu kwa jumla. *by and ~,* kwa kufikiri mambo yote. **~ly** *adv.* hasa; zaidi.

**larva** /'lɑ:və/ *n.* (**larvae**) mtoto wa mdudu; kiwavi; buu; kiluwiluwi; funza.

**larynx** /'lærɪŋks/ *n.* zoloto: mwanzo wa koromeo panapohusika na utoaji sauti.

**laser** /'leɪzə(r)/ *n.* chombo cha kukuza na kushadidia miale kuelekea upande mmoja. *~ beams,* mwangaza leza.

**lash** /læʃ/ *n.* mjeledi; kiboko; mchapo; kipigo cha kiboko; ukope. *v.t./i.* chapa; piga.

**lass lassie** /læs/ *n.* msichana mpenzi.

**last**[1] /lɑ:st/ *n./adj. / adv.* mwiso; -a mwisho; -hopita; mwishoni.

**last**[2] /lɑ:st/ *v.i.* endelea; dumu; tosha kwa; ishi. *enough food to ~ us three days,* chakula cha kutosha kwa siku tatu. **~ing** *adj.* -a aushi; -enye kudumu.



**latch**

**latch** /lɑ:tʃ/ *n.* kia; komea; kitasa; kikomeo. *v.t.* funga kwa kia au komeo.

**late** /leɪt/ *adj.* -liochelewa; liokawia. *be ~,* kawia; chelewa; taahari. **2.** marehemu; hayati. **3.** - liopita, -liokwisha; a kisasa; -a karibuni. *of ~,* hivi karibuni; majuzi. **~ly** *adv.* hivi karibuni; juzijuzi. **~st** *adj.* -a kisasa. *the ~ fashion,* mtindo wa kisasa. *at the ~,* kabla ya; siyo zaidi ya.

**latter** /'leɪtə(r)/ *adj.* -a karibuni; -liofuata; -a pili.

**latent** /'leɪtnt/ *adj.* -sioonekana. **~ heat,** joto fichu· kiasi cha joto kinachotakiwa kubadili duru kutoka hali moja hadi nyingine bila ya kuathiri halijoto yake.

**lateral** /'lætərəl/ *adj.* -a upande; -a mbavuni; -a kando. *~ root,* mzizi tanzu; tawi la mzizi mkuu.

**lath** /lɑ:θ, laθ/ *n.* uwasa; upapi.

**lathe** /leɪð/ *n.* kerezo.

**lather** /'lɑ:ðə, 'laðə/ . povu la sabuni; jasho.

**Latin** /'lætɪn/ *n.* Kirumi; Kilatini. *adj.* -a kirumi; -a kilatini.

**latitude** /'lætɪtju:d/ *n.* **1.** latitudo. **2.** nafasi; hiari; uhuru. **3.** maeneo.

**latitudinarian** *n. /adj.* mvumilivu; mwenye upana wa mawazo.

**latrine** /le'tri:n/ *n.* choo. *go to the ~,* enda msalani, chooni.

**lattice** /'lætɪs/ *n.* kimia: **1.** mpangilio mahsusi wa atomu katika muundo wa fuwele wa mango. **2.** vitu vimwatukaji na visovimwatukaji, hususani vitulizi, vilivyopangwa

katika tanuri la nyuklia kwa mpangilio mlinganifu wa kijiometri.

**laud** /lɔ:d/ *v.t.* sifu. **~able** *adj.* -a kustahili sifa. **~atory** *adj.* -a kusifu.

**laugh** /lɑ:f/ *n.* kicheko. *v.i./t.* cheka; chekelea; furahi. ~ *in one's sleeve*, cheka kwa siri. **~able** *adj.* -a kuchekesha. **~ing-stock** *n.* mpumbavu. **~ter** *n.* kicheko.

**launch** /lɔ:ntʃ/ *n.* ushuaji; mashua kubwa ya melini; motaboti. *v.t./i.* cheleza; shua; anzisha; anza; zindua; peleka chombo angani. ~ *out into*, anza.

**launder** /'lɔ:ndə(r)/ *n.* dobi. *v.t./i.* fua nguo. **laundry** *n.* nguo chafu; mahali pa kufulia ngua; udobi.

**lava** /'lɑ:və/ *n.* lava.

**lavatory** /'lævətri/ *n.* choo.

**law** /lɔ:/ *n.* sheria; kanuni. **~ of conservation of energy**, kaida ya hifadhi nishati: kaida inayoeleza kuwa nishati haiundwi wala haiharibiwi ila hubadilika katika maumbo mbalimbali. **~ of conservation of mass**, kaida ya hifadhi masi: kaida inayoeleza kuwa wakati wa utendanaji wa kemikali, atomu huji-panga upya lakini haziundiki wala haziharibiki. **~ of conservation of momentum**, kaida hifadhi momenta: kaida inayoeleza kuwa katika mgongano wa vitu, jumla ya momenta haibadiliki. **~ abiding** *adj.* -tiifu. **~court** *n.* korti; mahakama. **~ful** *adj.* -a haki, halali. **~less** *adj.* -siotii sheria. **~suit** *n.* daawa; madai; mashtaka. **~yer** *n.* mwanasheria; wakili.



**lawn mower**

**lawn** /lɔ:n/ *n.* bustani ya majani; bafta. **~mower** *n.* mashine ya kukata majani. **~ tennis** *n.* tenisi.

**lax** /læks/ *adj.* -zembe; si -angalifu; -legevu. **laxative** *n./adj.* haluli; dawa ya kuharisha; -a kuharisha; -a kuendesha. **~ity** *n.* uzembe; ulegevu.

**lay**[1] /leɪ/ *v.t./i.* (**laid**). **1.** taga. **2.** tandika; funika. **3.** weka; laza; tandaza. ~ *about one*, piga pande zote. ~ *sth. aside*, weka akiba; weka. ~ *aside old habits*, acha tabia za zamani. ~ *bare*, funua. ~ *sth. by*, weka. ~ *claim to*, dai kuwa kitu fulani ni chako. ~ *down one's life*, jitolea mhanga. ~ *down the law*, fundisha; amuru. *I can't ~ my hands on the book*, kitabu sikioni. ~ *hold of (on)*, shika. ~ *in*, weka akiba ya. ~ *sb. low*, shinda. ~ *on*, weka umeme au maji katika jengo. ~ *out*, tengeneza. ~ *oneself out to*, jiandaa; jitahidi. ~ *up*, weka akiba. *be laid up*, -wa kitandani kwa ugonjwa. **~out** *n.* taratibu; matengenezo. **~er** *n.* safu; tabaka; kuku wa mayai.

**lay**[2] /leɪ/ *adj.* -a kawaida; si -eledi. **~man** *n.* mtu wa kawaida; asiyekuwa mtaalamu.

**laze** /leɪz/ *v.i.* -wa -vivu; jikalia kivivu. **lazily** *adv.* kivivu. *adv.* **laziness** *n.* uvivu. **lazy** *adj.* -vivu.

**leaching** *n.* uchujuaji: kuosha na kuondoa kijenzi kimumunyaji katika mchanganyiko.

**lead**[1] /li:d/ *n.* risasi; chubwi; timazi. **~-pencil** *n.* penseli. **~-acid cell** *n.* seli ya asidi risasi: aina ya kilimbikizi ambacho ndani yake mna kathodi za sifongo ya risasi na anodi za plumbi dioksaidi. **~en** *adj.* -a risasi; -zito; -a rangi ya risasi. ~ *clouds*, mawingu ya mvua.

**lead**[2] /lɛd/ *n.* uongozi; usimamizi; mwongozo. *v.t./i.* tangulia; ongoza; simamia. ~ *a life*, ishi. ~ *sb. a dog's life*, ishisha maisha ya dhiki. ~ *to*, enda; elekea. ~ *sb. to think*, pelekea kufikiri. *have a ~ of five metres*, -wa mbele kwa mita tano. *take the ~ in a play*, -wa mkuu katika igizo. **~er** *n.* kiongozi; mkuu; msimamizi. **~ership** *n.* uongozi. **~ing** *adj.* -kuu; -a kwanza. ~ *article*, maoni ya mhariri. ~ *question*, swali linalodokeza jibu.

**leaf** /li:f/ *n.* (**leaves**) jani; karatasi. *(fig.) turn over a new ~*, anza mwenendo mpya. ~ *of a table*, ubao uwezao kufanya meza iwe ndogo zaidi. **~let** *n.* jani changa; ukurasa wenye matangazo. **~y** *adj.* -enye majani mengi.

**leak** /li:k/ *n.* ufa; tundu; uvujaji. *v.i.* vuja. *(fig.)* kujulikana; fichuka. **~age** *n.* uvujaji; ufichukaji. **~y** *adj.* -enye kuvuja.

**lean**[1] /li:n/ *n.* mnofu. *adj.* -embamba; -liokonda; hafifu. *~ harvests,* mavuno hafifu. **~ness** *n.* wembamba.

**lean**[2] /li:n/ *v.i./t.* (**leaned**, **leant**) inama; enda upande; lala upande; elekea; inamia. *~ upon, (fig.)* egemea; tegemea. **~ing** *n.* mwelekeo; upendeleo. **~-to** *n.* upenu.

**leap** /li:p/ *n./v.i./t.* (**leapt**, **leaped**) mruko; nyunju; chupa; ruka. *by ~s and bounds,* upesi sana.

**learn** /lɜ:n/ v.t./i. (**learnt**, **learned**) jifunza; arifiwa; pata habari. ~ed adj. -enye elimu; msomi. **~ing** n. elimu; hekima; usomi.

**lease** /li:s/ *n.* hati ya kukodisha; mkataba wa kukodisha. *a new ~ of life,* nguvu mpya. *v.t.* panga; kodisha; pangisha; kodi. **~hold** *n./adj.* mali iliyokodishwa; -a kukodi; -a kupanga. **lessee** *n.* mwenye kukodi. **lessor** *n.* mwenye kukodisha.

**least** /li:st/ *adj.* -dogo kuliko -ote. **~ common multiple**, kigawe kidogo cha shirika. **~ common denominator**, kigawe kidogo cha asili. *adv.* kidogo; hata kidogo. *at ~,* angalau; alau; walau.

**leather** /'leðə(r)/ *n.* ngozi iliyotengenezwa iwe laini na ili isioze.

**leave** /li:v/ *n.* ruhusa; idhini; likizo; livu. *v.t./i.* (**left**) toka; ondoka; acha; baki; bakisha; achia; -pa; kabidhi; pita; rithisha. *~ go (of),* achilia. *~ off,* isha; acha; koma. *~ out,* acha; ruka; totia. *be left,* baki; salia; achwa. **leavings** *n.* mabaki; makombo. *take ~,* aga; agana na. *take ~ of one's senses,* jitia hamnazo; pata wazimu.

**leaven** /'lɛv(ə)n/ *n.* chachu; hamira. *v.t.* chacha; chachua; umua kwa hamira.

**lecture** /'lektʃə(r)/ *n./v.i./t.* mhadhara; hotuba; hotubia; kemea; onya. **~r** *n.* mhadhiri. **~ship** *n.* uhadhiri.

**ledge** /ledʒ/ *n.* shubaka; mwamba chini ya maji.

**ledger** /'ledʒə(r)/ *n.* leja: daftari kubwa ya hesabu ya matumizi.

**lee** /li:/ *n.* mahali pasipoelekea upepo; upande wa demani. **~way** *n.* mwendo wa chombo kikichukuliwa upande wa demani; uhuru wa kuwa na mawazo tofauti. *(fig.) make up ~way,* fidia muda.

**leek** /li:k/ *n.* liki: aina ya kitunguu kidogo.

**left** /left/ *n./adj./adv.* upande wa kushoto; -a kushoto; kushoto.

**leg** /leg/ *n.* mguu; tendegu. *give sb. a ~ up,* saidia mtu. *pull sb. s ~,* fanyia mzaha; dhihaki. *not to have a ~ to stand on,* shindwa kabisa katika kesi. *on its last ~s,* -wa karibu kuisha.

**legal** /'li:gl/ *adj.* -a kisheria; halali; -a haki. *~ tender,* fedha halali kwa malipo. **~ity** *n.* uhalali; haki. **~ize** *v.t.* halalisha.

**legend** /'ledʒənd/ *n.* ngano; hekaya; maandishi katika sarafu, medali au ramani. **~ary** *adj.* -a hadithi za kale.

**legible** /'ledʒəbl/ *adj.* -a kusomeka; dhahiri. **legibility** *n.* usomekaji. **legibly** *adv.* kwa kusomeka.

**legislate** /'lɛdʒɪsleɪt/ *v.* tunga sheria. **legislation** *n.* utungaji sheria; sheria zilizotungwa. **legislative** *adj.* -a kutunga sheria. **legislator** *n.* mbunge; mwakilishi. **legislature** *n.* bunge; baraza la wawakilishi; baraza la kutunga sheria.

**legitimate** /lɪ'dʒɪtɪmət/ *adj.* halali; -a haki; -a sheria; -a halali; halisi. **legitimacy** *n.* uhalali; haki.

**legume** /'lɛgju:m/ *n.* jamiikunde: mimea jamii ya kunde.

**leguminous** /lɪ'gju:mɪnəs/ *adj.* -a jamii ya kunde.

**leisure** /'lɛʒə/ *n.* wasaa; wakati wa mapumziko; nafasi. **~d** *adj.* -enye wasaa **~ly** *adv.* taratibu; polepole.

**lemon** /'lemən/ *n.* limau. *~ tree,* mlimau. **~-ade** /ˌləmə'neɪd/ *n.* juisi au maji ya limau.

**lemur** /'li:mə/ *n.* komba wa bukini.

**lend** /lend/ *v.t.* (**lent**) azima; kopesha; karidhi; toa; -pa. *~ a hand,* saidia. *it ~s itself to,* yafaa kwa.

**length** /lɛŋθ, lɛŋkθ/ *n.* urefu; kipande cha kitu kinachotosha kwa kazi fulani. *at ~*, mwishowe; hatimaye; kwa undani; *at full ~*, kwa urefu wote; kwa kunyooka. *keep sb. at arm's ~*, kataa urafiki na; tenga; sukumia mbali. *go to all ~s*, *(any ~s)*, fanya kila linalowezekana. **~en** *v.t./i.* refusha; refuka. **~wise, ~ways** *adv.* kwa urefu. **~y** *adj.* (kwa maneno, maandiko) - refu mno.

**lens** /lenz/ *n.* lenzi.

**lent** /lent/ *n.* kwaresima.

**leopard** /'lepəd/ *n.* chui. **~ess** *n.* chui jike.

**leper** /'lepə(r)/ *n.* mkoma. **leprosy** *n.* ukoma. **leprous** *adj.* -enye ukoma.

**less** /les/ *adj.* -dogo zaidi. *adv.* kidogo. *prep.* kasoro. *$10 ~ $3 for taxes*, dola 10 kasoro dola 3 za kodi. **~en** *v.t./i.* punguza; punguka **~er** *adj* -dogo zaidi.

**lesson** /'lesn/ *n.* somo; sura; funzo; onyo. *Let that be a ~ to you*, naliwe funzo kwako.

**let** /let/ *v.t./i.* ruhusu; achilia; pangisha; kodisha. *~ sb. do sth.*, ruhusu mtu afanye. *~ fire out*, acha moto uzimike. *~ sth. down*, shusha; angusha. *~ oneself (sb.) in for*, jiingiza bila kujua. *~ sb. into a secret*, funulia mtu siri. *~ off*, piga; fyatua; samehe. *~ oneself go*, acha; achilia; achia huru; fungulia. kujizuia. *~'s start at once!* tuanze mara moja! *~ every man do his duty*, acha kila mtu afanye wajibu wake.

**lethal** /'li:θl/ *adj.* -a kuua.

**letter** /'letə(r)/ *n.* herufi; barua; waraka; elimu; fasihi. *keep the ~ of the law (an agreement)*, fuata sheria (mkataba). *a man of ~s*, msomi; mwandishi.

**lettuce** /'letɪs/ *n.* saladi.

**leucocyte** /'lu:kə(ʊ)sʌɪt/ *n.* lukosaiti: selidamu nyeupe.

**levee** /'lɛvi, 'lɛveɪ/ *n.* baraza iliyojengeka kimaumbile pembezoni mwa mto; ukuta uliojengwa kuzuia mafuriko; lambo.

**level** /'levl/ *n.* usawa; kiwango; pimamaji. *on a ~ with*, sawa na. *adj.* sawa. *a ~ crossing*, njia panda ya reli na barabara; tambuka reli. *have a ~ head, be ~ headed*, -wa mtulivu. *do one's ~ best*, fanya vizuri uwezavyo. *a ~ race*. nguvu sawa. *v.t.* (**-ll-**) sawazisha; fanya sawa; bomoa; elekeza; lenga. *~ up (down)*, linganisha.

**lever** /'li:və/ *n.* wenzo. **~-age** *n.* nguvu za wenzo.

**levy** /'lɛvi/ *n.* ada; kodi. *v.t.* toza; changisha. *~ war (upon) against*, anzisha vita.

**liable** /'laɪbl/ *adj.* -a kupaswa; -a kuwajibika kisheria; -a kustahili. **liability** *n.* deni; mwelekeo; madaraka. *unlimited liability*, madaraka yasiyo mpaka.

**liaison** /li'eɪzn/ *n.* kiungo; ushirikiano; uhusiano. *~ officer*, ofisa ushirikiano; ofisa mahusiano.

**liar** /'laɪə(r)/ *n.* mwongo.

**libel** /'laɪbl/ *n.* maandishi ya kashfa; kashfa. *v.t.* (**-ll-**) kashifu kimaandishi. **~lous** *adj.* -a kukashifu; -a kusingizia.

**liberal** /'lɪbərəl/ *adj.* -paji; -karimu; -ema; enye mawazo mapana; -a kupanua mawazo. **~-ity** *n.* upaji; wema; ukarimu; upana wa mawazo.

**liberate** /'lɪbəreɪt/ *v.t.* komboa; fanya huru. **liberty** *n.* uhuru. *take liberties with*, fanya yasiyofaa.

**library** /'laɪbreərɪən; 'laɪbri/ *n.* maktaba. **librarian** *n.* mkutubi.

**licence**[1] /'laɪsns/ *n.* leseni; ruhusa; hati. *~ to drive a car*, leseni ya kuendesha gari.

**license**[2] /'laɪsns/ *v.t.* pa leseni. *shops licensed to sell linen*, maduka yenye leseni ya kuuza vitambaa. *licensed premises*, mahali paliporuhusiwa kuuza (ulevi).

**lichen** /'lʌɪk(ə)n/ *n.* kuvumwani: mimea ya jamii ya kuvu na mwani.

**lick** /lɪk/ *n.* urambaji; mahali mifugo wanaporamba magadi. *v.t./i.* ramba; gusagusa. *(colloq.)* shinda; piga sana. **~ing** *n.* *(colloq.)* kupiga; kupigwa, kushinda; kushindwa.


lid

**lid** /lɪd/ *n.* kifuniko; ukope (wa jicho).

**lie**[1] /laɪ/ *n./v.i.* uwongo; sema uwongo.

**lie**[2] /laɪ/ *n.* hali. *the ~ of the land,* hali ya nchi ilivyo. *v.i.* (**lay lain**) lala; jinyoosha; -wa juu ya; -wa; -wa katika hali fulani; -wa mahali; kaa; baki; enea; zagaa; tanda. *The mistake ~s at your door,* ni kosa lako. *The trouble ~s in the lack of goods,* tatizo liko katika ukosefu wa bidhaa. *~ down under,* vumilia. *~ in,* kawia kuamka; -wa katika uchungu. *~ low, (colloq.)* kaa kimya. *~ up,* lala kwa ugonjwa. *n. (of the land)* hali ya nchi; jinsi mambo yalivyo.

**lieutenant** /lɛf'tɛnənt/ *n.* luteni; naibu. **~-colonel** luteni kanali.

**life** /laɪf/ *n.* uhai; viumbe hai; maisha; uzima; starehe; uhusiano; uchangamfu; kipindi cha maisha. **~belt** *n.* ukanda wa kujiokolea. **~cycle** *n.* duru ya maisha: hatua anazopita kiumbe toka anapoanza kuumbika hadi anapozaliwa. **~less** *adj.* -fu; -siovutia.


life buoy

**lift** /lɪft/ *n.* lifti; uinuaji; msaada. *v.t./i.* inua; pandisha; kweza; nyanyua; tweka; ruka; ondoka; panda; paa; iba; ondoa. *~ up one's voice,* paza sauti. *give sb. a ~,* -pa mtu lifti; saidia mtu.

**ligament** /'lɪgəm(ə)nt/ *n.* nyugwa; mkano: tishu ambayo huunganisha viungo mbalimbali vya mwili.

**light** /laɪt/ *n.* nuru; weupe; mwanga; taa; uchangamfu; ufafanuzi; mtazamo; uwezo; kipaji; mtu mashuhuri; uangavu. *come to ~, be brought to ~,* bainika. *strike a ~,* washa kiberiti. *adj.* -enye nuru; mwangaza; -eupe; -epesi; -siokoza. *v.t./i.* (**lit**) washa; waka; angaza; mulika; ongoza. *~ dependent resistor (LDR),* kikinzanishi tegemezi mwanga: kifaa cha elektroniki kilicho na ukinzani mdogo katika mwangaza kuliko katika giza. **~-emitting diode** *(LED),* diodi mwanga: kifaa cha elektroniki kilicho na ukinzani mkubwa na hutoa mwanga badala ya joto. **~ energy,** nishati mwanga: nishati ya sumakuumeme iliyomo katika mwanga. *~ year,* mwaka wa nuru: umbali wa masafa unao-safiriwa na nuru kwa mwaka mmoja. **~en** *v.t./i.* angaza; toa miale ya nuru; fanya -epesi; rahisisha. **~er** *n.* tishali; kiberiti cha gesi. **~-fingered** *adj.* -epesi kutumia vidole; stadi katika kuiba **~-hearted** *adj.* -kunjufu; -changamfu. **~house** *n.* mnara wa kuongozea vyombo vya baharini. **~ning** *n.* umweso; radi. *~ travel,* safiri bila mizigo mingi.


light house

**lignite** /'lɪgnʌɪt/ *n.* ligniti: kisukuku chenye rangi ya hudhurungi nyeusi kinachofanana na mkaa wa mawe.

**like**[1] /laɪk/ *adj.* sawa; -a kufanana. *nothing ~ as good,* -siofanana hata kidogo kwa uzuri. *'adv. I don't feel ~ working today,* sijisikii kufanya kazi leo. *conj.* sawa na; mfano wa; kama; kama vile; kama kwamba. **~ly** *adj.* -a kuelekea; -a kutaka kuwa. **~lihood** *n.* uwezekano; welekeo. *There is a ~ lihood,* yamkini; labda. **~n** *v.t.* fananisha; linganisha. **~ness** *n.* mfanano; mshabaha. **~wise** *adv.* kadhalika; vilevile.

**like**[2] /laɪk/ *v.t.* penda; taka; pendelea. *I didn't ~ to trouble him,* sikutaka kumsumbua. *They would ~ to come,* wangependa kuja. **likable (likeable)** *adj.* -a kupendeka. **liking** *n.* mapenzi; upendeleo; matakwa. *have a liking for,* penda. *to one's liking,* kama apendavyo.

**lily** /'lɪli/ *n.* yungiyungi. **~-livered,** oga. **~-white,** eupe pepe; isiyo na makosa; safi.

**limb** /lɪm/ *n.* kiungo; tawi.

**lime**[1] /laɪm/ *n.* chokaa. **~-kiln** *n.* tanuri. **~light** *n.* taa yenye nuru kali. *He is fond of the ~light,* apenda

kujionyesha. **~stone** *n.* chokaa-mawe: kabonati ya kalisi ya kiasili. **~ water** *n.* majichokaa: mmumunyo wa hidroksidi ya kalisi katika maji. **~water test**, jaribio la majichokaa: dioksidi kaboni inapopitishwa kwenye majichokaa, majichokaa hayo hugeuka kuwa kama maziwa.

**lime**[2] /laɪm/ *n.* ndimu. *~ tree*, mdimu.

**limit** /'lɪmɪt/ *n.* mpaka; upeo; kikomo; kiasi. *v.t.* wekea mpaka; zuia. **~ed** *adj.* -enye mpaka; -pungufu; -dogo; finyu. **~less** *adj.* bila kikomo. **~ation** *n.* mpaka; upungufu; kikomo; kizuizi.

**limp**[1] /lɪmp/ *adj.* teketeke; -legevu; nyong'onyevu.

**limp**[2] /lɪmp/ *v.i.* chechemea. **~ingly** *adv.* kwa kuchechemea.

**line** /laɪn/ *n.* mstari; safu; foleni; uzi; kamba; waya; kunyazi; kontua; mpaka; shirika la usafiri; mwelekeo; ukoo; mstari wa maneno; kazi. *fishing ~*, mshipi. *telephone ~s*, nyuzi za simu. *Send me a ~ to say you have arrived*, nitumie habari ya kunifahamisha ya kuwa umewasili. *hard ~s!* pole!; bahati mbaya. *v.t.i.* piga mstari; panga safu. *roads ~d with trees*, barabara zenye safu za miti. *~ up soldiers*, panga askari kwa safu. **~age** *n.* ufungu; shajara. **~al** *adj.* -a nasaba. **~ar** *adj.* -a mstari; -a mistari. **~ combination**, mtanga-mano mstari. **~ equation**, mlinganyo mstari. **~ transformation**, mbadiliko mstari. **~r** *n.* meli; ndege ya kampuni. **~sman** *n.* msaidizi wa mwamuzi; fundi wa umeme.

**linen** /'lɪnɪn/ *n.* kitani, nguo ya kitani, hasa shati na nguo za meza na kitanda. **~-draper** *n.* muuza nguo za kitani. *wash one's dirty ~ in public*, toa siri za nyumba ya fulani hadharani.

**linger** /'lɪŋgə(r)/ *v.i.* kawia; kaa karibu; zengea.

**linguist** /'lɪŋgwɪst/ *n.* mtu ajuaye lugha nyingi; mwanaisimu. **~ic** *adj.* -a isimu; -a lugha. **~ics** *n.* isimu: sayansi ya lugha.

**liniment** /'lɪnɪm(ə)nt/ *n.* fututa; dawa ya mafuta ya kusugua au kuchukua.

**link** /lɪŋk/ *n.* pete; kiungo; kifungo. *v.t./i.* ungana na; unga.

**lion** /'laɪən/ *n.* simba dume. *the ~'s share*, fungu kubwa. **~ess** *n.* simba jike. **~-hearted,** shujaa; mtu mashuhuri. **~ize** *v.t.* tukuza.

**lipase** /'lɪpeɪz, 'lʌɪp-/ *n.* lipasi: aina ya kimeng'enya chenye uwezo wa kumeng'enya kikemikali chakula cha asili ya mafuta na kukigeuza kuwa gliseroli na asidi ya mafuta.

**lipid** *n.* kundi la misombo ya kaboni ambalo ni esta za asidi shahamu na ambayo haimumunyiki katika maji lakini humumunyika katika vimumunyishaji vya kaboni.

**liquid** /'lɪkwɪd/ *n.* kioevu; maji; kimiminiko. *adj.* -oevu; -a majimaji; -eupe; -angavu; -enye kubadilika-badilika; laini; -ororo; -epesi kusarifika. **liquefaction** *n.* kugeuka maji; kuyeyuka. **liquefy** *v.t./i.* yeyusha; yeyuka.

**liquidate** /'lɪkwɪdeɪt/ *v.t.* lipa deni; filisi; filisika.

**liquor** /'lɪkə(r)/ *n.* pombe; ulevi.

**list**[1] /lɪst/ *n.* orodha; hesabu. *v.t.* orodhesha.

**list**[2] /lɪst/ *n.* kulala ubavu. *v.i.* (meli, merikebu) lala ubavu.

**listen** /'lɪsn/ *v.i.* sikiliza; sikia. *~ in*, sikiliza simu ya upepo. **~er** *n.* msikilizaji.

**literacy** /'lɪtərəsi/ *n.* kujua kuandika na kusoma. **literal** *adj.* -a herufi; halisi; -a maneno yenyewe; si -bunifu. *a literal copy*, nakala halisi. *literal translation*, tafsiri sisisi. **~ly** *adv.* neno kwa neno.

**literary** /'lɪtərəri/ *adj.* -a fasihi; -a maandishi; -a waandishi.

**literate** /'lɪtərət/ *n./adj.* -enye kujua kuandika na kusoma; -somi; mtu ajuaye kusoma na kuandika.

**literature** /'lɪtrətʃə(r)/ *n.* fasihi; maandiko mbalimbali ya nchi; maelezo.

**lithium** /'lɪθɪəm/ *n.* lithi, lithiamu:

elementi metali laini na nyepesi kuliko metali zote.

**lithosphere** /'lɪθəsfɪə/ *n.* tabaka-mwamba: sehemu mango ya dunia ya nje kabisa ambayo hufunika sehemu moto zaidi za ndani.

**litmus** /'lɪtməs/ *n.* litmasi: dutu mumunyikaji ya rangi ya zambarau ambayo hugeuka nyekundu ikikutana na asidi au buluu ikikutana na alkali, hutumika kama kiashirio.

**litre** /'li:tə(r)/ *n.* lita.

**litter** /'lɪtə(r)/ *n.* machela; takataka; fujo; (kwa wanyama) majani ya kulalia; watoto wa mnyama wa fuko moja. *v.t./i.* chafua; fuja; tia takataka; (kwa wanyama) zaa.

**little** /'lɪtl/ *n.* kidogo. *adj.* -dogo; haba; chache; fupi. *the ~ finger,* kidole cha ncha. *after (for) a ~,* baadaye kidogo. *adv.* kidogo. *He's a ~ better today,* leo hajambo kidogo.

**littoral** /'lɪt(ə)r(ə)l/ *n./adj.* pwani; -a pwani.

**live** /lɪv/ *v.i./t.* -wa na uzima; ishi; wa hai; dumu; kaa. *~ on,* ishi kwa; -la; endelea kuishi. *What does he ~ on?* ana kazi gani, hula nini ? *~ sth. down,* sahaulisha. *~ up to,* fikia matarajio. *adj.* -enye uhai; hai; motomoto; -a kisasa; -enye kurushwa hewani palepale naposemwa bila kurekodiwa kabla. *~ wire,* waya wenye umeme. **~lihood** *n.* kazi; riziki. *the ~long day,* mchana kutwa. **~ly** *adj.* -cheshi; - kunjufu; -epesi; changamfu. **~n** *v.t./i.* sisimua; changamsha; changamka. **~stock** *n.* mifugo.

**living** /'lɪvɪŋ/ *n.* riziki. *adj.* hai; -zima; hasa; halisi; enye kusisimua. *make a living as a farmer,* ishi kwa kutegemea kilimo. *plain living,* maisha ya kawaida. *high living,* maisha ya anasa. *a living wage,* mshahara wa kukimu mahitaji.

**liver** /'lɪvə(r)/ *n.* ini. **~wort** *n.* livawoti: jamii ya mimea midogomidogo inayomea katika sehemu zenye unyevu na ina majani kama maini.

**livid** /'lɪvɪd/ *adj.* -a rangi ya risasi; -a kijivu; -a samawati; -liokasirika sana. *~ with anger,* lioiva kwa hasira.


**lizard**

**lizard** /'lɪzəd/ *n.* mjusi; guruguru. *monitor ~,* kenge.

**load** /'ləʊd/ *n.* mzigo; shehena; kiwango cha kazi. *(fig.) ~ of sorrow,* huzuni nyingi. *v.t./i.* pakia; sheheni; tia risasi.

**loaf** /ləʊf/ *n.* (**loaves**). mkate; boflo. *~ sugar,* sukari ya kidonge.

**loan** /ləʊn/ *n.* karadha; mkopo; ukopeshaji. *v.t.* karidhi; kopesha.

**loath, loth** /ləʊθ/ *adj.* *be ~,* totaka. *nothing ~,* -enye kutaka; kwa hiari.

**loathe** /ləʊð/ *v.t.* chukia kabisa. **loathing** *n.* uchukivu; karaha. **loathsome** *adj.* a kuchukiza mno.

**lobby** /'lɒbi/ *n.* sebule; ukumbi; ushinikizaji.

**lobe** /ləʊb/ *n.* ndewe.


**lobster**

**lobster** /'lɒbstə(r)/ *n.* kamba

**local** /'ləʊkl/ *adj.* -a mahali maalumu; -a sehemu. **~ity** *n.* mahali; mtaa; ujirani; janibu. **~ize** *v.t.* weka (zuilia) mahali maalumu; fanya ya mahali maalumu.

**locate** /ləʊ'keɪt/ *v.t.* onyesha mahali pa; tambua. *be ~d,* wekwa mahali.

**lock**[1] /lɒk/ *n.* shungi la nywele.

**lock**[2] /lɒk/ *n.* kufuli; kitasa; komeo; kifungio; mtambo; ukwamaji; milango. *v.t./i.* komea; funga kwa kufuli; shikamanisha. **~er** *n.* kabati; kasha lenye kufungwa kwa kufuli. **~jaw** *n.* ugonjwa wa pepopunda. **~out** *n.* kufungia nje. **~smith** *n.* mtengeneza kufuli.

**locomotion** /ˌləʊkə'məʊʃn/ *n.* mwendo; uwezo wa kwenda. **locomotive** *n.* garimoshi. *adj.* -enye uwezo wa kwenda.

**locus** /'ləʊkəs/ *n.* **1.** lokasi: nafasi au nukta inayoonyesha nafasi ya kitu fulani. **2.** nafasi maalumu ya jeni fulani katika kromosomu.

**locust** /'ləʊkəst/ *n.* nzige.

**lodge** /lɒdʒ/ *n.* nyumba ndogo; nyumba ya chama; klabu. *v.t./i.*

pangisha; panga; ingia na kukwama; weka; tia. ~ *a complaint*, shtaki. **~r** *n.* mpangaji. **lodging** *n.* nyumba ya kupanga.

**loft** /lɒft/ *n.* ghorofa ya juu kabisa; darini. **lofty** *adj.* -a juu sana; -refu; bora, -ema; -a kiburi; -a fahari.

**log**[1] /lɒg/ *n.* gogo la mti. **~ging** *n.* ukataji miti.

**log**[2] /lɒg/ *n.* kipimamwendo wa meli baharini. ~ *book*, batli: kitabu chenye habari zote za safari ya chombo.

**logarithm** /'lɒgərɪð(ə)m/ *n.* logi: nambakipeo ya namba ambayo namba msingi (kizio) haina budi kupandishwa kupata namba fulani (antilogi).

**logic** /'lɒdʒɪk/ *n.* tawi la falsafa lihusulo mantiki; mantiki. **~al** *adj.* -enye mantiki. *in ~ order*, -a kufuatana sawasawa. *It's not ~*, si -a mantiki.

**lone** /ləʊn/ *adj.* -a pekee; pweke. **~liness** *n.* upweke; ukiwa. **~ly** *adj.* bila rafiki; pweke; -a ukiwa. *feel ~*, jisikia mpweke.

**long**[1] /lɒŋ/ *n./adj.* kipindi kirefu; muda mrefu; -refu. *This work will take ~*, kazi hii itachukuwa muda mrefu. *a ~ face*, uso wa huzuni. *in the ~ run*, mwishowe; hatimaye. *all day ~*, mchana kutwa. *before ~*, baadaye kidogo. *the ~ and short of it*, kijumla. *adv. as (so) ~ as*, mradi; ilimradi. ~ *drawn out*, liorefushwa bila sababu. **~evity** /lɒn'dʒevəti/ *n.* maisha marefu. **~-winded** *adj.* -a maneno mengi; domokaya.

**long**[2] /lɒŋ/ *v.i.* tamani sana. **~ing** *n.* hamu; shauku.

**longitude** /'lɒn(d)ʒɪ'tju:d 'lɒŋgɪ-/ *n.* longitudo. **longitudinal wave**. wimbi mtambaa: wimbi lenye chembechembe za midia zinazo tetemeka mbele na nyuma kufuata pitio ambamo wimbi husafiria kwenye njia yake.

**look** /lʊk/ *n.* mtazamo; utazamaji; sura. *v.i./t.* tazama; angalia; onekana; elekea; tafuta. ~ *after*, tunza. ~ *down on*, dharau. ~ *for*, tafuta. ~ *forward to*, ngojea kwa hamu. ~ *in (on)*, zuru; tembelea. ~ *into*, chungulia; chunguza; peleleza. ~ *on*, tazama; -wa mtazamaji. ~ *(up) on*, *sb. or sth. as*, ona kuwa. ~ *out*, jihadhari. ~ *sth. over*, kagua sehemu. ~ *sth. through*, kagua kitu kwa makini. ~ *to*, tazamia. ~ *up*, angalia juu; ongezeka ufanisi. ~ *sth. up*, tafuta. ~ *up to*, heshimu. ~ *like*, elekea. *it ~s like rain*, inaelekea kutanyesha mvua. ~ *alive (sharp)*, changamka. *good ~s*, sura nzuri. **~er-on** *n.* mtazamaji. **~-in** *n.* fursa; nafasi. **~ing-glass** *n.* kioo. **~out** *n.* mahali pa kupelelezea; mlinzi; mpelelezi; mustakbala. *It's poor ~-out for these people*, mustakbala wa watu hawa ni mbaya. *That's your ~ out*, ni juu yako.

**loom**[1] /lu:m/ *n.* kitanda cha mfumi; mtande.

**loom**[2] /lu:m/ *v.i.* onekana kama -kubwa kwa kutisha; tisha kwa kuonekana kama kubwa.


**loop**

**loop** /lu:p/ *n.* kitanzi; shwara. *v.t./i.* piga kitanzi. ~ *sth. up (back)*, funga kufanya kitanzi. **~ hole** *n.* kitundu cha kupenyezea bunduki katika ukuta; *(fig.)* njia ya kuokoka; mwanya.

**loose** /lu:s/ *adj.* -liofunguka; -lioachwa huru; lioachiwa; -siokazwa; -a kulegalega; -potovu; -baya. *be at a ~ end*, -wa bila ya shughuli. **~n** *v.t.* fungua; legeza.

**loot** /lu:t/ *n.* nyara; mateka; uporaji; utekaji nyara. *v.t./i.* teka; teka nyara; pora.

**lord** /lɔ:d/ *n.* mtawala mkuu; Mwenyezi Mungu; lodi; maulana; bwana; mwinyi; mheshimiwa. *the ~ mayor*, mstahiwa meya. *v.i. ~ it over*, tawala kimwinyi. **~ly** *adj.* -a heshima; -a kimwinyi; -a fahari; -enye kiburi. **~ship** *n.* utukufu; mamlaka ya umwinyi. *Your ~*, mtukufu.

**lorry** /'lɒri/ *n.* lori.

**lose** /lu:z/ *v.t./i.* (**lost**) poteza; potewa na; potea; -fa; chelewa; kosa kuona; kosesha; shindwa; pata hasara. ~ *one's way*, ~ *oneself*,

*be lost,* potea njia; angamia. ~ *track of,* -tojua habari ya mtu au jambo. *He lost the ship,* aliikosa meli. ~ *heart,* vunjika moyo, kata tamaa. ~ *a battle, a game, a match,* shindwa. ~ *one's temper,* kasirika. ~ *one's head,* fadhaika. ~ *face,* aibika; tahayari. ~ *no time in doing sth.,* fanya kitu mara moja. *be lost to all sense of shame,* tojali aibu kabisa. *be lost in wonder,* shangaa sana. *My watch ~s five minutes a day,* kila siku saa yangu inapoteza dakika tano.

**loss** /lɒs/ *n.* hasara; msiba; upoteaji; upotezaji. *be at a loss,* fadhaika.

**lot**[1] /lɒt/ *n.* -ote; idadi yote. *~s of people come,* watu wengi huja. *adv.* sana.

**lot**[2] /lɒt/ *n.* kura; bahati nasibu; ajali; bahati; jumla ya vitu viuzwavyo kwa pamoja mnadani. *to draw (cast) ~s,* piga kura. *a bad ~, (colloq.)* mtu mbaya. **~tery** *n.* bahati nasibu.

**lotion** /ˈləʊʃn/ *n.* losheni.

**loud** /laʊd/ *adj.* -enye sauti kubwa; -a makelele; -a mvuto; -a kujitangaza. **~ly** *adv.* sana. **~-speaker** *n.* bomba; kipaza sauti.

**lounge** /laʊndʒ/ *n.* ukumbi; sebule. *v.i.* kaa kivivu; jikalia. **~suit** *n.* suti ya kiume. **~ chair** *n.* kiti cha kupumzikia.

**louse** /laʊs/ *n.* (**lice**) chawa; utitiri. **lousy** *adj.* -enye chawa; *(colloq.)* bovu; ovyo.

**love** /lʌv/ *n.* upendo; huba; mapenzi; mahaba. *be in ~ (with),* penda mwanamke au mwanamme. *make ~ to,* lala; jamiiana; fanya mapenzi; onyesha kupendana na. *v.t.* penda; furahia; chunuka; taka. **lovable** *adj.* a kupendeka. **~r** *n.* mchumba; mpenzi; shabiki. **~ly** /ˈlʌvli/ *adj.* -a kupendeza; -a kufurahisha; -zuri sana; -a kuburudisha. **~liness** *n.* uzuri. **loving** *adj.* -enye upendo.

**low** /ləʊ/ *adj.* a chini; fupi; -nyonge; dhaifu; -a kishenzi. *adv. be running ~,* pungua.

**loyal** /ˈlɔɪəl/ *adj.* -tiifu; -aminifu. **~ty** /ˈlɔɪəlti/ *n.* utii; uaminifu; uwajibikaji.

**lubricate** /ˈlu:brɪkeɪt/ *v.t.* lainisha; legeza kwa mafuta; rahisisha kufanya jambo. **lubricant** *n.* mafuta ya kulainisha. **lubrication** *n.* ulainishaji.

**luck** /lʌk/ *n.* bahati; sudi. *in ~,* -enye bahati nzuri. *out of ~,* -enye bahati mbaya. *for ~,* kwa kuleta heri. **~less** *adj.* -a bahati mbaya; -enye kisirani. **~y** *adj.* -a bahati njema; -a heri; -enye bahati. **~ily** *adv.* kwa bahati nzuri.

**ludicrous** /ˈlu:dɪkrəs/ *adj.* -a kuchekesha; -a mzaha; -puuzi; pumbavu.

**luggage** /ˈlʌgɪdʒ/ *n.* mizigo.

**lumber** /ˈlʌmbə(r)/ *n.* magogo; mbao; makorokoro. *v.i./t.* ~ *along (by, past)* -enda kwa mwendo mzito. ~ *up,* jaza makorokoro. **~man, ~jack** *n.* mkata miti; mpasua mbao. ~ **mill** *n.* kiwanda cha mbao.

**luminary** /ˈlu:mɪn(ə)ri/ *n.* jua; mwezi; nyota; kitu king'aacho angani; mtu mashuhuri kwa busara na akili. **luminescence** *n.* mng'aro; mwanga wa kutoka kwenye kitu kwa njia yoyote isiyokuwa ya kukweza halijoto yake.

**luminous** /ˈlu:mɪnəs/ *adj.* dhahiri; -a kung'aa. **luminosity** *n.* mng'aro; utoaji mwanga.

**lump** /lʌmp/ *n.* bonge; jumla; uvimbe. *a ~ sum,* malipo ya jumla. *v.i./t. ~ together,* jumuisha; tutika; changanya. *If you don't like it, you can ~ it,* ni lazima uvumilie upende usipende. **~ish** *adj.* nene na fupi; bongebonge. **~y** *adj.* -enye vibonge.

**lunar** /ˈlu:nə/ *adj.* -a mwezi. *a* **~ month,** kadiri ya siku 29 na nusu; mwezi mwandamo. **~ eclipse,** kupatwa kwa mwezi **~ module,** njia ya chombo kinachozunguka na kutua mwezini. **~ orbit,** uzungukaji mwezi.

**lunatic** /ˈlu:nətɪk/ *n.* mwenda-wazimu; kichaa. **lunacy** *n.* wazimu; kichaa.

**lunch** /lʌntʃ/ *n.* chakula cha



**lunar eclipse** kupatwa kwa mwezi

mchana. *v.i.* -la chakula cha mchana. **~eon** *n.* chakula cha mchana.
**lung** /lʌŋ/ *n.* pafu. ~ *fish*, kambaremamba.
**lurch** /lɜ:tʃ/ *n.* msepetuko. *v.i.* pepesuka; sepetuka; enda mrama; lala bavu. *live sb. in the* ~, acha katika shida.
**luxury** /'lʌkʃəri/ *n.* anasa. **luxurious** *adj.* -a anasa.
**lymph** /lɪmf/ *n.* limfu: kioevu kisicho na seli nyekundu na ambacho husafiri katika mishipa limfu. **~nodes** *n.* fundo limfu: kiogani kwenye mlimfu chenye tishu ya kilimfu. **~atic system** *n.* mfumo wa limfu: mpangilio wa neli ndogo sana zinazoitwa kapilari za limfu, huchukua giligili za tishu.
**lymphocite** *n.* limfosaiti: seli nyeupe ya damu inayoumbika kwenye tishu za limfu.

# Mm

**macaroni** /ˌmakə'rəʊni/ *n.* makaroni: aina ya tambi.
**mach** /mɑ:k, mak/ *n.* machi. ~ *number*, uwiano wa kasi ya mwendo wa ndege na kasi ya mwendo wa sauti.
**machine** /mə'ʃi:n/ *n.* mashine; mtambo; kikundi kinachoongoza chama cha siasa. **~ry** *n.* mashine kwa jumla; mfumo wa jambo; urasimu.
**mad** /mæd/ *adj.* enye wazimu; -enye kichaa; -liojaa jazba; -enye hasira. **~den** *v.t.* tia wazimu; kasirisha sana. **~cap** *n.* jasiri. **~ly** *adv.* kwa hasira nyingi; kiwazimu. **~ness** *n.* wazimu; kichaa; ujinga.
**madam** /'mædəm/ *n.* bibi; mama.
**madame** /mə'dɑ:m/ bibi (latumika kabla ya majina ya wanawake walioolewa).
**magazine** /ˌmægə'zi:n/ *n.* ghala; stoo; bohari ya silaha; chemba ya risasi katika bunduki; jarida.
**maggot** /'mægət/ *n.* buu; funza.
**magic** /'mædʒɪk/ *n.* uchawi; kiini macho; mazingaombwe; uramali. *adj.* -a uchawi; -enye uchawi. **~ian** *n.* mchawi.
**magistrate** /'madʒɪstrət, -streɪt/ *n.* hakimu; mwamuzi. *district* ~, hakimu wa wilaya. *resident* ~, hakimu mkazi. *the* ~, mahakimu. **magisterial** *adj.* -a hakimu; -enye amri; -enye mamlaka.
**magma** /'magmə/ *n.* magima: lahamu yenye mata mango na oevu; maunzi teketeke chini au ndani ya ganda la dunia ambako mwamba-moto huumbika.
**magnesium** /mag'ni:zɪəm/ *n.* magnesi: elementi metalia nyepesi ya rangi ya fedha ya mfululizo wa madini alkalini ambayo huungua moto mkali mweupe.
**magnet** /'mægnət/ *n.* sumaku, sumaku. **~ic** *adj.* -a sumaku. **~ compass**, dira: chombo cha sumaku cha kuonyesha uwelekeo wa kaskazini. **~ needle**, sindano ya dira. **~ field**, ugasumaku. **~ pole**, ncha sumaku. **~ tape**, ukandasumaku. **~ism** *n.* usumaku; nguvu ya sumaku; mvuto. **~ize** *v.t.* tia sumaku; vuta kama sumaku. **~o** *n.* magneto; mashine ya umeme. **~osphere** *n.* ugosumaku: ugasumaku ambao umeizunguka dunia na kuikinga na chembe chaji zitolewazo na jua.
**magnificent** /mæg'nɪfɪsnt/ *adj.* -zuri kabisa; -tukufu; adhimu. **magnificence** *n.* utukufu; adhama; fahari; uzuri.
**magnify** /'mægnɪfaɪ/ *v.t.* kuza; tia

chumvi; tukuza; sifu; adhimisha. **magnitude** *n.* ukubwa; cheo; ubora; ukuu.

**mahogany** /mə'hɒgəni/ *n.* mkangazi; mbambakofi.

**maid** /meɪd/ *n.* mwanamwali; mwanamwari; mwali; mwari; msichana; mtumishi wa kike. ~ *of honour,* mtumishi wa aila ya kiongozi wa nchi. **~en** *n.* msichana; mwari; binti. ~ *name,* jina kabla ya kuolewa. ~ *head,* kizinda.

**mail** /meɪl/ *n.* barua za posta; posta. ~ *bag,* mfuko wa barua za posta. ~ *box,* sanduku la posta. *v.t.* postia; peleka kwa posta. *~ing list,* orodha ya watu wanaopelekewa kitu kwa posta.

**main** /meɪn/ *n.* bomba kuu la maji; njia kuu ya umeme; bomba kuu la maji machafu. *adj.* -kubwa; -kuu. *have an eye on the ~ chance,* fikiria faida yako tu katika jambo. *a ~s set,* simu itumiayo umeme. *with might and ~,* kwa bidii kubwa. *in the ~,* kwa kiasi kikubwa; kwa jumla; aghlabu. **~land** *n.* bara. **~ly** *adv.* zaidi; hasa. **~stay** *n.* nguzo; tegemeo; *(fig.)* msaada.

**maintain** /meɪn'teɪn/ *v.t.* hifadhi; dumisha; endeleza; lisha; shikilia; kimu; gharimia; sisitiza; sema. **maintenance** *n.* kiamu; matengenezo.

**maize** /meɪz/ *n.* mahindi; ~ *plant,* muhindi.

**major** /'meɪdʒə(r)/ *n.* meja. ~ *general,* meja jenerali. *adj.* kubwa; -kuu; -enye maana zaidi. **~ity** *n.* wingi; zaidi ya nusu; umri wa utu uzima.

**make** /meɪk/ *n.* namna; aina; mtindo. *This computer is of a good ~,* kompyuta hii ni ya aina nzuri. *v.t./i.* (**made**) umba; fanya; tunga; tengeneza; sababisha; lazimisha; dhani; fikiria; kadiria; chukuana; pata; funga; shinda; fanikiwa; -wa sawa na; chagua; teua. ~ *cloth,* fuma nguo. ~ *a hole in sth.,* toboa. ~ *a noise,* fanya kelele. *made of wood,* -liotengenezwa kwa mbao. ~ *money,* pata pesa. ~ *tea,* pika chai. ~ *a bed,* tandika kitanda. ~ *fun (game, sport) of (sb.),*dhihaki; tania. ~ *light of (sth.),* dharau. ~ *the most of sth.,* tumia kitu vyema. ~ *sb. do sth.,* lazimisha mtu kufanya jambo. ~ *sb. happy,* furahisha mtu. ~ *the fire burn,* washa moto. *The cotton trade made Manchester,* kazi ya kutengeneza pamba iliuimarisha mji wa Manchester. ~ *port,* fika bandarini. *What do you ~ the time?* unadhani ni saa ngapi? ~ *for,* endea; elekea. ~ *off,* kimbia. ~ *out (a cheque, a bill, &c.)* andika; weza kuona; fahamu. ~ *sth. over (to sb.),* sihia mali kwa. ~ *up,* buni; tunga. ~ *up one's mind (to),* amua. ~ *believe,* jisingizia. **~shift** *n.* badala; kitu kitumikacho kwa sababu kitu halisi hakipatikani. **~-up** *n.* vipodozi. **making** *n.* utendaji; usitawi; uendeleaji. *be the making of,* sababisha kusitawi.

**mal-** /mæl/ *prefix* -baya; kijenzi cha maana ya kinyume.

**malaria** /mə'leəriə/ *n.* malaria.

**male** /meɪl/ *n.* dume. *adj.* dume; -a kiume.

**malleable** /'mɑlɪəb(ə)l/ *adj.* -a kufulika; *(fig.)* -elekevu; -epesi kuongozwa. **malleability** *n.* ufulikaji.


mallet

**mallet** /'mælɪt/ *n.* nyundo ya mti; rungu ya kuchezea polo.

**malnutrition** /ˌmælnju:'trɪʃn/ *n.* utapiamlo.

**malt** /mɔ:lt, mɒlt/ *n.* kimea cha pombe.

**maltreat** /ˌmæl'tri:t/ *v.t.* onea; dhulumu. **~ment** *n.* uonevu; dhuluma.

**mamma** /'mɑmə, mə'mɑ:/ *n.* neno la kitoto kwa mama.

**mammal** /'mæml/ *n.* mamalia: mnyama anayenyonyesha watoto wake. **~ia** *n.* chuchu: kichomozo kwenye titi, ambacho ni kiishio cha vichirizi kutoka kwenye titi hadi kwenye mfereji wa kutolea maziwa.

**mammary glands** *n.* matiti: tezi ambazo wakati fulani hutoa maziwa, hasa kwa wanyama majike

wenye watoto wachanga.


man

**man** /mæn/ *n.* (**men**) mtu; watu; binadamu; mwanamme; mume. *the ~ in the street*, mtu wa kawaida. *~ of the world*, mjuzi wa mambo ya ulimwengu. *~ of letters*, msomi. *v.t.* tia watu katika amali; pakia wanamaji; wekea ulinzi. **~ful** *adj.* hodari; shupavu. **~-handle** *v.t.* sukuma; vurumisha; sogeza kwa nguvu. **~hood** *n.* utuuzima; urijali; udume; ujanadume. **~kind** *n.* wanadamu. **~like** *adj.* -enye tabia za kiume; -a kiume. **~nish** *adj.* a kama mwanamme; -a kiume. **~slaughter** *n.* kuua mtu bila kukusudia.

**manacle** /'manək(ə)l/ *n.* pingu.

**manage** /'mænɪdʒ/ *v.t./i.* ongoza; simamia; endesha; tawala; weza; fanikiwa; tunza. *I can't ~ without help*, siwezi bila msaada. **~ment** *n.* usimamizi; uongozi. *Bankruptcy was caused by bad ~ment* kufilisika kulitokana na utawala mbaya. *the* **~ment**, uongozi; menejimenti; utawala. **~r** *n.* meneja. **~ress** *n.* meneja mwanamke.

**mandate** /'mandeɪt/ *n.* mamlaka; uwakili; agizo; hukumu; udhamini.

**mangenese** /'mæŋgəni:z/ *n.* manganizi: metali ya rangi ya kijivu na kechu.

**mange** /meɪn(d)ʒ/ *n.* ugonjwa wa upele wa wanyama. **mangy** *adj.* -enye upele huu; duni; liochakaa; dhaifu.

**manger** /'meɪndʒə(r)/ *n.* hori, chombo cha kulishia wanyama kama vile ng'ombe chenye umbo la mtumbwi.


mangrove

**mango** /'mæŋgəʊ/ *n.* (**-oes**) mwembe; embe

**mangrove** /'mæŋgrəʊv/ *n.* mkandaa; mkoko; msuti; msindi.

**mania** /'meɪniə/ *n.* wazimu; ushabiki mkubwa; shauku kubwa. **~c** *n.* mwenye wazimu.

**manifest** /'mænɪfest/ *adj.* dhahiri; wazi; bayana. *v.t.* onyesha; dhihirisha; jidhihirisha. *n.* orodha ya shehena melini. **~o** *n.* (**-os**) ilani.

**manifold** /'manɪfəʊld/ *adj.* -a namna nyingi; -a mara nyingi.

**manipulate** /mə'nɪpjʊleɪt/ *v.t.* endesha; tengeneza; fanya; tawala kwa ufundi. **manipulation** *n.* kufanya kwa ufundi.

**manner** /'mænə(r)/ *n.* jinsi; njia; namna; mwenendo; tabia; adabu. *He has no ~s*, hana adabu. *all ~ of*, kila namna ya. **ill-(well-) mannered** *adj.* -bila (-enye) adabu. **~ism** *n.* mtindo; upekee wa tabia. **~ly** *adj.* -enye adabu; -enye heshima.

**manoeuvre** /mə'nu:və/ *n.* manuva; werevu; hila; ujanja. *v.i./t.* fanya manuva; tumia werevu; shawishi.

**mansion** /'mænʃn/ *n.* nyumba.


mantis

**mantis** /'mantɪs/ *n.* vunjajungu.

**mantle** /'mæntl/ *n.* utando mzito wa tabaka la miamba yenye mango oevu ya wastani wa kati, takriban umbali wa kilomita 2900 chini ya ganda la dunia.

**manual** /'mænjuəl/ *n.* kitabu kinachotoa maelekezo ya namna ya kutumia kitu fulani kama vile mashine.

**manufacture** /ˌmænju'fæktʃə(r)/ *n.* utengenezaji; uzalishaji; vitu vilivyozalishwa kiwandani. *v.t.* tengeneza; zalisha; buni.

**manure** /mə'njʊə(r)/ *n.* mbolea; samadi. *v.t.* tia mbolea.

**many** /'meni/ *adj./pron.* -ingi; tele; maridhawa; kadha wa kadha. *be one too ~ for*, shinda kwa werevu. **~-sided** *adj.* -enye pande nyingi; *(fig.)* enye vipaji vya namna nyingi.

**map** /mæp/ *n.* ramani. *~ scale*, skeli. *v.t.* chora ramani; onyesha kwenye ramani. *~ out*, panga.

**mar** mɑ:(r)/ *v.t.* (**-rr-**) haribu; umbua; hasiri. *be ~red*, sawijika; umbuka; haribika.

**marathon** /'mærəθən/ *n.* marathoni; mbio za masafa marefu; *(fig.)* jaribio la ustahamilivu.

**maraud** /mə'rɔ:d/ *v.i.* nyang'anya; iba; teka nyara. **~er** *n.* mnyang'anyi; mwizi.

**marble** /mɑ:bl/ *n.* marumaru; gololi. *a ~ breast,* katili.

**March** /mɑ:tʃ/ *n.* Machi: mwezi wa tatu wa mwaka wa kizungu.

**march** /mɑ:tʃ/ *n.* mwendo wa kijeshi; mwendo; safari. *a ~ past,* gwaride. *(fig.)* matukio. *the ~ of events,* maendeleo ya mambo; matukio. *v.i./t.* tembea kama askari; peleka.

**mare** /mɛ:/ *n.* farasi jike. *~'s nest n.* uvumbuzi wa uwongo au usio na maana.

**margarine** /ˌmɑ:dʒə'ri:n/ *n.* majarini; siagi.

**margin** /'mɑ:dʒɪn/ *n.* **1.** pambizo; nafasi ya pembeni katika kitabu. **2.** ukingo. **3.** ziada ya. **~al** *adj.* -a pembezoni; - kando.

**marine** /mə'ri:n/*n.* askari wa manowari. *adj.* -a bahari; - a mambo ya bahari; -a baharini. *merchant ~,* jumla ya meli zote za taifa fulani. *~ corps,* jeshi la wanamaji. **~r** *n.* baharia. **maritime** *adj.* -a bahari; -a baharia; -a pwani.

**mark** /mɑ:k/ *n.* **1.** alama; dalili; ishara; athari. **2.** doa; baka; waa; kovu; chale. **3.** chapa; nembo. **4.** hesabu. **5.** shabaha. *beside (wide of) the ~,* haimo; haihusiki. **6.** kiwango. *up to the ~,* kiasi kinachohitajika. **7.** cheo. *make one's ~,* pata -wa mashuhuri. *v.t.* tia alama; pigia chapa; sahihisha; tia maksi; zingatia; -wa dalili ya; wa kitambulisho cha. *~ how it is done,* angalia jinsi lifanywavyo. *~ time,* chapa mguu. *(fig.)* subiri. *~ sth. off,* weka mipaka ya kitu. *~ sth. out,* tia mipaka. *~ sb. out for,* chagua, teua, fulani kwa. **~ed** *adj.* dhahiri; wazi. *a ~ difference,* tofauti iliyo dhahiri. *a ~ man,* mtu aliyeainishwa. **~edly** *adv.* kwa uwazi. **~ing** *n.* mapaku; alama. **~sman** *n.* mtu stadi wa kulenga shabaha. **~smanship** *n.* uhodari katika kulenga shabaha.

**market** /'mɑ:kɪt/ *n.* soko; kutakwa kwa bidhaa; ununuzi na uuzaji. *the coffee ~,* soko la kahawa. *a lively ~,* hali nzuri ya biashara. *v.i./t.* uza; nunua; peleka kuuza. **~able** *adj.* inayouzika. **~garden** *n.* bustani ya mboga za kuuza.

**marmalade** /'mɑ:məleɪd/ *n.* mamaledi: jemu ya machungwa.

**marrow** /'mærəʊ/ *n.* uloto. *vegetable ~,* mung'unye. *chilled to the ~,* ona baridi kali.

**marry** /'mæri/ *v.t./i.* oa; oza; oana; olewa; funga ndoa.

**marriage** /'mærɪdʒ/ *n.* ndoa; nikahi. **~able** *adj.* -a kufaa kuoa au kuolewa.

**Mars** /mɑ:z/ *n.* Mirihi: sayari ya nne kutoka kwenye jua.

**marsh** /mɑ:ʃ/ *n.* bwawa; ziwa lenye matope; kinamasi. **~y** *adj.* -a matope; -a kinamasi.

**marsupials** /mɑ:'su:pɪəls/ *n.* wanyamapochi: mamalia wanaozaa watoto na kuwalea katika mifuko maalumu iliyomo katika miili yao, e.g. kangaruu.

**martial** /'mɑ:ʃ(ə)l/ *adj.* -a vita; -a kupenda vita; -a kijeshi. *~ law,* sheria za kijeshi.

**martyr** /'mɑ:tə(r)/ *n.* mfiadini; shahidi. *be a ~ to a complaint,* umwa sana. *v.t.* ua, tesa kishahidi. **~dom** *n.* mateso, kifo cha kishahidi.

**marvel** /'mɑ:vl/ *n.* ajabu; muujiza; mtu au kitu -a kushangaza. *v.i.* (**-ll-**) shangaa. **~lous** *adj.* -a ajabu; -a kushangaza.

**masculine** /ˌmæskju'lɪnəti/ *adj.* -ume; -a kiume; dume. *~ gender,* jinsia ya kiume. **masculinity** *n.* uume.

**maser** /'meɪzə/ *n.* meza: chombo cha kuongezea wimbimaikro.

**mash** /mæʃ/ *n.* ponde; mponda mseto. *v.t.* ponda; seta.



masks

**mask** /mɑ:sk/ *n.* kinyago; barakoa. *v.t.* vaa kinyago; ficha; geuza; sitiri.

**mason** /'meɪsn/ *n.* mwashi. **~ry** *n.*

uashi.

**mass**[1] /mæs/ *n.* masi; fungu; chungu; wingi; bonge. *the ~es,* umma. **~ media**, vyombo vya habari. **~ number**, namba masi; jumla ya namba ya protoni na nyutroni katika nyuklia. **~ production**, uzalishaji kwa wingi.*v.t./i.* kusanya; kusanyika.

**mass**[2] /mæs/ *n.* misa. *high ~,* misa kuu. *low ~,* misa ndogo. **~ive** *adj.* -kubwa; -nene; -zito; imara.

**massacre** /'mæsəkə(r)/ *n.* mauaji ya kinyama ya halaiki. *v.t.* ua ovyo watu wengi.

**massage** /'masa:ʒ, mə'sa:ʒ, -dʒ/ *n.* ukandaji; uchuaji; upunaji; usingaji. *v.t.* kanda; singa; puna; chua. **masseur** *n.* msingaji mwana mme. **masseuse** *n.* msingaji mwanamke.

**massif** /'masɪf, ma'si:f/ *n.* mkusanyiko wa vilele vya milima.

**mast** /ma:st/ *n.* mlingoti. **~ head** *n.* ncha ya mlingoti. *sail before the ~,* fanya kazi kama baharia wa kawaida.

**master** /'ma:stə(r)/ *n.* **1.** bwana. **2.** shahada ya pili. *~ of arts,* shahada ya pili ya sanaa. **3.** fundi; stadi; mjuzi. **4.** nahodha; kapteni. *v.t.* shinda; tawala; -wa hodari; -wa mweledi. **~ful** *adj.* -enye kupenda kutawala wingine; stadi. **~-key** *n.* ufunguo malaya. **~ly** *adj.* -a ustadi mkubwa. **~piece** *n.* kazi bora. **~y** *n.* ustadi; ujuzi; umahiri; madaraka.

**mat** /mæt/ *n.* mkeka; jamvi; kirago; kitanga; busati; msala. **~ted** *adj.* -liosukwa; -liosokotwa; - liotatizika.

**match**[1] /mætʃ/ *n.* ujiti wa kiberiti. **~box** kiberiti.

**match**[2] /mætʃ/ *n.* **1.** mechi; shindano. *a football ~,* mechi ya mpira. *return ~,* mechi ya marudiano. **2.** mwenza; sawa; mshindani; sawa. **3.** ndoa; mwenza wa ndoa. *They made the ~ of it,* walioana. **4.** ulinganifu. *v.t./i.* lingana na; linganisha; pambanisha; shindanisha; oza; oana. **~less** *adj.* -sio na kifani. **~maker** *n.* mshenga.

**mate** /meɪt/ *n.* mwenza; rafiki; sarahangi; msaidizi; mume; mke; dume; jike. *the lioness and her ~,* simba jike na dume wake. *v.t./i.* pandana.

**material** /mə'tɪəriəl/ *n.* nyenzo; vifaa. *raw ~s,* malighafi. *adj.* -a mwili; yakinifu; muhimu; -a kiini. **~ism** *n.* uyakinifu; shauku ya vitu au anasa kuliko mambo ya kiroho. **~ize** *v.t./i.* fanya kuwa kitu; tokeza -enye umbo; kamilishwa; timizwa.

**maternal** /mə'tɜ:nl/ *adj.* -a mama; -a kuukeni. *~ aunt,* mama mdogo au mama mkuu. **maternity** *n.* uzazi. *maternity nurse,* mkunga. *maternity hospital,* hospitali ya wazazi.

**mathematics** /'mæθə'mætɪks/ *n.* hesabu; hisabati. **mathematical** *adj.* -a hisabati. **mathematician** *n.* mtaalamu wa hisabati.

**matriculate** /mə'trikjʊleɪt/ *v.t./i.* ingia chuo kikuu; ingizwa chuo kikuu; pasi mtihani wa kuingia chuo kikuu.

**matriculation** /mə,trɪkju'leɪʃn/ *n.* kuingia au kuingizwa chuo kikuu; mtihani wa kuingia chuo kikuu.

**matrimony** /'matrimənі/ *n.* ndoa; kuoana. **matrimonial** *adj.* - a ndoa.

**matrix** /'meɪtrɪks/ *n.* (**matrices**, **~es**) kalibu; mawe ya asili yenye madini; chanzo; solo; matriki.

$$\begin{pmatrix} 3 & 12 & 8 \\ 4 & 8 & 13 \\ 12 & 9 & 3 \end{pmatrix}$$

**matrix**

**matron** /'meɪtrən/ *n.* matroni; mwanamke anayetunza bweni; mwanamke anayesimamia wauguzi wa hospitali; mwanamke aliyeolewa. **~ly** *adj.* -a kimatroni.

**matter** /'mætə(r)/ *n.* mata; maada; maudhui; machapisho; maandishi; jambo; kisa; hoja; habari; umuhimu; maana; kadiri. *printed ~,* machapisho. *money ~s,* mambo ya fedha. *as a ~ of fact,* kwa kweli. *a ~ of course,* jambo la kawaida; jambo la kutarajiwa. *be the ~(with),* -wa na. *What is the ~ with him?* ana nini? *no ~ what,* lolote liwalo. *no ~ when,* siku yoyote iwayo. *v.i.* faa;

[illegible]



mattress

[illegible]

**may** [illegible] *vi* **might** [illegible]

[illegible]

**meal** [illegible] *n* chakula [illegible] unga wa [illegible] **~ie** *n* unga wa mahindi **~y** *adj* -a unga **~ bug** *n* [illegible] **~ mouthed** [illegible]

**mean** [illegible] **meant** [illegible]

[illegible]

**medicine** [illegible] uganga tiba udaktari dawa [illegible] **medicine man** *n* mganga [illegible]

**medieval -iaeval** [illegible]

[illegible]

taamuli; tafakari. **meditation** *n.* mazingatio; taamuli; tafakuri.

**medium** /'mi:diəm/ *n.* (**media**) njia; chombo; wastani; mazingira. *adj.* a kati; -a kadiri; -a wastani. **~ wave** *n.* masafa ya kati; mawimbi ya kati (ya urefu wa mita 100 -1000).

**meet** /mi:t/ *v.t./i.* kuta; kutana; fahamiana; pokea; laki; faa; tosheleza mahitaji; kabili. *Will this ~ the case?* hii itafaa? *~ a person's wishes,* ridhia matakwa ya mtu. **~ing** *n.* mkutano; mkusanyiko.

**megahertz** /'megəhɜ:ts/ *n.* megahezi: hezi milioni moja.

**megaphone** /'megəfəʊn/ *n.* megafoni; bomba; kipaza sauti.

**megawatt** /'megəwɒt/ *n.* megawati: wati milioni moja.

**meiosis** /mʌɪ'əʊsɪs/ *n.* meosisi: utaratibu wa mgawanyiko wa kukamilika ambapo kromosomu hupunguzwa kutoka kwenye gameti.

**melody** /'melədi/ *n.* lahani; tuni, mpangilio wa nota na maneno kimuziki. **melodious** *adj.* -a sauti tamu; -a maghani; -a tuni.

**melon** /'melən/ *n.* tikiti maji.

**melt** /melt/ *v.t./i.* yeyusha; yeyuka; lainisha; tia huruma; fifia; toweka. **~ing** *n.* uyeyukaji *a heart ~ with pity,* moyo uliojaa huruma. **~ point**, kiwango myeyuko: kiasi cha halijoto ambapo dutu hubadilika kutoka mango kuwa kioevu.

**molten** /'məʊltən/ *adj.* -lioyeyuka; *molten gold,* dhahabu iliyoyeyuka.

**member** /'membə(r) *n.* mwana chama; mjumbe; kiungo cha mwili. **~ship** *n.* uanachama.

**membrane** /'membreɪn/ *n.* kiwambo: ngozi nyembamba inayoweza kupenyeza molekuli za ukubwa fulani; utando.

**memory** /'meməri/ *n.* uwezo wa kukumbuka; masafa ya kuweza kukumbukia; kumbukumbu; ukumbukaji; mambo yaliyopita. *have a good ~,* -wa na uwezo mku-bwa wa kukumbuka. *within living ~,* wakati huu; wakati wetu. **memorable** *adj.* -a kukumbukwa; mashuhuri; -a sifa kubwa.

**memorandum** /,memə'rændəm/ *n.* maandiko ya kumbukumbu; taarifa. **memorial** *n./adj.* kumbukumbu; hati ya maombi.

**memorize** /'meməraɪz/ *v.t.* hifadhi kwa moyo.

**menace** /'menəs/ *n.* hatari; tishio; hamaniko; kamio. *v.t.* tisha; kamia; hamanisha. **menacingly** *adv.* kwa namna ya kutisha.

**mend** /mend/ *v.t./i.* tengeneza; rekebisha; ongoka; pona. *He is on the ~,* ameanza kupoa.

**menial** /'mi:nɪəl/ *n./adj.* mtumishi; boi; -a mtumishi; duni.

**meniscus** /mɪ'nɪskəs/ *n.* meniskasi: uso wa kiowevu uliopinda ndani ya bomba au chombo chembamba.

**menstrual cycle** *n.* mzunguko hedhi: kipindi maalumu kutoka hedhi mpaka hedhi.

**mensuration** *n.* upimaji wa urefu na maeneo.

**mental** /'mentl/ *adj.* -a akili; -a kichwa. **~ arithmetic**, hesabu za kichwa; hesabu za moyo. *~ patient,* mwendawazimu; mgonjwa wa kichaa. **~ home**, hospitali ya wagonjwa wa akili. **~ity** *n.* akili; tabia; mtazamo; hisia. **~ly** *adv.* kwa moyo.

**mention** /'menʃn/ *n./v.t.* utajaji; utajo; taja. *not to ~,* licha ya. *Don't ~ it,* haidhuru; si kitu.

**menu** /'menju:/ *n.* menyu; orodha ya vyakula.

**mercenary** /'mə:sɪn(ə)ri/ *n./adj.* mamluki; askari wa kukodiwa. *~ motives,* kwa ajili ya kujipatia faida tu.

**merchandise** /'mə:tʃ(ə)ndʌɪs, z/ *n.* bidhaa; biashara. **mercantile** *adj.* -a biashara. *mercantile marine,* meli ya abiria na bidhaa.

**merchant** /'mɜ:tʃənt/ *n.* mfanyabiashara. **~ marine** *n.* meli ya biashara ya kupakia bidhaa.

**mercury** /'mɜ:kjəri/ *n.* zebaki; hidragiri. **mercurial** *adj.* -a zebaki; geugeu.

**mercy** /'mɜ:si/ *n.* rehema; huruma; upole; wema; msamaha. **merciful**

*adj.* -enye rehema; -enye huruma. **merciless** *adj.* -sio na huruma; katili.

**mere** /mɪə/ *adj.* -tupu; tu. **~ly** *adv.* tu.

**merge** /mɜ:dʒ/ *v.t./i.* unganisha; ungana. **~r** *n.* muungano; kuungana; kuunganisha.

**meridian** /mə'rɪdɪən/ *n.* meridiani; mstari kutoka kaskazini kusini ya dunia; upeo; usitawi; kipeo. *the ~ of Greenwich,* meridiani ipitayo Greenwich.

**merit** /'merɪt/ *n.* sifa njema; tabia nzuri; stahili; matendo mema. **~orious** *adj.* enye kustahili; -a sifa njema.

**merry-go-round** *n.* bembea yenye farasi; pembea, magari ya kufurahisha watoto.



merry-go-round

**mesh** /meʃ/ *n.* jicho la wavu. *v.t./i.* tega; nasa; umana; ingiana.

**mesolithic** *adj.* -a zama za mawe kijiolojia, nao ni mwisho wa utando wa theluji na mwanzo wa kilimo.

**mess**[1] /mes/ *n.* matata; fujo; machafuko; takataka. *make a ~ of sth.,* fuja; haribu; tatanisha. *get into a ~,* ingia matatizoni. *v.t./i.* chafua; vuruga; fuja. *~ about,* chezea; fanya purukushani; fanya jambo bila mpango. **~y** *adj.* -chafu; -a fujo.

**mess**[2] /mes/ *n.* mesi; bwalo la kulia chakula; watu walao pamoja. *v.i.* -la bia; -la kikoa; -la pamoja.

**message** /'mesɪdʒ/ *n.* habari; maneno; taarifa; barua; ujumbe.

**messenger** /'mesɪndʒə(r)/ *n.* mjumbe; tarishi; mtume.

**metabolism** /mɪ'tabəlɪz(ə)m/ *n.* metaboli; umetaboli: hali ya ujenzi na uvunjajivunjaji kemikali katika viumbe hai.

**metal** /'metl/ *n.* metali; kitu cha metali; kokoto za kutengenezea barabara. **~lic** *adj.* -a metali. **~lurgy** *n.* metalujia: sayansi ya metali na aloi zake; ufuaji metali; taaluma ya ufuaji metali.

**metamorphic** *adj.* (kwa majabali) -enye kubadilika umbo au sifa zake kutokana na kani za maumbile.

**metamorphosis** /ˌmətə'mɔ:fəsɪs/ *n.* metamofosisi: mgeuko mkubwa wa umbile la kiumbe katika utaratibu wao wa kukua kutoka hali ya yai mpaka kufikia kiumbe kamili.

**metaphor** /metəfə(r)/ *n.* sitiari: mtindo wa usemaji ambao hulinganisha bila ya kutumia vilinganishi. *She has a heart of stone,* ana moyo wa jiwe.

**meteor** /'mi:tiə(r)/ *n.* kimondo: gimba la kumetameta kutoka anga za mbali. **~ic** *adj.* a kimondo. **~ite** *n.* kimondo. **~ology** *n.* metorolojia: saya-nsi ya utabiri wa hali ya hewa.

**meter** /'mi:tə(r)/ *n.* mita: chombo cha kupimia umeme, masafa, kasi ya mwendo etc.



meter

**methane** /mi:θe:ɪn/ *n.* methani: gesi ya kihidrokaboni ya chini kabisa iliyojaa hidrojeni ambayo haina rangi na hushika moto haraka.

**method** /'meθəd/ *n.* njia; mbinu; utaratibu; desturi. **~ical** *adj.* -enye utaratibu; -liofanywa kwa utaratibu.

**methodism** /'meθədɪzəm/ *n.* umethodisti: madhehebu ya Kikristo ya kiprotestanti yaliyoanzishwa na John Wesley na wenzake. **methodist** *n./adj.* mmethodisti; -a methodisti.

**methylated spirit** *n.* spiriti iliyomethilishwa: mchanganyiko wa ethanoli, piridini, petroli na rangi.

**metre** /'mi:tə(r)/ *n.* **1.** mita: kizio cha msingi cha urefu katika mfumo wa SI sawa na inchi 39.4. **2.** mita: mpangilio wa silabi zenye mkazo na zisizo mkazo ili kuunda mfuatano maalumu katika shairi. **metric** *adj.* -a mita; -a kuhusu kizio cha mita. **metric system**, mfumo meta: mfumo wa vipimo unaotumia vizio msingi vya meta.

kilogramu na sekunde. **metrical** *adj.* -a kupima mashairi, nyimbo, etc. -a kipimo.

**metropolis** /mɪ'trɒp(ə)lɪs/ *n.* mji mkuu wa nchi; makao makuu ya nchi. **metropolitan** *adj.* -a mji mkuu.

**mica** /'mʌɪkə/ *n.* madini aina ya ulanga.

**microbe** /'mʌɪkrəʊb/ *n.* kijidudu maradhi.

**microbiology** /ˌmaɪkrəʊbaɪ'ɒlədʒi/ *n.* mikrobiolojia: tanzu ya biolojia inyohusika na muundo na kazi za viumbe vidogovidogo kama bakteria na virusi.

**microchip** /'maɪkrəʊtʃɪp/ *n.* mikrochipu: kipande kidogo sana cha silikoni kinachotumika kama saketi changamano ya umeme.

**micrometer** /mʌɪ'krɒmɪtə/ *n.* mikromita: chombo cha kupimia vitu vidogo sana kwa kiwango cha sehemu moja katika milioni.

**micro-organism** *n.* kijiumbe: kiumbe kidogo sana kinachoonekana kwa hadubini tu kama vile virusi na bakteria.

**microphone** /'maɪkrəfəʊn/ *n.* mikrofoni: chombo cha kugeuza mawimbi sauti kuwa mawimbi umeme na kugeuzwa tena kuwa sauti baada ya kurushwa.



microphone




microscope | hadubini

**microprocessor** /ˌmaɪkrəʊ'prəʊsesə(r)/ *n.* mikroprosesa: kompyuta ndogo yenye mikrochipu moja au zaidi.

**microscope** /'maɪkrəʊskəʊp/ *n.* hadubini: chombo kinachofanya vitu vidogo visivyoonekana kwa macho kuonekana vikubwa. **microscopic** *adj.* -dogo mno kuweza kuonekana kwa macho matupu.

**microwave** /'maɪkrəweɪv/ *n.* wimbi-mikro, kijiwimbi: kiwimbi sumaku umeme kitumikacho katika mawasiliano.

**microwave oven** /'maɪkrəweɪvʌvn/ *n.* chombo kinachotumika kupikia kwa kutumia mawimbi ya umeme.

**mid** /mɪd/ *adj.* -a kati. **~day** *n.* saa sita ya mchana; adhuhuri. **~night** *n.* saa sita ya usiku; usiku wa manane. *burn the ~night oil ~,* kesha. **~-ocean ridge**, tuta-bahari: tuta la milima lililo chini ya bahari.

**middle** /'mɪdl/ *n./adj.* kati; -a kati. **~man** *n.* mchuuzi; dalali; mlanguzi; mtu wa kati. **middling** *adj.* -a katikati; -a kadiri; -a wastani. *~ ages,* zama za kati (500-1500 AD).

**midst** /mɪdst/ *n. in the midst,* katikati ya; wakati wa. *in our ~,* miongoni mwetu.

**midwife** /'mɪdwaɪf/ *n.* (**~wives**) mkunga, mtu anayewasaidia akina mama wakati wa kujifungua. **~ry** *n.* ukunga.

**might** /maɪt/ *n.* uwezo; nguvu; ukuu. **~y** *adj.* -enye uwezo, nguvu, amri na ukuu.

**migrate** /mʌɪ'greɪt, 'mʌɪgreɪt/ *v.i.* hama; hamia; hajiri. **migrant** *n./adj.* mhamaji; -hamaji. **migration** *n.* uhamaji; uhamiaji. **migratory** *adj.* -enye tabia ya kuhama. *migratory birds,* ndege wahamao na kurudi kila mwaka.

**mild** /maɪld/ *adj.* -pole; -sio kali; laini; -dogo. **~ly** *adv.* kwa upole; **~ness** *n.* upole; ulaini.

**mile** /maɪl/ *n.* maili. **~age** *n.* maili zilizoendwa; posho la usafiri; malipo ya usafirishaji kwa maili. **~stone** *n.* jiwe la maili; tukio

muhimu katika maisha.
**militant** /'mɪlɪtənt/ *n.* mpigania haki; mpiganaji. *adj.* -a kupigana, -a kutaka vita.
**military** *adj.* -a kijeshi; -a kivita. *the military,* jeshi; wanajeshi; askari.
**militarism** /'mɪlɪtərɪzəm/ *n.* tabia ya kupenda vita. **militate** *v.i.* -wa mbali na; pinga; zuia.
**milk** /mɪlk/ *n.* maziwa. *butter~,* mtindi. *condensed ~,* maziwa ya kopo. *~ powder,* maziwa ya unga. *v.t.* kama; toa maziwa. **~y** *adj.* -a maziwa; kama maziwa. *the ~ way,* nyota ndogo nyingi sana zinazotoa nuru hafifu mbinguni.
**mill** /mɪl/ *n.* kinu. *flower ~,*kinu cha kusagia unga. *~ stone,* kiwe; jiwe la kusagia. *v.t./i.* saga, sindika kwenye kinu. *~ed edge,* ukingo uliotiwa mikato kama ule wa sarafu. **~er** *n.* msagishaji.
**millenium** /mɪ'lɛnɪəm/ *n.* milenia: miaka elfu moja.
**millet** /'mɪlɪt/ *n.* mtama; wimbi; serena; ulezi; lulu; uwele.
**milli-** /'mɪli/ *prefix* mili: sehemu moja ya elfu ya kipimo.
**millibar** /'mɪlibɑ:(r)/ *n.* milibaa: kizio cha kanieneo kitumikacho katika metrolojia ambacho ni sawa na daini 1000 kwa kila sentimita ya mraba.
**milligram** /'mɪligræm/ *n.* miligramu: sehemu ya 1/1000 ya gramu moja.
**millilitre** /'mɪlili:tə(r)/ *n.* mililita: sehemu moja katika elfu ya lita moja.
**millimetre** /'mɪlimi:tə(r)/ *n.* milimita: sehemu moja katika elfu ya mita moja.
**million**/'mɪljən/ *n.* milioni. **~aire** *n.* milionea.
**mimic** /'mɪmɪk/ *n.* mwigaji; mwigo wa lafudhi. *adj.* - liyoigwa. *v.t.* iga, hasa kwa kuchekesha; fanana kabisa. **~ry** *n.* wigo; uigaji.
**minaret**/'mɪnərɛt, mɪnə'rɛt/ *n.* mnara wa msikiti.
**mince** /mɪns/ *n.* kima (nyama ya kusaga). *v.t./i.* **1.** kata vipande vidogovidogo. **2.** tafuna maneno; tembea kwa mikogo. *not to ~ matters,* sema waziwazi. **~meat** *n.* mchanganyiko wa unga na viungo vyote kwa kufanyia maandazi. **~-pie** *n.* andazi lililofanywa kwa mchanganyiko huo.
**mind** /maɪnd/ *n.* **1.** ukumbukaji; kumbukumbu. *keep (bear) sth. in ~,* kumbuka jambo fulani. *call to ~,* kumbuka. *put sb. in ~ of,* kumbusha mtu. **2.** nia; dhamiri. *make up one's ~,* amua kufanya jambo. *change one's ~,* ghairi. *be in two ~s (about sth.),* sita; -wa na mashaka. *speak one's ~,* sema ukweli. *be of one ~,* afikiana. *have a good ~ to,* taka; elekea. *take sb.'s ~ off (the matter),* sahaulisha. **3.** akili. *be out of one's ~,* -wa na wazimu. *(have great) presence of ~,* weza kuamua haraka. **~ful** *adj.* -enye kuzingatia. *v.t./i.* angalia; tunza; kirihika. *~ (out)!* tahadhari! *Do you ~ my smoking!* hutajali nikivuta? *Would you ~ shutting the door?* tafadhali ufunge mlango.
**mine**[1] /maɪn/ *pron.* -angu.
**mine**[2] /maɪn/ *n.* machimbo; mgodi; kware; bomu la kutega. *v.t./i.* chimbua madini; tega mabomu. **~field** *n.* eneo lililotegwa mabomu; eneo lililo na migodi. ` *n.* mchimba madini; mtega mabomu. **~ral** *n.* madini. **~ salts** chumvi madini: kemikali zenye madini yahitajikayo kwa maisha na ukuaji wa wanyama na miti. *adj.* ya madini. **~ralogy** *n.* sayansi ya madini. **~ral water** *n.* maji yaliyotiwa madini.
**mingle** /'mɪŋgl/ *v.t./i.* changanya; changanyika.
**miniature** /'mɪnətʃə(r)/ *n.* kisanamu; mfano mdogo.
**minimum** /'mɪnɪməm/ *n./adj.* kiasi kidogo iwezekanavyo. - dogo sana; -a chini kabisa.
**minister** /'mɪnɪstə(r)/ *n.* waziri; balozi; mchungaji; kasisi. *prime ~,* waziri mkuu. *v.i.* saidia; tumikia. **~ial** *adj.* -a waziri; -a wizara; -a kasisi.
**ministration** *n.* utumishi; msaada.

**ministry** /'mɪnɪstri/ *n.* wizara; jamii ya makasisi. *enter the ministry,* -wa kasisi.
**minor** /'maɪnə(r)/ *n.* mtoto wa chini ya miaka kumi na nane. *adj.* -dogo; hafifu; -a chini. **~ity** *n.* utoto; wachache; walio wachache.
**mint** /mɪnt/ *n.* kiwanda cha kutengenezea pesa. *v.t.* tengeneza pesa, sarafu.
**minus** /'maɪnəs/ *prep.* kasoro; bila. *adj.* -ya kutoa. *the ~ sign,* alama ya kutoa hii ( - ).
**minute**[1] /'mɪnɪt/ *n.* dakika; kumbukumbu; taarifa. *in a ~,* sasa hivi.
**minute**[2] /maɪ'nju:t/ *adj.* -dogo sana; halisi.
**miracle** /'mɪrəkl/ *n.* muujiza; ajabu. **miraculous** *adj.* -a muujiza; -a kustaajabisha.
**mirage** /'mɪrɑ:ʒ, mɪ'rɑ:ʒ/ *n.* mazigazi; mangazimbwe. *(fig.)* mazingaombwe.
**mirror** /'mɪrə(r)/ *n.* kioo cha kujitazamia. *~ image,* taswira geu.
**mis-** /mɪs/ *prefix* -baya; vibaya; visivyo sawasawa.
**miscarriage** /'mɪskærɪdʒ/ *n.* uhari bikaji mimba; kutowasilisha; kutofika mahali utakiwapo. *~ of justice,* potosha haki. *~ of goods,* bidhaa kutofika zilikopangiwa. **miscarry** *v.i.* haribika; -tofaulu; tokea vibaya; -tofika salama.
**miscellaneous** /ˌmɪsə'leɪnɪəs/ *adj.* anuwai; -a namna nyingi pamoja. **miscellany** *n.* mchanganyiko wa vitu vya namna mbalimbali.
**mischief** /'mɪstʃɪf/ *n.* madhara; hasara; fitina; utundu; utukutu. *make ~ between,* tia fitina; gombanisha. **mischievous** *adj.* -tundu; fitinishaji.
**misconduct** /ˌmɪs'kɒndʌkt/ *n.* tabia mbaya; uongozi mbaya; mwenendo mbaya. *v.t.* ongoza vibaya; -wa na tabia mbaya.
**misdeed** /ˌmɪs'di:d/ *n.* tendo baya; kosa.
**miser** /'maɪzə(r)/ *n.* bahili. **~ly** *adj.* -a kibahili. **~able** *adj.* -enye taabu; maskini; duni; -nyonge. **~ably** *adv.* kinyonge. **~y** *n.* umaskini; unyonge. mateso; taabu.
**misfire** /ˌmɪs'faɪə(r)/ *n.* kutoripuka; kutowaka; kutofaulu; kutofyatuka; kutolia. *v.i.* -tolia; -toripuka; -towaka; tofaulu.
**misfit** /'mɪsfɪt/ *n.* vazi lisilo sawa na kimo; *(fig.)* mtu asiyefaa; mtu asiyepatana na wenziwe.
**misfortune** /ˌmɪs'fɔ:tʃu:n/ *n.* msiba; taabu; bahati mbaya· mkosi; balaa.
**misguide** *v.t.* ongoza vibaya; elekeza vibaya. **~d** *adj.* -potofu; -jinga.
**mishap** /'mɪshæp/ *n.* bahati mbaya; ajali.
**mislay** /ˌmɪs'leɪ/ *v.t.* (**-laid-**) weka (kitu) pasipo pake; poteza.
**mislead** /ˌmɪs'li:d/ *v.t.* ongoza vibaya; kosesha; potosha.
**misrule** /ˌmɪs'ru:l/ *n.* utawala mbaya. *v.t.* tawala vibaya.
**miss** /mɪs/ *n.* msichana; binti. *v.t./i.* (**~ed**). kosa. *Fire at a lion and ~ it,* piga risasi simba na kumkosa. *Try to catch a ball and ~ it,* jaribu kudaka mpira na kuukosa. *He ~ed the train,* aliikosa treni. *~ sth. out,* ruka; acha; -toingiza; sahau. **~ing** *adj.* siokuwapo; -liopotea; -sioonekana.
**missile** /'mɪsaɪl/ *n.* kombora. *guided ~,* kombora linaloongozwa na mitambo ya elektroniki.
**mission** /'mɪʃn/ *n.* ujumbe; misheni; kazi maalumu. **~ary** *n.* mmishionari; -a misheni.
**mist** /mɪst/ *n.* ukungu; umande; kiwi. **~y** *adj.* **1.** -enye ukungu; si dhahiri.
**mistake** /mɪ'steɪk/ *n.* kosa. *by ~,* kwa makosa. *v.t./i.* (**mistook**, **mistaken**) kosea; kosa; dhania visivyo; -tofahamu vyema *~ (sb. or sth.) for,* changanya na.
**mistress** /'mɪstrəs/ *n.* bibi; kimada; hawara; mpenzi; mweledi wa kike; mwalimu wa kike; mkuu wa kaya wa kike.
**mistrust** /ˌmɪs'trʌst/ *n./v.t.* shaka; tuhuma; tilia shaka; -toamini. **~ful** *adj.* -enye shaka.
**misunderstand** /ˌmɪsʌndə'stænd/

*v.t.* elewa vibaya. **~ing** *n.* kutoelewana.

**mitochondria** /ˌmʌɪtə(ʊ)ˈkɒndrɪə/ *n.* mitokondria: oganeliseli ambamo utoaji wa nishati kutokana na chakula sahili hufanyika.

**mitosis** /mʌɪˈtəʊsɪs/ *n.* mitosisi: utaratibu wa mgawanyiko wa seli za kawaida na baada ya mgawanyiko huo seli moja huwa mbili.

**mitre** /ˈmɪtrə(r)/ *n.* kofia ya kiaskofu



mitre

**mix** /mɪks/ *v.t./i.* changanya; changanyika; vuruga; boronga. *be ~ed up in (with),* jihusisha na jambo fulani. *feel ~ed up (about sth.),* changanyikiwa. **~ed** *adj.* -a mchanganyiko. **~ture** *n.* mchanganyiko.

**moan** /məʊn/ *n.* kite; kilio; uuguaji. *v.i.* ugua; lia; piga kite.

**mob** /mɒb/ *adj.* kundi la watu wenye fujo.

**mobile** /ˈməʊbʌɪl/ *adj.* -a kwenda; -a kuweza kwenda; -epesi kugeuka. *phone n.* simu ya mkononi, simu tamba. **mobility** *n.* mwendo; wepesi wa kugeuka. **mobilize** *v.t.* hamasisha. **mobilization** *n.* uhamasishaji.

**mock** /mɒk/ *v.t./i.* fanyia mzaha; dhihaki; fanyia tashtiti; fanyia stihizai. *adj.* -a kuiga; bandia; -a mzaha; sio halali. **~ingly** *adv.* kidhihaka. **~ery** *n.* dhihaka; mzaha.

**mode** /məʊd/ *n.* jinsi; namna; mtindo; hali; modi. **modal** *adj.* -a hali; modi. **modality** *n.* hali; namna. **~l** *n.* modeli; kifani; mfano; kielelezo; mtindo; kigezo. *a ~ wife,* mke wa kuigwa. *v.t.* (**-ll-**) finyanga kwa kufuata mfano; iga mtu mwingine; onyesha mtindo. **~lling** *n.* ufinyanzi; uonyeshaji mitindo.

**modem** /ˈməʊdɛm/ *n.* modemu: chombo kinachounganisha kompyuta na simu ili data iweze kurushwa toka kompyuta hadi nyingine.

**moderate** /ˈmɒdərət/ *adj.* -a kiasi; -a wastani. *v.t./i.* punguza; tuliza; pungua; tulia; simamia mtihani; ongoza mjadala; rekebisha mtihani. **~ly** *adv.* kwa kiasi. **moderation** *n.* kiasi; kadiri; wastani; uongozaji mjadala; usimamiaji mtihani.

**modern** /ˈmɒdn/ *adj.* -a siku hizi; -pya; -a kisasa. **~ize** *v.t.* fanya kuwa ya kisasa.

**modest** /ˈmɒdɪst/ *adj.* -siojivuna; -a kadiri; -a wastani; -a staha. **~ly** *adv.* kiheshima; kwa kiasi. **~y** *n.* staha; kiasi.

**modify** /ˈmɒdɪfaɪ/ *v.t.* geuza; badilisha; badili kidogo; punguza; vumisha. **modification** *n.* ubadilishaji; badiliko; uvumishaji.

**modulate** /ˈmɒdjʊleɪt/ *v.t./i.* rekebisha; geuza; rekebu. **modulation** *n.* ubadilishaji sauti; urekebusauti namnisho. **modulator** *n.* moduleta; kirekebusauti.

**moist** /mɔɪst/ *adj.* -a majimaji; -enye unyevu. **~en** *v.t.* tia maji kidogo; rowesha kidogo. **~ure** *n.* unyevu.

**molar** /ˈməʊlə(r)/ *n./adj.* gego.

**molasses** /məˈlæsɪz/ *n.* molasi.

**mole** /məʊl/ *n.* fuko. **~hill** *n.* chungu ya udongo ifanywayo na fuko.

**molecule** /ˈmɒlɪkjuːl/ *n.* molekuli: chembe ndogo sana ya msombo inayoweza kushiriki katika mabadiliko ya kikemikali.

**mollusc** /ˈmɒləsk/ *n.* moluska: kabila safu ya wanyama kama vile konokono, ngisi, pweza na chaza ambao huishi baharini, kwenye maji baridi na hata nchi kavu.

**moment** /ˈməʊmənt/ *n.* **1.** kitambo kidogo; muda mfupi sana; kufumba na kufumbua; mara; maana. *affairs of great ~,* mambo ya maana sana. **~ary** *adj.* -a mara moja; -a kupita upesi sana. **~ous** *adj.* -a maana sana. **2.** momenti: athari za mgeuko wa kani. **~um** *n.* momenta, nguvumwendo: kiasi cha mwendo wa gimba ambacho huelezwa kama zao la masi na kasimwelekeo ya gimba hilo.

**monastery** /ˈmɒnəstri/ *n.* nyumba ya watawa.

**Monday** /'mʌndeɪ/ *n.* Jumatatu.
**money** /'mʌni/ *n.* fedha (sarafu, noti) itumikayo katika kuuza na kununua; pesa. **~order** *n.* hawala ya fedha.
**mongoose** /'mɒŋgu:s/ *n.* nguchiro.
**mongrel** /'mʌŋgrəl/ *n.* mbwa chotara.
**monitor** /'mɒnɪtə(r)/ *n.* **1.** kiranja; msimamizi. **2.** manowari ndogo. **3.** msikilizaji na mtoaji habari za kituo cha nje. **4.** chombo cha kufuatilia urukaji wa makombora. **5.** chombo cha kufuatilia urushaji wa matangazo ya redio na televisheni. **6.** chombo mfano wa seti ya televisheni cha kompyuta.
**monk** /mʌŋk/ *n.* mtawa wa kiume; sufii.
**monkey** /'mʌŋki/ *n.* kima; tumbili; ngedere; mbega. *v.i.* chezeachezea; iga. **~bread** *n.* buyu. **~nut** *n.* njugu nyasa.


**monkey**

**mono-** /'mɒnəʊ/ *prefix* -a moja tu; -enye moja tu; -a mara moja tu.
**monochrome** /'mɒnəkrəʊm/ *n./adj.* (picha) ya rangi moja.
**monocotyledon** /ˌmɒnə(ʊ)kɒtɪ'li:d(ə)n/ *n.* monokotiledoni: mmea ambao mbegu yake ina kotiledoni moja.



**monocotyledon | monokotiledoni**

**monocyte** /'mɒnə(ʊ)sʌɪt/ *n.* monositi: aina kubwa ya seli damu nyeupe ambayo inaweza kumeza bakteria, virusi na vipande vya seli.
**monogamy** /mə'nɒgəmi/ *n.* ndoa ya mke mmoja kwa wakati mmoja.
**monohybrid cross** *n.* kizazi kitokanacho na wazazi wawili kila mmoja mwenye jeni tawala moja na jeni tawaliwa moja.
**monologue** /'mɒnəlɒg/ *n.* mazungumzo binafsi ya mtu peke yake hasa katika maigizo.
**monopoly** /mə'nɒpəli/ *n.* ukiritimba; uhodhi. ~ *capitalism*, ubepari kiritimba. **monopolist** *n.* mkiritimba; mhodhi. **monopolize** *v.t.* hodhi.
**monosyllable** /'mɒnəsɪləbl/ *n.* silabi moja. **monosillabic** *adj.* -a silabi moja.
**monotone** /'mɒnətəʊn/ *n.* toni moja; kidatu bainifu kimoja cha sauti.
**monotreme** /'mɒnə(ʊ)tri:m/ *n.* mtundumwe: mamalia wa oda monotremata ambaye ogani za jinsia, mkojo na mmeng'enyo vina tundu moja kwa nje.
**monoxide** *n.* monoksaidi: oksaidi yenye atomu moja ya oksijeni.
**monsoon** /ˌmɒn'su:n/ *n.* monsuni: pepo za msimu; kaskazi.
**monster** /'mɒnstər/ *n.* dubwana; kiumbe cha kutisha kutokana na umbo lake lisilo la kawaida; mtu katili mno.
**monstrosity** /mɒn'strɒsəti/ *n.* kioja; dubwana. **monstrous** *adj.* kubwa mno; -a ajabu.
**month** /mʌnθ/ *n.* mwezi. **~ly** *adj./adv.* -a mwezi; kila mwezi; jarida litokalo kila mwezi.
**monument** /'mɒnjumənt/ *n.* jengo au sanamu ya ukumbusho; kazi ya mfano bora. **~al** *adj.* kubwa sana; -enye thamani ya daima; -a ukumbusho.
**mood** /mu:d/ *n.* hali; hali ya moyo. **~y** *adj.* -enye tabia ya kubadilikabadilika. **~ily** *adv.* kihamasa.
**moon** /mu:n/ *n.* mwezi. *new ~*, mwezi mwandamo; mwezi mchanga. *full ~*, mwezi mpevu.
**moor** /mʊə/ *n.* nyika; mbuga. *v.t.* tia nanga. **~ings** *n.* amari; chelezo; bandari.
**mop** /mɒp/ *n.* ufagio; tamvua; nywele za matimutimu. *v.t.* (**-pp-**) piga deki; pangusa kwa tamvua. ~ *sth. up*, futa; maliza.

**moraine** /mə'reɪn/ *n.* takataka na mawemawe zinazokokotwa na kutuliwa na mto wa barafu.

**moral** /'mɒrəl/ *n.* fundisho; maadili; murua. *adj.* - adilifu; -ema; -zuri; -nyofu; -enye hiari ya kuchagua mema au mabaya. *a ~ life,* maisha mema. *~ books,* vitabu vyenye kufunza maadili. *~ victory,* ushindi wa utu. *~ certainty,* jambo lielekealo kuwa kweli kabisa. **~e** *n.* hamasa; nguvu; moyo; imani. **~ist** *n.* mwalimu wa maadili; mwadilifu. **~ity** *n.* uadilifu; murua; maadili. **~ize** *v.i.* shajiisha uadilifu. **~ly** *adv.* kwa maadili.

**morbid** /'mɔ:bɪd/ *adj.* -gonjwa; -chafu; -enye kuwaza mambo mabaya. **~ity** *n.* ugonjwa. **~ly** *adj.* kigonjwa.

**more** /mɔ:(r)/ *adj.* zaidi. *adv.* zaidi; tena. *a little ~,* zaidi kidogo. *~ than,* kuliko; zaidi ya. *be no ~,* -fa; isha. *~ or less,* takriban. *grow (get, be) ~,* zidi kuwa. **~over** *adv.* tena; aidha; zaidi ya.

**moribund** /mɒrɪbʌnd/ *adj.* -a karibu na kufa; mahututi.

**morning** /'mɔ:nɪŋ/ *n.* asubuhi. *early ~,* alfajiri; mapambazuko.

**morse** *n.* *~ code,* namna ya kupeleka habari kwa mapigo marefu na mafupi ya sauti au ya vimulimuli vya taa.

**mortal** /'mɔ:tl/ *n.* binaadamu. *adj.* -enye kufa; -a kufisha; -a kudumu hadi kifo. *~ hatred,* chuki ya kudumu. *~ combat,* mapambano ya kufa na kupona. *in ~ fear of death,* -enye kuogopa sana mauti. **~ly** *adv.* kwa kufisha; sana; mno. **~ity** *n.* mauti; vifo; hali ya kuweza kufa. *~ rate,* kiwango cha vifo.



**mortise**

**mortar** /'mɔ:tə(r)/ *n.* mota; kinu; kombora. **~ board** *n.* chano; ubao wa kuwekea udongo; kofia ivaliwayo na wanafunzi wa chuo.

**mortise**, **-tice** /'mɔ:tɪs/ *n.* tunduunganishi.

**mortuary** /'mɔ:tjʊəri/ *n.* nyumba ya maiti; mochari.

**mosque** /mɒsk/ *n.* msikiti.

**mosquito** /mə'ski:təʊ/ *n.* mbu. **~net** *n.* chandarua. **~ proof** *adj.* -siopitisha mbu.

**moss** /mɒs/ *n.* kuvu; mwani; kuvumwani.

**most** /məʊst/ *adj.* -ingi kupita -ote; -ingi sana. *make the ~ of,* tumia vizuri. *for the ~ part,* zaidi; kwa kawaida; aghlabu; kwa jumla. **~ly** *adv.* kwa kawaida; hasa; karibu yote.

**moth** /mɒθ/ *n.* mdudu aina ya nondo.

**mother** /'mʌðə(r)/ *n.* mama mzazi; kiongozi wa jumuia ya watawa; kiini; chanzo. *~ tongue,* lugha mama. *v.t.* tunza; lea kama mama. **~-in-law** *n.* mkwe. **~hood** *n.* umama. **~less** *adj.* bila mama. **~ly** *adj.* kama mama.

**motion** /'məʊʃn/ *n.* wendo; msogeo; hoja; pendekezo. *move a ~,* toa hoja. *v.t.* ashiria; elekeza; ongoza. **~less** *adj.* tuli; -siojongea.

**motive** /'məʊtɪv/ *n.* nia; kusudio; matilaba; maarubu; sababu; lengo. *adj.* -enye kuendesha. *~ power,* nguvu za kuendesha jambo. **motivate** *v.t.* hamasisha; -pa motisha; sababisha.

**motor** /'məʊtə(r)/ *n.* mota; kitumi; musuli wa mwendo. *~ neuron,* mshipa wa fahamu unaoratibu msogeo wa viungo. *~cycle,* pikipiki. *~cade,* msafara wa vipando vya moto. *~car,* motokaa. *~boat,* motaboti. *v.i./t.* safiri kwa motokaa; safirisha kwa motokaa.

**motto** /'mɒtəʊ/ *n.* (**-oes**) wito; tamko

**mould** /məʊld/ *n.* kalibu; kielezo; tabia. *v.t.* finyanga; subu kwa kalibu; *(fig.)* ongoza; nyoosha; ongoa.

**mould**[1] /məʊld/ *n.* udongo wa mboji; udongo mweusi wenye rutuba.

**mould**[2] /məʊld/ *n.* kuvu. **~er** *v.i.* ota kuvu; oza; liwa na kutu; vunjikavunjika; chakaa.

**moult** /məʊlt/ *v.i.* jigeuza rangi ya manyoya; nyonyoka manyoya.

**mound** /maʊnd/ *n.* chungu; kilima; tuta; rundo; kichuguu.
**mount** /maʊnt/ *n.* mlima; kiunzi; farasi; baiskeli. *v.t.i.* panda; kwea; fanya; onyesha mchezo jukwaani; weka mahali pake; tundika picha. ~ *up,* zidi; ongezeka. ~ *guard over,* linda. **~ain** *n.* mlima. **~eer** *n.* mkaa mlimani; mpanda mlima. **~ous** *adj.* -a milima mingi.


moustache

**mourn** /mɔ:n/ *v.i./t.* lia; lilia; huzunika; huzunikia; omboleza; kaa matanga. **~er** *n.* mwombolezaji. **~ful** *adj.* -enye huzuni; -a kuhuzunisha. **~fully** *adv.* kwa majonzi. **~ing** *n.* kilio; matanga; msiba; maombolezo; majonzi.
**mouse** /maʊs/ *n.* (**mice**) panya.
**moustache** /mə'stɑ:ʃ/ *n.* sharubu.
**mouth** /maʊθ/ *n.*(**~s**) kinywa; mdomo; uwazi; tundu. *v.t./i.* sema sana; kula. **~ful** *n.* funda; kinywa tele. **~-organ** *n.* kinanda cha mdomo. **~piece** *n.* msemaji; chombo cha kupulizia; mdakale.
**move** /mu:v/ *n.* mwendo; zamu; tendo; jambo; uhamisho. *v.t./i.* sogeza; sogea; hamisha; hama; sisimua; gusa hisi; pendekeza; toa hoja; chukua hatua; endelea. ~ *sb. to do sth.,* shawishi mtu kufanya jambo. *He is always on the ~,* hana kituo; daima yumo mbioni. **~ment** *n.* mwendo; tapo; tendo; maendeleo; uhamaji.
**mow** /məʊ/ *v.t./i.* (**mowed**, **mown**) kata majani; fyeka.
**Mr.** /'mɪstə(r)/ *n.* ufupisho wa *mister:* bwana. **Mrs.** *n.* ufupisho wa *missis:* bibi.
**much** /mʌtʃ/ *n./ adj./adv.* -ingi; tele; sana; wingi. ~ *of a,* karibu sawasawa.
**muck** /mʌk/ *n.* samadi; taka; uchafu; mbolea. *v.t./i.* ~ *sth. up,* buruga; fuja; chafua. ~ *about,* zurura. **~y** *adj.* chafu.
**mucous membrane** *n.* kiwambo-ute: sehemu ya kiwambo cha seli inayozunguka mfereji wa chakula.
**mucus** /'mju:kəs/ *n.* uteute: aina ya kemikali nzito inayoteleza inayotokana na teziute yenye kazi ya kulinda tishu za tabaka-nje zisikauke, na pia kuzuia viumbe maradhi visidhuru kiumbe.
**mud** /mʌd/ *n.* tope. ~ *hut,* kibanda cha udongo. ~ *wall,* ukuta wa udongo. **~dy** *adj.* -enye matope; -liochafuka. **~guard** *n.* madigadi; (kwa baiskeli) panga.
**muddle** /mʌdl/ *n.* fujo; mkanganyo. *v.t./i.* chafua; fuja; tatiza; kanganya; tibua; vuruga. ~ *along,* boronga.
**mufti** /'mʌfti/ *n.* mufti; nguo za kiraia avaazo mtu anayevaa sare.
**mug** /mʌg/ *n.* magi; kopo; *(colloq.)* baradhuli; mjinga; uso.
**mulch** /mʌl(t)ʃ/ *n.* matandazo: majani yanayotandazwa shinani mwa mche kuhifadhi unyevu. *v.t.* weka matandazo.
**mule** /mju:l/ *n.* nyumbu; baghala. **mulish** *adj.* -kaidi; - shupavu.
**multi** /'mʌlti/ *-prefix* -enye -ingi. *-farious,* -a namna nyingi mbalimbali. **~form**, -enye maumbo mengi. **~lateral**, -enye wahusika wengi.
**multiple** /'mʌltɪpl/ *n.* kigawe. *adj.* -enye sehemu nyingi; -a mara nyingi.
**multiplicand** *n.* kizidishio; hesabu ya kuzidishwa.
**multiplication** /ˌmʌltɪplɪ'keɪʃn/ *n.* kuzidisha.
**multiply** /'mʌltɪplaɪ/ *v.t./i.* zidi; zidisha; ongezeka. **multiplicity** *n.* wingi.
**multitude** /'mʌltɪtju:d/ *n.* wingi; umati. *the ~,* kaumu. **multitudinous** *adj.* - ingi; tele.
**mummy** /'mʌmi/ *n.* mumiani; maiti iliyotiwa mumiani au dawa ya kuhifadhi maiti ili asiharibike; mama (hutumiwa hasa na watoto).
**mumps** /'mʌmps/ *n.* ugonjwa wa matubwitubwi; matukwi; matumbwitumbwi.


muscle cell | seli ya musuli

**munch** /'mʌntʃ/ *v.t./i.* tafunatafuna; guguna; mumunya.

**municipal** mjʊ'nɪsɪp(ə)l/ *adj.* -a manispaa. **~ity** *n.* manispaa; baraza la mji.

**munitions** /mju:'nɪʃnz/ *n.* zana za vita.

**mural** /'mjʊər(ə)l/ *n.* picha iliyochorwa ukutani. *adj.* a ukutani.

**murder** /'mɜ:də(r)/ *n.* uuaji wa mtu kwa kusudi. *v.t.* ua kwa kusudi. **~er** *n.* muuaji. **~ess** *n.* muuaji wa kike. **~ous** *adj.* katili; -a kiuaji.

**murky** /'mɜ:ki/ *adj.* -enye kiza.

**murmur** /'mɜ:mə(r)/ *n.* mvumo; mnong'ono; manung'uniko. *v.i.* vuma; nong'ona; nung'unika.

**muscle** /'mʌsl/ *n.* musuli; msuli; mnofu; mkano. **muscular** *adj.* -a musuli; -enye nguvu ya mwili.

**museum** /mju'zɪ:əm/ *n.* makumbusho.

**mushroom** /'mʌʃrʊm/ *n.* uyoga. ~ *growth,* liokuwa upesi.

**music** /'mju:zɪk/ *n.* muziki. *face the ~,* kabili matatizo kijasiri. **~al** *adj.* -a muziki; -enye kupenda muziki; enye kipaji cha muziki. **~ally** *adv.* kimuziki. **~ian** *n.* mwanamuziki. **~-hall** *n.* ukumbi wa maonyesho.

**must** /məst/ *n.* jambo la lazima. *aux.v.* hapana budi; sharti; lazima; yapasa. *I ~ go,* sina budi kwenda.

**mustard** /'mʌstəd/ *n.* hardali; mhardali.

**mutation** /'mju:'teɪʃn/ *n.* ubadilikaji: mbadiliko wa ghafla wa muundo wa kikemikali wa jeni au kromo-somu katika seli za kiumbe.

**mute** /mju:t/ *n.* bubu. *adj.* kimya; bubu; -siotamkwa.

**mutilate** /'mju:tɪleɪt/ *v.t.* kata; haribu; kata kiungo cha mwili; lemaza. **mutilation** *n.* kilema; ukataji.

**mutiny** /'mju:teni/ *n.* maasi; uasi. *v.i.* asi; halifu. **mutineer** *n.* mwasi. **mutinous** *adj.* -a kuasi; -halifu.

**mutter** /'mʌtə(r)/ *v.t./i.* nung'unika; sema chinichini.

**mutton** /'mʌtn/ *n.* nyama ya kondoo.

**mutual** /'mju:tʃʊəl/ *adj.* -a pande mbili; -a wenyewe; -a wote wawili ~ *affection,* upendano. ~ **agreement**, mapatano. **~ism** *n.* ufaano: hali ya viumbe viwili kuishi pamoja katika hali ya kuambatana na ambapo wote vinafaidika na uhusiano wao. **~ly** *adv.* kwa pamoja.

**muzzle** /'mʌzl/ *n.* pua na mdomo wa mnyama; kitunga; kitundu cha kasiba; mtutu wa bunduki au mzinga. ~ *velocity,* kasi ya risasi. *v.t.* nyamazisha; nyamazisha vyombo vya habari; tia kitunga. msumari.

**mystery** /'mɪstri/ *n.* siri; muujiza; fumbo. **mysterious** *adj.* -a siri; -a fumbo; -sioelezeka.

**mystify** /'mɪstɪfaɪ/ *v.t.* fumba; tatanisha; tatiza. **mystification** *n.* utatanishaji; kitu cha kutatanisha.

**myth** /mɪθ/ *n.* kisasili: ngano zinazoeleza asili ya ulimwengu na vilivyo ndani yake; uwongo; jambo lililobuniwa. **~ical** *adj.* -a kisasili; -a uwongo; a kubuniwa. **~ology** *n.* mithiolojia: elimu ya visasili; visasili.

# Study pages




| | | | |
|---|---|---|---|
| A Map of East Africa | A 2 | Ramani ya Afrika ya Mashariki | A 2 |
| Short History of Kiswahili | A 3 | Historia Fupi ya Kiswahili | A 3 |
| Parts of Speech | A 4 | Aina za Maneno | A 4 |
| Kiswahili Proverbs | A 7 | Methali za Kiswahili | A 7 |
| Figures of Speech | A 8 | Tamathali za Semi | A 8 |
| Fractions | A 9 | Sehemu | A 8 |
| Words that go together | A 9 | Majina ya Makundi | A 9 |
| Computer and Internet Terms | A 9 - A 11 | Istilahi za Kompyuta na Mdahalishi | A 9 - A 11 |
| Common Prefixes and Suffixes | A 11 - A 14 | Vitanguzi na Vikomo | A 11 - A 14 |
| Common Abbreviations | A 14 - A 15 | Mafupisho | A 14 - A 15 |

## East Africa | Ramani ya




international boundary mipaka ya kimataifa

national park mbuga za taifa

capital city mji mkuu

city or town jiji au mji

land over 2000 metres above sea level ardhi iliyo juu ya meta 2000 usawa wa bahari

lake ziwa

mountain mlima

## Historia Fupi ya Lugha ya Kiswahili

Wabantu wa kwanza ambao inasemekana ndiyo chimbuko la Kiswahili waliishi karibu mwa mto Tana kwenye mabonde ya Kaskazini kwenye maeneo ya Shupate na Shungwaya. Lugha walizozizungumza zilikuwa na asili ya kibantu. Kwa mujibu wa mabadiliko ya kijamii na kimakazi watu hawa walianza kutofautiana kimatamshi na kukaanza kuzuka kwa lahaja mbalimbali zikiwemo zile za Kiunguja, Kipemba, Kimafia, Kibajuni, Kingazija na Kimvita.

Majilio ya Waarabu mnamo karne ya 10 A.D yaliziunganisha lugha hizi. Waarabu waliuita mchanganyiko wa lugha hizo kuwa ni lugha ya watu wa pwani 'sawaheli'. Kuanzia hapo msamiati wa Kiswahili ulianza kukua kwa kasi japo miundo na maumbo ya maneno ya Kiswahili hayakuathirika. Utawala wa Waarabu ulileta pia maingiliano baina ya makabila ya mwambao na watu wa bara za ndani. Wa aidha uenezi wa dini ya Kiislamu pia ulichangia ukuzi wa Kiswahili. Kwa mfano, 'Utenzi wa Fumo Lyongo' na 'Utenzi wa Rasi L' ghuli' uliandikwa kwa Kiswahili. Kiswahili kimechukua misamiati mingi katika historia yake ya ukuzi ikiwemo kutoka Kireno (leso, meza, gereza, pesa (peso); Kishirazi (achari, serikali, diwani, sheha); Kiingereza (baiskeli, basi, penseli, mashine, koti); Kijerumani (shule, hela). Wamisheni nao pia walisaidia sana katika uenezi wa Kiswahili na kamusi za kwanza za Kiswahili zilisanifiwa nao.

Kutokana na shughuli za biashara kukua na watu kuhamahama kutoka mwambao na kuingia ndani ya bara hasa katika karne ya 19, lugha hii imezidi kumea hapa Tanzania na imefika Uganda, Burundi, Kongo, Msumbiji na kwingineko. Kiunguja kilichaguliwa kama lahaja sanifu ya Kiswahili kwa vile Zanzibar ilikuwa ni kituo muhimu kwa utamaduni na biashara.

Mijadala, makongamano na warsha nyingi hufanywa ili kuitathmini lugha ya Kiswahili si katika nyanja ya sarufi tu bali pia kuutathmini uwezo wake na kuikuza kama lugha inayokimu haja ya maendeleo ya sayansi na teknolojia.
Hadi leo, lahaja hii imebaki kama kiashirio cha ubora wa matumizi ya Kiswahili. Juhudi kubwa zinafanyika ili kukifanya Kiswahili kitumike katika ngazi zote za taaluma hadi za vyuo vikuu. Kadhalika Kiswahili kinafundishwa karibu duniani kote.

## JINSI YA KUTUNZA MSAMIATI MPYA

Ili kutunza na kukumbuka maneno mapya kuna mbinu mbalimbali unazoweza kuzitumia. Baadhi yao ni:

### KIJITABU CHA MANENO:

| *JOBS* | *KAZI* |
|---|---|
| *secretary* | *katibu* |
| *accountant* | *mhasibu* |
| *barber* | *kinyozi* |

Kielelezo A

| *H* | |
|---|---|
| *honey* | *asali* |
| *however* | *japokuwa* |
| *headline* | *kichwa cha habari* |

Kielelezo B

Nunua daftari ndogo maalumu kwa ajili ya kuhifadhia msamiati mpya. Gawanya kijitabu chako katika mada tofauti kama katika kielelezo A. Pia unaweza kuhifadhi msamiati kialfabeti kama katika kielelezo B. Hifadhi maneno machache utakapokuwa unaanza, kisha zidi kuongeza kila upatapo msamiati mpya.

### KADI ZA MSAMIATI

| SHALLOW | Not deep<br>EXAMPLE<br>The sea is very *shallow* |
|---|---|

Mbinu nyingine ya kutumia ni kuandika neno jipya juu ya kadi na kuziweka kwenye kiboksi. Andika neno jipya upande wa kushoto na upande wa kulia andika maana yake. Baadaye unaweza kujipima kwa kuangalia kama unalikumbuka na kuweza kuangalia maana yake ili kupata uhakika wa maana halisi.

### KUHIFADHI MAANA

Kuna njia nyingi za kuhifadhi maneno mapya, kwa mfano:

1. chora picha ya *butterfly* 
2. andika maana ya neno: salary: the money you receive, usually every month for work
3. andika neno jipya katika lugha yako uliyoizoea: tired –*liochoka*
4. onyesha neno kwa kutumia mfano wa sentensi.

> *Although*, it was raining, we decided to go for a walk (Ingawa kulikuwa na mvua, tuliamua kwenda matembezini

### MAZOEZI

Panga maneno yafuatayo kulingana kwa namna inayofanana na aina za maneno yenyewe.

*autumn, banana, since, above, museum, rich*

### KUHIFADHI TAARIFA

Kuna taarifa kadhaa ambazo ungependa kuzihifadhi kuhusu neno fulani. Tafuta neno, kisha weka taarifa fulani unayoitaka kuhusu neno hilo. Ili kulikumbuka neno hilo litungie mfano:

lazy ( adjectives) → word class
= not wanting to work

Don't be so lazy. Come and help us! → example sentence
adverb – lazily
noun – laziness → related words

## MAZOEZI

Andika taarifa ambazo unahisi ni muhimu kuhusu maneno haya. Tumia kamusi ikibidi

*bleed, deaf, on the ball, fluent, swap*

## JEDWALI NA MCHORO

Kuandika maneno kwa mafungu pia ni njia mojawapo nzuri Tumia kamusi ikibidi

1. maneno katika jedwali:

| MICHEZO | MCHEZAJI | MAHALI |
|---|---|---|
| football | footballer | pitch |
| athletes | athlete | track |
| golf | golfer | course |
| tennis | tennis player | court |

2. maneno katika mchoro




## MAZOEZI

1. Tengeza jedwali kwa kutumia maneno:

Jobs (aina za kazi mbalimbali)
Places of work (vituo vya kazi)
Things people use in their jobs ( zana ambazo watu hutumia katika shughuli zao)

2. Chora mchoro unaoonyesha msamiati unaohusiana na likizo. Unaweza kuugawanya katika mafungu yafuatayo:

places to stay (sehemu za kufikia)
ways of traveling (aina za usafiri)
activities (mambo yatakayofanyika)

## BARUA RASMI

*P. O. Box 7700*
*Dar es Salaam*
*Tanzania*

Your address (but Not your name)

*6th May 2002*

the date

*The Principal*
*Dar es salaam Institute of Technology*
*P. O. Box 53095*
*Dar es salaam*

the name or title of the person you are writing to and his or her address

*Dear Sir or Madam*

begin with:
Dear Sir, Madam, Sirs, Mr, Mrs or Miss (name of the person)

*I am a student in my last year of "O" level, and am interested in becoming an engineer in the future. I am trying to find out what qualifications and experience I would need to train when I finish my studies.*

*I would be grateful if you could send me information about your college and any other relevant information or advice.*

*I look forward to hearing from you.*

*Yours faithfully*

end with:
Yours faithfully (when you began with Dear Sir,etc)
Yours sincerely (when you began with Dear Mr etc)
Yours truly (US)
Sincerely yours (US)

*H Kalala*

## Aina za Maneno

| | |
|---|---|
| Nomino (Majina) | Nomino ni jina la mtu, kitu, mahali au neno linaloelezea pia hali, tendo au jambo hata kama ni la kufikirika.<br>*Mfano:* Zuhura; kabati; Tanzania; ujanja; hasira; ukulima; ujenzi. |
| *Nomino za Pekee (Majina ya Pekee)* | Nomino za pekee ni majina ya vitu visivyokuwa na maumbile ya namna moja.<br>*Mfano:* *John* atakuja leo; *Jumatano* ni siku ya tatu ya wiki; *Kagera* ni mkoa wa *Tanzania.* |
| *Nomino za Kawaida (majina ya kawaida)* | Ni majina ya watu; ndege; wanyama na vitu mbalimbali vyenye maumbile ya namna moja.<br>*Mfano:* hasira, wizi, furaha. |
| *Nomino za Mafungu (majina ya jamii)* | Ni majina yanayotaja vitu au watu katika mafungu. *Mfano:* jeshi, kamati, taifa, matunda n.k. |
| Kivumishi | Kivumishi ni neno ambalo huongeza maana au kutoa habari kuhusu nomino.<br>*Mfano:* mti *mdogo*; kabati *kubwa*; wachezaji *wachache.* |
| *Aina za Vivumishi* | Vivumishi vya maelezo (vivumishi vya sifa)<br>*Mfano:* kiti *kidogo*; mtoto *mrefu*; wanafunzi *wembamba.* |
| *Vivumishi vya Kumiliki* | Vivumishi vya kumiliki huonyesha kuwa kitu au mtu fulani ni mali ya kitu au mtu fulani.<br>*Mfano:* wanyama *wake*; kiti *changu*; watoto *wao.* |
| *Vivumishi vya Idadi* | Kundi lenye maneno haya huonyesha idadi ya watu au vitu fulani. Yaani kundi hili linatufahamisha ni vitu vingapi vinavyohusika au ni watu wangapi wanaoshiriki katika jambo fulani.<br>*Mfano:* wanamaji *wengi*; ndege *wachache*; joto *jingi*; mikate *mitano*; makuli *wanane*; mjukuu wa *kwanza.* |
| *Vivumishi vya Kuonyesha* | Vinatumika kuonyesha kwamba ni kitu au mtu fulani ndiye anayezungumzwa.<br>*Mfano:* kijana *huyu*; kuku *hawa*; mzungu *yule.* |
| *Vivumishi vya a-unganifu* | Neno moja au zaidi linalosifia nomino fulani.<br>*Mfano:* jumba *la* wananchi; lugha *ya* taifa; baiskeli *ya* kitoto; habari *za* kuhuzunisha. |
| *Vivumishi vya Pekee* | Vivumishi hivi ni vya aina tano: -enye, -enyewe, -ingine, -ote na -o-ote.<br>*Mfano:* Amejikata yeye *mwenyewe*; Mtoto *mwenye* kilema alidondoka; Watu *wingine* walikuja; Chakula *chote* kimemalizika; Lete kitu *chochote* ukija. |

*Kitenzi*

Neno linaloeleza waziwazi kuwa kitu au mtu anafanya jambo fulani linaitwa *kitenzi.*

*Mfano:* Asha *anakula* wali; Mwingira *anaendesha* baiskeli; Yeye *hali* wala *hanywi.*

*Tabia za Vitenzi*

1. **kuonyesha tendo lenyewe**
   cheza
   kula

2. **kuonyesha wakati tendo linapotendeka**
   a*na*kula (wakati uliopo, sasa)
   a*ta*kula (wakati ujao, baadaye)
   a*li*kula (wakati uliopita, zamani)

3. **kuonyesha hali ya tendo**
   a*me*kula (tendo limetimia)
   a*na*kula (tendo linaloendelea)
   *hu*la (tendo la kuzoea, kawaida)

4. **kuonyesha masharti**
   a*ki*la
   a*nga*likula, a*nge*kula

5. **kuonyesha kauli ya tendo**
   cheza (kutenda)
   chezwa (kutendwa)
   chezeka (kutendeka)

6. **kuonyesha kuyakinisha au kukanusha**
   atakula : hatakula
   nimecheza: sijacheza (sikucheza)

*Aina za Vitenzi*

(a) Vitenzi halisi
(b) Vitenzi vikuu na vitenzi saidizi
(c) Vitenzi vishirikishi

*Kitenzi Halisi*

Ni neno linaloarifu jambo linafanywa na mtu, mnyama, mdudu au kitu kingine chochote. Kitenzi halisi kinaweza kikatokea kama kitenzi kikuu pekee au kitenzi kikuu kilichoambatana na kitenzi-saidizi kimoja au zaidi.

*Mfano:* mtoto *amekula*; mhudumu amewahi *kukutayarishia* chakula;
mtoto alikuwa amekwisha *kula* chajio; mimi *ni* mwalimu;
wewe *si* mwanafunzi

*Kitenzi Kikuu na Kitenzi-Saidizi*

Kitenzi kikuu hutoa taarifa kamili kuhusu tendo lenyewe linalofanyika.

*Mfano:* mchezo *umemalizika*; kijana *anachunga* ng'ombe.

*Kitenzi-Saidizi*

Husaidia kitenzi kikuu ili sentensi ipate maana kamili na kwa wakati unaotakiwa.

*Mfano:* *babu alikuwa* akichunga mbuzi; Paulo *ataweza* kuchimba shimo

| | |
|---|---|
| *Kitenzi kishirikishi* | Vitenzi vishirikishi huchukua viambishi vya wakati ingawa huweza kuchukua viwakilishi nafsi-viambata au viambishi -ngeli. Viambishi: *ni, si, ndi, li*<br>Mfano: Mimi *ni* mfuga kuku mashuhuri<br>Mashaka *si* fundi mzuri<br>Mimi *ndiye* (ndimi) babu yake<br>Sisi *tu* wanafunzi wa shule ya msingi |
| Vielezi | Kielezi ni neno au maneno yanayoelezea kuhusu tendo linavyofanyika.<br>*Mfano:* Angelo anaumwa *sana*; ameondoka hapa sasa *hivi*. |
| *Aina za Vielezi* | |
| *1. Vielezi vya Mahali* | Huelezea matendo kuhusu mahali yanapofanyika.<br>*Mfano:* mtoto ametoka *nje*, ameelekea *Kaskazini*; ametoka *chooni*; waliendesha baiskeli *barabarani*; |
| *2. Vielezi vya Wakati* | *Mfano:* tulikula pilau *juzi*; shule itafunguliwa *Jumatatu*. |
| *3. Vielezi vya Idadi* | Hutujulisha kwamba tendo fulani limetokea mara ngapi au kwa kiasi gani.<br>*Mfano:* Watoto huanguka *mara kwa mara*. |
| *4. Vielelezi vya Namna* | Hueleza jinsi tendo linavyofanyika.<br>*Mfano:* kobe anatembea *taratibu*; tunakuja kwa *baiskeli*; alipoitwa alikuja *upesi*. |
| Viwakilishi | Neno linalotumika badala ya jina kama vile: *mimi, sisi, wao, yeye, wangu*. |
| *Viwakilishi Nafsi (mtenda)* | *Mfano:* *yeye* ni kijana; *mimi* ni mdogo; *sisi* ni wanafunzi wa chekechea. |
| *Viwakilishi vya Kumiliki* | Viwakilishi vyenye mizizi *ya -angu, -ako, -ake, -etu, -enu,* na *-ao*.<br>*Mfano:* *mwetu* hamwingiliki; kuku ni *wangu* bata ni *wako*. |
| *Viwakilishi vya Kuonyesha* | Ni viwakilishi vyenye mizizi ya *ha-, -hi, -hu,* na *-le*.<br>*Mfano:* nitakula (chakula) *hiki*; *yule* hapendi viazi wala ugali; *hawa* ni watoto wa Shule ya Kigurunyembe. |
| *Viwakilishi vya Kuuliza* | Vina mizizi ya -pi, -ngapi, nani, nini.<br>*Mfano:* *kipi* kinachokusikitisha?; *wangapi* mnawaona na *vingapi* hamvioni?; *nani* wanapendelea Simba?; *nini* anachosema? |
| *Viwakilishi vya Kurejesha* | Hurejesha tendo kwa mtenda au kwa mtendwa. Huundwa na mzizi wa *-amba* na *-o- rejeshi*.<br>*Mfano:* mtu *ambaye* ulimtaja ametokea; ali*cho*kisema hakieleweki. |

| | |
|---|---|
| Viunganishi | Ni maneno au vikundi vya maneno yanayounganisha neno na neno, neno na kikundi cha maneno au sentensi na sentensi. Kuna viunganishi vingi, baadhi yao ni: *lakini, ingawa, ama, mpaka, labda, yaani, halafu,* ila n.k. |
| *Viunganishi-Vitegemezi* | *Mfano:* anakula *lakini* hanywi.<br>*Mfano:* nitakuja *ingawa* sitafanya kazi; analia *kama kwamba* amepigwa bakora |
| *Viunganishi-Vihusishi* | Hutokea katikati ya neno zima.<br>*Mfano:* uli*po*kuja, u*li*ambiwa sipo; wali*vyo*kusanya sivyo<br>Ni maneno au vikundi vya maneno vinavyounga tungo mbili.<br>*Mfano:* alikuja *lakini* hakukaa; mama *na* mwana wamefanana |
| Vihisishi | Maneno yanayodokeza hisia kama vile furaha, uchungu, mshangao, mshituko. Haya si maneno ya lazima kutumika bali yakitumika hupamba lugha na kuleta mkazo fulani.<br>*Mfano:* *Ala!* Wewe kumbe ndio yule mtunzi maarufu?<br>*Lo!* Sikujua kuwa wewe ni jabari namna hivi. |

## Kiswahili Proverbs Methali za Kiswahili

**Chanda chema huvikwa pete**
A favourite finger gets a ring on.
*An award or privilege usually goes to the one who deserves it.*

**Kazi mwanamandanda, kulala njaa kupenda**
Work is an obedient child, sleeping hungry is one's choice.
*If you work hard you will succeed, if you don't work hard, you are bound to live a miserable life.*

**Mgaagaa na upwa hali wali mkavu**
A person who walks and searches thoroughly around a beach never eats "dry" rice (rice with no fish stew).
*If you work hard looking for something, you will never come out empty handed.*

**Mtumai cha ndugu hufa masikini**
One who relies on one's relative's property, dies poor
*Encourages self-reliance.*

**Dunia duara**
The Earth is round.
*Go wherever you go, but you'll return to the same old place.*

**Mama ni mama japokuwa rikwama**
A mother is a mother even if it is a "coolie's cart."
*Even a bad mother is still a mother worthy of respect, love and care.*

**Mchezea wembe humkata mwenyewe**
He, who plays with a razor, cuts himself.
*If one gets involved in a dangerous exercise, one is bound to get harmed.*

**Njaa mwanamalegeza, shibe mwanamalevya**
Hunger weakens, but food satisfaction intoxicates.
*When one is hungry, one becomes weak but when stomach-full one becomes lazy to work.*

### Nazi mbovu harabu ya nzima

A bad coconut renders good ones bad. *A bad person or thing in the midst of good ones can easily spoil either the attributes or even the character of the good ones.*

### Umdhaniaye ndiye kumbe siye

The one whom you think is the right one is the wrong one *You are barking up a wrong tree.*

### Pema usijapo pema ukipema si pema tena

A nice place is one where you have not dwelt on, once you do, ceases to be good.
*Often times you get fascinated with things you have little knowledge about. Once you have knowledge and experience with that thing it ceases to interest you.*

### Usiache mbachao kwa msala upitao

Don't abandon your old rug for a passing mat. *Value more what is yours and more permanent rather than a temporary thing that is not yours even though it is better than yours.*

---

## Figures of Speech Tamathali za semi

| | |
|---|---|
| 1. Simile | (Tashibiha) |
| Fat as a calabash tree | Mnene kama mbuyu |
| Angry as fire | Mkali kama moto |
| 2. Metaphor | (Sitiari) |
| Water is life | Maji ni uhai |
| Education is wealth | Elimu ni mali |
| 3. Personification | (Tashhisi) |
| Death entered the town | Kifo kiliingia mjini |
| Fear enveloped the atmosphere | Hofu ilitanda anga zote |
| 4. Assonance | (Takriri) |
| Haba na haba hujaza kibaba. | Many a pickle makes a mickle |
| 5. Tanakali sauti | (Onomatopoeia) |
| The cat cried 'meuw' | Paka alilia 'nyau' |
| The lion roared 'grr' | Simba alinguruma 'grr' |
| 6. Euphemism | (Tasifida) |
| To go to the water closet (lavatory) instead of going to the toilet | Kwenda msalani badala ya kwenda chooni |
| To help oneself instead of to urinate | Kujisaidia badala ya 'kukojoa' |

## Fractions Sehemu



a half | nusu



a quarter | robo



an eighth | thumni



three quarters | robo tatu

## Words that go together Majina ya Makundi

a pair of shoes jozi ya viatu
a string of beads mkufu wa shanga
a bar of chocolate mchi wa chakleti
a row of houses msururu wa nyumba
a bundle of newspapers bunda la magazeti
a drop of water tone la maji
a bunch of flowers shada la maua
a crowd of people kundi la watu
a slice of bread slesi ya mkate
a pile of books rundo la vitabu
a queue of people foleni ya watu
a lump of coal chungu ya mkaa

## Computer and Internet Terms Istilahi za Kompyuta na Mdahalishi



address bar mstari anwani
bookmark kariri, hifadhi
computer kompyuta, tarakilishi
cd-rom sidiromu
chat rooms kumbi za gumzo
cursor kasa
disk diski
data data
diskette disketi
drive kisukumishi
dvd-rom dividiromu
electronic world ulimwengu pepe
e-mail barua pepe, tarifalishi
fax nukushi
fax machine nukunishi
floppy diskette diski laini
hard disk diski ngumu
hard drive kisukumo msingi
homepage ukurasa wa mtandao
hyperlink kiungwa, kiungwa-hipa
hypertext kiungo, kiungo-hipa
keyboard kibodi
keyword kidokezo
menu menyu
modem modemu
monitor monita, skrini
mouse mausi, kipanya
network mtandao
printer printa
program programu
processor prosesa, kichakato
scanner skena
search engine mashine taftishi
server seva
sound card kadi sauti
webcam kamera pembuzi
webmaster msimamizi wa kurasa pembuzi
website kurasa pembuzi, tovuti

internet mdahalishi, mtandao wa internet
ISP (internet service provider) mtoaji huduma za mdahalishi
random access memory (RAM) kumbukumbu ya fikio nasibu (KUFINA)
world wide web (www) mfumo enezi wa habari katika mdahalishi

## Computer and Internet

**Internet** can be defined as a **network** of networks. Group of networked computers, such as those at universities, organizations and companies all connected together. The Internet allows people across the whole world to find out information and share it with others. Any organization, company or individual can create a website, providing information about themselves or certain services they offer.

There are several services that are provided on the Internet. One can meet people by exchanging messages in a **chat room E-mail (electronic mail)** is an electronic equivalent of the postal service. It involves reading and sending electronic mail. A user composes an e-mail message on his/her computer, and then transmits it immediately at a touch of a button to any of the millions of the other users on the Internet. As for **Internet Relay Chat (IRC)**, unlike the e mail, IRC lets you type messages to other users who are online at the same time as you. Messages are more like sentences and replies are immediately seen on the computer **screen**. You can make video and vocal connections as well. People you talk to over in chat rooms could be anywhere in the world, and generally are On the Internet, you can find virtually any information you want. A **search engine** allows you to search for material in its enormous directory of **websites**

## Kompyuta na Mdahalishi

Prosesa ni chombo kidogo kinachoendesha mfumo mzima ndani ya kompyuta kwa kusababisha mfanyiko tendani. Kasi ya prosesa hupimwa kwa megahezi (MHz) au gigahezi (GHz). Kompyuta huhifadhi taarifa kama vile programu, nyaraka, michezo n.k. katika diski ngumu. Nafasi ya diski ngumu ya kawaida ina uwezo wa kuhifadhi data nyingi mno. Programu inapofunguliwa hutumia kumbukumbu ya fikio nasibu (KUFINA). Na kila kukiwa na nafasi nyingi katika diski ngumu ndipo KUFINA hurahisisha programu nyingi kuweza kutumika kwa wakati mmoja.

Siku hizi kompyuta huwa tayari zina modemu zinazoweza kuunganishwa kwenye simu. Hii inamuwezesha mtumiaji wake aweze kutuma barua pepe na nukushi kwa urahisi mara akishajiunga na mdahalishi. Tena ikiwa kompyuta ina sidiromu, spika na kadi sauti mtumiaji anaweza kusikiliza muziki na ikiwa ana dividiromu anaweza kuangalia filamu. Ili kuweza kupiga chapa toleo fulani italazimu kuiunganisha kompyuta na printa. Vifaa vingine vinavyoweza kuunganishwa kwenye kompyuta ni skena inayokopi taswira ya picha au chapa ya maneno na kamera dijitali inayochukua picha halisi.

Kompyuta inaweza kutumika kwa kufanya shughuli mbalimbali kutegemea na programu zilizomo. Mdahalishi ni mtandao wa mawasiliano wa kimataifa unaoziunganisha kompyuta zote duniani. Mtandao huu huwawezesha watu kupokea na kupashana habari. Mfumo enezi wa habari katika mdahalishi (world wide web - www) ni mtandao unaomwezesha mtumizi kupokea taarifa za picha, muziki, programu za kompyuta kwenye kompyuta yake. Unaweza kutumia mdahalishi kutafuta taarifa yoyote katika nyanja anuwai. Isitoshe, shirika, chuo, taasisi au mtu binafsi anaweza kujiundia ukurasa wake pembuzi kwa minajili ya

kujitangaza, kuuza bidhaa au hudumu fulani. Msimamizi wa kurasa pembuzi anaweza kujua ukurasa gani umepitiwa mara ngapi na hivyo kujua umaarufu wake. Unaweza pia kuwasiliana na watu ulimwenguni kote kwa kutumia barua pepe au hata kuonana uso kwa uso ukiwa na kamera pembuzi Kadhalika unaweza kuzungumza na watu katika kumbi za gumzo. Lakini kabla ya yote hayo ili kujiunga na mdahalishi itakulazimu uwasiliane na kampuni inayotoa huduma hiyo inayojulikana kama Mtoaji Huduma za Mdahalishi (MHM).

Mhudumu huyo anaweza kukupatia anwani ya barua pepe na nafasi katika seva yao ili uweze kujiundia ukurasa pembuzi binafsi. Tena anaweza kukupatia mashine taftishi inayoweza kukusaidia kutafuta habari yoyote ile. Na ili kuanza kutafuta habari fulani ingiza neno kidokezo au maneno vidokezi na hapo mashine taftishi itakupatia muhtasari wa kurasa pembuzi zote zenye habari zinazohusiana na mada unayoitafuta. Tena utafuata kiungwa ambacho kitakuwa na rangi maalumu (kwa kawaida ni buluu) na hapo ukurasa pembuzi utafunguka.

Ikiwa unaijua anwani ya ukurasa pembuzi fulani basi chapa kwenye mstari wa anwani na utapelekwa hadi kwenye ukurasa pembuzi husika. Ikiwa unadhani kuwa utaupitia tena ukurasa huo basi ni vyema ukauhifadhi katika kompyuta. Mfano wa anwani ni http://www.oup.com ambayo hutamkwa www dot yahoo dot com.

## Common Prefixes and Suffixes Vitangulizi na vikomo vitumikavyo sana

Maana ya **prefixes** ( vitangulizi) huelezwa chini ya maneno yenyewe katika kamusi hii lakini **suffixes** (vikomo) haviandikwi mbalimbali kama vitangulizi vionyeshwavyo na kwa sababu hii vitaelezwa hapa chini.

### Common Prefixes

| | | | |
|---|---|---|---|
| *acro-* | *dis-* | *mid-* | *re-* |
| *air-* | *ex-* | *milli* | *self-* |
| *anglo-* | *fore-* | *mis-* | *semi-* |
| *ante-* | *grand-* | *multi-* | *step-* |
| *anti-* | *great-* | *multi-* | *sub-* |
| *arch-* | *hecto-* | *over-* | *super-* |
| *be-* | *hydro-* | *pan-* | *tele-* |
| *bi-* | *il-* | *poly-* | *trans-* |
| *by-* | *im-* | *post-* | *ultra-* |
| *co-* | *in-* | *pre-* | *un-* |
| *contra-* | *ir-* | *pro-* | *under-* |
| *deci-* | *kilo-* | *pseudo-* | *vice-* |
| *demi-* | *mal-* | *radio-* | *well-* |

### Common Suffixes

**-able, -ible** Hutumika kwa kufanya **adjectives** kwa Kiingereza , lakini kwa Kiswahili kikomo huongezwa katika **verb**, kwa kuleta maana hii. (a) that can be is liable to be: ponya = cure, ponyeka = be curable; pata = obtain, patika = be obtainable; soma = read, someka = be readable, legible. (b) having the qualities of, -enye tabia ya: comfortable, fariji, tuliza = comfort, -enye kufariji, kutuliza =

comfortable; peace =amani, peaceable = -a amani. (c) likely to, -a kuelekea ku (fanya); kubali = agree, -kuelekea kukubali = agreeable; kujua = know, -a kuelekea kujua =knowledgeable or like to know.

**-ably, -ibly** Hutumika kwa kugeuza adjs zanye vikomo -able, -ible ziwe adverbs, e.g. peaceably, legibly, comfortably.

**-al** Hutumika kwa kugeuza **nouns** ziwe **adjectives** e.g. baptisimal, -a ubatizo, national, -a taifa.

**-age** Hutumika kwa kufanya **nouns** maana yake ni kama vile gharama ya...postage, gharama ya posta, haulage gharama ya kubeba kwa lori.

**-(a)n** Hutumika kwa kufanya **nouns** na **adjectives** e.g. African, American, republican.

**-ance, -ence** Hutumika kwa kugeuza **verbs** ziwe **nouns** maana yake ni tendo la, hali ya. (a) avoidance, kuepuka, kuepua; annoyance, kuudhika; abesence, kutohudhuria. (b)kitu cha kufanyia: hindrance, kizuizi,; conveyance, chombo cha kuabirisha.

**-ant, -ent** (a) Hutumika kwa kugeuza **verbs** ziwe **adjectives**, triumphant, -a kuonyesha furaha kuu, -a ushindi, -a shangwe; peristent, -a kuendelea bila ya kubadilika. (b) kwa kufanya **nouns** kuonyesha mtenda au ala: applicant, mwombaji; irritant, kitu kiudhicho; assistant, msaidizi; superintendent, msimamizi; student, mwanafunzi.

**-ary, -ory** (a) Hutumika kwa kufanya **adjectives** maana yake - kutumika kwa, a kuleta: exemplary -a kuleta mfano; advisory, -a kutumika kwa kuleta shauri. (b) Hutumika kwa kufanya **nouns** kwa maana ya mtu afanyaye kitu au kitu kitendacho jambo: boundary, mpaka; commentary, maelezo, -a desturi; secondary, -a pili; contradictory, -a kubishana; obligatory, -a lazima.

**-dom** Hutumika kwa kufanya **nouns** (a) hali ya kuwa: freedom, uhuru. (b) cheo cha , milki ya: kingdom, milki ya mfalme.

**-en** Hutumika kwa kufanya **verbs** (a) kutoka **adjectives**, e.g. short = fupi, shorten =fupisha; soft =laini, soften = lainisha. (b) kutoka noun: length = fanya refu; hearten = tia moyo.

**e (n)** Hutumika kwa kufanya **adjectives** ikimaanisha cha kitu gani: (a) wooden, -a mti, -a mbao; woollen, -a sufi. (b) maana yake ni cha kufananana: silken, kama hariri; golden, kama dhahabu.

**-e** (r) Hutumika kwa kupambanisha. long = refu, longer = refu zaidi, smaller = -dogo zaidi.

**-er, -or** Hutumika kwa kufanya **nouns**: (a) mtu afanyaye kitu au kitu kifanyacho: teacher, mfundishaji; learner, msomaji; actor, mchezaji; survive, okoka; survivor, aliyeokoka; elevator, mtambo wa ngazi. (b) mkazi: villager, mkazi wa kijiji.; Londoner, mkazi wa jiji la London.

**-e, ry** Hutumika kwa kufanya **nouns** (a) mahali pa kufanyizia: (oil, sugar) refinery kinu cha kusafishia au kutengenezea mafuta, sukari. (b) hali ya kuwa: slavery, utumwa, robbery, wizi.

**ess,** -a kike: manageress, meneja mwanamke; heiress, mrithi mwanamke; lioness, simba jike.

**-(e) st** Kwa kupambanisha katika cheo cha kupita yote: strongest, -a nguvu kushinda -ote; smallest, -dogo mno; widest, -pana kabisa.

**-ful** Huongezwa mwisho wa **nouns** (a) kwa kufanya **adjective**, wonderful , -a ajabu; plentiful, tele; truthful, -a kusema kweli.

**-hood** Hutumika kwa kufanya **nouns** (a) wakati au hali kuwa: manhood, utu uzima; boyhood, ujana. (b) jamii ya: priesthood, upadri, jamii ya makuhani (ya makasisi); brotherhood, udugu, umoja wa watu.

**-ic** (al) Hutumika kwa kufanya **adjectives**, -enye hali ya , -a namna ya: alcaholic, -a vileo: artistic , -a msanii, alphabetic(a.l) -a kialfabeti.

**-ian** Hutumika kwa kufanya **nouns** na **adjectives** -a: -enye kuhusu: Christian, Mkristo, -a Kikristo: electrician, fundi umeme: musician, mwanamuziki Austrian, -a Austria (taz. -(a) n.).

**-ify** Hutumika kwa kufanya **verbs**, fanya au -wa: e.g. simple =rahisi, simplify = fanya kuwa rahisi; solidify = kuwa ngumu, mango; glorify = tukuza.

**-ing** Hutumika katika shina la **verb** kwa kufanya (a) the **present participle**, e.g. swim = ogelea, swimming = akiogelea. (b) the participial adjective e.g. amuse = chekesha, amusing = -a kuchekesha: pleasing, -a kupendeza. (c) the gerund ( verb inayofanya kazi ya noun) e.g. go = enda, the going = kwenda, mwendo: seeing is believing, kuona ni kusadiki. (d) kitu kilichofanyizwa: the binding of a book, jalada: floor sweepings, takataka iliyofagiliwa; wood shavings, takataka za mbao. (e) **nouns** ya kuonyesha jumla ya vitu pamoja: e.g. ship = meli, shipping = jamii ya meli (ya nchi fulani): bedding, shuka, blanketi, mito: washing, nguo za kufuliwa.

**-ish** Hutumika kwa kufanya **adjectives** maana yake: (a) kama; -a kufalia: foolish , -jinga -pumbavu: childish, -a kitoto. (b) kidogo si sana: oldish, -zee kidogo. (c) (hasa pamoja na rangi) -a kuelekea kuwa: greenish, kijani kibichi kidogo.

**-ism** Hutumika kwa kufanya abstract **nouns** (yaani ya kudhanika tu). (a) kutoka verbs zenye viambishi -ise, -ize, e.g. baptism, criticism. (b) kwa kuonyesha matengeneo au mafundisho: communism, socialism conservatism. (c) kwa kuonyesha tabia ya, sifa ya: heroism, ushujaa: barbarism, ushenzi.

**-ist** Hutumika kwa kufanya **nouns** ikiwa na maana ya mwenye kufanya kazi ya...tobacconist, muuza sigara, tumbaku; stadi wa kupiga ala ya muziki: pianist, violinist.

**-itis** Hutumika kwa kufanya **nouns** hasa majina ya magonjwa: appendicitis, bronchitis.

**-(i) ty** Hutumika kwa kufanya abstract **nouns** ikiwa na maana ya hali ya: loyalty, kuwa -aminifu; profanity, kufuru kwa Mwenyezi Mungu; penalty, adhabu.

**-ize** Hutumika kwa kufanya **verbs**, maana yake ni fanya au -wa: harmonize, patanisha, linganisha matao ya sauti; anglicise, fanya kuwa ya Kiingereza; legalize, halalisha; materialize, tokeza kwa umbo.

**-less** Hutumika kwa kufanya **adjectives** (a) bila, pasipo: childless, -sio na watoto; homeless, -sio na makao; countless, -siohesabika. (b) kwa kuleta kinyume cha verb e.g. cease = koma, ceaseless = -siokoma, bila ya kukoma; tireless, -siochoka.

**-logist** Hutumika kwa kufanya **nouns** maana yake ni stadi jambo taaluma fulani: geologist, stadi wa jiolojia.

**-logy** Hutumika kwa kufanya **nouns** maana yake majina ya elimu au mafundisho: geology, biology, theology.

**-ly** (a) Hutumika kwa kugeuza **adjectives** ziwe **adverbs** e.g. recent = -a siku hizi, recently = siku hizi. (b) Hutumika kwa kugeuza **nouns** ziwe adjectives zenye maana kama, -a kufalia: manly, -a kufalia mtu mzima; brotherly , -a ndugu; ghostly, kama mzuka. (c) Hutumika kwa kugeuza nouns ziwe **adverbs** na **adverbs** ziwe **adjectives** - hourly, -a kila saa; daily, -a kila siku; yearly, -a kila mwaka: kama adverbs, he went daily to work, alikwenda kila siku kufanyakazi; hourly recurrent fever, homa yenye kurudiarudia kila saa.

**-ment** Hutumika kwa kufanya **nouns** na maana yake ni tendo, neno au hali ya kufanya au kufanywa: enjoyment, furaha, raha,; management, utawala, improvement, uboreshaji; amazement, mshangao.

**-ness** Hutumika kwa kufanya **nouns** maana yake ni hali ya kuwa:goodness, wema; blackness, weusi; carefulness, hadhari, uangalifu.

**-(i)ous** Hutumika kwa kufanya **adjectives** na maana yake ni -a kama, -enye:ambitious, enye tamaa (ya kukuza hali); religious, a dini; dangerous, -a hatari; joyous, -enye furaha.

**-ship** Hutumika kwa kufanya **nouns** ikimaanisha (a) tabia au hali ya kuwa: membership, hali ya kuwa mwanachama; friendship, urafiki ; ownership, umiliki. (b)ustadi: horsemanship, ustadi wa kupanda farasi. (c) cheo: headship, kuwa mkuu wa chuo; apprenticenship, uanafunzi.

**-tion** Hutumika kwa kufanya **nouns** maana yake: (a) tendo la ku ..., hali ya ku .., e.g. oppose zuia, pinga, opposition, upingaji au hali ya kupinga; action, tendo; addition, kujumlisha, kuongeza. (b) hali ya kuwa...ed: e.g be exhausted, choka sana, exhaustion, uchovu. revision, kusahihisha, mapitio.

---

## Common Abbreviations Mafupisho yatumiwayo sana

| | |
|---|---|
| **A.C.** | alternating current, mkondo geu wa umeme |
| **A.D.** | (Latin) Anno Domini, tangu kuzaliwa kwa Yesu Kristo |
| **A.H.** | mwanzo wa mwaka wa Kiislamu kuanzia mwaka 622 A.D |
| **a.m.** | ante meridian, kabla ya adhuhuri |
| **Apr.** | April |
| **Aug.** | August |
| **Ave.** | avenue |
| **B.A.** | Bachelor of Arts |
| **B.C.** | Before Christ |
| **B.Litt.** | Bachelor of Letters |
| **Bros.** | Brothers |
| **B.Sc.** | Bachelor of Sciences |
| **C. (Latin)** | centum, mia moja (100) |
| **C.** | Centigrade |
| **c. cent (s);** | century; circa |
| **Capt.** | Captain |
| **Cent.** | Centigrade; Century |
| **Cf.** | compare, kama, kwa mfano |
| **C.I.D.** | Criminal Investigation Department, Idara ya Polisi ya Upelelezi wa makosa ya jinai |
| **cm.** | centimeter |
| **C.O.D.** | cash to be paid on delivery, malipo yalipwayo baada ya kupokea mzigo |
| **Col.** | Colonel |
| **Co-op.** | Co-operative society, Ushirika |
| **Cub.** | Cubic |
| **Cwt.** | Hundred weight |
| **D.D.** | Doctor of Divinity |
| **Dec.** | December |
| **Deg.** | Degree |
| **Dept.** | department |
| **D.Litt.** | Doctor of Literature |
| **D.O.** | District Officer |
| **Dr.** | Doctor |
| **D. Sc.** | Doctor of Science |
| **Ed.** | Editor |
| **Etc.** | (Latin) et cetera, and the other things |
| **Exc.** | Except |
| **F.** | Fahrenheit |
| **Feb.** | February |
| **Fig.** | Figure, diagram |
| **Ft.** | foot, feet |
| **Gen.** | General |

| | |
|---|---|
| G.M.T. | Greenwich Mean Time |
| H.E. | His Excellency |
| H.H. | Her (His) Majesty |
| Hon. | The Honorable, Honorary |
| h.p. | horse power, kipimo cha nguvu za mashine |
| Hr(s) | hours |
| i.e. (Latin) | id est, that is |
| Jan. | January |
| Jr. | junior |
| Jul. | July |
| Kg. | Kilogram(me) |
| Lat. | Latitude |
| Lat. | Latin |
| Lb. | Pound(s) in weight, ratili |
| Lieut. | Lieutenant |
| Litt. D. | Doctor of Letters |
| LL.B. | Bachelor of Laws |
| Long. | Longitude |
| Lt. | Lieutenant |
| Ltd. | Limited |
| M.A. | Master of Arts |
| Maj. | Major |
| Mar. | March |
| M.D. | Doctor of Medicine |
| mm. | millimeter (s) |
| M.O. | Medical Officer |
| MS; MSS. | Manuscript (s) |
| M.V. | Motor Vessel |
| N. | North |
| N.B. (Latin) | nota bene, note well |
| No. | Number |
| Nos. | Numbers |
| Nov. | November |
| N.Y. | New York. |
| N.Z. | New Zealand |
| Oct. | October |
| O.K. | All correct, agreed |
| O.T. | Old Testament |
| Oz. | Ounce, wakia |

| | |
|---|---|
| p. | page; participle; past |
| Ph.D. | Doctor of Philosophy |
| Pl. | plural |
| P.M. | Prime Minister |
| p.m. | post meridian |
| p.p. | pages, participle |
| Pres. | President |
| Prof. | Professor |
| Pt. | Pint |
| P.T.O. | please turn over |
| Q.E.D. (Latin) | Quod erat demonstrandum |
| Qt. | Quarts |
| S. | Saint; South |
| Sat. | Saturday |
| Sen., Senr., Sr. | senior |
| Sept. | September |
| Sergt, Sgt. | Sergeant |
| S.O.S. | Save our souls |
| Sq. | square |
| t. | ton (s) |
| Thurs. | Thursday |
| Treas. | Treasurer |
| Tues. | Tuesday |
| U.N. | The United Nations |
| US, U.S.A | United States (of America) |
| V.I.P. | very important person |
| Viz. | namely, yaani |
| Vol. | Volume |
| W. | West |
| W.H.O. | World Health Organization |
| Wt. | Weight |
| Xmas. | Christmas |
| Yr (s). | year(s); your (s) |

# Nn

**nail** /neɪl/ *n.* ukucha; msumari. *on the ~,* mara moja. *hit the ~ on the head,* sema au kufanya kama itakiwavyo. *v.t.* gongomea, pigilia *the ~ eye,* kwa macho angavu. **~ly** *adv.* uchi; bila kificho; bayana. **~ness** *n.* uchi; utupu.

**naive** /nʌɪ'i:v/ *adj.* -nyofu; sio na hila; jinga; -shamba. **~te** *n.* unyofu; ukweli; ujinga.

**naked** /'neɪkɪd/ *adj.* -tupu; uchi; -siofunikwa. *with the ~,* kwa macho angavu. **~ly** *adv.* uchi; bila ya kificho; bayana. **~ness** *n.* uchi; utupu.

**name** /neɪm/ *n.* jina; sifa; mtu mashuhuri. *call sb. ~s,* tukana; kashifu. *not have a penny to one's ~,* - wa maskini hohehahe. *win a good ~ for oneself,* jipatia sifa njema. *v.t.* taja; ainisha; -a jina; toa bei. **~less** *adj.* -sio na jina; -baya sana hata kutostahili kutajwa; -sioelezeka. **~ly** *adv.* yaani. **~sake** *n.* somo; wajina.

**nape** /neɪp/ *n.* ukosi; kikosi.

**napkin** /'næpkɪn/ *n.* **1.** kitambaa cha kufutia mikono hasa mezani; winda; kitambaa avalishwacho mtoto mchanga kupitia mapajani kuzuia mkojo; **2.** nepi.

**narrate** /nə'reɪt/ *v.t.* hadithia; simulia. **narration** *n.* masimulizi; usimuliaji. **narrative** *n./adj.* masimulizi; hadithi; -a masimulizi. **narrator** *n.* msimuliaji.

**narrow** /'nærəʊ/ *adj.* -embamba; -dogo; -a shida; chache; chupuchupu; finyu. *a ~ escape,* ponea chupuchupu. **~ly** *adv.* kwa shida; kidogo tu; kwa uangalifu. **~-minded** *adj.* -enye mawazo finyu.

**nasal** /'neɪz(ə)l/ *n.* nazali. *adj.* a pua, -a puani; -a nazali. **~ize** *v.t.* nazalisha.

**nasty** /'nɑ:sti/ *adj.* -chafu; -a kuchukiza; -enye chuki; -enye hatari; -sio murua; -baya.

**nation** /'neɪʃn/ *n.* taifa. **~al** *n.* raia; mwananchi. *adj.* -a taifa; -a watu wote. **~ anthem**, wimbo wa taifa. **~ assembly**, bunge. **~ debt**, deni la taifa. **~ grid**, mtandaoumeme wa taifa: mtandao wa nyaya na transfoma za umeme uwezeshao umeme kusambazwa nchi nzima. **~ monument**, kumbukumbu ya taifa. **~ park**, mbuga ya taifa. **~ service**, jeshi la kujenga taifa; kipindi cha kujenga taifa. **~alism** *n.* utaifa; uzalendo; upiganiaji uhuru. **~alist** *n.* mzalendo; mpigania utaifa. **~ality** *n.* uraia. **~alize** *v.t.* taifisha; andikisha uraia. **~alization** *n.* utaifishaji.

**native** /'neɪtɪv/ *n.* mwenyeji; mzalia. *adj.* -enyeji; -a asili; -a kimaumbile. *your ~ land,* nchi yako ulipozaliwa. *~ ability,* uwezo wa kimaumbile. **nativity** *n.* uzaliwa; siku ya kuzaliwa.

**natural** /'nætʃrəl/ *adj.* -a asili; -a kawaida; -a maumbile; -a lazima; -a haramu. **~ forces**, nguvu za kimaumbile. **~ gas**, gesi asili: mchanganyiko wa hidrokaboni za kigesi wenye methani nyingi zaidi unaotoka ardhini hususan karibu na mafuta ya kimadini. **~ history**, elimuviumbe. **~ selection**, uteuzi asilia: nadharia ya Darwin juu kanuni ya mabadiliko inayowawezesha viumbe hai kuishi katika mazingira yanayobadilika. *animal living in their ~ state,* wanyama waishio katika hali ya asili. *He is a ~ orator,* ana kipaji cha asili cha usemaji. *It is ~ for a bird to fly,* ni jambo la kawaida ndege kuruka. **~ly** *adv.* kimaumbile; kiasili; kwa desturi; kwa kawaida; bila shaka. **~ist** *n.* mtaalamu wa viumbe. **~ize** *v.t.* andikisha kuwa raia; zoeza tabia ngeni; tohoa. **~ization** *n.* utoaji uraia.

**nature** /'neɪtʃə(r)/ *n.* ulimwengu; viumbe vyote; asili; nguvu za asili; hulka; maumbile; desturi; mazoea; jinsi; namna; aina. *~ study,* elimu ya viumbe hai. *~ worship,* ibada ya viumbe vya asili. *mankind's*

*struggle against ~*, mapambano ya binadamu na mazingira. *in a state of ~*, hali ya uchi. *a woman with a kind ~*, mwanamke mwenye tabia ya wema. *proud by ~*, -enye desturi ya kujivuna. *It is the ~ of dogs to bark*, ni maumbile ya mbwa kubweka. *things of this ~*, vitu vya namna hii. **good-~d** *adj.* -enye tabia njema. **ill-~d** *adj.* -enye tabia mbaya.

**naughty** /'nɔ:ti/ *adj.* -tundu; -tukutu. **naughtness** *n.* utundu; utukutu.

**nausea** /'nɔ:s:ɪə/ *n.* kichefuchefu. **~te** *v.t.* chefua moyo; tapisha. **nauseous** *adj.* -enye kutia kichefuchefu; -a kutapisha.

**nautical** /'nɔ:tɪkl/ *adj.* -a baharia; -a ubaharia.

**naval** /'neɪvl/ *adj.* -a manowari; -a mwanamaji.

**navy** /'neɪvi/ *n.* jeshi la wanamaji; uanamaji.

**nave** /neɪv/ *n.* ukumbi wa kanisa au msikiti.

**navel** /'neɪvl/ *n.* kitovu.

**navigate** /'nævɪgeɪt/ *v.t.* ongoza chombo; safiri baharini. **navigable** *adj.* -a kupitika kwa chombo; -a kuweza kusafiri. **navigation** *n.* usafiri wa angani au baharini; uongozaji vyombo baharini au angani. **navigator** *n.* nahodha; baharia; mwongoza njia.

**near** /nɪə(r)/ *adv.* karibu. *prep.* karibu na; karibu ya. *adj.* -a karibu; -a upande uliokuelekea; -a choyo; -a bahili; -nyimivu. *a ~ escape*, okoka kwa shida. *~ friend*, rafiki wa ndani. *the ~ front wheel of a car*, gurudumu la mbele. *v.t./i.* karibia; sogea karibu. *The ship is ~ing land*, meli inakaribia nchi kavu. **~ly** *adv.* karibu; kama; takriban. **~ness** *n.* ukaribu.

**neat** /ni:t/ *adj.* -liopangwa vizuri; nadhifu; maridadi; - zuri; kavu. **~ly** *adv.* vizuri; kwa usafi. **~ness** *n.* usafi; umaridadi; unadhifu.

**nebula** /'nɛbjʊlə/ *n.* (**~e**) jamii ya nyota nyingi ndogo kama wingu. **nebulos** *adj.* -kama wingu; si wazi; si dhahiri.

**necessary** /'nesəsəri/ *n.* mahitaji muhimu ya lazima. *adj.* - a lazima; - a sharti; -a kujuzu; -a wajibu. **necessarily** *adv.* kwa lazima; sharti. **necessitate** *v.t.* lazimisha. **necessity** *n.* ulazima; haja; shida.


necktie

**neck** /nek/ *n.* shingo; rasi. *~ and ~*, bega kwa bega. *~ or nothing*, kufa na kupona. *~ and crop*, pia; kabisa. **~band** *n.* ukosi. **~lace** *n.* mkufu. **~tie** *n.* tai.

**nectar** /'nektə(r)/ *n.* nekta: maji yenye utamu katika maua ambayo nyuki hutengezea asali.

**need** /ni:d/ *n.* mahitaji; haja; matakwa; umaskini; ufukara; ukata. *v.t.* hitaji; taka. *There is no ~ to hurry*, hakuna haja kukimbiliza. **~ful** *adj.* -enye kuhitajika; -a lazima. **~less** *adj.* -a bure; -sio -a lazima. **~s** *adv.* lazima; sharti; hapana budi. **~y** *adj.* maskini.

**needle** /'ni:dl/ *n.* .sindano; ncha. *packing ~*, shazia. *magnetic, compass ~*, dira. *thread a ~*, tunga sindano. **~woman** *n.* mshoni mwanamke. **~work** *n.* ushoni.

**negative** /'negətɪv/ *n.* ukanaji; negativu; kanusho; uhasi. *adj.* -a kukana; -a kukanusha; hasi. **~ number**, namba hasi. *~ pole*, ncha hasi. **~ quantities**, idadi hasi. **~ electricity**, mkondo wa umeme hasi. *v.t.* kana; kanusha; tangua.

**neglect** /nɪ'glekt/ *n.* upuuzaji; uzembe; utelekezaji; hali ya kutotunzwa. *v.t.* -totunza; -toangalia; -tojali; telekeza; -tofanya; acha; puuza; zembea. **~ful** *adj.* -vivu; -zembe; si -angalifu; mapuuza; sahaulifu. **negligence** *n.* uzembe. **negligent** *adj.* si -angalifu; -zembe; mapuuza. **~ly** *adv.* kizembe. **negligible** *adj.* -sio muhimu; -dogo sana.

**negotiate** /nɪ'gəʊʃieɪt/ *v.i./t.* shauriana; jadiliana; patana bei; badili kwa fedha; pita. **negotiable** *adj.* -a kupitika; -a kubadilishika; -a kuweza kujadiliwa; **negotiation** *n.* majadiliano; mashauriano; mapa-

tano. **negotiator** *n.* mpatanishi; msuluhishi.

**neigh** /neɪ/ *n.* mlio wa farasi. *v.i.* lia (kama farasi).

**neighbour** /'neɪbə(r)/ *n.* jirani. **~hood** *n.* ujirani; mahali pa karibu. **~ing** *adj.* -enye kupakana. **~ly** *adj.* -ema; karimu; -a ujirani mwema. **~liness** *n.* ujirani; ukarimu.

**neither** /'nʌɪðə, 'ni:-/ *adj.* -ote. *of the two ~ man lived,* wote wawili hawakuishi. *pron.* -moja. *I can see ~,* siwezi kuona hata -moja. *conj.* wala; si wala. *~ this nor that,* si hii wala ile. *We are not working ~ are they,* sisi hatufanyi kazi wala wao hawafanyi.

**nematocyst** /nɪ'mɑtə(ʊ)sɪst/ *n.* seliuzi: aina maalumu ya seli katika ngozinje ya baadhi ya wanyama katika ngeli selenterata, ambayo ina kifuko kilichojaa sumu ya kuulia mawindo yao au ya kujihami dhidi ya adui.

**nematode** *n.* nematodi: mnyoo.

**neolithic** /ˌni:ə(ʊ)'lɪθɪk/ *adj.* neolithiki: a mwishoni mwa zama za mawe.

**neon** /'ni:ɒn/ *n.* neoni: elementi gesi isiyo na rangi. *~ lamp,* taa ya neoni: taa ya mshumaa ambayo hutumia gesi ya neoni na ambayo hutoa mwanga mwekundu wakati umeme unapo-pitishwa ndani yake.

**nephew** /'nefju:/ *n.* mpwa, yaani mtoto wa kiume wa dada au kaka.



**nerve cell | seli neva**

**Neptune** /'neptju:n/ *n.* Neptuni: sayari ya nane katika mfumo wa jua.

**nerve** /nɜ:v/ *n.* **1.** neva: mkusanyiko wa nyuroni. **2.** mshipafahamu: mshi-pa wa fahamu ambao hukamilisha mawasiliano baina ya mfumoneva mkuu na sehemu za mwili. **~ cell**, nyuroni: mkusanyiko wa seli ambazo huunda tishu ya neva. **~ cord**, kodi neva: tita kubwa la neva zipitazo ndani ya uti wa mgongo. **3.** hali ya wasi-wasi; wahaka. *noises that get on my ~s,* kelele zinazonitia wasiwasi. *strain every ~,* fanya juu chini; jitahidi sana. **~less** *adj.* -legevu; dhaifu; -siotishika; tulivu. **nervous** *adj.* -a neva; -oga; -enye wahaka; -enye wasiwasi. **~ system**, mfumo wa neva. **nervy** *adj.* *(colloq.)* -enye wasiwasi.

**nest** /nest/ *n.* kiota; mahali pa mapumziko; maficho. **~ egg** *n.* akiba ya fedha.

**net** /net/ *n.* wavu; nyavu; jarife; juya; kimia; mtego. *mosquito ~,* chandarua. *v.t.* (**-tt-**) vua kwa wavu; tega kwa wavu; funika kwa wavu. **~ting** *n.* wavu. *adj.* bila kupungua; kamili; halisi. *~ profit,* faida halisi. *v.t.* (**-tt-**) pata faida halisi.

**neurone** /'njʊərəʊn/ *n.* nyuroni: mkusanyiko wa seli ambazo huunda tishu ya neva.

**neutral** /'nju:trəl/ *adj.* -siofungamana na upande wowote; siopendelea upande wowote; -sio na sifa bainifu. **~ity** *n.* hali ya kuto-fungamana na upande wowote. **~ization** *n.* *(chem.)* mka tisho. **~ize** *v.t.* tangua; batilisha; zimua.

**neutrino** /nju:'tri:nəʊ/ *n.* nyutrino: punje ya kimsingi imara isiyokuwa na chaji yoyote ya umeme au masi tuli lakini yenye piamzunguko nusu.

**neutron** /'nju:trɒn/ *n.* nyutroni: chembe zisizo na chaji zilizo katika nyuklia ya atomu.

**never** /'nevə(r)/ *adv.* kamwe; asilani; hata kidogo; hata. *n.* *~ mind!* haidhuru! *well I ~!* lahaula! **~more** *adv.* si tena kabisa. **~theless** *conj.* hata hivyo.

**new** /nju:/ *adj.* -pya; ngeni; -a siku hizi; -a kisasa. *adv.* karibuni. *~ comers,* wageni. *~-laid eggs,* mayai yaliyotagwa punde tu. *~-fangled,* -pya tena -geni. *~ moon,* mwezi mwandamo: awamu ya mwezi wakati unapounganika na jua na kuonekana katika umbo la hilali. **~ly** *adv.* karibuni. **~ness** *n.* upya; ugeni.

**news** /nju:z/ *n.* habari. **~ agency** *n.* shirika la habari. **~ agent** *n.* muuza magazeti. **~boy** *n.* kijana atembe-

zaye na kuuza magazeti. **~paper** *n.* gazeti. **~reel** *n.* filamu ya taarifa ya habari. **~-stand** *n.* kituo cha kuuzia magazeti.

**newton** *n.* nyutoni: kizio cha kazi kinachofafanuliwa kuwa kani ambayo ikitumiwa kwa masi ya kilogramu moja huipatia mcha puko wa mita moja kwa sekunde. **~'s laws of motion**, kaida za Newton za mwendo: kaida tatu ambazo zilielezwa na Sir Isaac Newton zinazobainisha athari ya kani juu ya vitu vinavyotembea.

**next** /nekst/ *adj.* -enye kufuata; kando; -jao. *adv.* tena; baadaye. *prep.* karibu ya.

**nexus** /'nɛksəs/ *n.* kiungo; mfululizo

**nib** /nɪb/ *n.* nibu.

**nibble** /'nɪbl/ *v.t./i.* guguna; bebenya; bebuna; guguna. /

**nice** /naɪs/ *adj.* -a kupendeza; -zuri; -ema; -a kuhitaji uangalifu; chaguzi; -teuzi. **~ly** *adv.* vyema; vizuri; barabara. **~ty** *n.* usahihi; undani; mambo madogo madogo.

**nickel** /'nɪkl/ *n.* nikeli: aina ya madini nyeupe ngumu kama fedha.

**nickname** /'nɪkneɪm/ *n.* jina la utani; lakabu.

**nicotine** /'nɪkəti:n/ *n.* nikotini: sumu iliyo katika tumbaku.

**niece** /ni:s/ *n.* mpwa mwanamke.

**night** /naɪt/ *n.* usiku. *make a ~ of it*, kesha kwenye starehe. **~dress ~gown** *n.* vazi la kulalia usiku. **~fall** *n.* magharibi; kuchwa. **~ly** *adj.* -a usiku; -a kila usiku. *adv.* usiku. **~mare** *n.* jinamizi. **~watchman** *n.* mlinzi wa usiku.

**nil** /nɪl/ *n.* sifuri; bila. *The result of the game was 3 - nil*, matokeo ya mchezo yalikuwa goli tatu kwa bila.

**nimble** /'nɪmbl/ *adj.* -epesi; -elekevu; hodari; (kwa akili) -kali. **nimbly** *adv.* kwa wepesi.

**nine** /naɪn/ *n./adj.* tisa. *a ~ days' wonder*, jambo la kushangaza kwa muda mfupi tu. **~teen** *n./adj.* kumi na tisa. **~ty** *n./adj.* tisini. **ninth** *n./adj.* -a tisa.

**nip** /nɪp/ *n.* mminyo; mfinyo; mbinyo; mkato. *a ~ in the air*, baridi kali. *v.t./i.* (**-pp-**) minya; finya; binya; nyakua; uma; haribu. *~ in the bud*, haribu toka mwanzoni. **~per** *n.* *(colloq.)* koleo; kibano; gando.

**nipple** /'nɪpl/ *n.* chuchu; kitu chenye umbo la chuchu.

**nitrate** /'nʌɪtre:ɪt/ *n.* nitrati: chumvi au esta ya asidi nitriki. **nitric** *adj.* nitriki: -a nitrojeni; -enye nitrojeni. **~ acid**, asidi nitriki: kioevu cha kiasidi kisichokuwa na rangi na kilishaji chenye kiwango mchemko cha 86°C. **nitrification** *n.* unitrishaji: **1.** utendanishaji wa kitu cha asidi nitriki. **2.** mfanyiko tendani wa kugeuza kwa kutumia bakteria misombo ya nitrojeni kutoka kwenye mabaki au takataka, uozo wa wanyama au mimea ili kuwa nitrati katika udongo. **nitrifying bacteria**, bakteria nitrojeni: bakteria wanaogeuza kampaundi sahili za nitrojeni kuwa nitrati zinazoweza kutumiwa na mimea.

**nitrogen** /'nʌɪtrədʒ(ə)n/ *n.* nitrojeni: elementi gesi ambayo sio metali. **~ cycle**, duru ya nitrojeni: mzunguko wa matumizi ya nitrojeni ya angahewa kwa viumbe mbalimbali. **~ fixation**, uambishi nitrojeni: kitendo cha kugeuza nitrojeni kutoka katika hali ya gesi na kuwa kampaundi ambayo inaweza kunyonywa na kutumiwa na mimea. **~-fixing bacteria**, bakteria nitrojeni: bakteria wanaotumia nitrojeni iliyo katika hewa kujenga kampaundi kwa kutumia mfanyikotendani kemikali.

**no**. *n.* ufupisho wa *number:* namba; nambari.

**no** *adj.* hapana; hakuna; hamna; hiwezekani; marufuku; siyo; si. *adv.* zaidi. *int.* la! hasha! hapana!

**noble** /'nəʊbl/ *n.* sharifu; lodi. *adj.* sharifu; -a kilodi; bora; -enye tabia nzuri; adilifu. **~ gases**, gesi ajizi: kundi la elementi sita (heli, neoni, agoni, kriptoni, zenoni, na radoni)

zilizomo mwenye kundi la sifuri la jedwali mrudio. **nobility** *n.* usharifu; uungwana; ulodi; masharifu; malodi; waungwana. **nobly** *adv.* vizuri; vyema; kwa uadilifu. **~man** *n.* sharifu; lodi; muungwana.

**nocturnal** /nɒk'tɜ:nl/ *adj.* -a usiku.

**nod** /nɒd/ *n.* ishara ya kichwa. *v.t./i.* (**-dd-**) inamisha kichwa; tikisa kichwa; sinzia; kubali. *have a ~ding acquaintance with,* jua mtu juujuu tu. *the land of ~,* ndoto; usingizi.

**node** /nəʊd/ *n.* **1.** kifundo: sehemu ya wimbi ambapo tambo lina thamani ya sifuri. **2.** fundo: sehemu ya shina ambapo majani huchipukia.

**nodule** /'nɒdju:l/ *n.* tezi kwenye mizizi ya baadhi ya mimea ambazo hufuga bakteria watengenezao nitrojeni.

**Noel** /nəʊ'el/ *n.* Noeli; Krismasi.

**noise** /nɔɪz/ *n.* kelele; ghasia; sauti; mlio; kishindo; mvumo. **~less** *adj.* -a kimya. **noisily** *adv.* kwa kelele. **noisy** *adj.* -a makelele.

**nomad** /'nəʊmæd/ *n.* mhamahamaji. **nomadic** *adj.* -a kuhamahama.

**nominal** /'nɒmɪnl/ *adj.* -a jina tu; si halisi; -liotajwa; - dogo; -a nomino. *the ~ ruler,* mtawala wa jina tu. *a ~ rent,* kodi ndogo tu. **~ly** *adv.* kwa jina; kwa maneno tu.

**nominate** /'nɒmɪneɪt/ *n.* teua; chagua; pendekeza.

**nomination** /ˌnɒmɪ'neɪʃn/ *n.* uteuzi; pendekezo; chaguo.

**nominee** /'nɒmɪ'ni/ *n.* mtu aliyependekezwa; mteuliwa.

**non-** /nɒn/ *prefix* si; sio; -tokuwa.

**non-metal** *n.* simetali; isometali: elementi ambayo haina tabia za kimetali na ambayo huweza kuunda ioni hasi.

**non-renewable energy** *n.* nishati hulu: vyanzo vya nishati ambavyo havina mbadala kimaumbile vikishakutumika.

**none** /nəʊn/ *adj./pron.* hata -moja; bila. *adv.* hata kidogo; sio; hapana. *~ the worse for his experiences,* bila kupata hasara kwa mambo yaliyompata.

**nonsense** /'nɒnsns/ *n* upuuzi. *talk ~,* piga domo.

**nonsensical** /nɒn'sensɪkl/ *adj.* -a upuuzi.

**noon** /nu:n/ *n.* adhuhuri; saa sita mchana.

**noose** /nu:s/ *n.* tanzi; shemere; shwara.

**nor** /nɔ:(r)/ *conj.* wala.

**normal** /'nɔ:ml/ *n.* kawaida. *adj.* -a kawaida; -a desturi; -a siku zote. *above ~,* zaidi kuliko kawaida.

**north** /nɔ:θ/ *n.* kaskazini; kibla. *adj.* -a kaskazini; -a kibla. *adv.* upande wa kaskazi. **~ern** *adj.* -a kaskazini. **~wards** *adv.* kuelekea kaskazi.

**nose** /nəʊz/ *n.* pua. *pay through the ~,* lipa thamani kubwa sana. *v.t./i.* nusa; endelea mbele polepole. *The ship ~d its way through the ice,* meli iliendelea polepole katika barafu. **~dive** *v.i.* anguka kichwakichwa. **~gay** *n.* shada la maua.

**nostril** /'nɒstrəl/ *n.* chochwe; tundu ya pua.

**not** /nɒt/ *adv.* si; sio; hapana.

**notable** /'nəʊtəbl/ *n.* mtu mashuhuri. *adj.* -a kujulikana sana; -enye sifa; mashuhuri. **notably** *adv.* hasa; zaidi. **notability** *n.* umashuhuri; mtu mashuhuri.


notches

**notch** /nɒtʃ/ *n.* keo; pengo. *v.t.* piga keo; tia pengo.

**note** /'nəʊt/ *n.* ukumbusho; muhtasari; barua; noti; maoni; ishara; dalili; fahamu; sifa; cheo. *A ~ of self-satisfaction was heard in his speech,* aliashiria kuridhika katika hotuba yake. *~ of exclamation,* alama ya mshangao hii ( ! ). *a family of ~,* familia bora. *It is worthy of ~,* yafaa izingatiwe. *Take ~ of what I say,* fahamu vyema ninalosema. *v.t.* angalia; ona; kumbuka; andika. *~ sth. down,* andika. **~d** *adj.* mashuhuri. **~worthy** /'nəʊtwɜ:ði/ *adj.* -a kufaa kuzingatiwa.

**nothing** /'nʌθɪŋ/ *n.* si kitu; hakuna kitu. *come to ~,* - tofaulu. *make ~ of,* toka kapa; -toelewa. *~ but,* tu.

**notice** /ˈnəʊtɪs/ *n.* tangazo; notisi; taarifa; uzingatiaji. *give a servant a month ~,* -pa mtumishi notisi ya mwezi mmoja. *Take no ~ of what they say,* msiyatilie maanani maneno yao. *v.t./i.* angalia; ona. **~able** *adj.* -a kuonekana kwa urahisi.

**notify** /ˈnəʊtɪfaɪ/ *v.t.* tangaza; arifu; julisha. **notifiable** *adj.* -liolazimu kutangazwa. **notification** *n.* taarifa; tangazo; ilani.

**notion** /ˈnəʊʃn/ *n.* wazo; dhana; fikira.

**notorious** /nəʊˈtɔːriəs/ *adj.* -enye kuvuma kwa ubaya; -enye sifa mbaya. **notoriety** *n.* sifa mbaya; ubaya.

**notwithstanding** /ˌnɒtwɪθˈstændɪŋ/ *prep.* licha. *conj.* ijapokuwa. *adv.* hata hivyo. *~ advice he went,* ijapokuwa alionywa bado alikwenda.

**nought** /nɔːt/ *n.* si kitu; si neno; sifuri. *come to ~,* shindikana; tanguka; batilika.

**noun** /naʊn/ *n.* *(grammar)* jina; nomino.

**nourish** /ˈnʌrɪʃ/ *v.t.* lisha; chunga; lea; stawisha; rutubisha; tunza moyoni. **~ment** *n.* chakula.

**nova** /ˈnəʊvə/ *n.* nova: nyota ambayo nuru yake huwa kubwa sana na baada ya muda hufifia.

**novel** /ˈnɒvl/ *n.* riwaya. *adj.* -pya; -geni. **~ette** *n.* riwaya fupi. **~ist** *n.* mwandishi wa riwaya. **~ty** *n.* upya; ugeni; kitu kipya.

**November** /nəʊˈvembə(r)/ *n.* Novemba: mwezi wa kumi na moja wa mwaka wa kizungu.

**now** /naʊ/ *adv.* sasa; mara moja; sasa hivi. *~ and again, ~ and then,* mara kwa mara. *now then ! now now!* sasa. **~adays** *adv.* siku hizi.

**nowhere** /ˈnaʊweə(r)/ *adj.* si popote. *I went ~,* sikwenda popote. *The man is ~ to be seen,* mtu mwenyewe haonekani mahali popote.

**nozzle** /ˈnɒzl/ *n.* nozeli: kizibo cha chuma kilichounganishwa kwenye ncha ya neli ya mpira.

**nuclear** /ˈnjuːkliə(r)/ *adj.* -a kiini; -nyuklia. **~ energy**, nishati ya nyuklia. **~ energy plant**, mtambo wa nishati ya nyuklia. **~ fission**, mwatuko nyuklia: utendanaji wa kinyuklia unaokisababisha kiini kizito cha atomu kumeguka katika sehemu mbili na kutoa nishati. **~ fusion**, uyeyunganishaji kinyuklia: utendanaji wa kinyuklia baina ya viini vya atomu nyepesi unaosababisha uundaji wa kiini kizito zaidi. **~ radiation**, mnururisho nyuklia: mnururisho alfa, beta, na gama unaotolewa wakati viini nururishi vinapooza. **~ reaction**, utendanaji kinyuklia: utendanaji wowote unaosababisha mabadiliko katika kiini cha atomu. **~ reactor**, tanuri nyuklia: chombo ambamo utendanaji wa kimnyororo wa ujotoevushaji kinyuklia unaendeshwa na unadhibitiwa ili kuunda nishati ya nyuklia, isotopu nururishaji au elementi bandia. **~ waste**, takataka za sumu: mabaki yoyote ya dutu nururishi. **~ weapons**, silaha za nyuklia.

**nucleic acid** *n.* asidi kiiniseli: asidi muhimu iliyomo katika kila seli ya kiumbe hai yenye kuhifadhi na kuhamisha msombo jeni.

**nucleon** /ˈnjuːklːɪɒn/ *n.* nyuklioni: kijenzi cha kiini cha atomu, yaani protoni au nyutroni. **~ number**, namba kiini: namba ya chembe za atomu katika kiini cha atomu.

**nucleus** /ˈnjuːklɪəs/ *n.* (**nuclei**) kiini; asili; chanzo.

**nude** /njuːd/ *n.* uchi. *adj.* -tupu; uchi; bila kuvaa nguo; bila mapambo. **nudist** *n.* mtu ahusuduye kukaa uchi.

**nudge** /nʌdʒ/ *n.* kikumbo. *v.t.* piga kikumbo.

**nugget** /ˈnʌgɪt/ *n.* kipande cha dhahabu.

**nuisance** /ˈnjuːsns/ *n.* udhia; usumbufu; adha; kero.

**numb** /nʌm/ *v.t.* fanya ganzi. *adj.* -enye ganzi; -zito; -legevu. *fingers ~ed with cold,* vidole vilivyokufa ganzi kwa baridi.

**number** /ˈnʌmbə(r)/ *n.* namba;

nambari; hesabu; kiwango; tarakimu; idadi; wingi; toleo. *a back ~, (fig.)* kitu, au mtu aliyepitwa na wakati. *v.t.* tia nambari; taja nambari; fikia; pata; timia. *Those present ~ed fifty,* waliohudhuria walitimia hamsini. **~less** *adj.* -ingi sana; -siohesabika; bila idadi; -sio namba.

**numeral** /'nju:mərəl/ *n.* tarakimu; herufi ya hesabu; nyumerali. **numerator** *n.* kiasi. **numerical** *adj.* -a nyumerali.

**numerous** /'nju:mərəs/ *adj.* -ingi sana.

**nun** /nʌn/ *n.* mtawa wa kike. **~nery** *n.* nyumba ya watawa wa kike.

**nurse** /nɜ:s/ *n.* mlezi; yaya; muuguzi; nesi. *v.t.* uguza; nyonyesha; lea; tunza. **~ry** *n.* chumba cha watoto; jalbe: kitalu cha miche. **~ryman** *n.* mfanya kazi katika jalbe la mimea. *~ school,* shule ya chekechea.

**nurture** /'nə:tʃə/ *n.* malezi; elimu; mafunzo. *v.t.* lea; elimisha.


nut

**nut** /nʌt/ *n.* kokwa; njugu; lozi; nati. *ground ~, pea ~,* njugu nyasa; karanga. *coco~,* nazi. *cashew ~,* korosho. **~crackers** *n.* ala ya kubanjia kokwa. **~shell** *n.* ganda; gamba la kokwa. *in a ~shell,* kwa muhtasari.

**nutmeg** /'nʌtmeg/ *n.* kungumanga; basibasi.

**nutrient** /'nju:triənt/ *n./adj.* kirutubishi; -a kirutubishi.

**nutriment** *n.* chakula bora.

**nutrition** /nju'trɪʃn/ *n.* lishe. **nutritious** *adj.* rutubishi.

**nylon** /'naɪlɒn/ *n.* nailoni.

**nymph** /nɪmf/ *n.* tunutu: wadudu wachanga walio na maumbile yanayofanana na wazazi wao, ila hawajapevuka.

## Oo

**o, oh** /əʊ/ *interj.* mlio wa mshangao au hofu.

**oak** /əʊk/ *n.* mti aina ya mwaloni.

**oar** /ɔ:(r)/ *n.* kasia; kafi. **~sman** *n.* mpiga kasia.

**oasis** /əʊ'əɪsɪs/ *n.* (**oases**) oasisi: mahali penye miti na chemchemi katika jangwa.

**oath** /əʊθ/ *n.* (**~s**) kiapo; yamini; laana; apizo.

**oats** /əʊts/ *n.* shayiri. *sow one's wild ~,* ponda maisha ujanani. **oatmeal** *n.* unga wa shayiri.

**obedience** /ə'bi:diəns/ *n.* utii; usikivu. **obedient** *adj.* -tiifu; -sikivu. **obediently** *adv.* kwa utii.

**obey** /ə'beɪ/ *v.t./i.* tii; sikia; tumikia.

**object** /'ɒbdʒɪkt/ *n.* kitu; jambo; nia; kusudi; madhumuni; shamirisho; kiolwa. *an ~ lesson,* somo lenye vielelezo vya vitu halisi. *with no ~ in life,* bila lengo lolote katika maisha. *succeed in one's ~,* timiza lengo. *Money is no ~,* lengo si fedha; fedha si kitu. *v.t.* kataa; bisha; pinga; zuia. **~ion** *n.* katazo; kizuizi; pingamizi. **~ionable** *adj.* -a kuchukiza. **~or** *n.* mpingaji; mbishi. **~ive** *n.* lengo; shabaha.*adj.* bila upendeleo; -a kuhusu jambo. *My advice is quite ~,* nasaha yangu haina upendeleo. *My statement on the purpose of the war is quite ~,* tamko langu kuhusu vita halimlengi yeyote.

**obligation** /ˌɒblɪ'geɪʃn/ *n.* wajibu; faradhi; jukumu.

**obligatory** /ə'blɪgət(ə)ri/ *adj.* -a lazima; faradhi; -a wajibu.

**oblige** /ə'blaɪdʒ/ *v.t.* lazimisha; shurutisha; fadhili. **obliging** *adj.* tayari kusaidia; karimu.

**oblique** /ə'bli:k/ *adj.* -a mshazari; -a kukingama; -a kuzunguka; si wazi.

**obliterate** /ə'blɪtəreɪt/ *v.t.* futilia mbali; ondoa kabisa; haribu.

**oblivion** /ə'blɪviən/ *n.* hali ya kusahauliwa kabisa. **oblivious** *adj.* -sio na kumbukumbu; -liosahau kabisa.

**oblong** /'ɒblɒŋ/ *n./adj.* mstatili; -a mstatili.

**obscene** /əb'si:n/ *adj.* (kwa maneno, desturi) -chafu; pujufu. **obscenity** *n.* maneno au matendo machafu; matusi ya wazi.

**obscure** /əb'skjʊə(r)/ *adj.* -a giza; -a kujificha; -sioonekana wala kufahamika vyema; -siojulikana vizuri. *v.t.* tia giza; fumba; ficha. **obscurity** *n.* giza; fumbo.

**observe** /əb'zɜ:v/ *v.t./i.* ona; angalia; chungua; chunguza; tanabahi; fuata; shikilia; shika; adhimisha; sema. **observable** *adj.* -a kutazamika; -a kuonekana. **observance** *n.* desturi; kawaida; kushikilia kanuni za mila na desturi. **observant** *adj.* -angalifu; -elekevu; -epesi kubaini.

**observation** /'ɒbzə'veɪʃn/ *n.* kuangalia; uangalizi; maoni; ugunduzi. **observatory** *n.* mahali pa kuchunguzia sayari na nyota. **~r** *n.* mtazamaji; mchunguzi; mwangalizi.

**obsess** /əb'ses/ *v.t.* shika, shikilia, jaza katika akili au moyo. **~ion** *n.* tamaa; shauku isiyozuilika; kupagawa.

**obsolete** /'ɒbsəli:t/ *adj.* -siotumika tena; -liopitwa na wakati; -siofaa; -kongwe.

**obsolescent** /ˌɒbsə'lesnt/ *adj.* -liopitwa na wakati; -siofaa tena.

**obstacle** /'ɒbstəkl/ *n.* kizuizi; pingamizi; kikwazo.

**obstinate** /'ɒbstɪnət/ *adj.* -kaidi; -bishi; -sugu; -nye inadi; -shupavu. **~ly** *adv.* kikaidi; kiubishi.

**obstinacy** /'ɒbstɪnəsi/ *n.* ukaidi; usugu; inadi.

**obstruct** /əb'strʌkt/ *v.t.* zuia; pinga; kataza. *~ a bill in the parliament,* zuia mswada bungeni. **~ion** *n.* uzuiaji; kizuizi; pingamizi. **~ive** *adj.* -a kuzuia; -a kupingia; -enye pingamizi.

**obtain** /əb'teɪn/ *v.t./i.* nunua; pata; jipatia; kubalika; enea; tumika. **~able** *adj.* -a kupatikana.

**obtrude** /əb'tru:d/ *v.t./i.* jiingiza; jitia kati; jidukiza. **obtrusive** *adj.* -a kuingilia kati; -a kujidukiza.

**obtuse** /əb'tju:s/ *adj.* butu; dugi; -pumbavu. *~ angle,* pembebutu.

**obviate** /'ɒbvɪeɪt/ *v.t.* ondoa; katiza; toa.

**obvious** /'ɒbviəs/ *adj.* wazi; dhahiri; -a kuonekana; -a kueleweka.

**occasion** /ə'keɪʒn/ *n.* fursa; wasaa; nafasi; sababu; haja; tukio. *not an ~ for laughter,* si wakati wa kucheka. *rise to the ~,* patiza; onyesha uwezo unaohitajika. *There's no ~ for you to lose your temper,* huna sababu ya kukasirika. *v.t.* sababisha; fanya; leta. *He was late and this ~ed anxiety,* alichelewa na jambo hilo lilileta wasiwasi. **~al** *adj.* mara moja; -a kufaa wakati fulani. **~ally** *adv.* pengine; mara mojamoja.

**occupy** /'ɒkjupaɪ/ *v.t.* kalia; shika; miliki; chukua; shughulika na; shughulisha; tumia; -wa na. *He was occupied with his work,* alishughulika na kazi yake. *Many thoughts occupied my mind,* nilishughulishwa na mawazo mengi. **occupant** *n.* mkaji; mwenyeji; mmilikaji.

**occupation** /ˌɒkju'peɪʃn/ *n.* utwaaji; umilikaji; shughuli; kazi; biashara.

**occur** /ə'kɜ:(r)/ *v.i.* (**-rr-**) tokea; pitikia akilini; -wa. *Which letter of the alphabet ~s most commonly?* herufi ipi hutokea mara nyingi katika alfabeti? *~ to,* pitikia akilini. **~rence** *n.* tukio; kadhia.

**ocean** /'əʊʃn/ *n.* bahari. *~ going,* -enye kusafiri baharini. **~ography** *n.* sayansi ya bahari. **~ trench,** handaki bahari; handaki refu jembamba lililopo chini ya bahari.


octagon

**octagon** /'ɒktəgən/ *n.* pembenane. **~al** *adj.* -enye pembe nane.

**October** *n.* Oktoba: mwezi wa kumi wa mwaka wa kizungu.


octopus

**octopus** /'ɒktəpəs/ *n.* pweza.

**ocular** /'ɒkjʊlə/ *adj.* -a macho; kwa kuona; kwa macho. **~ proof,** uthibitisho

wa kuona. **oculist** *n.* daktari wa macho.

**odd** /ɒd/ *adj.* witiri; -moja pasipo mwenzake; moja peke yake; -ngeni; -a ajabu; -a kuchekesha; -a mzaha; -sio -a kawaida; -a muda mfupi; pamoja na -ingine -liobaki. *a hundred shillings and some ~ cents,* shilingi mia moja na senti kidogo. *~ jobs,* kazi anuwai. *at ~ times,* nyakati za dhiki. **~ity** *n.* ugeni; ajabu; shani; kioja. **~ly** *adv.* kwa namna ya pekee. **~s** *n.* tofauti; ziada; matumaini; uwezekano; kutopatana. *be at ~s with,* gombana; bishana; zozana. *~ and ends,* takataka; vikorokoro.

**odour** /'əʊdə(r)/ *n.* harufu; sifa; upendeleo. *be in good ~ with,* pendelewa na. **~less** *adj.* -sio harufu.

**oesophagus** /ɪ'sɒfəgəs/ *n.* umio: sehemu ya mfereji wa chakula iliyoko kati ya kinywa na tumbo.

**of** /əv/ *prep.* -a; kwa; katika; kuhusu.

**off** /ɒf/ *prep.* katika; kwa; -ni; mbali na; juu ya; karibu na; -liochepuka kutoka. *an island ~ the south coast,* kisiwa karibu na pwani ya kusini. *a small street ~ the main road,* kichochoro kilichochepuka kutoka barabara kuu. *~ colour, ~ one's food,* bila tamaa ya chakula. *~ one's head, (slang)* -enye wazimu. *adv.* mbali; si juu. *~ and on,* mara mojamoja. *adj.* -a upande wa kuume. *the ~ side,* upande wa kuume. *on the ~ chance,* kwa bahati. *the ~ season,* msimu wa shughuli haba. *in one's ~ time,* wakati wa mapumziko. **~hand** *adj.* -sioandaliwa. *adv.* kwa haraka; bila maandalizi; bila kufikiri; ghafla.

**offal** /'ɒfl/ *n.* matumbo ya mnyama; takataka.

**offence** /ə'fens/ *n.* kosa; dhambi; uhalifu; hatia; chuki; uchungu; mashambulizi. *weapons of ~,* silaha za vita.

**offend** /ə'fend/ *v.i./t.* kosa; chukiza; udhi; chokoza; sumbua. **offender** *n.* mhalifu; mkosaji.

**offensive** /ə'fensɪv/ *n.* shambulio; mashambulizi. *adj.* -a kuchokoza; -a kusumbua; -a kushambulia; -a kuanzisha vita; -a kuchukiza. *take the offensive,* anzisha vita. **offensively** *adv.* kivita; kiuchokozi.

**offer** /'ɒfə(r)/ *n.* ahadi; mwaliko; bei; zabuni; pendekezo. *v.t.* toa; tolea; tia bei; jitolea; -wa tayari; nunua; toa sadaka; tambika; zabuni. *~ prayers,* omba Mungu. *They ~ed no resistance,* hawakupinga. **~ing** *n.* utoaji; sadaka; mhanga. **~tory** *n.* sadaka.

**office** /'ɒfɪs/ *n.* ofisi; wizara; idara; madaraka; cheo; dhamana; wajibu; kazi; fadhila; msaada; huduma.**~r** *n.* ofisa; afande; kiongozi.

**official** /ə'fɪʃl/ *n.* ofisa. *adj.* rasmi; -a serikali; -enye madaraka. **~ly** *adv.* kwa urasimu; kwa utaratibu. **officiate** *v.i.* fanya kazi kwa cheo fulani.

**officious** /ə'fɪʃəs/ *adj.* -a kujidukiza; -a kujitiatia; -a kuingilia.

**offshoot** /'ɒfʃu:t/ *n.* chipukizi; chipwi.

**offspring** /'ɒfsprɪŋ/ *n.* mtoto; kizazi; kinda.

**often** /'ɒf(ə)n, 'ɔft(ə)n/ *adv.* mara kwa mara; mara nyingi.

**ohm** /əʊm/ *n.* omu: kizio cha SI cha ukinzani sawa na uwiano kati ya volteji na mkondo umeme. **Ohm's law**, kaida ya Ohm: kaida inayoeleza kuwa volteji inayopita katika kipitishi ikiongezeka maradufu basi umeme unaopita katika kipitishi utaongezeka maradufu.

**oil** /ɔɪl/ *n.* mafuta. *v.t.* tia mafuta; paka mafuta. **~cloth** *n.* kitambaa kisichopenyeza maji. **~er** *n.* kopo la mafuta; fundi mafuta; meli ya mafuta. **~skin** *n.* kitambaa kisichopenyeza maji.**~ refinery**, mtambo wa kusafishia mafuta ghafi. *~ tanker,* meli ya mafuta. **~well** *n.* kisima cha mafuta. **~y**. *adj.* -enye mafuta; laini; -janja.

**ointment** /'ɔɪntmənt/ *n.* malihamu; dawa ya kuchua.

**old** /əʊld/ *n.* zamani; kale. *adj.* -zee; kongwe; -enye umri wa; -a zamani;

kuukuu. *in days of ~,* siku za kale. **~en** *adj.* -a zamani; -a kale. *in ~ days,* siku za kale. **~-fashioned** *adj.* -a kale; -liopitwa na wakati; zilipendwa.

**olive** /'ɒlɪv/ *n.* mzeituni; zeituni. *hold out the ~ branch,* onyesha ishara ya amani. *~ oil,* mafuta ya halizeti. *adj.* -a zeituni.

**omelette** /'ɒmlət/ *n.* kimanda: yai la kukaanga.

**omen** /'əʊmən/ *n.* ishara; dalili; njozi. *a good ~,* njozi njema. *a bad ~,* ndege mbaya. **ominous** *adj.* -a ndege mbaya; -a kisirani; -a nuhusi.

**omit** /ə'mɪt/ *v.t.* (**-tt-**) acha; pitiliza; ruka; kosea. **omission** *n.* urukaji; upitilizaji; koseo; -lioachwa.

**omnipotence** /ɒm'nɪpətəns/ *n.* kudura. **omnipotent** *adj.* -enye kudura. *The Omnipotent God,* Mungu mwenye uwezo wa yote.

**omniscient** /ɒm'nɪsɪənt/ *adj.* -a kujua yote. *The ~ God,* Mungu mjuzi wa yote. **omniscience** *n.* ujuzi wa yote.

**omnivorous** /ɒm'nɪv(ə)rəs/ *adj.* enye kula chochote.

**on** /ɒn/ *prep.* juu ya; katika; -ni; kuhusu; kwenye. *adv.* juu; mbele.

**once** /wʌns/ *adv.* mara moja; hapo kale; hapo nyuma; wakati fulani; mara tu. *~ in a while,* mara mojamoja. *~ and for all,* mwanzo na mwisho. *~ upon a time,* hapo kale. *at ~,* mara moja; papo hapo; bila kuchelewa. *~ you begin to feel afraid,* mara tu ukiogopa. *For ~ you're right,* kwa mara ya kwanza u sahihi.

**one** /wʌn/ *adj.* -moja; -a kwanza; fulani. *pron.* -moja; mojawapo; fulani; mtu. *~ by ~,* -moja -moja; *It's all ~ to me,* ni mamoja kwangu. **~self** *pron.* mwenyewe. *please ~self,* jifurahisha. **~-sided** *adj.* -a upande mmoja; -a upendeleo. *a ~-argument,* hoja zinazopendelea upande mmoja.

**onerous** /'əʊn(ə)rəs/ *adj.* -enye kuhitaji jitihada nyingi; -a kutaabisha.

**onion** /'ʌnjən/ *n.* kitunguu maji.

**onlooker** /'ɒnlʊkə(r)/ *n.* mtazamaji.

**only** /'əʊnli/ *adj.* tu; -a pekee. *adv.* tu; basi. *conj.* ila; lakini; isipokuwa.

**onomatopoeia** /ˌɒnə(ʊ)mɑtə'piːə/ ono-matopia; tanakali sauti.

**opacity** /ə(ʊ)'pɑsɪti/ *n.* hali ya kutopitisha nuru; utatanishi wa maana.

**opaque** /əʊ'peɪk/ *adj.* -siopitisha nuru; -enye utatanishi wa maana.

**onward(s)** /'ɒnwəd/ *adj./adv.* mbele.

**ooze** /uːz/ *n.* matope; kinamasi. *v.i.* vuja; tona; tiririka. *(fig.) Their courage ~d away,* uhodari wao uliyeyuka.

**opaque** /ə(ʊ)'peɪk/ *adj.* buye: -enye tabia ya kutoruhusu nuru kupita.

**open** /'əʊpən/ *n.* nje. *adj.* wazi; -siozingirwa; -siofunikwa; -sio kipaa; -sio kizuizi; -liochanua. *in the ~ air,* nje. *with ~ arms,* kwa mikono miwili. *an ~ boat,* mashua isiyo na sitaha. *~ competitions,* mashindano ya wazi. *the ~ country,* uwanda; chanjaa. *keep ~ house,* -wa karimu kwa watu wote. *have an ~ mind,* -wa tayari kupokea mawazo mapya. *in ~ order,* -lioachana sana kwa nafasi; -a wazi; -a watu wote; -a bure. *an ~ question,* jambo lisiloamuliwa; swali lenye jawabu zaidi ya moja. *the ~ sea,* bahari kuu. *be ~ to,* karibisha; -wa bila kinga; -wa tayari kwa. *v.t./i.* fungua; funua; funguka; funuka; anzisha rasmi. *~ fire,* piga risasi. **~ing** *n.* mwanzo; kipenyo; nafasi; uwazi; mlango; tundu; ufa; ufunguzi. **~-handed** *adj.* karimu. **~ly** *adv.* waziwazi. **~-hearted** *adj.* -kweli; -kunjufu; -nyofu.

**opera** /'ɒprə/ *n.* opera: mchezo wa kuigiza.

**operate** /'ɒpəreɪt/ *v.t./i.* endesha; tenda kazi; pasua; fanya operesheni; fanya manuva.

**operation** /ˌɒpə'reɪʃn/ *n.* utendaji; upasuaji; kazi; shughuli; ukokotoaji; operesheni; kampeni. *come into operation,* anza kufanya kazi; tumika. **operative** *n.* mfanyakazi; fundi mitambo. *adj.* -enye kutenda kazi; -enye kutumika; -a nguvu za

kisheria; -a kupasua. **operator** *n.* opereta; mfanya kazi; mwendeshaji.

**opinion** /ə'pɪnjən/ *n.* maoni; wazo; dhana. *get a lawyer's ~,* pata ushauri wa mwanasheria. **~ated** *adj.* -shupavu; -enye kushikilia maoni yake.

**opium** /'əʊpiəm/ *n.* afyuni; kasumba; aina ya dawa ya kulevya itokanayo na mmea uitwao mpopi.

**opponent** /ə'pəʊnənt/ *n.* mshi ndani; adui; mpinzani.

**opportune** /'ɒpətju:n, ˌɒpə'tju:n/ *adj.* -a kufaa; -liotokea -lipohitajika; -a wakati muafaka.

**opportunity** /ˌɒpə'tju:nəti/ *n.* nafasi; wasaa; fursa.

**oppose** /ə'pəʊz/ *v.t.* pinga; kataa; shindana.

**opposite** /'ɒpəzɪt/ *adj.* -enye kukabiliana; kinyume; ' -enye kuelekeana;

**opposition** /ˌɒpə'zɪʃn/ *n.* upinzani; ushindani; uelekeanaji. *the opposition,* kambi ya upinzani.

**oppress** /ə'pres/ *v.t.* dhulumu; kandamiza; onea; taabisha. **~ion** *n.* udhalimu; ukandamizaji; mateso. **~ive** *adj.* dhalimu; -kandamizaji; -a kulemea; -zito; -a taabu. **~or** *n.* mkandamizaji; dhalimu.

**optic** /'ɒptɪk/ *adj.* -a macho. **~al** *adj.* -a macho. **~al fibre**, fiba maonzi: fiba ndefu nyembamba ya kioo ambamo mwangaza unaweza kupita na kupoteza kiasi kidogo sana cha mng'aro wake. **~ illusion**, sarabi; mauzauza. **~s** *n.* elimunuru: sayansi ya nuru na vifaa vinavyohusishwa na matu-mizi au vipimo vya nuru. **~ian** *n.* mtengenezaji au muuzaji miwani.

**optimism** /'ɒptɪmɪzəm/ *n.* imani ya matumaini mema. **optimist** *n.* mtu mwenye imani ya matumaini mema. **optimistic** *n.* -enye imani ya matumaini mema.

**option** /'ɒpʃn/ *n.* uchaguzi; hiari; haki ya kutenda; chaguo. **~al** *adj.* -a hiari; si -a lazima.

**or** /ɔ:(r)/ *conj.* au ; ama; kama sivyo; la sivyo.

**oracle** /'ɒrəkl/ *n.* mzimu; uaguzi; kahini; mwaguzi; mshauri; mtu mwenye hekima. **oracular** *adj.* -a mizimu; -a uaguzi; -a hekima; -a fumbo.

**oral** *adj.* -a mdomo, -sioandikwa; simulizi; -a kusemwa. **~ contra-ceptive**, kidonge: kidonge kiliwacho kuzuia mimba. **~ literature**, fasihi simulizi. **~ly** *adv.* kwa mdomo; kwa kusema.

**orange** /'ɒrɪndʒ/ *n.* chungwa; *~ tree,* mchungwa; danzi. *adj.* -a rangi ya chungwa. **~ry** *n.* shamba la michu-ngwa.

**oratory** /'ɒrətri/ *n.* ufasaha wa kusema.

**orbit** /'ɔ:bɪt/ *n.* mzunguko; mzingo. *the earth's ~ round the sun,* mzingo wa dunia kuzunguka jua.

**orchard** /'ɔ:tʃəd/ *n.* shamba la miti ya matunda.

**orchestra** /'ɔ:kɪstrə/ *n.* okestra: kundi la watu wapigao muziki kwa pamoja. *~ pit,* ukumbi wa wapiga muziki kwenye thieta. **orchestral** *adj.* -a okestra.

**ordeal** /ɔ:'di:l/ *n.* mateso; majaribu. *~ by fire,* jaribu la moto. *trial by ~,* hukumu ya majaribu.

**order** /'ɔ:də(r)/ *n.* taratibu; mpango; usahihi; usawa; amani; utulivu; nidhamu; amri; agizo; aina; jinsi; cheo; tabaka; daraja; upadri; chama cha watawa; kanuni; oda; hawala; hundi; hati; madhumuni; kusudi; kibali. *by ~ of the president,* kwa amri ya rais. *goods on ~,* bidhaa zilizoagizwa. *in ~ that,* ili. *take holy ~s,* -wa padri. *v.t.* amuru; agiza; panga. **~ly** *n.* mhudumu wa hospitali; askari mtumishi. *adj.* -enye adabu; -enye taratibu; makini; -a amani.

**ordinal** /'ɔ:dɪnl/ *n./adj.* -a mpango; *~ numbers,* nambari -a kuonyesha -a ngapi katika mfululizo, e.g. -a kwanza, -a pili, -a tatu.

**ordinary** /'ɔ:dɪnri/ *adj.* -a desturi; -a kawaida. *out of the ~,* si -a kawaida. **ordinarily** *adv.* aghalabu; mara nyingi; kwa kawaida; kwa desturi.

**ordination** *n.* kufanya kasisi.

**ore** /ɔ:(r)/ *n.* mbale: mawe yenye madini. *~ body,* mbalekwimbi: kiasi kikubwa cha mbale za madini ghafi.

**organ** /'ɔːgən/ *n.* chombo; kinanda; ogani: sehemu ya mwili wa kiumbe hai ifanyayo kazi maalumu. *the ~s of speech*, viungo vya matamshi. **~elle** *n.* kioganeli: vijisehemu maalumu ndani ya seli ambavyo vinaonekana kwa hadubini ambavyo hufanya kazi maalumu katika seli. **~ic** *adj.* -a ogani; -a kiumbe hai; -mfumo; -a sehemu linganifu. **organic chemistry**, kemia kaboni. **~ compound**, msombo kikaboni: msombo wa kikemikali wenye atomu za kaboni zilizoungana na atomu za hidrojeni, oksijeni, nitrojeni au elementi nyingine. **~ism** *n.* kiumbehai. **~ist** *n.* mpiga kinanda.

**organize** /'ɔːgənaɪz/ *v.t.* tunga; tengeneza. **~d** *adj. highly ~ forms of life*, -enye mfumo wa viungo uliokamilika.

**organization** /ˌɔːgənaɪ'zeɪʃn/ *n.* mfumo; utaratibu; mpangilio; chama; shirika. **organize** *v.t.* tunga; anzisha; simamia; andaa; panga; ratibu. **~r** *n.* mtungaji; msimamizi; muandaaji.

**orgasm** /'ɔːgæzem/ *n.* kilele cha hamu wanachofikia viumbe katika kujamiiana.

**orient** /'ɔːrɪənt, 'ɒr-/ *n.* nchi za mashariki. **~al** *adj.* -a mashariki; matlai.

**orifice** /'ɒrɪfɪs/ *n.* tundu; mlango; kipenyo.

**origin** /'ɒrɪdʒɪn/ *n.* asili; mwanzo; chimbuko; chanzo; wazazi; ukoo; jadi; nasaba; sababu. **original** *n.* lugha ya kwanza ya utungo; asili; mbunifu; mtu wa mtindo wa pekee. *adj.* -a kwanza; -a asili; -pya; -enye akili za kubuni; bunifu. **~ly** *adv.* kwanza; kwa asili; kwa ubunifu. **~ate** *v.t./i.* anza; anzisha; tokana; umba; tunga.

**ornament** /'ɔːnəm(ə)nt/ *n.* pambo; madoido; urembo. *v.t./i.* pamba; remba; tia madoido. **~al** *adj.* -a kupamba; -zuri; -a urembo.

**orphan** /'ɔːfn/ *n.* yatima. *v.t.* fanya yatima. **~age** *n.* nyumba ya mayatima.

**orthodox** /'ɔːθədɒks/ *adj.* -enye imani kamili; sahihi; barabara; halisi. **~y** *n.* imani halisi; matamshi sahihi yaliyokubaliwa.

**orthography** /ɔː'θɒgrəfi/ *n.* tahajia.

**oscillate** /'ɒsːɪleɪt/ *v.i./t.* bembea; bembeza; pembea.

**osmosis** /ɒz'məʊsɪs/ *n.* osimosisi: mfyonzo, mnyonyo, mnyweshelezo wa uoevu.

**ostentation** /ˌɒsten'teɪʃn/ *n.* majivuno; fahari; ushaufu.

**ostentatious** /ˌɒsten'teɪʃəs/ *adj.* -shaufu; -a mikogo; -a kujidai.

**ostracize** /'ɒstrəsʌːɪz/ *v.t.* fukuza nchini; tenga toka kwenye jamii; tenganisha.

**ostrich** /'ɒstrɪtʃ/ *n.* mbuni.

**other** /'ʌðə(r)/ *pron./adj.* ingine. *~ than*, isipokuwa; ila. **~wise** *adv.* vinginevyo; upande mwingine. *conj.* kama sivyo; la sivyo; au.

**otter** /'ɒtə(r)/ *n.* mnyama anyonyeshaye anayeishi mtoni na nchi kavu ambaye hula samaki.

**ought** /'ɔːt/ *v.* paswa; bidi; takiwa. *We ~ to stay here*, tunapaswa kukaa hapa.

**ounce** /aʊns/ *n.* wakia; aunsi.

**our** /ɑː(r)/ *adj./pron.* -etu. **~s** *pron.* -etu. **~selves** *pron.* sisi wenyewe.

**out** /aʊt/ *adv.* nje. **~of** *prep.* kutoka kwa. *~ and ~*, kabisa. *~ of date*, -liopitwa na wakati. *be ~ of breath*, isha pumzi. *~ of doors*, nje. *~ of one's mind*, -enye wazimu. *~ of temper*, -enye hasira. *~-of the way*, -geni; -a ajabu. *The truth will be ~*, ukweli utajulikana. **~er** *adj.* -a nje; -a upande wa nje. **~ermost** *adj.* -a nje kabisa.

**outbreak** /'aʊtbreɪk/ *n.* mripuko; kuanza kwa nguvu.

**outburst** /'aʊtbɜːst/ *n.* kutoka kwa ghafla; mripuko. *~ of anger*, hasira ya ghafla.

**outcast** /'aʊtkɑːst/ *n./adj.* mtu aliyetengwa na jamii.

**outcome** /'aʊtkʌm/ *n.* matokeo.

**outcry** /'aʊtkraɪ/ *n.* makelele; mayowe; kilio.

**outdo** /ˌaʊt'duː/ *v.t.* pita; shinda; zidi; fanya vyema zaidi. *He was not to be ~ne*, hakutaka kushindwa.

**outdoor** /'aʊtdɔː(r)/ *adj.* a nje. **~s** *adv.* nje.

**outfit** /'aʊtfɪt/ *n.* zana kwa kazi maalumu; sare ya kazi maalumu. **~ter** *n.* muuza nguo.
**outgrow** /ˌaʊt'grəʊ/ *v.t.* kua sana; pita kwa kukua upesi; acha kwa vile umeshakua.
**outlaw** /'aʊtlɔ:/ *n.* haramia; mhalifu. *v.t.* haramisha; fukuza kwenye jamii.
**outlay** /'aʊtleɪ/ *n* gharama; matumizi.
**outlet** /'aʊtlet/ *n.* mlango; tundu la kutokea maji, mvuke, etc.; fursa ya kutoa dukuduku.
**outline** /'aʊtlaɪn/ *n.* mstari wa kuonyesha umbo au mpaka; muhtasari. *a map in ~,* ramani ya mistari. *v.t.* chora mstari; eleza kwa muhtasari.
**outlive** /ˌaʊt'lɪv/ *v.t.* ishi au dumu kuliko; dumu hata jambo lisahauliwe.
**outlook** /'aʊtlʊk/ *n.* mandhari; matarajio; mtazamo; msimamo.
**out-patient** /'aʊtpeɪʃnt/ *n.* mgonjwa wa nje: mgonjwa atibiwaye na kurudi nyumbani.
**output** /'aʊtpʊt/ *n.* uzalishaji; habari zitokazo kwenye kompyuta.
**outrage** /'aʊtreɪdʒ/ *n.* tendo la ukatili au jeuri; tendo la kufedhehesha. *v.t.* tendea uovu; halifu. **~ous** *adj.* -a kufedhehesha; -a jeuri.
**outright** /'aʊtraɪt/ *adv.* mara; papo hapo; moja kwa moja; *He killed him ~,* alimuua papo hapo. *adj.* -a wazi.
**outset** /'aʊtset/ *n.* mwanzo. *at the ~,* mwanzoni. *from the ~,* toka mwanzo.
**outside** /ˌaʊt'saɪd/ *n./adv.* nje; mpaka; upeo; sura. *prep.* nje -a. *adj.* -a nje. *at the very ~,* sanasana.
**outskirts** /'aʊtskɜ:ts/ *n.* kiunga cha mji; kando; pembezoni.
**outspoken** /aʊt'spəʊkən/ *adj.* -enye kusema yalivyo; -nyofu.
**outstanding** /aʊt'stændɪŋ/ *adj.* -liojipambanua; -liobaki, -siolipwa; -liosalia; -liopo.
**outward** /'aʊtwəd/ *adj.* -a upande wa nje; -a usoni; -a kuonekana; -a kuelekea nje. ~(**s**) *adv.* kuelekea nje; usoni. **~ly** *adv.* kwa juujuu; kwa nje.
**outwit** /ˌaʊt'wɪt/ *v.t.* (**-tt-**) shinda kwa akili au ujanja.
**oval** /'əʊvl/ *n./adj.* umbo la yai; -enye umbo la yai.


**oval**

**ovary** /'əʊv(ə)ri/ *n.* ovari: ungo la kiumbe linalotoa gameti za kike.
**ovation** /əʊ'veɪʃn/ *n.* shangwe; vifijo; makofi.
**oven** /'ʌvn/ *n.* joko; oveni.
**over** /'əʊvə(r)/ *n.* (katika kriketi) idadi ya mipira inayotupwa mfululizo. *adv./prep.* juu; juu ya; zaidi; kupita; zaidi ya; kuhusu. *~ and above,* zaidi. *~ polite,* -enye adabu kupita kiasi. *~tired,* -liochoka kupita kiasi. **~do** *v.t.* (**~did ~done**) fanya kupita kiasi; piga chuku.
**overall** (**s**) /ˌəʊvər'ɔ:l/ *n.* ovaroli; bwelasuti.
**overboard** /'əʊvəbɔ:d/ *adv.* kutoka chomboni. *fall ~,* anguka baharini.
**overcoat** /'əʊvəkəʊt/ *n.* koti kubwa la kuvaa juu ya nguo nyengine.
**overcome** /ˌəʊvə'kʌm/ *v.t.* (**overcame, overcome**) shinda; pita; weza; dhoofisha; tiisha.
**overdraw** /ˌəʊvə'drɔ:/ *v.t./i.* (**overdrew, overdrawn**) toa kuliko fedha zilizopo.
**overdraft** *n.* ovadrafti: deni katika akaunti ya benki.
**overdue** /ˌəʊvə'dju:/ *adj.* -a kuchelewa; -a kupitiliza muda.
**overgrown** /ˌəʊvə'grəʊn/ *adj.* -liokuwa upesi zaidi; -liofunikwa kwa majani. *garden-beds ~ with weeds,* matuta yaliyofunikwa na magugu.
**overhang** /ˌəʊvə'hæŋ/ *n.* sehemu iliyotokeza. *v.t./i.* (**-hung**) tokeza juu ya; elekea kutokeza.
**overhaul** /ˌəʊvəhɔ:l/ *n.* ukaguzi wa jumla; utengenezaji. *v.t.* chunguza kwa makini; suka upya.
**overhead** /ˌəʊvə'hed/ *adj.* -a juu; -a uendeshaji. *~ expenses,*gharama za uendeshaji. *adv.* juu ya kichwa. *the stars ~,* nyota mbinguni.
**overhear** /ˌəʊvə'hɪə(r)/ *v.t* (**overheard**) sikia bila kukusudia; dukiza.

**overlap** /ˌəʊvəˈlæp/ *n.* sehemu inayolingana; kitu kilicho juu ya. *v.t./i.* (**-pp-**) pishana; pishanisha; lingana kwa mambo mengine.

**overlook** /ˌəʊvəˈlʊk/ *v.t.* tazama kutoka juu; -toangalia; samehe; simamia; -togundua; -totilia maanani. ~ *an error,* samehe kosa.

**overnight** /ˌəʊvəˈnaɪt/ *adv.* usiku kucha. *adj.* -a usiku kucha; -a ghafla sana.

**overpower** /ˌəʊvəˈpaʊə(r)/ *v.t.* shinda; tiisha. **~ing** *adj.* -enye nguvu nyingi; -lioshinda kwa nguvu. *an ~ing stink,* harufu mbaya tena kali sana.

**overrule** /ˌəʊvəˈruːl/ *v.t.* tangua; batilisha.

**overrun** /ˌəʊvəˈrʌn/ *v.t.* (**overran, overrun**) enea; tanda; pitiliza muda uliopangwa. *The weeds have ~the whole garden,* magugu yameenea bustani yote.

**overseas** /ˌəʊvəˈsiːz/ *adj.* -a ng'ambo; -a nje; -a ughaibuni. *go ~s,* enda ng'ambo.

**oversee** /ˌəʊvəˈsiː/ *v.t.* (**oversaw, overseen**) simamia; angalia. **~r** *n.* msimamizi.

**oversight** /ˈəʊvəsaɪt/ *n.* usimamizi; uangalizi; koseo; usahaulifu.

**oversleep** /ˌəʊvəˈsliːp/ *v.i.* lala mno; chelewa kuamka; pitiliza usingizi.

**overt** /əʊˈvɜːt/ *adj.* -a wazi; -a hadharani. **~ly** *adv.* dhahiri shahiri.

**overtake** /ˌəʊvəˈteɪk/ *v.t.* (**over-took, overtaken**) pita; kuta; pata kwa ghafla.

**overthrow** /ˌəʊvəˈθrəʊ/ *v.t.* (**over-threw, overthrown**) shinda; angamiza; angusha; pindua. *n.* maangamizi.

**overtime** /ˌəʊvətaɪm/ *n./adv.* ova-taimu: saa za ziada.

**overwhelm** /ˌəʊvəˈwelm/ *v.t.* ghari-kisha; angamiza; shinda kabisa; funikiza; funika.

**oviduct** /ˈəʊvɪdʌkt/ *n.* kirijaova: jozi ya virija ambavyo hutokea kwenye tungu la mwili kwenda nje kwa majike na hufanya kazi ya kuisafirisha na kuilisha ova.

**ovipositor** /ˌəʊvɪˈpɒzɪtə/ *n.* ovipozita: ungo kwenye ncha ya nyuma ya wadudu ambapo mayai hutolewa yanapotagwa.

**ovulation** /ˌɒvjuˈleɪʃn/ *n.* uovishaji: uzalishaji au utoaji mayai kutoka kwenye ovari.

**ovule** /ˈɒvjuːl, ˈəʊ-/ *n.* chembekike: kigimba kinachokuwa na kifuko cha kiinitete na kwa hivyo seli ya kike baada ya utungishaji hukua na kuwa mbegu.

**ovum** /ˈəʊvəm/ *n.* ova: gameti ya kike kwa wanyama inayotolewa na ovari.

**owe** /əʊ/ *v.t.* wiwa; -wa na deni; wajibika; paswa; pata kwa; tokana na. *He ~s me money,* namwia; namdai. *(fig.) I ~ my success to hardwork,* kufanikiwa kwangu ni kwa jitihada yangu. *I ~ loyalty to my president,* napaswa kumtii Rais wangu. **owing** *adj.* -siolipwa bado; -enye kudaiwa. **owing to** *prep.* kwa sababu ya. *It is all owing to you,* yote ni juu yako.

**owl** /aʊl/ *n.* bundi; babewatoto.


owl

**own** /əʊn/ *adj.* enyewe. *my ~,* -angu. *your ~,* -ako. *v.t.* miliki. *v.i.* kiri; tambua. **~er** *n.* mwenyewe; mmiliki. **~erless** *adj.* bila mwenyewe. **~ership** *n.* umilikaji.

**ox** /ɒks/ *n.* (**~en**) ng'ombe; maksai. **~bow** *n.* **1.** nira ya ng'ombe. **2.** ziwapinde (kwa mto).

**oxidation** /ˌɒksɪˈdeɪʃn/ *n.* uoksi-dishaji: utaratibu wa kuongeza oksijeni, kupunguza hidrojeni au elektroni kwenye kemikali yoyote au madini.

**oxide**/ˈɒksʌɪd/ *n.* oksaidi: kampaundi yoyote ya oksijeni na elementi nyengine. **oxidize** *v.t./i.* unganika au unganisha na oksijeni.

**oxygen** /ˈɒksɪdʒən/ *n.* oksijeni: hewa safi isiyo na harufu, rangi wala ladha. **~ cycle**, duru oksijeni: mzunguko wa oksijeni katika mazingira kimaumbile. **~ debt**, deni oksijeni: hali inayojitokeza wakati ikiwa misuli haipati

oksijeni ya kutosha ambapo seli huanza kupumua bila oksijeni. **~ated blood**, damu safi: damu yenye oksijeni.

**oyster** /'ɔɪstə(r)/ *n.* chaza; kombe.



oyster

**ozone** /'əʊzəʊn/ *n.* ozoni: aina ya oksijeni yenye atomu tatu kwenye molekuli na ina harufu inayolingana na ile ya klorini. **~ hole**, tundu ozoni: tundu ambazo zinajitokeza katika tabaka ya ozoni kutokana na tabaka hiyo kuathiriwa na kemikali zinazochafua mazingira. **~ layer**, tabaka ya ozoni: tabaka iliyoko kwenye angahewa ya juu, kilomita 15 hadi 30 juu ya uso wa dunia ambako ozoni hupatikana kwa wingi.

# Pp

**pace** /peɪs/ *n.* hatua; mwendo wa kutembea au kukimbia. *keep ~ with (sb.)*, enda sambamba na. *v.i./t.* tembea polepole; pima kwa hatua; pima mwendo wa mkimbiaji katika mashindano.

**pacific** /pə'sɪfɪk/ *adj.* -a amani; -tulivu; pole. **~ation** *n.* amani; suluhu; mapatano. **pacifism** *n.* nadharia ya kupinga vita vyovyote. **pacifist** *n.* mshikilia nadharia ya amani. **pacify** *v.t.* tuliza; suluhisha; patanisha.

**pack** /pæk/ *n.* mzigo; mtumba; robota; furushi; bunda; genge; kundi; jozi ya karata. *~animal*, mnyama anayebeba mizigo. *a ~ of thieves*, kundi la wezi. *v.t./i.* funga; fungasha; songa; songamana; hifadhi ndani ya makopo. *~ sb. off, send sb. ~ing*, fukuza. **~age** *n.* kipeto; bahasha; furushi; robota. **~et** *n.* kifurushi; kibunda; pakiti. **~ing** *n.* ufungaji mizigo; kitu kihifadhicho vingine katika kufunga.

**pad** /pæd/ *n.* **1**. pedi; kinga; namna ya kitambaa laini kitumikacho kunyonya vitu vya majimaji; fungu la karatasi za kuandikia. **2**. pedi ya wino wa muhuri. **3**. unyayo laini wa mnyama. **4**. jukwaa la kurushia makombora; **5**. mto mdogo. **6**. kata. *v.t.* tia pedi ili kukinga. *~ out*, refusha kwa kutia maneno yasiyo na maana.

**padding** /'pædɪŋ/ kitu cha kujazia tu.

**paddle** /'pædl/ *n.* kafi; kasia. *v.t./i.* piga kafi; tembeatembea majini. **~steamer** *n.* meli iendeshwayo kwa magurudumu ya kafi. **~ wheel** *n.* gurudumu la kafi.

**paddy** /'pædi/ *n.* mpunga. **~field** *n.* shamba la mpunga.

**padlock** /'pædlɒk/ *n.* kufuli. *v.t.* funga kwa kufuli.



padlock

**padre** /'pɑːdreɪ, -dri/ *n.* kasisi; padiri.

**pagan** /'peɪg(ə)n/ *n./adj.* mpagani; -a kipagani. **~ism** *n.* upagani.

**page** /peɪdʒ/ *n.* ukurasa; laha; mtoto mtumishi; tarishi. *v.t.* tia namba za kurasa.

**pail** /peɪl/ *n.* ndoo.



pail

**pain** /peɪn/ *n.* maumivu; uchungu; huzuni; sikitiko. *on ~ of death*, kwa kulipa kisasi cha mauti. *take ~s*, fanya juhudi. *v.t.* umiza; huzunisha; kera; tia uchungu. **~ful** *adj.* -a kuumiza; -a kuhuzunisha. **~fully** *adv.* kwa maumivu; kwa huzuni. **~less** *adj.* -sioumiza; bila maumivu. **~lessly** *adv.* bila maumivu. **~staking** *adj.* -enye kujitahidi; -enye bidii.

**paint** /peɪnt/ *n.* rangi; dalia. *v.t./i.* paka rangi; chora picha ya rangi; remba; fafanua habari. **~er** *n.* mpaka rangi; mchoraji. **~ing** *n.* picha ya rangi; uchoraji picha ya rangi; utiaji rangi.

**pair** /peə(r)/ *n.* jozi; pea; doti; mume na mke. *a ~ of shoes*, pea ya viatu. *a ~ of scissors*, mkasi. *a ~ of trousers*, suruali. *a ~ of spectacles*, miwani. *in ~s*, wawili wawili; mbili mbili; etc.

**palace** /'pæləs/ *n.* ikulu; kasri; hekalu; jumba kubwa.

**palatial** /pə'leɪʃl/ *adj.* -a kasri; -a jumba kubwa; -a anasa.

**palaeolithic** /ˌpalɪə(ʊ)'lɪθɪk/ *adj.* paliolithiki: -a enzi ya zana za mawe.

**palaeontology** /ˌpalɪɒn'tɒlədʒi/ *n.* paleontolojia: elimu ya viumbe vilivyomo ardhini vilivyogeuka kuwa mawe miaka mingi iliyopita.

**palate** /'pælət/ *n.* kaakaa; maonjo. *soft ~*, kaakaa laini. *hard ~*, kaakaa gumu.

**palatable** /'pælətbl/ *adj.* -tamu; -a kupendeza hasa kwa kula; -a kukubalika.

**pale** /peɪl/ *adj.* -liokwajuka; ranga: -enye rangi nyepesi.

**pallet**, **palliasse** /'palɪt/ *n.* godoro la majani makavu.

**pallisade cells** *n.* seli palisadi: seli za jani zenye kloroplasti nyingi ambamo usanisi mwanga hutendeka.

**palm**[1] /pɑ:m/ *n.* **1.** kiganja; kitanga cha mkono; gao. *v.t.* fumbata. *~ sth. off (on sb.)*, toa, -pa kwa hila. **~ist** *n.* mtabiri asomaye kiganja. **~istry** *n.* usomaji kiganja.

**palm**[2] /pɑ:m/ *n.* mti wa jamii ya mnazi, mvumo, etc.; *date ~*, mtende. *~ leaf*, kuti. *carry off the ~*, shinda. *~ Sunday*, Jumapili kabla ya pasaka; jumapili ya mitende/matawi. **~y** *adj.* -enye kusitawi; -enye neema. *in my ~ days*, siku zangu za neema.

**palpitate** /'palpɪteɪt/ *v.i.* pigapiga; puma; tetemeka. **palpitation** *n.* kiherehere au mpapatiko wa moyo.

**pamper** /'pæmpə(r)/ *v.t.* dekeza; endekeza.

**pamphlet** /'pamflɪt/ *n.* kijitabu; kabrasha. **~eer** *n.* mwandishi wa vijitabu.

**pan**[1] /pan/ *n.* chungu; sufuria; chuma; kikaango. *frying ~*, kikaango. **~cake** *n.* gole; mkate wa maji; mkate wa chila; kitumbua.

**pan**[2] /pæn/ *prefix* -a -ote.

**pancreas** /'paŋkrɪəs/ *n.* kongosho: tezi iliyo karibu sana na utumbo ambayo kazi yake ni kutengeneza vimeng'enya kadhaa ambavyo husaidia kumeng'enya chakula.

**pane** /peɪn/ *n.* kioo cha dirisha.

**panel** /'pænl/ *n.* peneri; paneli; jopo; kundi la wanenaji wakuu katika majadiliano.

**pang** /pæŋ/ *n.* kichomi; maumivu makali ya ghafla.

**panic** /'pænɪk/ *n.* hofu ya ghafla. **~-stricken** *adj.* -lioshikwa na woga mkuu wa ghafla. **~ky** *adj.* -enye kusababisha hofu ya ghafla.

**pant** /pænt/ *n.* utwetaji; uhemaji. *v.i./t.* tweta; hema; kukutika. *~ for*, taka sana; tamani. *~ out*, sema huku unahema.

**pantry** /'pæntri/ *n.* stoo ya vyombo vya kulia; stoo ya chakula.

**papa** /pə'pɑ:, 'pɑ:pə/ *n.* (neno la kitoto) baba.

**paper** /'peɪpə(r)/ *n.* karatasi; gazeti; hati; kitambulisho; makala; maswali ya mtihani. *v.t.* bandika karatasi ukutani; funika kwa karatasi. **~hanger** *n.* fundi wa kubandika karatasi za mapambo kwenye kuta. **~knife** *n.* kisu cha kufungulia barua. **~weight** *n.* uzito wa kuzuia karatasi zisipeperuke.

**papyrus** /pə'pʌɪrəs/ *n.* mafunjo; aina ya karatasi za kizamani huko Misri.

**par** /pɑ:(r)/ *n.* wastani; kiwango cha kawaida. *on ~ with*, sawa na. **~ity** *n.* usawa; ulinganifu. *parity of exchange*, viwango rasmi vya kubadilisha fedha.

**parable** /'pærəbl/ *n.* fumbo; hadithi ya fumbo yenye maadili.

**parabola** /pə'rab(ə)lə/ *n.* parabola: mchirizo bapa unaofanywa kwa kukata pia kwenye bapa sambamba na upande wake. **parabolic** *adj.* parabola: -enye kuhusiana au kufanana na piadufu.



parabola

**parachute** /'pærəʃu:t/ *n.* mwavuli;

parachuti. **parachutist** *n.* mtu arukaye kwa parachuti; askari wa miavuli.


parachute

**parade** /pə'reɪd/ *n.* gwaride; paredi; maonyesho; fahari; njia ya kutembelea pwani au bandarini. ~ *ground,* uwanja wa gwaride. *make a ~ of one's virtues,* jaribu kuwavutia watu kwa kujionyesha. *v.t./i.* panga kwa ajili ya gwaride; pangana; andamana; tembeza; onyesha. *He ~s his strength on every occasion,* aonyesha nguvu zake kila wakati.

**paradise** /'parədʌɪs/ *n.* peponi; mahali pa raha. *the gate of ~,* nyota ya jaha.

**paradox** /'pærədɒks/ *n.* kweli iliyo kama uwongo; kitendawili; neno linaloonekana kama kinyume kumbe ni sahihi; fumbo la maneno. **~ical** *adj.* -kinzani.

**paraffin** /'pærəfɪn/ *n.* mafuta ya taa. ~ *wax,* nta ya mshumaa. *liquid ~,* mafuta ya nyonyo.

**paragraph** /'pærəgrɑ:f/ *n.* aya; ibara.

**parallel** /'pærəlel/ *n.* mfano; kifani; mlinganisho; msambamba. **~ circuit**, saketi sambamba: vijenzi vya saketi vilivyounganishwa kwa kuelekeana. **~ of latitude**, msambamba wa latitudo. *adj.* sambamba; -a kulingana; sawa. *v.t.* fananisha; wa sambamba. **~ogram** *n.* msambamba.


parallelogram

**paralysis** /pə'ralɪsɪs/ *n.* kiharusi; maradhi ya baridi; upoozaji.

**paralyse** /'pærəlaɪz/ *v.t.* poozesha; pooza; duwaza; fadhaisha. **paralytic** *n. /adj.* mtu aliyepooza.

**parameter** /pə'ramɪtə/ *n.* parameta; kigezo; mfiko.

**paramount** /'pærəmaʊnt/ *adj.* -kuu; kubwa.

**parapet** /'parəpɪt/ *n.* ukingo au ukuta mfupi pembezoni mwa daraja.

**paraphrase** /'pærəfreɪz/ *n./v.t.* ufafanuzi; fasili; maelezo; eleza; fafanua; fasili; kuelezea aya/fungu la maneno kwa maneno mengine.

**parasite** /'pærəsaɪt/ *n.* kimelea; kupe; mnyonyaji. **parasitic** *adj.* -enye kunyonya; -enye kuishi kwa kudusa. **parasitism** *n.* umelea: hali ambapo kiumbe mmoja huishi kwa kumtegemea mwengine.

**parcel** /'pɑ:sl/ *n.* kifurushi. *part and ~ of,* sehemu muhimu ya. *v.t.* (**-ll-**) *~ out,* gawanya; gawa katika mafungu.

**parch** /pɑ:tʃ/ *v.t.* unguza; tia joto; kausha; choma.

**pardon** /'pɑ:dn/ *n.* msamaha; samahani. *v.t.* samehe. **~able** *adj.* -a kusameheka. **~ably** *adv.* kwa kusameheka.

**parent** /'pærənt/ *n.* mzazi. **~age** *n.* nasaba; ukoo; uzawa. *of unknown ~age,* -siojulikana ukoo halisi. **~al** *adj.* -a wazazi; -a kama wazazi.

**paranthesis** /pə'rɛnθɪsɪs/ *n.* mabano: alama hii ( ) au hii { } au hii [ ]. *in ~,* katika mabano.

**paranthentic(al)** *adj.* -a mabano; -a katika mabano.

**parish** /'pærɪʃ/ *n.* parokia; mtaa. **~ioner** *n.* mkazi wa parokia.

**park** /pɑ:k/ *n.* bustani; mbuga; kiwanja cha kuwekea silaha za vita. *car ~,* maegesho ya gari. **national ~**, mbuga ya taifa. *v.t.* egesha. **~ing** *n.* maegesho. *~ lot,* maegesho. **~ meter**, mita ya maegesho.

**Parkinson's disease** *n.* ugonjwa wa kutetemeka au kukukutaa.

**Parkinson's law** *n.* nadharia kwamba kasi ya kazi hufuatana na muda uliotengwa.

**parliament** /'pɑ:ləm(ə)nt/ *n.* bunge. **~arian** *n.* mbunge. **~ary** *adj.* -a bunge.

**parlour** /'pɑ:lə(r)/ *n.* sebule; ukumbi; chumba cha wateja.

**parody** /'pærədi/ *n.* mwigo wa kubeza. *v.t.* iga kwa kubeza.

**parrot** /'pærət/ *n.* kasuku; mtu aigaye kikasuku. *v.t.* iga kikasuku.

**parse** /pɑ:z/ *v.t.* ainisha; changanua; pambanua maneno kisarufi.

**parsley** /'pɑ:sli/ *n.* kotimiri; aina ya

mmea wenye maua meupe yenye harufu nzuri yatumikayo katika kuongeza ladha ya chakula.

**parsnip** /'pɑ:snip/ *n.* aina ya mboga kama kiazi.

**part** /pɑ:t/ *n.* sehemu; kipande; kiasi; janibu; nafasi; wajibu; upande; aina. *on my ~,* kwa upande wangu. *on the ~ of Asha,* kwa upande wa Asha. *take ~ in,* shiriki. *act a ~ in play,* igiza katika mchezo. *take sb.'s ~,* unga mkono. *take sth. in good ~,* kubali bila kinyongo. *(grammar) ~s of speech,* aina za maneno. *v.t./i.* tenga; tengana; gawa. *~ with,* acha; achana na. **~ing** *n.* mpaka wa nywele; uondokaji; kuagana; mfarakano; kuachana. *a man who doesn't like ~ with his money,* mtu bahili. **~ly** *adv.* kwa upande mmoja; nusu; sehemu; kidogo. **~song** *n.* wimbo wa pamoja. **~-time** *adj./adv.* -a muda maalumu. *~-time teaching,* ufundishaji katika muda maalumu. **~ial** *adj.* -a sehemu; sio kamili; -a kupendelea; -a kupenda. **~iality** *n.* upendeleo; mapenzi; shauku. **~ially** *adv.* kwa sehemu; kwa upendeleo. **~ition** *n.* mgawanyo; ugawanyaji; sehemu; chumba; kitenganishi. *v.t.* gawa; gawanya; tenga.

**partake** /pɑ:'teɪk/ *v.i.* (**partook**, **partaken**) shiriki; onja; chukua sehemu ya; -wa na sifa fulani.

**participate** /pɑ:'tɪsɪpeɪt/ *v.i.* shiriki. **participant** *n.* mshiriki. **participation** /pɑ:ˌtɪsɪ'peɪʃn/ *n.* ushiriki.

**participle** /'pɑ:tɪsɪp(ə)l/ *n.* badiliko la kitenzi kuonyesha hali inayoendelea. *present ~,* wakati uliopo; hali ya kuendelea.

**particle** /'pɑ:tɪkl/ *n.* chembe; *(grammar)* kishirikishi. **~ model and theory**, nadharia chembe: mbinu ya kuelezea mjengeko wa mata kwa atomu na molekuli.

**particular** /pə'tɪkjələ(r)/ *n.* habari kwa ukamilifu. *go into ~s,* eleza kwa urefu. *adj.* mahsusi; maalumu; -a pekee; -chaguzi; -angalifu. *He's very ~ in what he eats,* ni mchaguzi sana kwa chakula chake. *in ~,* hasa. **~ize** *v.t.* taja -moja -moja; orodhesha; pambanua. **~ly** *adv.* zaidi; hasa.

**partisan** /'pɑ:tɪzan, ˌpɑ:tɪ'zan/ *n.* mfuasi mwenye ari; mpiganaji mzalendo.

**partner** /'pɑ:tnə(r)/ *n.* mshirika; mwenza; mbia; patna. *v.t.* -wa mbia. **~ship** *n.* ubia.

**partridge** /'pɑ:trɪdʒ/ *n.* kwale.

**parts per million** (**ppm**) *n.* sehemu kadhaa katika sehemu milioni moja.

**parturition** /pɑ:tjʊ'rɪʃ(ə)n/ *n.* kuzaa: tendo la kutoa mtoto kutoka tumboni.

**party** /'pɑ:ti/ *n.* chama; mtu mmoja miongoni mwa wengi; jopo; dhifa; karamu; pati. *the* **~ system**, mfumo wa utawala kwa vyama vya siasa. *one* **~ system**, mfumo wa chama kimoja. **multi ~ system**, mfumo wa vyama vingi. *put public interest before ~,* weka mbele maslahi ya umma kuliko chama. *He was a ~ to their actions,* alishirikiana nao.

**pascal** /'pask(ə)l/ *n.* paskali: kizio cha kanieneo sawa na nyutoni moja kwa kila mita ya eneo.

**pass** /pɑ:s/ *n.* kufaulu mtihani; pasi; kibali; pasipoti; njia nyembamba. *v.i./t.* pita; pitisha; ruka; malizika; -pa; tawanya; idhinisha; kubali; -fa; tokea; fanyika; pasia; zidi. *~ a remark,* tamka. *~ the time of day with,* ongea na. *He ~ed away yesterday,* alifariki jana. *The pain will soon ~ off,* maumivu yataisha sasa hivi. *~ time,* pitisha wakati. *~ judgement, sentence,* toa hukumu. *~ sb. by,* puuza. *~ for,* kubalika kuwa. *~ off,* fanyika. *~ out, (colloq.)* zimia; zirai. *~ sth. or sb. over,* -tozingatia. *Things have come to a sad ~,* mambo yametatizika. *come to ~,* tokea. *bring to ~,* fanya, tekeleza. **~able** *adj.* (kwa njia, etc.) -a kuendeka; -a kupitika; -a kadiri; -a wastani. **~ably** *adv.* kwa kupitika; kwa kiwango cha wastani. **~age** *n.* upitaji; njia; safari; mlia; dondoo; fungu la maneno. *the ~ of times,* kupita kwa wakati. *book one's ~ to*

*Zanzibar,* kata tiketi ya kwenda Zanzibar. **~book** *n.* kitabu cha benki. **~-by** *n.* mpita njia. **~port** *n.* pasi; pasipoti. **~word** *n.* neno la siri la kutoa ruhusa au utambuzi.

**passenger** /'pæsɪndʒə(r)/ *n.* abiria; msafiri.

**passion** /'pæʃn/ *n.* hisia kali; hamaki; uchu. **~ate** *adj.* -enye hisia kali.

**passive** /'pæsɪv/ *adj.* -a kutoonyesha hisia; -a kukaa tu; baridi. **~ voice**, kauli ya kutendwa. **~ immunity**, kinga ya muda: kinga mwili ambapo fingo hutolewa kutoka mnyama mmoja na kutiwa kwenye mnyama mwingine ili kukinga maradhi. **~ smoking**, uvutaji sihiari: uvutaji wa moshi wa sigara kwa watu wasiovuta sigara unaosababishwa na wavutaji walio karibu nao. **~ transport**, usafirishaji sihiari: usafirishaji wa dutu iliyoyeyushwa katika seli kwa njia ya ueneaji. **~ly** *adv.* bila ya kuonyesha hisia. **~ness** *n.* hali ya kutoonyesha hisia.

**passivity** /pæ'sɪvəti/ *n.* hali ya kutoonyesha hisia; uvumilivu.

**passover** /'pɑ:səʊvə(r)/ *n.* pasaka; ni sherehe ya Kiyahudi kukumbuka kukombolewa kwa Wayahudi toka utumwani Misri.

**past** /pɑ:st/ *n.* zamani; wakati uliopita; mambo yaliyopita zamani. *adj.* -a zamani; -liopita. *~ tense*, -a wakati uliopita. *prep./adv.* kupita; kufikia; kuvuka.

**paste** /peɪst/ *n.* lahamu; gundi; unga uliopondwa; vyakula vilivyopondwa; vitobandia. *v.t.* gandamisha; ponda kuwa laini.

**pasteurize** /'pɑ:stʃərʌɪz/ *v.t.* ondoa vijidudu vya maradhi katika maziwa kwa kupasha moto.

**pastry** /'peɪstri/ *n.* unga uliopondwa.

**pasture** /'pɑ:stʃə(r)/ *n.* malisho. *v.t.* chunga. **pasturage** *n.* machunga; malisho.

**pat** /pæt/ *n.* kikofi; kibonge cha siagi. *v.t.* pigapiga. *~ sb. on the back,* shangilia; pongeza. *adv.* sawia; mara; papo hapo; bila kukawia; mara moja. *The answer came ~,* majibu yalikuja haraka. *stand ~,* kataa katakata.

**patch** /pætʃ/ *n.* kiraka; plasta; pechi; kidoa; kikataa. *not a ~ on,* haifikii hata kidogo. *v.t.* tia kiraka. *~ up,* chomelea. *(fig.) ~ up a quarrel,* patana; patanisha kwa muda. **~work** *n.* nguo iliyoshonwa kwa viraka; kazi iliyofanywa kwa kuondosha njiani. **~y** *adj.* -a virakaviraka; -a namna mbalimbali.

**patella** /pə'tɛlə/ *n.* kilegesambwa; piagoti: kifupa kidogo cha bapa na mviringo katika kiungo cha goti.

**patent** /'pat(ə)nt/, 'peɪt / *n.* hataza: kibali rasmi kinachotolewa kwa kutengeneza au kuuza bidhaa fulani; namna mpya ya kutengeneza bidhaa. *adj.* dhahiri; wazi; bayana; -enye kulindwa na serikali -siigwe na wingine; -a asili; -a akili. **~ defect**, dosari dhahiri. **letter ~**, amri ya serikali ya kuruhusu utengenezaji wa kitu na kukilinda kisiigwe na wingine. *~ leather,* ngozi iliyopakwa rangi ngumu yenye kung'aa sana. *v.t.* andikisha hataza. **~ee** *n.* -enye hataza.

**paternal** /pə'tɜ:nl/ *adj.* -a kuumeni; -a baba; -a kama baba. **~ly** *adv.* kama baba; kwa kuumeni. **paternity** *n.* ubaba; kuumeni.

**path** /pɑ:θ/ *n.* (**~s**) njia.

**pathetic** /pə'θetɪk/ *adj.* -a kutia huruma.

**pathogen** /'pɑθədʒ(ə)n/ *n.* pathojeni: kiumbe ambacho huleta ugonjwa katika mwili wa kiumbe kingine.

**pathology** /pə'θɒlədʒi/ *n.* patholojia: sayansi ya magonjwa.

**pathological** /ˌpæθə'lɒdʒɪkl/ *adj.* -a patholojia; -a maradhi.

**pathologist** /pə'θɒlədʒɪst/ *n.* mwanapatholojia.

**patience** /'peɪʃns/ *n.* subira; uvumilivu; ustahamilivu; mchezo wa karata wa mtu peke yake.

**patient** /'peɪʃnt/ *n.* mgonjwa; mwele. *adj.* -stahamilivu; -enye subira.

**patriot** /'pɑtrɪət, 'peɪt-/ *n.* mzalendo. **~ic** *adj.* -a uzalendo. **~ism** *n.* uzalendo.

**patrol** /pə'trəʊl/ *n.* doria; vyombo vya doria; watu wa doria. *v.t./i.* (**-ll-**) fanya doria.
**patron** /'peɪtrən/ *n.* mlezi; mteja wa kila siku dukani; mfadhili. **~age** *n.* msaada; ulezi; uangalizi. **~ize** *v.t.* lea; linda; -a mteja wa kudumu.
**patter** /'pætə(r)/ *n.* **1.** vishindo vidogovidogo vya mfululizo: *the ~ of rain on a roof,* vishindo vya mvua kwenye paa. **2.** kiwizi: lugha ya kikundi cha watu fulani. *v.i./t.* fanya vishindo vidogovidogo kama mvua; sema upesiupesi.
**pattern** /'pætn/ *n.* kiolezo; ruwaza; ruzuni; sampuli; nakshi; mkondo; mwelekeo; mpangilio.
**pauper** /'pɔ:pə(r)/ *n.* maskini; fukara; mkata; ombaomba; lofa. **~ize** *v.t.* fukarisha.
**pause** /pɔ:z/ *n.* kikomo; kituo; kipumziko; mapumziko. *give ~ to,* fanya mtu asite na afikiri kwanza. *v.i.* pumzika kidogo; sita; tua kwa muda.
**pave** /peɪv/ *v.t.* tia mawe chini; tia kibamba. *(fig.) ~ the way for,* andalia njia. **~ment** *n.* njia ya miguu pembezoni mwa njia kuu.
**pavilion** /pə'vɪliən/ *n.* banda la maonyesho; kibanda cha wachezaji na watazamaji.
**paw** /pɔ:/ *n.* unyayo wa mnyama wenye makucha. *v.t.* parura; papasa.
**pawn**[1] /pɔ:n/ *n.* kitunda; *(fig.)* kibaraka.
**pawn**[2] /pɔ:n/ *n.* rehani; uwekaji rehani. *v.t.* weka rehani. *His watch is in ~,* saa yake ameiweka rehani. **~-broker** *n.* mweka rehani. **~shop** *n.* duka la rehani.
**pay** /peɪ/ *n.* malipo; mshahara; ujira; haki. *v.t./i.* (**paid**) lipa; fidia. *~ for,* lipia; adhibiwa kwa. *~ attention,* angalia; sikiliza. *~ a visit,* zuru. *~ a compliment to sb.,* salimu; sifu. *~ out,* (kwa kamba) legeza polepole. **~able** *adj.* -a kulipwa. **~ee** *n.* mlipwaji. **~master** *n.* mlipaji. **~ment** *n.* malipo; ulipaji.
**pea** /pi:/ *n.* njegere; mbaazi; choroko; dengu; adesi; kunde. **~nut** *n.* njugu; karanga.
**peace** /pi:s/ *n.* amani; salama; raha; utulivu. **~able** *adj.* -tulivu; -a kutaka amani; -pole. **~ably** *adv.* kwa amani. **~ful** *adj.* -a amani; -tulivu. **~fully** *adv.* kwa amani. **~maker** *n.* mpatanishi; msuluhishi. **~offering** *n.* dhabihu; uradhi; kitulizo.
**peacock** /'pi:kɒk/ *n.* tausi.
**pea-hen** /'pi:hen/ *n.* tausi jike. **pea-chick** *n.* kinda la tausi.


peacock

**peak** /pi:k/ *n.* kilele; upeo; kikomo.
**peal** /pi:l/ *n.* mlio wa kengele; seti ya kengele zipigwazo pamoja. *~ of thunder,* ngurumo. *v.t. /i.* vumisha; piga; liza; lia; vuma; nguruma.
**pear** /peə(r)/ *n.* pea; piasi/peasi: aina ya tunda lenye nyama laini na majimaji. *~ tree,* mpea.


pear

**pearl** /pɜ:l/ *n.* lulu. *~-white,* nyeupe pe.
**peasant** /'peznt/ *n.* mkulima mdogo. **~ry** *n.* wakulima.
**pebble** /'pebl/ *n.* mbwe; changarawe.
**peck** /pek/ *n.* dono; udonoaji; busu la haraka. *v.t./i.* donoa; gogota; onjaonja. *(colloq.) ~ at one's food,* -la chakula kidogo. **~ish** *adj.* -enye njaa.
**peculiar** /pɪ'kju:liə(r)/ *adj.* -geni; -a ajabu; -a peke yake. **~ly** *adv.* hasa; zaidi; kigeni; kiajabu. **~ity** *n.* upekee; kioja; kitu cha ajabu.
**pedal** /'pɛd(ə)l/ *n.* pedeli. *v.t./i.* endesha kwa pedeli.
**pedestrian** /pə'destriən/ *n.* mwenda kwa miguu. *adj.* -a kwenda kwa miguu; (kwa maandishi au hotuba) -siovutia. **~ crossing**, kivuko cha waenda kwa miguu barabarani.
**peel** /pi:l/ *n.* ganda; gamba. *v.t.* menya; chuna; papatua; bambua. *v.i.* banduka; chunika.
**peep** /pi:p/ *n.* bodi; kuchungulia; mapambazuko. *v.i.* chungulia; piga bodi; onekana; chomoza. *The sun ~ed out from the clouds,* jua lilichomoza kidogo tu.
**peer**[1] /pɪə(r)/ *v.i.* angalia kwa makini; kazia macho.

**peer**[2] /pɪə(r)/ *n.* mwenza; rika; aliye sawa kwa cheo etc. **~age** *n.* watu wanaolingana; ulinganifu wao. **~ess** *n.* mke wa lodi; lodi mwanamke. **~less** *adj.* bila kifani.

**peg** /peg/ *n.* kigingi; mambo; kibanio; hesi; hoja; kisa; sababu; pegi. *a square ~ in a round hole,* mtu asiyefaa kwa kazi afanyayo. *v.t./i.* (**-gg-**) pigilia vigingi; weka kima cha bei au malipo. *~ away at,* fanya kazi sana. *~ out, (colloq.)* -fa; kata kamba.

**pelican** /ˈpelɪkən/ *n.* ndege aitwaye mwari.


**pelican**

**pelt** /pelt/ *n.* ngozi ya mnyama ikiwa na manyoya; kasi. *v.t./i.* **1.** shambulia kwa kutupia vitu **2.** nyesha kwa nguvu. *at full ~,* mbio sana; haraka iwezekanavyo.

**pen**[1] /pen/ *n.* kalamu ya wino; mwandiko; kazi ya uandishi. *v.t.* (**-nn-**) andika barua, etc. **~manship** *n.* sanaa ya uandishi. **~knife** *n.* kisu kidogo cha kukunja.

**pen**[2] /pen/ *n.* zizi; ua; tundu; kizimba. *v.t.* (**-nn-**) fungia. *~ sb. up,* fungia ndani.

**penal** /ˈpi:nl/ *adj.* -a adhabu. *~ servitude,* kazi ngumu. **~ize** *v.t.* adhibu; tia hatiani; onea. **~ty** *n.* adhabu; malipo ya kosa; penalti.

**penance** /ˈpenəns/ *n.* toba.

**pencil** /ˈpensl/ *n.* penseli. *v.t.* (**-ll-**) andika kwa penseli. *~ sharpener,* kichongeo. *eyebrow ~,* wanja wa penseli.

**pending** /ˈpendɪŋ/ *adj.* siokwisha bado. *prep.* mpaka; wakati wa; kabla.


**pendulum**

**pendulum** /ˈpɛndjʊləm/ *n.* penduli; mizani ya saa; timazi. **compound ~**, penduli changamano. **simple ~**, penduli sahili.

**penetrate** /ˈpenɪtreɪt/ *v.t.* ingia; penya; enea; *(fig.)* fahamu. **penetrating** *adj.* -elekevu; -enye akili nyingi; -enye kupenya.

**penetration** /ˌpenɪˈtreɪʃn/ *n.* upenyaji; uingiliaji; welekevu; nguvu ya kupenya.

**penguin** /ˈpeŋgwɪn/ *n.* pengwini: ndege wa maji mwenye miguu mifupi asiyeweza kuruka juu.


**penguin**

**penicillin** /ˌpenɪˈsɪlɪn/ *n.* penisilini: aina ya dawa itengenezwayo kutokana na kuvu.

**peninsula** /pɪˈnɪnsjʊlə/ *n.* rasi; mkono wa nchi; sehemu ya ardhi iliyojiingiza/tokeza baharini au ziwani. **~r** *adj.* -a rasi.

**penis** /ˈpi:nɪs/ *n.* uume; dhakari; mboo.

**penny** /ˈpeni/ *n.* (**pennies**, **pence**) peni: sarafu ya Kiingereza. **penniless** *adj.* fukara.

**pension** /ˈpɛnʃ(ə)n/ *n.* pensheni; kiinua mgongo; malipo ya uzeeni. *v.t.* lipa pensheni. **~er** *n.* alipwaye pensheni.

**pensive** /ˈpensɪv/ *adj.* -liyezama katika mawazo; -enye kufikiri kwa makini.

**pentagon** /ˈpentəgən/ *n.* pembetano.

**penultimate** /penˈʌltɪmət/ *n./adj.* (silabi, neno, etc.) -a pili kutoka mwisho.

**penumbra** /pɪˈnʌmbə/ *n.* kivuli chepesi; kisuka.

**people** /ˈpi:pl/ *n.* watu; jamii; taifa; kabila; wananchi; jamaa; ndugu. *v.t.* jaza watu.

**pep** /pep/ *n. (slang)* nguvu; bidii; msisimko. *~ pill,* kidonge cha kuchangamsha mwili. *put some ~ into sb.,* hamasisha mtu.

**pepper** /ˈpepə(r)/ *n.* pilipili. *corn ~,* pilipili manga. *red ~,* pilipili hoho. *v.t.* tia pilipili. *~ sb. with stones,* rushia mtu mawe. *~ sb. with questions,* lenga mtu maswali. **~mint** *n.* peremende.

**peptide** /ˈpɛptʌɪd/ *n.* pepetidi: msombo wa asidi amino ulioundwa kwa jozi moja au zaidi na hivyo kufanya mnyororo.

**per** /pə(r)/ *prep.* kwa kila -moja. **~ annum**, kwa kila mwaka. *~ man,* kwa kila mtu mmoja. **~ cent**, kwa kila mia.

**perceive** /pəˈsi:v/ *v.t.* ona; tambua;

fahamu. **perceptible** *adj.* -a kuonekana; -a kutambulikana. **[illegible]** /pə'sepʃn/ *n.* uono utambuzi. **perceptive** *adj.* -ng'amuzi; -tambuzi.

**percentage** /pə'sentɪdʒ/ *n.* asilimia: uwiano wenye kuchukua namba 100 kuwa ndio msingi; sehemu.

**perch** /pɜ:tʃ/ *n.* kitulio cha ndege; wadhifa wa juu. *Nile ~*, (samaki) sangara. *v.t. /i.* tua; kaa juu ya; -wa juu ya.

**percolate** /'pɜ:kəleɪt/ *v.i./t.* (kwa vioevu) penya; penyeza; chuja; vuja. **percolator** /'pɜ:kəleɪtə(r)/ *n.* kichujio; chujio; kung'uto; mashine ya kutengenezea kahawa.

**percussion** /pə'kʌʃn/ *n.* mgongano; ugonganishaji. **~ist** *n.* mpiga ngoma.

**perennial** /pə'reniəl/ *adj.* -a kudumu; -a kuishi zaidi ya miaka miwili.

**perfect** /'pə:fɪkt/ *adj.* kamili; -zima; sahihi; safi; bila kasoro; -timilifu. *v.t.* kamilisha. **~ion** *n.* upeo; ukamilifu; usitawi.

**perforate** /'pə:fəreɪt/ *v.t.* toboa; pekecha. **perforation** *n.* kitobo; utoboaji. **perforator** *n.* kitoboleo

**perform** /pə'fɔ:m/ *v.t.* fanya; tenda; tekeleza; onyesha penye hadhira; (hasa) mbele ya watu; piga, cheza; imba muziki. **~er** *n.* mchezaji; mwimbaji; mutribu.

**perfume** /pə:fju:m/ *n.* manukato; uturi. *v.t.* tia manukato. **~r** *n.* muuza manukato.

**perhaps** /pə'hæps/ *adv.* labda; huenda; pengine.

**pericarp** *n.* ganda; perikapi, ukutatunda: ukuta wa nje ya tunda ambao chanzo chake ni tishu za ukuta wa ovari.

**peril** /'perəl/ *n.* hatari; kitu kisababishacho hatari. **~ous** *adj.* -enye hatari.

**perimeter** /pə'rɪmɪtə(r)/ *n.* mzingo: mpito wa nje kupakana na ubapa wa umbo.

**period** /'pɪəriəd/ *n.* kipindi; nukta; wakati; kituo kikuu; muda wa mzunguko mmoja; sentensi kamili; hedhi. **~ic, ~ical** *adj.* -a kipindi; -a muhula; -a kurudiarudia; jarida litolewalo kila baada ya kipindi fulani. **~ acid**, asidi periodiki. *~ law*, kaida mrudio **~ [illegible]** jedwali ya elementi kulingana na uzito na tabia zao. **~ically** *adv.* kila baada ya kipindi fulani.

**periscope** /'perɪskəʊp/ *n.* periskopu: darubini ya kuonea juu ya upeo wa macho, hutumika sana katika nyambizi.



periscope

**perish** /'perɪʃ/ *v.i.* -fa; potea; haribika; hiliki; chakaa; angamia; fifia; toweka; isha. *~ed with cold*, - naosumbuliwa na baridi. **~able** *adj.* -a kuharibika upesi; si -enye kudumu.

**peristalsis** /ˌpɛrɪ'stɑlsɪs/ *n.* mnyezo: usagaji chakula katika utumbo kwa namna yake maalumu; kusogea au kujongea kwa chakula tumboni kwa mwendo kama wa mawimbi.

**permanent** /'pɜ:mənənt/ *adj.* -a kudumu. *the ~ way*, njia ya reli. **~ wave**, mtindo wa nywele wa kutia mawimbi ya kudumu. **~ly** *adv.* bila kubadilika. **permanence** *n.* kudumu.

**permeable** /'pɜ:miəbl/ *adj.* -enye kupitisha maji.

**permeate** /'pɜ:mieɪt/ *v.t./i.* sambaa; penya; enea na kujaza sehemu zote.

**permit** /pə'mɪt/ *n.* kibali; ruhusa; idhini. *v.t./i.* (**-tt-**) ruhusu. **permissible** *adj.* halali; -enye kukubalika; -enye kuruhusika.

**permission** /pə'mɪʃn/ *n.* ruhusa; idhini.

**peroxide** /pə'rɒksaɪd/ *n.* peroksidi: oksidi inayounda peroksidi ya hidrojeni inapotendana na asidi.

**perpendicular** /ˌpə:p(ə)n'dɪkjʊlə/ *n.* mstari sulubi; mstari wima; hali ya kuwa sulubi au wima. *adj.* -a wima; -a mstatili; -a sulubi. **~ity** *n.* usulubi.

**perpetrate** /'pɜ:pətreɪt/ *v.t.* fanya kosa. **perpetrator** *n.* mkosaji.

**perpetration** /ˌpɜ:pə'treɪʃn/ *n.* ukosefu; ukosaji.

**perpetual** /pə'pɛtʃʊəl, -tjʊəl/ *adj.*

siokoma; -a kuendelea muda mrefu; a kurudiarudia; -a kudumu.
**perpetuate** /pə'pɛtʃʊeɪt, -tjʊ-/ *v.t.* dumisha; endeleza. **perpetuity** *n.* milele; dawamu; aushi. *in perpetuity,* milele.
**perplex** /pə'pleks/ *v.t.* tatiza; fadhaisha; kanganya; tatanisha; emeza. **~ed** *adj.* -enye kufadhaika; -enye kukanganyika. **~edly** *adv.* kwa fadhaa; kwa uemevu. **~ity** *n.* fadhaa; uemevu; mkanganyiko; kitu kisababishacho fadhaa.
**perquisite** /pə:kwɪzɪt/ *n.* marupurupu; bahshishi.
**persecute** /'pɜ:sɪkju:t/ *v.t.* tesa; sumbua; adhibu. **persecutor** *n.* mtesaji. **persecution** *n.* usumbufu; mateso.
**persevere** *v.i.* vumilia; stahamili. **perseverance** *n.* uvumilivu.
**persist** /pə'sɪst/ *v.i.* shikilia; kataa kubadili msimamo; chagiza; endelea kuwapo. *He ~ed in turning them away,* alishikilia kuwafukuza. **~ence** *n.* ushikiliaji; jitihada; chagizo. **~ent** *adj.* -enye kushikilia; thabiti; -enye kuendelea bila mabadiliko.
**person** /pɜ:sn/ *n.* mtu; mwenyewe; mwili; maisha; kiwiliwili; nafsi. *He was present in ~,* alihudhuria mwenyewe. **~able** *adj.* maridhia; -enye sura nzuri. **~age** *n.* mtu mashuhuri; mhusika. **~al** *adj.* -enyewe; -a mtu binafsi; -a mwili. *He paid him a ~ visit,* alikwenda mwenyewe kumzuru. *He made ~ remarks about me,* alinikashifu. **~ally** *adv.* kibinafsi. **~ality** *n.* nafsi; dhati; wasifu; haiba; hulka; tabia; mtu mashuhuri. *a strong ~,* haiba. *a man with little ~,* mtu mwenye haiba ndogo.
**personify** /pɜ:sn/ *v.t.* -pa nafsi; -wa mfano wa.
**personification** *n.* tashihisi.
**personel** *n.* watumishi; utumishi.
**perspective** /pə'spektɪv/ *n.* taswira; uhusiano; mtazamo; wazo; matumaini; uono.
**perspire** /pə'spaɪə(r)/ *v.i.* toka jasho. **perspiration** *n.* jasho; utokaji jasho.
**persuade** /pə'sweɪd/ *v.t.* shawishi; fanya mtu aamini. **persuasion** *n.* ushawishi; imani; madhehebu; itikadi. **persuasive** *adj.* -enye kushawishi; -a kuaminisha; -a kutoa wasiwasi.
**pertain** /pə'teɪn/ *v.i.* husu; fungamana na. *~ to,* -wa mali au sehemu ya; husiana na.
**pertinent** /'pɜ:tɪnənt/ *adj.* -a kuhusu; -a kufungamana na; -a kufaa; -a kupasa.
**pervade** /pə'veɪd/ *v.t.* sambaa; zagaa; enea kote.
**pervert** /pə'vɜ:t/ *n.* murtadi; mpotofu. *v.t.* potosha; ongoza vibaya. **perversion** *n.* upotofu; kuritadi.
**pervious** /'pə:vɪəs/ *adj.* -enye kupenyeka; -enye kupitika; -enye kufikika; -enye kuruhusu kitu kupenya.
**pessimism** /'pesɪmɪzəm/ *n.* ukosefu wa rajua; imani kuwa mambo yote ni mabaya; hali ya kukata tamaa. **pessimist** *n.* mtu aaminiye hivyo. **pessimistic** *adj.* bila rajua.
**pest** /pest/ *n.* mnyama au mdudu mharibifu. **~er** *v.t.* sumbua; udhi; chokoza; chagiza. **~icide** *n.* uadudu: dawa ya kuulia wadudu. **~ilence** *n.* maradhi ya kuambukiza; tauni. **~ilent** *adj.* -a kuleta madhara au maradhi; *(colloq.)* -a kusumbua. **~ology** *n.* pestolojia: sayansi ya wadudu na mbinu za kupambana nao.
**pestle** /'pɛs(ə)l/ *n.* mchi wa kutwangia.
**pet** /pet/ *n.* kipenzi; mnyama kipenzi. *v.t.* (**-tt-**) busu; tomasatomasa; papasapapasa; bembeleza.
**petal** /'petl/ *n.* petali.
**petition** /pə'tɪʃn/ *n.* ombi; rufaa; dua. *v.t.* omba; omba dua; kata rufaa; sihi; lalamika. **~er** *n.* mlalamikaji.
**petrification** *n.* ugeukajikisukuku: badiliko la kitu cha kaboni kuwa na umbile la kijiwe au kimadini.
**petrochemicals** *n.* petrokemikali: vitu vya kikemikali vinavyotokana na mafuta ya kipetroli au gesi asili.
**petrol** /'pətrəl/ *n.* petroli. **~eum** *n.*

petroliamu; mafuta ya kipetroli: mchanganyiko wa asili wa hidrokaboni ghafi wenye rangi nyeusi au kijani ambao huwa na misombo mingine pia ya kikaboni.

**petticoat** /'petɪkəʊt/ *n.* gwaguro; shimizi.

**petty** /'pəti/ *adj.* -dogo; -siokuwa muhimu; uchwara; -finyu. ~ *cash,* fedha kichele. ~ *officer,* ofisa mdogo katika manowari.

**petulant** /'pɛtjʊl(ə)nt/ *adj.* -sio vumilivu; -epesi kukasirika; -a kasikasi. **~ly** *adv.* kichukichuki.

**petulance** /pə'tjuləns/ *n.* chuki; kinyongo.

**pew** /pju:/ *n.* benchi la kanisani.

**pewter** /'pju:tə(r)/ *n.* pyuta: aloi ya bati na risasi.

**pH** /ˌpi: 'eɪtʃ/ *n.* kipimo cha uasidi au ualkali katika mmumunyo. **~ meter**, kipima pH. **~ scale**, kipimo pH. **~ value**, thamani ya pH.

**phagocyte** /'fɑgə(ʊ)sʌɪt/ *n.* fagosaiti: seli kama amiba au protozoa ambayo huzingira chembechembe au vidubini vinavyoshambulia tishu.

**phantom** /'fæntəm/ *n.* mzuka; mfano wa mwili wa mtu utumiwao na madaktari wanafunzi kujifunza upasuaji.

**pharaoh** /'fɛ:rəʊ/ *n.* firauni; farao.

**pharmacy** /'fɑ:məsi/ *n.* famasia: utayarishaji na utoaji dawa; duka la dawa. **pharmaceutic** *adj.* -a madawa. **pharmacist** *n.* mfamasia. **pharmacology** *n.* sayansi ya matumizi, athari na ufanyaji kazi wa dawa mwilini.

**phase** /feɪz/ *n.* mkupuo; awamu; sura. *~s of the moon,* awamu za mwezi: maumbo anuwai ya uso wa mwezi yanavyoonekana kutoka kwenye dunia.

**phenomenon** /fə'nɒmɪnən/ *n.* (**phenomena**) kitu; jambo; tukio; ajabu. **phenomenal** *adj.* -a ajabu sana; si - a kawaida.

**philanthropy** /fɪ'lænθrəpi/ *n.* huruma; hisani; fadhila; mapenzi kwa binadamu. **philanthropist** *n.* mtu mwenye kusaidia wingine. **philanthropic** *adj.* -a hisani; -enye hisani.

**philology** /fɪ'lɒlədʒi/ *n.* filolojia: taaluma ya ukuaji wa lugha. **philologist** *n.* mwanafilolojia. **philological** *adj.* -a elimu ya lugha.

**philosophy** /fə'lɒsəfi/ *n.* falsafa; siasa; busara. **philosopher** *n.* mwanafalsafa; mtu makini; mtulivu. **philosophical** *adj.* -a falsafa; -enye kufuata taratibu za kifalsafa.

**phlegm** /flɛm/ *n.* kohozi; utulivu; usiri; upole. **~atic** *adj.* -tulivu; -siri.

**phloem** /'fləʊɛm/ *n.* floemu: tishu katika mimea inayohusika na usafirishaji wa chakula kutoka kwenye majani kupitia kwenye shina hadi mizizini.

**phobia** /'fəʊbɪə/ *n.* hofu; woga mwingi usio kifani juu ya kitu fulani.

**phone** /fəʊn/ *n.* *(linguistics)* foni. *(colloq.)* simu. *v.t./i.* piga simu. **~tic** *adj.* -a fonetiki; -a jinsi ya kutamka. **~tics** /fə'netɪks/ *n.* fonetiki: elimu ya sauti za usemi.

**phosphate** /'fɒsfeɪt/ *n.* fosfati: chumvi ya asidi fosforiki; mbolea.

**phosphorus** /'fɒsf(ə)rəs/ *n.* fosforasi: elementi ya njano simetali ambayo huwaka haraka.

**phosphorescent** /ˌfɒsfə'resnt/ *adj.* -a kung'aa gizani. **phosphorescence** *n.* mmemetuko.

**photocell** /'fəʊtesel/ *n.* selimwanga: zana inayotumika kutambulia na kupimia mwanga kwa kutumia tabia yake ya kubadilika kiumeme inapoathiriwa na mwanga.

**photochemical reaction** *n.* utendanaji kikemikali mwanga: utendanaji kikemikali unaoanzishwa, kusaidiwa au kuchapushwa kwa kuangazwa kwenye mwanga.

**photochemical smog** *n.* ukungu kemikali: aina ya uchafuzi wa mazingira hewa unaosababishwa na moshi wa magari.

**photoelectric** /ˌfəʊtəʊɪ'lektrɪk/ *n.* -enye kupata umeme kutokana na mwanga; -a umememwanga. **~ cell**, seli umememuru: zana inayotumika kutambulia na

kupimia mwanga kwa kutumia tabia yake ya kubadilika kiumeme inapoathiriwa na mwanga.

**photograph** /ˈfəʊtəgra:f/ *n.* picha. *v.t.* piga picha; fotoa. **~er** *n.* mpiga picha. **~y** *n.* upigaji picha; sanaa ya upigaji picha. **~ic** *adj.* -a picha; -a kupiga picha

**photon** /ˈfəʊtɒn/ *n.* fotoni: chemchemi ya wimbi la sumaku umeme linalobeba nishati

**photosensitive** /ˌfəʊtəʊˈsensətɪv/ *adj.* -a nyetimwanga; -enye kuathiriwa na mwanga kwa urahisi

**photosphere** *n.* angamwanga: sehemu ya juu inayoonekana ambayo ina mng'aro mkali sana na ambayo ina halijoto kubwa mno.

**photosynthesis** /ˌfəʊtəˈsɪnθəsɪs/ *n* usanidimwanga: ujenzi wa chakula katika seli za mimea kwa kutumia nishati ya mwanga na nyenzo nyingine.

**phototropism** *n.* uelekeomwanga: hali ya kukua sehemu ya mmea kuelekea kwenye upande wa nuru.

**phrase** /freɪz/ *n.* kirai: fungu la maneno lililo sehemu ya sentensi msemo; kifungu cha muziki. **~ology** *n.* jinsi ya kutumia maneno; uteuzi wa maneno.

**phylum** /ˈfʌɪləm/ *n.* faila:mgawanyo wa ngeli za viumbe wenye sifa -ma ehusiana

**physical** /ˈfɪzɪkl/ *adj.* a kuonekana; a mwili; a viumbe; -a maumbile. **~ change** badiliko la kiumbo: badiliko katika kitu ambalo ni la umbo tu na sio la kikemikali. **~ geography** jiografia ya umbo la dunia. ~ *strength* nguvu za mwili. ~ *impossibility to be in two places at once* haiwezekani kuwepo mahali pawili wakati mmoja.

**physician** /fɪˈzɪʃn/ *n.* daktari mganga; tabibu

**physicist** /ˈfɪzɪsɪst/ *n.* mwana fizikia

**physics** /ˈfɪzɪks/ *n.* fizikia.

**physique** /fɪˈzi:k/ *n.* umbo; umbile; maungo gimba

**piano** /pɪˈanəʊ/ *n.* piano. **pianist** *n.* mpiga piano.


piano

**pick** /ˈpɪk/ **~-axe** *n.* sururu; chombo kidogo kama kijiti cha kiberiti. *a tooth ~.* kichokolea meno; uteuzi; uchaguzi; chaguo. *v.t.* chuma; donoa; chagua; teua; iba; chambua; onja; piga; chokoa. ~ *up,* okota; inua; chagua. *The train ~s up passengers,* treni inachukua abiria. *He has been sick but is ~ing up,* yu mgonjwa lakini anapata nafuu. ~ *sb. up,* fahamiana na. ~ *oneself up,* inuka. ~ *sb.'s pocket,* chomoa mtu. ~ *sb.'s brains,* chota akili; chota mawazo. ~ *a lock,* fungua si kwa ufunguo. ~ *a quarrel with sb.,* chokoza; anzisha ugomvi. ~ *hole in sth.,* tafuta kasoro. **~-me-up** *n.* kitu cha kutia nguvu; kiburudisho. **~pocket** *n.* mcho-moaji.


pickaxe

**pickle** /ˈpɪkl/ *n.* achari; hali. *in a sad ~,* katika hali mbaya. *v.t.* tengeneza achari.

**picnic** /ˈpɪknɪk/ *n.* mandari; pikniki. *v.i.* enda mandarini; enda pikniki.

**pictorial** /pɪkˈtɔ:riəl/ *adj.* -a picha.

**picture** /ˈpɪktʃə(r)/ *n.* picha; sura; mchoro; taswira; uono; mfano; mithali; maelezo; sinema; filamu. *be the picture of health,* -wa mfano wa afya bora. *the ~ s, (colloq.)* sinema. *v.t.* eleza kwa maneno; waza moyoni. **~sque** *adj.* -enye sura nzuri; -a kusisimua; si -a kawaida.

**pie** /paɪ/ *n.* pai; sambusa; andazi. *have a finger in the ~,* ingilia kati; husika.

**piece** /pi:s/ *n.* kipande; sehemu; tukio; kipimo maalumu; kitu kimoja katika seti; sarafu. *in ~s,* vipande vipande. *take to ~s,* vunja; kongoa. *a ~ of luck,* bahati. *a ~ of news,* habari. *a ~ of cloth,* kitambaa. *cloth sold only by the ~,* kitambaa kiuzwacho kwa jora tu. *a ten-shilling ~,* sarafu ya shilingi kumi. *v.t.* unganisha; kamilisha. ~

*out,* maliza kwa kuunganisha sehemu zake. **~meal** *adv.* kidogo kidogo; hatua kwa hatua. **~work** *n.* pande; ujira ulipwao kwa mujibu wa kazi iliyofanywa.

**pierce** /pɪəs/ *v.t./i.* penya; choma; toboa; toga; dunga; umiza.

**pig** /pɪg/ *n.* nguruwe; *(colloq.)* mchafu. **pigheaded** *adj.* -kaidi; kichwa ngumu; kichwa maji. **pigsty** *n.* zizi la nguruwe.

**pigtail** /'pɪgteɪl/ *n.* nywele zilizofungwa nyuma na kuning'inia mabegani.

**pigeon** /'pɪdʒn/ *n.* njiwa. **~-hole** *n.* kishubaka; tundu la njiwa. *v.t.* ahirisha kitu.

**pigment** /'pɪgmənt/ *n.* pigmenti: rangi ya asili.

**pigmy**, **pygmy** *n.* mbilikimo; mtu mfupi sana.

**pile** /paɪl/ *n.* nguzo; mhimili; fungu; chungu; rundo; biwi; jumba kubwa. **~driver** *n.* mashine ya kushindilia nguzo. *(colloq.) make a ~,* jitajirisha. *v.t.* rundika; tutika; jaza.

**pilgrim** /'pɪlgrɪm/ *n.* haji; hujaji. **~age** *n.* hija.

**pill** /pɪl/ *n.* kidonge; tembe. *the ~,* kidonge cha kuzuia mimba; kidonge cha majira. *go on the ~,* anza kutumia vidonge vya majira.

**pillage** /'pɪlɪdʒ/ *n.* utekaji nyara; uporaji; nyara. *v.t.* teka nyara; pora.

**pillar** /'pɪlə(r)/ *n.* nguzo; mhimili; mwimo. **~box** *n.* sanduku la barua barabarani.

**pillion** /'pɪliən/ *n.* kiti au kibao cha nyuma cha mtu baiskeli, skuta au pikipiki.

**pillow** /'pɪləʊ/ *n.* mto; takia; mhimili. **~case ~slip** *n.* foronya. *take counsel of one's ~.* ahirisha uamuzi mpaka siku inayofuata.

**pilot** /'paɪlət/ *n./adj.* rubani; -a majaribio. *v.t.* ongoza; endesha chombo cha angani au cha baharini.

**pin** /pɪn/ *n.* pini; kipingwa; kiwi. *I don't care ~,* sijali kabisa. *My leg has got ~s and needles,* mguu wangu umekufa ganzi. *v.t.* (**-nn-**) funga kwa pini; bandika kwa pini; bana. **~-cushion** *n.* kichomekea pini. **~-money** *n.* fedha apewayo mke kwa haja zake ndogondogo. **~prick** *n.* *(fig.)* jambo dogo lenye kuchukiza.

**pincers** /'pɪnsə(r)/ *n.* koleo. *~movement,* shambulia mbele na nyuma kwa wakati mmoja

**pinch** /pɪntʃ/ *n.* mfinyo; shida; mashaka; udokozi; kiasi kidogo. *v.t./i.* finya; bana; umia; hisi athari ya; iba; dokoa; bana matumizi; -wa bahili; kamata. *be ~ ed for money,* kosa fedha. *a ~ of salt,* chumvi kidogo. *at a ~,* katika mashaka; katika shida. *if it comes to the ~,* ikiwa hapana budi.



**pincers**

**pine** /paɪn/ *n.* msonobari.

**pineapple** /'paɪnæpl/ *n.* mnanasi; nanasi.

**pinhole camera** *n.* kamera tobwe: namna ya kamera sahili

**pink** /pɪŋk/ *n.* rangi ya waridi.

**pinnacle** /'pɪnəkl/ *n.* mnara mrefu juu ya paa la nyumba; *(fig.)* kilele




**pinhole camera | kamera tobwe**

cha mlima; upeo; kipeo. *at the ~ of his prosperity,* katika upeo wa usitawi wake.

**pint** /paɪnt/ *n.* painti. *a ~ of milk,* painti ya maziwa.

**pioneer** /ˌpaɪə'nɪə(r)/ *n.* mtangulizi; mwasisi; mpelelezi; payonia. *young ~,* payonia; chipukizi. *v.i./t.* tangulia; ongoza; asisi; peleleza.

**pious** /'paɪəs/ *adj.* -cha Mungu; (la zamani) -enye kutii wazazi.

**pip** /pɪp/ *n.* mbegu ya tunda.

**pipe** /paɪp/ *n.* paipu; bomba; zumari; filimbi; kiko; koromeo. *v.t./i.* pitisha kioevu katika bomba; piga zumari; piga king'ora; pamba nguo kwa kichuruzio. **~r** *n.* mpiga zumari.

**piping** *n.* kipande cha bomba; kichuruzio; sauti ya zumari. *adj.* -enye sauti ya filimbi; enye sauti nyembamba. *adv. piping hot,* joto sana.

**pirate** /'paɪrət/ *n.* haramia; mwizi wa haki miliki. *v.t.* iba kazi ya mwingine. **piracy** *n.* uharamia; wizi.

**Pisces** /pʌɪsi:z/ *n.* **1.** samaki: oda inayojumuisha samaki wote; **2.** Samaki: nyota ya unajimu ya thenashara.

**pistil** /'pɪstɪl/ *n.* pistili: sehemu ya ua inayotoa mbegu.

**pistol** /'pɪstl/ *n.* bastola.

**piston** /'pɪst(ə)n/ *n.* pistoni. **~ engined**, -a injini enye pistoni. **~ ring**, ringi ya pistoni. **~ rod**, mkono wa pistoni.

**pit** /pɪt/ *n.* shimo; mgodi; machimbo; mtego wa shimo; mvungu; gulio la biashara maalumu; uwanja wa kati wa thieta. *v.t.* (**-tt-**) fanya kovu. *a face ~ted with smallpox,* uso uliojaa kovu za ndui. *~ against,* shindanisha mtu au mnyama. **~fall** *n.* rima: mtego wa shimo; hatari iliyofichika.

**pitch** /'pɪtʃ/ *n.* lami. *~ dark,* giza totoro. *~ black,* -eusi tititi; mrama; msukosuko; mvurumisho; uwanja wa kuchezea; mahali pa kuuzia vitu; mwanguko; mshuko; mteremko; mwinamo; kiwango; uzito wa sauti; nafasi baina ya meno ya gurudumu. *v.t./i.* piga hema; tupa; vurumisha; anguka; enda mrama; rekebisha sauti; sukasuka; tia mwinamo katika paa. *~ in,* anza kwa bidii. *~ into,* shughulika kwa bidii; piga; *~ upon sb.,* chagua fulani kwa bahati. *~ed battle,* mapigano yaliyoandaliwa kabla. **~ fork** *n.* uma wa nyasi.

**pith** /pɪθ/ *n.* moyomti; upande wa ndani wa ganda la chungwa; nguvu; juhudi; wepesi; *(fig.)* kiini; maana. **~y** *adj.* -enye maana sana; -a nguvu. **~ ily** *adv.* kwa nguvu; kwa bidii.

**pittance** /'pɪtns/ *n.* ujira mdogo kuliko unaostahili.

**pituitary gland** *n.* tezi pituitari: tezi homoni iliyopo katikati ya sehemu ya chini ya ubongo inayosaidia ukuaji na udhibiti wa tezi nyengine.

**pity** /'pɪti/ *n.* huruma; jambo la kusikitisha. *What a ~,* inasikitisha. *v.t.* hurumia; sikitikia. **pitiable** *adj.* -a kutia huruma; -a kusikitisha; -a kuhuzunisha. **pitifully** *adv.* kwa huruma; kwa masikitiko. **pitiless** *adj.* -katili; sio na huruma. **pitilessly** *adv.* kikatili; bila huruma.

**pivot** /'pɪvət/ *n.* egemeo; *(fig.)* asili; chimbuko; kiini; msingi; mtu aendeshaye kikosi cha askari. *v.t./i.* egemea; geuka katika egemeo.

**placard** /'plakɑ:d/ *n.* bango. *v.t.* bandika bango ukutani; tangaza habari kwa bango.

**place** /pleɪs/ *n.* mahali; mji; jiji; kijiji; jengo; sehemu katika maandishi; nafasi; nyumba; mtaa. *~ of worship,* mahali pa ibada. *~s of amusement,* mahali mwa burudani. *out of ~,* pasipofaa. *take ~,* tokea. *give ~ to,* pisha nafasi. *in ~ of,* badala ya. *lose one's ~,* achishwa kazi au kusoma. *keep sb. in his ~,* weka mtu badala yake. *v.t.* weka; panga; teua; agiza bidhaa.

**placenta** /plə'sɛntə/ *n.* plasenta: tishu maalumu katika uterasi ambako kiungamwana kutoka tumboni mwa mtoto mchanga kimeunganika na tishu za mama mjamzito katika ukuta wa uterasi.

**plague** /pleɪg/ *n.* tauni; mateso; balaa; kitu kinachosumbua. *v.t.* sumbua; udhi; kera; taabisha.

**plain** /pleɪn/ *n.* uwanda; tambarare. *-adj.* dhahiri; wazi; -a kawaida; -sio na marembo; -sio na mapambo; -nyofu; -a kweli; si zuri. *~ food,* chakula bila kitoweo. *in ~ clothes, katika* vazi la kiraia. *in ~ words, to be ~ with you,* kwa kusema kweli. **~ly** *adv.* kwa uwazi. **~ness** *n.* uwazi; udhahiri; udufu.

**plaintiff** /'pleɪntɪf/ *n.* mdai.

**plait** /plat/ *n.* unywele uliosukwa; msokoto. *v.t.* suka; sokota.

**plan** /plæn/ *n.* ramani; picha;

mchoro; kielelezo; mpango. *v.t.* (**-nn-**) nuia; panga kabla; chora ramani.



**plaits**

**plane** /pleɪn/ *n.* bapa: uso mfuto; ubapa; hatua; kiwango; landa; ndege. *v.t./i.* piga landa. *adj.* -enye uso mfuto.

**planet** /'plænɪt/ *n.* sayari. **~arium** *n.* jengo linaloigiza nyendo za sayari. **~oid** *n.* sayari ndogo.

**plank** /plæŋk/ *n.* ubao; hoja ya msingi katika sera. ~ *bed*, kitanda cha falka tupu bila godoro.

**plankton** /'plaŋ(k)t(ə)n/ *n.* plankitoni: jamii ya viumbe vidogo sana ya wanyama na mimea viishivyo katika maji, huonekana kwa hadubini tu.

**plant** /plɑ:nt/ *n.* mmea; mche; mtambo; vifaa; mashine; kiwanda; karakana; hila; mtego; askari kanzu aliyejiunga na majambazi ili awakamate. *v.t.* panda; atika; pandikiza; otesha; ingiza wazo akilini; weka; kaza; simamisha; piga; anzisha; asisi; lowea. **~ation** *n.* shamba kubwa; mgunda.




**plant cell | seli ya mti**

**plantain** /'plæntɪn/ *n.* ndizi; mgomba.

**plasma** /'plazmə/ *n.* plazma: sehemu ya majimaji katika damu; limfu bila seli.

**plasmodium** /plaz'məʊdɪəm/ *n.* plasmodia: jamii ya protozoa waishio katika ini na damu ya binadamu na ambao husababisha malaria.

**plaster** /'plɑ:stə(r)/ *n.* plasta; ripu; mchanganyiko wa chokaa au saruji, mchanga na maji. *v.t.* piga plasta; piga ripu; bandika plasta; tia ingi. *His hair is ~ed with oil*, nywele zake zinachuruzika mafuta. **~er** *n.* mwashi.

**plastic** /'plæstɪk/ *n.* plastiki. *adj.* -a plastiki; -a kinamo; -a kutengeneza; -a kunyumbuka. *The bag was made of ~ material, not of real leather*, mkoba ule ulikuwa wa plastiki, si wa ngozi halisi. **~s** *n.* taaluma ya kutengeneza vitu vya plastiki. **~ity** *n.* unyumbukaji.

**plate** /pleɪt/ *n.* sahani; bamba; pleti; picha ya kitabuni; vyombo vya dhahabu au fedha. **dental ~**, menobandia. *v.t.* chovya vitu vya madini katika madini ya namna nyengine.

**plateau** /'plɑtəʊ/ *n.* uwanda wa juu; nchi tambarare iliyoinuka.

**platelet** /'pleɪtlət/ *n.* chembelele; kigandishadamu: aina ya kigimba kidogo cha utehai chenye umbo la kisahani katika damu, hutoa kemikali yenye uwezo wa kugandisha damu.

**plate tectonics** *n.* nadharia ya visahani: nadharia inayodai kwamba ardhi imeundwa kwa vipande vya mango viitwavyo visahani na ambavyo daima vimo katika mwendo.



**platelets**

**platform** /'plætfɔ:m/ *n.* jukwaa; ulingo; ilani ya uchaguzi ya chama cha siasa.

**platinum** /'plɑtɪnəm/ *n.* platinamu: madini nzito nyeupe ya thamani.

**plausible** /'plɔ:zəbl/ *adj.* -enye kukubalika; -enye kuelekea; -enye kutoa hoja za kukubalika. **plausibility** *n.* ukubalikaji; uelekeaji.

**play** /pleɪ/ *n.* mchezo; uchezaji; zamu katika mchezo; tamthilia; kamari; nafasi ya kufanya jambo; kazi; shughuli. *in ~*, kwa mzaha. *~ on words*, cheza na maneno. *the ~ing of sunlight*, kurukaruka kwa mionzi ya jua. *give your fancy full ~*, fikiri kama upendavyo. *a joint with too much ~*, kiungo chenye nafasi ya kutembea. *come into ~*

anza kufanya kazi. *bring into* anza kutumika au kutumia. *v.t./i.* cheza; fanya mzaha; hadaa; tania; piga chombo cha muziki; fuata kanuni; igiza tamthilia; onyesha maigizo. ~ *a trick on sb.,* fanyia mzaha. ~ *at sth.,* fanya mzaha. ~ *with,* chezea. ~ *up,* ongeza bidii. ~ *up to sb.,* jipendekezea. ~ *upon sb.'s fears,* tumilia woga wa mtu. ~ *into sb.'s hands,* jiuza kwa mtu. *be ~ed out,* choka kabisa. **~er** *n.* mchezaji; mpigaji kinanda; mshindanaji. **~fellow**, **~mate** *n.* mwenza katika mchezo. **~ful** *adj.* -cheshi; -enye mzaha. **~fully** *adv.* kwa mzaha. **~thing** *n.* kitu cha kuchezea.

**plead** /pli:d/ *v.t./i.* tetea; toa hoja; tetea hoja; kiri; omba; sihi. ~ *guilty,* kiri kosa. ~ *not guilty,* kana kosa.

**pleasant** /'pleznt/ *adj.* -a kupendeza; -zuri; tamu. **~ly** *adv.* kwa furaha. **~ness** *n.* furaha. **~ry** *n.* ubishi; ucheshi; mzaha.

**please** /pli:z/ *v.t./ i.* pendeza; ridhisha; furahisha. ~ *oneself,* fanya -pendavyo. *if you ~,* tafadhali.

**pleasing** /'pli:zɪŋ/ *adj.* -a kupendeza; zuri; -tamu.

**pleasure** /'pleʒə(r)/ *n.* furaha; raha. *take ~ in,* furahia. *with ~,* kwa furaha. *at his ~,* atakapotaka. **pleasurable** /'pleʒərəbl/ *adj.* -a kupendeza; -enye kufurahisha.

**pledge** /pledʒ/ *n.* rehani; zawadi ya kuonyesha upendo; ahadi; kiapo; dhamana; mdhamini. *v.t.* weka rehani; apa; ahidi; -nywa kwa afya ya.

**plenty** /'plenti/ *n.* wingi. **plentiful** *adj.* -ingi; maridhawa; tele. **plenteous** *adj.* -a wingi; maridhawa.

**pleurisy** /'plʊərɪsi/ *n.* ugonjwa wa ngozi ya nje ya mapafu.

**pliable** /'plaɪəbl/ *adj.* -a kupindika kirahisi; -enye kushawishika kirahisi. **pliability** *n.* sifa ya kupindika au kushawishika kirahisi.

**pliers** /'plaɪəz/ *n.* koleo.

**plight** /plaɪt/ *n.* hali mbaya; taabu.

**plod** /plɒd/ *n.* kazi ngumu. *v.i.* (**-dd-**) jikokota. **~der** *n.* mtu ajikokotaye lakini mwenye bidii.

**plot** /plɒt/ *n.* kiwanja; muundo wa riwaya; njama; shamba. *v.t.* (**-tt-**) panga; kula njama; weka alama; panga matukio katika riwaya.

**plough** /plaʊ/ *n.* plau; kundi la nyota saba zifanyazo umbo la plau. *v.t.* lima kwa plau; penya kwa nguvu. *The ship ~ed through the heavy waves,* meli ilikata mawimbi makubwa. **~share** *n.* chuma cha plau.

**plow** *n.* plau.

**pluck** /plʌk/ *n.* ushujaa; ujasiri; unyakuaji. *v.t./i.* nyonyoa manyoya; chuma matunda au maua. ~ *up weeds,* ng'oa magugu. ~ *up courage,* jipa moyo; piga moyo konde. **~ily** *adv.* kwa ushupavu; kwa kunyakua.

**plug** /plʌg/ *n.* plagi; kizibo; msokoto wa tumbaku; tangazo la biashara la mara kwa mara. *v.t./i.* (**-gg-**). ziba; funga. *(colloq.)* ~ *away at,* shughulikia kwa juhudi. ~ *in,* chomeka plagi.

**plum** /plʌm/ *n.* plamu: tunda kama zambarau; kitu bora. ~ *tree,*mplamu.

**plumage** /'plu:mɪdʒ/ *n.* manyoya ya ndege. **plume** *n.* nyoya. *plume oneself on sth.,* jipongeza kwa.

**plumb** /plʌm/ *n.* timazi; chubwi. *out of ~,* tenge; si wima. *adv.* hasa; sawasawa. *v.t. (fig.)* fikia kiini cha jambo.

**plumber** /'plʌmə(r)/ *n.* fundi bomba. **plumbing** *n.* ufundi bomba; mabomba; matangi; etc.

**plump** /'plʌmp/ *adj.* -nene; -nono; -a mviringo.

**plunge** /'plʌndʒ/ *n.* mbizi. *v.t./i.* tumbukiza; tumbukia; enda mrama; piga mbizi. *(fig.)* ~ *a room into darkness,* tia giza ghafla chumbani kwa kuzima taa.

**plural** /'plʊərəl/ *n.* wingi. *adj.* wingi; -ingi. **~ism** *n.* mfumo unaokubali watu wa mitazamo tofauti ya kisiasa, kitamaduni na kidini kuishi pamoja.

**plus** /plʌs/ *prep.* na; pamoja na; zaidi

ya. *the ~ sign,* alama ya kujumlisha hii ( + ). *adj.* chanya; -a kujumlisha.

**Pluto** /'plu:təʊ/ *n.* Utaridi: sayari ya tisa katika mfumo wa jua.

**plutonium** /'plu:'təʊniəm/ *n.* platoniamu: elementi ya kikemikali yenye harakatiredio inayotumika katika vinu vya nyuklia.

**ply** /plaɪ/ *n.* tabaka; uzi. *three ~ wood,* ubao uliofanywa kwa tabaka tatu za mbao. *three ~ wool for knitting,* uzi wa sufi uliofanywa kwa kusokota nyuzi tatu.

**pneumatic** /nju:'mætɪk/ *adj.* -a hewa; -enye kuendeshwa kwa nguvu ya hewa. *~ tyres,* tairi hewa.

**pneumonia** /nju:'məʊnɪə/ *n.* nimonia: homa ya mapafu.

**poach**[1] /'pəʊtʃ/ *v.t. ~an egg,* tokosa ute na kiini cha yai katika maji yanayochemka.

**poach**[2] /'pəʊtʃ/ *n.* ujangili. *v.t./i.* **1.** winda wanyama bila ruhusa. **2.** tokosa yai. *~ed egg,* yai la kutokosa.

**pocket** /'pɒkɪt/ *n.* mfuko; kishimo. *be in ~,* pata faida. *be out of ~,* pata hasara. *v.t.* tia mfukoni; ficha; iba. **~book** *n.* kitabu kidogo cha kuandikia. **~ money** *n.* pesa za matumizi madogomadogo.

**pod** /pɒd/ *n.* kega; ganda.

**poem** /pəʊɪm/ *n.* shairi. **poet** *n.* mshairi. **poetic (al)** *adj.*-a mashairi; -a kishairi. **poetry** *n.* ushairi.

**poikilotherm** /'pɔɪkɪlə(ʊ),θə:m/ *n.* mnyama ambaye halijoto ya damu yake huirekebisha kulingana na mazingira yake.

**point** /pɔɪnt/ *n.* ncha; nukta; alama; kizio cha kupimia ukubwa wa herufi; pointi; wazo; hoja; kusudio; sababu; sifa; sakiti ya umeme; umuhimu. *(fig.) ~ of view,* mtazamo. *from their ~ of view,* kwa mtazamo wao. *at this ~,* wakati huu; sasa; mahali hapa. *on the ~ of,* karibu na. *when it comes to the ~,* wakati ukiwadia. *~s of the compass,* pembe za dira. *He undestood my ~,* alilifahamu wazo langu. *Come to the ~,* sema ulichokusudia. *carry one's ~,* shinda. *be off the ~,* toka nje ya mada. *be to the ~,* sema kile tu ulichokusudia. *the first ~ of my argument,* hoja yangu ya kwanza. *What are his best ~s as a clerk?* sifa zake nzuri ni zipi kama karani? *Her score was twenty ~s,* alipata alama ishirini. *The boxer won on ~s,* bondia alishinda kwa pointi. *v.t./i.* elekeza; onyesha kwa kidole; ainisha. *Everthing ~s to his guilt,* kila kitu kinamtia hatiani. **~-blank** *adv.* papo kwa papo; karibu mno; kinagaubaga; waziwazi. **~ed** *adj.* -kali; -enye ncha kali; -a wazi. **~er** *n.* fimbo ya kuelekezea; mkono; mshale; akarabu ya saa. **~less** *adj. (fig.)* -sio maana.

**poise** /pɔɪz/ *n.* mwendo; mkao; makini. *v.t./i.* tuliza sawasawa; tulia sawasawa.

**poison** /'pɔɪzn/ *n.* sumu. *v.t.* tia, lisha sumu; *(fig.)* potosha. **~er** *n.* muuaji kwa sumu. **~ous** *adj.* enye sumu; fisadi; ovu.

**poke** /pəʊk/ *v.t.* sukuma; chochea; sukumiza; chakura; subukua. *~ the fire,* chochea moto. *~ one's nose into sb.'s business,* jiingiza katika mambo ya watu. *~ fun at,* fanyia mzaha. **~r** *n.* mchocheleo; mchezo wa karata wenye mizaha.

**polar** /'pəʊlə(r)/ *adj.* -a ncha ya dunia; -a nchi ya baridi sana. **~ coordinates,** majiranguzo **front,** mkingamo wa ukanda wa baridi na joto. **~ity** *n.* jinsincha: tabia ya ncha umeme kuwa na ama chaji chanya au chaji hasi. **~ize** *v.t.* jinsishancha: fanya dutu au molekuli za dutu kuwa na ncha umeme; fanya nuru ya mitetemo kupita katika bapa fulani tu.

**pole** *n.* **1.** ncha ya kaskazini au kusini ya dunia. **~-star,** nyota ya kaskazini. **2.** ncha ya sumaku; pembe ya betri ya umeme.

**pole** /pəʊl/ *n.* ufito; upau; boriti; upondo; mhimili; mwimo; mwega.

**police** /pə'li:s/ *n.* polisi. **military ~,** polisi wa jeshi. *v.t.* simamia kwa kutumia polisi. **~ station** *n.* kituo cha polisi.

**policy** /'pɒləsi/ *n.* sera; busara; hati.

**self-reliance** ~, sera ya kujitegemea. **insurance** ~, hati ya bima.

**polio** /'pəʊliəʊ/ *n.* polio: maradhi ya kupooza mwili.

**polish** /'pɒlɪʃ/ *n.* ulaini; mng'aro; polishi. *v.t./i.* ng'arisha; kwatua; sugua; ongoza; noa. *a ~ed performer*, stadi. *a ~ed young man*, kijana mwenye heshima. *~ sth. off*, maliza upesi.

**polite** /pə'laɪt/ *adj.* -a adabu; -taratibu; -pole. **~ly** *adv.* kwa upole. **~ness** *n.* upole.

**political** /pə'lɪtɪkl/ *adj.* -a siasa; a kisiasa. **~ asylum**, hifadhi ya kisiasa. **~ party**, chama cha siasa. **~ prisoners**, wafungwa wa kisiasa. **~ geography**, jiografia ya mgawiko wa dunia kiutawala. **~ economy**, ikitisadi ya kisiasa. **~ly** *adv.*

**politics** /'pɒlətɪks/ *n.* siasa. *racial ~*, siasa ya ubaguzi. **politician** *n.* mwanasiasa. **politicize** *v.t./i.* hamasisha au hamasika kisiasa.

**poll** /pəʊl/ *n.* kura; hesabu ya kura; mtu; maoni ya watu. *go to the ~*, piga kura. *be at the head of the ~*, shinda kwa kuchaguliwa kwa wingi wa kura. **~ tax** *n.* kodi ya kichwa.

**pollen** /'pɒlən/ *n.* chavua; chavuo.

**pollinate** /'pɒləneɪt/ *v.t.* chavusha: hamisha chavuo kutoka chavulio hadi stigma.

**pollute** /pə'lu:t/ *v.t.* tia taka; chafua. **pollutant** *n.* kichafuzi.

**pollution** /pə'lu:ʃn/ *n.* uchafuzi; uchafu. **environmental ~**, uchafuzi wa mazingira.

**poly** /'pɒli/ *prefix* -ingi.

**polygamy** /pə'lɪgəmi/ *n.* mitala: desturi ya mume kuwa na wake wawili au zaidi wakati mmoja.

**polyglot** /'pɒlɪglɒt/ *adj.* -a lugha nyingi; -enye kuzungumza lugha nyingi.

**polygon** /'pɒlɪg(ə)n/ *n.* poligoni; pembe nyingi.

**polymer** /'pɒlɪmə/ *n.* polima: kampaundi yenye uzani mkubwa wa molekuli iliyotenguliwa ama kwa uongezaji wa molekuli au kwa kugandishiana molekuli. **~ization** *n.* upolimishaji: muungano wa kikemikali wa molekuli mbili au zaidi za msombo huohuo mmoja ili kuunda molekuli kubwa zaidi.

**polysyllable** /'pɒlisɪləbl/ *n.* neno lenye silabi nyingi.

**polytechnic** /,pɒli'teknɪk/ *n.* chuo cha ufundi anuwai.

**pompous** /'pɒmpəs/ *adj.* -enye majivuno; -enye kiburi; -enye kujidai. **pomposity** *n.* ushaufu; majivuno.

**pond** /pɒnd/ *n.* kidimbwi; dimbwi.

**ponder** /'pɒndə(r)/ *v.t./i.* fikiri; tafakari; waza. **~ous** *adj.* zito sana; kubwa.

**pontoon** /pɒn'tu:n/ *n.* pantoni.

**pony** /'pəʊni/ *n.* farasi mdogo.

**pool**[1] /pu:l/ *n.* kiziwa; kidimbwi; kilindi mtoni.

**pool**[2] /pu:l/ *n.* fedha za dau katika kamari; mchango wa ubia; huduma za ubia. *v.t.* changa fedha.

**poor** /pɔ:(r)/ *adj.* maskini; fukara; -nyonge; -chache; duni hafifu. *a ~ supply of teachers*, walimu haba. **~house** *n.* (la zamani) nyumba ya maskini. **~ly** *adv.* vibaya. *He is ~ off*, hana pesa nyingi. *adj.* -gonjwa. *He feels ~*, hajisikii vizuri. **~-spirited** *adj.* -liokata tamaa; -oga. **~ness** *n.* umaskini; ukosefu; unyonge. **poverty** *n.* umaskini; ufukara; ukata. *poverty striken*, hohehahe; fukara.

**pop** /pɒp/ *n.* sauti inayotoka kizibo kinapofunguka ghafla. *v.t./i.* (**-pp-**) zibua; tembelea; ingia; ingiza; kaanga bisi. *He is always ~ping in and out*, daima hatulii.

**pope** /pəʊp/ *n.* papa; baba mtakatifu.

**poplar** /'pɒplə(r)/ *n.* mpopla: mti mrefu na mnyoofu unaokua haraka sana.

**poppy** /'pɒpi/ *n.* mpopi: mmea ambao maua yake hutengenezewa kokeini na dawa anuwai za kulevya.

**populace** /'pɒpjʊləs/ *n.* watu; wananchi; umma.

**popular** /'pɒpjələ(r)/ *adj.* -a watu; -a

umma; -a wananchi; -pendwa. ~ **government**, serikali iliyochaguliwa wananchi. ~ *prices*, bei rahisi. ~ **science**, sayansi inayokimu watu kadiri ya elimu yao. **~ity** *n.* umashuhuri; kupe-ndwa na wengi.

**populate** /ˈpɒpjuleɪt/ *v.t.* jaza viumbe hai; jaza watu. **~d** *adj.* -enye watu; -enye viumbe hai.

**population** /ˌpɒpjuˈleɪʃn *n.* watu; mimea au wanyama wa sehemu fulani. **populous** *adj.* -enye watu wengi.

**porch** /pɔ:tʃ/ *n.* ukumbi; baraza.

**porcupine** /ˈpɔ:kjupaɪn/ *n.* nungu.

**pore** /pɔ:(r)/ *n.* kinyweleo; tundu katika ngozi. *v.i.* ~ *over*, soma kwa makini.

**pork** /pɔ:k/ *n.* nyama ya nguruwe. **~er** *n.* nguruwe wa nyama.

**porous** /ˈpɔ:rəs/ *adj.* -enye vinyweleo; -enye kunyonya unyevu; -enye kuruhusu maji kupenya.

**porridge** /ˈpɒrɪdʒ/ *n.* uji.

**port** /pɔ:t/ *n.* **1.** bandari; mji wenye bandari; mahali pa usalama. *free* ~ bandari huru. **2.** mlango wa ubavuni mwa meli. ~*hole*, dirisha la ndege au meli. **3.** upande wa kushoto wa meli ukikabili gubeti mbele. **4.** poto: divai nyekundu nzito na tamu.

**portable** /pɔ:təbl/ *adj.* -a kuchukulika; -epesi.

**portal** /ˈpɔ:tl/ *n.* mlango mkubwa.

**porter** /ˈpɔ:tə(r)/ *n.* mchukuzi; mpagazi.

**portfolio** /pɔ:tˈfəʊliəʊ/ *n.* jalada la kuwekea nyaraka; dhamana katika kazi; ofisi ya waziri wa nchi.

**portion** /ˈpɔ:ʃn/ *n.* sehemu. *v.t.* gawanya katika sehemu.

**portrait** /ˈpɔ:treɪt/ *n.* picha; taswira. **~ure** *n.* ustadi wa kuchora picha.

**portray** /pɔ:ˈtreɪ/ *v.t.* chora picha; eleza; fafanua; simulia; igiza. **portrayal** /pɔ:ˈtreɪəl/ *n.* uchoraji picha; uelezaji; ufafanuzi.

**pose** /pəʊz/ *n.* mkao; sura; hali; uigizaji. *v.t./i.* kukaa namna maalumu; kujifanya; kujidai; kuiga; toa hoja au swali. **~ur** *n.* mpenda makuu. **posture** *n.* mkao; hali; msimamo.

**position** /pəˈzɪʃn/ *n.* mahali; hali; namna; msimamo; uwezo; nafasi; kazi; cheo. *What's your ~ on this problem?* una msimamo gani juu ya jambo hili?

**positive** /ˈpɒzətɪv/ *adj.* -a hakika; halisi; waziwazi; bayana; dhahiri; -a kujenga; -a kusaidia; -a kuunga mkono; chanya. *Are you ~ about what time it was?* una hakika ilikuwa saa ngapi? *a ~ suggestion*, wazo la kufaa. ~ *help*, msaada wa hakika. *(grammar)* -a kukubali. **~ly** *adv.* kwa kukubali.

**possess** /pəˈzəs/ *v.t.* miliki; -wa na; hodhi; tawala; shika: ~ *one's soul in patience*, stahamili; vumilia. ~ *oneself of*, jimiliki; jizuia. *be ~ed*, pagawa; chagawa. **~ion** *n.* umilikaji; mali; miliki. *be in ~ion of*, miliki. **~ive** *adj.* -a kumiliki; -enye tamaa; *(grammar)* -milikishi.

**possible** /ˈpɒsəbl/ *adj.* -a kuwezekana; -a kuyumkinika; -a kufaa. **possibly** *adv.* kwa kadiri iwezekanavyo; labda.

**possibility** /ˌpɒsəˈbɪləti/ *n.* uwezekano; kitu kiwezekanacho.

**post**[1] /pəʊst/ *n.* **1.** lindo. **2.** mahali pa kufanya biashara. **3.** cheo; daraja; nafasi katika kazi. *v.t.* weka walinzi; weka mahali pa kazi. **4.** posta. *v.t. /i.* peleka kwa njia ya posta; andika katika daftari; enda kwa farasi. ~ *up*, andika katika daftari. *keep sb. ~ed*, fahamisha mtu juu ya habari yote. **~age** *n.* ada ya posta. **~al** *adj.* -a posta: ~ *al order*, hundi ya posta. **~card** *n.* postikadi. **~er** *n.* bango. **~man** *n.* mtu wa posta. **~master** *n.* postamasta. **~mistress** *n.* postamasta wa kike. **~office** *n.* posta. **5.** mhimili; nguzo; mwimo; tendegu. *v.t.* ~ *sth. up*, bandika mahali wazi; tangaza.



**post office box**

**post**[2] /pəʊst/ *-prefix* baada ya. **~date** *v.t.* weka tarehe ya mbele. **~graduate**

*adj.* -a uzamili; -ya baada ya digirii ya kwanza. **~humous** *adj.* -a baada ya kufa. **~-mortem** *n.* uchunguzi wa maiti. **~script** *n.* *(ps)* maneno ya nyongeza katika barua; taarifa ya ziada.

**postpone** /pəˈspəʊn/ *v.t.* ahirisha. **~ment** *n.* uahirisho.

**pot** /pɒt/ *n.* chungu; sufuria. *a coffee~,* mdeli. *a tea ~,* buli. *~s of money, (slang)* fedha nyingi sana. *v.t.* (**-tt-**) hifadhi katika chungu; panda mche katika chungu. **~-hole** *n.* shimo lililochimbika kwa taathira ya maji. **~luck** *n.* chakula. *take ~ luck,* -la kwa kuwa umetokea watu wanakula. **~ter** *n.* mfinyanzi. **~tery** *n.* vyombo vya udongo; ufinyanzi.

**potash** /ˈpɒtæʃ/ *n.* shura; potashi.

**potassium** /pəˈtasɪəm/ *n.* potasiamu. **~ carbonate**, magadi.

**potato** /pəˈteɪtəʊ/ *n.* (**~es**) kiazi; mbatata.

**potent** /ˈpəʊtnt/ *adj.* -enye nguvu.

**potency** /ˈpəʊtnsi/ *n.* nguvu. **~ate** *n.* mtu mwenye nguvu. **~ial** *adj.* -enye kuwezekana; -enye kuweza kuwa. **~ difference**, tofauti uweza: mwachano wa uweza kati ya sehemu au nukta mbili tofauti. **~ energy**, nishati weza: nishati inayotokana na jinsi ya kitu au mahali kitu kilipo.

**potter** /ˈpɒtə(r)/ *v.i.* fanya kazi bila juhudi; chezacheza na kazi. *n.* mfinyanzi

**potty** /ˈpɒti/ *adj.* *(colloq.)* hafifu, -dogo; -sio muhimu. *n.* poti: chombo cha mtoto cha kuendea haja; -enye kichaa.

**pouch** /paʊtʃ/ *n.* pochi; kifuko; mbeleko wa kangaruu; kifuko cha mbegu katika mmea.

**poultry** /ˈpəʊltri/ *n.* jamii ya kuku, mabata, etc. **~ farm**, shamba la kuku. **poulterer** *n.* muuza kuku, mabata, etc.

**pounce** /paʊns/ *v.i.* rukia; shambulia ghafla; vamia. *n.* mruko wa ghafla.

**pound** /paʊnd/ *n.* **1.** ratili. **2.** pauni. **3.** zizi la kuhifadhia wanyama waliopotea. *v.t.* twanga; ponda; funda. **~er** *n.* mchi.

**pour** /pɔ:(r)/ *v.t.* mimina; mwaga; toa kwa wingi. *v.i.* miminika; mwagika; toka kwa wingi; nyesha sana. *People ~ ed into the town,* watu walimiminika mjini.

**powder** /ˈpaʊdə(r)/ *n.* poda; unga; vumbi; baruti. *gun ~,* baruti. *~ magazine,* ghala ya baruti.*v.t./i.* tia poda; paka poda; ponda; saga.

**power** /ˈpaʊə(r)/ *n.* uwezo; nguvu; enzi; amri; mamlaka; mwenye nguvu; madaraka; mzimu; kipeo: *He gave me all the help in his ~,* alinisaidia kwa nguvu zake zote. *have sb. in your ~,* dhibiti mtu. **~house**, **~ station** *n.* kituo, kinu cha umeme. **~less** *adj.* dhaifu; -sio na nguvu.

**practice** /ˈpræktɪs/ *n.* mazoezi; utekelezaji; utendaji; mazoea; desturi; weledi; hila. *put a plan into ~,* tekeleza mpango. *the ~ of closing shops on Sundays,* desturi ya kufunga maduka Jumapili. *sharp ~,* tendo la ujanja. **practicable** *adj.* enye kuweza kufanyika; -enye kuweza kutumika; -a kupitika. **practical** *adj.* -a utendaji; -a busara; -a kufaa. *pratical difficulties,* matatizo ya kiutendaji. **practically** *adv.* kwa busara; kwa kweli.

**practise** /ˈpræktɪs/ *v.t.* fanya mazoezi; -wa na desturi; tenda; fanya kazi. *practise the piano,* jizoeza kupiga piano. *Practise what you preach,* fanya unavyohubiri. *practise the law,* fanya kazi ya sheria. **practised** *adj.* -stadi; -zoefu.

**prairie** /ˈpreəri/ *n.* uwanda; nyika.

**praise** /preɪz/ *n.* sifa; utukufu; *v.t.* sifu; tukuza; himidi; adhimisha. *sing one's own ~s,* jisifu. **~worthy** *adj.* -a kustahili sifa.

**prawn** /prɔ:n/ *n.* kamba.

**pray** /preɪ/ *v.i./t.* omba Mungu; sali; omba dua; sihi; taka; tafadhalisha. **~er** *n.* sala; dua; haja; maombi; ibada. *~ leader,* imamu. *~ mat, ~ rug,* msala.

**pre-** /pri:/ *prefix* kabla ya.

**preach** /pri:ʃ/ *v.t.* hutubu; hutubia; hubiri; hubiria; shawishi; shauri.

**~er** *n.* khatibu; mhubiri.

**precaution** /prɪ'kɔ:ʃn/ *n.* hadhari; uangalifu. *take ~s,* jihadhari.

**precede** /prɪ'si:d/ *v.t.* tangulia; sabiki. **~nce** *n.* kipaumbele. *This question takes ~ over all others,* suala hili lipewe kipaumbele. **~nt** *n.* kigezo; kitangulizi.

**precinct** /'pri:sɪŋ(k)t/ *n.* uwa; mahali jirani; mpaka; eneo.

**precious** /'preʃəs/ *adj.* -a thamani; ghali; -a tunu.

**precipice** /'presəpɪs/ *n.* genge; jabali. **precipitous** *adj.* -a kama genge; -enye mwinuko mkali sana.

**precipitate** /prɪ'sɪpɪteɪt/ *n.* mango isomumunyika inayounndwa kwenye mmumunyo baada ya utendanaji wa kimaumbo au kikemikali.

**precipitation** /prɪˌsɪpɪ'teɪʃn/ *n.* ukapishaji: uundaji wa makapi ya msombo usiomumunyika kwa uvunjika jirejea maradufu.

**precis** /'preɪsi/ *n.* muhtasari; ufupisho wa maneno au maandishi.

**precise** /prɪ'saɪs/ *adj.* sahihi; sawasawa kabisa; -a taratibu; -angalifu; wazi; dhahiri; -a kushika kawaida barabara. **~ly** *adv.* kabisa; naam; kwa uangalifu; kwa usahihi.

**precision** *n.* usahihi; utaratibu.

**predator** /'predətə(r)/ *n.* mwinda: mnyama anayewinda na kula wanyama wingine.

**predecessor** /'pri:dɪsesə(r)/ *n.* mtangulizi; kitu kilichotangulia.

**predicament** /prɪ'dɪkəmənt/ *n.* mashaka; hatari; shida; hali ngumu.

**predicate** /'prɛdɪkət/ *n.* kiarifu: neno lenye maelezo ya kiima. *v.t.* semea; arifu; sababisha; leta.

**predict** /prɪ'dɪkt/ *v.t.* bashiri; tabiri; agua.

**predominant** /prɪ'dɒmɪnənt/ *adj.* kuu; -enye kuzidi -ingine.

**predominance** /prɪ'dɒmɪnəns/ *n.* ukuu; uzidifu; kuwa na nguvu.

**predominate** /prɪ'dɒmɪneɪt/ *v.i.* pita; shinda; zidi.

**pre-eminent** *adj.* -a kushinda ingine -ote; bora kabisa.

**preface** /'prɛfəs/ *n.* utangulizi; dibaji.

**prefer** /prɪ'fɜ:(r)/ *v.t.* (**-rr-**) penda zaidi. **~able** *adj.* -ema zaidi; bora; afadhali. **~ably** *adv.* zaidi; kwa kupendelea. **~ence** *n.* upendeleo; hiari; uteuzi; kitu kilichoteuliwa. **~ential** *adj.* -a kupendelea. **~ment** *n.* kupandisha cheo.

**prefix** /'pri:fɪks/ *n.* *(grammar)* kiambishi awali; lakabu. *v.t.* tia mwanzoni; tanguliza lakabu; ambisha awali.

**pregnant** /'pregnənt/ *adj.* -enye mimba; -enye maana nyingi. **pregnancy** *n.* mimba; ujauzito.

**prehensile** /prɪ'hɛnsʌɪl/ *adj.* -enye nguvu za kushika.

**prehistoric** /ˌpri:hɪ'stɒrɪk/ *adj.* -a kabla ya historia.

**prejudice** /'predʒudɪs/ *n.* hisia kuhusu mtu au kitu au jambo lisilo na uthibitisho; athari; madhara; dhuluma; *to the ~ of sb.,* -a kuelekea kumletea fulani madhara. *v.t.* chukia; pendelea; bagua; athiri; dhuru; haribu; punguza upendeleo wa mtu.

**prejudicial** /ˌpredʒu'dɪʃl/ *adj.* -a kudhuru.

**preliminary** /prɪ'lɪmɪnəri/ *n.* tendo la mwanzo. *adj.* -a mwanzo; tangulizi.

**premature** /'premətʃə(r)/ *adj.* -a kabla ya wakati wake. **~ly** *adv.* upesi; kabla ya wakati wake.

**premeditate** /ˌpri:'medɪteɪt/ *v.t.* waza; panga mapema; azimia; dhamiria.

**premier** /'prɛmɪə/ *n.* waziri mkuu. *adj.* -a kwanza; kuu.

**premium** /'prɪ:mɪəm/ *n.* malipo ya uanagenzi; ada; zawadi; bonasi; thamani ya juu. *put a ~ on good behaviour,* ahidi zawadi kwa mwenendo mwema. *be at a ~,* zidi kuwa na thamani.

**premolar** *n.* sagego: jino ambalo kazi yake ni kusaga chakula na ambalo linakuwemo katika seti ya meno ya utotoni.

**premonition** /ˌprɛmə'nɪʃ(ə)n/ *n.*

wasiwasi kuwa jambo litatokea.
**prepare** /prɪ'peə(r)/ *v.t./i.* fanya; tayarisha; zatiti; andaa; pika. *be ~d to,* -wa tayari; weza.
**preparation** /ˌprepə'reɪʃn/ *n.* matayarisho; maandalizi; utayarishaji.
**preponderant** /prɪ'pɒndərənt/ *adj.* -a kuzidi; -kubwa; -ingi. **preponderance** *n.* hali ya uzidifu, ukubwa au wingi.
**preposition** /ˌprɛpə'zɪʃ(ə)n/ *n.* *(grammar)* kihusishi. **~al** *adj.* -a kihusishi.
**prerequisite** /pri:'rɛkwɪzɪt/ *n./adj.* kanuni; sharti.
**prerogative** /pri'rɒgətɪv/ *n.* haki; ridhaa; hiari.
**prescribe** /prɪ'skraɪb/ *v.t.* agiza; amuru; shauri.
**prescription** /prɪ'skrɪpʃn/ *n.* agizo; agizo la daktari.
**present** /'prɛz(ə)nt/ *n.* **1.** siku hizi; wakati uliopo; wakati wa sasa. **2.** zawadi; tunzo; hiba. *adj.* -liopo; -a sasa; -a wakati huu; -a siku hizi; -a wakati mwafaka; -a mara moja. *~ company,* watu waliopo. *v.t.* toa; tunukia; tunza; fichua; onyesha; dhihirisha; hudhuria; fika; wasili. *~ sb. to sb.,* tambulisha rasmi. *~ arms,* toa heshima kwa silaha. *~ a cheque at the bank,* peleka cheki benki kwa malipo. *~ oneself,* hudhuria.
**presence** /'prezns/ *n.* kuwapo; sura; umbo; namna mtu anavyo-onekana. *in the presence of his friends,* mbele ya rafiki zake. *presence of mind,* welekevu wa akili; busara. **~able** *adj.* -a kupendeza; -zuri; -a kufaa. **~ation** *n.* kupa; kutoa; kuwasilisha. **~er** *n.* mtangazaji wa vipindi vya redio au televisheni; mtoa zawadi. **~ly** *adv.* hivi karibuni; sasa hivi.
**preserve** /prɪ'zɜ:v/ *n.* hifadhi. *v.t.* tunza; linda; hifadhi; weka.
**preservation** /ˌprezə'veɪʃn/ *n.* hifadhi; kulinda. **preservative** *n.* kitu kinachozuia kitu kingine kisioze. *adj.* -enye kulinda; -enye kuhifadhi.
**preside** /prɪ'zaɪd/ *v.i.* -wa kiongozi; -wa mkuu; -wa mwenyekiti. **~ncy** *n.* uraisi; ofisi ya raisi. **~nt** *n.* raisi. **~ntial** *adj.* -a raisi. *presidential commission,* tume ya raisi.
**press** /pres/ *n.* mgandamizo; shinikizo; mtambo wa kusindikia; magazeti; waandishi wa magazeti; upigaji chapa; msongamano wa watu. *the ~,* magazeti. *v.t.* gandamiza; minya; bonyeza; kamua; sindika; piga pasi; nyoosha; bana; sisitiza; songamana. *~ for,* omba sana; sihi; himiza. *be ~sed for time,* -wa na wakati mchache. *the matter is ~ing,* jambo linahitajika sana. *time ~es,* wakati unasonga. *~ sb.'s hand,* shika mkono wa fulani. *in the ~,* katika kupigwa chapa. **~ing** *adj.* muhimu; -a dharura. **~man** *n.* mwandikaji habari magazetini. **~ure** *n.* shinikizo; kani eneo; mkazo; mbano; uelemeaji **atmospheric ~**, shinikizo angahewa. *bring ~ to bear on sb. to do sth.,* shinikiza. *work at high ~,* fanya kazi kwa nguvu nyingi.
**prestige** /pre'sti:ʒ/ *n.* sifa njema; heshima; fahari; hadhi.
**presume** /prɪ'zju:m/ *v.i.* dhania; waza; kisia; thubutu. *~ upon,* tumia vibaya ukarimu wa mtu.
**presumption** /prɪ'zʌmpʃn/ *n.* **1.** jambo linalowezekana. **2.** ufedhuli; usafihi; kiburi; ujuvi. **presumptive** *adj.* -a kutarajiwa; -a kusadikiwa.
**presumptuous** /prɪ'zʌmptʃuəs/ *adj.* -enye kiburi; fedhuli; -juvi; safihi; -enye kujiamini mno.
**pretend** /prɪ'tend/ *v.i.* jifanya; jisingizia; danganya. **~er** *n.* mtu anayejifanya, anayejidai, anaye danganya ili anufaike.
**pretence** /prɪ'tens/ *n.* kujisingizia; kisingizio; uwongo; kujifanya; hila; ulaghai.
**pretext** /'prɪ:tekst/ *n.* kisingizio.
**pretty** /'prɪti/ *adj.* -zuri; safi; -a kupendeza. /*adv.* *(colloq.)* -a kutosha. *I'm ~ well,* sijambo vyema. **prettily** *adv.* vizuri. **prettiness** *n.* sura nzuri; uzuri.
**prevail** /prɪ'veɪl/ *v.i.* shinda; tapakaa; enea. *~ upon sb. to do sth.,* shawishi.

**prevalence** /'prevələns/ *n.* uenevu; ushindi. **prevalent** *adj.* -enye kuenea; tele.
**prevent** /prɪ'vent/ *v.t.* zuia; pinga; kataza; kinga. **~able** *adj.* -a kuzuilika. **~ion** *n.* kuzuia; kukinga; kinga. **~ive** *adj.* -a kuzuia; -a kulinda; -a kukinga.
**previous** /'pri:viəs/ *adj.* -a kwanza; -liotangulia; -a zamani. **~ly** *adv.* hapo nyuma; hapo awali.
**prey** /preɪ/ *n.* mateka; mawindo; nyara. *bird of ~*, ndege mbuwai, e.g. tai. *be a ~ to fears*, shikwa na hofu.
**price** /praɪs/ *n.* thamani; bei. *v.t.* tia,weka, panga bei. **~ less** *adj.* -a thamani mno.
**prick** /prɪk/ *n.* mchomo; maumivu; kitobo; kichomi. *v.t./i.* toboa; choma, hisi maumivu makali. *my finger ~s*, kidole changu kinani chomachoma. *~ up the ears*, simamisha masikio; sikiliza kwa makini. **~le** *n.* mwiba. *v.i./t.* chomachoma; washa. **~ly** *adj.* -enye miiba; -enye kuchomachoma. *~ heat*, harara: vipele vya joto. *~ pear*, mpungate.
**pride** /praɪd/ *n.* fahari; heshima; kitu cha kujivunia; kiburi; majivuno. *v.t. ~ oneself on*, jivunia; jidai.
**priest** /pri:st/ *n.* kasisi; kuhani; padri. **~hood** *n.* ukuhani; ukasisi; upadri; jumuia ya makasisi. **~ly** *adj.* -a kasisi; -a padri; -a kuhani.
**primary** /'praɪməri/ *adj.* -a kwanza; -a msingi; -a awali. **~ cell**, seliumeme ya msingi: seliumeme ambayo haiwezi kuchajiwa. **~ colours**, rangi za msingi, yaani nyekundu, buluu na manjano. **~ consumers**, walamajani: wanyama wanaokula majani. **~ sexual characteristics**, sifamsingi jinsia: mabadiliko ya msingi yatokeayo kwa mtu katika umri wa baleghe.
**primate** /'prʌɪmeɪt/ *n.* mamalia wa hali ya juu; askofu mkuu.
**prime** /praɪm/ *n.* mwanzo; upeo; usitawi; ukamilifu; sehemu iliyo bora; sala ya alfajiri. *adj.* -kuu; bora; -a kwanza; tasa; -a asili; -a msingi. **~ number**, namba tasa. *v.t.* tengeneza; andaa.
**primer** /'praɪmə(r)/ *n.* kitabu cha masomo ya kwanza.
**primitive** /'prɪmətɪv/ *adj.* -a kale; -a asili; -siostaarabika.
**prince** /prɪns/ *n.* mwana wa kiume wa mfalme. **~ss** *n.* binti mfalme. **~ly** *adj.* -a fahari; -a kustahili ufalme.
**principal** /'prɪnsəpl/ *n.* mkuu; mtaji; wakala; mhalifu mkuu; mhimili mkuu. **~ focus**, fokasi kuu: fokasi wakati miali mtuo inapokuwa sambamba na mhimili mkuu. *adj.* -kuu. **~ity** *n.* mamlaka ya mwana wa mfalme. **~ly** *adv.* hasa; aghalabu.
**principle** /'prɪnsəpl/ *n.* kanuni; maadili; msimamo.
**print** /prɪnt/ *n.* chapa; alama; kitabu; chapisho; kitambaa cha maua; picha; mchoro; mwandiko wa wima. *v.t.* piga chapa; safisha picha; tia, weka alama; tia moyoni; chapisha. *finger ~s*, alama za vidole. *foot ~s*, nyayo. **~able** *adj.* -enye kuchapika. **~er** *n.* mpiga chapa. **~ing press** *n.* matbaa: kiwanda cha kupigia chapa. **~ out** *n.* karatasi zilizochapwa kwa kompyuta.
**prior** /'praɪə(r)/ *n.* mkuu wa nyumba ya watawa. *adj.* -a kwanza; liotangulia. **~ity** *n.* kipaumbele; umuhimu wa kwanza; haki ya kutangulia.
**prism** /'prɪzəm/ *n.* prizimu: umbo lenye ncha sambamba na sawa.
**prison** /'prɪzn/ *n.* jela; gereza. *~ breaker*, mtoroka jela. **~er** *n.* mfungwa; mahabusi. **~ of conscience**, mfungwa wa kisiasa. **~ of war**, mfungwa wa vita.


prism

**private** /'praɪvət/ *n.* askari; faragha; siri. *in ~*, kwa siri. *adj.* -a binafsi; -a faragha; si -a serikali. **~ soldier**, askari asiye cheo. **~ly** *adv.* kwa siri.
**privacy** /'prɪvəsi/ *n.* faragha; upweke; siri.
**privation** prʌɪ'veɪʃ(ə)n/ /*n.* upungufu; ukosefu; ufukara; shida; taabu.
**privilege** /'prɪvəlɪdʒ/ *n.* fursa;

marupurupu; faida; haki; heshima; upendeleo. **~d** *adj.* -liopendelewa; -liobahatika.

**prize** /praɪz/ *n.* **1.** tunzo; zawadi; kitu cha thamani. **2.** mateka. *v.t.* thamini sana; fungua kwa kitu kama mtaimbo. **~fight** *n.* shindano la ngumi la kulipwa.

**pro-** /prəʊ/ *prefix* -a kuunga mkono. *~ government,* -enye kuunga mkono serikali.

**pros and cons** *n.* uzuri na ubaya; sifa na kasoro; ubora na udhaifu.

**probability** /ˌprɒbəˈbɪləti/ *n.* welekeo. **~ distribution of electrons**, mgawanyo wezekani wa elektroni. **balance of probabilities**, kipimo cha welekeo.

**probable** /ˈprɒbəbl/ *adj.* yamkini; -lioelekea kuwa au kutokea.

**probably** /ˈprɒbəbli/ *adv.* yumkini; huenda; labda; asaa.

**problem** /ˈprɒbləm/ *n.* tatizo; mzozo; utatanishi; mgogoro; swali; mashaka; hoja; fumbo. **~atic** *adj.* -tatanishi.

**proboscis** /prəˈbɒsɪs/ *n.* **1.** kifyonzeo: sehemu ya mdomo iliyorefuka na kuwa mrija katika baadhi ya wadudu na wanyama. **2.** mkonga: sehemu ya tembo inayojitokeza kwa mbele ambayo huitumia kama mkono na pua yake.

**procedure** /prəˈsiːdʒə(r)/ *n.* utaratibu; au jinsi ya kutenda. **procedural** *adj.* -a utaratibu.

**proceed** /prəˈsiːd/ *v.i.* endelea mbele; shika njia; enda; toka; shtaki. **~ing** *n.* tendo; jambo; utendaji jambo; *take ~s against sb.,* shtaki; dai mahakamani. **proceedings** *n.* **1.** kumbukumbu; mashauri mafupi. **2.** mlolongo wa matukio yaliyowekwa kwa taratibu maalumu.

**proceeds** /prəʊsiːdz/ *n.* mapato; faida.

**process** /prəʊsɛs/ *n.* mfuatano; mlolongo; maendeleo; njia; jinsi; namna; hati; mfanyiko tendani; mchakato. **legal ~**, daawa. *v.t.* tengeneza; tenda; andamana; safisha. **procession** *n.* mwandamano, maandamano.

**proclaim** /prəˈkleɪm/ *v.t.* tangaza; mpiga mbiu; toa ilani; eneza; bainisha; onesha. **proclamation** *n.* tangazo; ilani; mbiu; taarifa.

**prod** /prɒd/ *n.* chombo chenye ncha; uchochezi. *v.t.* choma; chokoa; chokoza; chochea.

**prodigious** /prəˈdɪdʒəs/ *adj.* -ingi mno; -a ajabu mno.

**prodigy** /ˈprɒdədʒi/ *n.* muujiza; kioja; ajabu.

**produce** /prəˈdjuːs/ *n.* mazao; mavuno. *v.t.* leta; onyesha; tengeneza; buni; tunga; sababisha; zaa; taga; zalisha; *(math.)* refusha. *~ a play,* tunga mchezo. **~r** *n.* mzalishaji mali; mtungaji, mwonyeshaji mchezo.

**product** /ˈprɒdʌkt/ *n.* mazao; mavuno; bidhaa; matokeo; *(arith.)* zao.

**production** /prəˈdʌkʃn/ *n.* uzalishaji mali. **productive** *adj.* -enye kuzaa; -zazi; -enye kuzalisha mali; -enye rutuba. *discussions that are productive only of quarrels,* mazungumzo yaletayo ugomvi tu.

**profess** /prəˈfes/ *v.t.* shuhudia; ungama; tangaza; toa hoja; kiri; weka nadhiri; dai; jidai; -wa mweledi; fanya kazi ya. *I don't ~ to be an expert,* sijadai kuwa mtaalamu. *a ~ed friend,* rafiki wa kujidai. **~edly** *adv.* kwa maneno yako mwenyewe. **~ion** *n.* kazi; ungamo; ahadi. **~ional** *n.* mchezaji wa kulipwa. *adj.* -a kitaalamu; -a kazi ya kulipwa. *~ skill,* ustadi. *~ men,* wenye kazi za kitaalamu. *~ footballer,* achezaye mpira kwa kulipwa. **~or** *n.* mwalimu; mtangaza imani; profesa. **assistant ~**, profesa msaidizi. **associate ~**, profesa mshiriki.

**proficient** /prəˈfɪʃnt/ *adj.* hodari; bingwa; -enye maarifa; -elekevu; stadi. **proficiency** *n.* ustadi; ubingwa; uhodari; welekevu.

**profile** ˈ/prəʊfaɪl/ *n.* maelezo mafupi juu ya mtu; sura ya mtu au kitu kwa upande; ukingo wa kitu.

**profit** /ˈprɒfɪt/ *n.* faida; manufaa. **~**

**and loss account**, akaunti ya faida na hasara. ~ **margin**, faida halisi. *v.t./i.* faidika; saidia; saidiwa; pata faida. **~able** *adj.* -a kufaa; -enye faida; -enye kusaidia. **~eer** *n.* mlanguzi. *v.t.* langua.

**profound** /prə'faʊnd/ *adj.* -a kina; -a ndani sana; -kubwa; -a wingi; -a maana sana; -zito; -enye kuhitaji maarifa mengi. *a ~ sleep*, usingizi mzito. ~ *thinker*, mtu mwenye fikra nyingi. **~ly** *adv.* sana; kwa kina; kwa akili nyingi. **~ity** *n.* kina; kwenda ndani.

**progesterone** /prə'dʒɛstərəʊn/ *n.* projesteroni: homoni za kike ambazo huwezesha kukua hali ya uzazi katika uterasi na kukuza kiinitete hadi mtoto kuzaliwa.

**programme** /'prəʊgræm/ *n.* programu; utaratibu; mpango; mfuatano wa vipindi vya redio au televisheni. *v.t.* tengeneza programu (ya kompyuta).

**progress** /'prəʊgres/ *n.* mwendo wa mbele; maendeleo; kwenda mbele; safari rasmi ya kiongozi wa nchi. *v.i.* endelea; piga hatua; songa mbele. **~ion** *n.* kuendelea; uendeleaji; kwenda; kuendelea mbele. **modes of ~**, aina za miondoko. **~ive** *n.* mpenda maendeleo. *adj.* -a kuendelea mbele; -a kuongezeka hatua kwa hatua; -a kupendelea maendeleo; -a moja kwa moja.

**prohibit** /prə'hɪbɪt/ *v.t.* kataza; piga marufuku; zuia. **~ion** *n.* makatazo; kizuizi. **~ive** *n.* ghali mno; -a kukataza; -enye kuzuia.

**project** /'prɒdʒekt/ *n.* mradi; mpango. *v.t./i.* panga; sanifu; onyesha; chora picha au ramani ya kitu; vurumisha; chomoza. **~ile** *n.* kombora. **~ion** *n.* mtupo; mvurumisho; uchomozaji; usanifishaji mipango; picha; ramani; utupaji kivuli au picha mbele. **~or** *n.* projekta: chombo kitupacho picha mbele e.g. katika sinema.

**proletarian** /,prəʊlɪ'tɛ:rɪən/ *n.* mfanyakazi wa tabaka la chini. *adj.* a mfanyakazi. ~ **internationalism**, mshikamano wa kimataifa wa wafanyakazi. **proletariat** *n.* tabaka la wafanyakazi; tabaka la watu wa kawaida.

**prolific** /prə'lɪfɪk/ *adj.* -a kuzaa sana; -a kufanya mengi.

**prologue** /'prəʊlɒg/ *n.* utangulizi; dibaji; shairi la utangulizi.

**prolong** /prə'lɒŋ/ *v.t.* refusha. **~ed** *adj.* -liorefushwa. **~ation** *n.* urefushaji.

**prominent** /'prɒmɪnənt/ *adj.* mashuhuri; maarufu; -a kujulikana; -a kuchomoza; -a kutokeza. **prominence** *n.* umaarufu; umashuhuri; utokezaji.

**promiscuous** /prə'mɪskjʊəs/ *adj.* -zinzi; -liochangamana; -sio na taratibu; shaghalabaghala; vivi hivi; -a fujofujo; ovyoovyo.

**promise** /'prɒmɪs/ *n.* ahadi; kiaga; miadi; matumaini; tarajio. **promising** *adj.* -a kutumainiwa.

**promissory** /'prɒmɪs(ə)ri/ *adj.* -a ahadi; -enye ahadi. *a promissory note*, hawala; waraka wa ahadi.

**promontory** /'prɒm(ə)nt(ə)ri/ *n.* rasi.

**promote** /prə'məʊt/ *v.t.* pandisha cheo; tangaza; imarisha; saidia kuanzisha. **~r** *n.* msaidizi. **promotion** *n.* kupanda cheo; uanzishaji; ukuzaji.

**prompt** /prɒmpt/ *adj.* -a papo hapo; -epesi. *v.t.* chochea; shawishi; kumbusha. **~er** *n.* mkumbushaji.

**prone** /prəʊn/ *adj.* a kifudifudi. ~ *to*, -a kuelekea.

**prong** /prɒŋ/ *n.* ncha ya uma.

**pronoun** /'prəʊnaʊn/ *n.* kiwakilishi.

**pronounce** /prə'naʊns/ *v.t.* tamka; nena wazi; tangaza; toa hukumu. **~able** *adj.* a kutamkika. **~d** *adj.* thabiti; wazi. **~ment** *n.* hukumu; tangazo; maelezo ya nia au shauri.

**pronunciation** /prə'nʌnsi'eɪʃn/ *n.* matamshi; lafudhi.

**proof** /pru:f/ *n.* ushahidi; uthibitisho; ithibati; prufu: nakala ya kitabu ya kupitiwa kwa masahihisho; uelekezaji; jaribio; uchunguzi. *adj.* -siopenyeka; hodari; thabiti; imara. *a rain-~ coat*,

rinkoti. ~ *against temptation*, imara; -siovutwa kwa mabaya.

**prop** /prɒp/ *n.* mhimili; nguzo. *pit ~s*, mihimili ya dari za migodi; *(fig.)* mtu wa kutegemewa. *He was the ~ of his parents during their old age*, alikuwa tegemeo la wazazi wake walipozeeka. *v.t.* (**-pp-**) ~ *up*, saidia; wekea mwega; weka sawa.

**propaganda** /ˌprɒpəˈgændə/ *n.* propaganda; uenezi habari; kampeni. **health ~**, kampeni ya afya.

**propagate** /ˈprɒpəgeɪt/ *v.t.* eneza; tangaza; zaa; zalisha. **propagation** *n.* uzaliano; usambazaji; uenezaji. ~ *of light*, msambazo wa mwanga.

**propel** /prəˈpel/ *v.t.* (**-ll-**) sogeza mbele;endesha; sukumia mbele. **~ler** *n.* rafadha. ~ *shaft*, mtaimbo endeshi.



propeller

**proper** /ˈprɒpə(r)/ *adj.* -a kufaa; -a kustahili; stahiki; -a adabu; -a heshima; halisi; maalumu kwa; kamili. *do something ~ to the occasion*, fanya jambo mwafaka kwa tukio. **~ fraction**, sehemu halisi. **~ noun**, jina la pekee. **~ly** *adv.* vizuri; kikamilifu. ~ *speaking*, kwa kusema kweli.

**property** /ˈprɒpəti/*n.* mali; miliki; sifa; tabia; nguvu; rasilimali. **immovable ~**, mali isiyo-hamishika. **real ~**, ardhi na majengo.

**prophecy** /ˈprɒfɪsi/ *n.* utume; unabii; uaguzi; bishara. **prophesy** *v.t.* agua; bashiri; tabiri.

**prophet** /ˈprɒfɪt/ *n.* mtume; nabii; mwaguzi; mwanzilishi; mwasisi. **prophetic** *adj.* -a nabii; -a kubashiri.

**prophylactic** /ˌprɒfɪˈlaktɪk/ *n./adj.* dawa ya kuzuia ugonjwa; -a kukinga ugonjwa.

**proportion** /prəˈpɔːʃn/ *n.* uwiano; urari; sehemu; hisa; vipimo; *(maths)* kadri ya uhusiano baina ya seti mbili za namba. *wide in ~ to the height*, -pana kwa kulinganisha na urefu wake. *A large ~ of North Africa is desert*, sehemu kubwa ya Afrika ya Kaskazini ni jangwa. *v.t.* linganisha; gawanya; gawa. **~al** *adj.* -a uwiano; -a urari; -a kuwiana. **~ate** *adj.* -linganifu.

**propose** /prəˈpəʊz/ *v.i.* pendekeza; shauri; posa. ~ *marriage*, posa.

**proposal** /prəˈpəʊzl/ *n.* pendekezo; posa; shauri; mradi. **proposition** *n.* neno; shauri; swali; fumbo; suala; wazo; rai; pendekezo; kauli.

**propound** /prəˈpaʊnd/ *v.t.* toa; leta; nena. ~ *a riddle*, toa kitendawili.

**proprietor** /prəˈpraɪətə(r)/ *n.* mmilikaji. **proprietress** *n.* mmilikaji wa kike.

**propriety** /prəˈpraɪəti/ *n.* adabu; utaratibu; uzuri; makini; usahihi; urazini.

**propulsion** /prəˈpʌlʃn/ *n.* nguvu ya kusogeza mbele; msukumo. **jet ~**, mwendo wa jeti.

**prose** /prəʊz/ *n.* nathari; lugha ya mjazo.

**prosecute** /ˈprɒsɪkjuːt/ *v.t.* endesha mashtaka; shtaki; endelea na. *He ~d his enquiry*, aliendelea na uchunguzi wake. **prosecution** *n.* mashtaka. **prosecutor** *n.* mshataki; mdai. **public ~**, mwendesha mashtaka wa serikali.

**prospect** /ˈprɒspekt/ *n.* mandhari; uono; matazamio; matarajio; matumaini; mteja. *There is little ~ of success*, kuna matumaini madogo ya kufanikiwa. *v.t.* tafuta madini. ~ *for gold*, tafuta dhahabu. **~ive** *adj.* -a kutarajiwa. **~or** *n.* mtafuta madini.

**prospectus** /prəˈspektəs/ *n.* muhtasari wa shughuli za chuo au kampuni.

**prosper** /ˈprɒspə(r)/ *v.i.* sitawi; fanikiwa; pata heri. *God ~ you*, Mungu akujaze heri. **~ity** *n.* heri; baraka; usitawi; neema. **~ous** *adj.* -enye heri; -liofanikiwa; -a neema; enye usitawi.

**prostate** /ˈprɒsteɪt/ *n.* tezi shahawa: tezi ya homoni ya sehemu za kiume za uzazi wa mamalia zinazosaidia kuunda manii.

**prostitute** /ˈprɒstɪtjuːt/ *n.* malaya;

kahaba. *v.t.* tumia vibaya; fanya ukahaba. **prostitution** *n.* ukahaba; umalaya.
**prostrate** /'prɒstreɪt/ *adj.* kifudifudi. *v.t.* sujudu; nyenyekea; angusha chini. *trees ~d by the wind,* miti iliyoangushwa chini kwa upepo. *~ oneself,* sujudia; nyenyekea. *be ~d,* zimia; shindwa kabisa.
**prostration** /prɒ'streɪʃn/ *n.* unyong'onyevu; kusujudia; sijda.
**protease** /'prəʊtɪeɪz/ *n.* proteasi: kundi la vimeng'enya linaloweza kuzivunjavunja protini kuwa asidi amino au kinyume chake.
**protect** /prə'tekt/ *v.t.* linda; hifadhi; tunza; hami; zinga; kinga. **~ion** *n.* ulinzi; kinga; himaya. **~ive** *adv.* -a kuhifadhi; -a kukinga. **~or** *n.* mlinzi. **~orate** *n.* mahmiya.
**protein** /'prəʊti:n/ *n.* protini.
**protest** /'prəʊtest/ *n.* lalamiko. *v.t./i.* lalamika; pinga; kana; kataa. *do sth. under ~,* fanya jambo kwa kupinga. **~ant** *n./adj.* mprotestanti: mkristo asiyekubali baadhi ya mafundisho ya kanisa la Roma. **~antism** *n.* uprotestanti.
**proton** /'prəʊtɒn/ *n.* protoni: chembe yenye chaji chanya iliyo katika nyuklia ya atomu.
**protoplasm** /'prəʊtə(ʊ),plaz(ə)m/ *n.* protoplazimu: jina jumuishi la sehemu hai za seli ambamo umetaboli hufanyika.
**prototype** /'prəʊtətaɪp/ *n.* sampuli kifani; mfano wa awali.
**protozoa** /ˌprəʊtə'zəʊə/ *n.* protozoa: jina la kabila linalojumuisha viumbe vyenye seli moja na ambao wana nyuklia za kawaida.


**protractor**

**protract** /prə'trækt/ *v.t.* refusha; zidisha; endeleza. **~or** *n.* kipimapembe.
**protrude** /prə'tru:d/ *v.t./i.* toa nje; tokeza; chomoza. *~ the tongue,* toa ulimi. *a shelf protruding from the wall,* shubaka lililochomoza ukutani.
**proud** /praʊd/ *adj.* -a kiburi; -a kujivunia; -a fahari; -a maji-vuno. *~ of his success,* mwenye fahari juu ya kufanikiwa kwake. *He was too ~ to ask for help,* alijiona mno kiasi cha kutoomba msaada. *This is a ~ day for our nation,* hii ni siku ya fahari kwa taifa letu. *a ~ show,* tamasha zuri sana.
**prove** /pru:v/ *v.t./i.* thibitisha; hakikisha; bainika. *~ sb.'s guilt,* thibitisha kuwa ana hatia. *~ sb.'s worth,* bainisha ubora wa mtu. *The new clerk ~ed to be useless,* karani mpya alibainika kuwa hafai.
**proverb** /'prɒvɜ:b/ *n.* methali; mfano halisi. *He is a ~ for hypocracy,* ni mfano halisi wa unafiki. **~ial** *adj.* -a kufahamika sana; -a kutumika sana.
**provide** /prə'vaɪd/ *v.t./i.* toa; andaa; auni; kimu; taja; weka wazi. *~ for the children,* kimu watoto. *He ~ s his children with clothes,* awakatia nguo wanawe. *~ against,* jiweka tayari; jizatiti. **~d** *conj.* kwa sharti kwamba; mradi; alimradi.
**providing** /prə'vaɪdɪŋ/ *conj.* kwa sharti kwamba.
**Providence** /'prɒvɪdəns/ *n.* Mungu; majaliwa. **provident** *adj.* -enye busara; -a kuona mbele; -a kuweka akiba. *provident fund,* mfuko wa akiba ya uzeeni. **providential** *adj.* -a kudra; a bahati njema.
**provision** /prə'vɪʒn/ *n.* utoaji wa vitu kwa akiba; vitu vinavyotolewa; chakula; bidhaa; sharti. *make ~ for,* jitayarisha kwa baadaye.
**provisional** /prə'vɪʒənl/ *adj.* -a muda; -a kitambo. **provisionally** *adv.* kwa sharti; kwa muda.
**province** /'prɒvɪns/ *n.* jimbo; mkoa; uwanja wa kitaaluma. *the ~s,* mashamba. *the ~ of medicine,* uwanja wa tiba. *It is outside my ~,* si uwanja wangu; si kazi yangu. **provincial** *adj.* a jimbo; -mikoani; -enye mawazo finyu; mshamba.
**provoke** /prə'vəʊk/ *v.t.* kasirisha; chokoza; sababisha; chochea. **provocation** *n.* uchokozi; ushari; kitu kinachoudhi; kichocheo. **provocative** *adj.* -a kukasirisha; -a

kuchokoza. **provoking** *adj.* -a kuudhi.

**prow** /praʊ/ *n.* gubeti; omo.

**prowess** /'praʊəs/ *n.* ushujaa; uhodari; umahiri; ujasiri.

**prowl** /praʊl/ *v.i.* zungukazunguka (kama simba usiku).

**proximity** /'prɒk'sɪməti/ *n.* kuwa karibu; ujirani; upakanaji.

**prudent** /'pru:dnt/ *adj.* -enye busara; -angalifu; -a taratibu. **prudence** *n.* busara; hadhari; utaratibu; uwekevu. **~ly** *adv.* kwa hadhari; kwa busara.

**prune** /pru:n/ *n.* plamu kavu; mtu mjinga. *v.t.* pogoa matawi; kata; punguza.

**pry** /praɪ/ *v.i.* ~ *into,* chunguza; dadisi; peleleza; ulizia. *v.t.* banua; binua.

**psalm** /sɒ:m/ *n.* zaburi.

**pseudo** /'su:dəʊ/ *prefix* -a uwongo. **~nym** *n.* jina la bandia.

**psychiatry** /sʌɪ'kʌɪətri/ *n.* taaluma ya tiba juu ya magonjwa ya akili. **psychiatrist** *n.* mtaalamu wa magonjwa ya akili.

**psychic** /'sʌɪkɪk/ *adj.* -a akili.

**psychoanalysis**/,saɪkəʊə'næləsɪs/ *n.* taaluma ya tiba nafsia.

**psychology** /saɪ'kɒlədʒi/ *n.* saikolojia: elimu nafsia. **psychological** *adj.* -a saikolojia; -a kisaikolojia. **psychologist** *n.* mwanasaikolojia.

**pub** /pʌb/ *n. (colloq.)* bwalo; baa.

**puberty** /'pju:bəti/ *n.* baleghe: kipindi au umri ambao mtu anaweza kuzaa kijinsia.

**public** /'pʌblɪk/ *n.* watu, umma; kundi la watu. *adj.* -a serikali; -a watu wote; -a wananchi; -a umma. ~ *house,* kilabu; baa. ~ *school,* skuli ya serikali. ~ *spirit,* moyo wa kusaidia jamii. *the football-watching* ~, wapenzi wa mpira.

**publican** /'pʌblɪkən/ *n.* mwenye baa.

**publication** /,pʌblɪ'keɪʃn/ *n.* uchapishaji; uenezi; chapa.

**publicist** /'pʌblɪsɪst/ *n.* mwandishi habari; mwenezi habari.

**publicity** /pʌb'lɪsəti/ *n.* utangazaji; umaarufu; kuwa hadharani; uenezi wa habari. **publicly** *adv.* hadharani.

**publish** /'pʌblɪʃ/ *v.t.* tangaza; chapisha. **~er** *n.* mchapishaji.

**pudding** /'pʊdɪŋ/ *n.* pudini; aina ya soseji.

**puddle** /'pʌdl/ *n.* kidimbwi. *v.t.* ponda au kandika udongo. **~r** *n.* mkandikaji.

**puff** /pʌf/ *n.* mpumuo; uhemaji; tahakiki inayosifu kupita kiasi. *powder-~,* kipakazi poda. *v.i.* puliza; hema; tweta; sifu kupita kiasi; zima kwa kupuliza; vimbisha kwa hewa. *He ~ed at his pipe,* alivuta kiko kwa kutoa moshi kwa kishindo. *He ~ed out his chest with pride,* alivimbisha kifua chake kwa kiburi.

**puff-edder** *n.* aina ya nyoka kipilili; kifutu; bafe; moma. **~y** *adj.* -liofurafura; -a kutweta.

**pugnacious** /pʌg'neɪʃɪs/ *adj.* -gomvi; -piganaji.

**pugnacity** /pʌg'næsəti/ *n.* ushari.

**pull** /pʊl/ *n.* uvutaji; mvuto; nguvu ya kwenda dhidi ya mvuto; uwezo wa kushawishi; kishikizio. *v.t./i.* vuta; kokota; buruta; shua; ng'oa. ~ *sb. or sth. about,* tatua; tendea ubaya. ~ *sth. down,* bomoa. ~ *sb.down,* dhoofisha. ~ *sb. round,* saidia mgonjwa kupata nafuu. ~ *through,* fanikiwa; okoka. ~ *oneself together,* jizuia. ~ *up,* simamisha; simama. ~ *a face,* kunja uso. ~ *one's weight,* wajibika. ~ *sb.'s leg,* kejeli. *a ~ at a bottle,* kunywa katika chupa. **~-over** *n.* fulana nzito inayofunika sehemu ya juu ya kiwiliwili.


pulley

**pulley** /'pʊli/ *n.* roda.

**pulmonary artery** *n.* ateri mapafu: mshipa wa damu unaochukua damu isiyo na oksijeni kutoka kwenye moyo kuipeleka kwenye mapafu ili ipate oksijeni.

**pulmonary vein** *n.* vena mapafu: mshipa wa damu unaochukua

damu yenye oksijeni kutoka kwenye mapafu kuipeleka kwenye moyo ili isambazwe mwilini.

**pulp** /pʌlp/ *n.* nyama ya tunda bivu; kitu laini; mseto; ubao uliosagwa kutengenezea karatasi. *v.t.* seta; ponda.

**pulpit** /'pʊlpɪt/ *n.* mimbari.

**pulsate** /pʌl'seɪt/ *v.i.* pigapiga; puma; tuta; tutuma.

**pulse** /pʌls/ *n.* **1.** pigo la moyo; kipigo cha mshipa wa damu. **2.** jamii ya kunde. *v.i.* puma.

**pumice** /'pʌmɪs/ *n.* jabali volkano lenye tundu na viriba vingi vya hewa vilivyosababishwa na hewa iliyotanuka katika lava.

**pump** /pʌmp/ *n.* pampu: bomba ya kuvutia maji au mafuta; chombo cha kujazia upepo. *v.t./i.* vuta kwa bomba; jaza upepo; sukuma.

**pumpkin** /'pʌmpkɪn/ *n.* mboga; boga.

**punch** /pʌntʃ/ *n.* **1.** panchi: chombo cha kutobolea. **2.** pigo la ngumi. *v.t.* **1.** toboa kwa panchi. **2.** piga ngumi.

**punctilious** /pʌŋ(k)'tɪlɪəs/ *adj.* -enye kushikilia itifaki.

**punctual** /'pʌŋ(k)tʃʊəl/ *adj.* siochelewa; -a wakati upasao. **~ity** *n.* hali ya kutochelewa. **~ly** *adv.* bila kuchelewa.

**punctuate** /'pʌŋ(k)tʃʊeɪt, -tjʊ-/ *v.t.* weka vituo katika kuandika; ingilia mara kwa mara. *His speech was ~d with cheers,* maneno yake yalidakizwa mara kwa mara kwa vifijo. **punctuation** *n.* uwekaji vituo katika maandishi; kituo. *~ marks,* alama za vituo.

**puncture** /'pʌŋktʃə(r)/ *n.* pancha. *v.t.* toboa; toka upepo; pata pancha.

**punish** /'pʌnɪʃ/ *v.t.* adhibu; tia adabu; rudi. **~ment** *n.* adabu; adhabu; rada. **capital ~**, adhabu ya kifo.

**pup** /pʌp/ *n.* mbwa mchanga.

**pupa** /'pju:pə/ *n.* (**pupae**) pupa: hatua ya mwisho katika metamofosisi ya mdudu kabla hajageuka kiumbe kamili.

**pupil** /'pju:pl/ *n.* mwanafunzi; mboni ya jicho.

**puppet** /'pʌpɪt/ *n.* karagosi; kibaraka. **~ state**, dola kibaraka.

**puppy** /'pʌpi/ *n.* mbwa mchanga.

**purchase** /'pɜ:tʃes/ *n.* ununuzi; kitu kilichonunuliwa; thamani. *v.t.* nunua.

**pure** /'pjʊə(r)/ *adj.* tupu; tu; safi; menyu; halisi; kwa ajili ya nadharia tu. **~ water**, maji safi. *~ nonsense,* upuuzi mtupu. *a ~ accident,* bahati mbaya tu. **~ly** *adv.* kabisa. **~ness** *n.* usafi.

**purity** /'pjʊərəti/ *n.* usafi; utakatifu; tohara.

**purify** /'pjʊərɪfaɪ/ *v.t.* takasa; safisha; chuja; toharisha. **purification** *n.* tohara.

**purgative** /'pə:gətɪv/ *n./adj.* haluli; -a kuharisha.

**purgatory** /'pə:gət(ə)ri/ *n.* mahali pa mateso ya muda ahera; utakaso.

**purge** /'pɜɪdʒ/ *n.* kuharisha; haluli. *v.t.* takasa; safisha; harisha (tumbo).

**purple** /'pɜ:pl/ *n./adj.* rangi ya zambarau; vazi la kadinali; vazi la kifalme.

**purpose** /'pɜ:pəs/ *n.* azma; nia; kusudio; matilaba. *on ~,* makusudi. *to little (no) ~,* bure. *to the ~,* -a kufaa. *v.t./i.* kusudia; azimia. **~ful** *adj.* enye nia.

**purse** /pɜ:s/ *n.* pochi; mkwiji. *hold the ~ strings,* dhibiti matumizi.

**pursue** /pə'sju:/ *v.t.* fuatilia; winda; shikilia; ganda; andama; saka; endelea na.

**pursuit** /pə'sju:t/ *n.* ufuatiliaji; ukimbizaji; kazi; shughuli. *He is engaged in literary ~s,* anashughulikia uandishi.

**pus** /pʌs/ *n.* usaha.

**push** /pʊʃ/ *n.* msukumo; bidii; tendo la kujiendeleza. *v.t.* sukuma; himiza; uza madawa ya kulevya; bonyeza. *~ on,* endelea. *be ~ed for time,* pata shida. *at a ~,* ikibidi; ikilazimu.

**puss** /pʊs/ *n.* paka.

**put** /pʊt/ *v.t.* (**put**) tia; weka; jiweka; pachika; wekea; athiri maendeleo; sababisha; kadiria; tupa. *be much ~*

*about*, fadhaika; udhika. ~ *across*, ~ *sth. away*, ondosha. ~ *sth. back*, rudisha. ~ *by*, weka akiba. ~ *down*, andika; komesha. ~ *down as*, dhania; hesabu; fikiria. ~ *forth*, toa. ~ *forward*, pendekeza. ~ *in for sth.*, leta maombi rasmi. ~ *in an appearance*, hudhuria. ~ *off*, ahirisha; vua. ~ *sb. off*, ahirisha mpango wa. ~ *sb. off his game*, sitisha. ~ *sb. off his food*, poteza ladha ya. ~ *on*, ulaghai; ongeza bei. ~ *out*, zima. ~ *sth. through*, kamilisha; fanikisha. ~ *up*, toa hoja; panga. ~ *up a fight*, shindwa. ~ *sb. up to sth.*, chochea. ~ *up with*, vumilia. ~ *an end to*, komesha. *be hard ~ to it*, wia ugumu. ~ *to death*, ua. ~ *sb. in mind of*, kumbusha. ~ *sb. in the wrong*, fanya aonekane mkosa. ~ *sth. in hand*, anzisha.

**putty** /'pʌti/ *n.* puti: aina ya gundi ngumu.

**puzzle** /'pʌzl/ *n.* fumbo; chemshabongo; kitendawili; mkanganyiko. *v.t.* kanganya. ~ *sth. out*, jaribu kupata ufumbuzi wa jambo.

**pygmy** /'pɪgmi/ *n.* mbilikimo; mbirikimo.

**pyjamas** /pə'dʒɑːməz/ *n.* pajama: nguo za kulalia.

**pylon** /'paɪlən/ *n.* pailoni: nguzo za umeme.

**pyramid** /'pɪrəmɪd/ *n.* piramidi. **~ of biomass**, piramidi biomasi: mchoro unaoonesha uwiano wa jumla wa masi ya viumbe hai katika kila ngazi ya mtungo wa chakula. **~ of numbers**, piramidi ya nambari: mchoro unaoonyesha uwiano wa jumla wa idadi ya viumbe hai katika kila ngazi ya mtungo wa chakula.

**python** /'paɪθən/ *n.* chatu.

# Q

**quadrangle** /kwɒdræŋgl/ *n.* umbo lenye pande nne na pembe nne; behewa kati ya nyumba; uwanja uliozungukwa na nyumba pande zote.

**quadratic** /kwɒ'dratɪk/ *adj.* -a mraba. **~ equation**, hesabu ya kipawa cha pili.

**quadrilateral** /ˌkwɒdrɪ'lætərəl/ *n.* -a pembe nne.

**quadruped** /'kwɒdrʊpɛd/ *n.* mnyama wa miguu minne.

**quadruple** /'kwɒdrʊp(ə)l/ *n.* mara nne. *adj.* -a sehemu nne; -enye kukubaliwa na pande nne. **~t** *n.* mmoja wa mapacha wanne.



quadrilaterals

**quail** /kweɪl/ *n.* tomboro: ndege mdogo kama kwale. *v.t.* jikunyata kwa hofu; tetema kwa hofu.

**quake** /kweɪk/ *v.i.* tetemeka. *earth ~*, tetemeko la ardhi.

**Quaker** /'kweɪkə(r)/ *n.* madhehebu ya kikristo yanayofuata misingi ya amani na urafiki.

**qualify** /'kwɒlɪfaɪ/ *v.t./i.* stahilisha; stahili; wekea mipaka; pambanua; *(grammar)* vumisha. **qualification** *n.* sifa; tabia; kikwazo; mipaka; sharti; uwezo. *a doctor's qualifications*, sifa za kuwa daktari.

**qualified** /'kwɒlɪfaɪd/ *adj.* enye sifa zinazostahili.

**qualifier** /'kwɒlɪfaɪə(r)/ *n.* kivumishi; sharti.

**quality** /'kwɒləti/ *n.* sifa; tabia; aina; ubora; jinsi.

**qualm** /kwɑːm/ *n.* shaka; wasiwasi; kubirukwa na tumbo.

**quantify** /'kwɒntɪfaɪ/ *v.t.* pima, eleza kiasi cha.

**quantity** /'kwɒntəti/ *n.* kiasi; kadiri; kima; wingi; idadi. *an unknown ~*, mtu (au kitu) asiyetabirika; alama ya hesabu ionyeshayo idadi

isiyofahamika.

**quantum** /'kwɒntəm/ *n.* kiasi; kinachotakiwa; kwanta: namba za kwanta. **~ mechanics**, umakanika wa kwanta. **~ numbers**, namba za kwanta. **~ theory**, nadharia ya kwanta: nadharia inayoeleza tabia za mata na mnururiko kwa kutumia dhana ya kwanta.

**quarantine** /'kwɒrənti:n/ *n.* karantini.

**quark** /kwɑ:k/ *n.* kwaki: moja kati ya chembe sita za msingi zinazosadikiwa kujenga protoni na nyutroni.

**quarrel** /'kwɒrəl/ *n.* ugomvi; utesi; mzozo; kisa cha ugomvi. *v.i.* gombana. **~some** *adj.* gomvi.

**quarry** /'kwɒri/ *n.* kware; machimbo; karakana ya mawe.

**quart** /kwɔ:t/ *n.* kwati: kipimo cha ujazo cha painti mbili; robo galoni.

**quarter** /'kwɔ:tə(r)/ *n.* robo; kiga cha mnyama; upande; mtaa; makazi. *a ~ of mutton*, kiga cha kondoo. *Men ran from all ~s*, watu walikimbia kutoka pande zote. *at close ~s*, karibu sana. *v.t.* gawa sehemu nne; -pa malazi. **~ day** *n.* siku ya mwisho ya robo mwaka. **~deck** *n.* shetri; sitaha ya nyuma. **~ly** *adj.* -a kila miezi mitatu. *n.* jarida litokalo kila miezi mitatu. **~master** *n.* msimamizi ugavi; sarahangi; baharia msimamizi.

**quartile** /'kwɔ:tʌɪl/ *n.* mojawapo ya sehemu ambamo data ya takwimu imegawiwa kupata mafungu manne sawa.

**quartz** /kwɔ:ts/ *n.* kwazi: silika ya kiasili ya kifuwele; namna ya jiwe gumu jeupe la kung'aa.

**quasar** /'kweɪzɑ:, -sɑ:/ *n.* kitu kama nyota ambacho ndicho chanzo cha mawimbi ya sumakuumeme; mawimbi; mwanga wa radio ya mbali sana.

**quay** /ki:/ *n.* gati; liko; diko.

**QED** *n.* ufupisho wa **quod erat demonstrandum**: kilichotakiwa kuthibitishwa.

**queen** /kwi:n/ *n.* mke wa mfalme; malkia. **~ly** *adj.* -a malkia; kimalkia.

**queer** /kwiə(r)/ *adj.* -geni; -enye kutia wasiwasi. *v.t. (colloq.)* haribu; potosha.

**quell** /kwel/ *v.t.* komesha; zuia; tuliza; nyamazisha.

**quench** /kwentʃ/ *v.t.* zima; zimisha; poza chuma. *~ thirst*, kata kiu. *~ hope*, ondoa matumaini.

**query** /'kwɪeri/ *n.* swali; alama ya kuuliza. *v.t.* taka maelezo zaidi juu ya jambo; saili.

**question** /'kwestʃən/ *n.* swali; suala; mada. *It is out of the ~*, haiwezekani. *It is only a ~ of time*, ni suala la wakati tu. *beyond ~*, hakika; hakika. *call in ~*, zungumzia; jadili juu ya *v.t./i.* uliza; hoji; saili; -a na shaka. *~ whether*, uliza ikiwa. **~able** *adj.* -a mashaka; si hakika. **~mark** *n.* alama hii (?). **~naire** *n.* orodha ya maswali.

**queue** /kju:/ *n.* foleni; msururu; msuko wa nywele wa mkia.

**quibble** /'kwɪbl/ *n.* ukwepaji wa swala. *v.i.* piga chenga swala kwa kuzungumza jambo lingine.

**quick** /kwɪk/ *n.* nyama chini ya kucha. *-adj.* -epesi; hodari; -elekevu; -enye akili. *~ to understand*, -epesi wa kufahamu; *~-witted*, -erevu. *~ to take offence*, -epesi wa kuudhika. *~-tempered*, -epesi wa hasira. *the ~ and the dead*, wazima kwa wafu. *(fig.) It touched him to the ~*, -limchoma moyoni. **~ly** *adv.* haraka; upesi. **~ness** *n.* wepesi. **~en** *v.t./i.* himiza; chochea; sisimua; ongeza mwendo. **~lime** *n.* chokaa mbichi. **~sand** *n.* mchanga wa kutopeza. **~silver** *n.* zebaki.

**quiet** /'kwaɪət/ *n.* utulivu; kimya. *adj.* -tulivu; kimya; -a siri. *an hour's ~*, saa moja ya kimya. **~ly** *adv.* kimya; kimyakimya; taratibu. **~ness** *n.* kimya; utulivu.

**quinine** /'kwɪni:n/ *n.* kwinini.

**quit** /kwɪt/ *v.t./i.* (**-tt**, **~ted**, **quit**). acha; achilia; ondoka; ondosha. *They ~ted themselves like men*, waliondoka kiume. *adj.* -lioachiliwa; -lioondokana na. *be ~s*, ridhiana; patana.

**quite** /kwaɪt/ *adv.* kabisa; kamwe; hasa. *He is ~blind*, yu kipofu. *It is ~*

*cool to day*, baridi imekolea kidogo leo. ~ *so*, ndivyo hasa.

**quiver** /'kwɪvə(r)/ *n.* mtetemeko. *v.i.* tetemeka; tikisika; mfumo wa kutunzia mishale.

**quiz** /kwɪz/ *n.* chemsha bongo; fumbo; jaribio la maswali; mtihani mdogo. *v.t.* uliza maswali ya mtihani; dhihaki; chokoza. **~zical** *adj.* -tani; -chokozi.

**quota** /'kwəʊtə/ *n.* sehemu ya haki iliyopasa; idadi ya kikomo; kiasi kilichopasa.

**quotation** /kwəʊ'teɪʃn/ / *n.* kidondoa; dondoo. **~ marks**, alama za madondoo.

**quote** /kwəʊt/ *v.t.* dondoa; tumia maneno ya; toa maneno kushuhudia; taja.

**quotient** /'kwəʊʃ(ə)nt/ *n.* mgao; hisa.

## Rr

**rabbi** /'rɑbʌɪ/ *n.* rabi: mwalimu au kiongozi wa dini ya Kiyahudi.

**rabbit** /ræbɪt/ *n.* sungura.

**rabble** /'ræbl/ *n.* watu wengi wenye ghasia.

**rabies** /'reɪbi:z/ *n.* kichaa cha mbwa.

**rabid** /'rɑbɪd/ *adj.* -enye kichaa cha mbwa.

**race**[1] /reɪs/ *n.* shindano la mbio: mkondo wa maji wa kasi. *v.i.* shindana mbio. ~ *against time*, kimbilia wakati. *v.t.* shindanisha mbio; endesha kwa kasi. **racing** *n.* mashindano ya mbio ya farasi. **~course** *n.* uwanja wa mbio za farasi. **~horse** *n.* farasi wa mbio.

**race**[2] /reɪs/ *n.* kabila.

**racial** /'reɪʃl/ *adj.* -a kabila; -a kikabila au rangi. **racial discrimination**, ubaguzi wa kikabila. **racial segregation**, ubaguzi wa kikabila.

**rack** /ræk/ *n.* uchaga; chanja; shubaka la kuwekea mizigo ndani ya basi; kitanda cha kutesea. *v.t.* tesa; nyanyasa. *He was ~ed with grief*, aliteswa na majonzi. ~ *one's brains*, fikiri sana; tafakari.

**racket** /'rækɪt/ *n.* ghasia; makelele; utapeli. **~eer** *n.* mlanguzi; tapeli.

**racket**, **racquet** /'rækɪt/ *n.* raketi; kiatu cha kutelezea kwenye theluji.

**radar** /'reɪdɑ:(r)/ *n.* rada: chombo cha kuvuta sura za viumbe vinavyokaribia katika eneo.

**radial** /'reɪdiəl/ *adj.* -a miali au -a nusu kipenyo.

**radiance** /'reɪdiəns/ *n.* mwanga; wangavu; uzuri; nuru.

**radiant** /reɪdiənt/ *adj.* angavu; -a kung'aa; ng'avu; -enye kupeleka miali ya mwanga; -enye uso wa furaha; -enye kusafirishwa kwa miali.

**radiate** /'reɪdieɪt/ *v.t./i.* sambaa kama nusuvipenyo; nururisha; onyesha furaha; toka, tokeza pande zote kama miali.

**radiation** /ˌreɪdi'eɪʃn/ *n.* mnuru risho.

**radiator** /'reɪdietə(r)/ *n.* rejeta.

**radio** /'reɪdieʊ/ *n.* simu ya upepo; redio; matangazo ya redio. **~ link**, mtandao wa matangazo ya redio. **~ telescope**, darubini ya kuchunguzia viumbe vya angani. *v.t./i.* peleka kwa simu ya upepo.

**radio-** /'reɪdieʊ/ *prefix* -a miali; -a radiamu.

**radioactive** /ˌreɪdieʊ'æktɪv/ *adj.* -enye uwezo wa kunururisha; nururishi. **~ dating**, upimaji tarehe nururishi: ukisiaji wa umri wa dutu oganiki yenye kaboni kwa kupima kima cha isotopuredio ya kaboni -14 katika dutu hiyo. **~ waste**, taka nururishi: mabaki ya dutu nururishi.

**radioactivity** /ˌreɪdieʊæk'tɪvəti/ *n.* chembe alfa au chembe beta za mnururisho; unururifu. **radio astronomy**, unajimuredio: mtaala wa magimba kwenye ulimwengu na matukio yake kwa kutumia njia

ya ishara za redio. **radio-isotope**, isotopuredio: isotopu ya elementi ambayo ni rediotendaji. **radio wave**, wimbi redio: wimbi la sumakuumeme linalotumiwa na mbembeo wa chaji ya umeme na kubadilishwa kuwa sauti kwenye chombo cha kupokelea.

**radium** /'reɪdɪəm/ *n.* radiamu: madini ya thamani kubwa yenye kutoa nuru na nguvu za umeme. **~therapy** *n.* terapia radiamu: miali inayotumika kutibu maradhi kama saratani.

**radius** /'reɪdɪəs/ *n.* (**radii**) nusu kipenyo.

**raffia** /'ræfiə/ *n.* chane kama za ukindu; mwale; mbale.

**raffle** /'ræfl/ *n.* bahati nasibu. *v.t.* piga kura kwa fedha.

**raft** /rɑ:ft/ *n.* chelezo; boya.

**rafter** /'rɑ:ftə(r)/ *n.* kombamoyo; pau.

**rag** /rɑg/ *n.* tambara; chepe. **~ged** /'rægɪd/ *adj.* -iorarukа; -enye umbo au upande usio sawa.

**rage** /reɪdʒ/ *n.* hasira kali; ghadhabu; uchu. *suits are all the ~*, watu wote hutamani suti. *v.i.* kasirika; ghadhibika; (kwa tufani, etc.) chafuka.

**raid** /reɪd/ *n.* shambulio la ghafla la vita; uvamizi wa polisi. *v.t./i.* shambulia; pora; vamia.

**rail** /reɪl/ *n.* chanja za kitalu; mwanjo; reli. *go off the ~s*, toka katika njia; *(fig.)* pata wazimu; enda kombo. *v.t.* safirisha kwa reli. **~ing** (**s**) *n.* papi za kitalu. **~road**, **~way** *n.* njia ya reli.



railing

**rain** /reɪn/ *n.* mvua. *long ~s*, masika. *v.i.* nya, nyesha; tiririka. *v.t.* toa kwa wingi. **~bow** *n.* upinde wa mvua. **~fall** *n.* kiasi cha mvua; mvua. **~forest** *n.* msitumvua: jamii muhimu ya kibiolojia ya mimea ambayo ni chanzo kikuu cha mvua. **~gauge** *n.* kipimamvua. **~proof** *adj.* siopenywa na mvua. **~ shadow**, kingamvua: sehemu kavu upande wa pili wa mlima inayokingwa na pepo zenye kuleta mawingu ya mvua. **~y** *adj.* -a mvua nyingi. *save for a ~ day*, weka akiba kwa siku za shida.

**raise** /reɪz/ *n.* nyongeza. *-v.t.* inua; kweza; pandisha; sababisha; leta mjadala; otesha; fuga; lea; changa; kuza. *The motorcars ~ed the dust*, gari zilitifua vumbi. *~ a new point*, leta wazo jipya. *~ a question*, uliza swali. *~ an army*, unda jeshi. *~ a loan*, kopa fedha. *~ a siege*, komesha uzingiaji.

**rake** /reɪk/ *n.* reki: kifaa chenye mpini na meno kitumikacho katika bustani. *v.t./i.* zoa au sawazisha kwa reki. *~ through*, tafuta kwa bidii. *~ sth. up*, fufua; fichua.



rake

**rally** /'ræli/ *n.* mkusanyiko wa watu; mashindano ya magari. *v.t.* kusanya tena; unga mkono. *v.i.* kusanyika tena.

**ram** /ræm/ *n.* kondoo dume; mtambo wa kubomolea. *v.t.* (**-mm**) shindilia; piga kwa nguvu.

**RAM** /ræm/ *n.* ufupisho wa **random access memory**: kumbukumbu ya fikio nasibu (KUFINA): kumbukumbu ambazo mfumo wa uendeshaji diski (MUDI) katika kompyuta huhifadhi programu na data kwa muda.



ram

**random** /'rændəm/ *n. at ~*, bila taratibu; ovyo.

**range** /reɪndʒ/ *n.* safu ya milima; uwanja wa shabaha; masafa ya risasi au mzinga; masafa ya sauti kusikika; eneo; mawanda; eneo la kuchungia. *out of rifle ~*, nje ya masafa ya risasi. *at shot ~*, kwa karibu. *at long ~*, kwa mbali. *a wide ~ of prices*, bei anuwai. *a wide ~ of colours*, rangi anuwai. *the annual ~ of temperature*, kima cha vipimo vya hali ya hewa vya mwaka. *v.t.* panga; enea; fikia. *~ oneself*, jitia.

*man who ~d themselves on the side of the rebels,* watu waliojitia upande wa waasi. **~finder** *n.* kitafuta umbali.

**rank** /ræŋk/ *n.* safu; safu ya askari; cheo; daraja; tabaka; kiwango. *other ~s,* askari wasio maafisa. *He was promoted to the ~ of sergeant,* alipandishwa cheo cha usajini. *v.t.* weka; panga. *v.i.* wekwa; pangwa.

**ransom** /rænsəm/ *n.* kikomboleo; fidia. *v.t.* komboa; fidia.

**rap** /ræp/ *v.t./i.* (**-pp-**) bisha; ropoka; gonga; piga kibao; gota. *~ sth. out,* sema kwa ghafla au kwa ukali.

**rape** /reɪp/ *n.* ubakaji; uporaji. *v.t.* baka; pora. **rapist** *n.* mbakaji.

**rapid** /'ræpɪd/ *n.* maporomoko; mkondo mkali. *adj.* -epesi; -a kasi. **~ity** *n.* hima; wepesi; haraka. **~ly** *adv.* hima; kwa haraka.

**rare** /reə(r)/ *adj.* adimu; -sio na kifani; -sio ya kawaida. **~ly** *adv.* mara chache. *the ~fied air of the mountain tops,* hewa haba ya vilele vya milima. **rarefaction**, mtanzuko; uchechefushaji: upunguzaji wa kanieneo. **~ gas**, gesi adimu: kundi la elementi sita (heli, neoni, arigoni, kriptoni, zenoni, na radoni) zilizomo kwenye kundi la sifuri mrudio.

**rarity** /'reərəti/ *n.* uadimifu; tunu.

**rash** /ræʃ/ *adj.* ukurutu; upele.

**rat** /ræt/ *n.* panya.

**rate** /reɪt/ *n.* kima; kiasi; daraja. *at this ~,* kwa kiwango hiki. *at any ~,* kwa vyovyote vile. *first ~,* bora kabisa. *~ of reaction,* kasi tendanaji: kasi ambayo utendanaji kikemikali hufikia ukomo. *v.t./i.* tathmini; kadiria.

**rather** /'rɑ:ðə(r)/ *adv.* kidogo; kiasi; heri; afadhali. *He is ~ better,* hajambo kidogo. *I would ~ do this than that,* heri nifanye hivi kuliko vile. *yes ~!* hakika!

**ratify** /'rætɪfaɪ/ *v.t.* ridhia; idhinisha; thibitisha. **ratification** *n.* idhini; ridhaa; uthibitisho; uhakikisho.

**ratio** /'reɪʃiəʊ/ *n.* uwiano.

**ration** /'ræʃn/ *n.* resheni; mgao; posho. *v.t.* gawa.

**rational** /'ræʃnəl/ *adj.* -kimantiki; -a kirazini; razini; -a uwiano.

**rattle** /'rætl/ *n.* mtatariko; mtataliko; kayamba; manyanga; ubwataji. *v.t./i.* tatarisha; tatarika; tatalika; sema upesi upesi.

**rave** /reɪv/ *v.i.* payuka. *~ about,* sifu sana bila kufikiri.

**ravenous** *adj.* -enye njaa kuu.

**ravine** /rə'vi:n/ *n.* bonde; korongo.

**raw** /rɔ:/ *adj.* -bichi; ghafi; -sio na uzoefu; -enye unyevu; changa. **~ materials**, mali ghafi. *~ recruit,* askari kuruta. *~ weather,* baridi tena yenye unyevu.

**ray** /reɪ/ *n.* mwonzi; mstari utokao kwenye kitovu cha kitu.

**razor** /'reɪzə(r)/ *n.* wembe.

**re**$^1$ /reɪ/ *prep.* juu ya; mintarafu; kuhusu.

**re-**$^2$ /reɪ/ *prefix* tena; kwa namna nyingine.

**reach** /ri:tʃ/ *n.* uwezo wa kufikia; mnyoosho wa mkono. *v.t./i.* nyoosha mkono; fika hadi; fikia. *as far as the eye can ~,* upeo wa macho.

**react** /ri'ækt/ *v.t./i.* onyesha hisia; athiri; pinga; kataa. jibu; tendana. *Children ~ to kind treatment by becoming more confident,* watoto huwa jasiri kwa upole. *~ against,* pinga; kataa. **~ion** *n.* jibutiko; mmenyuko; jibu; athari; upingaji; utendanaji. **~ionary** *adj.* mpinga maendeleo; -a kupinga maendeleo. **~ivity series**, jadweli tendanaji: jadweli ambayo huonyesha mpangilio wa nguvu za utendanaji wa elementi mbalimbali.

**read** /ri:d/ *v.t./i.* (**read**) /red/ soma; jifunza. *The book ~ s well,* kitabu kizuri. *~ between the lines,* tambua maana iliyojificha. *He was having a quiet ~,* alikuwa anasoma kimyakimya. **~able** *adj.* enye kusomeka. **~er** *n.* msomaji; kitabu cha kiada; profesa mshiriki; mfasiri. **~ing** *n.* usomaji; maarifa ya vitabuni; kipimo. *the ~ings on the thermometer last month,* kipimo cha joto mwezi uliopita.

**ready** /'redi/ *adj.* tayari; -a upesi; -

enye kupatikana kwa urahisi; liokwisha tayarishwa. *he always has a ~ ~ answer,* ni mwepesi wa kujibu. ~ *money,* fedha taslimu. ~ *reckoner,* kitabu cha mikokotoo muhimu. ~ *made,* ntungulie; tayari kutumika. **readily** *adv.* bila shida; bila kusita; bila wasiwasi. **readiness** *n.* utayari; ukubalifu; wepesi; haraka.

**reagent** /ri'eɪdʒ(ə)nt/ *n.* kitendanishi: dutu ya kikemikali inayosababisha au kuleta utendanaji wa kikemikali.

**real** /ri:l/ *adj.* -a kweli; halisi. *(law)* ~ *property, estate,* mali isiyohamishika. ~ *image,* taswira halisi: taswira inayotokana na mkutano wa miali ya kweli ambayo huweza kutupwa kwenye kiwambo. **~ism** *n.* uhalisia. **~istic** *adj.* -a kweli; -enye uhalisi; -enye kuwezekana. **~ity** *n.* hali ya kuwa kweli; uhalisi; hakika; ukweli. *in ~* , kwa kweli. **~ly** *adv.* kwa kweli.

**realize** /'ri:əlaɪz/ *v.t.* elewa; tambua; limka; fanikisha; pata faida au bei; badilisha mali kwa fedha.

**realization** /ˌri:əlaɪ'zeɪʃn/ *n.* utambuzi; matunda; matokeo; ubadilishanaji mali kwa fedha.

**ream** /ri:m/ *n.* rimu: karatasi takriban 500 za kuandikia zilizofungwa katika robota moja.

**reap** /ri:p/ *v.t./i.* vuna; chuma; pata; pewa. **~er** *n.* mvunaji. **~ing-hook** *n.* mundu; mndu.

**rear**[1] /rɪə(r)/ *n.* nyuma.

**rear**[2] /rɪə(r)/ *v.t./i.* fuga; chunga; lea; (kwa farasi) simama kwa miguu ya nyuma; inua (kichwa); jenga; simamisha

**reason** /'ri:zn/ *n.* sababu; akili; mantiki; urazini; kweli; maana; madhumuni. *it stands to ~ that,* imebainika kuwa. *do anything in ~,* fanya chochote chenye maana au cha kiasi. *v.i/t.* tumia akili; waza; fikiri; jenga hoja. ~ *sb. into doing sth.,* shawishi. ~ *sth. out,* fikiri kimantiki. **~able** *adj.* -enye akili; -a akili; -a maana; tayari kusikia hoja; -a kutosha; -a kiasi. **~ably** *adv.* kwa kiasi; kimantiki.

**reassure** /ˌri:ə'ʃʊə(r)/ *v.t.* ondolea mashaka; thibitishia; tuliza; pa moyo; poza.

**rebate** /'ri:beɪt/ *n.* nafuu ya bei kwa kulipa fedha taslimu.

**rebel** /'rɛb(ə)l/ *n.* mwasi. *v.i.* (**-ll-**) asi; kataa. **~lion** *n.* maasi; uasi. **~lious** *adj.* -asi; -kaidi.

**rebound** /rɪ'baʊnd/ *n.* mduto. *v.i.* duta; rudi nyuma.

**recall** /rɪ'kɔ:l/ *v.t.* kumbuka; tangua; batilisha; ita tena. *beyond ~,* sioweza kurudi; -siofanyika tena; -siobatilika.

**recapitulate** /ˌri:kə'pɪtjʊleɪt/ *v.t./i.* eleza tena.

**recapitulation** /ˌri:kəpɪtjʊ'leɪʃ(ə)n/ *n.* muhtasari; ufupisho.

**recede** /rɪ'si:d/ *v.i.* enda nyuma; rudi; pungua. ~ *from view,* tokomea.

**receipt** /rɪ'si:t/ *n.* risiti; stakabadhi; upokeaji; mapato; maduhuli. *On ~ of the news he went,* alipopata habari alikwenda. *The ~s of the business increased,* mapato ya biashara yaliongezeka.

**receive** /rɪ'si:v/ *v.t./i.* pokea; karibisha; pata. **~d** *adj.* -liokubaliwa. **~r** *n.* mpokeaji; mkono wa simu.

**receiving-set** *n.* redio.

**reception** /rɪ'sepʃn/ *n.* mapokezi; mlahaka; makaribisho; tafrija; kusikika kwa redio. *Is radio reception good in your town?* Je redio husikika vizuri mjini kwenu? *a reception desk,* mapokezi.

**receptive** /rɪ'septɪv/ *adj.* sikivu; -epesi kupokea ushauri.

**receptor** /rɪ'sɛptə/ *n.* kipokezi: ogani yenye tishu za neva ambazo huitikia kwa kiamshi maalumu.

**recent** /'rɪ'snt/ *adj.* -a karibuni; -ya siku hizi; -pya. **~ly** *adv.* karibuni; juzijuzi.

**recess** /rɪ'sɛs, 'ri:sɛs/ *n.* muda wa mapumziko; mahali pa ndani; shubaka. **~ion** *n.* kushuka kwa uchumi; kurudi nyuma. **recessive gene,** jeni tawaliwa: jeni ambayo hutawaliwa na jeni tawala na

hivyo athari yake ni kuwa dhaifu katika urithi wa tabia katika viumbe hai.

**recipe** /'resɪpi/ *n.* maelezo ya mapishi; maelezo ya kufanya jambo.

**recipient** /rɪ'sɪpiənt/ *n.* mwenye kupokea.

**reciprocal** /ri'sɪprək(ə)l/ *adj.* -a kubadilishana; -a kupeana; -a wao kwa wao; -a kukubaliana; -a kutendana; -a kutendeana. ~ *help,* kusaidiana. **reciprocate** *v.t./i.* peana; tendana; lipa; rudisha; enda mbele na nyuma.

**recite** /rɪ'saɪt/ *v.t./i.* tongoa; ghani; kariri; soma kwa ghibu; orodhesha; simulia. **recital** *n.* masimulizi; kughani. **recitation** *n.* masimulizi; mashairi yasimuliwayo.

**reckon** /'rekən/ *v.t./i.* hesabu. ~ *up,* jumlisha. ~ *in,* ingiza katika jumla. ~ *with,* fikiria; zingatia; shughulikia; ~ *upon,* tegemea; tumainia. **~ing** *n.* **1.** orodha ya madeni ya hoteli. *day of ~ing.* **2.** siku ya kiyama. *be out of one's ~ing,* potea.

**reclaim** /rɪ'kleɪm/ *v.t.* ongoa; hidi; dai kitu kirudishwe; rudisha katika hali nzuri. *The desert was ~ed by hard work,* jangwa lilirudishwa katika hali ya kulimika kwa juhudi kubwa. **reclamation** *n.* urudishaji; uongoaji.

**recline** /rɪ'klaɪn/ *v.i.* inama; lala; jinyoosha; egemea.

**recognize** /'rekəgnaɪz/ *v.t.* jua; tambua; maizi; fahamu; ungama; kiri; kubali. *I ~ that man,* namtambua mtu yule. *They ~ the present government,* wanai tambua serikali iliyopo. *He ~d that he was unable to run as fast as he used to do,* alimaizi kuwa hawezi kukimbia kwa kasi kama zamani. *He ~d the danger of the journey,* alikubali kuwa safari ilikuwa na hatari. *His long years of service have been ~d,* kazi yake ya miaka mingi imetambuliwa. **recognition** *n.* utambuzi; kukiri.

**recoil** /rɪ'kɔɪl/ *v.i.* rudi nyuma; jivuta nyuma; nywea; sita; kimbia.

**recollect** /ˌrɛkə'lɛkt/ *v.t./i.* kumbuka. **~ion** *n.* kumbukumbu; jambo lililokumbukwa.

**recommend** /ˌrekə'mend/ *v.t.* sifu; pendekeza; shauri; nasihi. **~ation** *n.* sifa; upendekezaji; pendekezo.

**reconcile** /'rɛk(ə)nsʌɪl/ *v.t.* patanisha; suluhisha; linganisha. ~ *sb.'s statement with the facts,* linganisha maneno ya mtu na mambo yalivyo. ~ *oneself to sth.,* vumilia; ridhia. **reconciliation** *n.* suluhu; upatanishi.

**record** /'rekɔ:d/ *n.* rekodi; kumbukumbu; taarifa iliyo-andikwa; sahani ya santuri; ushahidi; sifa. *v.t.* andika; rekodi; onyesha. *What temperature does the thermometer ~?* kipimajoto kinaonyesha kiasi gani? *a man with a good ~,* mtu mwenye sifa nzuri. *break the ~,* vunja rekodi.

**recount**[1] /rɪ'kaʊnt/ *v.t.* simulia; eleza.

**recount**[2] /ri:kaʊnt/ *n.* hesabu ya mara ya pili. *v.t./n.* hesabu mara ya pili.

**recover** /rɪ'kʌvə(r)/ *v.t.* pata tena; pona; pata nafuu; pona. **~y** *n.* nafuu; upatikanaji tena.

**recreation** /ˌrɛkrɪ'eɪʃ(ə)n/ *n.* burudani; mapumziko.

**recruit** /rɪ'kru:t/ *n.* mwanachama mpya; kuruta. *v.t/i.* andikisha. ~ *one's strength,* jiburudisha; pumzika. **~ment** *n.* uandikishaji askari au wanachama.

**recrystallization** *n.* ufuwelikaji mrudio: njia ya kusafisha dutu kwa kurudia ufuwelikaji.

**rectangle** /'rektæŋgl/ *n.* mstatili. **rectangular** *adj.* a mstatili.

**rectification** /ˌrektɪfɪ'keɪʃn/ *n.* urekebishaji; usahihishaji; kirekebishi. **rectifier** *n.* mtu au kitu kinachorekebisha au kinachosahihisha.

**rectify** /'rektɪfaɪ/ *v.t.* sahihisha; rekebisha; takasa; safisha badili mkondo.

**recuperate** /rɪ'ku:pəreɪt/ *v.i.* pona.

**recur** /rɪ'kɜ:(r)/ *v.i.* (**-rr-**) rudia; rejea. *~ring to what I said yesterday,*

kurejea niliyosema jana. **~rence** *n.* kurudiarudia. **~rent** *adj.* -a kurudiarudia; -a mara kwa mara. **~ expenditure**, matumizi ya kawaida. **~ring series**, mfulizo wa kurudiarudia.

**recycling** *n.* urejelezaji: gangiza dutu ambayo imetumika ili ifae kutumika tena.

**red** /red/ *n.* rangi nyekundu; nguo nyekundu. *adj.* -ekundu. **~blood cell**, selidamu nyekundu: seli za damu zilizo na protini zenye rangi nyekundu iitwayo hemoglobini. **~ giant**, nyotazimwe: nyota kubwa sana ambayo imefikia ukomo wa mageuko yake na fueli yake kumalizika. **~ Sea**, Bahari ya Sham. **~ Cross**, Msalaba Mwekundu. **~ tape**, urasimu. *see ~*, ghadhibika sana. **~den** *v.t.* tia wekundu; iva uso; -wa -ekundu. *~-handed*, penye kitendo. **~-letter day** *n.* sikukuu.

**redeem** /rɪ'di:m/ *v.t.* komboa; okoa; fikiza ahadi; fidia. *the redeemer*, mwokozi. **redemption** *n.* ukombozi; fidia; wokovu. *past ~*, -siorekebishika.

**redouble** /ri:'dʌbl/ *v.t.* fanya maradufu; ongeza; zidisha. *v.i.* zidi.

**redox reaction** *n.* utendanaji unaksioksi: utendanaji wa uoksidishaji unakisishaji.

**redress** /rɪ'dres/ *n.* fidia; jaza; marekebisho *v.t.* fidia; rekebisha.*~ the balance*, sawazisha urari tena.

**reduce** /rɪ'dju:s/ *v.t.* punguza; shusha; lazimisha; geuza hali. *~ shillings to cents*, vunja shilingi kuwa senti. *~ wood logs to pulp*, sindika magogo. **reduction** *n.* kupunguza; kupunguka; nakisi; upungufu.

**reed** /ri:d/ *n.* utete; mafunjo; egea. *a broken ~*, kitu au mtu asiyeweza kutumainiwa. **~y** *adj.* (kwa sauti) embamba.

**reef** /ri:f/ *n.* mwamba.

**reel** /ri:l/ *n.* kireli. *v.t.* kunja kwenye kireli; sepetuka; shtuka; yumbayumba. *~ off a story*, simulia kwa mkato. *His mind ~ed when he heard the news*, akili zilimduru aliposikia habari .

**re-entrant** *n.* kipembe kilichoelekea ndani.

**refer** /rɪfə:/ *v.t.* pelekea. *v.i.* rejea. *~ to*, taja; kusudia. *I was not ~ring to you*, sikukusudia wewe. *~ to*, husiana na. **~ee** *n.* mwamuzi; rifa. *v.i.* chezesha. **~ence** *n.* mrejeo; kumbukumbu. *a ~ book*, marejeo. *a ~ library*, maktaba ya marejeo. *in ~ to*, kuhusu.

**referendum** /ˌrefe'rendəm/ *n.* kura ya maoni.

**refine** /rɪ'faɪnd/ *v.t.* takasa; safisha; adilisha; fanya nzuri zaidi. **~ment** *n.* usafishaji; usafi; ustaarabu. **~ry** *n.* kiwanda cha kusafishia. *a sugar ~*, kiwanda cha sukari. **refining** *n.* usafishaji: utoaji uchafu kwenye kitu ili kibakie safi.

**reflect** /rɪ'flekt/ *v.t./i.* akisi; rudisha (nuru, moto, etc.); fikiri; waza. *The quietness of the streets ~ed the grief of all the people*, kimya katika mitaa kilidhihirisha huzuni ya watu. *His action ~ed great credit upon him*, tendo lake lile lilimpatia sifa nyingi. **~ion**

**reflexion** /rɪ'flekʃn/ *n.* kuakisi; fikira; mawazo; mfano; picha; pindu; shutuma. **~or** *n.* kiakisi; kioo. *~ed ray*.

**reflex** /'rɪ:fleks/ *n.* tendosihiari; tendohisia. *-adj.* -a tendohisia; -a tendohiari; -a kujiendea. **~ action**, tendosihiari. **~ angle**, pembekuu. **~ arc**, tao lisohiari: njia maalumu zinapopitia habari za neva na kusababisha kitendo-kisohiari. **~ camera**, kamera akisi. **~ive** *adj.* rejeshi.

**reform** /rɪ'fɔ:m/ *n.* mageuzi; marekebisho; kuongoa. *v.t./i.* rekebisha; hidi; ongoa; ongoka. **~ation** *n.* mageuzi; marekebisho. **~atory** *adj.* -a kuadilisha. *n.* shule ya kuadilisha; shule ya manunda. **~er** *n.* mleta mabadiliko.

**refract** /rɪ'frækt/ *v.t.* chepuka; pinda; pindisha. **~ion** *n.* uchepukaji. **angle of ~**, pembe mchepuko. **~ laws**, kaida za mchepuko. **~ive**

**index**, kipeo mchepuko. **relative ~ index**, kipeo mchepuko wiani. **~ivity** *n.* uchepuko. **~ometer** *n.* kipimamchepuko.
**refrain** /rɪ'freɪn/ *n.* kiitikio; kibwagizo; kipokeo. *v.i.* jizuia; acha kufanya; epuka.
**refresh** /rɪ'frʃ/ *v.t.* burudisha; changamsha; kumbusha. *~ one's memory*, jikumbusha. **~ing** *adj.* -a kuburudisha; -zuri. **~ment** *n.* kiburudishaji.
**refrigerate** rɪ'frɪdʒəreɪt/ *v.t.* tia baridi; gandisha kwa baridi. **refrigerator** *n.* friji; jokofu; jorafu.
**refuge** /'refju:dʒ/ *n.* mahali pa salama; kimbilio. **~e** *n.* mkimbizi.
**refund** /'rɪ:fʌnd/ *n.* malipo. *v.t./i.* rudisha fedha; lipa.
**refuse**[1] /rɪ'fju:z/ *v.t./i.* kataa; katalia; nyima. **refusal** *n.* kukataa; haki ya kukubali au kukataa.
**refuse**[2] /'rɛfju:s/ *n.* takataka.
**regain** /rɪ'geɪn/ *v.t.* pata tena; rudia mahali.
**regal** /'rɪ:gl/ *adj.* -a kifalme; -a kustahili mfalme.
**regard** /rɪ'gɑ:d/ *n.* utazamaji; mazingatio; itibari; heshima; salamu; hoja. *v.t.* tazama kwa makini; angalia; heshimu; husu. *as ~s, ~ing*, kuhusu. *in ~ to*, kuhusu. **~ful** *adj.* -angalifu; -a kuheshimu. **~less** *adj.* bila kufikiri, kuangalia au kujali.
**regenerate** /rɪ'dʒenəreɪt/ *v.t.* ongoa; fufua; ota tena.
**regent** /'ri:dʒənt/ *n.* mtawala wa muda badala ya mfalme; naibu wa mfalme. **regency** *n.* utawala wa kukaimu.
**regime** /reɪ'ʒi:m/ *n.* mfumo wa utawala.
**regiment** /'rɛdʒɪm(ə)nt/ *n.* reji menti: kikosi chini ya kanali. *v.t.* amuru; lazimisha. **~ation** *n.* udhibiti mkali; nidhamu kali.
**region** /'ridʒən/ *n.* mkoa; eneo; sehemu. **~al** *adj.* -a mkoa; -a eneo maalumu.
**register** /'redʒɪstə(r)/ *n.* rejista; rejesta; daftari yenye rekodi; mashine ya kufanyia hesabu; kima cha sauti. *a cash ~*, mashine ya kurekodia mwenendo wa fedha. *v.t./i.* andikisha; rajisi; sajili; tuma barua ya rejista; onyesha hisia; onyesha kipimo.
**registrar** /'rɛdʒɪstrɑ/ *n.* msajili; mrajisi. **registration** *n.* uandi kishaji; usajili.
**registry** /'redʒɪstri/ *n.* ofisi ya msajili; usajili; masijala.
**regret** /rɪ'gret/ *n.* majuto; masikitiko; majonzi. *v.t.* (**-tt-**) juta; jutia; sikitika; sikitikia. **~ful** *adj.* -a kujuta; -a kusikitika. **~fully** *adv.* kwa majuto. **~table** *adj.* -a kujutia; -a kusikitisha.
**regular** /'regjələ(r)/ *adj.* -a kawaida; -enye kukubalika; -enye utaratibu unaofana; -enye kufuata sheria; -enye kufanyika mara kwa mara; enye minyambuliko na mabadiliko ya kawaida; linganifu. *a ~ soldier*, askari mzoefu. **~ity** *n.* kawaida; utaratibu; ulinganifu. **~ize** *v.t.* ratibu; rekebisha; halalisha. **~ly** *adv.* kwa kawaida, desturi, taratibu.
**regulate** /'regjuleɪt/ *v.t.* rekebisha; dhibiti. **regulation** *n.* kanuni; taratibu; urekebishaji. **regulator** *n.* kirekebishaji; mrekebishaji.
**rehabilitate** /ˌri:ə'bɪlɪteɪt/ *v.t.* karabati; tengeneza upya; wezesha kuishi maisha ya kawaida; rudishia mtu cheo.
**rehearse** /rɪ'hɜ:s/ *v.t./i.* kariri; simulia; fanya mazoezi.
**rehearsal** /rɪ'hɜ:sl/ *n.* mazoezi; masimulizi.
**reign** /reɪn/ *n.* utawala; enzi. *v.i.* tawala; miliki. *Silence ~s*, kimya kinatawala.
**reimburse** /ˌri:ɪm'bɜ:s/ *v.t.* lipa. **~ment** *n.* malipo; ulipaji.
**rein** /reɪn/ *n.* hatamu. *v.t.* zuia au ongoza kwa hatamu.
**reinforce** /ˌri:ɪn'fɔ:s/ *v.t.* ongeza nguvu; imarisha. **~ment** *n.* msaada; uimarishaji; askari au silaha za nyongeza.
**reinstate** /ˌri:ɪn'steɪt/ *v.t.* rudishia nafasi au heshima yake; rejesha mahali pake. **~ment** *n.* urudishaji

wa hali ya kwanza.

**reject** /rɪ'dʒɛkt/ *v.t.* tupa; kataa; kana. **~ion** *n.* kitu au mtu aliyekataliwa; ukataaji; ukanaji.

**rejoice** /rɪ'dʒɔɪs/ *v.i./t.* furahi; furahisha; shangilia; furahia. **rejoicing(s)** *n.* shangwe; furaha; nderemo.

**relapse** /rɪ'laps/ *n.* urudiaji hali mbaya ya awali. *v.i.* rudia hali mbaya; rudia mwendo mbaya.

**relate** /rɪ'leɪt/ *v.t./i.* simulia; toa habari; husiana na; husisha na. *~ results to their causes,* husisha matokeo na sababu zake. *be ~d to,* husu; husiana na.

**relation** /rɪ'leɪʃn/ *n.* masimulizi; maelezo; uhusiano; mahusiano; udugu; nasaba. *in ~ to,* kuhusu. *have business ~s with a firm in Zanzibar,* kuwa na mahusiano ya kibiashara na kampuni ya Zanzibar. *friendly ~s between countries,* urafiki baina ya nchi. **~ship** *n.* uhusiano; udugu; mahu siano.

**relative** /'rɛlətɪv/ *n.* jamaa; ndugu. **relative atomic mass** *(RAM):* masi atomia husianifu: uwiano wa masi wastani ya atomu ya elementi na ½ ya masi ya atomu ya kaboni. **relative humidity**, unyevu wiani: uwiano kati ya masi ya mvuke wa maji katika ujazo fulani wa hewa na masi ya mvuke wa maji inayotakiwa kukifu hewa hiyo katika halijoto yake. **relative pronoun**, kiwakilishi rejeshi. *adj.* -a kuwiana na; -a kuhusiana na; -naohusiana. *the ~ advantages of two methods,* ulinganifu wa faida za njia mbili. *They are living in ~ comfort,* waishi katika kwa raha kiasi. **~ly** *adv.* kiasi.

**relativity** /ˌrelə'tɪvəti/ *n.* nadharia ya Einstein kwamba vipimo vya mwendo, nafasi na wakati kama wanda wa nne vinawiana; nadharia tete ya Sapir na Whorf kwamba lugha hutawala namna watu wanavyosawiri ulimwengu wao.

**relax** /rɪ'læks/ *v.t./i.* legeza; legea; pumzika; pumzisha; burudika. *a ~ing climate,* hali ya hewa inayoleta burudani. **~ation** *n.* burudani; ulegevu; ulegezaji.

**relay** /'ri:leɪ/ *n.* ubadilishanaji zamu; mtambo wa kupokea na kurusha habari. *~ race,* mbio za kupokezana vijiti. *v.t. ~ a message,* peleka ujumbe; tandika upya.

**release** /ri'li:s/ *n.* kufunguliwa; kufungua; uwekaji huru; ruhusa. *v.t.* fungua; weka huru; ruhusu kutolewa; ruhusu kutangazwa.

**relevant** /'reləvənt/ *adj.* -a kuhusu jambo lenyewe; husika.

**reliable** /rɪ'laɪəbl/ *adj.* -a kutegemewa; -a kuaminika; -a kutuma iniwa. **reliance** *n.* imani; tegemeo; tumaini. **reliant** *adj.* -enye kujitegemea. *self reliant,* -a kujitegemea.

**relief** /rɪ'lɪ:f/ *n.* msaada; faraja; kitulizo; nafuu; burudisho; upokeanaji. *a ~ map,* ramani mwinuko wa ardhi. *in sharp ~,* kwa udhahiri. *The trees in the picture stood out in sharp ~,* miti katika picha ilitokeza waziwazi.

**relieve** /rɪ'li:v/ *v.t.* fariji; punguza; tuliza; dhihirisha. *~ one's feelings,* punguza mawazo. *relieve sb. of sth.,* saidia.

**religion** /rɪ'lɪdʒən/ *n.* dini; imani. **religious** *adj.* -a dini; -a ucha Mungu; -a utawa; -a imani.

**relinquish** /rɪ'lɪŋkwɪʃ/ *v.t.* acha; achilia. *~ hope,* kata tamaa.

**reluctant** /rɪ'lʌktənt/ *adj. be ~,* topenda; sita; kaidi. **reluctance** *n.* kukataa; ukaidi.

**rely** /rɪ'laɪ/ *v.i. ~ on,* tumainia; tegemea; amini; tawakali.

**remain** /rɪ'meɪn/ *v.i.* baki; salia; dumu; kaa. **~der** *vn.* baki; bakaa; salio. **~s** *vn.* salio; makombo; magofu; maiti.

**remark** /rɪ'mɒ:k/ *n.* maoni; tamko; neno. *v.t./i.* angalia; ona; sema; nena; toa maoni. *nothing worthy of ~,* hapana jipya. **~able** *adj.* -a ajabu; -a kusifika; -si kifani. **~ably** *adv.* sana.

**remedy** /remədi/ *n.* dawa. **remedial**

*adj.* -a kuponya; -a kurekebisha.

**remember** /rɪ'membə(r)/ *v.t./i.* kumbuka; dhukuru. *Please ~ me to him,* tafadhali mpe salamu zangu. **remembrance** *n.* ukumbusho; kumbukumbu; salamu.

**remind** /rɪ'maɪnd/ *v.t.* kumbusha; zindua. **~er** *n.* zinduo; kumbusho.

**remission** /rɪ:mɪʃn/ *n.* maghufira; msamaha wa deni au adhabu; kulegea au kupungua (kwa maumivu, bidii, etc.)

**remit** /rɪ:mɪt/ *v.t./i.* (**-tt-**) ghufiria; samehe; futa; peleka kwa posta; punguza; legeza; pungua; legea; peleka kwa mamlaka ya juu. *~ one's efforts,* punguza juhudi. **~tance** *n.* fedha iliyopelekwa; malipo; upelekaji fedha.

**remnant** /'remnənt/ *n.* bakaa; makombo; mabaki; masazo.

**remonstrate** /'rɛmənstreɪt/ *v.i.* pinga; lalamika. *~ against sth.,* kataa jambo. *~ with sb. that,* bishana na mtu kwamba

**remorse** /rɪ'mɔ:s/ *n.* majuto; toba; huruma. **~ful** *adj.* -a kujuta; -a kutubu.

**remote** /rɪ'məʊt/ *adj.* -a mbali; -a zamani; -liotengana; -liopishana sana. *I haven't the ~st idea,* sijui hata kidogo.

**remove** /rɪ'mu:v/ *v.t./i.* ondoa; hamisha; vua; menya; uzulu; fukuza; futa. **removal** *n.* kuondoa; kuondoka; kuhama; kuhamisha.

**remunerate** /rɪ'mju:nəreɪt/ *v.t.* lipa; -pa ujira; -pa zawadi; tunza. **remuneration** *n.* ujira; zawadi; tunzo; jaza. **remunerative** *adj.* -a kuleta faida.

**renaissance** /rɪ'neɪsns/ *n.* kipindi cha uhuishaji wa sanaa na fasihi katika karne ya 14 hadi 16 huko Ulaya; kipindi cha kuchipuka upya kwa tukio.

**renal** /'ri:n(ə)l/ *adj.* -a mafigo.

**render** /'rendə(r)/ *v.t.* toa; lipa; rudisha; leta; peleka; fanya; tafsiri; igiza; geuza; safisha kwa kuyeyusha. *The drink ~ed him speechless,* ulevi ulimfanya bubu.

**renew** /rɪ'nju:/ *v.t.* fanya -pya; tengeneza upya; -pa moyo; rudia tena. *Snakes ~ their skins,* nyoka hugeuza ngozi zao. **~able energy**, nishati rudishikaji: nishati ambayo vyanzo vyake vinaweza kimaumbile kurudishika tena. **~al** *n.* kufanya upya; kurudia mara ya pili.

**renounce** /rɪ'naʊns/ *v.t.* kataa; kanusha; kana; burai; acha; jitoa katika jambo. **renunciation** *n.* uachaji; kujihini.

**renovate** /'rɛnəveɪt/ *v.t.* karabati; tengeneza. **renovation** *n.* ukarabati; matengenezo.

**renown** /rɪ'naʊn/ *n.* sifa; fahari; jina; umashuhuri; utukufu. **~ed** *adj.* -enye sifa; mashuhuri; -tukufu.

**rent** /rent/ *n.* kodi. *v.t./i.* kodi; kodisha; panga; pangisha. **~al** *n.* kodi

**repair** /rɪ'peə(r)/ *n.* matengenezo; ukarabati. *v.t.* karabati; tengeneza. *a road under ~,* barabara inayotengenezwa. **~able** *adj.* -a kutengenezeka; -a kulipika; -a kuweza kufidiwa.

**reparation** /ˌrepə'rəɪʃn/ *n.* malipo; fidia; ufidiaji.

**repay** /rɪ'peɪ/ *v.t./i.* lipa; lipiza. **~ment** *n.* malipo; ulipaji; ulipizaji.

**repeal** /rɪ'pi:l/ *n.* utanguaji; ubatilishaji; ufutaji. *v.t.* tangua; futa; batilisha.

**repeat** /rɪ'pi:t/ *n.* urudiaji. *v.t./i.* rudia; kariri; soma ghibu. **~edly** *adv.* tena na tena. **repetition** *n.* urudiaji; takriri; kukariri.

**repel** /rɪ'pel/ *v.t.* (**-ll-**) fukuza; sukuma mbali; chukiza; zuia. **~lent** *adj.* -a fukuza; -siopendeza; -chukizi. *n.* kiwinga.

**repent** /rɪ'pent/ *v.t./i.* tubu; juta. **~ance** *n.* majuto; toba. **~ant** *adj.* -a toba; -a kutubu; -a kujuta.

**repercussion** /ˌrɪ:pə'kʌʃn/ *n.* mwangwi; athari; matokeo yasiyotazamiwa.

**replace** /rɪ'pleɪs/ *v.t.* badilisha; rudisha mahali pake; ingia mahali pa; -wa badala ya. **~ment** *n.* ubadilishaji; badala.

**replenish** /rɪ'plenɪʃ/ *v.t.* jaza tena.

**replete** /rɪ'pli:t/ *adj.* -liojaa; tele.

**repletion** *n.* shibe.
**replica** /replɪkə/ *n.* nakala. **~te** *v.t.* rudufu; toa nakala.
**reply** /rɪ'plaɪ/ *n.* jawabu; jibu; uitikiaji.
**report** /rɪ'pɔ:t/ *n.* ripoti; taarifa; uvumi; tetesi; sifa. - *v.t./i.* toa habari; toa taarifa; simulia; andika habari, shtaki; toa timamu. ~ *to the manager for work*, ripoti kwa meneja tayari kwa kazi. **~er** *n.* mwandishi habari; mtoa habari
**repose** /rɪ'pəʊz/ *n.* mapumziko; utulivu; raha; *v.t./i.* laza; egemeza; lala; pumzika; jinyoosha; sinzia; weka
**represent** /ˌreprɪ'zent/ *v.t.* leta; toa; fanya; sawiri; mfano wa; wakilisha; iga; igiza; eleza. *A picture that ~s the garden of Eden,* picha inayosawiri bustani ya Aden. **~ation** *n.* mfano; uwakilishi; picha; taswira; uonyeshaji; onyesho; maelezo; wakala; wakili. **~ative** *n.* mwakilishi; mfano; mjumbe; naibu. *adj.* -wakilishi; -a uwakilishi; -a ujumbe. **~ government** serikali ya uwakilishi.
**repress** /rɪ'pres/ *v.t.* zima; zuia; komesha; nyamazisha. **~ion** *n.* uonevu; unyamazishaji; uzimaji; ukomeshaji. **~ive** *adj.* -a uonevu; -a kukandamiza; -zuiaji; -a kukomesha
**reprieve** rɪ'pri:v/ *n.* achilio la muda; ucheleweshaji adhabu ya kifo kwa muda. *v.t.* ahirisha adhabu ya kifo; achilia kwa muda.
**reprimand** /'rɛprɪma:nd/ *n.* lawama; kemeo; karipio. *v.t.* laumu; kemea; karipia.
**reprisal** /rɪ'praɪzl/ *n.* ulipizaji kisasi; vitendo vya kulipiza kisasi.
**reproduce** /ˌri:prə'dju:s/ *.t./i.* nakili; fuatisha; leta mara ya pili; zaa; ota upya. **reproduction** *n.* nakala halisi; uzazi; uzaaji; uotaji upya; kitu kinachoota upya.
**reproductive** /ˌri:prə'dʌktɪv/ *adj.* -a uzazi; -enye uwezo wa kuzaa.
**reptile** /'reptaɪl/ *n.* mtambaazi: mnyama wa ngeli ya reptilia.
**republic** /rɪ'pʌblɪk/ *n.* jamhuri. **~an** *adj.* -a jamhuri.
**repudiate** /rɪ'pju:dɪeɪt/ *v.t./i.* kataa; kana. **repudiation** *n.* ukataaji; ukanaji.
**repugnant** /rɪ'pʌgnənt/ *adj.* -a kuchukiza; -a kukirihi; -kinzani; -enye kugongana. **repugnance** *n.* chuki; karaha.
**repulse** /rɪ'pʌls/ *n.* ufukuzaji; ufukuzwaji; chuki. *v.t.* rudisha nyuma; fukuza; kataa; katisha tamaa.
**repulsion** /rɪ'pʌlʃn/ *n.* uchukivu; kufukuzwa; kurudishwa nyuma. **repulsive** *adj.* -a kuchukiza; -baya.
**reputation** /ˌrepju'teɪʃn/ *n.* sifa; heshima. **reputable** *adj.* -a sifa njema; mstahiki.
**repute** /rɪ'pju:t/ *n.* sifa; heshima. **reputed** *adj.* sifika kwa; julikana kwa.
**request** /rɪ'kwest/ *n.* ombi; haja; matakwa. *be in ~*, hitajika; takiwa; tafutwa. *v.t.* taka; sihi; omba.
**requiem** /'rɛkwɪəm, -ɪɛm/ *n.*misa ya kuombea waliofariki.
**require** /rɪ'kwaɪə(r)/ *v.t.* hitaji; taka kwa nguvu; amrisha; lazimisha. **~ment** *n.* matakwa; mahitaji; sharti; taratibu.
**requisite** /'rɛkwɪzɪt/ *n.* mahitaji; lazima. *adj.* liotakiwa. **requisition** *n.* mahitaji. *v.t.* omba mahitaji.
**rescind** /rɪ'sɪnd/ *v.t.* tangua; batilisha; futa.
**rescue** /'reskju:/ *n.* wokovu; msaada; uokoaji; uokolewaji. *v.t.* okoa; saidia.
**research** /rɪ'sə:tʃ/ *n.* utafiti; uchunguzi. *v.i.* chungua; tafiti. **~er** *n.* mtafiti; mchunguzi.
**resemble** /rɪ'zembl/ *v.t.* fanana na; shabihi. **resemblance** *n.* mshabaha; ufananaji
**resent** /rɪ'zent/ *v.t.* chukia; udhika; kasirika. **~ful** *adj.* -enye chuki; -a kuudhi. **~ment** *n.* chuki; uchungu; maudhi; hasira.
**reserve** /rɪ'zɜ:v/ *n.* akiba; hifadhi. mchezaji au askari wa akiba. pingamizi. *v.t.* weka akiba; weka kwa matumizi maalumu. *a game ~,* mbuga ya wanyama. **forest ~,**

hifadhi ya msitu. *I accept his statement without ~,* nakubali tamko lake bila pingamizi.

**reservation** /ˌrezə'veɪʃn/ *n.* uwekaji au uwekwaji; shaka. *without ~,* bila kinyongo; bila ya gatigati. **~d** *adj.* -liohifadhiwa; nyamavu.

**reservoir** /'rezəvwɑ:(r)/ *n.* tangi; hodhi; bwawa; ziwa.

**residue** /'rɛzɪdju:/ *n.* masalio; makapi; machuba; machicha; mabaki.

**resign** /rɪ'zaɪn/ *v.t.* acha; jiuzulu; achisha; uzulu. *~ oneself to,* kubali bila kulalamika. **~ed** *adj.* vumilivu; -a kukata tamaa. *He is quite ~,* ameridhika. **~ation** *n.* kuacha kazi; kujiuzulu; ombi la kujiuzulu; uvumilivu.

**resilience** /rɪ'zɪliəns/ *n.* unyumbukaji; unepaji; unesaji. **resilient** *adj.* -a kunyumbuka; -a kunesa; -a kunepa.

**resin** /'rɛzɪn/ *n.* utomvu.

**resist** /rɪ'zɪst/ *v.t./i.* pingia; bisha; kinza; stahamili; jizuia; kataa kujisalimisha. *A kind of glass dish that ~s heat,* namna ya bakuli ya kioo isiyovunjika kwa moto. **~ance** *n.* nguvu kinzi; upinzani; uhasama; uadui. **electrical resistance**, ukinzani umeme. **internal resistance**, ukinzani ndanindani. **~ivity** *n.* ukinzanifu. **~or** *n.* kikinzanishi: sehemu ya saketi inayopitisha umeme kwa ukinzani.

**resolute** /'rɛzəlu:t/ *adj.* thabiti; shupavu; imara.

**resolution** /ˌrezə'lu:ʃn/ *n.* azimio; uamuzi; uthabiti; nia; mchanganuo; mgao.

**resolve** /rɪ'zɒlv/ *n.* azimio; azma; nia; kusudio; ushupavu. *v.t./i.* nuia; kusudia; amua; pitisha; tatua; komesha

**resonant** /'rezənənt/ *adj.* -a mwangwi; -a kuvuma; -a kufululiza kwa mtetemo.

**resonance** /'rezənəns/ *n.* mwangwi; mvumo; sauti yenye kuendelea kwa mtetemo.

**resort** /rɪ'zɔ:t/ *n.* msaada; tegemeo; kimbilio; mahali maalumu pa kutalii. *v.i. ~ to.* kimbilia; tumia; ishia; tembelea. *a seaside ~,* mahali pa kutalii ufukweni.

**resound** /rɪ'zaʊnd/ *v.i./t.* toa mwangwi; vuma; enea pote. *His reputation ~s in this country,* sifa zake zimeenea nchini humu.

**resource** /rɪ'sɔ:s/ *n.* mali; nyenzo; uwezo; werevu; akili. **~ful** *adj.* -a busara; -elekevu; -erevu; -a akili.

**respect** /rɪ'spekt/ *n.* heshima; taadhima; staha; itibari; salamu. *in this one ~,* kwa hili. *in all ~s,* kwa hali zote. *v.t.* heshimu; jali; pendelea; stahi. **~able** *adj.* -a heshima; -stahiki; -a kiasi. **~ably** *adv.* kwa heshima. **~ability** *n.* unyofu. **~ful** *adj.* -stahifu; -a heshima. **~ing** *prep.* juu ya; kwa; kuhusu. **~ive** *adj.* -a pekee; kwa kila mhusika. **~ively** *adv.* -moja -moja; mbalimbali.

**respire** /rɪ'spəɪə(r)/ *v.i.* vuta pumzi; pumua. **respiration** *n.* respiresheni; upumuo; upumuaji.

**respirator** /'respəreɪtə(r)/ *n.* kipumulio. **respiratory organ**, ungo pumuo: ungo katika wanyama linalowawezesha kuvuta oksijeni na kutoa dioksidi kaboni.

**respite** /'rɛspʌɪt, -spɪt/ *n.* nafasi; pumziko; buraha; uahirikaji. *v.t.* ahirisha; -pa nafasi.

**respond** /rɪ'spɒnd/ *v.i.* jibu; itika; itikia; vutika; ongezeka *He always ~s to kindness,* avutika daima kwa upole.

**response** /rɪ'spɒns/ *n.* jibu; jawabu; uvutikaji. **responsive** *adj.* -a kujibu; -a kuvutika; -a kushawishika; -a kuitikia; -a kuitika, -kuongozeka kwa urahisi au kwa upesi.

**responsible** /rɪ'spɒnsəbl/ *adj.* -enye madaraka; -a kuaminiwa. *be ~ to sb. for sth.,* -wa dhamana wa matendo fulani. *He is ~ for the whole loss,* ni dhamana wa hasara yote. *He's a really ~ person,* ni mtu mwaminifu sana. *~ government,* serikali wajibikaji. **responsibility** *n.* dhamana; jukumu; madaraka;

dhima; wajibu. *He undertook the ~ himself,* alibeba jukumu lile mwenyewe. *the heavy ~ of the prime minister,* jukumu kubwa la waziri mkuu.

**rest**[1] /rest/ *n.* raha; pumziko; usingizi; buraha; mhimili; kituo. *v.i./t.* tulia; tuliza; pumzika; pumzisha; egemeza; egemea. **~ful** *adj.* -tulivu; -a kuliwaza. **~ive** *adj.* -a kucheza cheza; -siotulia; - tukutu. **~less** *adj.* tukutu; -siotulia.

**rest**[2] /rest/ *n.* baki; sazo; -ingine -ote. *v.i.* kaa; dumu; tegemea; -wa mikononi mwa. *Success ~s on his answer,* mafanikio yanategemea jibu lake. *It ~s with you to decide,* uamuzi ni wako.

**restaurant** /'rɛst(ə)rɒnt/ *n.* hoteli; mkahawa.

**restitution** /ˌrestɪ'tju:ʃn/ *n.* kulipa; malipo; ukombozi.

**restore** /rɪ'stɔ:(r)/ *v.t.* rudisha; lipa; tengeneza; ponya; rudisha kazini. **restoration** *n.* matengenezo; ukarabati; urudishaji; ulipaji.

**restrain** /rɪ'streɪn/ *v.t.* zuia; rudisha. **~t** *n.* uzuiaji; kizuizi.

**restrict** /rɪ'strɪkt/ *v.t.* wekea mipaka; zuia. **~ion** *n.* mpaka; kizuizi; sharti.

**result** /rɪ'zʌlt/ *n.* matokeo; athari. *v.i.* tokea; wa.

**resume** /rɪ'zu:m/ *v.t.* anza tena; rudia tena; endelea.

**resumption** /rɪ'zʌmpʃn/ *n.* uendeleaji; urudiaji; uanzaji tena.

**resurrect** /ˌrezə'rekt/ *v.t.* fufua. **~ion** *n.* ufufuaji; ufufuo; siku ya kiyama.

**resuscitate** /rɪ'sʌsɪteɪt/ *v.t./i.* pata fahamu; rudisha fahamu; huisha; fufua; rejeza uzima; **resuscitation** *n.* uhuishaji; ufufuo.

**retail** /'ri:teɪl/ *n.* rejareja; uchuuzaji. *v.t./i.* uza rejareja; chuuza. **~er** *n.* mchuuzi; muuza rejareja.

**retain** /rɪ'teɪn/ *v.t.* shika; ajiri; shika; zuia. **~er** *n.* (la zamani) mtumishi wa mtu mkuu; ada ya wakili.

**retaliate** /rɪ'tɑlɪeɪt/ *v.i.* lipiza kisasi. **retaliation** *n.* kisasi; ulipizaji kisasi.

**retina** /'rɛtɪnə/ *n.* retina: sehemu ya nyuma ndani ya jicho ambayo hupokea nuru na kujenga taswira.

**retire** /rɪ'taɪə(r)/ *v.i./t.* ondoka; staafu; kaa faraghani; enda kulala; tawa; staafisha. **~d** *adj.* liostaafu; -liojitenga; pweke. **~ment** *n.* kustaafu; kujitenga; faragha.

**retiring** /rɪ'taɪərɪŋ/ *adj.* -nyamavu; makini.

**retort** /rɪ'tɔ:t/ *n.* jibu kali. *v.i./t.* jibu kwa ukali; itika kwa ukali; jibizana.

**retrace** /rɪ'treɪs/ *v.t.* fuata nyuma; rudi ulikotoka; fuatilia; rudia mambo yaliyopita. *He ~d his steps,* alirudi nyuma

**retract** /rɪ'trækt/ *v.t./i.* kana; rudisha kauli; rudisha ndani. **~able** *adj.* -a kurudishika ndani.

**retreat** /rɪ'tri:t/ *n.* ukimbiaji; kurudi nyuma; mahali pa faragha; kimbilio. *v.i.* rudi nyuma; kimbia.

**retrench** /rɪ'trentʃ/ *v.t./i.* punguza (gharama, etc.). **~ment** *n.* upunguzaji; ubanaji matumizi.

**retribution** /ˌretrɪ'bju:ʃn/ *n.* malipo yanayostahili; rada.

**retrieve** /rɪ'tri:v/ *v.t./i.* pata tena; ongoa; stawisha tena.

**retro-** /'retrəʊ/ *prefix* nyuma; kinyumenyume; kuelekea nyuma.

**retroactive** /ˌretrəʊ'æktɪv/ *adj.* -a kuhusu mambo ya nyuma; -a kutazama nyuma.

**retrograde** /'retrəgreɪd/ *adj.* -a kurudi nyuma; -a kuwa baya; -a kuharibika. **retrogression** *n.* kurudi nyuma; kuharibika. **retrogressive** *adj.* -a kurudi nyuma; -a kuharibu; -a kuharibika.

**retrospect** /retrəspekt/ *n.* utazamaji wa yaliyopita; ukumbukaji ya zamani. *in ~,* kwa mtazamo wa nyuma. **~ive** *adj.* -a kutazama nyuma; -a kuhusu wakati uliopita.

**return** /rɪ'tɜ:n/ *n.* kurudi; kurudishwa; kwenda; kupeleka; kuja; kutoa; faida; taarifa rasmi. - *v.i./t.* rudi; rejea; rudisha; rudia; lipa; jibu; itika; chagua tena kuwa mbunge au mwakilishi. ~ *ticket,* tiketi ya kwenda na kurudi.

**reunion** /rɪ:'ju:nɪen/ *n.* kuunganika tena; kupatana; kurudiana.

**reveal** /rɪ'vi:l/ *v.t.* funua; onyesha;

vumbua; gundua; fichua.

**revelation** /ˌrevəˈleɪʃn/ *n.* kufunua; ufunuo; habari iliyofunuliwa.

**revenge** /rɪˈvendʒ/ *n.* kisasi; ulipizaji kisasi. *v.t.* lipiza kisasi. *be ~ed on sb. for sth., ~ oneself on,* jilipiza kisasi. **~ful** *adj.* -a kutaka kulipiza kisasi.

**revenue** /ˈrevenju:/ *n.* mapato; maduhuli; ushuru.

**revere** /rɪˈvɪə/ *v.t.* heshimu sana; cha; tukuza; stahi sana. **~nce** *n.* heshima; uchaji; unyenyekevu.

**reverend** /ˈrevərənd/ *adj.* mheshimiwa; mstahiwa; mstahiki; padri; mchungaji.

**reverent** /ˈrevərənt/ *adj.* -a kustahi; -nyenyekevu. **~ntial** *adj.* -a kustahi; -ingi -a heshima.

**reverse** /rɪˈvə:s/ *n.* kinyume; upande wa pili; ushinde; mkosi; nyuma. -*adj.* -a kinyume; -a nyuma. *the ~ side of a gramophone record,* upande wa pili wa sahani ya santuri. *v.t.* pindua; geuza; rudi nyuma; rudisha nyuma; batilisha; tangua. **reversal** *n.* upinduaji; kupindua. **reversible** *adj.* -a kupindulika; -a kutumika kuwili. **reversible reaction**, mmenyuko pitukaji: utendanaji wa kikemikali katika hali zinazofaa ambao unaweza kufanywa uendelee mbele au kurudi nyuma na kupatikana msawazo kemikali.

**revert** /rɪˈvɜ:t/ *v.i.* rudia hali ya kwanza; rudi; rejea.

**review** /rɪˈvju:/ *n.* kuangalia upya; ukaguzi; muhtasari; tahakiki; mapitio; jarida la mambo ya sasa. *v.t./i.* angalia; tafakari; kagua rasmi; hakiki.

**revise** /rɪˈvaɪz/ *v.t.* fikiria upya; pitia kwa masahihisho; geuza; badilisha; tengeneza. **revision** *n.* masahihisho; kudurusu.

**revive** /rɪˈvaɪv/ *v.t./i.* fufua; fufuka; huisha; huika; anzisha tena; anza tena. **revival** *n.* ufufuo; ufufuaji; uhuishaji. **revivalist** *n.* mhuishaji, hasa dini.

**revoke** /rɪˈvəʊk/ *v.t* tangua; futa; kanusha; batilisha; ondoa. **revocation** *n.* utanguaji; ubatilishaji.

**revolt** /rɪˈvəʊlt/ *n.* maasi; uasi. *v.i./t.* asi; chukizwa; chukiza; kirihishwa; kirihi. *Scenes that ~ed all who saw them,* mambo yaliyowachukiza wote walioyaona.

**revolution** /ˌrevəˈlu:ʃn/ *n.* mzunguko; mapinduzi. **~ary** *adj.* -a mapinduzi; -a kimapinduzi. **~ize** *v.i.* pindua; badili kabisa.

**revolve** /rɪˈvɒlv/ *v.i./t* zunguka; zungusha; tafakari.

**revolver** /rɪˈvɒlvə(r)/ *n.* bastola.


revolver

**reward** /rɪˈwɔ:d/ *n.* zawadi; thawabu; jaza; tunzo. *v.i.* -pa zawadi; tunza; lipa.

**rheumatism** /ˈruˈmətɪzəm/ *n.* baridi yabisi; uele wa viungo; jongo.

**rheumatic** /rʊˈmatɪk/ *adj.* -a baridi yabisi.

**rhinoceros** /rʌˈnɒs(ə)rəs/ *n.* kifaru.

**rhizome** /ˈrʌɪzəʊm/ *n.* shinakoka: aina ya shina linalotambaa ndani ya ardhi.

**rhomboid** /ˈrɒmbɔɪd/ *n.* romboidi: msambamba wenye pande pakani si sawa. *adj.* -a kama rombasi.

**rhombus** /rɒmbəs/ *n.* rombasi: msambamba wenye pande zote sawa.

**rhyme** /raɪm/ *n.* kina; urari wa vina; mashairi ya vina; matumizi ya vina. *v.t./i.* tunga mashairi ya vina; -wa na sauti sawa mwishoni.


rhombus

**rhythm** /ˈrɪðəm/ *n.* wizani: mfuatano wiani wa mkazo mkali na hafifu wa lafudhi; mahadhi; sauti; mdundo wiani. **~ic (al)** *adj.* -enye wizani; -enye mdundo wiani.

**rib** /rɪb/ *n.* ubavu; taruma; ukuti; mshipa wa jani. **~bed** *adj.* -a nyuzinyuzi kama mishipa.

**ribbon** /ˈrɪbən/ *n.* utepe; riboni.

**rice** /raɪs/ *n.* mpunga; mchele; wali.

**rich** /rɪtʃ/ *adj.* -enye mali; tajiri; -a thamani; -enye rutuba; -enye lishe; -ingi; -zuri. **~es** *n.* mali; utajiri; ukwasi. **~ly** *adv.* sana; kabisa. **~ness** *n.* utajiri.

**Richter scale** *n.* kipimo cha Richter: kipimo cha kupimia nguvu za tetemeko la ardhi kwa mizani ya alama 1 hadi 10.

**rid** /rɪd/ *v.t.* (**rid** au **ridded**) toa; safisha; ondoa. *~ a house of mice,* ondoa panya nyumbani; *get ~ of a cough,* pona kikohozi. **~dance** *n.* uondokaji; uepukaji.

**riddle** /ˈrɪdl/ *n.* kitendawili; fumbo.

**ride** /raɪd/ *n.* kupanda; usafiri wa kupanda; safari ya kipando. *v.t./i.* (**rode**, **ridden**) panda kipando; endesha kipando; shindana kwa kipando; piga chuchuli; elea baharini. **~r** *n.* mpanda farasi; shauri lililotiwa katika mswaada baadaye.

**ridge** /rɪdʒ/ *n.* mgongo; mtwiko; tuta; mgongo wa vilima.

**ridicule** /ˈrɪdɪkju:l/ *n.* dhihaka; mzaha; cheko. *v.t.* cheka; fanyia mzaha; dhihaki; kebehi.

**ridiculous** /rɪˈdɪkjələs/ *adj.* -a kuchekwa; -a mzaha; -a upuuzi.

**rifle** /rɪfl/ *n.* bunduki; kikosi cha askari wa bunduki. *v.t.* chakura; pekua ili kuiba.

**rift** /rɪft/ *n.* ufa; bonde; mwatuko; mpasuko. **~ valley**, bonde la ufa; ugomvi; mtafaruku. *~ in the lute,* kifuja mchuzi; jambo linaloelekea kuharibu furaha.

**right**[1] /raɪt/ *n.* kulia; kuume; mrengu wa kulia. *adj.* -a kulia; -a kuume. *adv.* vyema; kwa upande wa kulia. *go ~ to the end,* enda mpaka mwisho kabisa.

**right**[2] /raɪt/ *n.* wema; haki; ukweli; hali halisi. *adj.* -a haki; nyofu; adilifu; -a kweli; -ema; sahihi; halisi; -a kufaa; **~ angle**, pembe mraba. *the ~ side,* upande unaofaa. *adv.* sawasawa; kabisa; hasa; moja kwa moja; sana. *by ~(s),* kwa haki; barabara; *by ~ of,* kwa sababu ya. *v.t.* simamisha wima; sahihisha; tengeneza. *a ~ about turn,* kugeuka kabisa. **~eous** *adj.* nyofu; -adilifu; -enye haki. **~eousness** *n.* wema; uadilifu; haki; unyofu; maadili. **~ful** *adj.* -a haki; -a adili; -ema. **~ly** *adv.* kwa haki; kwa kweli; kwa usahihi.

**rigid** /ˈrɪdʒɪd/ *adj.* -siopindika; -gumu; imara; -siobadilika. *a ~ rule,* kanuni isiyobadilika. **~ity** *n.* ukavu; ugumu; uthabiti; uimara.

**rigour** /ˈrɪgɔ:, ˈrʌɪgɔ:, -gə/ *n.* ugumu; ukali; hali ngumu. **rigorous** *adj.* -gumu; -kali.

**rim** /rɪm/ *n.* mzingo; ukingo; rimu; fremu. *v.t.* (**-mm-**) -wa ukingo; tia ukingo.

**rind** /raɪnd/ *n.* ganda; gome.

**ring**[1] /rɪŋ/ *n.* mviringo; pete; kipete; duara; genge; kundi; ulingo. **~leader** *n.* kiongozi wa uasi. *~ of fire,* zonimoto: eneo la matetemeko na miripuko ya volkano lenye urefu wa kilomita 32,500 ambalo limeizunguka Bahari ya Pasifiki. **~worm** *n.* choa; punye; chamvi; bato.

**ring**[2] /rɪŋ/ *v.i./ t.* (**rang**, **rung**) lia kama kengele; piga kengele; vuma. *~ up sb.,* pigia simu mtu. *~ off,* kata simu. *~ the changes,* fanya kwa namna mbalimbali.

**rinse** /rɪns/ *v.t.* osha kwa maji safi; suuza; sukutua.

**riot** /ˈraɪət/ *n.* ghasia; fujo; vurugu; makelele; jazba. *v.i.* fanya ghasia au fujo. **~er** *n.* mfanya ghasia. **~ous** *adj.* -a kuleta ghasia; -a makelele.

**rip** /rɪp/ *n.* mpasuko; mahali palipopasuka. *v.t./i.* (**-pp-**) rarua; tatua; pasua

**ripe** /raɪp/ *adj.* bivu; -pevu; tayari. **~n** *v.t./i.* ivisha; pevusha; iva; pevuka.

**ripple** /ˈrɪpl/ *n.* mlio wa wimbi; kiwimbi. *(fig.) a ~ of laughter,* sauti ya kicheko.

**rise** /raɪz/ *n.* mwinuko; kilima; ongezeko; kuchomoza; kuibuka; mwanzo; asili. *v.i.* (**rose**, **risen**) enda juu; paa; inuka; simama; amka; chomoza· tokeza; ibuka; asi. *~ to an occasion,* weza kukabili hali. *give ~ to,* -wa sababu ya. *take a ~ out of sb.,* kasirisha mtu kwa kumfanyia mzaha. **rising** *n.* uasi; mwinuko. *adj.* -a kupanda; -a kuendelea; -a kuongezeka. *the rising generation,* kizazi cha leo. *rising twelve,* -a karibu kufika umri

wa miaka thenashara.
**risk** /rɪsk/ *n.* hatari; mashaka; thamani ya bima. *take ~s,* jihatarisha; bahatisha. *at the owner's ~,* juu ya mwenye mali. *v.t.* hatarisha; bahatisha; jusurisha. *I will ~ failure,* hasara itakuwa juu yangu. **~y** *adj.* -enye hatari.
**rite** /raɪt/ *n.* kanuni ya dini; ibada; ada. **ritual** *n.* utaratibu wa dini; taratibu za ibada; tambiko.
**rival** /'raɪvl/ *n.* mshindani; mpinzani. *adj.* shindani; -pinzani. *v.t.* (**-ll-**) shindana na; jaribu kuwa sawa na; taka kushinda. **~ry** *n.* ushindani.
**river** /'rɪvə(r)/ *n.* mto.
**rivet** /'rɪvɪt/ *n.* ribiti. *v.t.* funga kwa ribiti; vutia; vutiwa.
**RNA** /ˌɑːr 'en 'eɪ/ *n.* ufupisho wa **ribonucleic acid**: asidi ribo-nyuklia: asidi zilizo na sukari ribosi ambazo kazi zake kuu ni kutengeneza protini kwenye seli, hasa katika oganeli ya ribosomu.
**road** /rəʊd/ *n.* njia; barabara. *take to the ~,* zurura. **~ safety**, usalama barabarani. **~man** *n.* mtengeneza barabara. **~metal** *n.* kokoto za kutengenezea njia. **~stead** *n.* bandari; chelezo.
**roan–antelope** *n.* korongo.
**roar** /rɔː(r)/ *n.* ngurumo; rindimo. *~s of laughter,* kicheko kikubwa. *v.i.* nguruma; rindima; sema kwa sauti kubwa.
**roast** /rəʊst/ *n.* nyama iliyookwa; ubanikaji. *v.t.* **1.** choma; oka; banika. **2.** kemea sana.
**rob** /rɒb/ *v.t* (**-bb-**) ibia; nyang'anya; pora; nyima. **~ber** *n.* mwizi; mnyang'anyi; mporaji; jambazi. **~y** *n.* wizi; unyang'anyi.
**robe** /reʊb/ *n.* joho. *v.t./i.* vika; visha; vaa; valia.
**robot** /'rəʊbɒt/ *n.* roboti: mashine ifanyayo kazi kama mtu au mbadala; mtu afanyaye kazi kama mashine ijiendeshayo yenyewe.
**robust** /rəʊ'bʌst/ *adj.* -enye afya na nguvu nyingi.
**rock**[1] /rɒk/ *n.* jiwe; jabali; mwamba. *as firm as a ~,* imara kabisa. *be on the ~s,* panda mwamba; *(fig.)* -wa katika mwambo. **~-bottom** *adj.* -a chini kabisa. **~y** *adj.* -enye mawe mengi; -gumu kama mawe.
**rock**[2] /rɒk/ *v.t./i.* pembeza; tikisa; pembea. **~ cycle**, durumwamba: muda wa mabadiliko ya aina moja ya jabali kuwa aina nyingine ambayo huchukua mamilioni ya miaka.
**rocket** /'rɒkɪt/ *n.* roketi; fataki; fashifashi.
**rod** /rɒd/ *n.* ufito; kiboko; fimbo. *a fishing ~,* mwanzi wa kuvulia samaki. **~ cells**, selifito: seli maalumu zipatikanazo katika tishu za retina katika jicho zenye umbile fito na ambazo zinafanya kazi ya kupeleka ujumbe wa mwanga unaoingia katika seli za neva za fahamu.
**rodent** /'rəʊdnt/ *n.* mnyama mgugunaji kama panya, panya-buku etc.
**roe** /rəʊ/ *n.* ng'ofu: mayai ya samaki.
**rogue** /rəʊg/ *n.* ayari; laghai; mhuni; jangili; jambazi; tapeli; mjanja. **~ry** *n.* ulaghai; hila; utapeli.
**roll** /rəʊl/ *n.* jora; robota; kata ya tumbaku; ukingo uliogeuzwa; mwendo wa kubingiria; orodha ya majina; mrama. *v.t./i.* bingirisha; bingiria; kunja; zongomeza; sukuma; sukasuka; yumbayumba; enda mrama; vuma. *~ in,* -ja kwa wingi. *be ~ing in money,* -wa tajiri sana. **~er** *n.* rola; wenzo; wimbi refu na kubwa.



roller skates

**ROM** /rɒm/ *n.* ufupisho wa **read only memory**: kumbukumbu ya soma tu (KUSOTU): sehemu ya kumbukumbu ya kompyuta ambayo imerekodiwa aushi.
**Roman** /'rəʊmən/ *adj.* -a kirumi. **~ catholic**, a kanisa la katoliki. **~ce** *adj.* -enye kuhusiana na lugha ya Kirumi.
**romance** /rə(ʊ)'mans/ *n.* hadithi ya mahaba; mapenzi; uzushi. **romantic** *adj.* -enye kujitungia mambo yaliyotiwa chumvi; -enye

hisia ya mapenzi; - enye kusisitiza hisia kuliko mantiki.

**romanticism** /rəʊ'mæntɪsɪzəm/ *n.* mrengu wa sanaa na fasihi mnamo karne ya 18 na 19 uliotilia nguvu kariha, udhahania na umuhimu wa mwanadamu kama mhusika mkuu wa matukio.

**romp** /rɒmp/ *v.i.* cheza; chawachawa; rukaruka.

**roof** /ru:f/ *n.* paa; dari; sakafu ya juu; kilele; kakaa.

**rook**[1] /rʊk/ *n.* ndege mweusi kama kunguru. **~ery** *n.* kiota cha ndege huyo.

**rook**[2] /rʊk/ *n.* laghai; ayari. *v.t.* laghai; danganya; ghilibu.

**room** /ru:m, rʊm/ *n.* chumba; nafasi; mwanya.

**roost** /ru:st/ *n.* kiota cha ndege; kizimba cha kuku. *v.i.* jikalia usiku katika kiota. **~er** *n.* jogoo; jimbi.

**root** /ru:t/ *n.* shina; mzizi; *(fig.)* sababu; asili; mwanzo; kiini; kipeo. **~ hair**, laika mzizi: kitu mfano wa unywele kinachokua kwenye mzizi kikiwa na kiambaza chembamba sana cha seli. **~ nodule**, tezimzizi: uvimbe katika mizizi ya baadhi ya mimea ambayo ni makazi ya bakteria wanaotengeneza nitrojeni. **~ system**, mfumo mizizi: mpangilio wa mizizi katika mmea. *v.i./t.* toa mizizi; anza kukua; -wa na mawazo thabiti; weka imara. *~ sth. up (out)*, ng'oa; ondoa kabisa.

**rope** /rəʊp/ *n.*kamba; ugwe; ukambaa. *know the ~s*, elewa jinsi ya kufanya jambo. *v.t.* funga kwa kamba. *(fig.) ~ sb. in*, shawishi mtu ajiunge kufanya jambo.

**rosary** /'rəʊz(ə)ri/ *n.* tasbihi; bustani ya mawaridi.

**rose** /rəʊz/ *n.* waridi; rangi ya waridi. **rosy** *adj.* -a rangi ya waridi; *(fig.)* -a kutia matumaini.

**rot** /rɒt/ *v.i./t.* **(-tt-)** oza; chakaa; *(fig.)* haribika; ozesha. **~ten** *adj.* -bovu; -liooza; viza.

**rotary** /'rəʊtəri/ *adj.* -a kuzunguka.



rose

**rotate** /rəʊ'teɪt/ *v.i./t.* zunguka kitu; zungusha; fuatana kwa zamu.

**rotation** /rəʊ'teɪʃn/ *n.* mzingo; mzunguko. *in ~*, kwa zamu. *the rotation of crops*, ubadilishaji mazao

**rough** /rʌf/ *n.* fedhuli; jeuri; safihi; mshari; jambazi; mhuni. *adj.* enye mashimoshimo; -a kukwaruza; enye mawimbi; -kali; -enye fujo; ghafi; siokamilika; -a kukisia. *a ~ sea*, bahari iliyochafuka. *a ~ idea*, wazo la juujuu. *~ and ready*, -a kutosha kwa haja ya ghafla. *take the ~ with the smooth*, furahia mambo ya kupendeza na kuvumilia taabu. *v.t. ~ sth. out*, sawiri juujuu. *~ it*, ishi maisha ya shida. **~en** *v.t./i.* fanya fujo; -wa na fujo. **~ly** *adv.* takriban; kwa ukali; kwa fujo. *There were ~ forty present*, takriban watu arobaini walihudhuria.

**round** /raʊnd/ *n.* mviringo; duara; raundi; mzunguko. *adj.* -a mviringo; -a duara; -a kuviringana; -a kuzunguka; -zima; kamili; -ote. *a ~ trip*, safari iishiayo pale ilipoanzia. *in ~ numbers*, kwa namba za makumi. *a good ~ sum of money*, fedha nyingi. *the daily ~*, utaratibu wa kila siku. *a ~ of applause*, vifijo. *adv.* kwa kuzunguka; katika duara; kwa kurudia mahali ulipoanza. *look ~*, tazama nyuma. *all the year ~*, mwaka mzima. *Hand these books ~*, gawa vitabu hivi kwa wote. *There is not enough food to go ~*, hakuna chakula cha kutosha kwa watu wote. *We came the long way ~*, tulifuata njia ya mzunguko. *bring sb. ~*, ziua. *come ~*,ziuka. *prep.* kwa kuzunguka au kuzungusha. *v.t./i.* viringisha; viringana. *~ a cape or corner*, zunguka rasi au kona. *~ sth. off*, maliza. *~ animals up*, kusanya wanyama pamoja. *~ up on sb.*, shambulia ghafla; geukia kwa lawama. **~about** *adj.* -enye kuzunguka. *a ~ about message*, habari yenye vipengele. **~ly** *adv. tell sb. ~ that he is lying* , -ambia mtu

wazi kuwa anasema uwongo.
**route** /ru:t/ *n.* njia.
**routine** /ru:'ti:n/ *n.* utaratibu; kawaida ya kila siku; desturi.
**row**[1] /rəʊ/ *n.* safu; mstari; msafa.
**row**[2] /reʊ/ *v.t* endesha kwa makasia. *v.i.* piga makasia.
**row**[3] /rɑʊ/ *n.* mabishano; kelele; ghasia; ugomvi; matata.
**royal** /'rɔɪəl/ *adj.* -a kifalme; -a mfalme; -a fahari. **~ty** *n.* aila ya mfalme; ufalme; mrabaha: malipo ya mwandishi.
**rtp** *n.* ufupisho wa **room temperature and pressure**: halijoto na kanieneo ya chumba: hali joto na kanieneo kama ilivyo katika chumba bila ya kuibadilisha kwa makusudi.
**rub** /rʌb/ *n.* usuguaji; msuguo; taabu; pingamizi. *v.t./i.* (**-bb-**) sugua; pangusa; futa; chua; fikicha. ~ *up,* ng'arisha; piga polishi; fanya kiwe kipya. **~ber** *n.* mpira; kifutio; mfutaji; raba.
**rubbish** /'rʌbɪʃ/ *n.* taka; takataka; upuuzi.
**rubble** /'rʌbl/ *n.* kifusi; kokoto. **ruby** /'ru:bi/ *n.* rubi: kito chekundu cha thamani; rangi ya rubi.
**rucksack** /'rʌksɑk, 'rʊk-/ *n.* shanta.
**rudder** /'rʌdə(r)/ *n.* usukani.
**rude** /ru:d/ *adj.* fedhuli; si -a adabu; -a kushtusha; -a fujo; -kali; ghafi. *get a ~ shock,* shtuka mno. **~ly** *adv.* kwa ufedhuli. **~ness** *n.* ufedhuli.
**rudiment** /'ru:dɪm(ə)nt/ *n.* maarifa ya kwanza; mwanzo; asili; msingi; chimbuko; chanzo. **~ary** *adj.* -a mwanzo; -sioendelea sawasawa; -siokamilika.
**ruffle** /'rʌfl/ *v.t.* chafua; vuruga; timua; timka; chafuka; kasirika. *easily ~d,* -a kuudhika kirahisi.
**rug** /rʌg/ *n.* zulia dogo nene; blanketi nene.
**rugged** /'rʌgɪd/ *adj.* -a mawemawe; si sawa; -sio -a kawaida; -enye mikunjo; -enye kunyanzi. ~ *features,* uso wenye kunyanzi.
**ruin** /'ru:ɪn/ *n.* maangamizi; uharibifu; magofu; kufilisika. *the ~ of my hopes,* kuharibika kwa matumaini yangu. *a ~ed house,* gofu. *v.t.* angamiza; vunja; haribu; filisi. **~ation** *n.* uangamiaji; maangamizi; kuharibika; uharibifu. **~ous** *adj.* -haribifu; -liovunjika.
**rule** /ru:l/ *n.* kanuni; kawaida; amri; desturi; serikali; utawala; mamlaka; dola; rula; mstari. *as a ~,* kwa desturi. *v.t./i.* tawala; hukumu; amuru; piga mstari; amua. ~ *sth. out,* futilia mbali. ~ *a line,* piga mstari. ~ *sth. off,* kata; ondoa. **~r** *n.* mtawala; rula.
**ruling** /'ru:lɪŋ/ *n.* hukumu; uamuzi; amri.
**rum**[1] /rʌm/ *n.* pombe ya miwa.
**rum**[2] /rʌm/ *adj.* *(colloq.)* -a kigeni; -sio -a kawaida; kioja.
**rumble** /'rʌmbl/ *v.i.* nguruma; vuma; tutuma; rindima.
**ruminant** /'ru:mɪnənt/ *n.* mcheuzi: mnyama anayecheua. -a kucheua; -enye kuzama katika fikra. **~ia** *n.* wacheuzi: jamii ya mamalia ambao hucheua kama ng'ombe, mbuzi etc.
**ruminate** /'ru:mɪneɪt/ *v.i.* tafuna; cheua; tafakari; waza.
**rumour** /'ru:mə(r)/ *n.* uvumi; tetesi; udaku; mnong'ono. *v.t.* vumisha. *It is ~ed that,* imevuma kuwa. *~ monger,* mzushi; mdaku; mvumishaji.
**rump** /rʌmp/ *n.* tako la mnyama; mkia wa ndege.
**run** /rʌn/ *n.* kukimbia; mwendo wa mbio; njia; mfululizo; safari; kipindi; mshuko wa ghafla; zizi; banda. *v.i./t.* (**-pp-**) (**ran**, **run**) kimbia; kimbiza; (kwa magari) tembea; (kwa mashine) fanya kazi; tiririka; ingia; pata; pita upesi; elekea; chujuka; toboa; choma; endelea; endesha. ~ *into debt,* ingia deni. ~ *short of food,* pungukiwa na chakula. *Many doubts ran through his mind,* mashaka mengi yalimjia moyoni mwake. *She ran a comb through her hair,* alichana nywele zake. *He ran his eyes over the page,* aliusoma ukurasa juujuu. *The road ~s due north,* barabara inaelekea kaskazini. *Shelves ~ round two*

*walls,* rafu zinazunguka kuta mbili. ~ *a splinter into one's finger,* jichoma kibanzi kidoleni. ~ *into,* gongana; ingia katika. *Don't ~ into a car,* usigongane na gari. ~ *a business,* endesha biashara. *The play ran for three months,* mchezo uliendelea kwa miezi mitatu. ~ *a risk,* jihatarisha. ~ *across sb.,* kuta fulani. ~ *after sb.,* kimbiza; kimbilia. ~ *away,* toroka. ~ *away with,* kimbia na. *His journey will ~ away with a lot of money,* safari yake itamgharimu fedha nyingi. ~ *down,* sita kufanya kazi. *be ~ down,* choka sana. ~ *sb. in,* kamata mtu na kumfunga. ~ *out of,* pungukiwa. ~ *over,* furika. ~ *over sb.,* ponda; kanyaga. ~ *up,* tweka; pandisha. *go for a ~ in the country,* enda shamba kwa matembezi. *on the ~,* katika kutoroka; katika kushindwa na maadui; katika shughuli nyingi. *a ~ of ill luck,* kipindi cha bahati mbaya. *in the long ~,* mwishowe; hatimaye. *(fig.) give sb. the ~ of the house,* karibisha vyema. *a ~ on the bank,* kuwepo watu wengi watoao fedha benki. *the common ~ of mankind,* watu wa kawaida. **~ner** *n.* mkimbiaji. **~ner-up** *n.* mshindi wa pili. **~ning** *adj.* -a kukimbia; moja kwa moja; mtawalia; mfululizo; -a kuchuruzika; -a kutoka usaha. *n.* mbio; kukimbia. *in the ~ning,* -a kuelekea kufanikiwa. *out of the ~ning,* -sioelekea kufanikiwa. **~way** *n.* njia ya kurukia ndege.

**rung** /rʌŋ/ *n.* kidato cha ngazi; taruma la kiti.

**rupture** /ˈrʌptʃə(r)/ *n.* mpasuko; mfarakano. *v.t./i.* pasua; pasuka; farakana.

**rural** /ˈrʊərəl/ *adj.* -a shamba; -ya vijijini

**rush**[1] /rʌʃ/ *n.* mwendo wa kasi; mahitaji makubwa ya ghafla; kukurukakara; ukurupukaji; toleo la kwanza bila ya kuhaririwa. *v.i./t.* kurupuka; kurupua; timua; harakisha; vamia; shambulia. *the ~ hours in the town,* saa za shughuli nyingi mjini.

**rush**[2] /rʌʃ/ *n.* utete.

**rust** /rʌst/ *n.* kutu; kanga. *v.i.* ingia kutu; fanya kanga. **~ing** *n.* ulikaji: utendanaji wa kikemikali unao tokea juu ya kitu hasa metali na kukifanya kilike na kumalizika polepole. **~y** *adj.* -enye kutu; -a kuchakaa; -enye kanga.

**rustle** /ˈrʌsl/ *n.* mchakacho; mchakarisho. *v.i./t.* chakacha; chakarisha.

**rut** /rʌt/ *n.* alama za magurudumu ya magari. *get into a ~,* fuata taratibu hizo kwa hizo daima.

**ruthless** /ˈruːθləs/ *adj.* pasipo huruma; -katili; -korofi.

**rye** /raɪ/ *n.* shayiri.

# Ss

**sabbath** /'sæbəθ/ *n.* sabato: siku takatifu ya kiyahudi, Jumamosi.
**sable-antelope** *n.* palahala.
**sabotage** /'sabətɑːʒ/ *n.* hujuma. *v.t.* kuhujumu.
**sack**[1] /sæk/ *n.* mfuko; gunia. **~cloth**, **~ing** *n.* nguo ya gunia. *clothed in ~cloth and ashes, (fig.)* kuvaa nguo ya huzuni.
**sack**[2] /sæk/ *n. get the ~,* fukuzwa kazi. *give sb. the sack,* fukuza mtu kazi. *v.t. (colloq.)* fukuza kazini
**sack**[3] /sæk/ *n.* uporaji. *v.t.* teka nyara; pora; nyang'anya.
**sacrament** /'sakrəm(ə)nt/ *n.* sakramenti. **~al** *adj.* -a kisakramenti
**sacred** /'seɪkrɪd/ *adj.* -a Mungu; takatifu; -a dhati; -tukufu. **~ness**. *n.* utakatifu.
**sacrifice** /'sækrɪfaɪs/ *n.* sadaka; mhanga; dhabihu; dhahiya; kafara. *v.t./i.* dhabihi; toa sadaka; toa mhanga. **sacrificial** *adj.* -a sadaka; a kama sadaka.
**sacrilege** /'sakrɪlɪdʒ/ *n.* kufuru. **sacrilegious** *adj.* -a kufuru.
**sacrosanct** /'sakrə(ʊ)saŋ(k)t/ *adj.* -liolindwa na maovu yote kwa sababu ya kuwa -takatifu; takatifu sana.
**sad** /sæd/ *adj.* -a huzuni; -a kusikitisha; -a aibu; -a kashfa. **~ly** *adv.* kwa huzuni. **~ness** *n.* majonzi; huzuni. **~den** *v.t./i.* huzunisha; huzunika.
**saddle** /'sædl/ *n.* tandiko la juu ya farasi au punda; soji; kibao cha baiskeli; safu ya milima iliyoinuka mwanzoni na mwishoni. *v.t.* tia tandiko; tandika; -pa mtu jukumu kubwa. **~bag** *n.* shogi; horji; mfuko wa zana za kutengenezea baiskeli.
**safe** /seɪf/ *n.* sefu; tajuri; kabati la chakula. *adj.* salama; -zima; bila madhara; -a salama; -angalifu; yakini; hakika; bila wasiwasi. *travel at a ~ speed,* -enda kwa mwendo wa salama. **~ conduct** *n.* hati ya usalama; kibali cha kupita. **~guard** *n.* kinga; ulinzi. **~ly** *adv.* kwa salama; salama. **~ sex**, mapenzi salama: mbinu ya kujamiiana yenye kuwakinga wapenzi kuambukizana magonjwa ya zinaa. **~ty** *n.* usalama. *play for ~,* tahadhari. *~ match,* kiberiti. **~ valve** *n.* vali ya usalama.
**sag** /sæg/ *v.i.* (**-gg-**) nepa; inama; bonyea; legea.
**saga** /'sɒːgə/ *n.* ngano; hadithi ndefu.
**sagacious** /sə'geɪʃəs/ *adj.* -a busara; -a akili. **sagacity** *n.* busara; akili; utambuzi. **sage** *n.* mtu mwenye hekima nyingi.
**sago** /'seɪgəʊ/ *n.* kopa: moyo wa mti kama mtende au mnazi, huliwa.
**Sahel** *n.* Saheli: ukanda wa nyanda kavu kusini mwa jangwa la Sahara katika Afrika Magharibi.
**sahib** /'sɑː(h)ɪb/ *n.* rafiki.
**sail** /seɪl/ *n.* tanga; safari ya chombo cha tanga. *set ~,* tweka. *strike ~,* tua tanga. *v.i.* safiri katika chombo cha baharini; pita baharini; elea polepole angani. *v.t.* endesha kwa tanga; endesha chombo cha baharini. **~or** *n.* baharia; mwanamaji.
**saint** /seɪnt/ (before a name usually) *n.* walii; mtakatifu; sufii; mtu mwema sana. **~liness** *n.* uwalii; usufii; utakatifu. **~ly** *adj.* -takatifu; kama -takatifu.
**sake** /seɪk/ *n.* ajili. *for the ~ of,* kwa ajili ya. *for my ~,* kwa ajili yangu.
**salad** /'sæləd/ *n.* saladi; kachumbari. *fruit ~,* fruti; saladi ya matunda.
**salary** /'sæləri/ *n.* mshahara.
**sale** /seɪl/ *n.* kuuza; kuchuuza; seli; mnada. *be on (for) ~,* kuuzwa; *It is not for ~,* haiuzwi. **~sman**, **~swoman** *n.* muuzaji. **~smanship** *n.* ujuzi wa uuzaji.
**salient** /'seɪlɪənt/ *adj.* -a kutokeza; -a maana; muhimu; -kubwa.
**saline** /'seɪlʌɪn/ *n.* machimbo ya chumvi. *adj.* -a chumvi. **salinity** *n.* uchumvichumvi.

**saliva** /sə'lʌɪvə/ *n.* mate; udenda; ute; dovuo; utavu.
**sallow** /'sæləʊ/ *adj.* -chakavu; ranga.
**salmon** /'samən/ *n.* samoni: aina ya samaki.
**saloon** /sə'lu:n/ *n.* sebule; ukumbi; gari ndogo; mesi ya melini.
**salt** /sɔ:lt, sɒlt/ *n.* chumvi; munyu; kampaundi ya metali na asidi; haluli. *take with a grain of ~,* sikiliza bila kusadiki moja kwa moja. *not worth one's ~,* -siostahili mshahara. *the ~ of the earth,* watu waadilifu. *an old ~,* baharia stadi. *adj.* -a chumvi. **~y** *adj.* -a chumvi.
**salutation** /ˌsælju'teɪʃn/ *n.* salamu;maamkizi.
**salute** /sə'lu:t/ *n.* salamu; maamkizi; saluti; mizinga ya heshima. *v.t./i.* piga saluti; amkia; salimu.


salute

**salvage** /'sælvɪdʒ/ *n.* uokoaji; ujira wa uokoaji; kitu kilichookolewa. *v.t.* okoa.
**salvation** /sæl'veɪʃn/ *n.* wokovu; uokoaji.
**same** /seɪm/ *adj./pron.* -a moja; sawa. *It's all the ~ to me,* ni mamoja kwangu. *all the ~,* hata hivyo.
**sample** /'sɒ:mpl/ *n.* sampuli; kielelezo; kifani; mfano. *v.t.* onja; jaribu.
**sanatorium** /ˌsanə'tɔ:rɪəm/ *n.* hospitali inayotoa tiba, chakula na mazoezi hasa kwa wasiojiweza kiafya.
**sanctify** /'sæŋktɪfaɪ/ *v.t.* takasa; fanya takatifu. **sanctification** *n.* utakaso; utakasikaji. **sanctimonious** *adj.* -a kujifanya -takatifu; -nafiki.
**sanction** /'sæŋkʃn/ *n.* ruhusa; idhini; kibali; kikwazo; adhabu. *v.t.* kubali; ruhusu.
**sanctuary** /'sæŋktʃuəri/ *n.* mahali patakatifu; madhabahu; kimbilio; hifadhi ya ndege. *bird ~,* mbuga ya ndege.
**sand** /sænd/ *n.* mchanga; ufukwe. **~paper** *n.* msasa. **~stone** *n.* jiwe mchanga. **~y** *adj.* -a mchanga; tifutifu; -a rangi ya lasi.
**sandal** /'sændl/ *n.* makubadhi; malapa; ndara; kandambili.
**sandwich** /'san(d)wɪdʒ/ *n.* sandwichi: slesi za mkate zenye nyama au chakula kingine katikati. *v.t.* bana; weka katikati.
**sane** /seɪn/ *adj.* razini; enye akili timamu; si -enye wazimu; -a busara.
**sanitary** /'sænətri/ *adj.* safi; -a kulinda afya; -a kutia afya. **sanitation** *n.* usafi; udhibiti afya.
**sanity** /'sænəti/ *n.* akili timamu; busara.
**sap** /sæp/ *n.* utomvu. *v.t.* (**-pp-**) ondoa nguvu; dhoofisha. **~ling** *n.* mti mchanga.
**saprophyte** /'saprə(ʊ)fʌɪt/ *n.* saprofiti: mimea inayopata chakula chake kwa kuotesha vinywelea juu ya viumbe vilivyokufa au vyakula vilivyooza.
**sarcasm** /'sɑ:'kæzəm/ *n.* kijembe; kejeli. **sarcastic** *adj.* -a kupiga kijembe; -a kejeli.
**sardine** /sɑ:'di:n/ *n.* sadini; dagaa.
**sardonic** /sɑ:'dɒnɪk/ *adj* -a kubeza; -a dhihaka. *~ laughter,* kicheko cha uchungu.
**sash** /sæʃ/ *n.* mshipi.
**satan** /seɪtn/ *n.* shetani; ibilisi. **~ic** *adj.* a shetani; -ovu; -a bilisi.
**satchel** /'sætʃəl/ *n.* mkoba; mfuko; shanta.
**satellite** /'sætəlaɪt/ *n.* setilaiti: nyota inayozunguka nyota nyingine au sayari. *(fig.)* kibaraka.
**satin** /'sætɪn/ *n.* satini; atlasi; hariri. *adj.* -a kung'aa kama satini
**satire** /'satʌɪə/ *n.* tashtiti. **satirical** *adj.* -a tashtiti. **satirist** *n.* mwandishi wa tashtiti. **satirize** *v.t.* dhihaki; andika tashtiti.
**satisfy** /'sætɪsfaɪ/ *v.t.* ridhisha; tuliza; tosheleza; kidhi, lipiza kisasi. **satisfaction** *n.* kuridhika; ridhaa; malipo; raha mustarehe; uradhi; fidia; kisasi.
**satisfactory** /ˌsætɪs'fæktəri/ *adj.* -a kuridhisha; -a kufaa; -a kutosha. **satisfactorily** *adv.* kwa kutosha.

**saturate** /'satʃəreɪt/ *v.t.* kifu; rowesha kabisa; koleza kabisa; jaza kabisa.
**saturation** /ˌsætʃə'reɪʃn/ *n.* ukifishwaji. **~ed compound**, msombo kifu. **~ed solution**, mmu-munyo kifu. **~ed vapour**, mvuke kifu. **~ed vapour pressure**, kanieneo ya mvuke kifu.
**Saturday** /'sætədeɪ/ *n.* Jumamosi.
**Saturn** /sætɜ:n/ *n.* Zohali: sayari ya sita katika mfumo wa jua.
**sauce** /sɔ:s/ *n.* rojo; mchuzi; sosi. *(colloq.)* ujuvi; mzaha.
**saucy** /'sɔ:si/ *adj.* -juvi; -tundu; -tanashati.
**saucepan** /'sɔ:spən/ *n.* sufuria.
**saucer** /'sɔsə(r)/ *n.* kisahani.
**saunter** /'sɔ:ntə(r)/ *v.i.* tembea polepole.
**sausage** /'sɒsɪdʒ/ *n.* soseji: nyama ya kusaga iliyokaangwa huku imezungushiwa utumbo laini. **~ tree** *n.* mwegea.
**savage** /'sævɪdʒ/ *n.* mshenzi. *adj.* -shenzi; -siostaarabika; -kali; katili; -uaji. **~ry** *n.* ushenzi; ukatili.
**save** /seɪv/ *v.t./i.* okoa; ponya; linda; hifadhi; nusuru; weka akiba. *If you walk, you'll ~ spending money on bus fares*, ukitembea kwa miguu utanusuru nauli ya basi. *~ trouble*, punguza kazi. *prep./conj.* ila; isipokuwa. **saving** *n.* akiba; uokoaji; uwekaji akiba. *adj.* -a kuokoa. *the saving grace of*, tabia nzuri ifidiayo tabia mbaya. **savings bank** *n.* benki ya akiba.
**saviour** /'seɪvjə(r)/ *n.* mwokozi.
**saw** /sɔ:/ *n.* msumeno. **~dust** *n.* unga wa mbao. **~mill** *n.* kiwanda cha mbao .
**saxophone** /'saksəfəʊn/ *n.* saksafoni: namna ya tarumbeta.


saxophone

**say** /seɪ/ *n.* kauli; maoni; neno. *v.t./i.* sema; nena; mathalan. *What do you ~ to going out for a walk?* unaonaje tukienda kutembea? *It goes without ~ing*, ni dhahiri kabisa. *that is to ~*, maana yake. *I must have no ~ in the matter*, niwe sina langu katika hili. **~ing** *n.* neno; methali; kauli.
**scab** /skæb/ *n.* kigaga. **~ies** *n.* upele; ukurutu.
**scabbard** /'skabəd/ *n.* ala ihifadhiyo silaha kali kama kisu au upanga.
**scaffold** /'skafəʊld/ *n.* jukwaa; kidungu; dungu; jukwaa wanaponyongwa wahalifu.
**scalar** /'skeɪlə/ *n.* skala: chochote chenye ukubwa lakini hakina uwelekeo. *adj.* -enye ukubwa lakini haina uwelekeo.
**scald** /skɔ:ld/ *n.* kidonda cha moto; lengelenge; tumbuja. *v.t.* babua; safisha kwa maji moto; pasha moto.
**scale**[1] /skeɪl/ *n.* alama za vipimo; kipimo; jamii ya sauti; mfumo wa vipimo; skeli: uwiano wa ukubwa halisi na kipimo cha ramani au mchoro; ngazi. *the* **decimal ~**, kipimo cha desimali. *a ~ of wages*, ngazi za mishahara. *a person who is high in the social ~*, mtu wa cheo kikubwa. *on a large ~*, kwa wingi. *v.t.* panda; kwea; nakili kwa vipimo vya ramani. *~ up*, pandisha. *~ down*, punguza. *All prices were ~d up by ten per cent.*, bei zote zilipandishwa kwa asilimia kumi.


scales

**scale**[2] /skeɪl/ *n.* kitanga cha mizani; *(pl.)* mizani. *turn the ~s*, amua na kuondoa mashaka; *hold the ~s even*, amua kwa haki.
**scale**[3] /skeɪl/ *n.* gamba la samaki; mba katika nywele; ukoko katika nywele; koya la meno.
**scalene** /'skeɪli:n/ *adj.* -enye pande zisizo sawa.
**scalp** /skælp/ *n.* ngozi ya kichwa na nywele zake.
**scalpel** /'skælpəl/ *n.* kisu kidogo cha kupasulia.
**scamper** /'skæmpə(r)/ *v.i.* enda mbiombio; puruka; kimbia.
**scan** /skæn/ *v.t.* pitia haraka; chungua; kagua; changanua maandishi, picha au michoro kwa mwale elektroniki; soma kwa

mapigo. **~ner** *n.* skena: kisoma maandishi na picha kielektroniki.
**scandal** /'skændl/ *n.* kashfa. **~monger** *n.* mbeya. **~ize** *v.t.* kashifu. **~ous** *adj.* -a kashfa; -enye kashfa; mbeya.
**scar** /skɑ:(r)/ *n.* kovu; baka.
**scarce** /skeəs/ *adj.* adimu; nadra; haba. **~ly** /skeəsli/ *adv.* kwa nadra; kwa shida; si sana; kidogo sana. *~ anyone knows what really happened,* watu wachache sana wajua yaliyotokea. **scarcity** *n.* uadimifu; uchache; uhaba.
**scare** /skɛ:/ *n.* hofu; fadhaa. *v.t.* ogofya; tisha; shtusha; gutusha; gutua; fadhaisha. **~crow** *n.* sanamu ya kuingia ndege. **~monger** *n.* mvumisha vitisho.
**scarf** /skɑ:f/ *n.* shali; skafu; shela; mtandio.
**scarlet** /'skɑ:lət/ *n.* rangi nyekundu. *adj.* ekundu.
**scatter** /'skætə(r)/ *v.t./i.* tawanya; tawanyika; tapanya; tapanyika. **~ed** *adj.* -liotengana sana; -liotawanyika. *~ villages,* vijiji vilivyotenganatengana.
**scavenger** /'skævɪndʒə(r)/ *n.* ndege mla mizoga; topasi.
**scene** /si:n/ *n.* sehemu ya tukio; mandhari; onyesho; ghasia; kituko; eneo. *be behind the ~s,* -wa nyuma ya jukwaa; *(fig.)* -enye kuathiri mambo kisirisiri.
**scent** /sent/ *n.* manukato; uturi; harufu; mavumba; mtara; buhuri. *throw sb. off the ~,* potosha; poteza kwa taarifa zisizo sahihi. *v.t.* sikia harufu; nusa; nukiliza. *(fig.)* ng'amua; tambua; shuku; tia manukato.
**sceptic** /'skeptɪk/ *n.* mwenye kushuku. **~al** *adj.* -enye kushuku. **~ism** *n.* nadharia ya kushuku ukweli kuhusu maoni yanayokubaliwa katika jamii au miongozo ya dini.
**sceptre** /'septə(r)/ *n.* fimbo ya kiongozi wa nchi; enzi.
**schedule** /'ʃɛdju:l/ *n.* orodha; jedwali; ratiba.
**scheme** /ski:m/ *n.* taratibu; mpango; hila; njama. *v.t.* fanya shauri; panga; fitini; pika majungu; panga njama.
**scholar** /'skɒlə(r)/ *n.* mwanafunzi; mtu afadhiliwaye katika masomo; mwanazuoni; mtaalamu; msomi. **~ship** *n.* msaada wa masomo; utaalamu.
**scholastic** /'skə'læstɪk/ *adj.* -a chuo; -a elimu; -a masomo.
**school** /sku:l/ *n.* skuli; shule; masomo; vipindi; kusoma; wanafunzi; tapo; madhehebu; wafuasi. *v.t.* fundisha; ongoza; adibu; zoeza. **~ing** *n.* elimu; mafundisho. **~master**, **~mistress** *n.* mwalimu.
**science** /'saɪəns/ *n.* sayansi; ubingwa; ujuzi; maarifa. *natural ~,* sayansi asili. **physical ~**, sayansi umbile. **social ~s**, sayansi jamii. **applied ~**, sayansi tumizi. **~ fiction**, riwaya ya kisayansi.
**scientific** /ˌsaɪən'tɪfɪk/ *adj.* -a sayansi; -a kanuni za sayansi; -a ujuzi; -a maarifa. **scientifically** *adv.* kisayansi. **scientist** *n.* mwanasayansi.
**scissors** /sɪ'zəz/ *n.* mkasi.
**scold** /skəʊld/ *n.* mkaripiaji. *v.t.* karipia; kemea.
**scoop** /sku:p/ *n.* upawa; mkamshi; bambo; *(colloq.)* habari iliyotangazwa na gazeti moja kabla ya mengine. *v.t.* pakua; chota kwa mwiko; komba; chimba kwa bambo.


scoop

**scope** /skəʊp/ *n.* upeo; eneo; nafasi; uwezo; mawanda.
**scorch** /skɔ:tʃ/ *n.* baka la kuungua. *v.t./i.* unguza; choma; ungua; nyausha; babua; *(colloq.)* enda kasi sana.
**score** /skɔ:(r)/ *n.* mfuo; mtai; chale; alama; mchoro; korija; ishirini; hesabu ya alama katika mchezo; goli; bao; pointi; sababu; noti za muziki. *pay off old ~s,* lipiza kisasi. *on the ~ of,* kwa sababu ya. *v.t./i.* tia bao; funga; hesabu; andika noti za muziki; tia pengo; chora; kata; pata faida. *~ off sb.,* shinda. **~r** *n.*

mwandishi wa mabao; mfungaji.

**scorn** /skɔ:n/ *n.* dharau; bezo; kitu au mtu wa kudharauliwa. *v.t.* dharau; beza. **~ful** *adj.* -enye dharau. **~fully** *adv.* kwa dharau.

**scorpion** /skɔ:piən/ *n.* nge; alama ya nane ya nyota za unajimu.

**scotch** /skɒtʃ/ *n.* haribu; zuia komesha.

**scot-free** *adv.* bila matatizo; salama usalimini.

**scoundrel** /'skaʊndrəl/ *n.* mtu mwovu kabisa.

**scour**[1] /'skaʊə(r)/ *v.t.* sugua sana; safisha kwa kusugua; ng'arisha.

**scour**[2] /'skaʊə(r)/ *v.t.* tafuta mtu harakaharaka.

**scourge** /'skɜ:dʒ/ *n.* mjeledi; *(fig.)* taabu. *v.t.* piga mjeledi; adhibu; tesa.

**scout** /skaʊt/ *n.* mpelelezi atumwaye kupata habari za adui; skauti. *v.i.* peleleza.

**scowl** /skaʊl/ *v.i.* kunja uso kwa ghadhabu.

**scramble** /'skræmbl/ *n.* kinyang'anyiro; fujo; vurugu. *v.i.* kwea; paramia; gombania; nyang'anyiana; shindania; pigania; piga mayai.

**scrap**[1] /skræp/ *n.* kipande; masalio; mabaki; takataka. **~py** *adj.* ovyo; -a wasiwasi.

**scrap**[2] /skræp/ *n./v.i.* (**-pp-**) *(colloq.)* mapigano; mzozo; zozana; pigana.

**scrape** /skreɪp/ *n.* mparuzo; mkwaruzo; mbuzi; shida; matata; mkasa. *v.t./i.* para; paruza; paa; chubua; kwaruza; komba; kuna nazi. *(fig.)* ~ *through an examination,* pasi mtihani.

**scratch** /skrætʃ/ mchoro; mtai; mfuo; mkuno; mstari wa kuanzia mbio. *v.t./i.* chora; futa; fukua; kuna; papura; paruza; kwaruza; chakura; toa katika mashindano. *escape without even a ~,* okoka salama usalimini. *come up to ~,* jitayarisha. *adj.* ovyo; -a bahati. *a ~ team,* timu iliyochaguliwa kwa haraka.

**scrawl** /skrɔ:l/ *n.* mwandiko mbaya; chora. *v.i./t.* andika vibaya; chora.

**scream** /skri:m/ *n.* ukwenzi; usiahi; mayowe. *v.i./t.* piga siahi; piga mayowe; piga ukwenzi.

**screen** /skri:n/ *n.* pazia; kioo; skrini; kinga; ngao. ~ *play,* mchezo wa sinema. *v.t.* sitiri; *(fig.)* linda; sitiri; chekecha; chuja; onyesha filamu.

**screw** /skru:/ *n.* parafujo; skurubu; parafujo shinikizi. *v.t./i.* funga, kaza



screens

kwa skrubu; songoa; jamiiana. ~ *up one's courage,* piga moyo konde; kaza moyo. **~driver** *n.* bisibisi.

**scribble** /'skrɪbl/ *v.i./t.* andika upesi; andika vibaya; chora.

**scribe** /skraɪb/ *n.* mwandishi.

**script** /skrɪpt/ *n.* mwandiko; mwandiko wa chapa. maandiko. **~ure** *n.* maandiko matakatifu; mafunzo ya maandiko matakatifu.

**scroll** /skrəʊl/ *n.* hati ya kukunja; nakshi kama hati za kukunja.

**scrotum** /'skrəʊtəm/ *n.* kifukokorodani; ngozi inayohifadhi kende katika mamalia.

**scrub**[1] /skrʌb/ *v.t./i.* (**-bb-**) sugua sana kwa brashi. **~bing brush** *n.* brashi ya kusugulia.

**scrub**[2] /skrʌb/ *n.* msitu; pori.



scrubbing brush

**scruple** /'skru:pl/ *n.* haya; aibu. *Have you no ~s about borrowing things without permission?* huoni haya kujiazimia vitu bila ruhusa?

**scrupulous** /'skru:pjələs/ *adj.* -angalifu sana; -a hadhari sana; -adilifu.

**scrutiny** /'skru:təni/ *n.* uchunguzi.

**scrutinize** /'skru:tənaɪz/ *v.t.* chunguza; angalia kwa makini.

**scuffle** /'skʌfl/ *n.* fujo; ugomvi. *v.i.* buburushana; vurumishana.

**scull** /skʌl/ *n.* kasia; upondo; kafi.

*v.t./i.* endesha kwa kasia; vuta kasia.
**sculpture** /'skʌlptʃə(r)/ *n.* sanaa ya uchongaji: kinyago; sanamu. *v.t./i.* chonga; tia nakshi. **sculptor** *n.*mchongaji au mfinyanzi vinyago au sanamu.
**scum** /skʌm/ *n.* povu; taka za juu; *(fig.)* mtu ovyo.
**scurry** /'skʌri/ *n.* mwendo wa haraka; manyunyu ya theluji; ghubari. *v.i.* kurupuka; enda upesi.
**scuttle**[1] /'skʌtl/ *v.t.* toboa meli ili kuizamisha
**scuttle**[2] /'skʌtl/ *v.i.* kimbia; enda mbio.
**sea** /si:/ *n.* bahari. *be at ~, (fig.)* -wa na mashaka. *go to ~,* -wa baharia. *a heavy ~,* mawimbi makubwa. *a ~ of trouble, (fig.)* shida nyingi. **~faring** *adj.* -enye kusafiri baharini. **~gull** *n.* shakwe; membe. *to find one's ~ legs,* kuzoea mrama. **~ level** *n.* usawa wa bahari. **~ lion** *n.* sili bahari: aina ya sili aishie baharini. **~man** *n.* baharia. **~manship** *n.* ustadi wa ubaharia. **~port** *n.* bandari. **~shore** *n.* ufukwe. **~sick** *adj.* -enye kichefuchefu cha bahari. **~weed** *n.* mwani. **~worthy** *adj.* -enye kufaa kusafiri baharini


sea lion

**seal**[1] /si:l/ *n.* muhuri; chapa; alama.
**seal**[2] /si:l/ *n.* sili: mnyama wa bahari


seal

**seam** /si:m/ *n.* mshono; bandi; upindo; tabaka ya madini katika mwamba; mkunjo.


seal

**sear** /sɪə(r)/ *v.t.* unguza, hasa kwa chuma cha moto; *(fig.)* fanya kuwa bila huruma.
**search** /s3:tʃ/ *n.* upekuzi; utafutaji. *v.t./i.* tafuta; pekua; chunguza. **~light** *n.* kurunzi. **~ warrant** *n.* hati ya upekuzi.
**season** /'si:zn/ *n.* msimu; majira; muhula; kipindi. *fruit is in ~,* ni msimu wa matunda. *v.t./i.* unga; zoea; zoeshwa; koleza; punguza makali. *The wood is well ~ed,* mbao zimekauka vyema. **~able** *adj.* -a wakati ufaao. **~ing** *n.* kukoleza viungo.
**seat** si:t/ *n.* kiti; kikalio; matako; nafasi; makao; mkao; makazi. *have a ~ in parliament,* -wa mbunge. *country ~,* nyumba ya shamba. *The capital is the ~ of government,* mji mkuu ni makao ya utawala. *v.t. ~ oneself ,* kaa; keti; -pa nafasi ya kukaa. *The room ~s about twenty,* chumba chachukua watu 20 takriban.
**secant** /'si:k(ə)nt/ *n.* sekanti: mstari mnyoofu ukatao duara au mchirizo.
**secede** /sɪ'si:d/ *v.i.* jitenga; jiondoa; jitoa. **secession** *n.* kujitoa; kujitenga.
**seclude** /sɪ'klu:d/ *v.t.* tenga; tawisha. *lead a ~d life,* ishi maisha ya upweke. **~d** *adj.* kimya; faragha; pekee.
**seclusion** /sɪ'klu:ʒn/ *n.* kujitenga; faragha; upweke; utawa. *live in seclusion,* tawa; jitenga.
**second** /sɛk(ə)nd/ *n.* msaidizi; mwingine; kingine; kitu cha pili; nukta; sekunde. *adj.* -a pili; -a baadaye; -a kufuata; -a zaidi. *v.t.* saidia; unga mkono; azima mfanya kazi wa serikali kwa kazi maalumu. **~ary** *n.* -a kufuata; -a baadaye; -a pili. **~ cell**, seli fuasi: seli ya volti ambayo inaweza kutiwa chaji kwa kupitisha mkondo wa umeme kinyume na mwelekeo wa kani mwendo-umeme. **~ colour,** rangi ya upili: rangi ya kijani au ya chungwa inayopatikana kwa kuchanganya rangi mbili za kimsingi. **~ consumer**, mla walamajani: mnyama ambaye hula wanyama walao majani. **~ sexual characteristics**, sifa jinsia fuatizi: mabadiliko ya kijinsia yanayotokea katika baleghe yasiyohusiana moja kwa moja na maungo jinsia. **~ school**, skuli ya sekondari. **~-hand** *adj.* -liokwishatumika. **~-hand clothes**, mitumba. **~rate** *adj.*

hafifu; duni.

**secret** /'si:krət/ *n.* siri; jambo la siri. *adj.* -a siri; -liofichwa; -a faragha. *in ~.* kwa siri; faragha. **~ly** *adv.* kwa siri. **secrecy** *n.* siri; usiri; ufichaji. **~ive** *adj.* msiri; -enye kufichaficha.

**secretary** /'sekrətri/ *n.* katibu; mwandishi; mhazili. **executive ~** katibu mtendaji. **principal ~** katibu mkuu. **private ~.** katibu myeka; katibu muhtasi. **publicity ~.** katibu mwenezi. **~ general** katibu mkuu. **~ of state.** waziri.

**secretarial** /,sekrə'teəriəl/ *adj.* -a uhazili; -a katibu; -a mwandishi.

**secretariat** /,sekrə'teəriət/ *n.* jopo la waandishi; ofisi ya mhazili; makarani wamsaidiao mkuu.

**secrete** /sɪ'kri:t/ *v.t.* ficha; sitiri; -nya; toa.

**secretion** /sɪ'kriːʃn/ *n.* mnyeso; utoaji utomvu au kioevu au umajimaji kama kimiminiko kutoka kwenye tishu au tezi; kitu chochote kinachotolewa kama takataka kutoka kwenye mwili wa kiumbe hai.

**sect** /sekt/ *n.* madhehebu; kikundi.

**section** /'sekʃn/ *n.* seksheni; sehemu; kipande; fungu; idara; kitengo; mkato.

**sector** /'sektə(r)/ *n.* sekta; sehemu ya medani; sehemu ya duara.

**secular** /'sɛkjʊlə/ *adj.* -a kilimwengu; -a kidunia; si -a kidini.

**secure** /sɪ'kjʊə(r)/ *adj.* salama; thabiti; -a hakika; -a kudumu; yakini. *v.t.* hifadhi; linda; tunza; funga; kaza; pata; jipatia; dhamini.

**security** /sɪ'kjʊərəti/ *n.* usalama; rehani; dhamana; amana; hati-sharti.

**sedate** /sɪ'deɪt/ *adj.* -tulivu; -pole; -a makini.

**sedative** /sɪ'detɪv/ *n.* /*adj.* dawa ya kutuliza; -a kutuliza; kitulizo.

**sedentary** /'sɛd(ə)nt(ə)ri/ *adj.* -a kukaa; -a utako.

**sediment** /'sedɪmənt/ *n.* mashapo; takataka za chini; matope ya mto; masimbi. **~ary** *adj.* -a mashapo. **~ rock** mwamba mashapo. **~ation** *n.* ushapishaji.

**sedition** /sɪ'dɪʃn/ *n.* uchochezi wa uasi; uhaini. **seditious** *adj.* -chochezi; asi.

**seduce** /sɪ'dju:s/ *v.t.* shawishi; potoa; tongoza. **seduction** *n.* upotoaji; utongozaji; ushawishi; upotofu; kivutio. **seductive** *adj.* -a kuvutia; -a kushawishi; -a kubembeleza.

**see** /si:/ *v.i./t.* (**saw**, **seen**) ona; fahamu; angalia; tazama; elewa; tambua; pitia; onana na; hakikisha. *~ about.* shughulikia. *~ into.* chunguza. *~ sb. off.* sindikiza. *~ through sb.,* ng'amua; baini. *~ through. ~ out.* linda hadi mwisho. *~ to.* shughulikia. *~ the last of.* achana na; malizana na. *~ double* ona vitu viwili mahali pa kimoja. *~ red* kasirika sana.

**seed** /si:d/ *n.* mbegu; punje; -asili; mwanzo. *~ing machine.* mashine ya kupanda mbegu. **~ling** *n.* mche.

**seek** /si:k/ *v.t./i.* (**sought**) tafuta; taka; omba; jitahidi; jaribu. *~ to do sth.,* jaribu kufanya jambo. *sought after.* liotakiwa sana.

**seem** /si:m/ *v.i.* onekana; fanana na; elekea kuwa; -wa kama. **~ing** *adj.* -a uongo; -a kujifanya; -a juujuu. **~ingly** *adv.* kwa kuonekana; kwa nje. **~ly** *adj.* -a kufaa; -a adabu; -a heshima.

**seep** /si:p/ *v.i.* vuja; penya. **~age** *n.* uvujaji; upenyaji.

**see-saw** *n.* pembea; bembea. *v.i.* panda na kushuka pembea.

**seethe** /si:ð/ *v.i.* chemka; jaa hasira.



**see- saw**

**segment** /'sɛgm(ə)nt/ *n.* mkato; sehemu; pingiti; pingili; sehemu ya duara; kipande. *a ~ of an orange.* kipande cha chungwa. **~ed worm** mnyoo pingili; mmoja wa minyoo ya jamii ya anelidi ambao miili yao imegawika katika pingili.

**segregate** /'sɛgrɪgət/ *v.t.* tenga; bagua; tenganisha.
**seismic** /'sʌɪzmɪk/ *adj.* -a tetemeko la ardhi. **~ wave**, wimbi tetemeko: wimbi ambalo husafirisha nishati kutoka chini ya ardhi ambapo miamba hutembea haraka.
**seismograph** /'sʌɪzmə(ʊ)grɑ:f/ *n.* seisimografu: ala ya kurekodi tetemeko na kuonyesha tambo lake. **seismology** *n.* seisimolojia: sayansi ya uchunguzi wa matetemeko ya ardhi.
**seize** /si:z/ *v.t./i.* kamata; twaa; nyang'anya; pokonya; teka. ~ *upon an idea*, fahamu vizuri wazo fulani na kulitumia vyema.
**seizure** /'si:ʒə(r)/ *n.* kukamata; kukamatwa; utekaji; ukamataji; kifafa
**seldom** /'seldəm/ *adv.* nadra; mara chache; kwa shida
**select** /sɪ'lekt/ *v.t.* chagua; teua. *adj.* -liochaguliwa; -teule; -a watu maalumu. **~ion** *n.* uchaguzi; uteuzi. **~ive** *adj.* -enye uwezo wa kuchagua; -teuzi; -chaguzi. **~ breeding**, uzalishaji teuzi: uzalishaji wa wanyama au mimea kwa kutumia wazazi wenye sifa maalumu. **~ logging**, ukataji miti pembuzi: ukataji wa baadhi ya miti katika msitu na kuacha mingine ipevuke. **~ively-permeable membrane**, kiwambo pitishi teuzi: kiwambo ambacho kina tundu zinazoruhusu kupita kwa baadhi ya chembechembe na kuzuia nyingine. **~or** *n.* mchaguzi; mteuzi.
**selenium** /sɪ'linɪəm/ *n.* seleni: elementi ya kikemikali iliyo kipitishi inayotumika sana katika kazi za elektroniki.
**self**[1] /self/ *n.* (**selves**) nafsi; moyo; mwenyewe. *a man with no thought of ~*, mtu asiyejifikiria hata kidogo.
**self**[2] /self/ *refl. pron.* -ji-. *to see one~*, kujiona. *The dog hid it~*, mbwa kajificha. *He has killed himself*, amejiua
**self-**[3] /self/ *prefix* -enyewe; -ji-; otomatiki. *~-taught*, aliyejifundisha mwenyewe. **~-control** *n.* kujizuia. **~-conscious** *adj.* -enye kujikisi. **~-goverment** *n.* kujitawala. **~-possessed** *adj.* -a kujiamini; tulivu. **~-reliant** *adj.* -a kujitegemea. **~-respect** *n.* kujistahi; kujiheshimu. **~-willed** *adj.* -kaidi.
**selfish** /'selfɪʃ/ *adj.* -enye choyo.
**sell** /sel/ *v.t./i.* (**sold**) uza; uzika; tapeli.
**semen** /'si:mən/ *n.* manii, shahawa; giligili ambayo hutolewa kutoka kwenye tezi katika pumbu pamoja na gameti za kiume.
**semi** /'semi/ *-prefix* nusu; -a upande mmoja; kidogo. **~circle** *n.* nusu duara. *be* **~-conscious**, -wa na fahamu kidogo. **~-annual**, -a mara mbili kwa mwaka. **~colon** *n.* nukta mkato; alama hii (;). **~-detached** *adj.* enye kuunganika kwa upande mmoja. **~-final** *n.* nusu fainali. **~-permeable membrane**, kiwambo penyipenyi; kiwambo ambacho kinaruhusu upitishaji wa dutu fulani tu na sio nyinginezo.
**semiconductor** /ˌsemikən'dʌktə(r)/ *n.* kipitishipitishi: dutu yenye tabia ya upitishaji umeme iliyo kati ya zile za kipitishi na kihami na hutumika katika transista.
**seminal vesicle** *n.* kibweta manii: sehemu katika pumbu ambako shahawa huhifadhiwa kabla hazijatolewa nje.
**seminary** /'sɛmɪn(ə)ri/ *n.* seminari; madrasa ya dini.
**senate** /'senət/ *n.* seneti (sehemu ya bunge); baraza la uongozi wa chuo kikuu.
**senator** /'senətə(r)/ *n.* seneta.
**send** /send/ *v.t./i.* (**sent**) /sent/ peleka; tuma; agiza; sababisha kuwa; jalia. ~ *for*, ita; agizia. **~** *forth*, toa. ~ *sb. mad*, tia wazimu. **~-off** *n.* muagano; usindikizaji.
**senile** /'si:naɪl/ *adj.* dhaifu kutokana na uzee. **senility** *n.* udhaifu wa uzee
**senior** /'si:nɪə/ *n.* mkubwa. *adj.* -kubwa kwa umri, daraja, cheo, etc.; -a kwanza; -a kutangulia; andamizi. **~ magistrate**, hakimu

mwandamizi. **~ lecturer**, mhadhiri mwandamizi. **~ity** *n.* ukubwa; utanguliaji.

**sensation** /sen'seɪʃn/ *n.* uono; hisi; kioja; kichocheo. **~al** *adj.* -a ajabu; -a kushtusha.

**sense** /sens/ *n.* hisi; fasili ya dhana akilini; busara; akili; kufahamu; kupambanua; maana. *He has a moral ~,* apambanua mema na mabaya. *the principal ~ of a word,* maana ya msingi ya neno. *be out of one's ~s,* potewa na akili. *bring sb. to his ~s,* komesha mtu kufanya mabaya. *come to one's ~s* jirudi; zinduka; tanabahi. **~less** *adj.* pumbavu; -jinga; -liozimia. *become ~less,* zimia.

**sensibility** /ˌsensə'bɪləti/ *n.* wepesi wa kuhisi. **sensible** *adj.* -a busara; enye akili. *be sensible of,* -wa -tambuzi. **sensitive** *adj.* -epesi kuhisi. **~ organ**, ungo hisishi: ungo ambalo lina vipokezi hisishi viitikiavyo viamshi katika mazingira na kupeleka taarifa kwenye ubongo.

**sensual** /'sɛnsjʊəl/ *adj.* -a ashiki; -tamanifu; -a kupenda anasa.

**sentence** /'sentəns/ *n.* sentensi; hukumu; fatwa; maamuzi. *v.t.* hukumu; kata hukumu.

**sentiment** /'sentɪmənt/ *n.* maono; hisia; mawazo; pendo; shauku; maoni. **~al** *adj.* -epesi wa hisia; -a kuchochea hisia; -a hisia. **~ality** *n.* wepesi wa kuibuka hisia.

**sentinel, sentry** /'sɛntɪn(ə)l/ *n.* askari wa zamu. **sentry-box** *n.* kibanda cha mlinzi. **sentry-go** *n.* wajibu wa mlinzi.

**sepal** /'sɛp(ə)l/ *n.* sepali.

**separate** /'seprət/ *adj.* mbalimbali; -liotengwa; -liotengana; -liogawanyika; -moja -moja. *v.t./i.* tenga; tenganisha; achana; farakana. **separable** *adj.* -a kutengeka; -a kugawanyika. **separation** *n.* utengano; mfarakano.

**September** /sep'tembə(r)/ *n.* Septemba: mwezi wa tisa wa mwaka wa kizungu.

**septic** /'sɛptɪk/ *adj.* -lioambukizwa; -a kuoza. *a ~ tank,* tangi la maji machafu.

**sepulchre** /'sɛp(ə)lkə/ *n.* kaburi lililochongwa kwenye mwamba. **sepulchral** *adj.* -a kaburi; -a maziko; -a majonzi.

**sequel** /'si:kwəl/ *n.* matokeo; mfuatano; matukio ya baadaye; katika hadithi ya pili lakini juu ya wahusika wa hadithi walewale.

**sequence** /'si:kwəns/ *n.* utaratibu; mfululizo; mwandamano; mfuatano.

**serene** /sə'ri:n/ *adj.* -eupe; safi; -liotakata; shwari; -tulivu. **~ly** *adv.* shwari. **serenity** *n.* utulivu; shwari.

**serf** /sɜ:f/ *n.* mtumwa. **~dom** *n.* utumwa.

**sergeant** /'sɑ:dʒ(ə)nt/ *n.* sajini. **~ major** *n.* sajini-meja.

**serial** /'sɪəriəl/ *adj.* -a mfululizo; -a sehemu ya.

**series** /'sɪəri:z/ *n.* mfuatano; mwandamano; mfululizo; safu; mfulizo.

**serious** /'sɪəriəs/ *adj.* -siocheka; -a kufikiri; -a maana; -kubwa; -a kweli; -enye hali mbaya; -a dhati. **~ly** *adv.* sana; kwa dhati. **~ness** *n.* uzito; ukweli.

**sermon** /'sɜ:mən/ *n.* hotuba; mahubiri.

**serpent** /sɜ:pənt/ *n.* nyoka. **~ine** *adj.* -enye mapindi.

**serum** /'sɪərəm/ *n.* damaji: ute mweupe wa damu; chanjo ya dawa.

**serval** /'sə:v(ə)l/ *n.* fungo.

**servant** /'sɜ:vənt/ *n.* mtumishi; hadimu; boi.

**serve** /sɜ:v/ *v.t./i.* tumikia; hudumia; tendea kazi; tenda kazi; faa mahali pa; tendea; faa; pakua; andalia; fungwa; hati za kisheria; auni; saidia; anzisha. *This box ~d as a seat,* sanduku hili lilikuwa kiti. *They ~d him shamefully,* walimuaibisha. *It ~s you right,* stahili yako. *~ up,* pakua; andalia. *~ one's time,* maliza muda wa kazi. *~ time,* fungwa.

**service** /'sɜ:vɪs/ *n.* utumishi; huduma; uwasilishaji; fadhila; msaada; sala; ibada; ukaguzi;

kuanzisha mchezo. *the fighting services*, ujeshi. *on active service*, jeshini. *service dress*, mavazi ya kijeshi. *the telephone service*, huduma za simu. *a tea service*,seti ya vyombo vya chai. *v.t.* tengeneza; tunza. **~able** *adj.* nayotumika; -a kufaa; -enye manufaa; -zima.

**server** /'sɜ:və(r)/ *n.* kompyuta hudumizi, yaani kompyuta inayotoa huduma kwa kompyuta nyingine; seva.

**serviette** /ˌsɜ:vi'et/ *n.* kipangusia mdomo, mikono.

**session** /'seʃn/ *n.* baraza; kipindi; muhula wa masomo; kikao.

**set** /set/ *n.* seti; kundi la watu; mwelekeo; mkao; wasifu; machweo; chipukizi; mandhari ya filamu au mchezo. *v.t./i.* (**set**) tua; chwa; shuka; sababisha; weka; tunga; rekebisha; unganisha; tengeneza. ~ *about one's work*, ~ *about doing sth.*, anza kazi; anza kufanya jambo. ~ *forth*, shika njia; ondoka. ~ *off*, shika njia; ondoka; ripua. ~ *sb. off laughing*, chekesha . ~ *(up)on sb.*, shambulia. ~ *sb. or sth. on*, himiza. ~ *out*, ondoka; shika njia. ~ *to*, anza kufanya jambo. ~ *up*, anzisha. ~ *sth. up*, anzisha; panga herufi za chapa. ~ *a bone*, unga mfupa. ~ *a clock*, rekebisha saa. ~ *sb. an example*, wa mfano kwa mtu. *I have never ~ eyes on him*, sijapata kumuona kamwe. ~ *a fashion*, anzisha mtindo. ~ *fire (a light) to sth.*, choma; tia moto; washa. ~ *one's heart on (sth.)*, tamani sana. ~ *a hen*, atamisha; lazia mayai. ~ *the pace*, rakibu mwendo. ~ *sail*, tweka. ~ *one's teeth*, kaza meno. ~ *a trap*, tega. ~ *to music*, tia lahani; tia sauti nyimbo. ~ *fair*, njema. ~ *fast*, -liokazwa sana. *a ~ time (date)*, wakati au tarehe maalumu. *a ~ smile*, uso wa bashasha. ~ *opinion*, wazo thabiti. *a wireless ~*, simu. *make a dead ~ at sb.*, jipendekeza; shambulia. *make a dead ~ at sth.*, dhamiria jambo. **~back** *n.* kikwazo; pingamizi; mgogoro; kizuizi. **~ square** *n.* kiguni. **~ting** *n.* mandhari: mahali pa matukio ya kazi ya fasihi.

**settle** /'setl/ *n.* benchi; kiti kirefu. *v.t./i.* fanya makazi; ishi; lowea; lipa deni; amua; hukumu; kata shauri; suluhisha; patanisha; tua; shuka; didimia. ~ *in the country*, ishi mashambani. *the Dutch ~d in South Africa*, Wadachi walilowea Afrika ya Kusini. **~ment** *n.* mapatano; mwafaka; suluhu; makazi;. **~r** *n.* mlowezi.

**seven** /'sevn/ *n./adj.* saba. **~th** *n./adj.* -a saba. *be in the ~th heaven*, furahi kabisa. **~teen** *n./adj.* kumi na saba. **~ty** *n./adj.* sabini. **~tieth** *n./adj.* -a sabini.

**sever** /'sevə(r)/ *v.t.* kata; vunja. *v.i.* katika; vunjika.

**several** /'sevrəl/ *adj.* kadhaa; -moja -moja; kila -moja.

**severe** /sɪ'vɪə(r)/ *adj.* bila huruma; -kali; -enye kuhitaji uvumilivu. **~ly** *adv.* kwa ukali. **severity** *n.* ukali; uzito.

**sew** /səʊ/ *v.t./i.* (**sewed**, **sewn**) shona. **~ing** *n.* mshono; ushoni. **~ing-machine** *n.* cherehani.

**sewage** /'su:ɪdʒ/ *n.* maji machafu.

**sewer** /'su:ə(r)/ *n.* mfereji wa maji machafu. **sewerage** *n.* utaratibu wa kuweka mifereji ya maji machafu.

**sex** /seks/ *n.* jinsia; uke; uume; mapenzi; kujamiiana. ~ *cell*, seli jinsia: seli ya uzazi yenye idadi haploidi ya chembeuzi kwenye kiini chake. **~ chromosomes,** chembeuzi jinsia: jozi ya chembe-uzi kwenye kiini cha seli ambayo huamua jinsia kuwa aidha ya kike au ya kiume. **~ual** *adj.* -a jinsia; -a mapenzi; -a kujamiiana. **~ intercourse**, jimai. **~ reproduction**, uzaliano kijinsia: uzaliano ambao dume na jike hushirikiana. **~ually transmitted disease**, maradhi ya zinaa: ugonjwa wowote unaoambukizwa kwa jimai au zinaa.

**shabby** /'ʃæbi/ *adj.* chakavu; -liovaa midabwada; -baya.

**shabbily** /'ʃæbɪli/ *adv.* kibahili;

kiovyoovyo.
**shade** /ʃeɪd/ *n.* kivuli; giza; utusitusi. *sun ~,* mwamvuli. *v.t./i.* tia kivuli; kinga jua au joto; tia giza.
**shady** /'ʃeɪdi/ *adj.* a kivuli; danganyifu; -a hila.
**shadow** /'ʃædəʊ/ *n.* giza; kivuli; utusitusi; njonzi; dalili. *without a ~ of doubt,* bila ya shaka hata chembe. *v.t.* tia giza; tia kivuli; fuata kwa siri; vizia.
**shaft** /ʃɑ:ft/ *n.* mpini; wano; shina; dohani; shimo; mtaimbo; mwanzi. *propeller ~,* mtaimbo endeshi.
**shah** /ʃɑ:/ *n.* shaha: mtawala wa zamani wa Irani.
**shake** /ʃeɪk/ *n.* mtikiso; tetemeko; msukosuko. *v.t./i.* (**shook**, **shaken**) tikisa; tikisika; tetemeka; tetemesha; tukuta; tingishika; tingisha; shtua. *~ hands (with sb.),* peana mikono. *~ off,* pukusa; epuka; ondoa; kung'uta; kwepa.
**shaky** /'ʃeɪki/ *adj.* dhaifu; -a kutikisika; sio imara; -sioaminika; sio salama.
**shale** /ʃeɪl/ *n.* mwambatope. *~ oil,* mafuta ya mwambatope.
**shall** /ʃəl/ *v. aux.* (**should**) /ʃʊd/ -ta-. *I ~ go,* nitakwenda.
**shallow** /'ʃæləʊ/ *adj.* -a kina kifupi. *(fig.)* -a juujuu; -sio makini.
**sham** /ʃæm/ *n.* mnafiki; unafiki; laghai. *v.t./i.* (**-mm-**) jifanya; jisingizia; iga; jigeuza. *~ sickness,* jisingizia ugonjwa. *adj.* bandia; -a kuiga; a uwongo. *a ~ fight,* mchezo wa vita.
**shame** /ʃeɪm/ *n.* haya; soni; aibu; fedheha; tahayuri. *It's a ~ to make fun of the old man,* ni aibu kumtania mzee. *v.t.* aibisha; fedhehesha; tia haya; tahayarisha. **~faced** *adj.* -enye haya nyingi. **~ful** *adj.* -a kutahayarisha; a kuaibisha; -a fedheha. **~less** *adj.* bila haya; -pujufu; -kavu wa macho.
**shape** /ʃeɪp/ *n.* umbo; sura; muundo; tambo; kalibu. *take ~,* tengenea. *v.t./i.* tengeneza; umba; tengenea; pata umbo; unda. **~less** *adj.* bila umbo zuri; -sio sura nzuri. **~ly** *adj.* -zuri; -enye umbo la kupendeza.
**share** /ʃeə(r)/ *n.* hisa; fungu; sehemu; mgawo. *go ~s in,* changa bia. *v.t./i.* gawa; gawanya; gawana; shirikiana; shiriki. **~holder** *n.* mshirika; mhisa; mshikadau.


shark

**shark** /ʃɑ:k/ *n.* papa; *(fig.)* ayari; laghai; mdanganyifu; mla riba.
**sharp** /ʃɑ:p/ *adj.* -kali; -enye ncha; wazi; dhahiri; -a kuonekana vizuri; -elekevu; hodari; -epesi kuona; -chungu; -embamba; -danganyifu; laghai. *adv.* ghafla; kamili. **~en** *v.t./i.* chonga; chongoa; chongoka; noa. **~er** *n.* ayari. **~ener** *n.* kichongeo.
**shatter** /'ʃætə(r)/ *v.t./i.* vunjavunja; vunjikavunjika; haribu kabisa.
**shave** /ʃeɪv/ *n.* kunyoa; unyoaji. *v.t.* (**shaved**, **shaven**) nyoa; lainisha kwa landa; ambaa. *a close (narrow) ~,* kuwa karibu sana na. *He had a narrow ~ from being killed,* nusura auwawe. **~n** *adj.* -lionyolewa. *clean-~, well-~,* -lionyolewa vizuri. **~r** *n.* mashine ya kunyolea. **shavings** *n.* makapi ya mbao.
**she** /ʃi/ *pron.* yeye (mwanamke). *adj.* -a kike, jike: *~-goat,* mbuzi jike.
**sheaf** /ʃi:f/ *n.* (**sheaves**) **1.** mashuke ya nafaka yaliyowekwa pamoja. **2.** gandatita: vitu kadhaa vilivyofungwa pamoja.
**shear** /ʃɪə(r)/ *v.t.* (**shorn**) kata manyoya ya kondoo. **~s** *n.* mkasi mkubwa.
**sheath** /ʃi:ðz, ʃi:s/) *n.* ala ya kuhifadhia kitu chenye makali au ncha. *contraceptive ~,* kondomu. **~e** *v.t.* futika; chomeka katika ala; funika.
**shed**[1] /ʃed/ *n.* banda; kibanda.
**shed**[2] /ʃed/ *v.t.* (**shed**, **-dd-**) nyonyoa; bambatua; mwaga; toa; ondoa; vua; tawanya; eneza. *a fire that ~s warmth,* moto unaotoa joto; *~ light on, (fig.)* toa mwanga.
**sheep** /ʃi:p/ *n.* (**sheep**) kondoo. **~dog** *n.* mbwa alindaye na kuchunga kondoo. *~ adj.* -enye haya; -a woga; -a kuona aibu.

**sheer** /ʃiə(r)/ *adv.* kabisa; moja kwa moja. *adj.* tu; -a wima; laini. *v.i.* -enda upande; acha uelekeo.
**sheet** /ʃi:t/ *n.* shuka; shiti; karatasi.
**shelf** /ʃelf/ *n.* (**shelves**) rafu; mwamba.
**shelve** /ʃelv/ *v.t./t.* weka, panga katika rafu; *(fig.)* ahirisha; weka kando; teremka taratibu.
**shell** /ʃel/ *n.* ganda; gome; risasi; kombora. ~ *fish,* jamii ya samakigamba. *v.t.* menya; bambatua; ambua; rusha kombora. ~ *out, (colloq.)* lipa; lipia; gharimia. **shell shock** *n.* kichaa kinachotokana na mitaharuki ya vita.
**shelter** /'ʃeltə(r)/ *n.* hifadhi; kimbilio; kinga; mahali pa kujisitiri. *v.t./i.* funika; linda; hifadhi; jificha; jilinda.
**shepherd** /'ʃepəd/ *n.* mchunga kondoo. *v.t.* chunga; ongoza.
**shield** /ʃi:ld/ *n.* ngao; ulinzi; kinga. *v.t.* linda; hifadhi.
**shift** /ʃɪft/ *n.* shifti; zamu; mabadiliko; shifti: gauni isiyo marinda; mkono wa gia. *v.t./i.* geuza; hamisha; hamia; sogeza; sogea; ghairi; badili. ~ *for oneself,* jitegemea. *He is on night ~,* ana zamu ya usiku. *He is doing an eight-hour ~,* zamu yake hudumu masaa manane. *make ~,* jitahidi; tumia maarifa. **~less** *adj.* -siojimudu; -zembe; -vivu. **~y** *adj.* -a hila; -danganyifu.
**shilling** /'ʃɪlɪŋ/ *n.* shilingi. *take the queen's ~,* jiandikisha uaskari.
**shin** /ʃɪn/ *n.* muundi. **~-guard** kikinga muundi.
**shine** /ʃaɪn/ *n.* uangavu; mng'ao; rangi ya viatu. *v.i./t.* (**shone**) ng'aa; waka; waa; angaza; ng'arisha. *(fig.)* -wa na fahari; -wa mashuhuri.
**shiny** /'ʃɪni/ *adj.* -enye kung'aa.
**shingle**[1] /'ʃɪngl/ *n.* kokoto.
**shingle**[2] /'ʃɪngl/ *n.* ubao mwembamba wa kuezekea na hutumika kama vigae.
**ship** /ʃɪp/ *n.* jahazi; meli. *v.t./i.* pakia katika chombo cha baharini; peleka kwa chombo cha baharini. **~mate** *n.* baharia mwenza. **~ment** *n.* upakiaji wa shehena melini; shehena. **~per** *n.* msafirishaji shehena. **~ping** *n.* meli zote za nchi. **~shape** *adj.* barabara; safi; sawasawa. **~wreck** *n.* kupanda mwamba; kuzama meli. **~yard** *n.* kiwanda cha meli.
**shire** /'ʃaɪə(r)/ *n.* mkoa. ~ *horse,* farasi wa kuvuta mkokoteni.
**shirt** /ʃɜ:t/ *n.* shati. *He was in his ~sleeves,* alikuwa kavaa shati, yaani bila ya koti.
**shiver** /'ʃɪvə(r)/ *v.i.* tetemeka.
**shock** /ʃɑk/ *n.* shindo; kishindo; mshtuko; mrusho. *v.t.* shtusha; fadhaisha. **~ing** *adj.* -baya sana; -a kushtusha.
**shoe** /ʃu:/ *n.* kiatu; kipande cha breki. *v.t.* valisha kiatu.


**shoe lace**

**shoot** /ʃu:t/ *n.* chipukizi; maporomoko ya mto; kundi la wawindaji. *v.t./i.* (**shot**) pita kasi; tupa; vurumisha; ruka; panda sana; chipua; mea; choma; shambulia ghafla; piga mzinga, risasi au upinde. *The flames are ~ing up from the burning house,* ndimi za moto zinaruka kutoka nyumba inayoungua. *The snake ~s out its tongue,* nyoka atoatoa ulimi wake. **~ing star** *n.* kimondo.
**shop** /ʃɒp/ *n.* duka; kiwanda; karakana; utaalamu; ujuzi; kazi. *closed ~,* kiwanda ambamo wanachama tu hukubaliwa kufanya kazi. *v.i.* (**-pp-**) nunua; enda dukani. *go ~ping,* enda dukani. *have some ~ping to do,* -wa na mahitaji ya vitu dukani. **~keeper** *n.* mwenye duka. **~steward** *n.* mjumbe wa wafanyakazi kiwandani.
**shore** /ʃɔ:(r)/ *n.* pwani; ufukwe. *on ~,* pwani.
**short** /ʃɔ:t/ *adj.* -fupi; -pungufu; haba; adimu. *The shopkeeper was fined for giving ~ measure,* mwenye duka alitozwa faini kwa kupunja. *This factory is working ~ time,* kiwanda hiki hufanya kazi muda mfupi. *a ~ cut,* njia ya mkato. *be ~ of,* pungukiwa na. *for ~,* kwa

kufupisha. *in ~,* kwa ufupi. *adv.* mara; ghafla; mapema. *stop ~, pull up ~,* simama ghafla. *come (fall) ~ of,* -wa pungufu. *~ of,* bila. **~age** *n.* upungufu; uchache; uhaba. **~circuit** *n.* saketi mkato: fanya umeme kufuata njia ya ukinzani mdogo wenye dosari. **~coming** *n.* ila; kasoro; dosari. **~en** *v.t./i.* fupisha; kata; punguka; pungua. **~hand** *n.* hatimkato. **~-handed** *adj.* -enye wasaidizi wachache. **~-lived** *adj.* -liodumu muda mfupi. **~ly** *adv.* mara moja; karibu; punde; kwa mkato; kwa ufupi. *~ after,* baadaye kidogo. **~ness** *n.* ufupi. **~s** *n.* suruali fupi; kaptura. **~-sighted** *adj.* -sioona mbali; si -a busara; -a kutofikiria mbele. **~-tempered** *adj.* -epesi wa hasira. **~-winded** *adj.* enye pumu; -a kutweta; -enye kuishiwa na pumzi haraka.

**shot** /ʃɒt/ *n.* mlio wa bunduki, mzinga, bastola, etc.; jaribio la kufanya jambo; shuti; picha; risasi; mpiga shabaha. *He was off like a ~,* alichomoka shoti. *He is a good ~,* ni mlenga shabaha mzuri. **~gun** *n.* aina ya bunduki ya kupiga masafa mafupi.

**shoulder** /ˈʃəʊldə(r)/ *n.* bega. *straight from the ~, (fig.)* waziwazi; bila kuficha. *v.t.* chukua begani; piga kikumbo. **~-blade** *n.* mtulinga; bega.

**shout** /ʃaut/ *n.* ukelele; yowe. *v.i./t.* piga kelele; paaza sauti.

**shovel** /ˈʃʌvl/ *n.* pauro; sepetu. *v.t.* pakua; ondoa; chota; safisha kwa pauro.

**show** /ʃəʊ/ *n.* kuonyesha; maonyesho; tamasha; sura; hali; dalili; maringo; kujionyesha. *v.t./i.* (**~ed, shown**) onyesha; elekeza; dhihirisha. *~ sb. in,* karibisha ndani. *~ sb. out,* sindikiza. *~ off,* jifaharisha. *~ up, (colloq.)* hudhuria. *~ sb. up,* chongea. *A man is ~n up by his own tongue,* mtu huchongewa na kauli yake. *~ fight,* taka kupigana. *~ one's hand,* dhihirisha nia ya mtu. *~ the way, (fig.)* onyesha mfano. **~down** *n.* kudhihirisha nia au uwezo wa mtu. **~y** *adj.* -shaufu; -limbwende; -a fahari. **~ily** *adv.* kwa fahari.

**shower** /ˈʃaʊə/ *n.* manyunyu; wingi; neema.

**shred** /ʃred/ *n.* uchane; kipande. *be torn to ~s,* raruka kabisa. *There is not a ~ of evidence,* hakuna ushahidi hata chembe.

**shrill** /ʃrɪl/ *adj.* (kwa sauti) embamba; kali.

**shrine** /ʃraɪn/ *n.* sanduku lenye mabaki matakatifu; mahali patakatifu; madhabahu; mzimu.

**shrink** /ʃrɪŋk/ *v.i./t.* (**shrank, shrunk**) nywea; (kwa kitambaa) ruka; jikunyata; kunyata; jitenga. **~age** *n.* unyweaji; urukaji wa kitambaa.

**shrivel** /ˈʃrɪvl/ *v.t./i.* (**-ll-**) nyauka; sinyaa; kunyaa.

**shroud** /ʃraʊd/ *n.* sanda; mtandio wa kike; kifuniko.

**shrug** /ʃrʌg/ *n.* kukweza mabega. *v.t./i.* (**-gg-**) kweza mabega.

**shudder** /ˈʃʌdə(r)/ *n.* mtetemeko. *v.i.* tetemeka.

**shuffle** /ʃʌfl/ *v.i./t.* burura; kokoteza miguu; changa; pigia karata; boronga; tapatapa.

**shun** /ʃʌn/ *v.t.* (**-nn-**) epuka; jitenga na.

**shunt** /ʃʌnt/ *v.t./i.* peleka njia nyingine; geuza njia; kwepa; ahirisha.

**shut** /ʃʌt/ *v.t./i.* (**shut, -tt-**) funga; fumba; bana. **~ter** *n.* shata: mlango wa dirisha; kilango cha kamera.

**shuttle** /ˈʃʌtl/ *n.* babili. **~cock** *n.* mpira wa vinyoya.

**shy** /ʃaɪ/ *adj.* -enye haya; -oga. **~ly** *adv.* kwa haya. **~ness** *n.* haya; soni.

**SI unit** *n.* ufupisho wa **international units of measurements**: vizio vya kimataifa vya vipimo vinavyojumuisha vizio saba vya msingi ambavyo ni mita, kilogramu, sekunde, ampea, kelvini, kandela na moli.

**sick** /sɪk/ *adj.* -gonjwa; -enye mawazo machafu; -enye majonzi. *be ~,* tapika; ugua. *feel ~,* sikia kichefuchefu. *(colloq.) be ~ of,* chukizwa na. **~en** *v.i./t.* kirihi;

chusha; chukiza; chosha. *be ~ening for,* anza kuugua. **~ening** *adj.* -a kuchukiza; -a kuchosha. **~ly** *adj.* -a kutapisha; dhaifu; -enye kuchefua; -enye kukirihi; -enye kutia maradhi.


sickle

**sickle** /'sɪkl/ *n.* mundu.

**side** /saɪd/ *n.* upande; pembeni; ubavu; nasaba. *on all ~s, on every ~,* pande zote. *by the ~ of, (fig.)* kwa kulinganisha na. *~ by ~,* bega kwa bega; sambamba; sako kwa bako. *put sth. on one ~,* tenga. *take ~s with,* unga mkono. *v.i. ~ with,* shirikiana na; unga mkono. **~board** *n.* meza au kabati la vyombo. **~-car** *n.* kigari cha pikipiki. **~line** *n.* mstari wa pembeni; kazi ya ziada; bidhaa za ziada. **~-track** *n.* ujia wa kando. *v.t.* epa; pita kando; ahirisha. **~ways** *adv.* kwa upande.

**siding** /saɪdɪŋ/ *n.* njia ndogo ya gari moshi.

**siege** /si:dʒ/ *n.* uzingiaji. *lay ~ to,* zingia katika vita.

**sierra** /sɪ'ɛrə, sɪ'ɛ:rə/ *n.* mlolongo wa milima.

**sieve** /sɪv/ *n.* chungio; ungo; tunga.

**sift** /sɪft/ *v.t.* chunga; chekecha; peta; chungua; pekua.

**sigh** /saɪ/ *n.* kushusha pumzi. *v.i.* shusha pumzi. *~ for,* tamani sana.

**sight** /saɪt/ *n.* uwezo wa kuona; kuona; kutazama; mtazamo; dira; shabaha. *lose one's ~,* pofuka. *have near ~,* ona vitu vya karibu tu. *have long ~,* ona vitu vya mbali tu. *know sb. only by ~,* jua kwa sura tu. *lose ~ of,* -toona. *(fig.)* -tojua; tokumbuka. *at (on) ~,* papohapo. *be out of ~,* toweka; toonekana. *do what is right in your own ~,* tenda haki kwa uono wako. *a ~, (colloq.)* kinyago; kichekesho. *She looks a real ~ in that old dress,* aonekana kinyago akivaa kanzu ile kuukuu. *v.t.* ona; angalia; tazama; lenga shabaha. *catch ~ of,* ona. **~seer** *n.* mtalii.

**sign** /saɪn/ *n.* dalili; alama; ishara. *~s of suffering are to be seen on his face,* dalili za mateso zaonekana usoni mwake. **~board** *n.* kibao au ubao wenye taarifa au maelekezo. *v.t./i.* tia dole; tia saini; ashiria. **~post** *n.* kibao cha kuonyesha njia. **~al** *n.* alama; ishara; dalili; mawimbi ya sauti. *v.t.* ashiria; toa ishara au saini. *adj.* mashuhuri; kubwa; -ya maana. **~ature** *n.* sahihi; saini; dole. **~ature tune** wimbo wa idhaa. **~ificance** *n.* maana; umuhimu. **~ificant** *adj.* -enye umuhimu; -enye maana; -kuu. **~ification** *n.* kumaanisha; kuashiria; maana. **~ify** *v.t./i.* onyesha; -wa na maana; -wa na umuhimu. *~ your approval,* onyesha kuwa umekubali. *It ~ifies much,* yaashiria kuwa ni kitu cha maana kubwa.

**silence** /'saɪləns/ *n.* kimya; unyamavu. *v.t.* nyamazisha. **~r** *n.* kizuia kelele.

**silent** /'saɪlənt/ *adj.* -a kimya; nyamavu. **silently** /'saɪləntli/ *adv.* kimyakimya.

**silica** /'sɪlɪkə/ *n.* silika: silikoni dioksidi, dutu ngumu sana nyeupe. **~te** *n.* mchanganyiko wa madini yenye silika.

**silicon** /'sɪlɪkən/ *n.* silikoni: elementi simetali enye maumbo fuwelia na hobela.

**silicone** /'sɪlɪkəʊn/ *n.* kampaundi zozote za kioganiki za silikoni ambazo hutumika sana katika rangi, vanishi na vilainishi.

**silk** /sɪlk/ *n.* hariri; vazi la hariri. **~en** *adj.* kama hariri; -a hariri; laini. *a ~ voice,* sauti nyororo. **~worm** *n.* nondo wa hariri. **~y** *adj.* -ororo; laini.

**silly** /'sɪli/ *adj.* -pumbavu; -puuzi; jinga. **silliness** *n.* upuuzi; upumbavu; ujinga.

**silo** /'sʌɪləʊ/ *n.* silo: ghala ya kuhifadhi chakula cha wanyama; kituo cha kurushia makombora toka chini ya ardhi.

**silt** /sɪlt/ *n.* matope; mashapo ya mto.

**silver** /'sɪlvə(r)/ *n.* fedha; sarafu; vitu vya fedha; rangi ya fedha. **~ jubilee** maadhimisho ya miaka 25.

**~y** *adj.* kama fedha; -a kung'aa; -eupe.

**similar** /'sɪmələ(r)/ *adj.* -a hali moja; -a kulandana; -a hali moja. **~ity** *n.* mfanano; mlandano. **~ly** *adv.* hali kadhalika; vivyohivyo; vilevile.

**simile** /'sɪməli/ *n.* tashbiha: usemi unaolinganisha kwa kutumia maneno ya ulinganishi. *As brave as a lion*, jasiri kama simba.

**simple** /'sɪmpl/ *adj.* rahisi; sahili; -siopambwa; -epesi; nyofu; -a kudanganyika kwa urahisi. **~ton** *n.* juha; punguani. **simplicity** *n.* wepesi; usahili; urahisi. **simplify** *v.t.* fanya -epesi; rahisisha.

**simply** /'sɪmpli/ *adv.* kirahisi; kabisa; hasa; kikawaida.

**simultaneous** /ˌsɪm(ə)l'teɪnɪəs/ *adj.* -a wakati uleule; papo hapo; palepale. **~ly** *adv.* sawia; palepale.

**sin** /sɪn/ *n.* dhambi; uovu. *He had sinned and repented*, alifanya dhambi na alitubia. *v.i.* (**-nn-**) fanya dhambi; kosa. **~ful** *adj.* a dhambi; -ovu. **~ner** *n.* mwenye dhambi; mkosaji.

**since** /sɪns/ *adv.* tangu wakati ule; tena. *prep.* tangu; baada ya; toka; tokea. *conj.* kwa kuwa; maadam; tangu.

**sincere** /sɪn'sɪə(r)/ *adj.* -a kweli; -enye moyo safi; -aminifu. **~ly** *adv.* kwa kweli; kwa moyo safi; kwa unyofu. **sincerity** *n.* uaminifu; unyofu; ukweli.

**sinew** /'sɪnju:/ *n.* mkano; nguvu; uwezo; misuli. *~s of war*, gharama za zana za vita.

**sing** /sɪŋ/ *v.i.* (**sang**, **sung**) imba; ghani; vuma. *~ out*, ita kwa nguvu. *~ up*, imba kwa sauti. *~ of*, simulia kwa ushairi. **~song** *n.* sauti doro. *He read in a ~song*, alisoma kwa sauti doro.

**singe** /sɪndʒ/ *v.t.* unguza; choma.

**single** /'sɪŋgl/ *n.* mchezo wa wachezaji mmoja mmoja; pointi moja; tiketi ya kwenda tu. *adj.* -moja; -moja tu; peke yake; -a mtu mmoja tu; -siooa; -sioolewa. **~-handed** *adv.* bila msaada. **~t** *n.* fulana. **singly** *adv.* -moja -moja; pekee.

**singular** /'sɪŋgjələ(r)/ *n.* umoja. *adj.* -sio -a kawaida; -a ajabu; -a kipekee; (kwa sarufi) -a umoja.

**sinister** /'sɪnɪstə(r)/ *adj.* -a kisirani; -a shari; -baya; -a kuogofya.

**sink** /sɪŋk/ *n.* sinki: karo ya maji machafu. *v.i./t.* (**sank**, **sunk**) zama; zamisha; tosa; chopea; didimia; chimba; zamisha; shuka. *(fig.) His heart sank at the news*, alihuzunika sana aliposikia habari ile. *The rain sank well into the dry ground*, mvua iliingia vyema ardhini. *The warning sank into his mind*, alitilia maanani onyo alilopewa. **~ing** *adj.* enye kuzama. *~ feeling*, hisia ya kukata tamaa au woga. *n.* kuzama.

**sip** /sɪp/ *n.* chubuo. *v.t./i.* (**-pp-**) chubua: -nywa kidogo kidogo.



siphon

**siphon** /'sʌɪf(ə)n/ *n.* mrija; kifyonzaji; neli. *v.t./i.* nyonya; fyonza.

**sir** /sɜ:(r)/ *n.* bwana; mheshimiwa.

**siren** /'saɪrən/ *n.* king'ora; honi; mwanamke shawishi.

**sirloin** /'sɜ:lɔɪn/ *n.* sarara: minofu iliyopakana na uti wa mgongo.

**sisal** /'sʌɪs(ə)l/ *n.* mkonge; katani.

**sister** /'sɪstə(r)/ *n.* dada; mtawa; sista; mwenza. *They were ~ships*, zilikuwa meli za aina moja. **~hood** *n.* udada; utawa. **~-in-law** *n.* shemeji; wifi.

**sit** /sɪt/ *v.t./i.* kaa; keti; fanya mkutano; atamia. *~ down under*, vumilia. *~ for*, wakilisha. *~ for an examination*, fanya mtihani. *~ on a committee*, mwanakamati. *~ up*, kesha. *make sb. ~ up*, shtua. **~ting** *n.* mkutano; kikao; baraza; mkao; mkupuo. *finish a book at one ~*, maliza kitabu kwa mkupuo mmoja.

**site** /saɪt/ *n.* saiti; mahali; eneo. *the ~ of the battle*, eneo la vita; *the ~ for the new school*, kiwanja cha skuli mpya.

**situated** /'sɪtʃueɪtɪd/ *adj.* -liopo mahali. *It is ~ in Egypt*, iko Misri. *I*

*am rather awkwardly* ~, nimo katika shida kidogo.
**situation** /ˌsɪtʃu'eɪʃn/ *n.* mahali; hali; kazi.
**six** /sɪks/ *n./adj.* sita. *at ~es and sevens,* -liochanganyikiwa. **~teen** *n./adj.* kumi na sita. **~ty** *n./adj.* sitini.
**size**[1] /saɪz/ *n.* ukubwa; kipimo; kiasi; saizi. *v.t.* panga kwa saizi. *~ up,* tathmini; pima. *~ up the situation,* pima hali. **~able** *adj.* -kubwa kidogo.
**size**[2] /saɪz/ *n.* gundi.
**skeleton** /'skelɪtn/ *n.* kiunzi cha mifupa. *~ key,* ufunguo malaya.


skeleton

**sketch** /sketʃ/ *n.* mchoro; kielelezo; muhtasari. *v.t./i.* andika; chora; eleza kwa ufupi.
**ski** /ski:/ *n.* skii; relitheluji.
**skid** /skɪd/ *v.i.* teleza; serereka.


skiing

**skill** /skɪl/ *n.* ustadi; ubingwa; ufundi; umahiri. **~ed** *adj.* stadi. **skilful** *adj.* -bingwa; stadi; mahiri. **skilfully** *adv.* kistadi; kimahiri.
**skim** /skɪm/ *v.t./i.* **(-mm-)** engua; soma kwa haraka; pitia upesi juujuu; ambaa. **~mer** *n.* kichujio; mwiko. **~ milk** *n.* maziwa yaliyoenguliwa.
**skin** /skɪn/ *n.* ngozi; ganda; gome; utando. *v.t./i.* chuna. **~-deep** *adj.* -a juujuu; -enye unafiki. **~flint** *n.* bahili hasa kwa wenziwe. **~ny** *adj.* -liokonda.


skiping

**skip** /skɪp/ *v.i./t.* rukaruka; ruka. *~ out of the way,* ondoka njiani. **skipper** *n.* nahodha; rubani.
**skirt** /skɜ:t/ *n.* sketi; mpaka; ukingo; pindo. *v.t.* wa mpakani; pakana na; ambaa.
**skull** /skʌl/ *n.* fuvu la kichwa.
**sky** /skaɪ/ *n.* mbingu; anga.


skirt

**~lark** *n.* ndege mdogo arukaye juu sana angani mwenye sauti nzuri.
**slab** /slæb/ *n.* slebu; namna ya kitu au jiwe bapa.
**slack** /slæk/ *n.* suruali; vumbi la makaa ya mawe; tanzi. *adj.* -legevu; -vivu; zembe; doro. *Business is ~,* biashara inadorora. *v.i.* legea; zembea. **~en** *v.t./i.* legeza; legea; punguza; pungua; zembea. **~er** *n.* *(colloq.)* mvivu; mzembe; mtegaji. **~ly** *adv.* kivivu; kizembe. **~ness** *n.* uvivu; ulegevu; uzembe.
**slaked lime** *n.* chokaa zimwe: chokaa iliyotiwa maji.
**slam** /slæm/ *n.* kishindo cha mlango uliofungwa kwa nguvu. *v.t./i.* funga mlango kwa kishindo.
**slang** /slæŋ/ *n.* simo; misimu; lugha ya mitaani. *v.t.* *(colloq.)* karipia vikali; tukana. **~y** *adj.* -a simo; -enye kupenda kutumia simo.
**slant** /slɑ:nt/ *n.* mwinamo. *v.i.* enda mshazari; inama; inamisha.
**slap** /slæp/ *n.* kofi. *v.t.* piga kofi; piga kibao; zaba kofi. *~down,* weka kwa kishindo. **~dash** *adj./adv.* bila hadhari; -a haraka.
**slash** /slæʃ/ *v.t./i.* tema; katakata; chanja; chapa; shutumu; punguza sana.
**slate** /sleɪt/ *n.* kigae; kibao; sleti. *(fig.)* *start with a clean ~,* anza upya.
**slaughter** /slɔ:tə(r)/ *n.* kuchinja; mauaji. *v.t.* chinja; ua kwa wingi. **~house** *n.* machinjioni.
**slave** /sleɪv/ *n.* mtumwa; hadimu. *He is a ~ to drink,* ni mtumwa wa ulevi. **~ trade**, biashara ya watumwa. **~r** *n.* mfanya biashara ya watumwa; meli ya watumwa. *v.i. ~ at,* fanya kazi kama punda. **~ry** *n.* utumwa.
**slavish** /'sleɪvɪʃ/ *adj.* kitumwa; -a kitumwa; -enye kukosa uhuru wa maamuzi.
**slay** /sleɪ/ *v.t.* (**slew**, **slain**) ua; chinja.
**sled sledge**[1] /sledʒ/ *n.* sleji: toroli ya kuteleza kwenye theluji.
**sledge**[2] /sledʒ/ *n.* nyundo kubwa nzito. *~hammer argument,* majadiliano makali.
**sleek** /sli:k/ *adj.* laini; -a kung'aa;

maridadi.




**sleep** /sli:p/ *n.* usingizi; kulala. *v.i.* (**slept**) lala. ~ *sth. off,* pona kwa kulala usingizi. *v.t.* laza; -wa na vitanda vya kutosha kwa. *This hotel can ~100 people,* wageni 100 waweza kulala katika hoteli hii. **~er** *n.* mlalaji; taruma la njia ya reli; kitanda katika treni. **~less** *adj.* -siopata usingizi. **~y** *adj.* -enye usingizi.

**sleeve** /sli:v/ *n.* mkono wa nguo. *laugh up one's ~* cheka kisirisiri *have something up one's ~,* -wa na mpango wa siri.

**sleigh** /sleɪ/ *n.* sleji inayokokotwa na farasi.

**slender** /'slendə(r)/ *adj.* -embamba; -dogo; -chache; haba.

**slice** /slaɪs/ *n.* slesi; cheche; mwiko bapa. *v.t.* kata slesi.

**slide** /slaɪd/ *n.* mtelezo; utelezi; kuteleza; slaidi. ~ *rule,* kikokotoo penyezi. *sliding scale,* kapani. *sliding seat,* kiti telezi. *v.t./i.* (**slid**) teleza; ingia polepole; penyeza. *The drawer of the cupboard ~s well,* mtoto wa kabati wateleza vyema. *Let things ~,* acha mambo yalivyo; telekeza.

**slight**[1] /slaɪt/ *adj.* -embamba; -dogo; kidogo. **~ly** *adv.* kidogo. *I'm ~ better today,* sijambo kidogo leo.

**slight**[2] /slaɪt/ *n.* twezo, bezo, dharau. *v.t.* dharau; tweza; beza.

**slim** /slɪm/ *adj.* -embamba; -dogo; haba.

**slime** /slaɪm/ *n.* kinamasi; kinamo; ute.

**slimy** /'slaɪmi/ *adj.* -a kuteleza kwa tope au ute.

**sling** /slɪŋ/ *n.* teo; kombeo; kitambaa cha kuzuilia mkono. *v.t.* (**slung**) tupa kwa teo. **~shot** *n.* panda; manati.

**slink** /slɪŋk/ *v.i.* (**slunk**) nyatia.

**slip** /slɪp/ *n.* utelezi; kujikwaa; kosa dogo; kuponyoka; foronya. *v.i./t.* (**-pp-**) ponyoka; nyatia; chopoka; serereka; teleza; penyeza; vaa; vua; kosea. ~ *(on, off)* vaa, vua upesi. *give sb. the ~,* epa kwa hila. ~ *of the pen (tongue),* kosa dogo la kimaandishi au la kilafudhi. **~per** *n.* kiatu chepesi. **~pery** *adj.* -telezi; laghai; nyeti. **~shod** *adj.* ovyoovyo.

**slit** /slɪt/ *n.* ufa; mwatuko; mfuo; mpasuko. *v.t.* pasua; chana; chanja.

**slogan** /'sləʊgən/ *n.* wito; maneno ya kuvutia katika utangazaji wa kitu fulani

**slop** /slɒp/ *n.* maji machafu. *v.i./t.* mwagika; mwaga; chezea maji machafu. **~py** *adj.* -a juujuu; -a ovyo; -a purukushani; -a uongo.

**slope** /sləʊp/ *n.* mteremko; mwinamo. *v.i./t.* inama; inamisha; teremka; fanya mteremko. ~ *arms,* -wa na bunduki begani.

**slot** /slɒt/ *n.* tundu jembamba; upenyo.

**sloth** /sləʊθ/ *n.* uvivu; uzembe; ulegevu.

**slow** /sləʊ/ *adj.* -a polepole; -a kukawia; -zito. *v.t./i.* punguza mwendo; punguka mwendo. **~ness** *n.* usiri.

**slug** *n.* aina ya konokono, koa.




**sluice** /slu:s/ *n.* mlizamu. ~*-gate,* mlango mlizamu. **~-valve**, vali mlizamu. *v.t.* mwagia maji; rowanisha; chekecha kwa kutumia maji. ~ *out,* osha kwa maji mengi.

**slum** /slʌm/ *n.* kibanda cha ovyo; mtaa wa vijumba ovyoovyo vya watu maskini.

**slumber** /'slʌmbə(r)/ *n/v.i.* usingizi; lala; sinzia.

**slump** /slʌmp/ *n.* mshuko wa ghafla wa bei; upungufu wa biashara wa ghafla. *v.i.* anguka ghafla; pungua ghafla.

**slur** /slɜ:(r)/ *n.* aibu; fedheha; kashfa. *v.t./i.* (**-rr-**) kokoteza maneno. ~ *over,* pitia upesi ili kuficha jambo.

**sly** /slaɪ/ *adj.* -janja; -danganyifu; -a mzaha; -bishi; -tundu.

**smack** /smæk/ *n.* kofi; kibao; mwaliko. *v.t.* piga kofi; zaba kibao. ~ *one's lips,* rambitia. *adv.* kwa kishindo; ghafla. *run ~ into a wall,* gonga ukuta ghafla.

**small** /smɔ:l/ *adj.* -dogo. *look (feel) ~,* ona haya; fedheheka. *~ change,* sarafu ndogondogo. *the ~ hours,* usiku wa manane. *~ talk,* soga; porojo. *on the ~ side,* -dogo mno. **~ arms** *n.* silaha nyepesi. **~pox** *n.* ndui; ugonjwa wa kupooza.

**smart**[1] /smɑ:t/ *n.* mwasho; kichomi; maumivu makali. *v.i./t.* washa; choma; chochota; ona uchungu.

**smart**[2] /smɑ:t/ *adj.* nadhifu; maridadi; hodari; -epesi; -kali; -a kisasa. *a ~ blow,* pigo kali. **~en** *v.t./i.* *~en up,* kwatua; jikwatua; himiza; shajiisha. *~en up the step,* chapuka. **~ly** *adv.* kimaridadi; hima; kwa akili. **~ness** *n.* unadhifu; wepesi; uhodari.

**smash** /smæʃ/ *n.* mvunjiko; kishindo; maangamizi. *v.t./i.* vunja; vunjika; shinda; angamiza.

**smear** /smɪə(r)/ *n.* waa; doa; mpako. *v.t./i.* paka; tia madoa; paka matope.

**smell** /smel/ *n.* harufu. *v.t.* (**smelt**) nusa; sikia harufu. *v.i.* toa harufu.

**smelt** /smelt/ *v.t.* yeyusha madini. **~ing** *n.* uyeyushaji (wa mbale): uziduaji wa metali kutoka kwenye mbale zake kwa njia ya mfanyi-kotendani unaohusisha joto.

**smile** /smaɪl/ *n.* tabasamu; kukenya. *v.i.* tabasamu; kenya. *~ on,* ridhia. *~ at,* furahia. **smilingly** *adv.* kwa furaha.

**smith** /smɪθ/ *n.* sonara; mhunzi. **~y** *n.* kiwanda cha mhunzi au sonara.

**smoke** /sməʊk/ *n.* moshi; mvuke; sigara. *end up in ~,* enda arijojo. *v.t./i.* toa moshi; fuka; vuta sigara; kausha kwa moshi; fukiza moshi. **~r** *n.* mvuta sigara; behewa la wavutaji. **smoky** *adj.* -enye moshi mwingi; kama moshi. **~less** *adj.* -siotoa moshi. **~screen** *n.* wingu la moshi la kuficha manowari au askari vitani. **~stack** *n.* bomba la moshi.

**smooth** /smu:ð/ *adj.* laini; shwari; sawa; mfuto; -liopendeka vizuri; rahisi; taratibu; -pole; -bembelezi. *v.t.* lainisha; sawazisha; piga landa; piga msasa; piga pasi. *~ away sb.'s objections,* lainisha mtu. **~ly** *adv.* bila taabu; kirahisi; kwa wepesi; bila kukwaruza. **~ness** *n.* ulaini; upole; usawa; urahisi. **~-faced** *adj.* *(fig.)* -zuri wa sura -baya wa tabia. **~-spoken, ~-tongued** *adj.* -a maneno matamu; -nafiki.

**smother** /ˈsmʌðə(r)/ *v.t.* kaba roho; gubika; ficha; zima kwa kufunika majivu au mchanga; zuia.

**smoulder** /ˈsməʊldə(r)/ *v.i.* waka bila kutoa miale; endelea kuwepo kisirisiri.

**smug** /smʌg/ *adj.* -a kujisikia; -a kinaya; -a kuridhisha nafsi.

**smuggle** /ˈsmʌgl/ *v.t./i.* fanya magendo. **~r** *n.* mfanya magendo.

**snack** /snæk/ *n.* sneki; asusa.

**snag** /snæg/ *n* kikwazo.



snail

**snail** /sneɪl/ *n.* koa; konokono.

**snake** /sneɪk/ *n.* nyoka.

**snap** /snæp/ *n.* mwaliko; udataji; picha. *v.t./i.* (**-pp-**) ng'ata; data; piga picha; katika; alisa vidole. *~ sb.'s head off,* karipia; dakuliza; rukia maneno. a **shot,** picha iliyopigwa haraka. *a cold ~* kipindi cha baridi ya ghafla. **~py** *adj.* -a kukolea; -a hamaki; -a chuki.



snake

**snare** /sneə(r)/ *n.* mtego. *v.t.* tega; nasa.

**snarl** /snɑ:l/ *n.* kemeo; karipio. *v.i.* bwekea; ng'aka; karipia; kemea.

**snatch** /snætʃ/ *n.* unyakuaji; ukwapuaji; kipindi kifupi. *v.t.* nyakua; kwapua; chomoa; chopoa. *~ a meal,* -la upesi. *~es of song,* kuimba kwa vipindi.

**sneak** /sni:k/ *n.* mwoga; chakubimbi; msaliti; mbukuzi; mchongezi; mbeya. *v.i.* nyatia; nyemelea. *v.t.* *(colloq.)* iba.

**sneeze** /sni:z/ *n.* chafya. *v.i.* piga chafya.

**sniff** /snɪf/ *v.i.* nusanusa; vuta kamasi; beua.

**snob** /snɒb/ *n.* mpenda makuu; mdharau wanyonge; -enye

kujivunia hadhi. **~bery** *n.* kupenda makuu; kujiona. **~bish** *adj.* -a kupenda makuu; -a kujiona.

**snooker** /'snu:kə(r)/ *n.* snuka: mchezo utumiao tufe nyeupe kugonga nyingine 15 nyekundu na 6 za rangi mbali mbali juu ya meza.

**snore** /snɔ:(r)/ *n.* *n.* mkoromo. *v.i.* koroma.

**snort** /snɔ:t/ *n.* pura; mkoromo. *v.i.* piga pura; koroma.

**snout** /snaʊt/ *n.* pua ya nguruwe.

**snow** /snəʊ/ *n.* theluji. *v.i.* -nya theluji; anguka kama theluji. *be ~ed up,* kwamishwa na theluji. *be ~ed under with requests,* elemewa na maombi.

**snuff** /snʌf/ *n.* tumbaku ya kunusa; ugoro.

**snug** /snʌg/ *adj.* -a raha mustarehe; -a buraha. **~gle** *v.i.* sogelea ili kupata joto; kumbatia.

**so** /səʊ/ *adv.* sana; kiasi hicho; kiasi kwamba. *conj.* kwa hivyo; hivyo; basi; ndiyo maana. *pron. so- and-so,* fulani.

**soak** /səʊk/ *v.t./i.* rowesha; rowa; rowana; roweka. *~ up,* -nywa; fyonza; nyonya.

**soap** /səʊp/ *n.* sabuni. *soft ~, (fig.)* sifusifu. **~berry** *n.* mharita; harita. *v.t.* tia sabuni; osha, fua kwa kutumia sabuni; visha kilemba cha ukoka.

**soar** /sɔ:(r)/ *v.i.* ruka juu kwa mabawa; paa angani. *The price is ~ing* , bei inapanda.

**sob** /sɒb/ *n.* kwikwi. *v.i.* lia kwa kwikwi.

**sober** /'səʊbə(r)/ *adj.* -a kiasi; -enye busara; -a makini; -siolewa; (kwa rangi) baridi. *v.t./i.* leua; leuka.

**sobriety** /'sə'braɪəti/ *n.* busara; kiasi; utulivu.

**soccer** /'sɒkə(r)/ *n.* *(colloq.)* mpira wa miguu; futboli; soka; kandanda.

**sociable** /'səʊʃəbl/ *adj.* -kunjufu; -changamfu; -a bashasha.

**social** /'səʊʃl/ *adj.* -a ushirikiano; -a jamii; -a bashasha; -changamfu; -cheshi; -a pamoja; -a jumuia. *your ~ equals,* wa rika lako. **~ism** *n.* ujamaa. **~ist** *n.* mjamaa; msoshalisti.

**society** /sə'saɪəti/ *n.* jamii; mfumo wa jamii; chama; shirika; umoja. *spend an evening in the ~ of one's friends,* tembelea marafiki jioni.

**sociologist** /ˌsəʊsi'ɒlədʒist/ *n.* mwanasosiolojia.

**sociology** /ˌsəʊsi'ɒlədʒi/ *n.* sosiolojia; elimu-jamii.

**sock** /sɒk/ *n.* soksi. *pull one's ~ up,* ongeza juhudi.

**socket** /'sɒkɪt/ *n.* soketi; tundu kama la jicho.

**sod** /sɒd/ *n.* tabaka la udongo na majani yake. *under the ~,* kaburini.

**soda** /'səʊdə/ *n.* magadi. **~ water**, maji ya gesi. *baking ~,* hamira ya unga.

**sodium** /'səʊdiəm/ *n.* sodiamu: metali ya rangi ya fedha. **~ hydroxide**, sodiamu hidroksidi: alkali ipatikanayo kwa utendanaji wa sodiamu na maji hutumika kutengenezea sabuni na karatasi.

**sofa** /'səʊfə/ *n.* kochi; sofa.



**sofa**

**soft** /sɒft/ *adj.* -ororo; laini; (kwa rangi) si -angavu; (kwa sauti) -pole; -tamu. **~en** *v.t./i.* lainisha; lainika; punguza ukali; rahi-sisha. **~ly** *adv.* polepole; kimyakimya; kwa utulivu. **~ water** *n.* maji laini: maji yasiyokuwa na chumvi za kalisi au magnesi. **~ware** *n.* programu: maelekezo kwa kompyuta katika umbo la programu ambayo huhifadhiwa katika ukanda sumaku au diski na hudhibiti utekelezaji wa kazi za kompyuta.

**soil** /sɔɪl/ *n.* udongo; nchi; uchafu. *v.t./i.* tia uchafu; chafua; chafuka. **~ erosion** *n.* mmong'onyoko wa udongo: uondoshaji udongo kwenye uso wa ardhi kwa upepo au kubururwa na maji.

**solar** /'səʊlə(r)/ *adj.* -a jua; ya sola. **~ cell**, betri inayotumia nishati ya jua; kifaa kinachogeuza mwanga wa jua kuwa umeme. **~ eclipse**, kupatwa jua: kufunikwa mwa-

ngaza wa jua wakati kivuli cha mwezi kinapotua ardhini. ~ **energy**, nishati ya jua. ~ **flare**,




**solar eclipse | kupatwa kwa jua**

mchapuko nishati jua: mchapuko wa ghafla wa nishati ya jua ambao hudumu kwa muda mfupi. ~ **heating**, upashaji jua: utumiaji nishati jua katika nyumba. ~ **system**, mfumo wa jua: mpangilio wa jua, sayari pamoja na magimba mengine yanayolizunguka jua. ~ **wind**, upepo jua: mkondo wa chembechembe angani kutoka kwenye jua ambao kwa kawaida huathiri mawasiliano ya redio.

**solder** /'səʊldə,/ *n.* lehemu; risasi. *v.t.* lehemu; lihimu; unganisha kwa lehemu. **~ing-iron** *n.* nyundo ya kulehemia.

**soldier** /'səʊldə(r)/ *n.* mwanajeshi; askari. **~ly**, **~-like** *adj.* kikakamavu; kiaskari; kijeshi.

**sole**[1] /səʊl/ *n.* unyayo; soli; wayo (aina ya samaki). *v.t.* weka soli.

**sole**[2] /səʊl/ *adj.* -a peke yake; pekee; -a moja tu. **~ly** *adv.* tu.

**solenoid** /'sɒlənɔɪd, 'səʊl-/ *n.* zongomo; solenoidi: koili mduara yenye mapindi mengi ya waya wa shaba na hugeuka sumaku inapopitisha mkondo wa umeme.




**solenoids | solenoidi**

**solemn** /'sɒləmn/ *adj.* -enye taadhima; -a ibada; -a dhati; makini. **~ity** *n.* taadhima; umuhimu; makini; uzito. **~ly** *adv.* kwa heshima. **~ize** *v.t.* tukuza; tekeleza kiibada.

**solicit** /sə'lɪsɪt/ *v.t./i.* omba; sihi; tongoza. **~or** *n.* mwanasheria; wakili. **solicitous** *adj.* -enye kujali; -a kutaka kusaidia.

**solicitude** /sə'lɪsɪtju:d/ *n.* kutaka kusaidia; wasiwasi; tamaa.

**solid** /'sɒlɪd/ *n.* mango; kitu kigumu. *adj.* -a mango; -nene; -liozibwa kabisa; -gumu; yabisi; imara; -enye ujazo; thabiti; -zima; -a mfululizo; -aminifu; safi; -lioshikamana. *He was writing for two ~ hours*, alikuwa akiandika kwa masaa mawili mfululizo. **~ify** *v.t./i.* gandamiza; gandamana; ganda; gumuka; fanya -gumu; gandisha; imarisha. **~ity** *n.* umango; umadhubuti; uthabiti; uimara.

**soliloquy** /sə'lɪləkwi/ *n.* kujisemea; kusema na nafsi. **soliloquize** *v.i.* zungumza na nafsi.

**solitary** /'sɒlətri/ *adj.* pweke; -a kujitenga; -kiwa; -moja tu. **solitude** *n.* upweke; ukiwa; upekee; faragha.

**solo** /'səʊləʊ/ *n.* wimbo wa mtu mmoja. **~ist** *n.* mwenye kuimba peke yake.

**solstice** /'sɒlstɪs/ *n.* solistasi; solistisi: mojawapo ya nyakati mbili za mwaka ambapo jua huwa mbali kabisa na ikweta.

**soluble** /'sɒljəbl/ *adj.* mumunyifu: iwezayo mumunyika kwa urahisi. **solubility** *n.* umumunyifu.

**solute** *n* kimumunyishwaji: dutu itiwayo kwenye kimumunyishaji ili kufanya mmumunyo.

**solution** /sə'lu:ʃn/ *n* **1.** mmumunyo: tokeo la kuchanganya kimumunyishaji na kimumunyishwaji. **2.** ufumbuzi; jibu; utatuzi.

**solve** /sɒlv/ *v.t.* fumbua; tatua; tafuta jibu. **~nt** *n.* kimumunyishaji. *adj.* -a kuyeyusha; **~ncy** *n.* uwezo wa kulipa madeni.

**sombre** /'sɒmbə(r)/ *adj.* a giza; -eusi; -a huzuni.

**some** /səm/ *adj./pron.* baadhi ya; -ingine; fulani; kiasi. **~what** *adv.* kidogo; kwa kiasi fulani.
**somersault** /'sʌməsɒlt/ *n./v.i.* kichwangomba; pinduka; kichwa gomba.
**somnolent** /'sɒmnəl(ə)nt/ *adj.* -a kusinzia; -a usingizi; -a kutia usingizi. **somnolence** *n.* usingizi.
**son** /sʌn/ *n.* mtoto wa kiume. **~-in-law** *n.* mkwe.
**sonar** /'səʊnɑ:/ *n.* sona: ufupisho wa **sound navigation and ranging**: ala inayotumiwa na meli kupimia kina cha bahari kwa kutumia mawimbi ya sauti.



**sonar** | **sona**

**song** /sɒŋ/ *n.* wimbo. *for a ~,* rahisi sana.
**sonic** /'sɒnɪk/ *adj.* -a kuhusu sauti; kasi ya mawimbisauti; mawimbisauti.
**sonnet** /'sɒnɪt/ *n.* soniti: utenzi wa mistari 14.
**soon** /su:n/ *adv.* karibu; hivi punde; mapema; kabla ya. *I would as ~ die,* ni sawa kufa kwangu; afadhali nife; ni tayari kufa.
**soot** /sʊt/ *n.* masizi; gonya: tabaka ya masizi katika kitu kinachopigwa na moshi.
**soothe** /su:ð/ *v.t.* tuliza; fariji; ridhisha; burudisha.
**sop** /sɒp/ *n.* kitonge kilichochovywa katika mchuzi; rushwa; kitulizo. **~ping** *adj./adv.* -a kurowana; -a kutota.
**sophisticated** /sə,fɪstɪ'keɪtɪd/ *adj.* -a kisasa; -staarabu; changamano.
**sorcerer** /'sɔ:sərəs/ *n.* mchawi; mwanga. **sorceress** *n.* mchawi wa kike; gagula.
**sorcery** /sɔ:səri/ *n.* uchawi; sihiri; wanga; uramali.
**sordid** /'sɔ:dɪd/ *adj.* -nyonge; duni; dhalili; hafifu.
**sore** /sɔ:(r)/ *adj.* -a kuwasha; -a kuuma; -a huzuni; -a majonzi; -a kuhuzunisha; -a kero; (la zamani) -kubwa; mno; sana. **~ly** *adv.* sana; mno.
**sorghum** /'sɔ:gəm/ *n.* mtama.
**sorrow** /'sɒrəʊ/ *n.* huzuni; sikitiko; simanzi. **~ful** *adj.* -enye simanzi; -enye huzuni; -enye majonzi.
**sorry** /'sɒri/ *adj.* -a kusikitika; -a huzuni; -a majuto; -a jitimai.
**sort** /sɔ:t/ *n.* jinsi; namna; aina. *a good ~,* muungwana. *out of ~s, (colloq.)* hoi; taabani; -gonjwa; ovyoovyo. *He is out of ~s,* yu mgonjwa kidogo; hajiwezi. *v.t./i. ~ out,* tenga; ainisha; chambua; changanua; piga mafungu.
**SOS** /,es əʊ 'es/ *n.* ufupisho wa *save our souls:* wito wa kimataifa wa kuomba msaada wakati wa hatari.
**soul** /səʊl/ *n.* roho; nafsi; moyo. *There was not a ~ to be seen,* hakukuwa na mtu hata mmoja. *He is the ~ of bravery,* ni kielelezo cha shujaa. **~ful** *adj.* -a kuzindua; -a kuleta maono mema. **~less** *adj.* katili; -enye roho ngumu.
**sound**[1] /saʊnd/ *n.* sauti; mlio; mvumo. *v.i./t.* toa sauti; lia; liza; onekana; elekea; tangaza; piga chombo cha muziki. *His explanation ~s true,* maelezo yake yaelekea kuwa kweli. *The doctor ~ed my chest,* daktari alinipima kifua. **~proof** *adj.* -siopenyeza sauti. **~ wave**, wimbi sauti
**sound**[2] /saʊnd/ *n.* mlangobahari.
**sound**[3] /saʊnd/ *v.t./i.* tia bildi; pima maji kwa bildi; *(fig.)* jaribu moyo; hoji; ḍadisi. **~er** *n.* saunda: chombo cha kupeleka na kupokea habari kwa sauti.
**sound**[4] /saʊnd/ *adj.* -zima; kamili; timamu; -a mantiki; imara; -a busara; sana; barabara. *adv.* fofofo. *~ asleep,* -liolala fofofo. **~ly** *adv.* kwa busara; kabisa; fofofo. **~ness** *n.* uzima; utimamu.
**soup** /su:p/ *n.* supu; mchuzi. *be in the ~, (colloq.)* -wa matatizoni. *You're in the hot ~,* umepatwa na janga.
**sour** /'saʊə(r)/ *adj.* -chungu; -kali; -a kasirani; -liochachuka. *~ milk,*

mtindi. *v.t./i.* chacha; chachuka; chachua. **~ness** *n.* uchungu; ukali; uchachu.
**source** /sɔːs/ *n.* chimbuko; asili; shina; chanzo; chemchemi; rejeo; kumbukumbu.
**south** /saʊθ/ *n.* kusini. *adj.* -a kusini. *adv.* kwa kusini. **~erly** *adj./adv.* a kusini; -a upande wa kusini. **~ern** *adj.* -a kusini. **~ward(s)** *adv.* kwa kusini; -a kuelekea kusini. **south-wester** *n.* pepo za kusini magharibi.
**souvenir** /ˌsuːvəˈnɪə/ *n.* ukumbusho.
**sovereign** /ˈsɒvrɪn/ *n.* mtawala; kiongozi wa nchi. *adj.* -kuu; enye enzi; -enye mamlaka; -a kinchi. **~ty** *n.* enzi; mamlaka; utawala.
**soviet** /ˈsəʊvɪət/ *n.* bunge la Warusi enzi za ukomunisti; raia wa Urusi; Mrusi.
**sow**[1] /səʊ/ *v.t./i.* (**sowed**, **sown**) panda; sia.
**sow**[2] /səʊ/ *n.* nguruwe jike.
**soya bean** /ˈsɔɪ biːn/ *n.* soya: maharage meupe.
**space** /speɪs/ *n.* anga; nafasi; mahali; uwanda; muda; muhula; majira; kitambo; uwazi; kipindi. *v.t.* panga kwa nafasi kati. **spacious** *adj.* -kubwa; -enye nafasi; pana. **~probe** *n.* kichunguzi anga: chombo kisichokuwa na rubani kinachochunguza kuwepo kwa uhai katika anga za juu.
**spade** /speɪd/ *n.* pauro; sepetu; (kwa karata) shupaza. **~work** *n.* kazi ngumu ya matayarisho ya mwanzo.


spades

**span** /spæn/ *n.* shibiri; shubiri; nyanda; tao; muda; kitambo; upana. *v.t.* (**-nn-**) dumu; pima kwa shibiri; daraja lililo vuka mto.


spanner

**spanner** /ˈspænə(r)/ *n.* spana.
**spar**[1] /spɒː(r)/ *n.* boriti; mlingoti; mhimili; nguzo.
**spar**[2] /spɒː(r)/ *v.i.* (**-rr-**) pigana ngumi kwa mazoezi.
**spare** /speə(r)/ *n.* spea; kipuri. *v.t./i.* achilia; rehemu; hurumia; tumia kidogokidogo; -pa; toa. *~ no pains*, tumia nguvu zote. *He never ~s himself*, ni mwenye bidii daima. *We can't ~ the time for a holiday*, hatuna nafasi ya likizo. *Please ~ a copper*, kunradhi naomba pesa. *He has enough and to ~*, ana cha kutosha na zaidi. *adj* -a akiba; haba; chache; kiasi; -embamba; -liokonda. *I have no ~ cash*, sina fedha ya ziada. *a ~ tyre*, tairi la akiba. *a ~ room*, chumba cha wageni. **sparing** *adj.* -nyimifu; angalifu; kabidhi. **sparingly** *adv.* kidogo; kwa uchache; kwa kiasi.
**spark** /spɑːk/ *n.* cheche; kimeta; kiasi kidogo. **~ing-plug** *n.* plagi.


sparking-plug

**sparkle** /ˈspɑːkl/ *v.i.* metameta; ng'aa; ng'ara; memetuka.
**sparrow** /spærəʊ/ *n.* shorewanda; ziwarde; ziwaridi.
**sparse** /spɑːs/ *adj.* haba; -chache; kidogo; -a kutawanyika; -a kusambaa. **~ly** *adv.* kwa uchache
**spasm** /ˈspæzəm/ *n.* mshtuko; tukio la ghafla; mpasuko wa nishati; mtukutiko. **~odic** *adj.* -a ghafla; -a kusababishwa na mshtuko; -a kutokea kwa vipindi visivyotabirika.
**spate** /spæt/ *n.* kufurika kwa mto.
**spawn** /spɔːn/ *n.* mayai ya samaki au chura. *v.i.* taga mayai kwa wingi.
**speak** /spiːk/ *v.i./t.* (**spoke**, **spoken**) nena; sema; ongea; zungumza; jua; tamka; hutubia; wasiliana kwa ishara. *~ out (up)*, sema sana; sema waziwazi. *~ one's mind*, toa maoni yako waziwazi. *nothing to ~ of*, kitu kidogo tu. *We are not on ~ing terms*, hatusemeshani; tumenuniana. **~er** *n.* msemaji; mzungumzaji; kipaza sauti; spika.
**spear** /spɪə(r)/ *n.* mkuki; fumo.
**special** /speʃl/ *adj.* -a namna; maalumu; -a pekee; spesheli. **~ist** *n.* mtaalamu. **~ity** *n.* utaalamu maalumu; kazi maalumu; hulka maalumu. **~ize** *v.i.* bobea katika jambo, kazi, taaluma maalumu.

**species** /'spi:ʃi:z/ *n.* spishi; aina; namna; jinsi.
**specific** /spə'sɪfɪk/ *adj.* dhahiri; maalumu; bayana; mahususi. ~ *gravity,* uzito linganifu mahususi. **~ation** *n.* vipimo; uainishaji; uonyeshaji uhalisi.
**specify** /'spesɪfaɪ/ *v.t.* taja; pambanua; ainisha; eleza bayana.
**specimen** /'spɛsɪmɪn/ *n.* kiolezo; kielelezo; sampuli; mfano.
**speck** /spek/ *n.* waa; doa; chembe; alama. **~ed** *adj.* -enye madoa. **~le** *n.* doa; paku. **~led** *adj.* -enye madoa-doa; -enye mapaku.
**spectacle** /'spektəkl/ *n.* tamasha; sherehe; maonyesho. *make a ~ of oneself,* jifanya kinyago. *a pair of ~s,* miwani.
**specs** /speks/ *n.( colloq.)* miwani.
**spectacular** /spek'tækjələ(r)/ *adj.* -a sherehe; -a kustaajabisha.
**spectator** /spek'teɪeə(r)/ *n.* mtazamaji.
**spectrum** /'spektrəm/ *n.* spektra: mpangilio maalumu wa taswira zinazotokana na miali ya mnururisho kufuatana na lukoka mbalimbali zilizo katika mnururisho huo. **absorption ~**, spektra mfyonzo. **band ~**, spektra milia. **continuous ~**, spektra fulizi. **electromagnetic ~**, spektra sumakuumeme. **emission ~**, spektra utokezo. **line ~**, spektra nyoofu.
**speculate** /'spɛkjʊləɪt/ *v.i.* kisia; bahatisha; cheza pata potea; dhania; langua.
**speculator** /'spekjuleɪtə(r)/ *n.* mlanguzi; mbahatishaji.
**speculation** /ˌspekju'leɪʃn/ *n.* ubahatishaji; ukisiaji; ulanguzi; dhana.
**speech** /spi:tʃ/ *n.* kipaji cha kusema; hotuba; kauli; msemo; usemi; lugha. **~less** *adj.* -sioweza kusema; liopigwa na butwaa.
**speed** /spi:d/ *n.* mwendo; spidi; haraka; kasi; mbio. *at a ~ of thirty k.p.h.,* mwendo wa kilomita thelathini kwa saa. *travel at full ~,* enda upesi iwezekanavyo. *exceed the ~ limit,* pindukia spidi iliyoruhusiwa. *more haste less ~,* haraka haraka haina baraka. *~ of sound,* spidi ya sauti: mwendo wa kasi ya sauti ya mita 340 kwa sekunde moja. *v.t./i.* (**sped**) himiza; enda upesi; ongeza mwendo; endesha kasi. **~ometer** *n.* kipima spidi; spidomita; kipimamwendo. **~y** *adj.* -a kasi; -epesi; -a haraka. **~ily** *adv.* hima; upesi; kwa haraka.
**spell**[1] /spel/ *v.t./i.* (**spelt/spelled, spelt**) /spelt/ endeleza; taja, andika tahajia za neno; eleza kinagaubaga; ashiria. *Delay may ~ danger,* kuchelewa kunaashiria hatari. **~ing** *n.* tahajia: herufi zinazounda neno.
**spell**[2] /spel/ *n.* uchawi; mvuto; laana; apizo. **~bound** *adj.* -a kuteka akili; -a kushangaza.
**spell**[3] /spel/ *n.* muda; kipindi.
**spend** /spend/ *v.t./i.* (**spent**) tumia. **~thrift** *n.* mbadhirifu. **spent** *adj.* -liochoka sana; hoi; liotumiwa; -liokwisha.
**sperm** /spɜ:m/ *n.* manii; shahawa. **~atozoa** *n.* manii: seli za gameti za kiume zilizopevuka.
**sphere** /sfɪə(r)/ *n.* tufe; fani; uwanja; mazingira; eneo. *~ of influence,* eneo la mamlaka.
**spherical** /'sfɪərɪkl/ *adj.* -a mviringo; -a tufe.
**sphinx** /sfɪŋks/ *n.* sfinksi: sanamu ya jiwe yenye mwili wa simba na kichwa cha mwanamke; msiri.


sphinx

**spice** /spaɪs/ *n.* kiungo; *(fig.)* kidogo; mvuto; msisimko. *a ~ of humour,* kichekesho; -a kuchekesha kidogo. *v.t.* unga; tia chumvi.
**spider** /'spaɪdə(r)/ *n.* buibui. *spider's web,* utando wa buibui.


spider

**spike** /spaɪk/ *n.* njumu; msumari; mwiba; shuke.
**spill**[1] /spɪl/ *n.* anguko; uangukaji. *v.i./t.* (**spilt/spilled**) mwagika; mwaga; bwaga; dondosha. *have a ~ from a bicycle,* anguka baiskeli.
**spill**[2] /spɪl/ *n.* kibahaluli: karatasi ya kuwashia taa.

**spin** /spɪn/ *n.* mzunguko; ubingiriaji; kugeuka ghafla. *v.t./i.* (**spun/span, spun, -nn-**) pota; sokota; jenga utando; tunga hadithi; zungusha; zunguka; bingiria. *~ sth. out,* tumia kitu kwa muda mrefu. *~ a yarn,* piga chuku. **~dle** *n.* pia; mkono wa kisokotea nyuzi.

**spinach** /'spɪnɪdʒ/ *n.* mchicha; spinachi.

**spine** /spaɪn/ *n.* uti wa mgongo; mwiba. **spinal** *adj.* -a uti wa mgongo. **~less** *adj.* -sio uti wa mgongo. *(fig.)* -oga. **spiny** *adj.* -enye miba.

**spiracle** /spʌɪrək(ə)l/ *n.* tunduhewa: vitundu vilivyo mbavuni mwa vidudu vya ngeli ya wadudu, mamalia na samaki vinavyotumika kupitishia hewa.

**spiral** /'spaɪrəl/ *n./adj.* zongomo; mzunguko; -a zongomo; -a mzunguko. **~ galaxy**, kundinyota mtatio: mkusanyiko wa mamilioni ya nyota na vumbi katika anga zinazounda mfumo maalumu.

**spire** /'spaɪə(r)/ *n.* mnara-pia.

**spirit** /'spɪrɪt/ *n.* roho; nafsi; kizuu; mzuka; ari; msimamo; hisia; hali; mzimu; mwelekeo; spiriti. *It was done in a ~ of mischief,* -ilifanywa kwa nia ya kukomoana. *Obey the ~ not the letter of the law,* tii sheria vilivyo. *in high ~s,* -enye furaha. *in poor (low) ~s, out of ~s,* enye majonzi. *v.t. ~ away,* torosha. **~ed** *adj.* -enye ari; jasiri. **~ual** *adj.* -a roho; -a kidini; -a kiroho; -a mzimu. *n.* wimbo wa dini wa Wamarekani weusi.

**spirogyra** /ˌspʌɪ'rə(ʊ)'dʒʌɪrə/ *n.* spirojira: mmea sahili wa maji baridi wenye tanzi zongomo za klorofili;


spirogyra

**spit**[1] /spɪt/ *n.* mate. *v.t./i.* (**spat, -tt-**) tema; tema mate; alika; nyonyota; toa ukali. **~tle** *n.* mate.

**spit**[2] /spɪt/ *n.* mbano; sehemu nyembamba ya nchi kavu iliyoingia majini. *v.t.* banika. *He is the dead ~ of his father,* amefanana kabisa na baba yake.

**spite** /spaɪt/ *n.* chuki; ubaya; ukorofi; fundo; inda. *He has a ~ against me,* ana chuki dhidi yangu. *It was done out of ~,* ilifanywa kwa inda. *in ~ of,* ingawa; bila kujali; ijapokuwa. *They went in ~ of the rain,* walikwenda ijapokuwa kulikuwa na mvua. *I shall do it in ~ of you,* nitafanya ijapokuwa hutaki. **~ful** *adj.* -a chuki; -korofi; -enye inda. **~fully** *adv.* kwa chuki; kwa inda.

**splash** /splæʃ/ *v.t./i.* rusha (maji, matope, etc.); ruka; rushia; **~ing** *n.* mruko wa maji au matope. *make a ~,* jifaharisha kwa kutapanya fedha.

**spleen** /spli:n/ *n.* wengu; bandama; chuki; hasira.

**splendid** /'splendɪd/ *adj.* -a fahari; bora; -tukufu.

**splendour** /'splendə(r)/ *n.* fahari; ubora; utukufu.

**splice** /splaɪs/ *n.* kiungio. *v.t.* unganisha kamba kwa kuzisokota; fungamanisha vipande vya mti.

**splint** /splɪnt/ *n.* gango; kibanzi; kitata. **~er** *n.* kibanzi; uchane. *v.t./i.* vunjavunja; vunjikavunjika; chachata; chachatika.

**split** /splɪt/ *n.* mpasuko; ufa; mwatuko; utengano. *v.t./i.* (**-tt-, split**) pasua; pasuka; atua; atuka. gawa; gawanyika. *~ one's sides,* cheka sana. *a ~ting headache,* maumivu makali ya kichwa. *~ hairs,* bishania tofauti ndogondogo.

**spoil** /spɔɪl/ *n.* mateka; ngawira; mali ya kuiba; taka; kifusi; marupurupu. *v.t./i.* (**~t/~ed**) haribu; endekeza; dekeza; haribika; oza. *be ~ing for a fight,* tamani kupigana.

**spoke** /spəʊk/ *n.* spoki; taruma.

**spokesman** /'spəʊksmən/ *n.* msemaji mkuu; mwakilishi.

**sponge** /spʌndʒ/ *n.* sponji; sifongo. *throw up the ~,* kubali kushindwa. *v.t./i.* safisha kwa sponji. *~ on sb., (colloq.)* nyonya. **~-cake** *n.* mkate wa mayai; keki. **~r** *n.* mdusi; mdoezi.


sponge

**spongy** /'spʌndʒi/ *adj.* -a kama sponji.
**sponsor** /'spɒnsə(r)/ *n.* mdhamini. *v.t.* dhamini.
**spontaneous** /spɒn'teɪnɪəs/ *adj.* -a hiari; -a kujianzia; -enyewe.
**spool** /spu:l/ *n.* kireli cha uzi au filamu au karatasi.
**spoon** /spu:n/ *n.* mwiko; kijiko. **~ful** *n.* kijiko tele.
**spore** /spɔ:r/ *n.* kiiniyoga; kijimbegu.
**sport** /spɔ:t/ *n.* mchezo; burudani; mzaha; *(pl.)* mashindano ya michezo. *make ~ of*, fanya dhihaka. **~sman** *n.* mwanamichezo. **~smanlike** *adj.* -a kumstahikia mwanamichezo. **~smanship** *n.* uanamichezo; uungwana.
**spot** /'spɒt/ *n.* doa; baka; paku; chunusi; tone; tojo; kiasi kidogo; mahali. *do sth. on the ~*, fanya palepale. *the man on the ~*, mtu aliyekuwapo mwenyewe. *~ cash*, fedha taslimu. *v.t./i.* (**-tt-**) tia doa; chafua; haribu; tambua; ona. *~ a friend in a crowd*, tambua rafiki katika kundi. **~less** *adj.* bila doa; -eupe; safi. **~ty** *adj.* -enye chunusi; -enye madoa. *a ~ complexion*, uso wenye chunusi.
**spouse** /spaʊz, -s/ *n.* mume; mke.
**spout** /spaʊt/ *n.* mdomo wa birika; mlizamu; mrizabu; neli; ufokaji; ububujikaji. *v.t./i.* foka; bubujika *(colloq.)* piga domo; hubiri; huruju.
**sprain** /spreɪn/ *n.* mteuko; mtenguko; mshtuko. *v.t.* tegua; tenguka; shtua.
**sprawl** /sprɔ:l/ *v.i.* jinyoosha; tandawaa; tambaa; enea.
**spray** /spreɪ/ *n.* rasharasha; manyunyu; kinyunyizio; mrashi. *v.t.* nyunyizia; pulizia.
**spread** /spred/ *n.* upana; uenevu; upanuzi; kuenea; shuka. *v.t./i.* (**spread**) kunjua; nyosha; tanda; paka; tandika; eneza; enea; tawanya; tawanyika; dumu. **~sheet** *n.* warakatamvu: karatasi ya kazi kwa ajili ya ukokotoaji na uchambuzi wa data.
**spree** /spri:/ *n.* shamrashamra. *have a ~*, -wa katika shamrashamra; *be on the ~*, -wa katika shamrashamra.
**spring**[1] /sprɪŋ/ *n.* springi; kitawi; chemchemi; nyunju; kuduta; mnyumbuko; chimbuko; sababu. **~ balance**, mizani ya springi: mizani sahili ipimayo vitu kwa kutumia ukunjukaji wa springi. **~ tide**, maji makuu; bamvua. *v.i./t.* ruka ghafla; chupa; piga nyunju; tokeza; chipuka; fyatua; pasuka. *~ a leak*, anza kuvuja.
**spring**[2] /sprɪŋ/ *n.* majira ya vuli.
**sprinkle** /'sprɪŋkl/ *v.t.* nyunyiza; rashia.
**sprinkling** /'sprɪŋklɪŋ/ *n.* kidogo; uchache. *There was only a sprinkling of people present*, watu wachache walihudhuria .
**sprint** /sprɪnt/ *v.i.* timka.
**sprout** /spraʊt/ *v.i.* chipuka; chipua; anza kumea; anza kuota.
**spruce**[1] /spru:s/ *adj.* nadhifu; -a kimaridadi.
**spruce**[2] /spru:s/ *n.* aina ya msonobari.
**spur** /spɜ:(r)/ *n.* kitu; kikwaru; mwiba; kichokoo; msumari. *(fig.)* kichocheo. *act on the ~ of the moment*, fanya ghafla bila kufikiri. *a ~ of a hill*, tuta ubavuni mwa kilima. *v.t.* (**-rr**) choma; papura; himiza; chochea; chonjomoa.
**spurn** /spɜ:n/ *v.t.* sukumia mbali; piga teke; dharau.
**spurt** /spɜ:t/ *n.* mbubujiko; ufokaji; mtimko; kukurupuka. *v.i.* foka; bubujika; timka; kurupuka.
**spy** /spaɪ/ *n.* mpelelezi; jasusi; kachero. *v.t./i.* ona; peleleza; tambua; gundua; jasusi; duhushi.
**squabble** /'skwɒbl/ *n./v.i.* mzozo; ugomvi; mabishano; zozana; gombana; bishana.
**squad** /skwɒd/ *n.* kikosi cha askari. **~ron** *n.* kikosi cha askari wa farasi; kikosi cha manowari; kikosi cha ndege.
**squall** /skwɔ:l/ *n.* kilio kikali cha maumivu; dhoruba; tufani.
**squander** /'skwɒndə(r)/ *v.t.* badhiri; fuja; tapanya.
**square** /skweə(r)/ *n.* mraba; uwanja;

filifili: kipimapembe; kipeo. *adj.* -a mraba; kama pembemraba; liosawazishwa; -a haki; sawasawa; kamili. *a ~ deal,* maafikiano ya haki. *get ~ with sb.,* lipa deni lake; *(fig.)* lipiza kisasi. **~ measure**, kipimo cha eneo. *a ~ inch,* inchi mraba. *a ~ meal,* chakula cha kutosha. *v.t./i.* fanya mraba; sawazisha; patanisha; zidisha namba kwa yenyewe; lipa; fanya pembe mraba kwenye mstari. *~ with,* patana; patanisha na.


square

**squash** /skwɒʃ/ *n.* maji ya matunda; boga; mchezo wa skwashi; msongamano. *v.t.* ponda; songa; nyamazisha; komesha.

**squat** /skwɒt/ *v.i.* chuchumaa; chutama; kaa kitako; kalia ardhi bila ruhusa. *adj.* -fupi tena -nene. **~ter** *n.* mkaa mahali bila ruhusa ya sheria.

**squeak** /skwi:k/ *n.* kwichikwichi; kilio chembamba (kama cha panya). *a narrow ~,* kuponea chupuchupu. *v.i.* alika; sema kwa sauti ya juu.

**squeal** /skwi:l/ *n.* ukwenzi: kilio chembamba, kirefu cha hofu au maumivu. *v.i.* piga ukwenzi.

**squeeze** /skwi:z/ *n.* kuminya; kubana. *v.t.* songa; bana; minya; kamua; kaba. *~ the juice out of an orange,* kamua chungwa. *~ one's way through a crowd,* penya kwenye umati.

**squint** /skwɪnt/ *n./v.i.* makengeza; kijicho upembe; -a na makengeza; tupia jicho; chungulia. *(colloq.) have a ~ at,* tupia jicho.

**squirrel** /'skwɪrəl/ *n.* komba; kuchakuro.

**squirt** /skwɜ:t/ *n.* maji yatokayo kwa nguvu kwenye tundu ndogo; kibomba cha kurushia maji. *v.t./i.* toa; toka katika tundu ndogo kwa nguvu; foka.

**stab** /stæb/ *n.* mchomo; kichomi. *v.t.* **(-bb-)** choma kwa silaha; uma; choma; pwita.

**stable**[1] /'steɪbl/ *n.* zizi.

**stable**[2] /'steɪbl/ *adj.* thabiti; imara; siobadilika.

**stability** /stə'bɪləti/ *n.* uthabiti; uimara.

**stabilize** /'steɪbəlaɪz/ *v.t.* imarisha; tuliza; dhibiti. *a stabilized price,* bei isiyobadilika kila mara. **stabilizer** *n.* kidhibiti umeme.

**stack** /stæk/ *n.* tita; rundo; chungu. *v.t.* weka; panga, chunguchungu; rundika; tutika.

**stadium** /'steɪdiəm/ *n.* uwanja wa michezo.

**staff** /stɑ:f/ *n.* mkongojo; fimbo; gongo; mlingoti; nguzo; wafanyakazi; watumishi; mistari ya kuandikia noti za muziki; maafisa waandamizi wa jeshi.

**stag** /stæg/ *n.* paa dume.

**stage** /stædʒ/ *n.* jukwaa; ulingo; dungu; *(fig.)* mahali pa tukio; tukio; wakati; hatua; kipindi; mwendo kati ya vituo viwili. *at an early ~ in the history of our country,* katika kipindi cha awali cha historia ya nchi yetu. *by easy ~s,* kwa safari nyepesi. *v.t.* onyesha tamthilia.

**stagger** /'stægə(r)/ *v.t./i.* yumbayumba; pepesuka; sepetusha; shangaza; duwaza; pumbaza; fadhaisha; panga nyakati tofauti. *~ annual holidays to avoid closing the works,* panga mapumziko nyakati tofauti ili kazi zisisite.

**stagnant** /'stagnənt/ *adj.* -liotuama; *(fig.)* -liokwama; -a kudorora.

**stagnate** /'stægnənt/ *v.i.* tuama; *(fig.)* dorora; kwama.

**stain** /steɪn/ *n.* doa; alama; taka; rangi; *v.t./i.* chafua; haribu; tia doa; tia rangi; chujuka. **~ing** *n.* utiaji rangi: kutia rangi tishu ya kibiolojia isiyo na rangi kimaumbile ili iweze kuonekana vyema chini ya darubini. **~less** *adj.* -eupe; safi; -siopata kutu. **~ steel**, feleji pasiwaa: chuma ambacho hakiathiriwi na kutu.

**stair** /'steə(r)/ *n.* kipago; daraja. **~case**, *flight of ~s* *n.* vidaraja; ngazi.

**stake** /steɪk/ *n.* kiguzo; kigingi; mambo; nguzo ya kuchomea watu moto; kitegauchumi. *be at ~,* wa

hatarini; pata potea; kufa kupona. *v.t.* shikilia kwa kiguzo; weka mpaka kwa viguzo; bahatisha.

**stalactite** /'staləktʌɪt/ *n.* stalaktiti: chokaa iliyogeuka jiwe na kuning'inia kwa chini kwenye dari ya pango.

**stalagmite** /staləgmʌɪt/ *n.* stalagmiti: chokaa iliyogeuka jiwe na kuenea katika sakafu ya pango.

**stale** /steɪl/ *adj.* (kwa chakula) -liochacha; baridi; ovyo; -a kunyong'onyea. ~ *news,* habari iliyopitwa na wakati.

**stalk**[1] /stɔ:k/ *n.* shina; ubua; kikonyo.

**stalk**[2] /stɔ:k/ *v.t./i.* nyatia; nyemelea.

**stall** /stɔ:l/ *n.* zizi; banda; genge; kiti maalumu. *v.t./i.* weka; fuga zizini; kata moto; shindwa kuruka; kwepa au chelewesha jibu.

**stallion** /'stæliən/ *n.* farasi dume asiyehasiwa.

**stamen** /'steɪmən/ *n.* stameni.

**stamina** /'stæmɪnə/ *n.* nguvu; kutochoka upesi; uvumilivu

**stammer** /'stæmə(r)/ *n.* kigugumizi. *v.i.* sema kwa kigugumizi; babaika.

**stamp** /stæmp/ *n.* stempu; muhuri; chapa; alama; kuchapa mguu; kukanyaga. *v.t./i.* kanyaga; chapa miguu; *(fig.)* komesha; piga chapa; piga muhuri; tia alama; bandika stempu; pondaponda. *It ~s him as trustworthy,* yabainisha kuwa ni mwaminifu. *men of that ~,* watu wa namna ile.


stamp

**stampede** /stæm'pi:d/ *n.* ukimbiaji wa ghafla; mtimko; mkurupuko.

**stand** /stænd/ *n.* kisimamo; kituo; kikomo; stendi; steni; jukwaa; kinara; kibanda; msimamo. *v.i./t.* (**stood**) simama; -wa na urefu wa; -wa wima; -wa; kaa; wekwa; baki; dumu; simamisha; vumilia; himili; kubali; chukua; gharimia. *He ~s five feet ten,* ana urefu wa futi tano na inchi kumi. *Let his words ~,* maneno yake yabaki kama yalivyo. *I can't ~ heat,* siwezi kuvumilia joto. *~ drinks on round,* gharimia vinywaji kwa wote waliopo. *he ~s a good chance of,* anaelekea kuwa. *~ one's ground,* shikilia msimamo. *It ~s to reason,* yakubalika. *~ to win,* elekea kushinda. *~ away,* rudi nyuma. *~ by,* kaa tayari. *~ by a friend,* saidia rafiki. *~ by a promise,* timiza ahadi. *~ for,* wakilisha. *~ out,* tokeza. *~ up for,* tetea. *~ up to,* stahamili. *come to a ~ still,* koma; simama. *bring to a ~,* simamisha. *make a ~ for,* shindania. *make a ~ against,* shindana na. *take one's ~ on,* jenga hoja juu ya. **~by** *n.* mtu wa kutegemewa; msaada wa akiba. **~ing** *n.* nafasi; hadhi; cheo; aushi; wakati; muda; wakati. *of long ~,* -a muda mrefu. *man of high ~ing,* mtu wa sifa njema. *adj.* -a siku zote; -a kudumu; -a kusimama; *a ~ order,* kanuni kuu. **~-offish** *adj.* -a kiburi, si -a urafiki.

**standard** /'stændəd/ *n.* bendera; sanifu; kipeo; kipimo; darasa; kiwango. **~ize** *v.t.* fanya kawaida; sanifisha; fanya wastani; fanya aina moja. *The parts of motor-cars are usually ~d,* vipuri vya gari husanifishwa.

**staple**[1] /'steɪpl/ *n.* pini. **~r** *n.* mashine ya kubania pini.

**staple**[2] /'steɪpl/ *n.* bidhaa kubwa ya mahali; zao kuu la mahali; dhana kuu; wazo kuu; aina ya uzi.

**star** /stɑ:(r)/ *n.* nyota; mtu mashuhuri.

**starboard** /'stɑ:bɔ:d/ *n.* upande wa kulia wa meli ukitizama kutoka shetiri mpaka gubeti.


star

**starch** /stɑ:tʃ/ *n.* wanga.

**stare** /steə(r)/ *v.i.* kodoa, kaza macho.

**stark** /stɑ:k/ *adj.* -gumu; -siokunjika; -tupu; kabisa.

**starling** /'stɑ:lɪŋ/ *n.* aina ya ndege aitwaye kwenzi au mramba.

**start** /stɑ:t/ *n.* mwanzo; chanzo; chimbuko; mshtuko; kuondoka; utangulizi; asili. *v.i./t.* anza; anzisha; shtuka; shtua; gutuka; gutua; inuka ghafla. *by fits and starts,* kwa vipindi. **~le** *v.t.* shtusha; gutua; shtua.

**starve** /stɑ:v/ *v.i./t.* shinda na njaa; shindisha au fisha kwa njaa.
**starvation** /stɑ:veɪʃn/ *n.* njaa; ukosefu wa chakula.
**state**[1] /steɪt/ *n.* hali; fahari; heshima; daraja; cheo; enzi; dola; serikali. *lie in ~*, lazwa katika sanduku ya maiti ili kupewa heshima ya mwisho. *~s of matter*, hali za mata: hali za mata kuwa mango, kioevu au gesi. **~ly** *adj.* -a fahari; adhimu. **~sman** *n.* mtawala; mwanasiasa. **~smanlike** *adj.* -a busara; -a kama mtawala mweledi.
**state**[2] /steɪt/ *v.t.* eleza; nena; sema. **~d** *adj.* -liotajwa. *at ~ times*, katika nyakati zilizotajwa. **~ment** *n.* taarifa; maelezo; kauli; tamko; habari.
**static** /'statɪk/ *adj.* -liosimama; tuli. **~ electricity**, umeme tuli: umeme uliotulizana bila ya kusababisha mwendo kutokana na uga wa umeme tuli unaotolewa na chaji.
**station** /'steɪʃn/ *n.* stesheni; kituo; lindo; cheo; daraja. *v.t.* weka mahali; kalisha.
**stationary** /'steɪʃənri/ *adj.* -sio-geuka; -sioondosheka; -sioha-mishika.
**stationer** /'steɪʃənə(r)/ *n.* muuza vifaa vya kuandikia. **~y** *n.* vifaa vya kuandikia.
**statistics** /stə'tɪstɪks/ *n.* takwimu. **statistician** *n.* mtakwimu.
**statue** /'statju:/ *n.* sanamu iliyo-chongwa kwa mti, mawe, madini au kufinyangwa kwa udongo.
**stature** /'stætʃə(r)/ *n.* kimo; urefu wa mtu.
**status** /'steɪtəs/ *n.* hali; cheo; daraja; hadhi; manzili. **~ quo**, hali kama ilivyo. **~ quo ante**, hali kama ilivyokuwa kwanza.
**statute** /'statju:t/ *n.* sheria; amri ya serikali; katiba ya chama.
**staunch**[1] /stɔ:n(t)ʃ/ *v.t.* zuia utokaji wa damu.
**staunch**[2] /stɔ:n(t)ʃ/ *adj.* imara; madhubuti; aminifu; thabiti.
**stay** /steɪ/ *n.* kukaa; kikao; ustahamilivu; uvumilivu; ayari; msaada; tegemeo. *v.i./t.* kaa; zuia; simamisha; komesha; ahirisha; vumilia; stahamili. *~ing power*, ustahimilivu.
**stead** /sted/ *n.* badala. *in a person's ~*, badala ya mtu. *stand sb. in good ~*, saidia mtu sana. **~fast** *adj.* thabiti; imara. **~ily** *adv.* kwa uthabiti. **~iness** *n.* uthabiti; uimara; uaminifu. **~y** *adj.* thabiti; imara -sioanguka; -siogeuka; madhubuti; taratibu; -a adili-adilifu; sawa; -siobadilika. *v.t./i.* thibitisha; imarisha; tulia.
**steak** /steɪk/ *n.* steki; mnofu.
**steal** /sti:l/ *v.t./i.* (**stole**)
**stolen** /'steʊlən/ iba; nyang'anya; poka; pokonya; kwapua; pora; nyatia; nyemelea. *~ in*, nyatia; nyemelea. *~ a march on sb.*, tapeli; kata mtu bogi **~th** *n.* hila; ujanja; siri. *do sth. by ~*, fanya kitu kwa siri. **~thy** *adj.* -siri; -erevu; -janja; -a siri. **~thily** *adv.* kijanja; kimyakimya.
**steam** /sti:m/ *n.* mvuke; moshi. *v.i./t.* toa mvuke; enda kwa mvuke; pika kwa mvuke. **~ engine** *n.* injini inayoendeshwa kwa mvuke. **~ship** *n.* meli inayoendeshwa kwa mvuke. **~roller** *n.* rola inayoendea mvuke. **~er** *n.* stima; marikebu iendeshwayo kwa mvuke.
**steel** /sti:l/ *n.* chuma cha pua; feleji.
**steep**[1] /sti:p/ *n.* mwinuko au mteremko wa ghafla wa mlima. *adj.* (kwa mlima) -a kuinuka ghafla; (kwa bei) ghali; -a kupita kiasi.
**steep**[2] /sti:p/ *v.t.* rowesha; roweka.
**steeple** /'sti:pl/ *n.* mnara ulio chongoka juu. **~chase** *n.* shindano la farasi la kuruka viunzi.
**steer**[1] /stɪə(r)/ *n.* ng'ombe dume maksai.
**steer**[2] /stɪə(r)/ *v.t./i.* elekeza njia; shika usukani; ongoza. **~ing-wheel** *n.* usukani.
**stem**[1] /stem/ *n.* shina; ubua; kikonyo; shina: sehemu ya neno lenye mzizi na viambishi.
**stem**[2] /stem/ *v.t.* (**-mm-**) zuia; ziba; komesha.
**step**[1] /step/ *n.* hatua; kidaraja; kipandio; kipago; wayo; mwendo; tendo. *v.i./t.* (**-pp-**) enda; pima kwa

hatua. ~ *up*, ongeza; himiza. *~s, a pair of steps*, **~ladder** ngazi ya kukunja. *take ~s to prevent illness*, chukua hatua kuzuia ugonjwa.

**step**[2] /step/ *prefix* -a kambo. **~child** mtoto wa kambo. ~ *father*, baba wa kambo.

**steppe** /stɛp/ *n.* nyika.

**sterile** /'steraɪl/ *adj.* -gumba; tasa; kame; -sio na bakteria.

**sterility** /ste'rɪləti/ *n.* utasa; ugumba; kuua bakteria; ukame.

**sterilize** /'sterəlaɪz/ *v.t.* fanya kuwa tasa; hasi; ua bakteria. **sterilization** *n.* uhasishaji: tendo la kuhasi.

**sterling** /'stɜ:lɪŋ/ *adj.* safi; bora; -enye thamani iliyokubaliwa.

**stern**[1] /stɜ:n/ *adj.* -kali; -gumu; bila huruma.

**stern**[2] /stɜ:n/ *n.* tezi: shetri: sehemu ya mbele ya merikebu.

**stethoscope** /'stɛθəskəʊp/ *n.* steto-skopu: chombo cha daktari kusikilizia mapigo ya moyo au mapafu.

**stew** /stju:/ *n.* nyama, samaki, mboga iliyotokoswa. *v.t./i.* tokosa; tokoseka; chemsha; chemka polepole. *(colloq.) in a ~*, -enye wasiwasi.

**steward** /'stju:əd/ *n.* mhudumu wa abiria; wakala; msimamizi. **~ess** *n.* mhudumu wa kike.

**stick**[1] /stɪk/ *n.* fimbo; ujiti; kijiti; bakora; mkongojo; ufito.

**stick**[2] /stɪk/ *v.t./i.* (**stuck**) choma; chomeka; penyeza; kwama; bandika; gandamiza; nata; gandamana; shikilia; nasa; *(colloq.)* futika; fundika. *He stuck his hands in his pockets*, alitia mikono mifukoni. *The key stuck in the lock*, ufunguo ulikwama katika kufuli. *The engine is stuck*, injini imekufa. ~ *at*, sitasita; shikilia. *He ~s at his writing*, aendelea na kazi yake ya uandishi. *He ~s at nothing*, haogopi chochote. ~ *out*, tokeza; chomoza. ~ *out for*, shikilia kupata utakalo. ~ *it out*, *(colloq.)* vumilia. ~ *to*, shikilia; shikamana na. ~ *up for*, shindania; tetea; unga mkono. **~plaster** *n.* plasta. **~y** *adj.* -a kunata. **~ily** *adv.* kwa kunata; kwa kushikilia. **~iness** *n.* mnato; ushikiliaji.

**stiff** /stɪf/ *adj.* -gumu, -siopindika; -kavu; -liokacha; si -kunjufu; -zito. *be ~*, kauka; kazana. *I feel ~ after my work*, nahisi machofu baada ya kazi. *Mix flour and milk to a ~ paste*, changanya unga na maziwa uwe mzito. **~ly** *adv.* kwa kukacha. **~ness** *n.* kukacha; ugumu.

**stifle** /staɪfl/ *v.t./i.* songa; katiza; komesha; kaba; kabwa; songwa. *The heat in Kalahari was stifling*, joto la Kalahari lilikuwa komesha.

**stigma** /'stɪgmə/ *n.* stigma: ncha ya kapeli ambayo ina hali ya mnato na hupokea chavuo.

**still** /stɪl/ *adv.* hata sasa; bado; hata hivyo. *adj.* -tulivu; kimya. *v.t.* nyamazisha; tuliza. *n.* kikeneko: mtambo wa kukenekea vinywaji vikali.

**stilt** /stɪlt/ *n.* mronjo. **~ed** *adj.* (kwa usemi, mwandiko, mwenendo) si -kunjufu; rasmi mno.



stilt

**stimulant** /'stɪmjələnt/ *n.* kileo; kichocheo; kiburudisho; kichangamshi; kisisimuaji. **stimulate** *v.t.* amsha; chochea; himiza; changamsha; sisimua. **stimulus** *n.* kichocheo; kichangamshi.

**sting** /stɪŋ/ *n.* uvurenje; mwiba; *(fig.)* ukali; uchungu; kichomi. *v.t./i.* uma; choma; washa; chonyota. **~ing cell** *n.* wage: seli washaji inayotumiwa na baadhi ya wanyama, wadudu au samaki ili kujihami na adui.

**stink** /stɪŋk/ *n./v.i.* (**stank/stunk, stunk**) uvundo; nuka; fukiza harufu mbaya

**stipulate** /'stɪpjʊleɪt/ *v.t./i.* weka masharti. ~ *for*, shikilia jambo liingizwe katika mkataba au mapatano. **stipulation** *n.* sharti; mapatano.

**stir** /stɜ:(r)/ *n.* msisimko; kukoroga; kuvuruga. *v.t./i.* (**-rr-**) tikisa; koroga; vuruga; shtua; amsha; shtuka; amka. *The wind ~red the leaves*, upepo ulipeperusha majani.

*Nobody in the house was ~ring,* hapakuwa na mtu aliyekuwa macho nyumbani . *This news made quite a ~,* habari hizi zilileta msisimko. **~ring** *adj.* -a kuchochea; -a kusisimua.

**stitch** /stɪtʃ/ *n.* mshono; kushona. *v.t.* shona.

**stock** /stɒk/ *n.* shina; mti, tako la bunduki; wazazi; ukoo; jadi; nasaba; rasilimali; akiba; hisa; mifugo; supu. *He comes of farming ~,* wazazi wake ni wakulima. *The book is out of ~,* kitabu hakipatikani dukani. *take ~,* hesabu; kadiria; tathmini; pima. *take ~ of, (fig.)* tathmini. *live~,* mifugo *~ with,* jaza. *~ the shop with goods,* jaza duka kwa bidhaa. **~ breeder** *n.* mfugaji wa wanyama. **~broker** *n.* dalali. **~-still** *adv.* tuli; kimya kabisa.

**stocking** /'stɒkɪŋ/ *n.* soksi ndefu.

**stocky** '/stɒki/ *adj.* -fupi tena -nene.

**stoke** /stəʊk/ *v.t./i.* chochea; tia makaa tanurini. **~r** *n.* mchocheaji moto.

**stolid** /stɒlɪd/ *adj.* -zito; siodhihirisha hisia kirahisi.

**stoma** /'stəʊmə/ *n.* (**stomata**) stoma(ta): tundu ndogo katika majani ya mimea, hasa upande wa chini wa jani inayozungukwa na seli-linzi mbili.

**stomach** /'stʌmək/ *n.* tumbo. *~-ache,* kuumwa na tumbo. *v.t.* vumilia; stahamili : *I can't ~ his singing,* siwezi kuvumilia uimbaji wake.

**stone** /stəʊn/ *n.* jiwe; changarawe; kito; johari; kokwa. *v.t.* piga mawe; toa kokwa. *~-blind,* pofu kabisa. *~ dead,* -fu kabisa. *~-deaf,* kiziwi kabisa. **stony** *adj.* -enye mawe; -a mawe; -gumu; bila huruma.

**stool** /stu:l/ *n.* kiti kidogo; kibago; kibao; kigoda; stuli; kinyesi.

**stoop** /stu:p/ *n.* kibyongo. *v.i.* inama; *(fig.)* jitweza; jishusha.

**stop** /stɒp/ *n.* kituo; kikomo; nukta; mwisho; kizibo; kipasuo; kidhibiti mwanga. *v.t./i.* (**-pp-**) simamisha; komesha; simama; koma; ziba; funga; zuia; isha; katika; fikia. **~gap** *n.* badala; mbadala. **~per** *n.* kifuniko; kizibo.

**store** /stɔ:(r)/ *n.* akiba; vifaa; zana; ghala; bohari; stoo. *in ~,* -wapo tayari. *set great ~ on sth.,* thamini sana. *v.t. ~ up,* weka; kusanya; dunduliza.

**storey** /'stɔ:ri/ *n.* (**storeys**) ghorofa.

**stork** /stɔ:k/ *n.* korongo; gongo-singo.

**storm** /stɔ:m/ *n.* dhoruba; tufani. *take by ~,* vamia; twaa kwa nguvu. *v.t./i.* foka; vamia; ingia kwa nguvu. **~y** *adj.* -a dhoruba; -a tufani. **~ily** *adv.* kwa nguvu.

**story** /'stɔ:ri/ *n.* kisa; hadithi; masimulizi; hekaya; uzushi; makala.

**stout** /staʊt/ *adj.* -enye nguvu; hodari; thabiti; imara; nenenene. **~ly** *adv.* kwa ujasiri.

**stove** /stəʊtv/ *n.* stova; stovu.

**stow** /stəʊ/ *v.t.* weka; pakia; hifadhi; fungasha. **~away** *n.* mzamia meli; mdandia meli.

**straggle** /'strægl/ *v.i.* tapakaa; enea; tawanyika; chelewa; potea.

**straight** /streɪt/ *adj.* -a kunyooka; sawa; -a wima; sawasawa; -nyofu; -aminifu, -kweli; -a kufuata taratibu. *a ~ fight,* michuano ya wagombea wawili. *keep a ~ face,* jizuia kucheka. *adv.* moja kwa moja; bila kuchelewa. *~ away (off),* palepale. *say sth. ~ out,* sema waziwazi. **~en** *v.t./i.* nyoosha; fanya sawa; nyooka; -wa sawa. **~forward** *adj.* -aminifu; -a kwenda sawa; -epesi; rahisi.

**strain** /streɪn/ *n.* mkazo; lazima; mvuto; uchovu; mavune; machofu; kuteguka; dalili; mwelekeo; wimbo; uzao; ukoo; safumbegu. *v.t./i.* vuta kwa nguvu; nyoosha; kaza; jitahidi; chuja; tegua; teguka; lazimisha maana. *The rope broke under the ~,* kamba ilikatika kwa kuvutwa sana. **~ed** *adj.* -a shida; a mashaka. **~er** *n.* kichujio; chujio; kung'uto.

**strait** /streɪt/ *n.* mlango bahari; shida; taabu; dhiki; mashaka.

**strand** /strænd/ *n.* ufukwe; ufuko. *v.t.* pweleza; kwama; kwamisha. *be ~ed, (fig.)* achwa katika shida; kwama.

**strange** /streɪndʒ/ *adj.* -geni; -a ajabu. **~ly** *adv.* kiajabuajabu. **~ness** *n.* ugeni; ajabu; upya. **~r** *n.* mgeni. *He is a ~ here,* hajulikani hapa.

**strangle** /'stræŋgl/ *v.t.* nyonga; songa kwa kamba; kaba roho. **strangulation** *n.* kunyonga.

**strap** /stræp/ *n.* ukanda; kigwe. *v.t.* (**-pp-**) piga kwa ukanda; funga kwa ugwe.

**strategy** /'strætədʒi/ *n.* maarifa; mkakati; mbinu.

**stratosphere** /'stratəˌsfɪə/ *n.* angastrato; tabakastrato: tabaka la pili toka chini ya uso wa dunia hadi kufikia baina ya kilomita 50 na 60.

**stratum** /'strɑːtəm/ *n.* (**strata**) tabaka.

**stratification** *n.* utabakishaji.

**stratify** /'strætɪfaɪ/ *v.t.* tabakisha; gawanya; fanya matabaka.

**straw** /strɔː/ *n.* majani makavu; mrija. *the last ~,* pigo la mwisho.

**stray** /streɪ/ *v.i.* potea; tangatanga; zurura. *adj.* -liopotea; chache. *a ~ cat,* paka anayezurura; shume. *He was hit by a ~ arrow,* alipigwa kwa mshale uliokosa shabaha.

**streak** /striːk/ *n.* mfuo; mlia; mstari; mchirizi; kipindi kifupi; dalili; shubha. *like a ~ of lightning ,* upesi kama umeme. *He has a cruel ~ in his nature,* ana dalili ya ukatili. *v.t.* piga milia.

**stream** /striːm/ *n.* mto; mkondo; mwelekeo; mfululizo; msururu. *v.i.* tiririka; miminika; pepea. **~lined** *adj.* -lionyooka; -sio na mazonge.

**street** /striːt/ *n.* barabara; mtaa.

**strength** /strɛŋθ/ *n.* nguvu; uwezo; wingi. **~en** *v.t.* tia nguvu; imarika; imarisha.

**strenuous** /'streŋjʊəs/ *adj.* -enye bidii sana; -enye kuhitaji nguvu nyingi; -enye kutumia nguvu nyingi.

**stress** /stres/ *n.* msongo; kani; mkazo; shida; msisitizo; himizo. *v.t.* kaza; sisitiza.

**stretch** /stretʃ/ *n.* kujinyoosha; kupinda; eneo; upande ulionyooka. *v.t./i.* nyosha; jinyosha; panua; zidisha; eneza; enea. *~ a point in sb.'s favour,* pendelea mtu. **~er** *n.* machela; taruma.

**strew** /struː/ *v.t.* (**~ed**, **strewn**) tawanya; tapanya; tupatupa.

**stricken** /'strɪkən/ *adj.* -liojeruhiwa; -lioathiriwa; -liojaa majonzi; -liopatwa na maafa.

**strict** /strɪkt/ *adj.* -kali; -a kulazimisha utii; halisi; kamili; tupu. **~ly** *adv.* kabisa; kwa kweli; hasahasa; kwa ukali. **~ness** *n.* ukali; uhalisi; nguvu.

**stride** /straɪd/ *n.* hatua. *v.i.* panua miguu; tembea kwa hatua ndefu. *~ over,* chupa; ruka.

**strife** /straɪf/ *n.* ugomvi; mzozo; vita; mabishano.

**strike** /straɪk/ *n.* pigo; mgomo; ugunduzi; mashambulizi. *v.i./t.* (**struck**) piga; gonga; chapa; pata; gundua; shtusha; washa; choma; fikia; tua; shusha; panda mwamba; goma. *~ off (out),* futa; ondoa. *~ out,* anza. *~ out for yourself,* anzisha peke yako. *~ up, (music)* anza kupiga kinanda. *~ up a friendship with sb.,* anzisha usuhuba na mtu. *The clock struck four,* saa iligonga mara nne. *~ a flag,* shusha bendera. *~ a sail;* tua tanga. *~ a tent,* ng'oa hema. *~ a light,* washa taa. *~ a match,* washa kibiriti. *~ an average,* pata wastani. *~ a bargain,* patana. *~ a balance,* pata urari; afikiana. *~ oil* gundua mafuta. *~ the path,* vumbua njia. *~ terror into the enemy,* ogofya adui. *be struck dumb,* -wa bubu; pigwa na bumbuwazi. *How does the plan ~ you?* wauonaje mpango huu? *It has struck me that,* imenipitikia ya kuwa. *The porters are on ~,* wapagazi wamegoma. **~r** *n.* mgomaji; mshambuliaji. **striking** *adj.* -a kuvutia; -a ajabu.

**string** /strɪŋ/ *n.* uzi; kamba. *v.t./i.* (**strung**) funga uzi; tunga. *~ together a story,* tunga hadithi. *highly strung,* -epesi kuona wasiwasi; -epesi kuchacharika. **~y** *adj.* -a nyuzinyuzi; kama nyuzi. *~ meat,* nyama yenye nyuzinyuzi.

**stringency** /'strɪndʒənsi/ *n.* ukali;

mwambo. *financial stringency*, hali ngumu ya kifedha.
**strip** /strɪp/ *n.* ujororo; upapi; ubale; upapi. *v.t./i.* (**-pp-**) vua; vulia; chuna; kumba; safisha; nyang'anya.
**stripe** /straɪp/ *n.* mlia; mstari; tepe.
**strive** /straɪv/ *v.i.* (**strove**, **striven**) jitahidi; pania; hangaikia; pigania.
**stroke** /strəʊk/ *n.* pigo; mlio wa kengele; mlio wa saa; kifafa; kiharusi; mstari; tukio la jaribio moja. *on the ~ of three*, saa tatu barabara. *v.t.* papasa; singa; sugua; chuachua.
**stroll** /strəʊl/ *n./v.i.* matembezi; tembea polepole.
**strong** /strɒŋ/ *adj.* -a nguvu; imara; hodari; thabiti; kali; -a athari kubwa; -chungu. **~ acid**, asidi kali: asidi ambayo inavunjika rejea kwa ukamilifu na kuwa ioni tupu katika mmumunyo. **~ly** *adv.* kwa nguvu sana.
**strontium** /'strɒntɪəm/ *n.* strontiamu: elementi ya kikemikali laini ya rangi ya fedha yenye mionzi nururishi ikusanyikayo katika mifupa mwilini.
**structure** /'strʌktʃə(r)/ *n.* muundo; kiunzi; umbile; jengo. **structural** *adj.* -a muundo; -a jengo. **structural linguistics**, isimu miundo. **structural meaning**, maana kiuamilifu. **structural semantics**, semantiksi miundo. **structural word**, neno amilifu. **structuralism**, uisimu miundo.
**struggle** /'strʌgl/ *n.* bidii; jitihada; harakati; mapambano. *class ~*, harakati za kitabaka. *v.i.* shindana; jitahidi; pambana.
**strut**[1] /strʌt/ *v.i.* (**-tt-**) enda kwa mikogo.
**strut**[2] /strʌt/ *n.* taruma; kiegemeo.



**struts**

**stub** /stʌb/ *n.* kisiki; kipande; kibutu; kishungi. *v.t.* (**-bb-**) *~ one's toe*, jikwaa.
**stubble** /'stʌbl/ *n.* mashina ya majani au mabua yaliyokatika; ndevu fupi ngumu.
**stubborn** /'stʌbən/ *adj.* -kaidi; -sugu; -shupavu.
**stud** /stʌd/ *n.* kifungo; msumari; njumu.
**studio** /'stju:diəʊ/ *n.* studio: **1.** chumba cha msanii au mpiga picha. **2.** bwalo la kuigizia na kupigia filamu. **3.** chumba cha kurushia matangazo ya redio au televisheni.
**study** /'stʌdi/ *n.* chumba cha kusomea; kujifunza; mtaala; mtalaa; masomo; utafiti; uchunguzi. *v.t./i.* jifunza; soma; talii; durusu; chunguza; tafiti.
**student** /'stju:dnt/ *n.* mwanafunzi; mwanachuo.
**studied** /'stʌdɪd/ *adj.* ya makusudi; -liodhamiriwa; -liotafitiwa. *a ~ insult*, tusi la kukusudia. **studious** *adj.* -angalifu; -enye bidii katika masomo.
**stuff** /stʌf/ *n.* vitu; vyombo; zana; vikorokoro; vifaa. *v.t.* jaza; shindilia; danganya. **~y** *adj.* -sio hewa ya kutosha; -nunaji; siostahamili kitu.
**stumble** /'stʌmbl/ *v.i.* jikwaa; babaika; suudia; yumbayumba. *~ on*, kuta; pata kwa bahati.
**stump** /stʌmp/ *n.* kisiki; kigutu. *v.t./i.* enda kwa kishindo; *(colloq.)* fadhaisha. *His question completely ~s me*, swali lake linanitatiza kabisa. *(cricket)* toa kwa kugonga kijiti. **~y** *adj.* -fupi tena -nene.
**stun** /stʌn/ *v.t.* (**-nn-**) ziraisha; fadhaisha; tia bumbuazi; shtua.
**stunt**[1] /stʌnt/ *v.t.* viza; dumaza.
**stunt**[2] /stʌnt/ *n.* *(colloq.)* mkogo; tendo la kuonyesha ustadi.
**stupid** /'stju:pɪd/ *n.* zuzu; baradhuli; mpumbavu; mjinga. *adj.* pumbavu; -jinga; -zuzu. **~ity** *n.* upumbavu; uzuzu; ujinga; ubaradhuli.
**stupor** /'stju:pə/ *n.* mzubao.
**sturdy** /'stɜ:di/ *adj.* -enye nguvu; thabiti; hodari; imara; shupavu.
**stutter** /'stʌtə(r)/ *v.i./t.* gugumiza; gotagota maneno.
**sty(e)** /staɪ/ *n.* (katika jicho) chokea.
**style** /staɪl/ *n.* mtindo; ufahari. **stylish** *adj.* -a fahari kupindukia; -a mtindo. **stylist** *n.* msanifu mitindo.

**sub-** /sʌb/ *prefix* -a chini; -dogo. **~atomic particle**, chembe atomu: chembe yoyote ambayo hutokana na atomu.

**subconscious** /ˌsʌb'kɒnʃəs/ *adj.* -a kufichika akilini.

**subdivide** /'sʌbdɪvaɪd/ *v.t./i.* zidi kugawa; zidi kugawanyika.

**subdue** /səb'dju:/ *v.t.* shinda; tuliza; punguza nguvu; tuliza; tiisha. **~d light**, nuru iliyopunguzwa nguvu.

**subheading** *n.* kichwa kidogo cha habari.

**subject** /'sʌbdʒɪkt/ *n.* raia; mwananchi; mada; habari; mazungumzo; mhusika; somo; kiima. *adj.* liotawaliwa na serikali; -sio huru; -lioelekea kuathiriwa na. *~ to*, kwa sharti kwamba; ikiwa; kwa kutegemea. *~ to your approval*, ikiwa utaidhinisha. *v.t.* tawala; athiri; jitoa; toa. **~ion** *n.* kutawaliwa; kugandamizwa; kukomesha.

**subjugate** /'sʌbʒʊgeɪt/ *v.t.* shinda kabisa; komesha; tiisha.

**sublime** /sə'blaɪm/ *adj.* -a juu sana; bora sana; -kuu; adhimu; -tukufu; -a fahari; a ajabu.

**submarine** /ˌsʌbmə'ri:n/ *n.* sabmarini; nyambizi: aina ya merikebu itembeayo chini ya maji. *adj.* -a chini ya bahari.

**submerge** /səb'mɜ:dʒ/ *v.t./i.* zamisha; zama; didimiza; piga mbizi.

**submit** /səb'mɪt/ *v.t./i.* (**-tt-**) tii; jiweka chini; lazimisha; wasilisha; toa; ridhia; jisalimisha; vumilia; ridhia; toa hoja. **submission** *n.* utii; kujisalimisha; kukubali; unyenyekevu; uwasilishaji. **submissive** *adj.* -tiifu; -nyonge; nyenyekevu.

**subordinate** /sə'bɔ:dɪnət/ *adj.* -a chini; -dogo; -tegemezi; -saidizi.

**subscribe** /səb'skraɪb/ *v.t./i.* changa; lipia; tia saini; unga mkono. *~ $5 to a flood relief fund*, changia dola 5 kwa mfuko wa mafuriko. *~ to a newspaper*, jiandikisha na lipia ili uletewe gazeti. *~ to opinions*, kubaliana na maoni. **~r** *n.* mchangaji; mteja. **subscription** *n.* mchango; ada; utiaji saini.

**subsequent** /'sʌbsɪkwənt/ *adj.* -a baadaye; -a kufuatia; -a kutokea. **~ly** *adv.* baadaye; hatimaye.

**subset** /'sʌbset/ *n.* setindogo, sabseti: seti iliyomo au inayoweza kuwa ndani ya seti nyingine.

**subside** /səb'saɪd/ *v.i.* (kwa maji) zizimia; pungua; (kwa ardhi) didimia; (kwa majengo) musu: kudidimia jengo au sehemu yake katika ardhi; titia; (kwa upepo) tulia.

**subsidiary** /səb'sɪdiəri/ *adj.* -a kusaidia; saidizi; -dogo. **subsidize** *v.t.* toa ruzuku; saidia. **subsidy** *n.* ruzuku.

**subsist** /səb'sɪst/ *v.i.* ishi kwa; ponea; jikimu. **~ence** *n.* chakula; riziki. **~ crops**, mazao ya chakula. **~ allowance**, posho ya kujikimu. **~ economy**, uchumi wa kijungumeko.

**subsonic** /ˌsʌb'sɒnɪk/ *adj.* kasi yoyote iliyo chini ya kasi ya sauti.

**substance** /ˌsʌbstəns/ *n.* dutu; kitu; maana; kiini; nguvu; uthabiti; utajiri; mali.

**substantial** /səb'stænʃl/ *adj.* imara; -kubwa; thabiti; maridhawa; -tajiri; -kwasi; -a msingi; halisi.

**substitute** /'sʌbstɪtju:t/ *n.* badala. *v.t.* badili; chukua nafasi ya; weka mahali pa. **substitution** *n.* kibadala; ubadilishaji.

**subtend** /sʌb'tɛnd/ *v.t.* kingama; elekeana na; kabili; ngoeka; kuwa mkabala na.

**subterranean** /ˌsʌbteə'reɪnɪən/ *adj.* -a chini ya ardhi.

**subtle** /'sʌtl/ *adj.* -gumu kueleza; -a kutatiza; -a hila; -a akili; stadi. **~ty** *n.* werevu; busara; akili.

**subtract** /səb'trækt/ *v.t.* toa; ondoa; punguza. **~ion** *n.* kutoa; kuondoa.

**subtropical** /ˌsʌb'trɒpkl/ *adj.* -liopakana na tropiki.

**suburb** /'sʌbɜ:b/ *n.* kiunga cha mji; pambizo ya mji. **~an** *adj.* -a pambizoni; -a kiungani.

**subway** /'sʌbweɪ/ *n.* njia ya chini kwa chini; njia ya treni ipitayo chini kwa chini .

**succeed** /sək'si:d/ *v.i./t.* faulu;

fanikiwa; pata; fuzu; rithi. ~ *in passing an examination,* faulu mtihani.

**success** /sək'ses/ *n.* ufanisi; mafanikio **successful** *adj.* -a kufanikiwa; -a kufuzu; -a bahati njema.

**succession** /sək'seʃn/ *n.* mfuatano; mfululizo; msururu, maandamano; urithi. **successive** *adj.* -a kufuatana; -a moja kwa moja; -a mfululizo

**successor** /sək'sesə(r)/ *n.* mrithi.

**succumb** /sə'kʌm/ *v.i.* shindwa; -fa. ~ *to a temptation,* shindwa na matamanio ya nafsi.

**such** /sʌtʃ/ *adj./pron.* kama; hivyo; hivi; mno; hasa; hii; hiyo; hayo. ~ *a business,* shughuli kama hiyo. ~ *as,* kama; jinsi. ~ *as it is,* jinsi ilivyo. ~ *as to,* kiasi cha. ~ *that,* kiasi kwamba.

**suck** /sʌk/ *v.t.* fyonza; nyonya; mung'unya; -nywa; nywesheleza; vuta. *The plants ~ moisture from the soil,* mimea hufyonza unyevu kutoka ardhini. *(fig.)* nyonya maarifa. *He was merely out to ~ other people's brains,* nia yake ilikuwa kunyonya maarifa ya wingine. **~le** *v.t* nyonyesha; nyonya. **~ling** *n.* mtoto anyonyaye.

**suction** /'sʌkʃn/ *n.* ufyonzaji; uvutaji; mvuto; mfyonzo.

**sucrose** /'s(j)u:krəʊz/ *n.* sukrosi: disakaridi tamu nyeupe ya kifuwele, hupatikana toka kwenye miwa au jamii ya viazi vitamu.

**sudden** /'sʌdn/ *adj.* -a ghafla; -siotazamiwa. **~ly** *adv.* ghafla; mara.

**sue** /su:/ *v.t./i.* shtaki; omba; sihi. ~ *for peace,* omba amani. ~ *for mercy,* omba kuhurumiwa.

**suffer** /'sʌfə(r)/ *v.t./i.* sumbuliwa na; umwa; teseka; vumilia; patwa na; teswa; ruhusu. **~ance** *n.* uvumilivu; mateso; ustahamilivu. *He is here on ~,* ameruhusiwa kuwepo kwa shingo upande. **~ing** *n.* maumivu; mateso; taabu.

**suffice** /sə'faɪs/ *v.i./t.* tosha; tosheleza; kifu; kidhi.

**sufficient** /sə'fɪʃnt/ *adj.* -a kutosha maridhawa; -a kukifu; -a kuridhisha. **sufficiency** *n.* utoshelevu.

**suffix** /'sʌfɪks/ *n (gram.)* kiambishi tamati.

**suffocate** /'sʌfəkeɪt/ *v.t./i.* songa; kosa hewa, kaba roho, nyonga **suffocation** *n* kukosa hewa kusonga roho.

**sugar** /'ʃʊgə(r)/ *n.* sukari. **brown, unrefined,** ~ sukari guru. ~ **refinary**, kiwanda cha sukari.

**suggest** /sə'dʒest/ *v.t.* pendekeza; toa shauri; toa rai; maanisha; ashiria; dokeza. **~ion** *n.* maoni; pendekezo; wazo; fikra; rai; ushauri. **~ive** *adj.* -a kushawishi; pujufu; -enye kuashiria.

**suicide** /'s(j)u:ɪsʌd/ *n.* kujiua; kujiangamiza; mtu anayejiua. **suicidal** *adj.* -a kujiua; -a kujiangamiza.

**suit** /su:t/ *n.* suti; mashtaka; daawa; madai; karata za namna moja. *follow ~, (fig.)* fuata mkumbo. *v.t.* faa; stahiki; juzu; stahilia; pendeza; oanisha; patanisha; linganisha. ~ *sth to,* oanisha. *be ~ed for,* faa kwa. *He is ~ed for teaching,* afaa ualimu. **~ability** *n.* kufaa. **~able** *adj.* -a kufaa; -a kustahili. **~ably** *adv* kwa kufaa. **~case** *n.* sanduku la nguo. **~or** *n.* mdai; mchumba.

**sullen** /'sʌlən/ *adj.* -enye kununa; -chukivu; -enye kinyongo. **~ness** *n.* chuki; kinyongo.

**sully** /'sʌli/ *v.t.* chafua; paka matope; vunjia kadiri.

**sulphate** /'sʌlfeɪt/ *n.* sulfati: chumvi ya asidi sulfuriki.

**sulphur** /'sʌlfə(r)/ *n.* salfa; kibiriti; kibiriti upele. ~ **dioxide**, salfa dioksidi: gesi isiyo na rangi ikohozayo. **~etted** *adj.* -enye salfa. **~ic acid**, asidi sulfuriki. **~ous** *adj.* -enye salfa.

**sultry** /'sʌltri/ *adj.* -a joto kali; -a hari; -enye ashiki nyingi.

**sum** /sʌm/ *n.* jumla; *(arith.)* hesabu; kiasi cha fedha. *in ~,* kwa ufupi. *v.t.* ~ *up,* jumlisha; hesabu; soma; eleza kwa muhtasari. **~marize** *v.t.* fupisha; fanya muhtasari. **~mary**

n. muhtasari. *adj.* -a papo hapo; bila kukawia; -a mara moja. **~mation** *n.* kujumlisha; jumla; muhtasari.

**summer** /'sʌmə(r)/ *n.* kiangazi; kaskazi; majira ya joto.

**summit** /'sʌmɪt/ *n.* kilele; upeo. **~ meeting** *n.* mkutano wa wakuu wa nchi.

**summon** /'sʌmən/ *v.t.* ita; ita kortini; kusanya. ~ *up,* kusanya. *He ~ed up all his strength,* alikusanya nguvu zake zote. **~s** *n.* (**~es**) notisi ya kufika mahakamani; amri ya kufika mahali.

**sun** /'sʌn/ *n.* jua; mwangaza au joto la jua; nyota. *v.t.* (**-nn-**) ota jua; jianika juani. **~burn** *n.* wekundu au mbabuko wa ngozi kwa sababu ya jua kali. **~dial** *n.* saa ya kivuli. **~ny** *adj.* -a jua. *(fig.)* -a furaha; -kunjufu. **~rise** *n.* mapambazuko. **~set** *n.* machweo; kuchwa; magharibi. **~spots**, mabaka ya jua: madoa meusi yanayoonekana kwenye jua ambayo huwa ni vyeneo vya gesi iliyopoa. **~stroke** ugonjwa unaotokana kwa kupigwa sana na jua kali.

**Sunday** /'sʌndeɪ/ *n.* Jumapili.

**sundry** /'sʌndri/ *adj.* kadha wa kadha; anuwai; baadhi; -ingine. *all and ~,* watu wote. **sundries** *n.* magorogojo; vikorokoro.

**super-** /'su:pə(r)/ *prefix.* zaidi ya; -a kupita kiasi; -a juu; *(colloq.)* bora; -a kupendeza; safi sana.

**superannuate** /ˌs(j)u:pər'anjʊeɪt/ *v.t.* staafisha; lipa kiinua mgongo.

**superb** /'su:pɜ:b/ *adj.* -zuri sana.

**superconductivity** *n.* upitifuhuru: tabia ya baadhi ya metali kupitisha umeme bila ukinzani katika halijoto karibu na sifuri halisi.

**superficial** /ˌsu:pə'fɪʃl/ *adj.* -a juujuu; -a kubabaisha. **~ly** *adv.* kijuujuu; kwa kubabaisha.

**superfluous** /su:'pɜ:fluəs/ *adj.* -a kupita kiasi; -liozidi.

**superintend** /ˌsu:pərɪn'tend/ *v. t./i.* simamia; angalia; amuru kazi; rakibu; ongoza. **~ence** *n.* usimamizi; uongozi; urakibu. **~ent** *n.* msimamizi; mrakibu; mwangalizi; mwongozaji.

**superior** /su:'pɪəriə(r)/ *n.* mkuu. *adj.* bora; -ingi zaidi; enye kuzidi; -a cheo cha juu; -nye kiburi. *The enemy were in ~ numbers,* maadui walikuwa wengi. ~ *to,* -a kupita ingine.

**superlative** /su'pɜ:lətɪv/ *adj.* bora mno; *(gram.) the ~ degree,* sifa ya juu kabisa.

**supernova** /ˌs(j)u:pə'nəʊvə/ *n.* supanova: nyota ambayo mng'aro wake huongezeka ghafla kutokana na mripuko wake.

**supersede** /ˌs(j)u:pə'si:d/ *v.t.* chukua nafasi ya.

**supersonic** /ˌsu:pə'sɒnɪk/ *adj.* supasoniki: -a zaidi ya kasi ya sauti.

**superstition** /ˌsu:pə'stɪʃn/ *n.* ushirikina; imani ya uchawi. **superstitious** *adj.* -a ushirikina.

**supervise** /'su:pəvaɪz; 'sju:-/ *v.t.* simamia; angalia; ongoza. **supervision** *n.* usimamizi; uangalizi. **supervisor** *n.* msimamizi; mwangalizi.

**supper** /'sʌpə(r)/ *n.* chakula cha usiku.

**supplant** /sə'plɒ:nt/ *v.t.* twaa mahali pa; chukua nafasi ya; -wa badala. *Wooden implements are being ~ed by iron ones,* vyombo vya chuma vinachukua mahali pa vile vya mbao.

**supple** /'sʌpl/ *adj.* -a kunesa; -nyumbufu. *the ~ limbs of children,* viungo laini vya watoto; *a ~ mind, (fig.)* akili nyepesi.

**supplement** /'sʌplɪmənt/ *n.* nyongeza; ziada. *v.t.* ongeza; jaliza. **~ary** *adj.* -a kuongezea; -a ziada; -a kurudia. ~ *examinations,* mitihani ya marudio.

**supplicate** /'sʌplɪkeɪt/ *v.t./i.* omba; sihi; lalama. **supplicant** *n./adj.* mwombaji; -enye kuomba.

**supply** /sə'plʌɪ/ *n.* kuweka; kutoa; kuleta; ugavi; akiba. *v.t.* toa; leta; -pa; kimu; ruzuku.

**support** /sə'pɔ:t/ *n.* kuchukua; kutegemeza; mhimili; mwega; kiamu; msaada; muawana; mtetezi; uungaji mkono. *v.t.*

chukua; tegemeza; himili; egemeza; saidia; unga mkono; auni; fadhili; kimu; ruzuku; stahamili. *in ~ of*, kwa kusaidia.

**suppose** /sə'pəʊz/ *v.t.* dhani; chukulia kwamba; tuseme; waonaje; hitaji; kisia. *~ the world were flat*, tuseme dunia ni bapa. *The creation ~s a Creator*, kiumbe chahitaji Muumbaji. *~ we go for a swim*, waonaje tukienda kuogelea. *~ you have another try*, waonaje ukijaribu tena. *be ~d to*, tazamiwa; tarajiwa; takiwa. **supposing** *conj.* kama; ikiwa; iwapo. **supposition** *n.* wazo; dhana; kukisia.

**suppress** /sə'pres/ *v.t.* komesha; kandamiza; shinda; ficha; zima; zuia. **~ion** *n.* uzuiaji; ukandamizaji. **~or** *n.* mkomeshaji; mkandamizaji; kizuiaji: chombo kinachozuia nguvu za umeme.

**supreme** /su:'pri:m/ *adj.* -a juu kabisa; -enye mamlaka makubwa kabisa; -enye uwezo mkubwa kabisa; -kubwa kabisa.

**supremacy** /su:'preməsi/ *n.* uwezo wa juu kabisa; mamlaka ya juu kabisa. **~ly** *adv.* sana; mno.

**surcharge** /'sɜ:tʃɒ:dʒ/ *n.* malipo ya ziada; mhuri wa posta unaobadilisha thamani ya stempu; mzigo wa ziada.

**sure** /ʃʊə/ *adj.* -a hakika; -a yakini; -a kweli; -a kuaminika. *feel ~ of oneself*, jiamini. *be ~ to come*, usikose kuja. *make ~*, hakikisha. *adv. ~ enough*, kwa hakika; kwa kweli. **~ly** *adv.* bila shaka; kwa hakika. **~ty** *n.* dhamana; mdhamini.

**surf** /sɜ:f/ *n.* shanua; povu la mawimbi ya maji.

**surface** /'sɜ:fɪs/ *n.* umbo la nje; uso; sura; juu; sehemu ya juu. *adj.* -a nje; -a juu. **~ tension**, mkakamao uso: kani tanjiti katika uso wa kioevu wenye uelekeo sulubi na hivyo kufupisha ueneaji wake.

**surfeit** /'sɜ:fɪt/ *n.* shibe; kinaya.

**surge** /sɜ:dʒ/ *v.i.* enda mbele; enea; tapakaa; bingiria. *The crowds ~d out of the gate*, watu walitoka mlangoni kwa makundi.

**surgeon** /'sɜ:dʒən/ *n.* daktari mpasuaji.

**surgery** /'sɜ:dʒəri/ *n.* upasuaji; thieta. **surgical** *adj.* -a upasuaji; -a kupasulia.

**surly** /'sɜ:li/ *adj.* kali, -a kisirani; -gomvi. **surliness** *n.* ukali; kisirani; chuki; uchungu.

**surmount** /sə'maʊnt/ *v.t.* shinda; kiuka vikwazo.

**surname** /'sɜ:neɪm/ *n.* jina la ukoo.

**surpass** /sə'pɑ:s/ *v.t.* pita; shinda; zidi.

**surplice** /'sɜ:pləs/ *n.* kanzu ya kasisi.

**surplus** /'sɜ:pləs/ *n.* ziada.

**surprise** /sə'praɪz/ *n.* mshangao; fadhaa; mastaajabu; mzubao. *v.t.* shangaza; fadhaisha; duwaza; shtusha; shtukiza. **surprising** *adj.* a kushangaza; -a kustaajabisha.

**surrender** /sə'rendə(r)/ *n.* kujisalimsha; kusalimu amri; kuacha; kujitoa. *v.t./i.* jisalimisha; salimu amri; acha; jiachia; kubali kushindwa. *~ one's goods as a surety*, weka dhamana mali yako. *~ oneself to sb.'s care*, jiweka chini ya himaya fulani. *(fig.) ~ oneself to*, jisalimisha.

**surround** /sə'raʊnd/ *v.t.* zunguka; zungushia; zingia; zinga; zingira. **~ings** *n.* mazingira, mahali jirani.

**survey** /sə'veɪ/ *n.* ukaguzi; upimaji; mapitio; uchunguzi. *v.t.* tazama; kagua; aua; pitia; pima ramani. **~or** *n.* mkaguzi; sarufeya; mkadiriaji.

**survive** /sə'vaɪv/ *v.t./i.* ponea chupuchupu; endelea kuishi; okoka. **survival** *n.* kuendelea kuishi; kupona; wokovu; masalio. **survivor** *n.* muokokaji; msaliaji.

**susceptible** /sə'septəbl/ *adj.* -epesi kuathirika; -epesi kuhisi. *~ of proof*, -a kuweza kuthibitika.

**suspect** /sə'spɛkt/ *n.* mtuhumiwa; mshukiwa. *v.t.* dhani; kisi; tuhumu; tilia shaka; shuku; dhani; waza. *He ~ed that the enemy were hiding among the trees*, alishuku kuwa maadui walikuwa wamejificha katika miti.

**suspend** /sə'spend/ *v.t.* tundika;

angika; elea; ning'iniza; simamisha, ondoa kwa muda; zuia; weka kando; subirisha; ahirisha. **~er** *n.* ukanda wa kuzuia suruali isivuke. **suspension** *n.* kiangiko; kutungika; kuangika; kuondoshwa kwa muda; kusimamishwa. **suspension bridge**, daraja ning'inizi.

**suspense** /sə'spens/ *n.* mashaka; wasiwasi; hatihati.

**suspicion** /sə'spɪʃn/ *n.* tuhuma; shaka; tuhuma; dhana mbaya. **suspicious** *adj.* -enye shaka; -a kutuhumu; ya wasiwasi.

**sustain** /sə'steɪn/ *v.t.* himili; chukua; patwa na matatizo; vumilia; *(law)* kubaliana na; idhinisha; toa idhini. **sustenance** *n.* chakula; riziki.

**swagger** /'swægə(r)/ *v.i.* tamba; randa; enda kwa kujivuna. *n.* majivuno. ~ *cane,* kifimbo cha askari.

**Swahili** /swə'hi:li/ *n./adj.* Mswahili; Kiswahili.

**swallow**[1] /'swɒləʊ/ *n.* kumeza; funda. *v.t./i.* meza. ~ *one's words,* tia ulimi puani.

**swallow**[2] /'swɒləʊ/ *n.* kijumbamshale; barawai; mbayuwayu; mbiliwili.

**swamp** /swɒmp/ *n.* kinamasi. *v.t.* jaza maji; tosa majini; vuika majini; *(fig.)* lemea; lemewa na; zidi; zidiwa na. **~y** *adj.* -a topetope; -a majimaji; -a kinamasi.

**swan** /swɒn/ *n.* bata maji.

**swap** /swɒp/ *v.t./i.* (**-pp-**) badili mali kwa mali.

**swarm**[1] /swɔ:m/ *n.* kundi kubwa la wadudu au ndege. *v.i.* enda pamoja katika kundi. ~ *with,* -wa -ingi; jaa sana.



swan

**swarm**[2] /swɔ:m/ *v.i./t.* ~ *up;* paraga; paramia.

**sway** /sweɪ/ *n.* kuyonga; kuyumba; nguvu; mvuto. *v.i./t.* yonga; yumbisha; yumba; geuza; vuta; shawishi.

**swear** /sweə(r)/ *v.t./i.* (**swore**, **sworn**) apa; apisha; kula yamini; kula kiapo; lisha kiapo. ~ *by sth.,* apia kama shahidi; *(colloq.)* tegemea; laani; apiza; tukana. **~er** *n.* mwapizaji; mtukanaji.

**sweat** /swet/ *n.* jasho; unyevu; majimaji; *(colloq.)* kazi ngumu; sulubu. **~ glands**, tezi jasho: tezi ndogondogo zilizopo katika ngozi ya mamalia zitoazo jasho. *v.i./t.* toa; toka jasho; toza jasho; toa kitu; sulubika; nyonya. **~er** *n.* sweta.

**sweep** /swi:p/ *n.* kufagia; upeo; pigo; mkupuo; mkondo; msafisha dohani; kafi; kasia; upondo. *v.t./i.* (**swept**) fagia; pangusa; kumba; enda kwa fahari; tamba; enea; tanda; pita upesi; kokoa; peperusha; zoa; safisha. *Houses were swept away by the floods,* nyumba zilikokolewa na mafuriko. *She swept out of the room,* alitoka chumbani kwa madaha. *make a clean ~ of sth. (fig.)* ondolea mbali. **~ing** *adj.* -a jumla; -kubwa. **~stake** *n.* kamari ya fedha katika shindano.

**sweet** /swi:t/ *n.* kitu kitamu; mpenzi; kipenzi. *adj.* -tamu; safi; -zuri; -a kupendeza; -a kuvutia; -a kunukia. **~en** *v.t./i.* fanya tamu; -wa tamu. **~heart** *n.* mpenzi. **~meat** *n.* halua.

**swell** /swel/ *n.* mawimbi makubwa; uvimbaji. *v.i./t.* (**~ed ~ed**/**swollen**) vimba; vimbisha; tuna; tunisha; tunza; tanuka. **~ing** *n.* uvimbe; ziada; nyongeza.

**swelter** /'sweltə(r)/ *v.i* ona joto sana.

**swerve** /swɜ:v/ *n.* mchepuko. *v.i./t.* gauka; enda upande; chepuka; pinda ghafla.

**swift**[1] /swɪft/ *adj.* -epesi; -a ghafla; -a haraka; -a mbio. **~ly** *adv.* upesi; kwa haraka; hima.

**swift**[2] /swɪft/ *n.* kijumbamshale; mbiliwili; mbayuwayu; barawai.

**swim** /swɪm/ *n.* kuogelea. *v.i./t.* (**-mm-**, **swam**, **swum**) ogelea; ona kizunguzungu; jawa na. *His eyes were ~ming with tears,* macho yake yalijaa machozi. *be in the ~,* fahamu au shiriki katika mambo yanayotokea. **~mingly** *adv.* vizuri

kabisa; bila matatizo; kirahisi.
**swindle** /'swɪndl/ *v.t.* danganya; tapeli; laghai; ghilibu. **~r** *n.* ayari; tapeli; dhalimu.
**swing** /swɪŋ/ *n.* kubembea; pembea; bembea. *v.i./t.* (**swung**) pembea; pembeza; bembea; bembeza; geuka; geuza; enda upande. *go with a ~,* fuata mdundo. *be in full ~,* pamba moto.
**swirl** /swɜ:l/ *v.i./t.* zunguka mbiombio; zungusha mbiombio.
**switch** /swɪtʃ/ *n.* swichi; ufito; mchapo; mtambo wa kubadilisha njia za reli; kishungi; mgwisho. *v.t./i. ~ on,* washa; fungua. *~ off,* zima.



switch

**swivel** /'swɪvl/ *n.* pete yenye kuzunguka; ekseli. *v.t.* (**-ll-**) zungusha; zunguka.
**swoop** /swu:p/ *v.i.* shuka chini kwa kasi (kama tai, kipanga, etc.); ruka chini; chupa; pokonya; pora.
**swop** *v.t./i.* (**-pp-**) *(colloq.)* badili mali kwa mali.
**sword** /sɔ:d/ *n.* upanga; kitara; jambia; sime.
**swot** /swɒt/ *n.* mbukuaji; kazi nzito. *v.i.* (**-tt-**) *(slang)* soma kwa bidii; bukua.
**syllable** /'sɪləb(ə)l/ *n.* silabi.
**syllabus** /sɪləbəs/ ɔ*n.* muhtasari wa mafundisho.
**symbiosis** /ˌsɪmbɪ'əʊsɪs/ *n.* ufaano: utegemeanaji wa viumbe viwili hai.
**symbol** /'sɪmbl/ *n.* ishara; alama; dalili. **~ic** *adj.* -a mfano; -enye maana; -a ishara. **~ize** *v.t.* -wa ishara ya; onyesha kwa ishara; ashiria.
**symmetrical** /sɪ'metrɪkl/ *adj.* -a pacha; -a sawa; linganifu.
**symmetry** /'sɪmətri/ *n.* mpachano, pacha: mlingano wa kilingo; umbo na mpangilio wa sehemu mkabala za bapa, mstari au nukta; ulinganifu; usawa; mlingano.
**sympathy** /'sɪmpəθi/ *n.* upole; huruma; utu wema. *be in ~ with,* hurumia; sikitikia. **sympathetic** *adj.* -a huruma; -pole; -a roho nzuri. **sympathize** *v.i. be in ~ with;* hurumia; sikitikia.
**symphony** /'sɪmfəni/ *n.* simfoni: muziki upigwao kwa kutumia ala nyingi kwa pamoja.
**symptom** /'sɪmptəm/ *n.* alama; ishara; dalili. **~atic** *adj.* -a dalili; -a ishara.
**synagogue** /'sɪnəgɒg/ *n.* sinagogi; nyumba ya ibada ya Wayahudi.
**synchronize** /'sɪŋkrənʌɪz/ *v.t./i.* patanisha; oanisha.
**syncline** /'sɪŋklʌɪn/ *n.* sinklini: mkunjo katika tabaka ya majabali sedimenti unaosababishwa na msogeo wa tabaka za ardhi.
**syndicate** /'sɪndɪkət/ *n.* ushirika wa mashirika yenye shughuli za aina moja; ushirika wa waandishi makala magazetini.
**synod** /'sɪnəd,/ *n.* sinodi: eneo la majimbo ya kanisa; mkutano wa majimbo ya kanisa.
**synonym**. /'sɪnənɪm/ *n.* sinonimia; kisawe: neno lenye maana linalo-karibiana sana kimaana na lingine. **~ous** *adj.* -enye maana karibu sawa.
**synopsis** /sɪ'nɒpsɪs/ *n.* (**synopses**) muhtasari; ufupisho.
**synovial capsule** *n.* kibumba sinovia: kiwambo kama kifuko kinachozunguka mifupa miwili inayotembea kwenye kiungo.
**synovial fluid** *n.* ute lainishi: ute mwili ulioko katika sehemu wazi za viungo kama vile mfereji wa chakula.
**syntax** /'sɪntaks/ *n.* sintaksi: tawi la isimu linalohusu uhusiano wa kisarufi wa vipashio na maneno.
**synthesis** /'sɪnθɪsis/ *n.* usanisi.
**synthesize** /'sɪnθɪsʌɪz/ *v.t.* sanisi.
**synthetic** *adj.* sanisi. **synthetical** *adj.* -a usanisi. **synthetic chemistry**, kemia sanisi. **synthetically** *adv.* kisanisi.
**syphilis** /'sɪfɪlɪs/ *n.* kaswende: mojawapo ya maradhi ya zinaa.
**syphon** *n.* mrija; neli; kifyonzaji.
**syringe** /sɪ'rɪn(d)ʒ, 'sɪ-/ *n.* sirinji.
**syrup** /'sɪrəp/ *n.* shira.

**system** /'sɪstəm/ *n.* mfumo; utaratibu. **the nervous ~**, mfumo wa neva. *Too much alcohol is bad for the ~*, kunywa ulevi wa kupindukia ni hatari kwa afya ya mtu.

# Tt

**tab** /tæb/ *n.* nembo ya karatasi au ya kitambaa iliyo katika nguo; kibonye bapa ambacho ni ala ya kiibodi kwenye kompyuta kitoacho fursa ya mfulizo wa vituo na miruko.

**table** /'teɪbl/ *n.* meza; watu waliokaa mezani; ratiba; orodha; jedwali; jiwe. *His talk amused the whole ~*, mazungumzo yake yalifurahisha wote waliokuwa mezani. *keep a good ~*, andaa chakula vizuri. **~cloth** *n.* kitambaa cha meza. **~land** *n.* nchi tambarare kwenye mwinuko. **~spoon** *n.* kijiko cha kulia.

**tablet** /'tæblet/ *n.* (la zamani) kibao cha kuandikia; padi; kidonge cha dawa; kipande cha sabuni.

**tabular** /'tæbjələ(r) /*adj.* -liopangwa katika jedwali.

**tabulate** /'tæbjuleɪt/ *v.t.* panga katika jedwali; orodhesha.

**tabulator** *n.* mashine ya kuorodhesha; mashine ya kupangilia.

**taboo** /tə'bu:/ *n.* mwiko; miko; haramu.

**tack** /tæk/ *n.* msumari mfupi mdogo; kupiga bandi; kushikiza; mbisho wa meli; *(fig.) be on the right ~*, fuata mwelekeo mzuri. *v.t./i.* kupigilia kwa misumari midogo; shikiza; piga bandi; kisi.

**tackle** /'tækl/ *n.* vyombo; zana; vifaa; kukamata kwa nguvu. *fishing ~*, vyombo vya kuvulia samaki. *v.t./i.* shughulikia jambo; kamata kwa nguvu; shambulia.

**tact** /tækt/ *n.* hekima; busara. **~ful** *adj.* -a hekima; -a busara. **~fully** *adv.* kwa busara. **~less** *adj.* bila busara.

**tactics** /'tæktɪks/ *n.* mbinu; njia; mpango wa kutekeleza jambo; mbinu za kupanga mashambulizi katika vita.

**tactical** /'tæktɪkl/ *adj.* -a mbinu; -a mpango; -a maarifa ya vita;

**tactician** /tæk'tɪʃn/ *n.* stadi wa mbinu.

**tadpole** /'tædpəʊl/ *n.* pingiriti; kiluwiluwi.




**tag** /tæg/ *n.* tegi; kipande kidogo kilichofungiwa kitu kingine; kibandiko cha bei; msemo unaonukuliwa mara nyingi na watu. **question ~**, kirai shawishi. *v.t.* (**-gg-**) fungia; ambatisha; fuata kwa karibu sana; tia tegi.

**tail** /teɪl/ *n.* mkia; upande wa sarafu usio na kichwa cha mtu. *heads or ~s?* kichwa au mkia? *v.t./i. ~ after sb.*, fuata mtu karibu sana. *~ off*, punguka; legea; baki nyuma.

**tailor** 'teɪlə(r)/ *n.* mshonaji; fundi cherehani; mshoni.

**taint** /teɪnt/ *n.* doa; waa. *v.t./i.* tia doa; ozesha; oza.

**take** /teɪk/ *v.t./i.* (**took**, **taken**) twaa; shika; kamata; pata; chukua; peleka; pendeza; chagua; hitaji; taka; tumia; pokea; vumilia; stahamili; fahamu; tambua; kubali; dhani; -la; nywa. *~ a fortress*, teka ngome. *The rat was ~n in a trap*, panya alinasa katika mtego. *~ cold*, shikwa na mafua. *be ~n ill*, shikwa na ugonjwa. *~ fire*, anza kuwaka. *~ the fancy*, tamanisha. *I'm not much ~n with your plan*, mpango wako haunivutii sana. *~ a bath*, oga. *~ a holiday*, chukua likizo. *~ a meal*, -la. *~ a deep breath*, pumua kwa nguvu. *~ pride in one's work*, jivunia kazi. *~ a taxi*, kodi taksi. *~ a small house*, panga nyumba ndogo. *I will ~ 100/= for it*, nitakiuza

kwa shilingi mia. *Which newspaper do you ~ each day?* unanunua gazeti gani kila siku? ~ *notes of the lesson,* andika masomo ya darasani. ~ *a photograph,* piga picha. *The work took four hours,* kazi ilichukua masaa manne. *It ~s two to make a quarrel,* hakuna shari ya mtu mmoja. *I took him to be an honest man,* nilidhani kuwa ni mtu mwaminifu. ~ *after sb.,* fanana na. ~ *sth. back,* tangua. ~ *sth. down,* shusha, teremsha; andika. ~ *sb. down,* tweza. ~ *sb. in,* karibisha; punja. ~ *sth. in,* fahamu; pokea. ~ *sb. for,* fananisha kimakosa na mtu mwingine. *He was ~n for a Tanzanian,* alidhaniwa kuwa ni Mtanzania. ~ *sth. over,* rithi; chukua. *He will ~ over from you,* atachukua mahali pako. ~ *to,* penda. *He took to gardening when he retired,* alipenda sana kulima bustani alipostaafu. *I took to the man at once,* mara moja nilimpenda mtu yule. ~ *up,* tumia; twaa. **taking** *adj.* -a kuvutia. **takings** *n.* mauzo; mapato.

**tale** /teɪl/ *n.* hekaya; hadithi; taarifa; maelezo; kisa; ngano. *tell ~s about,* chongea.

**talent** /'tælənt/ *n.* kipawa; kipaji; watu wenye vipaji. *the local ~,* wasanii wa ridhaa wa mahali wenye vipaji. **~ed** *adj.* -enye kipaji.

**talk** /tɔ:k/ *n.* mazungumzo; mjadala; mhadhara; hotuba; maongezi. *small ~,* porojo; domo. ~ *of the town,* jambo linalovuma. *v.i./t.* nena; sema; ongea; zungumza. ~ *sth. over,* ongea juu ya jambo fulani. ~ *sb. out of doing sth.,* shawishi kutofanya kitu. ~ *sb. round,* shawishi mtu akubali. **~ative** *adj.* -semaji ; domo kaya.

**tall** /tɔ:l/ *adj.* -refu; -a kuzidi. *a ~ story,* hadithi yenye shaka. *a ~ order* agizo lisilotekelezeka; ombi la muhali.

**tally** /'tæli/ *n.* kitambulisho; hesabu. *v.i.* lingana; patana. **~clerk** *n.* karani wa forodha wa kukagua mizigo.

**talon** /'tælən/ *n.* kucha la ndege.

**tamarind** /'tam(ə)rɪnd/ *n.* *(tree)* mkwaju; *(fruit)* ukwaju.

**tame** /teɪm/ *adj.* -liofugwa; si -kali; nyenyekevu; tiifu; -liopooza. *v.t.* fuga; tiisha; tawala.

**tamper** /'tæmpə(r)/ *v.i.* haribu; geuza; vuruga; chezea.

**tan** /tæn/ *adj.* hudhurungi. *v.t./i.* **(-nn-)** (kwa ngozi) dibaghi; geuka hudhurungi. **~ner** *n.* mtengeza ngozi. **~nery** *n.* tasnia ya ngozi.

**tangent** /'tan(d)ʒ(ə)nt/ *n.* mstari mguso. *go off at a ~,* ghairi ghafla; enda mshazari.

**tangible** /'tan(d)ʒɪb(ə)l/ *adj.* -a kugusika; wazi; dhahiri. ~ *proof,* ithibati dhahiri.

**tangle** /'tæŋgl/ *n.* mfungamano; msokotano; msongamano; mvurugano; vurugu. *v.t./i.* sokotana; vuruga; songamana.

**tank** /tæŋk/ *n.* birika; tangi; hodhi; kifaru. *the petrol ~,* tangi la petroli. **~er** *n.* meli ya mafuta.

**tantamount** /'tæntəmaʊnt/ *adj.* ~ *to,* sawa na; mamoja.

**tap**[1] /tæp/ *n.* bomba; mfereji. *v.t.* gema; fyonza; kinga. *(fig).* jaribu kupata jambo kwa mtu.


tap

**tap**[2] /tæp/ *n.* kipigo chepesi; kugonga. *v.t.* gota; gonga.

**tape** /teɪp/ *n.* utepe; tepu. **~-measure** *n.* tepu; chenezo.

**taper** /'teɪpə(r)/ *v.t./i* chongoa; chongoka.

**taproot** /'tæpru:t/ *n.* mzizi mkuu: mzizi mkubwa kuliko yote wa mmea dikotiledoni unaokua kuelekea chini ardhini.

**tar** /tɑ:(r)/ *n.* lami. **~mac** *n.* mchanganyiko wa lami na kokoto.

**target** /'tɑ:gɪt/ *n.* shabaha; lengo; kusudio.

**tariff** /'tærɪf/ *n.* orodha ya bei; ushuru wa forodha.

**tarnish** /'tɑ:nɪʃ/ *v.i./t.* fifisha mng'ao; aibisha; tia jina baya.

**tarpaulin** /'tɑ:pɔ:lɪn/ *n.* turubali.

**tart**[1] /tɑ:t/ *adj.* chungu; kali.

**tart**[2] /tɑ:t/ *n.* pai ya matunda.

**task** /tɑ:sk/ *n.* kazi. ~ *force,* jopo.
**tassel** /'tæsl/ *n.* kishada; shada.
**taste** /teɪst/ *n.* kuonja; ladha; utamu; tamaa; upendo; shauku; akili za kupambanua mazuri. *v.t./i.* onja; dhuku; -wa na ladha ya. ~ *bud,* kionjio: ungo la fahamu katika ulimi ambalo huweza kugundua ladha ya kitu. ~ *the joys of freedom,* furahia uhuru. **~ful** *adj.* -enye ladha nzuri. **~fully** *adv.* kwa ladha nzuri. **~less** *adj.* chapwa; bila ladha.
**tasty** /'teɪsti/ *adj.* -tamu; -a kukolea.
**taut** /tɔ:t/ *adj.* -liokazwa; *(fig.)* -epesi kushtuka; -liokacha; -kavu. *a ~ smile,* kicheko kikavu.
**tawny** /'tɔ:ni/ *adj.* -a rangi ya mchanga wa pwani; hudhurungi.
**tax** /tæks/ *n.* kodi; ushuru. *a ~ on my strength,* mzigo kwangu; taklifa kwangu. *v.t.* toza kodi; lipisha ushuru; sumbua; kalifu. ~ *sb. with sth.,* shtaki; laumu. **~able** *adj.* -a kufaa kutozwa ushuru au kodi. **~ation** *n.* kutoza kodi; ushuru.
**taxi** /'tæksi/ *n.* teksi. **~ meter**, mita ya nauli katika teksi. **~ rank**, kituo cha teksi. *v.i.* ambaa chini.
**T cell** *n.* aina ya limfositi inayotoa kinga ya mwili dhidi ya antijeni.
**tea** /ti:/ *n.* chai. *high ~,* chajio; kijio. **~cloth** *n.* kitambaa cha kufutia vikombe. **~set**, **~-service** *n.* seti ya vyombo vya chai. **~-strainer** *n.* kichujio cha chai.
**teach** /ti:tʃ/ *v.t./i.* (**taught**) fundisha; funza; somesha; adibisha; ongoza; onya; zoeza. **~er** *n.* mwalimu; mfundishaji. **~ing** *n.* mafundisho; ufundishaji; kufundisha.
**teak** /ti:k/ *n.* msaji; mvule.
**team** /ti:m/ *n.* timu; wanyama wanaokokota gari pamoja. **~work** kazi ya kikoa. ~ *spirit,* moyo wa ushirikiano.
**tear**[1] /tɛ:/ *n.* mpasuko; mpasuo; ufa. *v.t./i.* (**tore**, **torn**) chana; pasua; rarua; tatua; ng'wafua; pasuka; raruka; chanika; kurupuka. *The country was torn by civil war,* nchi ilivurugwa kwa vita vya wenyewe kwa wenyewe.
**tear**[2] /tɪə/ *n.* chozi. *be in ~s,* lia. **~ful** *adj.* -enye machozi; -a kulia.
**tease** /ti:z/ *n.* mtani. *v.t.* chokoza; sumbua; tashtiti; tania. **~r** *n.* *(colloq.)* fumbo; tatizo; mchokozi; muudhi; mchekeshaji.
**technical** /'teknɪkl/ *adj.* -a kifundi; stadi; -a ufundi. ~ *terms,* maneno ya kiufundi; istilahi. *the ~ skill of a carpenter,* ustadi wa seremala. **~ity** *n.* jambo la kifundi.
**technician** /tek'nɪʃn/ *n.* fundisanifu.
**technique** /tek'nɪ:k/ *n.* mbinu; jinsi ya kufanya jambo.
**technology** /tek'nɒlədʒi/ *n.* teknolojia; elimu ya ufundi.
**tectonics** *n.* uunzi; tekitonikia: sanaa na ustadi wa kujenga majengo ya kufaa na kupendeza.
**tedious** /'ti:diəs/ *adj.* -a kuchosha; -a taabu; -a kutaabisha.
**tedium** /'tidiəm/ *n.* uchovu; taabu.
**teem** /ti:m/ *v.i.* jaa tele; zaa sana. **~ing** *adj.* -ingi sana.
**teens** ti:nz/ *n.* umri kati ya miaka kumi na tatu na ishirini. *youths in their ~,* vijana wa umri wa kati ya miaka kumi na tatu na kumi na tisa.
**teenage** /'ti:neɪdʒ/ *adj.* -a ujana.
**teenager** /'ti:neɪdʒə(r)/ *n.* kijana.
**tele-** /'tɛli/ *prefix* -a mbali sana.
**telecast** /telikɑ:st/ *n.* utangazaji kwa televisheni.
**telecommunication** *n.* mawasiliano ya simu, redio au televisheni.
**telegram** /'telɪgræm/ *n.* telegramu.
**telegraph** /'telɪgrɑf/ *n.* telegrafu; simu ya upepo. *v.t./t.* peleka habari kwa telegrafu. **~ic** *adj.* -a simu ya upepo. **~ist** *n.* mtaalamu wa kupeleka na kupokea telegrafu. **~y** *n.* telegrafia: utaalamu wa kupeleka na kupokea simu za upepo.


**telephone**

**telephone** /'telɪfəʊn/ *n.* simu. *v.t./i.* piga simu.
**televise** /'telɪvaɪz/ *v.t.* tangaza kwa televisheni.
**television** /'telɪvɪʒn/ *n.* televisheni.

**telepathy** /tə'lepəθi/ *n.* uwezo wa kupashana mawazo bila kutumia hisia za kawaida.



**television**

**telescope** /'telɪskəʊp/ *n.* darubini. *v.t./i.* ingiana kama sehemu za mtutu wa darubini. **tele-scopic** *adj.* -a darubini; -a kuonekana kwa darubini; -a kutazama mbali.



**telescope**

**tell** /tel/ *v.t./i.* (**told**) ambia; simulia. *~ the difference,* pambanua. *There is no ~ing what will happen,* haitabiriki kitakachotokea. *~ on,* athiri. *All this hard work is ~ing on him,* kazi hii ngumu inamwathiri. *all told,* kwa jumla. *~ off,* pangia kazi. *(colloq.)* simanga; karipia. **~er** *n.* mwenye kuhesabu. **~ing** *adj.* -a nguvu. **~tale** *n.* fitina; mmbeya.

**temper** /'tempə(r)/ *n.* **1.** matiko ya madini. **2.** hali; tabia; moyo; mwenendo. *good ~,* upole; ukunjufu. *bad ~,* hamaki; hasira. *keep one's ~,* tulia; jiweza; jizuia; poa. *lose one's ~,* kasirika; hamaki. *v.t. /i.* tia matiko; tuliza; punguza ukali etc. *~ justice with mercy,* -wa na huruma wakati wa kutoa adhabu. **~ament** *n.* tabia; mwenendo; silka. **~al** *adj.* -epesi kukasirika au kufurahi; -epesi wa kubadili tabia.

**temperature** /'tem'pɪst/ *n.* halijoto. *take sb.'s ~,* pima mtu kwa thamometa. *have a ~,* -wa na homa.

**tempest** /'tem'pɪst/ *n.* tufani; dhoruba. **~uous** *adj.* -a tufani; -a dhoruba; -enye kuchafuka sana. *(fig.)* -a ugomvi mwingi; -a kubishana.

**temple**[1] /'templ/ *n.* hekalu.

**temple**[2] /'templ/ *n.* paji la uso.

**temporary** /'temprəri/ *adj.* -a wakati; -a kitambo; -a muda. *~ hard water,* maji magumu ya muda: maji ambayo ugumu wake huondoka kwa kuchemshwa tu.

**tempt** /tempt/ *v.t.* tamanisha; shawishi. **~ation** *n.* kishawishi; ushawishi; matamanio. **~er** *n.* shawishi. *the ~,* shetani.

**ten** /ten/ *n./adj.* kumi. **~th** *n./adj.* sehemu ya kumi; -a kumi. *~ to one,* kumi kwa moja; yumkini.

**tenable** /'tenəbl/ *adj.* a kushikika; -a kulindika; -a kudumu kwa muda fulani; -a kuweza kutetewa. *The fortress is not ~,* boma halilindiki. *His argument was hardly ~,* ilikuwa taabu sana kuithibitisha hoja yake.

**tenacious** /tɪ'neʃəs/ *adj.* -enye kushika sana; -a kunata; -a kushikamana; -enye kushikilia kauli yake; -enye kunga'ng'ania.

**tenacity** /'tə'næsəti/ *n.* nguvu ya kushikamana; ushupavu; uthabiti.

**tenant** /'tenənt/ *n.* mpangaji. *~ farmer,* mkulima wa mfumo wa nyarubanja anayekodi ardhi.

**tenancy** /'tenənsi/ *n.* upangaji; kipindi cha upangaji. *life tenancy,* upangaji wa maisha.

**tend**[1] /tend/ *v.t.* tunza; chunga; hudumia. **~er** *n.* mtunzaji; mhudumiaji; meli saidizi; behewa la maji.

**tend**[2] /tend/ *v.i.* elekea. *Prices are ~ing upwards,* bei zinaelekea kupanda. *Their steps ~ed towards the bridge,* waliendea kwenye daraja. **~ency** *n.* mwelekeo; welekeo. *Your work shows a ~ to improve,* kazi yako ina mustakabali wa maendeleo.

**tender**[1] /'tendə(r)/ *n.* tenda; zabuni. *legal ~,* fedha halali ya nchi. *v.t./i.* toa. *~ for,* zabuni. *~ for the construction of a bridge,* zabuni ujenzi wa daraja.

**tender**[2] /'tendə(r)/ *adj.* -ororo; -epesi kudhurika; dhaifu; laini; -a huruma; -pole. *~ subject,* suala nyeti. *~ foot,* mgeni katika mazingira magumu. *~hearted,* -pole; -enye huruma; -enye upendo. *~ loin,* sarara. **~ly** *adv.* kwa huruma; kwa upole. **~ness** *n.* wororo; upole; ulaini.

**tendon** /'tɛndən/ *n.* mkano.

**tendril** /'tendrəl/ *n.* ukono; kikonyo (cha mmea).

**tenement** /'tɛnəm(ə)nt/ *n.* nyumba kubwa iliyojengwa kwa kusudi la kupangishwa; makao; mali ya

kudumu.

**tennis** /tenɪs/ *n.* tenisi. ~ *court,* kiwanja cha tenisi.

**tenor** /'tenə(r)/ *n.* mwendo; utaratibu wa maisha; mwelekeo; sauti nyembamba.

**tense** /tens/ *n.* njeo: kategoria ya kisarufi inayoainisha wakati ambao tendo hufanyika.

**tense** /tens/ *adj.* -liokazwa; liokakamaa; -enye fadhaa; *(gram.)* kaze: -enye kutumia nguvu nyingi za misuli katika kutamkwa. *Their faces were ~ with anxiety,* nyuso zao zilijaa fadhaa. **~ly** *adv.* kwa fadhaa. **~ness** *n.* fadhaa. **tensile** *adj.* -a kunyoosheka; -a kutanuka; a mkazo.

**tension** /'tenʃn/ *n.* mvuto; mkazo; fadhaa; wasiwasi; mgogoro; nguvu ya umeme.

**tensity** *n.* fadhaa.

**tent** /tent/ *n.* hema. ~ *cloth,* turubali.

**tentacle** /'tentəkl/ *n.* mnyiri; mkia; mwinyo; mkono.

**tentative** /'tentətɪv/ *adj.* -a kujaribia. *My suggestion was only* pendekezo langu lilikuwa la majaribio tu. **~ly** *adv.* kwa majaribio.

**tenure** /'tɛnjə/ *n.* muda wa kumiliki; umilisi; masharti ya kumiliki; muda wa kushika cheo.

**tepid** /'tepɪd/ *adj.* -a uvuguvugu. *be ~,* vuvuwaa.

**term** /tɜ:m/ *n.* muda; muhula; majira; kipindi; sharti; neno; istilahi. *come to ~s with,* kubaliana na hali ya. *be on good ~s with,* chukuana na. *v.t.* taja; ita. **~inal** *n.* kitu cha mwisho; kichwa; ncha. *adj.* -a kipindi; -a muhula; -a mwisho; a kufa; -a ncha. **~ velocity,** kasimwelekeo kikomo: kasi mwelekeo usiobadilika unaofikiwa na gimba linalosafiri. **~inate** *v.t./i.* komesha; zuia; koma; isha; vunjika; vunja; haribu. *~ a pregnancy,* toa mimba. **~ination** *n.* kikomo; mwisho; uvunjaji; *(gram.)* silabi au herufi ya mwisho wa neno.

**terminology** /'tɜ:mɪ'nɒlədʒi/ *n.* istilahi zitumikazo katika nyanja maalumu ya taaluma fulani.

**terminus** *n.* kituo cha mwisho cha treni.

**termite** /'tə:mʌɪt/ *n.* mchwa; kumbikumbi.

**terrace** /'terəs/ *n.* mahali palipoinuka pa kutembelea au penye nyumba.

**terrestrial** /tə'rɛstrɪəl/ *adj.* -a dunia; -a kuhusiana na matukio juu ya uso wa dunia.

**terrible** /'terəbl/ *adj.* -a kuogofya; a kuhuzunisha; -a kutisha; a bughudha. **terribly** *adv.* sana; mno.

**terrific** /tə'rɪfɪk/ *adj.* -a kutisha; -a kuogofya; -a hofu; *(colloq.)* -kubwa mno; -ingi mno. **terrify** *v.t.* tisha; ogofya; tia hofu.

**territorial** /,terə'tɔ:riəl/ *adj.* -a nchi au taifa fulani. *the ~ army,* jeshi la mgambo. **territory** *n.* nchi; taifa; jimbo; wilaya; eneo.

**terror** /'terə(r)/ *n.* woga; hofu kubwa. **~ism** *n.* ugaidi. **~ist** *n.* gaidi. **~ize** *v.t.* tisha sana.

**terse** /tɜ:s/ *adj.* -a maneno machache; -a maneno ya mkato.

**tertiary consumer** *n.* mnyama alae wanyama wenye kula wanyama wingine.

**test** /test/ *n.* jaribio; mtihani; kipimo; upimaji. *a ~ pilot,* rubani wa majaribio. *~ tube,* neli ya majaribio. **~tube** *baby,* mtoto wa maabara. *v.t.* jaribu, tahini, pima. *The long climb ~ed our powers of endurance* safari ndefu ya kupanda ilipima uvumilivu wetu.



testtubes

**testament** /'testəmənt/ *n. last will and ~,* wasia. **Old ~,** Agano la Kale. **New ~,** Agano Jipya.

**testicle** /'testɪkl/ *n.* pumbu; umbo la kiume ambapo gameti za kiume hutengenezwa.

**testify** /'testɪfaɪ/ *v.t./i.* shuhudia; thibitisha; toa ushahidi; -wa dalili ya. *Your work testifies to your ability,* kazi yako yathibitisha uwezo wako.

**testimonial** /ˌtestɪ'məʊniəl/ *n.* barua ya kuthibitisha uwezo wa mtu itolewayo na mwajiri.
**testimony** /'testɪməni/ *n.* ushahidi. *conflicting ~,* ushahidi wa uongo. *sworn ~,* ushahidi wa kiapo. *bear ~ to sth.,* shuhudia jambo.
**testis** /testɪs/ *n.* pumbu.
**tetrapod** *n.* mnyama mwenye maungo mane.
**text** /tekst/ *n.* maandishi. **~book** *n.* kitabu cha kiada. *~ errors,* makosa ya maandishi.
**textile** /'tekstaɪl/ *n.* kitambaa; nguo. *adj.* -enye kutengeneza vitambaa au nguo. **~ industries**, viwanda vya nguo.
**texture** /'tekstʃə(r)/ *n.* unamu: umbile asili la kitu laini, -a kukwaruza, -embamba, -nene, etc. *a cloth of fine ~,* kitambaa laini.
**thallium** /'θalɪəm/ *n.* thaliamu: elementi kemikali yenye rangi buluu ya weupe.
**than** /ðən/ *conj.* kuliko; zaidi ya; kupita. *He is taller ~ Juma,* yu mrefu kuliko Juma.
**thank** /θæŋk/ *v.t.* shukuru. **~s** *n.* shukrani; asante: *~s to,* kwa msaada wa. **~ful** *adj.* -enye shukrani. **~fully** *adv.* kwa shukrani. **~less** *adj.* bila shukrani.
**that** /ðæt/ *adj./pron.* (**those**) yule, ule, ile, etc. *rel. pron.* -o, -ye, -yo, -vyo, etc. *conj.* kama. *on condition ~,* ilimradi. *Oh ~ I could get that opportunity again,* laiti ningeipata fursa ile tena.
**thatch** /θætʃ/ *n.* kitu cha kuezekea. *v.t.* ezeka. *strip off ~,* ezua.
**thaw** /θɔ:/ *v.i./t.* (barafu na theluji) yeyuka; yeyusha; (kwa watu na mwenendo wao ) chamgamka; changamsha.
**the** /ðə/ *def. art.* -le. *The lion is a fierce animal,* simba yule ni mnyama mkali.
**theatre** /θɪətə(r)/ *n.* jumba la maonyesho ya tamthilia; thieta: ukumbi wa mihadhara; tamthilia. **operating ~**, chumba cha kupasulia. **theatrical** *adj.* -a tamthilia; (kwa mwenendo) -a kujidai.
**thee** /ði:/ *pron.* (la zamani) wewe.
**theft** /θeft/ *n.* wizi.
**their(s)** /ðeəz/ *adj./ pron.* -ao.
**theme** /θi:m/ *n.* dhamira; wazo.
**then** /ðen/ *adv.* wakati ule. *conj.* kisha; halafu; baadaye.
**theology** /θi'ɒlədʒi/ *n.* thiolojia: elimu ya dini na uungu. **theologian** *n.* mwanathiolojia. **theological** *adj.* -a thiolojia.
**theorem** /'θɪərəm/ *n.* kauli: usemi au mapendekezo ambayo yamethibitishwa kimantiki kutoka kwenye ukweli na dhana za kimsingi hasa katika hisabati.
**theory** /θɪəri/ *n.* nadharia. **theoretic(al)** *adj.* -a nadharia. **theoretician** *n.* mnadharia. **theoretics** *n.* elimunadharia. **theorist** *n.* mnadharia.
**there** /ðeə(r)/ *adv.* pale; hapo; kule; huko; mle; humo. *~ was a man,* palikuwa na mtu. *It was ~I saw him,* pale ndipo nilipomuona. **~abouts** *adv.* karibu. **~after** *adv.* baadaye; halafu. **~by** *adv.* kwa hivyo; kwa sababu hii. **~fore** *adv.* kwa sababu hiyo; kwa hivyo. **~upon** *adv.* pale; mara.
**therm** /θɜ:m/ *n.* kipimo cha kima cha joto. **thermal** *adj.* -a kuhusu joto **~ decomposition**, uchangukaji joto: uchangukaji kwa muda wa dutu kutokana na joto kuwa dutu sahili. **~ energy**, nishati joto: nishati inayotokana na halijoto ya kitu. **~ expansion**, upanukaji joto: uongezekaji wa kitu kutokana na kuongezeka kwa halijoto yake. **~ reactor**, tanuri la joto: tanuri la nyuklia ambamo miatuko ya nyuklia husababishwa na nyutroni za joto. **~istor** *n.* themista: aina ya themometa inayotengenezwa kutokana na kipitishipitishi ambacho ukinzani wake hupungua sana wakati halijoto inapoongezeka. **~ocouple** *n.* themokapo: aina ya themometa iliyotengenezwa kwa kulehemu metali mbili tofauti ili kufanya kiungo. **~odynamics** *n.* mwendo-

joto: sayansi ya uhusiano wa joto na aina nyinginezo za nishati. **~ometer** *n.* kipimajoto: chombo cha kupimia halijoto. **~onuclear reactor**, kitendaji nyukliajoto: mtambo utumikao katika utendanaji unaotoa nishati ya kinyukliajoto. **~oplastic** *n.* themoplastiki: dutu polimeria ambayo hugeuka huwa plastiki kwa kukanzwa na huweza kupewa umbo kwa kanieneo au joto bila kubadili tabia zake kikemikali. **~ostat** *n.* themostati: kirekebisha joto.

**thesis** /'θi:sɪs/ *n.* (**theses**) tasnifu; hoja au wazo linalotolewa kimantiki.

**they** /ðeɪ/ *pron.* (**them**) wao.

**thick** /θɪk/ *adj.* -nene; (kwa vitu vya majimaji) -zito; (kwa hewa au mvuke) -zito. ~ *with,* -liojaa. *adv. come ~ and fast,* -ja -ingi pamoja. **~en** *v.t./i.* fanya kuwa -nene; wa -zito, -nene. **~ly** *adv.* kwa wingi. **~ness** *n.* unene; tabaka; uzito. **~set** *adj.* (kwa mtu) -fupi; -nene. **~-skinned** *adj. (fig.)* sugu; -siyejali wingine.

**thief** /θɪ:f/ *n.* (**thieves**) mwivi; mwizi.

**thigh** /θaɪ/ *n.* paja.

**thimble** /'θɪmbl/ *n.* kastabini: kifuniko kidogo cha madini cha kulinda ncha ya kidole isiumie kwa sindano wakati wa kushona. **~ful** *n. (colloq.)* tone.


thimble

**thin** /θɪn/ *adj.* -embamba; -liokonda; (kwa mchuzi, uji, etc.) -epesi. *v.t./i.* fanya kuwa -embamba, - epesi; -wa -embamba. ~ *the plants out,* punguzia mimea. **~ly** *adv.* kwa wembamba. **~ness** *n.* wembamba; wepesi. **~-skinned** *adj.* -epesi kuudhika.

**thing** /θɪŋ/ *n.* kitu; *(pl.)* mambo. *your ~s,* vitu vyako. *Have you packed your ~s yet?* umekwishafunga mizigo yako? *the very ~,* kitu kinachofaa. *This is the very ~,* hiki ndicho hasa. *Not at all the ~ to do,* si jambo zuri hata kidogo.

**think** /θɪŋk/ *v.t./i.* fikiri; dhani; tafakari; waza. *We ~ well of him,* twadhani kuwa ni mtu mwema. *He ~s nothing of walking twenty miles,* haoni kitu kutembea maili ishirini. *He thought better of it,* aliachana nalo. ~ *sth. out,* fikiria kwa makini. ~ *sth. over,* fikiria tena jambo.

**third** /θɜ:d/ *n./adj.* thuluthi: sehemu moja katika tatu; -atatu. **~ly** *adv.* tatu. **~-rate** *adj.* hafifu; duni.

**thirst** /θɜ:st/ *n.* kiu; *(fig.)* shauku. **~y** *adj.* -enye kiu; -a kuleta kiu. **~ily** *adv.* kwa hamu.

**thirteen** /ˌθɜ:'ti'n/ *n./adj.* kumi na tatu. **~th** *n./adj.* sehemu ya kumi na tatu; -a kumi na tatu.

**thirty** /'θɜ:ti/ *n./adj.* thelathini. **thirtieth** *n./adj.* -a thelathini.

**this** /ðɪs/ *adj./pron.* (**these**) huyu, huu, hii, etc.

**thorax** /'θɔ:ræks/ *n.* kifua: sehemu iliyo katikati baina ya kichwa na tumbo.

**thorium** *n.* thoriamu: metali ya kikemikali nururishi ya nambari 90 yenye rangi nyeupe.

**thorn** /θɔ:n/ *n.* mwiba. **~y** *adj.* -enye miba ~ *bush,* mchongoma; mkwamba. ; *(fig.)* -a taabu, mashaka. *a ~ in one's flesh,* kero; maudhi.

**thorough** /'θʌrə/ *adj.* -kamilifu. *a ~ rascal,* ayari wa kupindukia. **~bred** *n./adj.* mbegu bora; -a asili bora. **~fare** *n.* njia ya watu wote. **~going** *adj.* kamilifu. **~ly** *adv.* kikamilifu. **~ness** *n.* ukamilifu.

**thou**, /ðaʊ/ **thee** *pron.* wewe.

**though** /ðəʊ/ *conj.* ingawa; ijapokuwa; hata hivyo.

**thought** /θɔ:t/ *n.* fikira; wazo. *take ~ for,* zingatia. *he had no ~ of,* hakuwa na nia ya. **~ful** *adj.* -a kufikiri; -angalifu. **~fully** *adv.* kwa uangalifu. **~fulness** *n.* uangalifu. **~less** *adj.* -si ya busara. **~lessly** *adv.* bila mazingatio. **~lessness** *n.* uzembe.

**thousand** /'θaʊznd/ *n./adj.* elfu.

*hundred* ~, laki
**thrash** /θræʃ/ *v.t.* piga; puta. *He ~ him with a whip,* alimcharaza kwa mjeledi. ~ *sth. out,* fikia suluhisho kwa majadiliano
**thread** /θred/ *n.* uzi; hesi ya parafujo. ~ *of thought,* mfululizo wa mawazo. *v.t.* tunga uzi katika sindano, ushanga, etc.
**threat** /θret/ *n.* kitisho. **~en** *v.t./i.* tisha; ashiria. *It ~s to rain,* kunaashiria kunyesha mvua. **~eningly** *adv.* kwa vitisho.
**three** /θri:/ *n./adj.* tatu; -tatu. **~fold** *adj.* mara tatu.
**thrice** /θraɪs/ *adv.* mara tatu.
**thresh** /θreʃ/ *v.t./i.* puta; pura.
**threshold** /'θreʃhəʊld/ *n.* kizingiti cha chini cha mlango.
**thrill** /θrɪl/ *n.* msisimko. *v.t./i.* sisimua; sisimka. **~er** *n.* -sisimuaji.
**thrive** /θraɪv/ *v.i.* (**throve**, **thriven**), sitawi; tononoka.
**throat** /θrəʊt/ *n.* koo. *force sth. down one's* ~, lazimisha mtu akubali maoni yako.
**throb** /θrɒb/ *n.* kututa; mapigo. *v.i.* (**-bb-**) puma; tuta
**throne** /θrəʊn/ *n.* kiti cha enzi; *(fig.) the* ~, enzi.
**throttle** /θrɒtl/ *n.* vali inayodhibiti mmiminiko wa mvuke katika injini. *v.t.* kaba roho. ~ *down,* dhibiti mmiminiko wa mvuke katika injini.
**through** /θru:/ *prep.* kwa; katika. *adv.* hadi mwisho. **~out** *adv.* kila mahali; kabisa; wakati wote; hadi mwisho.
**throw** /θrəʊ/ *v.t./i.* (**threw**, **thrown**) tupa; gea; rusha. ~ *away,* poteza. ~ *oneself into,* anza kufanya jambo kwa bidii . ~ *off,* acha. ~ *out,* tamka. ~ *over,* tupa; acha. ~ *up,* tapika; acha.
**thrust** /θrʌst/ *n.* kikumbo; msukumo. *v.t./i.* sukuma kwa nguvu. **~er** *n.* injini ndogo inayosaidia kurekebisha uwelekeo hasa katika ndege.
**thud** /θʌd/ *n.* mshindo. *v.i.* piga, anguka kwa mshindo.
**thumb** θʌm/ *n.* kidole cha gumba. *be under sb.'s* ~, wa chini ya. *rule of* ~, kanuni iliyotokana na mazoea au desturi tu. ~ *latch,* kitasa cha kuminya kwa kidole. ~ *a lift,* omba lifti barabarani.
**thump** /θʌmp/ *n.* ngumi; pigo la ngumi; mshindo. *v.t./i.* piga ngumi; dunda.
**thunder** /'θʌndə(r)/ *n.* radi; ngurumo. **~bolt** *n.* radi; *(fig.)* jambo la kushtusha sana. **~struck** *adj.* -enye kuduwaa. *steal sb.'s* ~, kata bogi.
**Thursday** /'θɜ:zdeɪ/ *n.* Alhamisi.
**thus** /ðʌs/ *adv.* hivi; hivyo. ~ *far,* mpaka hapa.
**thy** /ðaɪ/ *adj.* (la zamani) ako.
**thyroid** /'θaɪrɔɪd/ *n.* thiroidi: tezi iliyoko kwenye shingo ambayo hutoa homoni zenye athari muhimu kwa ustawi wa akili na mwili.
**tibia** /'tɪbiə/ *n.* goko: mfupa wa muundi wa mguu.
**tick**[1] /tɪk/ *n.* pigo jepesi kama la mlio kama wa saa; tiki: alama ya vyema. *on* ~, kwa kukopa. *v.i./t.* piga mlio kama saa; tia tiki. ~ *off,* tia tiki. ~ *sb. off, (colloq.)* karipia; kemea.
**tick**[2] /tɪk/ *n.* kupe; papasi.
**ticket** /'tɪkɪt/ *n.* tiketi; kipande cha bei katika bidhaa.
**tickle** /'tɪkl/ *v.t./i.* tekenya; nyengeresha. **ticklish** *adj.* -a kutekenyeka upesi
**tide** /taɪd/ *n.* maji kujaa na kupwa. *v.t.* ~ *sb. over,* kwamua mtu katika matatizo. *Will 6000/= ~ you over until you get your wages?* shilingi elfu sita zitakusaidia mpaka upate mshahara wako?
**tidal** /'taɪdl/ *adj.* -a maji kupwa na kujaa. *tidal power,* umeme wimbi: nguvu za umeme zitokanazo na mawimbi ya bahari.
**tie** /taɪ/ *n.* fundo; sare; kizuizi; tai. *v.t./i.* (**tying**, **tied**) /taɪd/ funga. ~ *sb. down,* nyima mtu uhuru. ~ *up,* muungano; ubia.
**tier** /tɪə(r)/ *n.* safu; daraja; rusu.
**tiger** /taɪgə(r)/ *n.* chui mwenye milia.
**tigress** *n.* chui jike.
**tight** /taɪt/ *adj.* -a kukaza; -liokazwa; -lionyoshwa sana. *pack* ~, funga

vizuri. *be in a ~ corner*, -wa hatarini. *air ~*, -siopitisha hewa. *water-~*, -siopitisha maji. *adv.* kwa kukaza. **~en** *v.t./i.* kaza. **~-fisted** *adj.* -bahili. **~ly** *adv.* kwa kukaza. **~ness** *n.* kukaza.

**tile** /taɪl/ *n.* kigae cha kuezekea, kubandikiza ukutani au sakafuni.

**till**[1] /tɪl/ *prep./conj.* hadi; mpaka.

**till**[2] /tɪl/ *n.* mtoto wa meza.

**till**[3] /tɪl/ *v.t.* lima. **~age** *n.* kilimo. **~er** *n.* mkulima.

**tiller** /ˈtɪlə(r)/ *n.* tela: mkono wa usukani wa mashua.

**tilt** /tɪlt/ *n.* mwinamo. *v.t./i.* inamisha; inama. *at full ~*, kwa mbio na nguvu nyingi sana.

**timber** /ˈtɪmbə(r)/ *n.* mbao; miti.

**time** /taɪm/ *n.* wakati; mara; majira. *be in ~*, wahi. *You will be able to speak Kiswahili in ~*, utaweza kuzungumza Kiswahili mapema. *in good ~*, mapema. *in no ~*, *(colloq.)* mara moja. *at one ~*, zamani. *at the same ~*, wakati huohuo. *from ~ to ~*, mara kwa mara. *~ and again*, mara nyingi. *for the ~ being*, kwa sasa. *work against ~*, fanya upesi kuwahi wakati. *Three ~s five is fifteen*, tatu mara tano ni kumi na tano. *Greenwich ~*, saa za zoni. *summer ~*, majira ya kiangazi. *in ~*, kwa kufuata wakati. *be out of ~*, kosa majira. *once upon a ~*, hapo kale. *v.t.* pima wakati. **~ly** *adj.* -a wakati wa kufaa. **~table** *n.* ratiba.

**timid** /ˈtɪmɪd/ *adj.* -oga; -enye haya. **~ly** *adv.* kwa woga. **~ity** *n.* woga; haya.

**timorous** /ˈtɪmərəs/ *adj.* -oga.

**tin** /tɪn/ *n.* bati; kopo; mkebe.

**tinge** /tɪndʒ/ *n.* rangi; dalili. *v.t.* tia rangi kidogo; geuza kidogo.

**tingle** /tɪŋgl/ *v.i.* sisimka.

**tinkle** /ˈtɪŋkl/ *n.* mlio wa njuga. *v.i.* lia kama njuga.

**tint** /tɪnt/ *n.* rangi. *v.t.* tia rangi kidogo. *~ed glasses*, miwani ya kiza.

**tiny** /ˈtaɪni/ *adj.* -dogo sana.

**tip**[1] /tɪp/ *n.* ncha; kilele. **~toe** *adv.* kwa ncha za vidole vya miguu.

**tip**[2] /tɪp/ *v.t./i.* (**-pp-**) (mara nyingi *~ up*,) inamisha upande mmoja; inama. *~ over*, pindua; pinduka. *~ out*, mwaga. *~up seat*, kiti cha kukunja. **~per** *n.* tipa; lori.

**tip**[3] /tɪp/ *n.* kidokezo; bahshishi. *v.t.* (**-pp-**) dokeza; -pa bahshishi.

**tire** /ˈtaɪə(r)/ *v.t./i.* chosha; choka. **~d** *adj.* -chovu; hoi. *I am ~ of this food*, chakula hiki kimenichosha. *They are ~*, wamechoka. *be ~ out*, hoi kabisa. **~less** *adj.* -siochoka; -siokwisha. **~some** *adj.* -a kutaabisha; -a kuchosha.

**tissue** /ˈtɪʃuː/ *n.* kitambaa; shashi; tishu: mkusanyiko wa seli mwilini. *a ~ of lies*, uwongo mtupu. **~paper** *n.* karatasi ya shashi. **toilet ~**, karatasi ya chooni.

**titanium** /tɪˈteɪniəm/ *n.* titaniamu: elementi metali ya kemikali nyepesi na madhubuti ya rangi ya fedha-kijivu ya nambari 20.

**title** /ˈtaɪtl/ *n.* jina; cheo; kichwa cha habari. **~ page**, ukurasa wa kwanza wenye jina la kitabu na mwandishi. **~ role**, jina la mhusika ambalo pia ni jina la tamthilia, kama Kinjeketile. **~ deed**, hatimiliki.

**titrate** *v.t.* tirisha: thibitisha kiasi cha kiambato maalumu kilichopo kwenye mmumunyo kwa kupima mjao wa kimenyushi kwa usahili kikiwa na nguvu inayoweza kubadili kiambato hicho kwa kingine.

**titter** /ˈtɪtə(r)/ *n.* kicheko. *v.i.* jichekea; chekelea.

**to** /tuː/ *prep.* kwa; kasoro; -ni; mpaka; -ea; ku-; ili; kuliko. *They defeated them three goals ~ one*, waliwafunga magoli matatu kwa moja. *It's quarter ~ nine*, saa tatu kasorobo. *She has gone ~ town*, amekwenda mjini. *He followed her ~ the end*, alimfuata mpaka mwisho. *He threw a stone ~ me*, alinitupia jiwe. *She came ~ save me*, alikuja ili kuniokoa. *I prefer milk ~ coffee*, napenda maziwa kuliko kahawa.

**toast**[1] /təʊst/ *n.* tosi; tosti. **~er** *n.* chombo cha kuchomea tosi.

**toast**[2] /təʊst/ *n.* kupongeza; kutakia

heri. *v.t.* takia heri; pongeza. *drink a ~,* kunywa kwa kumpongeza fulani. **~master** *n.* mtangazaji wa pongezi katika karamu

**tobacco** /tə'bækəʊ/ *n.* tumbaku. **~nist** *n.* muuza tumbaku au sigara.

**today** /tə'deɪ/ *n./adv.* leo. *a week ~,* baada ya wiki moja.

**to-do** /tə'du:/ *n.* *(colloq.)* fujo; matata; ghasia. *Don''t make a ~ about such a small matter,* usifanye fujo juu ya jambo dogo kama hilo.

**toe** /təʊ/ *n.* kidole cha mguu. *v.t./i.* gusa kwa vidole. *~ the line,* gusa mstari wa kuanzia mbio kwa vidole; *(fig.)* fanya ulivyoamriwa.

**together** /tə'geðə(r)/ *adv.* pamoja; -ote; kwa wakati mmoja. **~ness** *n.* umoja; udugu; mshikamano.

**toil** /tɔɪl/ *n.* kazi ya sulubu. *v.i.* jitahidi; fanya kazi kwa bidii; enda kwa taabu. **~er** *n.* mvuja jasho; mtu afanyae kazi ya sulubu.

**toilet** /'tɔɪlət/ *n.* choo; msala. *~ articles,* vifaa vya kujikwatua. **~paper** *n.* karatasi ya chooni. *~ table,* meza ya vipodozi yenye kioo. *make one's ~,* vaa; valia.

**token** /'təʊkən/ *n.* dalili; ishara. *~ payment,* malipo ya mwanzo.

**tolerate** /'tɒləreɪt/ *v.t.* vumilia; stahamili. **tolerable** *adj.* -a kuvumilika; -zuri kiasi. **tolerance** *n.* uvumilivu. **tolerant** *adj.* -vumilivu. **toleration** *n.* uvumilivu.

**tomato** /tə'mɒ:təʊ/ *n.* mnyanya; nyanya; tungule.

**tomb** /tu:m/ *n.* kaburi.

**tomorrow** /tə'mɒrəʊ/ *n./adv.* kesho. *day after ~,* keshokutwa.

**ton** /tʌn/ *n.* tani; kilo elfu moja. *(colloq.) He's worth ~s of money,* yeye ni tajiri mno. **~nage** *n.* uwezo wa kusheheni; gharama za kusafirisha tani moja ya shehena.

**tone** /təʊn/ *n.* sauti; toni: namna au tabia ya sauti. *in angry ~,* kwa sauti ya ukali. *The ~ of the school is good* , hali ya skuli ni nzuri. *v.t./i.* geuza rangi au sauti. *~ down,* punguza; pungua; tulia; zimua. *The crowd soon ~d down,* watu walitulia. *This colour ~s well with the others,* rangi hii inachukuana vizuri na nyinginezo.

**tongs** /tɒŋz/ *n.* koleo.

**tongue** /tʌŋ/ *n.* ulimi; lugha. **~tied** *adj.* -nyamavu. *hold one's ~,* nyamaza. *one's mother ~,* lugha asili ya mtu. *sharp ~d,* enye ulimi wa upanga.

**tonic** /'tɒnɪk/ *n.* toniki: dawa ya kutia afya na nguvu.

**tonight** /tə'naɪt/ *n./adv.* usiku huu.

**tonne** /tʌn/ *n.* tani: kizio cha masi sawa na kilogramu 1000.

**tonsil** /'tɒnsl/ *n.* tukwi; findo. **~litis** *n.* mafindofindo; matukwi.

**too** /tu:/ *adv.* mno; kupita kiasi; pia; vilevile. *have one ~ many,* kunywa zaidi ya kipimo.

**tool** /tu:l/ *n.* chombo; ala; zana; kifaa; kibaraka. **~ bag**, koba: mkoba wa vifaa vya ufundi. **~ box**, kisanduku cha vifaa.




**tools** | **zana za kazi**

**tooth** /tu:θ/ *n.* (**teeth**) /ti:θ/ jino. *fight ~ and nail,* pigana kufa kupona. *in the teeth of,* kwa kukabiliana na; dhidi ya. *false ~,* jino bandia. *escape by the skin of one's teeth,* ponea chupuchupu. *have a sweet ~,* penda

vyakula vitamu. **~less** *adj* kibogoyo



permanent teeth in humans / meno ya kudumu ya binadamu

**top**[1] top *n* upande wa juu kilele. *at the ~ of his voice* kwa sauti ya juu kabisa. *vt* tunuka kata juu. *~ the trees* kata vilele vya miti. **~coat** *n* koti. **~heavy** *adj* zito juu kuliko chini. **~mast** *n* cheleko mstamu sehemu ya juu ya mlingoti. **~most** *adj* -a juu kabisa

**top**[2] top *n* pia. *sleep like a ~* lala fofofo

**topee topi** *n* helmeti ya jua chepeu

**topic** 'topik *n* mada. *~ of the day* gumzo la siku. **~al** *adj* -a siku hizi

**topography** tə'pɒgrəfi *n* topografia taaluma ya maarifa ya hali ya eneo kwenye ramani

**topsoil** 'topsoil *n* dongojuu tabaka ya juu kabisa ya udongo yenye virutubisho vinavyohitajika na mimea

**torch** tɔ:tʃ *n* mwenge tochi. *hand on the ~* endeleza elimu. *carry a ~ for sb.* penda mtu asiyekupenda. **~singer** mwanamke anayeimba nyimbo za mapenzi za masikitiko

**torment** 'tɔ:ment *n* mateso adhabu. *vt* tesa adhibu. **~or** *n* mtesaji msumbufu

**tornado** tɔ:'neidəʊ *n* (**~es**) kimbunga

**torpedo** tɔ:'pi:dəʊ *n* (**~es**) kombora.



tortoise

**torrent** 'tɒrənt *n.* mkondo mbizamu wa maji. **~ial** *adj.* -a mbizamu. *~ rain* mvua nyingi

**tortoise** 'tɔ:təs *n.* kobe. **~shell** *n.* ng'amba.

**tortuous** 'tɔ:tʃuəs *adj.* -a kupindapinda *(fig.)* enye hila.

**torture** 'tɔ:tʃə(r) *n.v.t.* mateso adhabu tesa; adhibu. *~ of the damned* mateso ya motoni.

**tory** 'tɔ:ri *n.* enye kushikilia ukale

**toss** tɒs *v.t. i.* rusha juu sukasuka tupa juu. *~ sth. off* maliza mara moja.

**total** 'təʊtl *n.* jumla. *adj.* -ote kamili. **~ly** *adv* kabisa.

**totalitarian** təʊ,tælə'teəriən *adj.* -a imla -a kidikteta. *~ state.* nchi yenye utawala wa kidikteta.

**touch** tʌtʃ *n.* mguso kugusa. *at a ~* kwa kuguswa tu. *soft to the ~* laini nyororo. *final ~es* marekebisho ya mwishomwisho. *a touch of* shubha dalili. *There is a ~ of vanity in his speech* mna dalili ya kiburi katika hotuba yake. *be in touch with things* wa na habari ya matukio. *lose ~ with friends* poteana na marafiki. *v.t. i.* **1.** gusa papasa **2.** pasa husu sikitisha. *The sad story ~ed our hearts* hadithi ya huzuni ilitusikitisha. **3.** shinda *There's nobody to ~ him for running* hakuna mtu wa kumshinda kwa kukimbia. **4.** (kwa meli) wasili tia nanga. *~ upon* gusia eleza kidogo. *~ up* tengeneza. **~and-go** *adj.* *It was ~and-go whether he would arrive in time* ilikuwa bahati nasibu iwapo atawahi. **~ed** *adj.* *(colloq.) be ~ed* wa na kichaa. **~ing** *adj.* -a kuhuzunisha. *prep.* juu ya kuhusu kuhusiana na. **~y** *adj.* -epesi kuhamaki. **~iness** *n.* wepesi wa kuhamaki

**tough** tʌf *adj.* gumu -siotatuka shupavu. *~ customer (colloq.)* fedhuli korofi. *~ luck* mkosi. **~en**

*v.t./i.* imarisha; shupaza.
**tour** /tʊə(r)/ *n.* safari ya kitalii; matembezi. *on ~*, safarini. *v.t./i.* talii, tembelea. *~ing car*, gari ya kutembeza watalii. **~ism** *n.* utalii. **~ist** *n.* mtalii. *a ~ agency*, wakala wa utalii. *a ~ class*, daraja la pili.
**tournament** /ˈtʊənəmənt/ *n.* mashindano.
**tourniquet** /ˈtʊənɪkeɪ/ *n.* fundo la kuzuia damu.
**tow** /təʊ/ *n.* kamba, waya, au mnyororo wa kuvutia. *v.t.* vuta kwa kamba, waya au mnyororo.
**toward(s)** /təˈwɔːdz/ *prep.* kuelekea; kuhusu; kwa ajili ya; karibu ya. *What is your opinion ~ this programme?*, una wazo gani kuhusu programu hii? *save money ~ education*, tunza fedha kwa ajili ya elimu. *~ the end of the day*, karibu ya jua kutua.
**towel** /ˈtaʊəl/ *n.* taulo. *v.t.* futa kwa taulo.
**tower** /ˈtaʊə(r)/ *n.* mnara. *a ~ of strength*, mtu wa kutegemewa sana katika matatizo. *water ~*, mnara wa tangi la maji. *~ block*, jengo lenye ghorofa nyingi. *v.i* enda juu sana. *~ above*, *(fig.)* zidi kwa urefu, kimo, au akili. *be in a ~ing rage*, kasirika mno.
**town** /taʊn/ *n.* mji. **~ clerk**, karani wa halmashauri ya mji. **~ hall**, halmashauri ya mji. **~ planning**, mipango miji. *man about ~*, mpenda starehe za mji.
**toxic** /ˈtɒksɪk/ *adj.* -a sumu.
**toxin** /ˈtɒksɪn/ *n.* toksini: aina ya kemikali inayotolewa na bakteria yenye uwezo wa kudhuru seli za viumbe vingine.
**toy** /tɔɪ/ *n.* mwanasesere: kitu cha kuchezea watoto. *v.i.* chezea.
**trace** /treɪs/ *n.* dalili; alama; nyayo. *v.t.* nakili; fuatisha. **~ element**, elementi katiti: elementi ihitajikayo kiasi kidogo sana kwenye viumbe. **~less** *adj.* bila kuacha alama.
**trachea** /trəkiːə/ *n.* koromeo: mrija wa hewa kutoka kinywani kupitia shingoni hadi mapafuni.
**track** /træk/ *n.* njia; mkondo. *v.t* fuatia kwa alama za nyayo.
**tract**[1] /trækt/ *n.* eneo; nchi; jimbo.
**tract**[2] /trækt/ *n.* kijitabu kifupi kinachohusu mambo ya dini.
**tractable** /træktəbl/ *adj.* -tiifu.
**tractor** /ˈtræktə(r)/ *n.* trekta.
**trade** /treɪd/ *n.* biashara; kazi. *the cotton ~*, biashara ya pamba. *~ union*, chama cha wafanyakazi. *~ mark*, jina la bidhaa. *~ price*, bei ya jumla. **~winds**, pepo za bahari zivumazo daima kuelekea ikweta zikitokea kusini mashariki na kaskazini mashariki. *v.i./t.* fanya biashara. *~ upon*, tumilia. **~r** *n.* mfanya biashara; mchuuzi. **~sman** *n.* muuza duka.


tractor

**tradition** /trəˈdɪʃn/ *n.* mila; desturi. **~al** *adj.* -a desturi. **~lly** *adv.* kimila. **~alist** /trəˈdɪʃənəlɪst/ *n.* mfuata desturi; mkale.
**traffic** /ˈtræfɪk/ *n.* trafiki: jumla ya vipando barabarani au ndege angani; magendo. *v.i.* (**-k-**) *~ in*, fanya biashara. **~ker** *n.* mfanyabiashara za magendo. **drugs ~**, muuza dawa za kulevya.
**tragedy** /ˈtrædʒədi/ *n.* tamthilia ya tanzia, msiba.
**tragedian** /trəˈdʒiːdiən/ *n.* mwandishi au mwigizaji wa tamthilia za tanzia.
**tragic** /ˈtrædʒɪk/ *adj.* -a tanzia; -a huzuni. **tragically** *adv.* kwa huzuni.
**trail** /treɪl/ *n.* njia; lia; alama; nyayo. *The storm left a ~ of destruction*, tufani iliacha alama za maangamizi. *You have to set a trap on their ~ to catch these pigs*, lazima uwatege katika lia lao ili uwakamate nguruwe hawa. *v.t./i.* burura; tambaa. **~er** *n.* (kwa lori) tela.
**train** /treɪn/ *n.* treni; garimoshi; msururu. *v.t./i.* fundisha. *in ~*, nayoandaliwa. **~er** *n.* mkufunzi. **~ing** *n.* **~ college**, chuo cha mafunzo. *in ~*, katika afya nzuri.

*out of ~*, katika afya mbaya.

**trait** /treɪt/ *n.* tabia au sifa bainishi.

**traitor** /'treɪtə(r)/ *n.* msaliti; haini. **~ous** *adj.* mhaini. **traitress** *n.* mhaini wa kike.

**tram** /træm/ *n.* **~ car**, tramu: aina mojawapo ya treni ndogo ya umeme ya abiria katika maeneo ya miji.



tramcar

**tramp** /træmp/ *v. i.* tembea kwa kishindo; enda kwa miguu. *n.* mzururaji.

**trample** /'træmpl/ *v.t./i.* kanyaga; ponda kwa miguu.

**trance** /trɑ:ns/ *n.* kupagawa.

**trans-** /trænz/ *prefix* -a kuvuka; -a kupitia. **~atlantic**, -a kuvuka bahari ya Atlantiki. **~continental**, -a kuvuka kontinenti.

**transact** /træn'zækt/ *v.t.* fanya shughuli na fulani. **~ion** *n.* mapatano; shughuli.

**transcribe** /træn'skraɪb/ *v.t.* nukuu; nakili.

**transcript** /'trænskrɪpt/ *n.* nakala. **transcription** *n.* unukuzi; kunakili.

**transect** *v.t.* pita katikati; gawa kwa kupita katikati.

**transfer** /træns'fɜ:(r)/ *n.* uhamisho. *~ fee*, ada ya uhamisho. *v.t./i.* (**-rr-**) hamisha; hama. **~able** *adj.* -a kuhamishika; -a kubadilishika. **~ence** *n.* kupisha; kupita; kusihia, etc.

**transform** /træns'fɔ:m/ *v.t.* geuza; badili. **~ation** *n.* badiliko; ugeuzaji. **~er** *n.* transfoma.

**transfuse** *v.t.* tia damu. **transfusion** *n.* utiaji damu. *The patient had several blood transfusions*, mgonjwa aliongezwa damu mara kadhaa.

**transgress** /trænz'gres/ *v.t./i.* vuka mpaka; vunja sheria; vunja mwiko; tenda dhambi. **~ion** *n.* kosa; uhalifu; dhambi. **~or** *n.*mhalifu; mkosaji; mtenda dhambi.

**transient** /'trænziənt/ *adj.* -a kupita; -siodumu; -a muda mfupi tu.

**transistor** /træn'zɪstə(r)/ *n.* transista: kifaa cha dutu pitishi-pitishi chenye elektrodi tatu na kina uwezo wa kukuza umeme wa volteji ndogo.

**transit** /'trænzɪt/ *n.* kupita. *goods in ~*, bidhaa zinazosafirishwa. **~ visa**, viza ya kupita. **~ camp**, kambi ya wasafiri. **~ion** *n.* mageuzi; mpito; mabadiliko. **~ metal**, metali muunganisho: metali yenye tabia inayofanana na tabia za metali jirani yake upande wa kuume na kushoto katika jedwali mrudio wa elementi. **~ period**, kipindi cha mpito.

**transitive** /trænsətɪv/ *adj.* (kwa kitenzi) elekezi: chenye kutumika au kuelekezwa kwa mtendwa. **~ory** *adj.* -a kupita; -siodumu; -a muda mfupi tu.

**translate** /træns'leɪt/ *v.t.* fasiri. **translation** *n.* tafsiri.

**translator** /træns'leɪtə(r)/ *n.* mfasiri.

**transluscent** /træns'lu:snt/ *adj.* -enye ukungu: -enye kupitisha nuru bila taswira.

**transmit** /træns'mɪt/ *v.t.* (**-tt-**) peleka; ambukiza. **~ter** *n.* transmita: chombo cha kupeleka ishara, sauti, etc.

**transparent** /træns'pærənt/ *adj.* -angavu; -a kuona; wazi; bayana. **transparency** *n.* uwazi; uangavu.

**transpire** /træn'spaɪə(r)/ *v.i.* gemka: toka kupitia kwenye vinyweleo vya ngozi.

**transplant** /træns'plɑ:nt/ *v.t.* atika; pandikiza. **~ation** *n.* upandikizaji; uatikaji.

**transport** /'trænspɔ:t/ *n.* usafiri; uchukuzi. *v.t.* peleka; safirisha. *be ~ed with*, panda jazba; hemkwa. *in a ~s of delight*, -liohemkwa. **~ation** *n.* uchukuzi; usafirishaji. **~er** *n.* msafirishaji; mchukuzi; chombo cha uchukuzi.

**transpose** /træn'spəʊz/ *v.t.* badilishana nafasi. **transposition** *n.* ubadilishanaji nafasi.

**transversal** *n.* mkingamo: mstari wa kukingama. *adj.* -a kukingama.

**transverse** /'trænzvɜ:s/ *adj.* kingamo; kukingama. **transverse wave**, wimbi kingamo: wimbi

ambalo uwelekeo wa mitetemo hukingama uwelekeo wa mwendo wa wimbi. **~ly** *adv.* kwa kukingama.

**trap** /træp/ *n.* mtego; mtambo; hila. *v.t.* (**-pp-**) tega; nasa; danganya. **~door** *n.* mlango wa sakafuni au darini. **~per** *n.* mtega wanyama.

**travel** /'trævl/ *n.* usafiri; safari. *v.i.* (**-ll-**) safiri. **~ler** *n.* msafiri.

**traverse** /trə'vɜ:s/ *v.t.* pita; pitia; kingama.

**travesty** /'trævəsti/ *n.* mwigo; dhihaka. *v.t.* dhihaki kwa kuiga au kuvaa mavazi ya kike na kufanya vitimbi vingine.

**trawl** /trɔ:l/ *n.* nyavu ya kukokota chinichini. *v.i/t.* vua samaki kwa kukokota nyavu chinichini. **~er** *n.* meli ya uvuvi.

**tray** /treɪ/ *n.* sinia; chano; trei.

**treacherous** /'tretʃərəs/ *adj.* -danganyifu; -janja.

**treachery** /'tretʃəri/ *n.* udanganyifu; hila; usaliti.

**treacle** /'tri:kl/ *n.* asali ya miwa.

**tread** /tred/ *n.* kishindo; kidaraja cha ngazi; tredi: kashata ya tairi. *v.i/t.* kanyaga. *~ on air,* jawa na furaha.

**treason** /'tri:zn/ *n.* uhaini. **high ~**, uhaini mkubwa. **~able** *adj.* -a uhaini. **~ offence**, kosa la uhaini.

**treasure** /'treʒə(r)/ *n.* hazina. *~ house,* hazina. *v.t.* thamini sana. **~r** *n.* mhazini; mtunza hazina; mshika fedha. **treasury** *n.* hazina.

**treat** /tri:t/ *v.t./i.* **1.** tendea. *~ sb. well,* tendea fulani vyema. **2.** chukulia. *He ~ed the matter as a joke,* alichukulia kama utani. **3.** eleza. *He ~ed the subject thoroughly,* aliielezea vyema mada ile. **4.** (kwa hotuba, kitabu, etc.) *~ of,* husika na. *The essay ~s of insect pests,* insha yahusu wadudu waharibifu. **5.** tibu. **6.** karibisha. **7.** shauriana. **~ise** *n.* tasnifu. **~ment** *n.* utendeaji; matibabu.

**treaty** /'tri:ti/ *n.* mkataba. **~ port** bandari inayoruhusu bidhaa za nje kwa mkataba. **~ of friendship**, mkataba wa urafiki.

**treble**[1] /'trebl/ *v.t./i./adj.* zidisha au zidi mara tatu; a mara tatu.

**treble**[2] /'trebl/ *adj.* -a sauti nyembamba.

**tree** /tri:/ *n.* mti. *family ~,* ukoo; nasaba; usuli.

**trek** /trek/ *n.* safari ngumu na ndefu. *v.i.* (**-kk-**) enda safari ndefu.

**tremble** /'trembl/ *n.* mtetemeko; mtikisiko. *v.i.* tetemeka.

**tremendous** /trə'mendəs/ *adj.* kubwa mno. **~ ly** *adv.* vizuri mno.

**tremor** /'tremə(r)/ *n.* tetemeko; mtikisiko.

**trench** /trentʃ/ *n.* handaki; mfereji.

**trend** /trend/ *n.* mwelekeo. *set the ~,* anzisha mtindo. *v.i.* elekea.

**trepidation** /ˌtrepɪ'deɪʃn/ *n.* hofu; wasiwasi.

**trespass** /'trespəs/ *n.* uingiaji bila ruhusa. *v.i. ~ upon,* ingia bila ruhusa. **~er** *n.* mwingiaji bila ruhusa.

**trestle** /'tresl/ *n.* egemeo la meza au benchi lenye matendegu mawili.



**trestle**

**tri-** /traɪ/ *prefix* tatu.

**trial** /'trial/ *n.* hukumu; jaribio. *The child is a ~ to its teacher,* mtoto yule ni mtihani kwa mwalimu.

**triangle** /'traɪæŋgl/ *n.* pembe tatu. **triangular** *adj.* -enye pembe tatu; -a kuhusu washiriki watatu.



**triangle**

**tribe** /traɪb/ *n.* kabila. **tribal** *adj.* a kikabila. **tribalism** *n.* ukabila.

**tribunal** /traɪbju:nl/ *n.* mahakama. *military ~,* mahakama ya kijeshi.

**tribute** /'trɪbju:t/ *n.* ushuru; kodi. *pay ~ to a person,* shukuru; tukuza. **tributary** *n./adj.* mtawala wa serikali au serikali iliyo chini ya serikali nyingine; kijito.

**triceps** /traɪseps/ *n.* musuli ulioko nyuma ya sehemu ya juu ya mkono, karibu na bega.

**trick** /trɪk/ *n.* hila; mbinu. *play ~ on,* cheza shere. *v.t.* danganya. **~ery** *n.* udanganyifu. **~ster** *n.* laghai. **~y** *adj.* -danganyifu.

**trickle** /'trɪkl/ *n.* mchuruziko. *v.i./t.*

tiririka; churuzisha.

**tricuspid valve** *n.* vali kuspidi: vali baina ya chemba za chini na juu za moyo zizuiazo damu kuelekea upande sio.

**tricycle** /'traɪsɪkl/ *n.* baiskeli ya magurudumu matatu.

**trifle** /'traɪfl/ *n.* jambo dogo. *a ~,* kidogo. *v.i/t.* cheza cheza. **trifling** *adj.* dogo.

**trigger** /'trɪgə(r)/ *n.* mtambo wa kufyatulia risasi. *~ sth. off,* chokonoa mambo.

**trigonometry** /ˌtrɪgə'nɒmətri/ *n.* trigonometria: tawi la hisabati kuhusu uhusiano wa pembe na pembetatu na kazi zake.

**trim** /trɪm/ *adj.* nadhifu. *v.t./i.* (**-mm-**) punguza. *get into ~ for the sports meeting,* jiweka katika hali nzuri tayari kwa mashindano. **~ming** *n.* mapambo.

**trinity** /trɪnəti/ *n.* utatu.

**trio** /'tri:əʊ/ *n.* watatu pamoja; (muziki) wimbo wa watu watatu.

**trip** /trɪp/ *n.* safari; matembezi. *v.i./t.* (**-pp-**) tembea kwa hatua nyepesi; jikwaa. **~per** *n.* mtalii.

**triple** /trɪpl/ *adj.* -a mara tatu; -a tatu pamoja. **~ antigen**, antijeni utatu: chanjo wapewayo watoto kukinga kifaduro na pepopunda. **~t** *n.* pacha ya utatu; seti ya vitu vitatu.

**triplicate** /'trɪplɪkət/ *n.* nakala tatu. *v.t.* fanya nakala tatu.

**tripod** /'traɪpɒd/ *n.* kiweko chenye miguu mitatu.

**triumph** /'traɪʌmf/ *n.* furaha ya ushindi. *v.t. ~ over,* shangilia ushindi; shinda. **~ant** *adj.* -a furaha ya ushindi; -lioshinda.

**trivial** /'trɪviəl/ *adj.* dogo; -a kawaida. **~ity** *n.* jambo dogo lisilo na maana.



**trolley**

**trolley** /'trɒli/ *n.* kiberenge; toroli.

**trombone** /trɒm'bəʊn/ *n.* tromboni: tarumbeta yenye sauti nzito sana.



**trombone**

**troop** /tru:p/ *n.* kikosi; jeshi; kundi. **~ carrier**, chombo cha kusafirishia wana-jeshi. **~er** *n.* askari wa farasi au vifaru. *swear like a ~,* tukana sana.

**trophy** /'trəʊfi/ *n.* kumbu-kumbu ya ushindi; kikombe.

**tropic** /'trɒpɪk/ *n.* tropiki. *the ~s,* nchi za joto. **~al** *adj.* -a joto; -a tropiki.

**tropism** *n.* uwelekeokiamshi: hali ya kukua kwa sehemu ya mmea au mnyama kwa kuelekea upande mmoja maalumu.

**troposphere** *n.* angatropo: tabaka la chini kabisa katika angahewa, umbali wake ni wastani wa kilomita 7 toka pembe za dunia hadi kilomita 28 kwenye ikweta.

**trot** /trɒt/ *n.* mwendo wa matiti *v.t./i.* (**-tt-**) kimbia kwa hatua fupifupi. *on the ~,* mfululizo. **~ter** /trɒtə(r)/ *n.* farasi aliyefunzwa kukimbia kwa hatua fupifupi; kwato ya nguruwe.

**trouble** /'trʌbl/ *n.* shida; taabu. *in ~,* matatizoni. *~ maker,* mchochezi. *~ shooter,* msuluhishi. *v.t./i.* hangaisha; sumbua; hangaika. *fish in ~d water,* nufaika kutokana na vurugu.

**trough** /trɒf/ *n.* kihori; chombo cha kupondea unga.

**trounce** /traʊns/ *v.t.* piga sana.

**trousers** /'traʊzəz/ *n.* suruali.

**trousseau** /'tru:səʊ/ *n.* mapambo na mavazi ya bibi arusi.

**trout** /traʊt/ *n.* aina ya samaki wa mtoni huko Ulaya.

**trowel** /'traʊəl/ *n.* mwiko wa mwashi; kijiko cha kupandia mimea.

**troy** *n.* tola: kizio cha uzito wa vito vya thamani.

**truant** /'tru:ənt/ *n.* mtoro wa shule. *play ~,* toroka kazini au chuoni.



**trowels**

**truancy** /'tru:ənsɪ/ *n.* utoro.

**truce** /tru:s/ *n.* usimamishaji vita wa muda.

**truck** /trʌk/ *n.* lori; behewa la mizigo.

**trudge** /trʌdʒ/ *n.* mwendo mrefu wa kuchosha. *v.i.* jikokota.

**true** /tru:/ *adj.* kweli; aminifu.
**truly** /tru:li/ *adv.* kwa kweli; kwa dhati; kwa hakika.


trumpet

**truth** /tru:θ/ *n.* ukweli.
**trumpet** /'trʌmpɪt/ *n.* tarumbeta; parapanda; baragumu. *blow one's own ~*, jisifu; jigamba.
**truncheon** /trʌntʃən/ *n.* rungu.
**trundle** /'trʌndl/ *v.t./i.* biringisha; bingiria.
**trunk** /trʌŋk/ *n.* shina. *~ call*, simu ya mbali. *~ line*, reli kuu. *~ road*, barabara kuu.
**truss** /trʌs/ *n.* robota; mtumba; mkanda avaao mgonjwa wa ngiri. *~ sth. up*, fungasha katika mtumba.
**trust** /trʌst/ *n.* imani; amana. *~ fund*, mfuko wa dhamana. *v.t./i.* amini; tegemea. *~ in sb.*, amini mtu. *~ to sth.*, tegemea kitu. **~ee** *n.* mdhamini. **~eeship** *n.* udhamini; uamana. **public ~ee**, kabidhi wasii. **~ing** *adj.* -enye kuamini. **~worthy** *adj.* -a kutegemewa; -aminifu.
**try** /traɪ/ *n.* jaribio. *v.t./i.* **(tried)** jaribu. *~ sth. on*, jaribu; jigeza; jipimisha. *~ sth. out*, tumia kwa majaribio. **~-out** *n.* jaribio la awali. *~ for sth.*, jaribu kupata kitu. **~ing** *adj.* -sumbufu.
**tsetsefly** /'tsetsi flaɪ/ *n.* mbung'o; ndorobo.
**tsunami** /tsu:'nɒmi/ *n.* sunami: wimbi kubwa baharini linalo-sababishwa na tetemeko la ardhi chini ya bahari.
**tub** /tʌb/ *n.* beseni; pipa; hodhi. *~ thumper*, mhamasishaji.
**tube** /tju:b/ *n.* bomba; neli; tyubu; kioo cha televisheni; reli ya chini ya ardhi. **~ well**, kisima cha bomba.
**tubular** /'tju:bjələ(r)/ *adj.* -enye umbo la neli. **~less** *adj.* -sio na tyubu.
**tuber** /tju:bə(r)/ *n.* kiazi; kitunguu.
**tuberculosis** /tju:bɜ:kju'ləʊsɪs/ *n.* kifua kikuu. **tubercular** *adj.* liothiriwa na kifua kikuu. **tuberculous** *adj.* -a kifua kikuu.
**tuck** /tʌk/ *n.* pindo; keki. *~ shop*, duka la vyakula vitamu. *v.t./i.* chomelea. *~ in a shirt*, chomelea shati. *~ in a child*, fundika mtoto kwenye ubeleko.
**Tuesday** /tju:zdeɪ/ *n.* Jumanne.
**tug** /tʌg/ *n.* mvuto wa nguvu. *~ boat*, tagi: stima ya kuvuta meli kubwa. *~of war*, mchezo wa kuvutana kwa kamba.
**tuition** /tju'ɪʃn/ *n.* mafundisho. *~ fee*, ada ya mafundisho.
**tumble** /'tʌmbl/ *n.* anguko; kuporomoka. *v.t./i.* poromoka; chakaa; pindua; angusha. **~down** *adj.* -bovu. *~ to sth.*, gundua.
**tumbler** /'tʌmblə(r)/ *n.* bilauri.
**tumour** /'tju:mə(r)/ *n.* mtutuko: uvimbe wowote mwilini unaosa babishwa na ukuaji wa tishu usio wa kawaida.
**tundra** /'tʌndrə/ *n.* tundra: uwanda mpana usio na miti katika eneo la aktiki.
**tune** /tju:n/ *n.* tuni, lahani: mfuatano au uwiano wa sauti. *change one's tune*, badili tabia. *to the ~ of*, kiasi cha. *~ up*, tia lahani. *tuning fork*, uma wa tuni. **~r** *n.* kipokea mawimbi katika redio, televisheni, etc.; mrekebishaji sauti.
**tungsten** /'tʌŋsten/ *n.* tang'isteni: metali ya kemikali ya kijivu yenye sifa ya kufulika bamba, waya na isiyobabuka kirahisi ya nambari 74.
**tunic** /tju:nɪk/ *n.* koti refu; kanzu fupi; blauzi.
**tunnel** /'tʌnl/ *n.* njia ya chini kwa chini.
**turban** /'tɜ:bən/ *n.* kilemba.
**turbid** /'tɜ:bɪd/ *adj.* -enye matope; -liotibuliwa.
**turbine** /'tɜ:baɪn/ *n.* tabo: injini za maji, gesi, hewa, na mvuke. **turbogenerator**, tabojenereta: jenereta la mvuke au gesi. **turbo-jet**, tabojeti: ndege yenye injini ya mvuke au gesi.
**turbulent** /'tɜ:bjələnt/ *adj.* siodhibitika; -a ghasia. **turbulence** *n.* ghasia; fujo; maasi; zahama.
**turf** /tɜ:f/ *n.* majani mororo na udongo wake.
**turgid** /'tɜdʒɪd/ *adj.* -liovimba; (kwa lugha) -a kiburi. **~ity** *n.* uvimbe; kiburi.


turkey

**turkey** /'tɜ:ki/ *n.* batamzinga. *cold ~,* uachaji wa ghafla wa dawa ya kulevya.
**turmoil** /'tɜ:mɔɪl/ *n.* machafuko; zahama; ghasia.
**turn** /tɜ:n/ *n.* **1.** mzunguko. *three ~s,* mizunguko mitatu. *~ of the century,* mwanzo wa karne mpya. **2.** kona. *sudden ~s in the road,* kona kali barabarani. **3.** zamu. *do sth. ~ and ~ about,* fanya jambo kwa zamu. **4.** badiliko. *Events took a new ~,* mambo yalibadilika. **5.** tendo. *One good ~ deserves another,* matendo mema ni wajibu kulipwa. *do sb. a good ~,* tendea mtu wema. **6.** haja. *serve one's ~,* kidhi haja ya mtu. **7.** mshtuko. *The news gave me quite a ~,* habari zilinishtusha. *v.t./i.* zungusha; zunguka; badilisha; badilika; pindua; pinduka; geuza; geuka. *~ a deaf ear to sth.,* -tojali; -tosikiliza. *~ sb. adrift,* telekeza. *~ sb. down,* katalia. *~ up one's nose at sth.,* dharau. **~ing** *n.* kona.
**turnip** /'tɜ:nɪp/ *n.* ua la tanipu.
**turpentine** /'tɜ:pəntaɪn/ *n.* tarufeni: aina ya mafuta ya kuyeyushia na kuchanganyia rangi.
**turret** /'tʌrət/ *n.* mnara mdogo; banda la chuma lenye mizinga.
**turtle** /'tɜ:tl/ *n.* kasa. *turn ~,* (kwa meli) pinduka. *~ shell,* ng'amba: gamba la kasa.
**tusk** /tʌsk/ *n.* jino la ndovu; pembe. **~er** *n.* ndovu au nguruwe mwitu aliyepevuka.
**tussle** /tʌsl/ *n.* pambano. *v.i.* pambana vikali.
**tutor** /'tju:tə(r)/ *n.* mkufunzi; mhadhiri. *v.t.* fundisha. **~ial** *n.* semina ya ukufunzi. *adj.* -a ukufunzi.
**tweed** /twi:d/ *n.* nguo ya sufi.
**tweezers** /'twi:zəz/ *n.* kikoleo; kibanio.
**twelve** /twelv/ *n./adj.* kumi na mbili.
**twelfth** /twelfθ/ *adj.* -a kumi na mbili.
**twenty** /'twenti/ *n./adj.* ishirini. **twenties** *n.* miaka ya ishirini. **twentieth** *adj.* -a ishirini.
**twice** /twaɪs/ *adv.* mara mbili. *a ~ told tale,* habari inayofahamika vizuri.
**twig** /twɪg/ *n.* kitawi.
**twilight** /'twaɪlaɪt/ *n.* utusitusi wa asubuhi au jioni.
**twin** /twɪn/ *n.* pacha. *v.t. ~ with,* ungana na.
**twine** /twaɪn/ *n.* kitani; uzi.
**twinge** /twɪndʒ/ *n.* kichomi; maumivu makali ya ghafla.
**twinkle** /'twɪŋkl/ *n.* mmeremeto. *v.i.* meremeta; metameta. *in the twinkling of an eye,* kufumba na kufumbua; mara moja.
**twist** /twɪst/ *n.* msokoto; usokotaji. *v.t./i.* suka; sokota; songoa; geuza. *~ sb.'s arm,* popotoa mkono wa mtu. *~ sb. round one's little finger,* fanya mtu afanye unalotaka. **~er** *n. (colloq.)* laghai; jambo gumu. *tongue ~,* neno au sentensi ngumu kutamka.
**twitter** /'twɪtə(r)/ *n.* mlio wa sauti nyororo. v.i. (kwa ndege) lia kwa sauti nyororo.
**two** /tu:/ *n./adj.* mbili; pili; -wili. *put ~ and ~ together,* fahamu kwa kuunganisha mambo. **~some** *n.* mchezo wa watu wawili tu. **~-timer** *adj.* laghai. **~-tongued** *adj.* -enye kigeugeu.
**type** /taɪp/ *n.* aina; herufi za kupigia chapa. *true to ~,* mwakilishi hasa wa jamii yake. *~ face,* aina ya chapa. *~script,* kazi iliyopigwa chapa. *~ setter,* mtayarishaji chapa. **~writer**, mashine ya chapa. *~written,* iliyopigwa chapa. *v.t./i.* piga taipu; panga katika aina
**typist** /taɪpɪst/ *n.* mpiga taipu.
**typography** taɪ'pɒgrəfi/ *n.* taipografia: taaluma ya kupiga chapa. *faults of typography,* makosa ya uchapaji.
**typology** /taɪ'pɒlədʒi/ *n.* taipolojia: uainishi hasa wa maandiko ya Biblia na sayansi jamii.
**typhoid** /'taɪfɔɪd/ *n.* homa ya matumbo.
**typhoon** /taɪfu:n/ *n.* kimbunga; tufani.

**tyranny** /'taɪrəni/ *n.* uonevu; udhalimu; udikteta; utawala wa mabavu. **tyrannical** *adj.* -a kikatili; -a kidikteta; -a kidhalimu. **tyrannize** *v.i.* kandamiza; tawala kwa mabavu; onea; dhulumu. **tyrannous** *adj.* onevu.

**tyrant** /taɪrənt/ *n.* dikteta; mtawala wa mabavu.

**tyre** /'taɪə(r)/ *n.* mpira; tairi.

# Uu

**ubiquitous** /ju:'bɪkwɪtəs/ *adj.* -a kuwapo kila mahali. **ubiquity** *n.* ueneaji wa kila mahali.

**ugly** /'ʌgli/ *adj.* -baya; -a kutisha; -siovutia. *The sky looks ~,* kumefinga. *an ~ customer,* mtu wa hatari.

**ulcer** /'ʌlsə(r)/ *n.* kidonda.

**ulna** /'ʌlnə/ *n.* kigasha: mfupa mwembamba ndani ya mkono unaoanzia kikoni hadi kingajani.

**ultimate** /'ʌltɪmət/ *adj.* -a mwisho; -a msingi. **~ cause**, sababu ya msingi. **~ly** *adv.* hatimaye.

**ultimatum** /ˌʌltɪ'meɪtəm/ *n.* kauli ya mwisho. *give an ~ to a person,* toa kauli ya mwisho kwa mtu.

**ultra-** /'ʌltrə/ *prefix* -a kupita kiasi.

**ultrasonic** /ˌʌltrə'sɒnɪk/ *n.* kiuka sauti: kasimawimbi kubwa ambayo inavuka usikizi wa binadamu.

**ultrasound** /ˌʌltrəsaʊnd/ *n.* kiuka sauti: sauti ya kasimawimbi kubwa mno kiasi cha kuvuka usikizi wa mwanadamu.

**ultraviolet** /ˌʌltrə'vaɪələt/ *n.* urujuanimno: mnururisho sumakuumeme usioonekana katika mwangaza wa jua.

**umbel** *n.* shaziua mwamvuli: mpangilio wa shaziua kama mwamvuli ambao vikonyo vya viua vyake huanzia mahali pamoja.

**umbilical cord** /ʌmˌbɪlɪkl 'kɔ:d/ *n.* utovuti: tishu yenye umbo la kamba inayounganisha kitovu cha mtoto mchanga kabla ya kuzaliwa na plasenta katika uterasi wa mama.

**umbra** *n.* uvuligiza: kivuli ambacho huleta giza totoro katika kupatwa kwa jua ambapo nuru hukosekana.

**umbrella** /ʌm'brelə/ *n.* mwavuli; hifadhi. *under the ~ of AU,* chini ya hifadhi ya Umoja wa Afrika.

**umpire** /'ʌmpaɪə(r)/ *n.* mwamuzi hasa katika michezo ya tenisi na golfu; msuluhishi.

**un-** /ʌn/ *prefix* sio; hapana; tenda kinyume. e.g. *~certain,* si yakini. *~tie,* fungua. *~willingness,* kutotaka.

**unaccountable** /ˌʌnə'kaʊntəbl/ *adj.* -sioelezeka.

**unanimous** /ju'nænɪməs/ *adj.* -a pamoja; -a kauli moja; siopingwa. **~ly** *adv.* kwa kauli moja. **unanimity** *n.* umoja. *with ~,* kwa umoja.

**unawares** /ˌʌnə'weəz/ *adv.* ghafla; bila kutazamiwa; bila kutambua. *She dropped her money ~,* aliangusha pesa zake bila kutambua.

**unbalanced** /ˌʌn'bælənst/ *adj.* kichaa.

**uncle** /'ʌŋkl/ *n.* mjomba; ami.

**uncouth** /ʌn'ku:θ/ *adj.* -shenzi; jinga.

**under**[1] /'ʌndə(r)/ *prep./adv.* chini ya; chini. **~ age**, -siotimiza umri wa sheria. *~ discussion,* -nayojadiliwa. *~ protest,* kwa upinzani. *~ fire,* katika mapambano. *~ orders,* chini ya amri.

**under-**[2] /'ʌndə(r)/ *prefix* -a chini. *~clothes,* nguo za ndani. *~charge,* toza thamani pungufu ya. *~estimate,* kadiria pungufu. *~fed,* -siolishwa vya kutosha.

**undercurrent** /'ʌndəkʌrənt/ *n.* mkondo wa chini; *(fig.)* maoni ya chinichini.

**undercut** /'ʌndəkʌt/ *v.t.* uza kwa bei ya chini kuliko ya washindani

wako.
**underdog** /'ʌndədɒg/ *n.* anayeonewa; anayedhalilishwa.
**underdone** /ˌʌndə'dʌn/ *adj.* (hasa kwa nyama) -siopikwa vizuri; bichi.
**undergo** /ˌʌndə'gəʊ/ *v.t.* pitia; fanya.
**undergraduate** /ˌʌndə'grædʒuət/ *n.* mwanafunzi wa chuo kikuu wa shahada ya kwanza.
**underground** /'ʌndəgraʊnd/ *adv.* chini ya ardhi. *n. the ~,* treni ya chini ya ardhi.
**undergrowth** /'ʌndəgrəʊθ/ *n.* magugu; vichaka.
**underhand** /ˌʌndəhænd/ *adj./adv.* a hila; -danganyifu; kwa siri; kwa udanganyifu. *~ dealings,* njama.
**underlie** /ˌʌndə'laɪ/ *v.t.* -wa msingi wa; -wa chini ya.
**underline** /ˌʌndə'laɪn/ *v.t.* piga mstari chini; *(fig.)* sisitiza.
**undermine** /ˌʌndə'maɪn/ *v.t.* fukua chini; dhoofisha kidogo kidogo. *His health was ~d by over work ,* afya yake ilidhoofika kidogo kidogo kwa kazi nyingi.
**underneath** /ˌʌndə'ni:θ/ *adv./prep.* chini; chini ya.
**undersigned** /ˌʌndə'saɪnd/ *adj.* -liyotiwa saini hapa chini.
**understand** /ˌʌndə'stænd/ *v.t./i.* (**understood**) fahamu; elewa; tambua. **~able** *adj.* -nayoeleweka. **~ing** *adj.* -enye kuthamini mawazo ya wingine. *n.* ufahamu; mapatano. *In this ~ only I will come,* kwa sharti hili tu nimekubali kuja.
**undertake** /ˌʌndə'teɪk/ *v.t.* (**undertook**,**undertaken**) kubali kufanya jambo. **undertaking** *n.* ahadi; dhamana; kazi. **~r** *n.* mwenye kutayarisha maziko; mzishi.
**undertone** /'ʌndə'təʊn/ *n.* sauti ya kunong'ona.
**underwear** /'ʌndəweə(r)/ *n.* nguo za ndani.
**underworld** /'ʌndəwɜ:ld/ *n.* jahanamu; jamii ya watu waovu.
**underwrite** /ˌʌndə'raɪt/ *v.t.* kubali jukumu; dhamini. **~r** *n.* mdhamini.
**undo** /ʌn'du:/ *v.t.* (**undid**, **undone**) fundua; tangua. *be undone,* potea; angamia. **~ing** *n.* sababu ya kupotea au ya kuangamia.
**undue** /ˌʌn'dju:/ *adj.* -liyokiuka mpaka; -siyostahili. **unduly** *adv.* mno.
**undulate** /'ʌndjuleɪt/ *v.i.* inuka na kushuka; piga mapinde.
**unearth** /ʌn'ɜ:θ/ *v.t.* gundua; fukua. *~ a buried treasure,* fukua hazina. *~ new facts about the life of someone,* gundua habari mpya juu ya maisha ya fulani. **~ly** *adj.* -a peponi; si -a dunia hii.
**uneasy** /ʌn'i:z/ *adj.* si -a raha; si -tulivu; -a wasiwasi. **uneasily** *adv.* kwa wasiwasi.
**uneasiness** *n.* wasiwasi.
**unfailing** /ʌn'feɪlɪŋ/ *adj.* -a daima; -siokwisha; -siokwama.
**unfold** /ʌn'fəʊld/ *v.t.* kunjua; tangaza.
**unfounded** /ʌn'faʊndɪd/ *adj.* -sio na msingi. *~ rumours,* uvumi usio na msingi
**ungainly** /ʌn'geɪnli/ *adj.* -zito; si -zuri; ovyoovyo.
**ungovernable** /ʌn'gʌvənəbl/ *adj.* -siozuilika; -siotawalika; siodhibitika. *~ temper,* hasira isiyozuilika.
**unguarded** /ʌn'gɒ:dɪd/ *adj.* (hasa kwa maneno) -sio ya busara; -sio ya hadhari. *in ~ moment,* bila kufikiri; bila hadhari.
**unheard-of** /ʌn'hɜ:d ɒv/ *adj.* -a ajabu; -geni; -sio na kifani.
**unhinged** *adj.* -liyerushwa akili.
**unicorn** /'ju:nɪkɔ:n/ *n.* (katika hadithi za zamani) mnyama kama farasi mwenye pembe moja.
**uniform** /'ju:nɪfɔ:m/ *adj.* sare; sawasawa; -a kulingana; -a mfano mmoja. *n.* sare; unifomu. **~ity** *n.* ulinganifu. **~ly** *adv.* kwa kulingana.
**unify** /'ju:nɪfʌɪ/ *v.t.* unganisha; fanya kuwa moja. **unification** *n.* uunganishaji.
**union** /'ju:niən/ *n.* umoja; muungano; jumuia; chama. **~ist** *n.* mwanachama.
**unique** /ju'ni:k/ *adj.* -a pekee; -sio na kifani . **~ly** *adv.* kwa namna ya

pekee. **~ness** *n.* upekee.

**unison** /'ju:nɪs(ə)n/ *n.* upatano. *in ~,* kwa umoja; kwa mapatano. *They shouted in ~,* walipiga kelele kwa pamoja.

**unit** /'ju:nɪt/ *n.* kitu kimoja; kizio. *~ square,* kizio mraba. *~ furniture,* seti ya samani. *~ trust,* amana ya kikundi. **~ary** *adj.* -a moja.

**unite** /ju'naɪt/ *v.t./i.* unga; unganisha; ungana; unganika. **~d** *adj.* lioungana.

**unity** /ju'nəti/*n.* umoja.

**universe** /'ju:nɪvɜ:s/ *n.* ulimwengu; vitu vyote.

**universal** /ˌju:nɪ'vɜ:sl/ *adj.* -a watu wote; -a kazi zote; -a watu wote. *universal indicator,* kiashirio jumla: kiashirio ambacho kinaweza kuashiria kemikali mbalimbali. **universally** *adv.* kilimwengu.

**university** /ˌju:nɪ'vɜ:səti/ *n.* chuo kikuu.

**unless** /ən'les/ *conj.* ila; isipokuwa. *He will not come ~ you order him,* hatakuja mpaka umwamrishe.

**unmentionable** /ʌn'menʃənəbl/ *adj.* -baya sana; -siosemeka; - siotajika.

**unmistakable** /ʌnmɪ'steɪkəbl/ *adj.* dhahiri; bayana; wazi.

**unpleasantness** /ʌn'plezntnəs/ *n.* ugomvi; chuki; maudhi; ubaya.

**unprecedented** /ʌn'prɛsɪdɛntɪd/ *adj.* -sio na kifani; a pekee; - siwahi kutokea.

**unprincipled** /ʌn'prɪnsəpld/ *adj.* -potovu; -a tabia mbaya; sio aminifu.

**unravel** /ʌn'rævl/ *v.t./i.* (**-ll-**) fumua; tatua; fumbua.

**unremitting** /ˌʌnrɪ'mɪtɪŋ/ *adj..* siolegea; -siochoka; -a kufululiza; -a kudumu.

**unrest** /ʌn'rest/ *n.* wasiwasi; vurugu.

**unruly** /ʌn'ru:li/ *adj.* -kaidi; -tukutu; fedhuli; -tundu.

**unsavoury** /ʌn'seɪvəri/ *adj.* -sio-pendeza; -a ufedhuli.

**unscathed** /ʌn'skeɪðd/ *adj.* -sio-dhurika; salama salimini.

**unscrupulous** /ʌn'skru:pjələs/ *adj.* si -nyofu; fedhuli.

**unsettle** /ʌn'setl/ *v.t.* hangaisha; tia wasiwasi; fadhaisha.

**unsightly** /ʌn'saɪtli/ *adj.* -sio pendeza macho; a kuchukiza.

**unsound** /ˌʌn'saʊnd/ *adj.* si zima; si imara; -pungufu. *person of ~ mind,* punguani.

**unspeakable** /ʌn'spi:kəbl/ *adj.* -sio-semeka; -a kuchukiza kabisa.

**unthinkable** /ʌn'θɪŋkəbl/ *adj.* -sio-wazika.

**unthinking** /ʌn'θɪŋkɪŋ/ *adj.* -a pupa; bila kufikiri. *He did it ~ly,* alifanya bila kufikiri.

**until** /ən'tɪl/ *prep./conj.* hata; mpaka; hadi.

**untimely** /ʌn'taɪmli/ *adj.* -a wakati usiofaa.

**unto** /'ʌntə/ *prep.* (la zamani) kwa.

**untold** /ˌʌn'təʊld/ *adj.* -siosimuliwa; -siohesabika. *a man of ~ wealth,* mtu tajiri kupita kifani.

**untoward** /ˌʌntə'wɔ:d/ *adj.* sumbufu; -siofaa; -a bahati mbaya; -siyopendelewa.

**unutterable** /ʌn'ʌtərəbl/ *adj.* siosemeka; -baya mno.

**unwieldy** /ʌn'wi:ldi/ *adj.* kubwa tena -zito.

**unwitting** /ʌn'wɪtɪŋ/ *adj.* bila kujua; -siokusudiwa. **~ly** *adv.* bila kukusudia.

**up**[1] /ʌp/ *adv./prep.* **1.** juu. **2.** zaidi. *The price has gone ten shillings ~,* bei imezidi kwa shilingi kumi. *be ~,* amka; -wa macho. **3.** hadi. *He went ~ to the head office,* alikwenda hadi ofisi kuu. *~ to sth.,* -enye shughuli na. *What's he ~ to?* anashughulika na nini ? *He's ~ to no good,* hana la maana alifanyalo. *~ to,* sawa na. *His work is not ~ to much,* kazi yake hairidhishi. *I don't feel ~ to doing much,* najiona siwezi kufanya kazi sana. *What's ~? (slang)* kuna nini? *The game's ~, It's all ~,* mchezo umekwisha. *~ and down,* chini juu. *~s and downs, (fig.)* pata potea.

**up-**[2] /ʌp/ *prefix* kuelekea juu. *an upturned nose,* pua iliyoinuka.

**upbraid** /ʌp'breɪd/ *v.t.* karipia, laumu; shutumu; kemea.

**upbringing** /'ʌpbrɪŋɪŋ/ *n.* malezi.
**upheaval** /ʌp'hi:vl/ *n.* mabadiliko makubwa ya ghafla. *The country is in a state of ~,* nchi imo katika mabadiliko makubwa.
**uphill** /ˌʌp'hɪl/ *adj.* -a kupanda; -a shida; -gumu. *an ~ task,* kazi ngumu.
**uphold** /ʌp'həʊld/ *v.t.* (**upheld**) thibitisha; unga mkono.
**upkeep** /'ʌpki:p/ *n.* gharama za matunzo.
**upland** /'ʌpland/ *n.* nyanda za juu.
**uplift** /'ʌp'lɪft/ *v.t.* tia moyo.
**upon** /ə'pɒn/ *prep.* juu ya. *put ~ sb.,* -pa fulani kazi zaidi ya stahili yake.
**upper** /'ʌpə(r)/ *adj.* -a juu; bora. *get (have) the ~ hand,* shinda; dhibiti. **~most** *adj./adv.* -a juu kabisa; juu kabisa. *He said whatever came ~most,* alisema kile kilichomjia kwanza akilini. *be down on one's ~s,* fukarika.
**upright** /'ʌpraɪt/ *adj.* -a wima. *n.* nguzo. **~ly** *adv.* wima; kwa uaminifu.
**uprising** /'ʌpraɪzɪŋ/ *n.* maasi; machafuko.
**uproar** /'ʌprɔ:(r)/ *n.* makelele; fujo; ghasia; vurumai. **~ious** *adj.* -a makelele.
**uproot** /ˌʌp'ru:t/ *v.t.* ng'oa.
**upset** /ʌp'sɛt/ *n.* vurugu; mfadhaiko. *v.t./i.* **1.** pindua; pinduka. **2.** tia wasiwasi; vuruga; tibua.
**upside-down** *adv.* juu chini.
**upstairs** /ˌʌp'steəz/ *adv.* ghorofani.
**up-to-date** *adj.* -a kisasa; -pya kabisa.
**upward** /'ʌpwəd/ *adj.* -a kwenda juu; -a kuelekea juu.
**uranium** /jʊ'reɪnɪəm/ *n.* uraniamu; urani: madini nzito nyeupe inayotoa nguvu za atomiki katika mitambo ya nyuklia.
**Uranus** /'jʊərənəs/ *n.* Zohali: sayari ya saba katika mfumo wa jua.
**urban** /'ɜ:bən/ *adj.* -a mji. **~ planning**, mipango miji. **~ize** *v.t.* fanya kuwa -a mji.
**urbane** /ɜ:beɪn/ *adj.* a adabu sana. **urbanity** *n.* adabu; utu wema.
**urea** /jʊ'ri:ə, 'jʊəriə/ *n.* urea: msombo wa kikaboni wa kifuwele mweupe upatikanao kwenye mkojo.
**ureter** /jʊ'ri:tə, 'jʊərɪtə/ *n.* ureta: vifereji viwili katika figo ambavyo hupitisha mkojo na kuishia kibofuni.
**urethra** /jʊ'ri:θrə/ *n.* urethra: kibomba cha kupitishia mkojo kutoka kibofuni.
**urge** /ɜ:dʒ/ *n.* uchu; hamu kubwa. *v.t.* sihi sana; bembeleza. **~ncy** *n.* umuhimu; haraka. **~nt** *adj.* -a haraka; muhimu. **~ntly** *adv.* haraka.
**urine** /'jʊərɪn/ *n.* mkojo. **uric** *adj.* -a mkojo. **urinal** *n.* chombo cha kukojolea kitandani; msala; sehemu ya kutabawali. **urinary** *adj.* -a mkojo. **~ bladder**, kibofu mkojo: kifuko cha mkojo. **~ system**, mfumo wa mkojo. **urinate** *v.i.* kojoa.




**human urinary system | mfumo wa njia ya mkojo**

**urn** /ɜ:n/ *n.* buli; chombo cha kutilia majivu ya maiti aliyechomwa.
**usage** /'ju:sɪdʒ/ *n.* matumizi; mazoea; desturi.
**use** /ju:z/ *n.* **1.** matumizi. **2.** kazi. **3.** faida. **4.** uwezo wa kutumia. **5.** ruhusa ya kutumia. **6.** mazoea. *v.t.* tumia; tendea. *~ up,* tumia -ote. *~ others as you would like them to ~ you,* tendea wingine vile upendavyo wakutendee. **~d** *adj.* -

liotumika. -sio mpya. **~ful** *adj.* -a manufaa. **~fully** *adv.* kwa manufaa. **~fulness** *n.* manufaa. **~less** *adj.* -siofaa; -sio manufaa. **~lessly** *adv.* bure; bila manufaa. **~lessness** *n.* kutokuwa na manufaa. **~r** *n.* mtumiaji. *How many telephone ~s are there in your town?* kuna watumiaji wangapi wa simu mjini kwenu?

**usual** /'ju:ʒuəl/ *adj.* -a desturi; -a kawaida. **~ly** *adv.* kwa kawaida; aghlabu.

**uterus** /'ju:tərəs/ *n.* uterasi: sehemu ya kizazi cha mama ambapo kitoto hujishikiza na kuendelea kukua hadi kinapozaliwa.

**utensil** /ju:'tensl/ *n.* chombo; ala. *~s,* vyombo vya nyumbani.

**utility** /ju:'tɪləti/ *n.* manufaa; matumizi. **public utilities**, huduma za jamii.

**utilitarian** /ˌju:tɪlɪ'teəriən/ *adj.* -a kuzingatia manufaa.

**utilize** /'ju:təlaɪz/ *v.t.* tumia.

**utilization** /ˌju:təlaɪ'zeɪʃn/ *n.* matumizi.

**utmost** /'ʌtməʊst/ *n.* upeo. *do your ~,* fanya kila liwezekanalo. *adj.* -a juu. *in the ~ danger,* katika hatari kabisa. *of the ~ importance,* muhimu sana.

**utopia** /ju:'təʊpɪə/ *n.* jamii timilifu kidhahania. **~n** *adj.* -a njozi.

**utter**[1] /'ʌtə(r)/ *adj.* kabisa; -tupu. *~ darkness,* giza totoro. **~ly** *adv.* kabisa kabisa.

**utter**[2] /'ʌtə(r)/ *v.t.* sema; tamka. **~ance** *n.* usemi; tamko. *give ~ to one's feelings,* toa dukuduku.

**uttermost** /'ʌtəməʊst/ *adj.* -a mwisho. *~ part,* ncha.

# Vv

**vacant** /'veɪkənt/ *adj.* **1.** -tupu. **2.** (kwa akili) -sio na wazo; **~ly** *adv.* bila kuwa na kitu. **vacancy** *n.* **1.** uwazi. **2.** ukosefu wa mawazo. **3.** nafasi wazi ya kazi. *There are many vacancies for clerks,* kuna nafasi nyingi za ukarani.

**vacate** /veɪ'kɪt, vəeɪt/ *v.t.* hama; ondoka.

**vacation** /və'keɪʃn; veɪ'k/ *n.* **1.** kuacha; kuondoka; kuhama. **2.** muda wa kupumzika; likizo; livu.

**vaccinate** /'vaksɪneɪt/ *v.t.* chanja. **vaccination** *n.* chanjo; kuchanja. **vaccine** *n.* dawa ya chanjo.

**vacillate** /'vasɪleɪt/ *v.i.* sitasita; babaika; yumba. **vacillation** *n.* kuyumba; kubabaika; kusitasita.


vacuum cleaner

**vacuole** /'vakjʊəʊl/ *n.* vakuoli: uwazi mmoja wapo ndani ya sitoplazimu ya seli ya mmea iliyokomaa.

**vacuum** /'vakjʊəm/ *n.* ombwe; tupu. **~ cleaner**, kivuta vumbi. **~ flask**, chupa ya chai; themosi. **~ pump**, kivuta hewa; kivuta maji. **~ valve**, vali ombwe ya kuchunguzia mkondo wa umeme.

**vagina** /və'dʒʌɪnə/ *n.* uke: sehemu ya nje ya mfumo wa uzazi wa kiumbe kike hadi kwenye uterasi.

**vagrant** /'veɪgr(ə)nt/ *n./adj.* mzururaji; mhuni; -zururaji; -sio na kwao.

**vague** /veɪg/ *adj.* **1.** sio dhahiri. **2.** (kwa watu) -a wasiwasi; -sio na uhakika. **~ly** *adv.* kwa wasiwasi; si bayana. **~ness** *n.* ukosefu wa udhahiri.

**vain** /veɪn/ *adj.* **1.** -a bure; -siofaa. **2.** -a kujiona; -a kiburi . *in ~,* bure. **~glory** *n.* kiburi; kujiona; majisifu; majivuno. **~glorious** *adj.* -a kujiona; -a kujisifu. **~ly** *adv.* bure; kwa kiburi.

**valence** /'væləns/ *n.* valensi: uwezo wa atomu kuungana.

**valency** /'veɪl(ə)nsi/ *n.* valensi: tabia inayoukilia idadi ya atomu au radikali ambazo atomu moja au radikali moja itaunganika kwayo

kikemikali.
**valiant** /'væliənt/ *adj.* shujaa ; hodari; jasiri.
**valid** /'vælɪd/ *adj.* **1.** halali; -enye sheria thabiti. **2.** (kwa mapatano) -enye nguvu. **3.** (kwa hoja, sababu) -a akili. **~ly** *adv.* kihalali. **~ate** *v.t.* halalisha; thibitisha. **~ity** *n.* uhalali; uthabiti.
**valley** /'væli/ *n.* bonde.
**valour** /'vælə(r)/ *n.* ushujaa; ujasiri.
**valorous** *adj.* shujaa; jasiri.
**value** /vælju:/ *n.* thamani; faida; manufaa. **~ added tax** *(VAT)*, kodi ya ongezeko la thamani. *~s*, maadili. *v.t.* thamini; kadiria; tathmini.
**valuable** /'væljuəbl/ *adj.* -a thamani. **valuables** *n.* vitu vya thamani.
**valuation** /ˌvælju'eɪʃn/ *n.* ukadiriaji. **valuator** *n.* mkadiriaji thamani.
**valve** /vælv/ *n.* vali; kilango. **valvular** *adj.* -a mishipa ya damu; -a vali za moyo.


valve

**van**[1] /væn/ *n.* gari la mizigo.
**van**[2] /væn/ *n.* (jeshini) kikosi cha mbele.
**vanadium** /və'neɪdiəm/ *n.* vanadiamu: metali ngumu ya rangi ya fedha.
**vanish** /'vænɪʃ/ *v.i.* toweka; tokomea.
**vanity** /'vænəti/ *n.* kiburi; majivuno; majisifu.
**vanquish** /'vaŋkwɪʃ/ *v.t.* shinda; tiisha.
**vapour** /veɪpə(r)/ *n.* mvuke; ukungu. **vaporize** *v.t./i.* geuka au geuza mvuke; fusha. **vaporization** *n.* kuvukisha; mvukisho.
**varnish** /'vɑ:nɪʃ/ *n.* vanishi. *v.t.* paka vanishi.
**vary** /'veəri/ *v.i./t.* geuka; badilika; geuza; badilisha. **variable** *adj.* -a kugeuka; geugeu. **variability** *n.* ugeukaji; ubadilikaji. **variance** *n.* ugeukaji; mpishano.
**variant** /'veəriənt/ *n.* kibadala: namna nyingine ya neno moja. *adj.* tofauti. *~ tire' and ~ tyre' are variant spellings*, ~ tire' ~ tyre' ni vibadala vya neno moja. **variation** *n.* uhitilafiano: kubadilika hali ya vitu kutoka hali ya kawaida na kuwa tofauti kimaumbile au kijeni. **varied** *adj.* -a namna nyingi. **variety** *n.* namna; aina; jinsi. *for a variety of reasons*, kwa sababu mbalimbali. **various** *adj.* anuwai; mbalimbali; aina kwa aina.
**vascular system** *n.* mfumo kifereji: mfumo wa vifereji maalumu vyenye kazi ya kupitisha vioevu mwilini.
**vascular tissue** *n.* tishu kifereji: tishu maalumu yenye kazi ya kupitisha kioevu mwilini.
**vas deferens** *n.* tyubu inayotoa spamu kutoka kwenye kende.
**vase** /vɑ:z/ *n.* chombo cha kutilia maji, maua ya mapambo.
**vasectomy** /və'sɛktəmi/ *n.* uhasishaji: operesheni ya kumhasi dume ili asiweze kutoa mbegu za uzazi.
**vast** /vɑ:st/ *adj.* kubwa mno; -ingi mno.
**vault**[1] /vɔ:lt/ *n.* kuba; chumba cha chini kwa chini. **~ed** *adj.* -enye kuba.
**vault**[2] /vɔ:lt/ *n.* mruko. *v.i./t.* ruka juu kwa msaada wa upondo.
**veal** /vi:l/ *n.* nyama ya ndama.
**vector** /'vɛktə/ *n.* vekta: tabia yoyote ya kimaumbile ambayo ina ukubwa na uelekeo.
**veer** / viə(r)/ *v.i.* (hasa kwa upepo, kwa mawazo) badili welekeo. *the wind ~ed round to north*, upepo ulivumia kaskazini.
**vegetable** /'vɛdʒtəb(ə)l/ *n.* mboga. **~ marrow**, mung'unye. **~ soup**, supu ya mboga. *adj.* -a mboga, -a kuhusu mboga. **vegetarian** *n.* mla mboga za majani, yaani asiyekula nyama kabisa. *adj.* -a kula mboga za majani.
**vegetation** /ˌvedʒə'teɪʃn/ *n.* mimea.
**vehicle** /'vi:əkl/ *n.* gari; nyenzo. *use the newspapers as a ~ for political views*, tumia magazeti kuwa nyenzo ya kuenezea maoni ya kisiasa.
**vehicular** /və'hɪkjələ(r)/ *adj.* -a. magari.

**veil** /veɪl/ *n.* utaji; shela; mtandio. *v.t.* funika kwa shela; ficha.
**vein** /veɪn/ *n.* vena; kishipajani; mwelekeo wa mawazo. *He talked in comic ~,* aliongea kwa mzaha.
**velocity** /və'lɒsɪti/ *n.* kasimwelekeo.
**velvet** /'velvɪt/ *n.* mahameli.
**vend** *v.t.* (hutumika hasa kwa sheria) uza; chuuza. **~or** *n.* m c h u u z i ; mtembezi.



**vein | vena**

**venerable** /'venərəbl/ *adj.* -a kuheshimiwa; -a heshima; -a kustahiwa. **venerate** *v.t.* heshimu; stahi; tukuza. **veneration** *n.* heshima.
**venereal disease** *n.* ugonjwa wa zinaa.
**vengeance** /'vɛn(d)ʒ(ə)ns/ *n.* kisasi. *take ~,* lipiza kisasi. *with a ~, (colloq.)* kwa nguvu; sana. **vengeful** *adj.* -a kutaka kulipa kisasi.
**venn-diagram** *n.* mchoro veni: mchoro wa maumbo yanayo-kiukana unaotumiwa kuwakilisha seti na uhusiano baina ya seti.
**venom** /'venəm/ *n.* sumu ya nyoka, mdudu, etc.; chuki. **~ous** *adj.* -a sumu; -a chuki.
**vent** /vent/ *n.* tundu. *give ~ to,* toa dukuduku. *He gave ~ to his anger,* alitoa dukuduku la hasira yake. *v.t.* toa nje.
**ventilate** /'ventɪleɪt/ *v.t.* pitisha hewa safi; burudisha kwa hewa; eneza; tangaza. **ventilation** *n.* hewa safi.
**ventilator** /'ventɪleɪtə(r)/ *n.* tundu au chombo cha kupitishia hewa.
**ventricle** /'vɛntrɪk(ə)l/ *n.* ventrikali: mojawapo ya chemba mbili za chini katika moyo.
**ventriloquist** /vɛn'trɪləkwɪst/ *n.* mtu awezaye kutoa sauti kama kwamba inatoka kwa mtu mwingine mbali kidogo.
**venture** /'ventʃə(r)/ *n.* jambo la hatari. *v.t./i.* jusurisha; thubutu. **~some** *adj.* -a ujasiri.
**Venus** /'vi:nəs/ *n.* Zuhura: sayari ya pili kutoka kwenye jua iliyopo baina ya Mirihi na dunia.
**veracious** /və'reɪʃəs/ *adj.* -a kusema kweli. **veracity** *n.* kweli.
**veranda** (**h**) /ve'rændə/ *n.* baraza; varanda; roshani.
**verb** /vɜ:b/ *n.* kitenzi. *auxiliary ~,* kitenzi saidizi. **~al** *adj.* -a maneno tu. *a ~ error,* kuteleza ulimi. **~ally** *adv.* kwa maneno (si kwa maandishi). **~atim** *adv.* sisisi: kwa maneno yenyewe hasa. **~ose** *adj.* -a maneno mengi. **~osity** *n.* utumiaji maneno mengi.
**verdict** /'vɜ:dɪkt/ *n.* hukumu; uamuzi.
**verge** /vɜ:dʒ/ *n.* ukingo; mwisho; mpaka. *be on the ~ of,* karibia. *v.i.* karibia; pakana na.
**verify** /'vɛrɪfʌɪ/ *v.t.* hakikisha; thibitisha. **verifiable** *adj* -a kuthibitishika. **verification** *n.* uthibitisho; hakika.
**vermin** /'vɜ:mɪn/ *n.* wanyama au wadudu waharibifu. **~ous** *adj.* -haribifu; -enye chawa, utitiri, etc. **~ diseases**, magonjwa yaletwayo na wadudu au wanyama waharibifu.
**vernacular** /və'nakjʊlə/ *n.* lugha ya kienyeji; lahaja. *in the ~,* kwa lahaja ya kienyeji. *adj.* -a lahaja.
**versatile** /'vɜ:sətaɪl/ *adj.* hodari na enye kupendelea mambo mbali-mbali. **versatility** *n.* uhodari katika mambo anuwai.
**verse** /vɜ:s/ *n.* ushairi; aya; ubeti. *give chapter and ~ for,* toa kumbukumbu halisi. **versification** *n.* ushairishaji.
**version** /'vɜ:ʃn/ *n.* tafsiri; masi-mulizi; habari kama ilivyotolewa na mtu.
**versus** /'vɜ:səs/ *prep.* dhidi ya.
**vertebra** /'və:tɪbrə/ *n.* vetabra: moja ya mifupa ya uti wa mgongo wa mnyama. **~te** *n.* mnyama mwenye mtungo wa mifupa ya mgongo. **~l column** *n.* safu vetabra: safu ya mifupa ya uti wa mgongo wa mnyama.
**vertex** /'və:tɛks/ *n.* nukta ambapo mistari miwili au kingo mbili

hukutana.
**vertical** /'vɜːtɪkl/ *adj.* -a wima.
**very** /'veri/ *adv.* sana; kabisa. *adj.* halisi; hasa; kweli; -enyewe. *in this ~ place,* hapa hasa. *The ~ thing I wanted,* kitu chenyewe hasa nilichotaka.
**vessel** /'vesl/ *n.* chombo. *blood ~,* mshipa wa damu.
**vest** /vest/ *n.* fulana; kizibao. **vestment** *n.* vazi; vazi la kasisi.
**vestry** /'vestri/ *n.* chumba cha kuvalia nguo kanisani; baraza la waumini.
**vet** /vet/ *n.* *(colloq.)* mganga wa mifugo. *v.t.* (**-tt**) *(colloq.)* pima afya; chunguza kwa makini.
**veteran** /'vetərən/ *n./adj.* mkongwe; mstaafu.
**veterinary** /'vɛt(ə)rɪn(ə)ri/ *adj.* -a kuhusu elimu ya maradhi ya wanyama. *a ~ surgeon,* daktari wa wanyama.
**veto** /'viːtəʊ/ *n.* (**-es** ) kura ya turufu. *v.t.* kataza; zuia.
**vex** /veks/ *v.t.* chokoza; taabisha; udhi. *a ~ed question,* suala lenye kuleta mabishano mengi. **~ation** *n.* uchokozi; maudhi. **~atious** *adj.* -chokozi; -a kuudhi; -sumbufu.
**via** /'vaɪə/ *prep.* kwa njia ya; kupitia.
**viable** /'vʌəb(ə)l/ *adj.* -a kukimu; -enye uwezo wa kumea, kuzaliwa na kuendelea kuishi.
**viaduct** /'vaɪədʌkt/ *n.* daraja refu livukalo bonde au korongo.
**vibrate** /vaɪ'breɪt/ *v.i./t.* tikisika; tikisa; yumbayumba; tetemeka. **vibration** *n.* mtikisiko; mtetemo. **vibrator** *n.* kitingishi.
**vicar** /'vɪkə(r)/ *n.* kasisi wa usharika. **~age** *n.* nyumba ya kasisi.
**vice**[1] /vʌɪs/ *n.* uovu.
**vice**[2] /vʌɪs/ *n.* jiliwa ya seremala
**vice-**[3] /'vʌɪs/ *prefix* -dogo; naibu; makamo. **~-admiral**, makamo wa admirali. **~-chairman**, makamu mwenyekiti. **~ premier**, naibu waziri mkuu. **~-president**, makamu wa rais. **~roy** *n.* kaimu wa mfalme. **~regal** *adj.* -a makamu mfalme.
**vicious** /'vɪʃəs/ *adj.* -ovu.
**vice versa** /ˌvʌɪs 'vəːsə/ *adv.* kinyume chake. *I hate him and ~,* namchukia naye anichukia.
**vicinity** /və'sɪnəti/ *n.* ujirani; kuwa karibu.
**victim** /vɪktɪm/ *n.* mhanga; kafara; mwathiriwa na jambo baya. *He is the ~ of the tradesman's greed,* anaathirika kwa choyo cha mchuuzi. **~ize** *v.t.* onea; sumbua.
**victor** /'vɪktə(r)/ *n.* mshindi. **~y** *n.* ushindi. **~ious** *adj.* -lioshinda; -liofaulu; -a shangwe.
**video** /'vɪdiəʊ/ *n.* video: chombo cha kunasia picha na sauti hai. **~ cassette**, kaseti ya video. **~ tape**, ukanda wa video.
**vie** /vʌɪ/ *v.i.* *~ with,* shindana na.
**view** /vjuː/ *n.* **1.** upeo wa macho; kuangalia; kutazama. *be in ~, come into ~,* onekana. *on ~,* -nayoonyeshwa wazi. **2.** sura; mandhari. *a house with a ~,* nyumba iliyojengwa penye mandhari nzuri. **3.** maoni; shauri; rai. *in ~ of,* kwa kuzingatia. **4.** nia; kusudio. *fall in with sb.'s ~s,* kubaliana na. *with a ~ to,* ili; kwa nia ya. *I came with a ~ to seeing him,* nilikuja ili nimwone. *I came with a ~ to settling down,* nilikuja kwa nia ya makazi. *v.t.* tazama; angalia; kagua.
**vigil** /'vɪdʒil/ *n.* kesha; ukeshaji. **~ance** *n.* kuwa macho; uangalifu; hadhari. **~ant** *adj.* macho; -angalifu; -enye hadhari.
**vigour** /vɪgə(r)/ *n.* nguvu; bidii; juhudi. **vigorous** *adj.* hodari; -a nguvu; a juhudi.
**vile** /vaɪl/ *adj.* -ovu; -potovu; -baya sana.
**vilify** /'vɪlɪfaɪ/ *v.t* singizia; kashifu; sengenya; tukana.
**villa** /'vɪlə/ *n.* nyumba (ya shamba) yenye bustani kubwa.
**village** /'vɪlɪdʒ/ *n.* kijiji; kitongoji. **~r** *n.* mwanakijiji.
**villain** /'vɪlən/ *n.* mwovu; mhalifu.
**villus**, **villi** /'vɪləs/ *n.* vidoleutumbo: namna ya vijidole katika tabaka ya ndani ya utumbo mdogo.
**vindicate** /'vɪndɪkeɪt/ *v.t.* thibitisha.

**vindication** *n.* uthibisho.




**villi | vili**

**vindictive** /vɪn'dɪktɪv/ *adj.* -a kutaka kulipiza kisasi; -siosamehe.

**vine** /vaɪn/ *n.* mzabibu. **~-dresser** *n.* mkulima wa mizabibu. **~yard** *n.* shamba la mizabibu.

**vinegar** /'vɪnɪgə(r)/ *n.* siki.

**violate** /'vaɪəleɪt/ *v.t.* vunja kiapo, mapatano, etc.; ingilia bila heshima; baka. **violation** *n.* ukiukaji.

**violent** /vaɪələnt/ *adj.* -a nguvu nyingi; kali sana. **violence** *n.* nguvu; jeuri; vurugu.

**violet** /'vaɪələt/ *n.* urujuani. *adj.* -a rangi ya urujuani.

**violin** /ˌvaɪə'lɪn/ *n.* fidla. **~ist** *n.* mpiga fidla.



**violin**

**virgin** /'vɜ:dʒɪn/ *n.* bikira; mwanamwali. *adj.* safi; siyoguswa; -a asili: ~ *forest*. msitu usiopata kuguswa. **~al** *adj.* -a bikira; -a mwanamwali; safi. **~ity** *n.* ubikira.

**virile** /'vɪraɪl/ *adj.* -a kidume; -enye nguvu za kiume. **virility** *n.* nguvu za uume za uzazi.

**virtual** /'və:tjʊəl/ *adj.* a kweli lakini si bayana. *He is the ~ head*, yeye ndiye kiongozi (ingawa si wa dhahiri). **~ image**, taswira bandia: taswira inayotokana na mkutano wa miali ya kweli ambayo haiwezi kutupwa kwenye kiwambo. **~ly** *adv.* kwa kweli; ilivyo.

**virtue** /'və:tju:/ *n.* wema; maadili; ubora. *by (in) ~ of*, kwa sababu; kwa ajili ya. **virtuous** *adj.* -ema; -adilifu; (kwa wanawake) safi; lio bora.

**virus** /'vʌɪrəs/ *n.* kirusi: kijiumbe hai ambacho hakijafikia ngazi ya seli ambacho huweza kuzaana kinapo-ishi kwenye kiumbe hai kingine, kwa kawaida husababisha maradhi.




**virus | kirusi**

**visa** /'vi:zə/ *n.* viza. *v.t.* -pa viza.

**viscosity** /vɪ'skɒsɪti/ *n.* mnato: mwelekeo wa mmiminiko wenye kunata au kumwagika taratibu sana.

**visible** /'vɪzəbl/ *adj.* -a kuonekana wazi. **~ spectrum**, spektra bayana: spektra yenye kuweza kuonekana na jicho. **visibility** *n.* hali ya kuonekana wazi. *Visibility is bad today*, mwangaza hautoshi leo.

**vision** /'vɪʒn/ *n.* uwezo wa kuona au kuwaza; busara; njozi; ndoto. **~ary** *adj.* -a kubuni tu; -a ndoto; -enye njozi. **visual display unit** *(VDU)*, chombo chenye kiwambo ambacho huonyesha taarifa, hasa kutoka kwenye kompyuta.

**visit** /'vɪzɪt/ *n.* matembezi; ziara. *state ~*, ziara ya kiserikali. *v.t./i.* zuru; tembelea. **~ation** *n.* rada: adhabu ya Mungu; patilizo. **~or** *n.* mgeni. *state ~*, mgeni wa kiserikali.

**vista** /'vɪstə/ *n.* mandhari; taswira. *(fig.)* mfululizo wa taswira katika mawazo.

**visual** /'vɪʒjʊəl/ *adj.* -a kuona; -a macho. *~ aid*, vielelezo. **~ize** *v.t.* pata taswira akilini; pata sura.

**vital** /'vaɪtl/ *adj.* -uhai; -a lazima kwa uzima; muhimu sana. **~ly** *adv.* kwa ulazima. **~ity** *n.* uhai; uzima; uchangamfu. **~ize** *v.t.* tia uzima; tia nguvu.

**vitamin** /'vɪtəmɪn/ *n.* vitamini. **~ A**, vitamini A: msombo oganiki ambao hauwezi kutengenezwa na wanyama na ulio muhimu sana kwa nuru ya macho. **~ B complex**, vitamini B changamano: msombo oganiki ambao ni muhimu sana kwenye utendanaji katika mwili. **~ C**, vitamini C: msombo oganiki ambao binadamu hawezi kutengeneza ulio muhimu sana kwa seli na tishu za mwili. **~ D**,

vitamini D: msombo oganiki ulio lazima kwa ukuaji wa mifupa ya mnyama. **~ E**, vitamini E: msombo oganiki upatikanao katika nafaka na ni muhimu kwa uzaanaji wa wanyama. **~ K**, vitamini K: msombo oganiki unaopatikana katika mbogamboga na mayai na ulio lazima katika ugandishaji wa damu.
**vitiate** /'vɪʃɪeɪt/ *v.t.* haribu ; punguza nguvu; dhoofisha.
**vivacious** /vɪveɪʃəs/ *adj.* -changamfu; -a furaha; -cheshi; -enye bashasha. **vivacity** *n.* uchangamfu; ukunjufu; ucheshi; bashasha.
**vivid** /'vɪvɪd/ *adj.* (kwa rangi) ng'avu; (kwa maelezo) dhahiri; wazi. **~ly** *adv.* waziwazi.
**viviparous** /vɪ'vɪp(ə)rəs/ *adj.* -a kuzaa watoto, si mayai.
**viz** /vɪz/ *adv.* (husomeka *namely*) yaani; ndio kusema.
**vocabulary** /və'kæbjələri/ *n.* msamiati; maneno.
**vocal** /'vəʊkl/ *adj.* -a sauti. **~ chords**, vinyuzi sauti: mikunjo ya ngozi katika shingo karibu na koo za baadhi ya wanyama ambayo husaidia katika kutoa sauti. **~ organs**, ala za sauti. **~ic** *adj.* -a vokali; -a irabu. **~ism** *n.* mfumo wa irabu. **~ist** *n.* mwimbaji.
**vocation** /və(ʊ)'keɪʃ(ə)n/ *n.* **1.** wito. **2.** kazi; shughuli; utaalamu; amali; ufundi. **3.** uwezo; welekevu; moyo. **~al** *adj.* -a kazi; -a ufundi. **~ guidance**, ushauri wa kuchagua kazi.
**vodka** /'vɒdkə/ *n.* vodka: aina ya pombe kali ya Kirusi.
**vogue** /vəʊg/ *n.* mtindo; fashini. *be in ~*, -wa katika fashini.
**voice** /vɔɪs/ *n.* sauti; *(gram.)* kauli ya kutenda au kutendwa au kutendewa. *v.t.* sema; eleza; tamka.
**void** /vɔɪd/ *n.* uwazi; upweke. *adj.* tupu; wazi; pasipo mtu. *~ of*, bila; -siokuwa na. *(law) null and ~*, batili.
**volatile** /'vɒlətʌɪl/ *adj.* fukivu, fushi: -a kugeuka mvuke; (kwa mtu) -epesi kubadilika; -changamfu.
**volcano** /vɒl'keɪnəʊ/ *n.* (**-es**) volkano. **volcanic** *adj.* -a volkano. **volcanic rock**, jabali volkano: mwamba uliofanyika kwa kupoa dutu iliyoyeyuka kutoka kwenye volkano.


volcano

**volley** /'vɒli/ *n.* mshindo wa silaha nyingi za moto zikipigwa pamoja; mfululizo wa matukio. *a ~ of abuse*, mfululizo wa matusi.
**volt** /vəʊlt/ *n.* volti: kizio cha nguvu za umeme. **~age** *n.* volteji: kani mwendoumeme ikipimwa katika volti. **~meter** *n.* voltimeta: chombo cha kupimia volteji ya umeme katika vipimo vya volti.
**volume** /'vɒlju:m/ *n.* **1.** juzuu. **2.** ukubwa; wingi. **3.** nafasi; ujazo. **4.** nguvu ya sauti. **voluminous** *adj.* -kubwa; (kwa mwandishi) -enye kuandika kazi nyingi.
**voluntary** /'vɒləntri/ *adj.* -a hiari; -a kujitolea. **~ helpers**, wasaidizi wa kujitolea. **voluntarily** *adv.* kwa hiari.
**volunteer** /ˌvɒlən'tɪə(r)/ *n.* valantia: askari wa kujitolea; mtu ajitoleaye. *v.t./i.* toa kwa hiari; jitolea.
**vomit** /'vɒmɪt/ *n.* matapishi; matapiko. *v.t./i.* tapika.
**vote** /vəʊt/ *n.* kura; kasma ya matumizi ya fedha. *v.i./t.* piga kura; chagua. **~r** *n.* mpiga kura.
**vouch** /vɑʊtʃ/ *v.i.* *~ for (sb. or sth.)* dhamini; chukua dhima ya. **~er** *n.* vocha; hati ya malipo.
**vow** /vaʊ/ *n.* nadhiri; kiapo. *v.t.* weka nadhiri.
**vowel** /'vaʊəl/ *n.* irabu; vokali. *back ~*, irabu nyuma. *front ~*, irabu mbele.
**voyage** /'vɔɪɪdʒ/ *n./v.i.* safari; safiri.
**vulcanization** *n.* uvulkanishi: mchakato wa kuufanya mpira asilia uwe mgumu zaidi kwa kuukanza na salfa.
**vulgar** /'vʌlgə(r)/ *adj.* -sio na adabu. **~ity** *n.* ukosefu wa adabu; usafihi.
**vulnerable** /'vʌlnərəbl/ *adj.* -enye kuweza kudhuriwa.
**vulture** /vʌltʃə(r)/ *n.* tai.
**vulva** /'vʌlvə/ *n.* njini.

# Ww

**wad** /wɒd/ *n.* fusho: kitu chochote laini cha kutenganishia vitu ili visitikisike na kugongana: kibunda cha noti.
**waddle** /ˈwɒdl/ *n.* mwendo wa bata. *v.i.* tagaa; enda kama bata.
**wade** /wəɪd/ *v.i.* enda kwa shida majini, matopeni au mchangani. **wading bird** *n.* ndege atembeaye majini. ~ *in,* shambulia kwa nguvu. **~rs** *n.* gambuti: viatu virefu vinavyofika magotini.
**wadi** /ˈwɑːdi/ *n.* bondejangwa: bonde kame ambalo hupitiwa na mto katikati yake wakati wa majira ya mvua.
**waft** /wɒft/ *v.t.* peperusha.
**wag** /wæg/ *n.* mtikisiko. *v.t./i.* (**-gg-**) tikisa. ~ *one's finger at sb.,* onyesha kidole.
**wage**[1] /weɪdʒ/ *n.* mshahara; ujira. **minimum ~,** kima cha chini cha mshahara.
**wage**[2] /weɪdʒ/ *v.t.* pigana; fanya vita.
**waggon** /ˈwægən/ *n.* mkokoteni; gari la kukokotwa na farasi au ng'ombe.
**waif** /weɪf/ *n.* msokwao (hasa mtoto). *~s and strays,* watoto wa mitaani.
**wail** /weɪl/ *n.* maombolezo. *v.i.* omboleza: lia kwa huzuni.
**waist** /weɪst/ *n.* kiuno. **~cloth** *n.* kikoi; shuka. **~coat** *n.* kizibao.
**wait** /weɪt/ *n.* ungojeaji; muda wa kungojea. *v.i./t.* ngoja; ngojea; subiri. ~ *upon sb.,* ngojea; tumikia. *lie in ~ for,* vizia. ~ *on sb. hand and foot,* kidhia haja zote. **~ing list,** orodha ya wanaosubiri. **~ing room,** chumba cha wanaosubiri. **~er, ~ress** *n.* mhudumu.
**waive** /weɪv/ *v.t.* samehe (deni, etc.).
**wake** /weɪk/ *v.i./t.* (**woke, ~d, woken**) amka; amsha. **~ful** *adj.* macho; -a kukesha. **~n** *v.t./i.* amsha; amka. *in the ~ of,* baada ya. *follow in sb.'s ~,* fuata nyayo za mtu.
**walk** /wɔːk/ *n.* matembezi; namna ya kutembea; njia. ~ *of life,* weledi; kazi katika maisha. *v.i./t.* enda kwa miguu; tembea. ~ *off with,* iba. ~ *away with,* shinda bila taabu. **~over** *n.* *(colloq.)* ushindi rahisi.
**wall** /wɔːl/ *n.* ukuta; kiambaza. *with one's back to the ~,* kwa kubanwa sana; kwa kuzingirwa. *go to the ~,* shindwa kabisa. **~paper,** karatasi za kupambia ukutani. *v.t.* ~ *up,* zungushia ukuta.


walls

**wallet** /ˈwɒlɪt/ *n.* pochi.
**wander** /ˈwɒndə(r)/ *n.* zurura; zunguka. **~er** *n.* mzururaji.
**wane** /weɪn/ *v.i.* pungua; fifia; legea.
**want** wɒnt/ *v.t.* taka; hitaji; tamani. *be ~ ing,* pungukiwa na. *a few pages of this book a ~ing,* kurasa nyingine za kitabu hiki zimepungua. *He is ~ing in courtesy,* hana adabu. ~ *for nothing,* jitosheleza kwa kila kitu. **~ing** *prep.* bila.
**war** /wɔː(r)/ *n.* vita. *You have been in the ~s, (colloq.)* umeumizwa vitani. *at ~,* katika hali ya vita. **~head,** kichwa cha kombora. **~rior** *n.* askari mpiganaji. **~y** *adj.* mgomvi.
**ward** /wɔːd/ *n.* **1.** mtoto wa kulea. **2.** *keep watch and ~,* linda; hifadhi. **3.** kata: mtaa wa mji. **4.** wadi. *v.t.* ~ *off,* kinga; epusha; kwepa. **~en** *n.* msimamizi; mwangalizi. **~er, ~ress** *n.* askari magereza wa kiume, wa kike.
**wardrobe** /ˈwɔːdrəʊb/ *n.* chumba au kabati la kuwekea nguo.
**warehouse** /ˈwɛːhaʊz/ *n.* ghala; bohari.
**warm** /wɔːm/ *adj.* -a uvuguvugu. *make things ~ for sb.,* adhibu fulani; letea matatizo. *v.t./i.* ~ *up,* pasha; pata moto. **~-blooded** *adj.* -a damu moto. **~-hearted** *adj.* -ema; -kunjufu. **~ly** *adv.* kwa moyo mkunjufu. **~th** *n.* joto; *(fig)* hasira; shauku.
**warn** /wɔːn/ *v.t.* onya; hadharisha; asa. **~ing** *n.* onyo.

**warrant** /'wɒrənt/ *n.* **1.** haki; sababu. **2.** kibali; waranti.
**wash** /wɒʃ/ *n.* josho; uoshaji. *v.t./i.* **1.** osha; oga; fua nguo; safisha kwa maji; nawa. **2.** fulika bila kuharibika. **3.** (kwa bahari, mto, etc.) pita. **~er** *n.* mashine ya kufulia nguo. **~erman** *n.* dobi. **~out** *n.* sehemu iliyobomolewa na mafu-riko.
**wasp** /wɒsp/ *n.* zinengo; nyigu; uvi. **~-waisted**, -enye kiuno chemba-mba.
**waste** /weɪst/ *n.* ufujaji; takataka; jangwa. *adj.* **1.** - siofaa; a jangwa. **2.** -a takataka; -ovyo. *v.t./t.* **1.** tumia vibaya; fuja. **2.** dhoofisha; dhoofika; lika; chakaa. **~ product**, uchafu; mabaki; takataka.
**wastage** /'weɪstɪdʒ/ *n.* hasara; uharibifu; takataka. **~ful** *adj.* -potevu; -fujaji; -haribifu. **~r** *n.* mfujaji; mharibifu.
**watch** /wɒtʃ/ *n.* ulinzi; lindo. *v.t./i.* **1.** tazama; angalia; chunga; linda. *~ over,* tunza; linda; kesha. *keep ~,* kuwa zamuni. **2.** saa ya mfukoni au mkononi. **~ful** *adj.* -a hadhari. **~man** *n.* mlinzi.
**water** /'wɔ:tə(r)/ *n.* maji. *fresh ~,* maji matamu. *salt ~,* maji chumvi. *under ~,* -liojaa maji. *get into (be in) hot ~,* pata matatizo. *throw cold ~ on,* pinga. *hold ~,* thibitika inapo jaribiwa. *high and low ~,* maji kujaa na kupwa. *(fig.) be in low ~,* kuwa maskini. *v.t./i.* mwagilia maji. *my eyes ~,* machozi yanitoka. *my mouth ~s,* natoka mate. *(fig.) ~ sth. down,* zimua. **~closet** *n.* (au *w.c.*) choo cha kuvuta. **~ cycle**, mzunguko maji: mzunguko wa daima wa maji katika hali ya uoevu au mvuke angani, ardhini na baharini. **~fall** *n.* maporomoko ya maji. **~proof** *n. /adj.* -siopenya maji. **~shed** *n.* eneo la mwinuko ligawalo mito. **~spout** *n.* chamchela ya maji ya bahari. **~ table**, wenzomaji: sehemu ambayo iko katika usawa wa maji yaliyoko ardhini ambayo wakati wa mvua hupanda juu zaidi na kuwa chanzo cha mtiririko wa mito au maji ya madimbwi. **~tight** *adj.* -siovuja maji. **~ vapour**, mvuke maji: maji katika hali yake ya kigesi au ya kimvuke. **~works** *n.* mfumo wa usambazaji maji.
**watt** /wɒt/ *n.* wati: kipimo cha umeme.
**wattle** /'wɒt(e)l/ *n.* ufito. *~ and doub hut,* kibanda cha fito kilicho-kandikwa; nyumba ya mbavu za mbwa.
**wave** /weɪv/ *n.* wimbi; ongezeko. *v.i./t.* punga; tikisa; tikisika. **~length** *n.* masafa; urefu wa wimbi. **waver** *v.i.* sitasita; yumbayumba; pepe-suka.
**wax**[1] /wæks/ *n.* nta. **~-chandler** *n.* mtengenezaji au muuzaji mishumaa.
**wax**[2] /wæks/ *v.i.***1.** (hasa kwa uso wa mwezi) kua. *~ and wane,* kuzidi na kupungua.
**way** /weɪ/ *n.* **1.** njia; barabara. **2.** upande; welekeo. *Look this ~,* tazama upande huu. *the wrong ~ round,* kuelekea upande sio. **3.** mwendo; masafa. *We're a long ~ from home,* tuko mbali na nyumbani. **4.** njia; mbinu; mkakati. *the ~ to do it,* njia ya kufanya. *Do it in this ~,* ifanye namna hii. *~s and means,* mbinu; njia. **5.** desturi; mazoea; utaratibu. **6.** namna. *They're in no ~s similar,* hawafanani hata kidogo. *He's clever in some ~s,* ni hodari kwa mambo mengine. *You're in my ~,* unanizuia. *Get out of the ~,* ondoka njiani; kujitenga. *by the ~,* pamoja na hayo. *by ~ of introduction,* kwa kutambulisha. *by ~ of bussiness,* kwa njia ya biashara. *in a ~,* kwa njia moja. *in a bad ~,* katika hali mbaya. *have (get) your own ~,* fanya upendavyo. *give ~,* shindwa. **~farer** *n.* msafiri kwa miguu. **~side** *n./adj.* (-a) kando ya njia.
**wayward** /'weɪwəd/ *adj.* -kaidi.
**weak** /wi:k/ *adj* **1.** dhaifu; -sio na nguvu. **2.** enye maji mengi; si -kali; -epesi. **3.** (kwa maarifa) -pungufu; chini ya kiwango cha kawaida. *I have ~ sight,* sioni vyema. *~ acid,*

asidi dhaifu: asidi kama vile asidi aseti ambayo sehemu yake huvunjika rejea katika mmumunyo. **~en** *v.t./i.* dhoofisha; dhoofika. **~-kneed** *adj (fig)* -enye moyo dhaifu; -nyonge. **~-minded** *adj.* -enye akili chache. **~ness** *n.* **1.** udhaifu. **2.** ila. **3.** kutojiweza. *have a ~ness for,* penda sana.

**wealth** /welθ/ *n.* utajiri; ukwasi. **~y** *adj.* tajiri.

**wean** /wi:n/ *v.t.* achisha mtoto maziwa ya mama.

**weapon** /wepən/ *n.* silaha.

**wear** /weə(r)/ *n.* kuvaa; vazi; uchakavu. *v.t./i.* (**wore**, **worn**) **1.** vaa; valia. **2.** dumu; stahamili. **3.** chakaa; chakaza. *~ off,* pita; -isha; pungua. *~ on,* (kwa wakati) pita polepole; potea. *~ out,* chakaa; lika; chakaza. *I'm worn out,* nimechoka kabisa. **~y** *adj.* -liochoka; -a kushosha. **~ily** *adv.* kwa hali ya kuchoka. **~iness** *n.* kuchoka; uchovu. **~isome** *adj.* -a kuchosha; -sumbufu.

**weather** /'weðə(r)/ *n.* hali ya hewa. *What sort of ~?* umekuwaje? *v.i./t.* **1.** pona; pita; epuka. **2.** nyauka. **~-beaten** *adj.* -lioathiriwa na hali ya hewa. **~cock**, **~vane** *n.* umbo la jogoo au mshale juu ya jengo kuonyesha welekeo wa upepo.

**weave** /wi:v/ *n.* mtindo wa ufumaji. *v.t.* (**wove**,**woven**) fuma; suka; *(fig.)* tunga; buni; sanifu. **~r** *n.* mfumaji. **~bird** *n.* ndege mnana.

**web** /web/ *n.* **1.** kilichofumwa; mfumo. *(fig.) a ~ of lies,* utungo wa uwongo. **2.** utando (wa buibui). **3.** utando wa ngozi kati ya vidole. **~bing** *n.* utepe wa nguo. **website** *n.* kurasa pembuzi; tovuti.

**wed** /wed/ *v.t./i.* (**~ded**) oa; olewa; funga ndoa. **~lock** *n.* ndoa. **wedding** /wedɪn/ *n.* harusi; ndoa. **~breakfast** *n.* chakula cha maharusi. **~ card** *n.* kadi ya mwaliko wa harusi.

**wedge** /wedʒ/ *n.* kabari. *the thin end of the ~,* jambo dogo linalozua jambo kubwa. *v.t.* kaza kwa kabari.

**Wednesday** /'wenzdeɪ/ *n.* Jumatano.

**weed** /wɪ:d/ *n.* gugu; majani. *~ killer,* kiua magugu. *v.t./i.* palia magugu. *~ out,* ondoa vitu hafifu visivyofaa kitu. **~y** *adj.* -enye magugu; embamba tena dhaifu. *~ young men,* vijana wembamba wadhaifu.

**week** /wi:k/ *n.* wiki; juma. **~day** *n.* siku yoyote ya wiki isipokuwa Jumamosi au Jumapili. **~end** *n.* wikiendi; Jumamosi na Jumapili. **~ly** *adj./adv.* kwa juma. *n.* gazeti litolewalo kila wiki.

**weep** /wi:p/ *v.i.* (**wept**) lia; toka machozi; omboleza.

**weigh** /weɪ/ *v.t./i.* **1.** pima uzito. **2.** -wa na uzito wa. **3.** pima umuhimu wa jambo. *~ (sth . or sb.) down,* chosha; lemeza; hangaisha. *(fig.) ~ upon,* lemea; sumbua. *~ anchor,* ng'oa nanga. **~t** *n.* uzito; jiwe la mizani; umaarufu; maana. *v.t.* tia uzito; lemeza. **~ty** *adj.* -zito; -a maana.

**weir** /wɪe(r)/ *n.* boma la kuzuia maji; kikinga mto; mgono: mtego wa samaki.

**welcome** /'welkəm/ *n.* mapokezi; makaribisho. *adj.* -a kupokewa kwa furaha; a- kufurahisha.*You are ~ to use my books,* nakuruhusu kutumia vitabu vyangu. *v.t.* karibisha vizuri; pokea kwa furaha. *I ~ your suggestion,* nakubali pendekezo lako kwa furaha.

**weld** /weld/ *v.t.* lehemu; lihimu. **~er** *n.* mtia weko.

**welfare** /'welfeə(r)/ *n.* hali njema; ustawi; neema; afya. **social ~**, ustawi wa jamii.

**well**[1] /wel/ *n.* kisima; chumba cha lifti au ngazi katika jengo. *v.i. ~ up,* bubujika; foka; chemka.

**well**[2] /wel/ *adj.* (**better**, **best** ) **1.** heri; afadhali; bora. *it would be ~ to,* afadhali. *~ and good,* vyema. *adv.* vyema; barabara; vizuri. *as ~ as,* pamoja na. *be ~ out of sth.,* jitoa katika jambo bila matatizo. **2.** haki. *You may ~ be suprised,* una haki ya kushangaa. *We may as ~ begin now,* tunaweza kuanza sasa hivi. *wish sb. ~,* takia mtu heri. *Let ~ alone,* usiingilie. *int.* je? nini tena?

**well**³ /wel/ *prefix* **~-being** *n.* hali njema; afya; raha; ustawi. **~-born** *n.* -a ukoo bora. **~connected** *adj.* -enye uhusiano na watu bora. **~-disposed** *adj.* -ema; -a hisani. **~-nigh** *adv.* karibu; nusura. **~-to-do** *adj.* tajiri. **~-worn** *adj.* -liotumika mno.

**wellingtons** *n.* viatu virefu vya mpira.

**wesleyan** *adj.* -a ufuasi wa madhehebu ya kikristo ya kiprotestanti yaliyoanzishwa na J. Wesley.

**west** /west/ *n./adj.* magharibi. **~erly** *adj./adv.* -a upande wa magharibi. **~ern** *adj.* -a magharibi. **~ward** *adv.* kuelekea upande wa magharibi.

**wet** /wet/ *adj.* majimaji; chapa-chapa. *v.t.* (**-tt-**) rowesha.

**whale** /weɪl/ *n.* nyangumi; aina ya mamalia mkubwa kuliko wote aishiye baharini.

**wharf** /wɔ:f/ *n.* (**~s**, **wharves**) gati. **~age** *n.* ushuru utozwao kwa matumizi ya gati. **~man** *n.* kuli. **~-master** *n.* msimamizi wa gati.

**what** /wɒt/ *pron/ adj./int.* nini; hata iweje; chochote; ipi; gani; kweli! *~ a wonderful thing*, kitu kizuri kilioje. **~ever** *pron./adj.* lolote; lingine. *No doubt ~*, hakuna shaka hata kidogo.

**wheat** /wi:t/ *n.* ngano. **~en** *adj.* -a ngano.

**wheel** /wi:l/ *n.* gurudumu; (katika meli) usukani. *~s within ~s*, mchanganyiko wa mambo. *put one's shoulder to the ~s*, saidia; jitahidi. *v.t./i.* sukuma, vuta kwa magurudumu. **~barrow** *n.* bero; toroli. **~wright** *n.* fundi wa magurudumu. **potter's ~** *n.* kurugo: gurudumu la kufinyangia vyungu.

**when** /wen/ *adv.* *(inter.)* lini? wakati gani? *(rel.)* -po- ambapo. *~ I went*, nilipokwenda. *~ I go*, niendapo. **~ever** *adv.* kila; wakati wowote. *~ I go*, kila nikienda, *~ he likes*, kila apendapo.

**where** /weə(r)/ *adv.* *(inter.)* wapi? mahali gani? *(rel.)* ambapo, -ko, -mo. *We must go ~ we can get food*, lazima twende ambako tutapata chakula. **~abouts** *adv.* wapi? karibu na wapi? sehemu gani? *n.* makazi. *I don't know his ~abouts at present*, sijui alipo sasa. **~as** *conj.* kwa maana ; kwa kuwa; lakini; wakati ambapo. **~fore** *adv.* (la zamani) kwa nini? *conj.* kwa sababu hii. **~upon** *adv.* hapo; ndipo; baadaye. **~ver** *adv.* kila; popote. *~ he likes*, popote apendapo. **~withal** *n.* *the ~withal*, uwezo; mali.

**whether** /'weðə(r)/ *conj.* kama. *~ you like or no*, ukipenda usipende.

**which** /wɪtʃ/ *adj./pron.* *(inter.)* -pi, gani. *(rel.)* amba (o, -ye, -yo, zo, etc). *the book ~ he has bought*, kitabu ambacho amenunua. *I like the things ~ I see*, navipenda vitu ninavyoviona. *that ~ I want to buy*, ambacho nitakachonunua. **~ever** *pron. /adj.* -o- -ote, ye yote, cho chote, etc.

**while** /waɪl/ *n.* wakati; muda. *-conj.* wakati. *~ he goes he sings*, aimba akienda. *once in a ~*, mara moja moja. *be worth ~*, faa. *v.t.* *~ away the time*, pitisha wakati.

**whine** /waɪn/ *n.* mlio wa mbwa anayeogopa; lalamiko. *v.i.* lia kama mbwa anayeogopa; lalamika.

**whip** /wɪp/ *n.* mjeledi; kiboko; mchapo. *have the ~ hand over sb.*, dhibiti; tawala. *v.t./i.* **1.** chapa piga mjeledi. **2.** piga mayai kwa mchapo. *~ out*, chomoa; toa ghafla. *He ~ped out a pistol*, alichomoa bastola. **~ping** *n.* adhabu ya kupigwa viboko.

**whirl** /wɜ:l/ *n.* mzunguko wa kasi. *v.t./i.* **1.** zungusha; zunguka kwa nguvu. **2.** ona kizunguzungu. *~ off*, twaa ghafla. **~pool** *n.* mzunguko wa maji. **~wind** *n.* kikuukuu; chamchela.

**whisk** /wɪsk/ *n.* **1.** brashi ya kupangusia nguo **2.** mchapo wa mayai; mpanguso. *v .t./i.* pangusa upesi; twaa upesi; punga mkia hewani.

**whisker** /'wɪskə(r)/ *n.* sharafa: ndevu za mashavuni; sharubu za paka.

**whisky** /'wɪski/ *n.* pombe kali; wiski.
**whisper** /'wɪspə(r)/ *n.* mnong'ono; uvumi. *v.i.* nong'ona.
**whistle** /'wɪspə(r)/ *n.* **1.** mluzi; ubinja. **2.** filimbi; kipenga. *v.i.* piga mbinja, kipenga. *v.t.* ~ *a tune*, imba kwa ubinja.
**white** /waɪt/ *n.* weupe; ute wa yai; mzungu. *adj.* -eupe. **~ blood cell** selidamu nyeupe: seli ya damu isiyo na maunzi ya rangi nyekundu, kazi yake kubwa ni kupigana na chembechembe za maradhi. ~ *dwarf*, ~ *lie*, uwongo usiodhuru. ~ *hair*, mvi.




**white cell | seli nyeupe ya damu**

**whitsun** /'wɪts(ə)n/ *n.* sikukuu ya Pentekoste. **~tide** *n.* juma lianzalo na sikukuu hiyo.
**whittle** /'wɪtl/ *v.t./i.* chonga; kata vipande vyembamba. *(fig.)* punguza kidogokidogo.
**who** /hu:/ *pron.* (**whom whose**) *(inter.)* nani? *(rel.)* amba (-o-, -ye-). *The man ~ came was very tall*, mtu aliyekuja alikuwa mrefu sana. *the men ~ I saw* , watu niliowaona. *the man ~se book I am reading*, mtu ambaye kitabu chake ninakisoma. **~ever** *pron.* yeyote; -o- ote.
**whole** /həʊl/ *n.* kitu kizima; jumla. *adj.* **1.** ote. *the ~ truth*, kweli yote. *He devoted his ~ energies to his task*, alitumia nguvu zake zote katika kazi yake. **2.** -zima. *He ascaped ~*, aliokoka bila ya kudhurika. *There's not a ~ plate in the house*, hamna sahani nzima nyumbani. **3.** -zima; kamili. *Rain fell for three ~ days*, mvua ilinyesha siku tatu nzima. *a ~ number*, namba nzima. *on the ~*, kwa jumla; kwa kuzingatia yote. **~hearted (ly)** *adj./adv.* kamili; -zima; kwa moyo mkunjufu. **~sale** *n.* jumla. **~some** *adj.* -enye lishe kamili.
**wholly** /'heʊlli/ *adv.* kabisa.
**why** /waɪ/ *adv.* kwa nini? kwa sababu gani? *the ~s and the wherefores*, kisa na mkasa.
**wick** /wɪk/ *n.* utambi; ujali wa taa.
**wicked** /'wɪkɪd/ *adj.* -ovu; -baya; habithi. **~ly** *adv.* kwa uovu. **~ness** *n.* uovu.
**wicker** /'wɪkə(r)/ *n.* fito (henzerani, tete) zilizosukwa.
**wicket** /wɪkɪt/ *n.* **1.** (vilevile **~-door**, **~gate**) kilango; kidirisha cha kuuzia tiketi. **2.** (katika mchezo wa kriketi) vijiti vitatu vilindwavyo na mshika beti. *take a ~*, shinda mshika beti.
**wide** /waɪd/ *adj.* **1.** -pana. **2.** -a kutapakaa; -ingi. *a man · with knowledge*, mtu mwenye maarifa katika nyanja nyingi. **3.** -a kukosa shabaha. *adv.* **1.** sana; kwa kiasi kikubwa. *search far and ~*, tafuta kila mahali. **2.** kabisa. *~ open* wazi kabisa. *~ awake*, macho kabisa. *~ apart*, -liotengana kabisa. *~ of*, mbali na shabaha. *The arrow fell ~ of the mark*, mshale ulikosa shabaha. **~n** *v.t./i.* tanua; tanuka; nanuka; eneza. **~spread** *adj.* -liotapakaa. **~ly** *adv.* sana; kwa kiasi kikubwa.
**width** /wɪtθ, wɪdθ/ *n.* upana.
**widow** /'wɪdəʊ/ *n.* mfiwa na mume; kizuka. **~er** *n.* mfiwa na mke; mjane.
**wield** /wi:ld/ *v.t.* shika na kutumia. *(fig.) ~ power*, shika madaraka.
**wife** /waɪf/ *n.* (**wives**) mke.
**wig** /wɪg/ *n.* wigi: nywele bandia.
**wild** /waɪld/ *adj.* **1.** (kwa wanyama) -a mwitu; -siofugwa; (kwa mimea) -a porini; -a kujiotea yenyewe. **2.** (kwa mahali) -a jangwa; -siokaliwa na watu. **3.** -a nguvu; -a tufani. ~

*with anger,* -liokasirika sana. **4.** bila kuangalia wala kufikiri. *(colloq.) be ~ about,* -wa na shauku kwa. *the ~s,* mwitu; nyika; pori. **~ly** *adv.* bila mpango; ovyoovyo. **~ness** *n.* hali ya kuwa -a pori. **~fire** *n.* moto wa nyika. *spread like ~,* enea upesi mno. **wilderness** *n.* jangwa; nyika; pori.

**will**[1] /wɪl/ *v.* (**would**) -ta-; tafadhali. *He ~ come,* atakuja. *~ you do me a favour?* tafadhali nifanyie hisani.

**will**[2] /wɪl/ *v.t.* (**~ed**) taka. *Let him do what he ~,* mwache afanye kama atakavyo. *would that,* laiti. *~ed to,* usia. *He ~ ed a house to him,* alimwandikia nyumba katika wosia.

**will**[3] /wɪl/ *n.* hiari; ridhaa. *free ~,* hiyari; akili. *He always has his ~,* daima ana hiari yake. *bear sb. good ~,* takia mtu heri. *last ~ and testament,* wosia. **~ing** *adj.* radhi; tayari. **~ly** *adv.* kwa hiari. **~ness** *n.* hiari; ridhaa.

**win** /wɪn/ *v.t.* (**won**) shinda; faulu. **~ner** *n.* mshindi.

**winch** /wɪntʃ/ *n.* winchi.

**wind**[1] /wɪnd/ *n.* **1.** upepo. *be in the ~,* eleweka baada ya kufichwa. *See how the ~ blows,* sikiliza maoni ya watu kuhusu jambo. *take the ~ out of sb.'s sails,* wahi mtu; katiza maslahi yake ghafla. **2.** pumzi. **3.** harufu; fununu. *get ~ of, (fig.)* sikia habari za. **4.** riahi; rihi; gesi ya tumboni; shuzi. **5.** upuuzi. *v.t.* **1.** kosesha pumzi. **2.** pumzisha. **3.** nukiliza: gundua kitu kwa harufu. **~mill** *n.* kinu cha upepo. **~pipe** *n.* koromeo. **~screen** *n.* kioo cha mbele cha gari. **~ward** *adj.* -a upande wa upepo.



**windmill**

**wind**[2] /wʌɪnd/ *v.i./t.* (**wound**) **1.** pindika; zunguka; zungusha. **2.** kunja; sokota. *~ up,* maliza; komesha; kamilisha. *ball wound up,* hangaika sana. **~ing-sheet** *n.* sanda.

**windlass** /'wɪndləs/ *n.* winchi.

**window** /'wɪndəʊ/ *n.* dirisha. *~ box,* sanduku la kuoteshea maua dirishani. **~ display**, maonyesho ya biashara dirishani. *~ envelop,* bahasha yenye kidirisha. *~ seat,* kiti cha dirishani. **~ shopping**, tia macho nuru; kutazama vitu dukani bila ya kununua.

**wine** /waɪn/ *n.* mvinyo; divai. *new ~ in old bottles,* mambo mapya yasiyoweza kuzuilika. *~ grower,* mlimaji zabibu za kutengenezea divai. *palm ~,* tembo la mnazi. **~ry** *n.* kiwanda cha mvinyo.

**wing** /wɪŋ/ *n.* **1.** bawa; ubawa. *be on the ~,* ruka; puruka. *under sb.'s ~,* chini ya himaya ya mtu. **2.** sehemu ya nyumba. **3.** (katika kandanda) wingi; mchezaji wa pembeni.

**winter** /'wɪntə(r)/ *n.* majira ya baridi kali; kipupwe. *v.i.* kaa majira ya baridi.

**wintry** /'wɪntri/ *adj.* -a baridi kali.

**wipe** /waɪp/ *v.t.* **1.** safisha kwa kufuta; pangusa; futa. **2.** *~ off,* futa. *~ out,* futa; *(fig.)* haribu kabisa. *~ up,* kausha maji kwa kupangusa.

**wire** /'waɪə(r)/ *n.* **1.** waya. **2.** *(colloq.)* simu ya upepo. *v.t./i.* **1.** funga kwa waya. **2.** funga nyaya za umeme. **3.** piga simu. **wiry** *adj.* -embamba na shupavu

**wise** /waɪz/ *adj.* -a hekima. **~ly** *adv.* kwa busara.

**wisdom** /'wɪzdəm/ *n.* **1.** hekima; busara. **2.** methali; semi; maadili.

**wish** /wɪʃ/ *n.* matamanio; matakwa; mapenzi. *v.t./i.* **1.** tamani **2.** taka. **3.** penda. *~ sb. a pleasant journey,* takia safari njema. **~ful** *adj.* tamanifu. *~ful thinking,* ndoto za mchana.

**wit** /wɪt/ *n.* **1.** akili. **2.** mwerevu. **~ticism** *n.* usemi wa hekima. **~ty** *adj.* -cheshi. **~tily** *adv.* kwa ucheshi.

**witch** /wɪtʃ/ *n.* mchawi mwanamke. **~craft** *n.* uchawi. **~-doctor** *n.* mchawi; mganga. **~ery** *n.* uchawi; uzuri wa kuzuga akili.

**with** /wɪð/ *prep.* na; kwa. *He went ~ his father,* alikwenda na baba yake. *Cut it ~ a knife,* ikate kwa kisu. *He was beaten ~ stick,* alipigwa kwa fimbo. *together ~,* pamoja na. *fall*

*out ~*, gombana na. **withdraw** *v.t./i.* (**withdrew**, **withdrown**) **1.** rudisha nyuma; rudi nyuma. **2.** ondoa; toa. **3.** tangua; futa. **~al** *n.* kuondoka; kufuta; kuondoa; kuchukua.

**wither** /'wɪə(r)/ *v.i./t.* **1.** -fa; dhoofu; fifisha; nyausha; nyauka. **2.** fadhaisha. *She gave him ~ing glance*, alimtupia jicho la kufadhaisha.

**withhold** /wɪð'həʊld/ *v.t.* (**withheld**) nyima; katalia; zuia.

**within** /wɪ'ðɪn/ *adv.* ndani. *prep.* ndani ya; chini ya; karibu. *~ an hour*, haipati saa. *~ my power*, chini ya uwezo wangu. *~ hearing*, karibu.

**without** /wɪ'ðaʊt/ *prep.* pasipo; bila. *I have arrived ~ my baggage*, nimefika bila mizigo yangu; *He tried ~ succes*, alijaribu bila mafanikio. *adv.* (la zamani) nje.

**withstand** /wɪð'stænd/ *v.t.* (**withstood**) himili.

**witness** /'wɪtnəs/ *n.* shahidi; ushahidi. *v.t./i.* shuhudia; thibitisha.

**wittingly** /'wɪtɪŋli/ *adv.* makusudi; kwa kujua.

**wizard** /wɪzəd/ *n.* mchawi.

**wobble** /'wɒbl/ *v.i./t.* yumbayumba; pepesuka. *(fig.)* sitasita. **wobbly** *adj.* legelege.

**woe** /wəʊ/ *n.* majonzi; huzuni; masikitiko. **~s** *n.* msiba; taabu; matatizo. **~ful** *adj.* -a huzuni nyingi; -a kuhuzunisha.

**wolf** /wʊlf/ *n.* (**wolves**) mbwa mwitu. *keep the ~ from the door*, weza kujikimu. *~ cry*, kilio cha uwongo. *v.t (colloq.)* -la kwa pupa.

**woman** /'wʊmən/ *n.* (**women**) mwanamke. **~hood** *n.* utuuke; uanamama. **~ish** *adj.* -a kike. **~ly** *adj.* kama mwanamke.

**womb** /wu:m/ *n.* tumbo la uzazi; uterasi.

**wonder** /'wʌndə(r)/ *n.* ajabu; mshangao. *v.i.* staajabu; shangaa; jiuliza. *Do you ~ I refused?* unastaajabu kwa kuwa nilikataa? *I ~ who he is*, sijui hata ni nani. *I ~ wether he'll come*, najiuliza iwapo atakuja. **~ful** *adj* -a kustajabisha. **~ment** *n.* mshangao; ajabu.

**wondrous** /'wʌndrəs/ *adj.* -a ajabu.

**won't** /wəʊnt/ (ufupisho wa *will not) He ~ come today*, hatakuja leo.

**wood** /wʊd/ *n.* ubao; mbao; msitu. *be out of the ~*,okoka; toka hatarini. **~cut** *n.* muhuri wa mbao. **~ed** *adj.* -enye miti, -a msitu. **~en** *adj.* -a mti; -a mbao. *(fig) ~ headed*, -zito -a akili. **~land** *n.* msitu. **~work** *n.* useremala; vitu vya mbao. **~y** *adj.* -a msitu; -enye miti.

**wool** /wʊl/ *n.* manyoya; sufu; sufi. **~len** *adj.* -a sufi. *n.* nguo za sufi. **~ly** *adj* .-a sufi. *(fig.)* (kwa akili) iliochanganyikiwa. *pull the ~s over sb.'s eyes*, danganya mtu.

**word** /wɜ:d/ *n.* neno; habari; kauli; ahadi. *have ~s with sb.*, gombana na mtu; sema na mtu. *by ~ of mouth*, kwa habari za mdomo. *take sb. at his ~*, amini kauli ya mtu. *Send me ~ tomorrow*, nijulishe kesho. *break one's ~*, vunja ahadi. *be as good as one's ~*, timiza ahadi. *v.t.* eleza kwa maneno.

**work** /wɜ:k/ *n.* kazi; ajira; shughuli; sanaa; vifaa vya kazi; mitambo. *She took her ~ into the garden*, alichukuwa vifaa vyake hadi bustanini. *the ~ of silversmiths*, vitu vya fedha. *needle ~*, ushonaji; ufumaji. *stone ~*, uashi. *wood ~*, useremala. *the ~s of Shakespeare*, maandiko ya Shakespeare. *the ~s of a clock*, mitambo ya saa. *public ~s*, huduma za jamii. *v.i./t.* (**~ed**) **1.** fanya, tenda kazi. **2.** (kwa mashine) tenda kazi iliyokusudiwa. **3.** faulu; fanikiwa. **4.** tendesha kazi. **5.** legea. *The screw has ~ loose*, skrubu imelegea. *They ~ their way forward*, waliendelea polepole. *~ into*, ingiza; changanya. *~ a few jokes into a speech*, tia mzaha kidogo katika hotuba. *~ off*, ondoa. *~ off superfluous energy*, tumia nguvu bure. *~ up*, chochea; hamasisha. **6.** umba; unda; finyanga. **~able** *adj.* -a kuweza **~manship** *n.* ustadi; usanii. **~shop** *n.* karakana; warsha. **~station** *n.* eneo linalofanywa kazi kwa kutumia mtandao wa kompyuta

**world** /wɜ:ld/ *n.* dunia; ulimwengu. *a man of the ~,* mtu mwenye maarifa ya dunia. *the old ~,* Ulaya, Asia, na Afrika. *the new ~,* Amerika. *a ~ of,* -ingi sana. **~ly** *adj.* -a dunia; -a kupenda anasa za dunia. *my ~ goods,* mali yangu. **~wide** *adj.* -a dunia nzima.
**worm** /wɜ:m/ *n.* funza; mnyoo. *earth ~,* nyungunyungu; nyungwinyungwi. *v.t. ~ one's way through,* ingia polepole. *~ one's way into favour,* jipendekeza taratibu. *~ out,* pata habari kwa kusaili sana. **~-eaten** *adj.* -liotobolewa na funza.
**worry** /'wʌri/ *n.* wasiwasi; wahaka; usumbufu. *v.t./i.* **1.** udhi; sumbua; hangaisha. **2.** jisumbua; hangaika. **3.** (kwa mbwa) rarua; ng'ata.
**worse** /wɜ:s/ *adj./adv.* -baya zaidi. *the ~ for wear,* -liochakaa sana. *~ off,* maskini. **~n** *v.t./i.* fanya, -wa -baya zaidi.
**worship** /'wɜ:ʃɪp/ *n.* ibada; sala; heshima kuu. *v.t./i.* abudu. **~per** *n.* mwabuduji; abidu.
**worst** /wɜ:st/ *adj./adv.* -baya kuliko -ote; -baya sana. *get the ~ of it,* shindwa. *if the ~ comes to the ~,*mambo yakiwa mabaya kabisa.
**worth** /wɜ:θ/ *n.* thamani. *adj.* **1.** -enye thamani. **2.** stahili. *The book is well ~ reading,* kitabu hiki chastahili kusomwa. *be ~ it, be ~while,* faa. **~less** *adj.* bure ghali; -sio na thamani. **~while** *adj.* -a kufaa; -a maana. **~y** *adj.* -a kustahili. **~ily** *adv.* kwa thamani.
**wound** /wu:nd/ *n.* jeraha; kidonda; uchungu. *v.t.* jeruhi; tia uchungu.
**wrap** /ræp/ *n.* shali; nguo ya kujifunikia. *v.t./i.* (**-pp-**) (pengine *~ up*) kunjia; funika. *be ~ ped up in,* fungwa; funikwa. **~per** *n.* karatasi ya kufungia kitu.
**wreck** /rek/ *n.* kuvunjika (hasa ya merikebu); merikebu iliyozama. **~age** *n.* mabaki ya chombo kilichovunjika.
**wrench** /rentʃ/ *v.t.* sokota; vuta kwa ghafla; maumivu makali. *n.* mshtuo; teguo; maumivu; uchungu.
**wrestle** /'resl/ *n.* mweleka; mwereka. *v.i./t.* pigana mieleka. *(fig.) (with)* shindana na. **~r** *n.* mpiganaji mieleka.
**wretch** /retʃ/ *n.* maskini; mnyonge; fukara; bazazi; mhuni. **~ed** *adj.* -duni; dhalili; -a huzuni.
**wring** /rɪŋ/ *v.t.* (**wrung**) songoa; popotoa; kamua. *(fig)* toza kwa nguvu . *~ing wet,* -lioroa chapachapa.
**wrinkle** /'rɪŋkl/ *n.* **1.** kunyazi; mkunjo. **2.** *(colloq.)* kidokezi; shauri la manufaa.
**wrist** /rɪst/ *n.* kifundo cha mkono.
**writ** /rɪt/ *n.* hati. **holy ~,** maandiko matakatifu.
**write** /raɪt/ *v.i./t.* (**wrote written**) andika. **~r** *n.* mwandishi. **writing** *n.* mwandiko; maandishi.
**writhe** /rʌɪð/ *v.i.* jinyonga; gaagaa.
**wrong** /rɒŋ/ *n.* kosa; ubaya; dhambi; uovu. *adj./adv.* -baya; si sahihi. *go ~,* potoka. *be in the ~,* kosa. *put sb. in the ~,* fanya mtu aonekane mkosa. *v.t.* tendea mabaya; onea; dhulumu. **~doing** *n.* uovu; dhambi; uhalifu; **~ful** *adj. si -a haki.* **~fully** *adj.* bila haki. **~ly** *adv.* vibaya. *~ informed,* -lioarifiwa vibaya.
**wry** /rʌɪ/ *adj.* -a upande. make a **~ face**. *a ~ smile,* tabasamu la kulazimisha.

# Xx

**x-chromosome** *n.* chembeuzi-x: chembeuzi ya kijinsia ambapo idadi ya seli za kike (XX) ni mara mbili kuliko zile za kiume.

**xenon** /'zɛnɒn/ *n.* zenoni: gesi adimu isiyo na rangi wala harufu.

**x-mas** /'krɪsməs/ *n.* ufupisho wa *christmas:* sikukuu ya kuzaliwa kwa Yesu Kristo.

**x-ray** /'eks reɪ/ *n.* eksirei: chombo cha uchunguzi wa kitiba kinachotumia mionzi ya nuru inayopenya kwenye mwili. **~ picture**, picha ya eksrei. *v.t.* piga picha ya eksrei.

**xylem** /'zʌɪli:m/ *n.* zailemu: tishu yenye seli mfano wa bomba na kuta nene zinazosafirisha maji na madini katika mmea.

# Yy

**yacht** /jɒt/ *n.* yoti: boti dogo jepesi la mashindano.

**yam** /jæm/ *n.* kiazi kikuu.

**yard**[1] /jɑ:d/ *n.* yadi: kipimo cha urefu sawa na mita 0.914. **~stick** kigezo.

**yard**[2] /jɑ:d/ *n.* ua; uwanja. **work ~**, kiwanda; karakana. **brick ~**, kiwanda cha matufali.

**yarn** /jɑ:n/ *n.* nyuzi zilizosokotwa; kitani; *(colloq.)* hadithi. *spin a ~*, simulia hadithi.

**yawn** /jɔ:n/ *n.* mwayo. *v.i.* piga miayo.

**y-chromosome** *n.* chembeuzi-y: chembeuzi ya jinsia ambayo ni moja ya jozi na chembeuzi-x kwa madume ya wanyama.

**year** /jiə, jə:/ *n.* mwaka. *~ in ~ out*, mwaka baada ya mwaka. *all the ~ round*, mwaka mzima. **~ling** *n.* mnyama wa mwaka mmoja. **~ly** *adj./adv.* -a kila mwaka; kwa kila mwaka. *~ long*, -a mwaka mzima mfululizo. *the academic ~*, mwaka wa masomo. *the fiscal ~*, mwaka wa fedha.

**yearn** /jə:n/ *v.i.* tamani sana. **~ing** *n.* uchu; shauku.

**yeast** /ji:st/ *n.* hamira: viumbe vyenye seli moja vinavyotoa zaimasi, yaani kimeng'enya kinachogeuza sukari kuwa alkoholi na dioksidi kaboni.

**yell** /jel/ *n.* ukelele. *v.i.* piga yowe.

**yellow** /'jeləʊ/ *n./adj.* rangi ya manjano; -a rangi ya manjano.

**yes** /jes/ *int.* ndiyo; naam. **~-man**, barakala.

**yesterday** /'jestədeɪ; 'jestədɪ/ *n./adv.* jana.

**yet** /jet/ *adv./conj.* bado; hata hivyo. *He has not ~ come*, hafika bado. *They haven't ~ done anything*, hawajafanya kitu bado. *He worked hard ~ he failed*, alijitahidi hata hivyo alifeli.

**yield** /ji:ld/ *n.* mavuno; mapato; chumo. *v.t./i.* zaa; shindwa. *This land doesn't give good ~*, ardhi hii haitoi mazao mengi. *Although his enemy was tough he did not ~*, ingawa adui yake alikuwa mwenye nguvu lakini hakukubali kushindwa. **~ing** *adj.* laini; *(fig.)* -tiifu; -epesi kushawishika.

**yolk** /jəʊk/ *n.* kiiniyai: dutu ya protini kwenye ova ambayo hulisha kiinitete.

**yoke** /jəʊk/ *n.* nira



yoke of oxen

**you** /ju/ *pron.* wewe; *(pl.)* nyinyi. **~r** *adj.* -ako; -enu. **~s** *pron./adj.* -ako; -enu.

**young** /jʌŋ/ *adj.* changa; -dogo. **~ster** *n.* mtoto. *~ and old*, vijana kwa wazee.

**youth** /ju:θ/ *n.* ujana; vijana. *the ~ of Zanzibar*, vijana wa Zanzibar. **~ful** *adj.* -a ujana.

**yule** /ju:l/ *n.* (vilevile **~tide** ) Sikukuu ya Krismasi.

# Zz

**zeal** /zi:l/ *n.* juhudi; bidii; ari. **~ot** *n.* mkereketwa; mlokole; mwenye ushabiki uliopindukia mipaka. **~ous** *adj* -enye bidii; enye ari.

**zebra** /'zɛbrə/ *n.*punda milia. **~ crossing** alama ya milia ya kuvuka barabara kwa waendeo kwa miguu.



**zebra**

**zebu** /'zib:u:/ *n.* ng'ombe mwenye nundu .

**zenith** /'zɛnɪθ/ *n.* anga; *(fig)* upeo; ustawi. **~al** *adj.* -a kiwango cha juu.

**zero** /'zɪərəʊ/ *n.* sifuri, tarakimu hii (0); ziro. ~ *hour,* saa ya kuanza mashambulizi. ~ *in,* elekeza mawazo kwenye.



**zig zag**

**zest** /'zest/ *n.* bidii; shauku kubwa.

**zigzag** /'zɪgzæg/ *n.* zigizaga; -a kupindapinda.

**zinc** /zɪŋk/ *n.* zinki: aina ya madini nyeupe.



**zipper**

**zipper**,/'zɪpə(r)/ **zip-fastener** *n.* zipu.

**zodiac** /'zəʊdiæk/ *n.* maeneo ya jua, mwezi na sayari nyinginezo zilizogawiwa na wanajimu katika alama thenashara ambazo huitwa nyota za unajimu.

**zone** /zəʊn/ *n.* zoni; ukanda; eneo maalumu. **~ of influence**, eneoathari: eneo ambalo kiumbe kimoja kinaweza kukiathiri kingine. **tropical ~**, ukanda wa joto. **eastern ~**, ukanda wa Mashariki.

**zoo** /zu:/ *n.* zuu: mahali wafugwapo wanyama pori. **~logical** *adj.*-a zuolojia. **~ garden**, bustani ya wanyama pori. **~logist** *n.* mwana zuolojia: mtaalamu wa wanyama. **~logy** *n.* zuolojia: sayansi ya wanyama.

**zygote** /'zʌɪgəʊt/ *n.* kiumbe kichanga: seli iliyoumbika kwa muungano wa gameti mbili.




**zodiac | nyota za unajimu**

## Irregular verbs

| Infinitive | Past tense | Past participle |
|---|---|---|
| be | was, were | been |
| bear | bore | borne |
| beat | beat | beaten |
| become | became | become |
| begin | began | begun |
| bend | bent | bent |
| bet | bet, betted | bet, betted |
| bind | bound | bound |
| bite | bit | bitten |
| bleed | bled | bled |
| blow | blew | blown |
| break | broke | broken |
| breed | bred | bred |
| bring | brought | brought |
| broadcast | broadcast | broadcast |
| build | built | built |
| burn | burnt, burned | burnt, burned |
| burst | burst | burst |
| buy | bought | bought |
| catch | caught | caught |
| choose | chose | chosen |
| cling | clung | clung |
| come | came | come |
| cost | cost | cost |
| creep | crept | crept |
| cut | cut | cut |
| deal | dealt | dealt |
| dig | dug | dug |
| do | did | done |
| draw | drew | drawn |
| dream | dreamt, dreamed | dreamt, dreamed |
| drink | drank | drunk |
| drive | drove | driven |
| eat | ate | eaten |
| fall | fell | fallen |
| feed | fed | fed |
| feel | felt | felt |
| fight | fought | fought |
| find | found | found |
| flee | fled | fled |
| fling | flung | flung |
| fly | flew | flown |
| forbid | forbade | forbidden |
| forget | forgot | forgotten |
| forgive | forgave | forgiven |
| freeze | froze | frozen |
| get | got | got |
| give | gave | given |
| go | went | gone |
| grind | ground | ground |
| grow | grew | grown |

| Infinitive | Past tense | Past participle |
|---|---|---|
| hang | hung, hanged | hung, hanged |
| have | had | had |
| hear | heard | heard |
| hide | hid | hidden |
| hit | hit | hit |
| hold | held | held |
| hurt | hurt | hurt |
| keep | kept | kept |
| kneel | knelt, kneeled | knelt, kneeled |
| know | knew | known |
| lay | laid | laid |
| lead | led | led |
| lean | leant, leaned | leant, leaned |
| leap | leapt, leaped | leapt, leaped |
| learn | learnt, learned | learnt, learned |
| leave | left | left |
| lend | lent | lent |
| let | let | let |
| lie | lay | lain |
| light | it, lighted | lit, lighted |
| lose | lost | lost |
| make | made | made |
| mean | meant | meant |
| meet | met | met |
| mislead | misled | misled |
| mistake | mistook | mistaken |
| misunderstand | misunderstood | misunderstood |
| mow | mowed | mown |
| overhear | overheard | overheard |
| oversleep | overslept | overslept |
| overtake | overtook | overtaken |
| pay | paid | paid |
| prove | proved | proved, proven |
| put | put | put |
| read | read | read |
| repay | repaid | repaid |
| ride | rode | ridden |
| ring | rang | rung |
| rise | rose | risen |
| run | ran | run |
| saw | sawed | sawn |
| say | said | said |
| see | saw | seen |
| seek | sought | sought |
| sell | sold | sold |
| send | sent | sent |
| set | set | set |
| sew | sewed | sewed, sewn |
| shake | shook | shaken |
| shed | shed | shed |
| shine | shone | shone |
| shoot | shot | shot |
| show | showed | shown, showed |

| Infinitive | Past tense | Past participle |
|---|---|---|
| shrink | shrank | shrunk |
| shut | shut | shut |
| sing | sang | sung |
| sink | sank | sunk |
| sit | sat | sat |
| sleep | slept | slept |
| slide | slid | slid |
| sling | slung | slung |
| slit | slit | slit |
| smell | smelt, smelled | smelt, smelled |
| sow | sowed | sown, sowed |
| speak | spoke | spoken |
| speed | sped, speeded | sped, speeded |
| spell | spelt, spelled | spelt, spelled |
| spend | spent | spent |
| spill | spilt, spilled | spilt, spilled |
| spin | spun | spun |
| spit | spat | spat |
| split | split | split |
| spoil | spoilt, spoiled | spoilt, spoiled |
| spread | spread | spread |
| spring | sprang | sprung |
| stand | stood | stood |
| steal | stole | stolen |
| stick | stuck | stuck |
| sting | stung | stung |
| stink | stank | stunk |
| stride | strode | stridden |
| strike | struck | struck |
| swear | swore | sworn |
| sweep | swept | swept |
| swell | swelled | swollen, swelled |
| swim | swam | swum |
| swing | swung | swung |
| take | took | taken |
| teach | taught | taught |
| tear | tore | torn |
| tell | told | told |
| think | thought | thought |
| throw | threw | thrown |
| thrust | thrust | thrust |
| tread | trod | trodden |
| understand | understood | understood |
| undo | undid | undone |
| upset | upset | upset |
| wake | woke | woken |
| wear | wore | worn |
| weave | wove | woven |
| weep | wept | wept |
| win | won | won |
| wind | wound | wound |
| wring | wrung | wrung |
| write | wrote | written |

Rev Mpindo
Home
LYBRARY

Aug: 2/13th — 26th Visit

A gift To

Dr. Yoggi Shsde

USA

Rev. [illegible]

# A Concise English-Swahili DICTIONARY

The revised English-Swahili Dictionary is a contemporary and easy-to-use reference book for all users whose mother tongue is Swahili. It not only gives detailed help with new scientific terms but also deals with difficult words in a simple way.

This unique dictionary contains:

| | |
|---|---|
| Words | • More than 10,000 headword entries, including new scientific vocabulary |
| Meanings | • 30,000 definitions |
| Examples of use | • Hundreds of phrases and sentences to show how words are used in their contexts |
| Usage | • Correct grammatical structures and usage |
| Illustrations | • More than 300 illustrations including a map of East Africa |
| IT terminology | • Many computer terms have been translated into Kiswahili for the first time |
| Study pages | • Short history of Swahili, proverbs, shapes and sizes, figures of speech, computer and internet vocabulary |

T2-FOJ-783

ISBN 9976 4 0016 0

OXFORD
UNIVERSITY PRESS